**CEKENA**
**102/1**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA KWANZA**
**INSHA**
**MACHI 2020**

**Swali la kwanza ( lazima)**

1. Wewe ni mwanahabari wa kituo cha runinga cha Mwelekezi. Andika mahojiano kati yako na Mwenyekiti wa Tume ya Umoja na Uwiano wa kitaifa kuhusu hasara za siasa chafu za mirengo ya kikabila . (Alama 20)
2. Mfumo wa ugatuzi ulioasisiwa kupitia katiba mpya umeboresha maisha ya wakenya. Fafanua. ( Alama 20)
3. Andika kisa kinachoafiki methali;

   Mgaagaa na upwa hali wali mkavu (Alama 20)

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo;
   …………………… Nilipofungua bahasha na kusoma kijikaratasi cha matokeo, ukweli ulinibainikia kuwa hali yangu haikuwa rahisi. (Alama 20)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA PILI**
**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**
**MACHI 2020**
**MUDA: SAA $2^1/_2$**

**A. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha maarufu ulimwenguni. Wataalamu wa lugha wanasema kuwa lugha hii ni ya sita ulimwenguni kwa umaarufu. Asili ya lugha hii imekuwa ikizua mjadala. Wanaisimu wamezama katika utafiti wa kina ili kubaini chimbuko lake.

Nadharia moja hueleza kuwa asili ya lugha hii ni pwani ya Afrika Mashariki. Wananadharia wanaunga msimamo huu mkono hupinga wanaoeleza kuwa Kiswahili ni lugha inayotokana na kiarabu. Wanaoshikilia chimbuko la Kiswahili kuwa Kiarabu husahau kuwa kila lugha mahali popote ulimwenguni hukua na kuathiriwa na lugha za kigeni kwa njia moja au linguine. Hivyo ndivyo Kiswahili kimeathiriwa na lugha za kigeni hasa kutoka kiarabu.

Wananandharia wengine hushikilia kuwa asili ya Kiswahili ni lugha ya kiarabu. Uchunguzi unaonyesha kuwa asili mia sitini na tanoya maneno ambayo hutumika katika Kiswahili sanifu yanatokana na lugha ya kiarabu, Aidha , asilimia tano ya maneno ya Kiswahili hutokana na maneno ya lugha zingine za kigeni.

Walioweka msingi wa kusafinisha lahaja sanifu ya Kiswahili walikubwa na tatizo la matumizi yake . Hii ilitokana na kuwepo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili. Baada ya mjadala mkali, lahaja ya kiunguja iliteuliwa kuwa Kiswahili sanifu na ikawa rasmi.

Lugha ya kiwahili ilitumika kama lugha ya biashara baina ya wenyeji wa pwani ya Afrika Mahariki na wageni. Aidha, wakoloni waliitumia katik shughuli zao za kuitawala. Hata hivyo, wakoloni waligundua kuwa lugha hii ilikuwa hatari kwani iliweza kuwa sambazi na hivyo kutumia lugha zao katika utawala wao. Iliweza kuwaunganisha Waafrika katika pilikapilika za kutaka uhuru wao.

Baada ya uhuru, viongozi mbalimbali wan chi za Afrika Mashariki wakiwemo hayati Mzee Jomo Kenyatta walihimiza sana matunizi ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali za taifa. Lugha hii ilifanywa kuwa lugha ya taifa nchini Kenya. Hayati Mwalimu Julius Nyerere naye hakjuachwa nyuma katika kukuza na kuendeleza Kiswahili katika nchi ya Tanzania. Viongozi wa nchi ya Uganda wlizembea kukitumia Kiswahili. Wao walihimiza kiingereza ni lugha za kiasili.

Hivi sasa, lugha ya Kiswahili ina wajibu muhimu katika nchi za Afrik Mashariki. Lugha hii sasa ni rasmi nchini Kenya. Inafuzwa na kutahiniwa katika viwango vyote vya elimu. Aidha, katika nchi ya Tanzania, lugha hii hivi sasa inatumika kufunzia masomo mengine yakiwemo hisabati nay a sayansi. Nchini Uganda, Kiswahili kinafundishwa katika shule za msingi.

Umaarufu wa lugha ya Kiswahili umevuka mipaka ya Bara la Afrika Mashirika ya kimataifa kama vile BBc na Radio China hutangaza taarifa za habari na baadhi ya vipindi kwa Kiswahili. Baadhi ya vyuo vikuu vya Ulaya na Marekani hufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hivi sasa matumizi yake yameingizwa hata katika mtandao wa intaneti

**Maswali:**

(a) Taja sababu mbili za Kiswahili kuwa maarufu ulimwenguni (ala. 2)
(b) Andika ushahidi ambao mwandishi anatumia kuonyesha kuwa kiswahili kina asili ya Kiafrika (ala. 3)
(c) Taja Masaibu mawili ya maenezi ya Kiswahili katika enzi za ukoloni (ala. 2)

(d) Eleza Majukumu ya kiswahili katika mataifa ya Afrika Mashariki (ala. 4)
(e) Thibitisha kwa kutoa ushahidi kutoka kwenye makala kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa (ala. 3)
(f) Eleza maana ya neno lahaja kama lilivyotumiwa katika makala (ala. 1)

**B. UFUPISHO (ALAMA 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Sisi vijana wa Kenya inatuwajibikia kufanya kazi kwa bidii, na dhati ya moyo wetu tuweze kupata ufanisi, na uwezekano wa kuinua nchi yetu change katika kiwango cha juu. Tukumbuke "ajizi ni nyumba ya njaa" kwa hivyo hatufai kulaza ndamu tukiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidia elimu ya vijana nay a watuwazima, kilimo, uchumina amani katika nchi yetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo.

Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao ya mashambani, kwani kila kukucha idadi ya watu nchini inaongezeka. Nisharti tuweze kujitok=sheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo oia lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sas ni wakenya wachache sana ambao lazima kila mmoja aajiriwa maishani. Yatupasa tijitahidi kuleta uchumi katika mikono ya mwananchi wa Kenya badala ya kuwaachia ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayoyapata majumbani, shuleni na hata katika jamii, lazoma yatuwezeshe kuatmbua mbinu za kipitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayoitamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbayo; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele, sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu lazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja, "utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kitatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu, wakati tunapokozea lazima tukubali tumekosa na kufanya masahihisho mara moja, Kwani "usipoziba ufa utajenga ukuta".

Tusikasirike kwa sababu tumesa hihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi. Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hay. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu mashuleni na majumbani mwetu. Utamanduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, Amani na upendo. Lazime tuwe na bidii na ushirikiano mwema kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo basi tutabaki nyuma kamna mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa

**Maswali:**

(a) Fupisha aya ya kwanza (Maneno 60-70) (ala. 7, mtiririko 1 )
Matayarisho
(b) Eleza mambo muhimu anayoibua mwandishi katika aya ya pili. (Maneno 90 – 100 ) (ala. 6, mtiririko 1)

Matayarisho
Jibu

**C. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Linganua sauti zifuatazo (alama 2)
i) /t/ na /d/________________________________________________
ii) /gh/ na /g/ ______________________________________________
iii) /n/ na /ny/ ______________________________________________
iv) /j/ na /y/ _______________________________________________

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Andika neno lenye muundo ufuatao wa mofimu; mofimu ya ukanusho wa nafsi umoja, wakati ujao, yambwa, mzizi, kauli tendea na kiishio (alama 3)

(c) Tumia neno **shirika** kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja (alama 2)

(d) Andika sentensi ifuatayo kwa umoja (alama 2)
Nyaraka zetu ziliwasilishwa rasmi kwenu na madiwani wa vyama tawala

(e) Tumia neno **hadi** katika sentensi kama kihusishi cha (alama 2)
(i) Wakati ______________________________________________
(ii) Mahali ______________________________________________

(f) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo (alama 2)

Sitakununulia nguo wala kukutembeza mjini usipomaliza mkate huo

(g) Unganisha sentenzi zifuatazo kwa kutumia neno ulilopewa katika mabano (alama 1)
Wageni watafika haraka. Wageni watatumia ndege (iwapo)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa (ala. 2)
"Kuandika kwa hati nadhifu kutawawezesha watahiniwa hawa wenu kupita", mtahini akatuambia

(i) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi. (ala.2)
Msomi hakutuzwa siku hiyo

(j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. Matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili yana virutubishi vingi. (Anza kwa; Virutubishi vingi……………….) (alama 1)

(k) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo (alama 2)
Mzee alijenga ukuta kuziba mtaro wa maji

(l) Andika miundo miwili ya nomino katika ngeli ya KI-VI (alama 1)

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale (alama 2)
Wanafunzi waliotia bidii masomoni walipata alama nzuri mno

(n) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Waziri mkuu hupigiwa nguo zake pasi an Maria

(o) Bainisha matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari (alama 2)
Mwalimu anakuita afisini umweleze ulikoweka kijitabu chake.

(p) Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo (alama 2)
(i) Kishazi tegemezi na kishazi huru

(ii) Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

(q) Akifisha sentenzi ifuatayo (alama 2)

Nataka uniletee vitu hivi vitatu kalamu viatu na nguo amina aliniambia

(r) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya tata na dada (alama 2)

(s) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendea (alama 1)
Mama alimpa mtoto uji

(t) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)
Mwalimu alichukuliwa na wanafunzi wake

(u) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kiria nomino (alama 2)

(v) Majoka ana mahasidi wengi kwa sababu anawakosea. Hata hivyo yeye hapendi kukosewa hata chembe (alama 1)

Andika methali inayoweza kutumiwa kueleza hali hii

## D. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

…… Bwana spika ninaomba kufahamishwa kwa nini Waziri wa biashara ameshindwa kuchukua hatua kukomesha uuzaji wa vileo hatari kwa watoto wa shule

(a) Tambua sajili hii (alama 2)

(b) Fafanua sifa zozote nane za sajili inayorejelewa na manenp haya (alama 8)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**CEKENA**
**102/3**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**MACHI 2020**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA 2020**
**SEHEMU A: Ushairi (alama 20)**

Nikiwa na njaa na matambara mwilini
Nimehudumika kama hayawani
Kupigwa na kutukanwa
Kimya kama kupita kwa shetani
Nafasi ya kupumzika hakuna
Ya kulala hakuna
Ya kuwaza hakuna
Basi kwani hili kufanyika
Ni kosa gani lilotendeka
Liloniletea adhabu hii isomalizika?

Ewe mwewe arukaye juu angani
Wajua lililomo mwangu moyoni
Niambie pale mipunga inapopepea
Ikatema miale ya jua
Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?
Je nadhari hujitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?
Mpenzi mama nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama maiti yangu imekatikakatika
Vipande elfu, elfu kumi
Nitarudi nyumbani
Nikipenya kwenye ukuta huu
Nikipita mwingine kama shetani
Nitarudi mpenzi mama…….
Hata kama kifoni.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**maswali**
1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)
2. Tambua nafsineni katika shairi hili (alama 2)
3. Eleza toni katika shairi hili (ala. 2)
4. Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (ala. 4)
5. Fafanua dhamira kuu katika shairi hili (ala. 2)
6. Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (ala. 2)
7. Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (ala. 2)
8. Fafanua mbinu tatu za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (ala. 3)
9. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (ala. 2)
   (i) Hayawani ____________________________________________
   (ii) Nadhari ____________________________________________

**SWALI LA PILI: Chozi la Heri**

"…………….. haifai kucheza na uwezo wa vijana, wao ni kama nanga. Huweza kuzamisha na kuiongoa merikebu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika dondoo (alama 4)

(c) Fafanua nafasi ya vijana katika jamii kwa mujibu wa Chozi la Heri (alama 12)

**SWALI LA TATU: Chozi la Heri**

" Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha Yule kiongozi wa kiimla wa kike."

(a) Eleza kwa ufupi yaliyowapata wahafidhina baada ya usemi huu (alama 4)

(b) Mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri anawaumbua wanawake kabisa. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja **kumi** (alama 16)

**SWALI LA NNE: TUMBO LISILOSHIBA**

" …..lakini kula kunatumaliza vipi?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumika katika dondoo hili (alama 2)

(c) Fafanua ukweli kwamba wahusika wachache wanakula vibaya (alama 6)

(d) Eleza jinsi kula kunavyotumaliza kwa mujibu wa hadithi (alama 8)

**SWALI LA TANO: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA**

1. "Tulipokutana Tena – Alfa Chokocho.

(a) Jadili jinsi maudhui ya umaskini yalivyoshughulikiwa katika hadithi ya "Tulipokutana Tena" (alama 10)
Mame Baka

(b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na changamoto nyingi. Tetea (alama 10)

**KIGOGO**
**MASWALI**

"…………. Kwa mama pima ni raha na maraha. Twasherehekea uhuru."

(a) Onyesha kinaya cha maneno yaliyopigiwa mstari ukirejelea hoja kumi kutoka tamthilia ya Kigogo (alama 10)

(b) Hakiki jinsi mbinu ya jazanda ilivyotumika katika tamthilia ya Kigogo (alama 10)

**FASIHI SIMULIZI ( ALAMA 20)**

(a) Eleza matatizo sita unayoweza kukabiliana nayo katika kutafiti bembelezi katika jamii (alama 8)

(b) Eleza dhima ya misimu katika jamii (alama 6)

(c) Jadili majukumu ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano (alama 6)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**CEKENA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2020**

**102/1**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA KWANZA**
**INSHA**

**MWONGOZO WA INSHA**

**Baadhi ya hoja**

1. Huleta chuki baina ya makabila
2. Kusababisha vita baina ya makabila
3. Kuchagua viongozi wasio na maono bora tu ni wa kabila Fulani.
4. Huharibu uhusiano na kuishi kwa woga kwa watu wasio wa kabila moja.
5. Hukwamiza maendeleo Mfano: biashara baina ya makabila hutatizika / umaskini/ masoko kuharibiwa.
6. Vifo – huenda makabila yakapigana
7. Hurudisha nyuma juhudi za serikali kuleta umoja na utangamano wa kitaifa.
8. Huwaogofya wawekezaji na hivyo kupunguza nafasi za kazi / huathiri uchumi
9. Uharibifu wa mali mfano, nyumba, magari n.k patokeapo vita baina ya makabaila.
10. Wanaopoteza wenzao huathirika kisaikolojia iwapo kuna vita

11. Hutatiza shughuli za elimu katika taifa
12. Shughuli kama vile ndoa baina ya makabila huwa ngumu (kuogopana)
13. Hunyima watu uhuru wa kutembea kwa sababu ya woga.
14. Husababisha ukimbizi wa ndani kwa ndani.

TANBIHI. Vipengele vifuatvyo vijitokeze:-

(i) Sura ya mahojiano (tamthilia) ijitokeze – (akose alama 4 akikosa sura)
(ii) Hoja zisipungue sita
(iii) Maneno yasipungue mia nne

Majibu ya swali la pili

i) Ugavi wa raslimali kufanywa wazi
ii) Uongozi mzuri wa uwajibikaji
iii) Kuwepo kwa usawa wa kimaeneo
iv) Maendeleo mashinani K.v. barabara, umeme n.k kupitia ushuru unaotozwa
v) Kushirikisha wakenya wote katika maendeleo kupitia vikao / wananchi kuhusishwa katika vikao/ utawala
vi) Idara ya mahakama imeanza kupatiana huduma bora mashinani.
vii) Demokrasia imeweza kuimarishwa
viii) Umepunguza uhamiaji wa watu mijini
ix) Nafazi za ajira zimeongezeka
x) Elimu ya kiufundi na chekechea imeweza kuenezwa mashinani

TANBIHI

Mwanafunzi ajadili kwa kuunga mkono tu
Hoja sita zikuzwe kikamilifu
Maneno yasipungue mia nne
Azingatie utaratibu wa kuandika mjadala.

**1. Mgagaa na upwa hali wali mkavu**

Kisa kionyeshe hali ambapo mhusika/ wahusika anahangaika /wanahangaika kupitia juhudi za hapa na pale na mwishowe wanazoa matunda/ wanafanikiwa

TANBIHI

Kisa kionyeshe pande mbili za methali: kujibidiisha hapa na pale na kule kufanikiwa.

**2. <u>Jibu la swali la nne</u>**

i) Insha hii ni ya mdokezo
ii) Sharti akamalishe kwa maneno aliyopewa. Iwapo hajamaliza maneno haya atuzwe alama tatu pekee kwa kuwa amejitungia swali
iii) Kisa kioane na mdokezo
iv) Nafsi ya kwanza itumiwe kusimulia kisa na wakati uliopita / urejeshi unaweza kutumika
v) Kisa kidhihirishe hali ambayo haikutarajiwa na iwe hali yenye ugumu kwa mhusika kukabiliana nayo.
vi) Maneno yasipungue mia nne.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**CEKENA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA 2020**
**102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**

**MWONGOZO WA LUGHA**

**2. UFAHAMU (Alama 15)**

a) Hutumiwa na masharika ya utangazaji ya kimataifa na pia mtandao wa intaneti.
b) Uchunguzi unaonyesha kuwa asilimia sitini na tano ya maneno ambayo hutumika katika Kiswahili sanifu yanatokana na lugha za Kibantu.
c) Wakoloni walitumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kiutawala. Hata hivyo, wakoloni waligundua kuwa hii ilikuwa hatari kwani iliweza kuwa sambazi na hivyo kuwaunganisha Waafrika kupigania uhuru. Wakoloni waliamua kutumia lugha zao katika utawala wao.
d) Hutumiwa kama: lugha ya kufundisha, lugha ya kibiashara, lugha ya taifa na lugha rasmi.
e) Hufundishwa katika vyuo vya Ulaya na Marekani, hutumiwa na mashirika ya utangazaji ya kimataifa na pia katika mtandao wa intaneti.
f) Lahaja ni mojawapo ya vijilugha vya lugha moja.

**3. MUHTASARI**

(a)

- Sisi vijana wa Kenya inatuwajibikia tujibidiishe kazini ili tufanikiwe na kuinua nchi yetu
- Haifai kulaza damu tukiwa matatizo yametuzonga.
- Lazima tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani.
- Bila elimu itakuwa vigumu kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo.
- Lazima tuzidishe mazao ya mashambani kwani idadi ya watu inaongezeka.
- Yatupasa kuleta uchumi mikononi mwa wakenya badala ya kuwaachia wasiohusika. (alama 7)

(b)

- Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni na katika jamii lazima yatutambulishe na mbinu za kupitia.
- Elimu tambuzi inapaswa imfanye mwanakenya kujua wajubu wake.
- Elimu pumbao inatufanya tusione mbele.
- Vijana wanapaswa kuwa kielezo chema kwa wengine
- Lazima watu washirikiane na kuwa na umoja.
- Lugha ya taifa ndicho chombo kinachotuunganisha
- Tunapokosea, tukubali na kufanya masahihisho.
- Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi kama wazalendo.
- Tujishughulishe na kuyangalia matatizo ya nchi na kuyatatua.
- Tuwe n nidhamu
- Tuwe na bidii na ushirikiano kuwachagua viongozi wanaopenda maendeleo.
- Tusichague viongozi kwa kufuata ukoo au utajiri (alama $12^1/_2$)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**4. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) (i) /t/ - Sighuna /d/ - ghuna
(ii) /gh/ - kikwamizo /g/ - kipasuo
(iii) /n/ - ufizi /ny/ - kaakaa gumu
(iv) /j/ - kipasuo /y/ - kiyeyusho / nusu irabu
(alama ½ x 4 = 2) (lazima mwanafunzi alinganue ili apate alama ½ )

(b) Hatamchezea / Hatampikia
(kadiria jibu la mwanafunzi) alama ½ x 6 = 3

(c) Wafanyakazi wa <u>shirika</u> lile walifanya kazi kwa <u>ushirikiano / Kishirika</u>
(alama 1 x 2 = 2)

(d) <u>Waraka</u> Wangu uliwasilishwa rasmi kwako na diwani wa chama tawala. (alama 1 x12 =2)

(e) Tulicheza kutoka asubuhi hadi adhuhuri - wakati wezi walinikimbiza hadi nyumbani mwangu – mahali (kadiria sentansi za wanafunzi) (alama 1 x 2 =2)

(f) Nitakununulia kiguo na kukutembeza kijijini ukimaliza kijikate hicho (alama 2/0)

(g) (i) Wageni watafika mapema iwapo watatumia ndege

(ii) Iwapo wageni watatumia ndege, watafika mapema (alama 1 x1 =1)

(h) Mtahini aliwaambia kuwa ✔ /kwamba kuandika kwa hati nadhifu kungewawezesha ✔ watahiniwa hao ✔ wao ✔ kupita (alama ½ x 4 = 2)

(i) Wasomi watakuwa wametuzwa siku hiyo katika matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili (alama 2/0)

(j) Virutubishi vingi vinapatikana/ hupatikana/vyapatikana katika matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili (alama 1 x 1 = 1)

(k) Mzee alijengua ✔ / bomoa ukuta kuzibua ✔ mtaro wa maji (apama 1 x 2 = 2)

(l) KI – VI kiatu - viatu
Ch - Vy chungu - vyungu
Vi - vita – vita (alama ½ x 2 = 2)

(m)

| | | | |
|---|---|---|---|
| S | - | KN + KT | alama 1 |
| KN | - | N + S | |
| N | - | wanafunzi | |
| S | - | Waliotia bidii masomoni | |
| KT | - | T + N + V + E | alama 1 |
| T | - | Walipata | |
| N | - | alama | |
| V | - | nzuri | |
| E | - | mno | |

(jumla alama 2)

(n) Waziri mkuu - yambwa tendewa / kitondo
Nguo zake - yambwa tendwa / shamirisho kipozi
Pasi - yambwa ala / kitumizi
Maria - kiima

(o) Ku - kiambishi cha nafsi ya pili
Ni - kielezi cha mahali (ndani ya)
Ko - mahali
Ki - udogo wa nomino

(alama ½ x 4 = 2)

(p) (i) kishazi tegemezi na kishazi huru
Motto aliyewasili leo amerudi kwao
S S
(ii) Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi
Angalilima kwa bidii angalivuna mavuno tele
S S (alama 1 x 2 = 2)

(q) "Nataka uniletee vitu hivi vitatu: kalamu, viatu na nguo," Amina aliniambia. (alama 2)
" " alama ½ , N na A – alama ½ , : - alama ½ , ,- alama ½ .

(r) Tata - patwa na hali ya kutoeleweka
Dada – ndugu wa kike

(s) Mama alimpatia / pea mooto uji (alama 1)

(t) Mwalimu pamoja na wanafunzi wake walichukuliwa na mtu mwingine
Mwalimu ndiye aliyechukuliwa na wanafunzi
Kitu Fulani kilichukuliwa kwa niaba ya mwalimu (alama 2)

(u) Nomino pekee (N)
Kiwakilishi (W)
N + U + N
N + V
N + V + V

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

N + V + E
N + S (kishazi + tegemezi) (alama 2)
**Tan: lazima mtahiniwa atolee mfano wa sentensi**

(v) Mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu u mchungu (alama 1)
(kadiria methali)

**5. <u>ISIMU JAMII (Alama 10)</u>**

Sajili ya bungeni

(i) Husheheni msamiati/ istihahi maalum - mfano Bw. Spika, mswada.
(ii) Huwa na fomyula/ mianzo maalum
(iii) Huwa na kuchanganya ndimi/ msimbo
(iv) Lugha sanifu
(v) Lugha ya adabu na heshima
(vi) Mseto wa sentensi ndefu na fupi.
(vii) Hurejelea vifungu vya sheria / katiba
(viii) Urudiaji/ takriri ya maneno
(ix) Kuna kukatizana kalima/ usemi
(x) Lugha ya ishara nyingi kama kuinama
(xi) Wabunge hupokezana zamu kuzungumza
(xii) Hutumia lugha kavu isiyo na mapambo
(xiii) Washirika hutajwa kwa majina (wahusika)
(xiv) Lugha huwa na maswali na majibu

(8 x 1 = 8)

Tanbihi mwanafunzi atoe mifano mwafaka ili kupata alama 1. ½ kwa sifa pekee

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>CEKENA</u>**
**102/3**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**MAJIBU YA SWALI YA KWANZA - USHAIRI**

(a) **Lipe shairi kichwa mwafaka** **(ala. 1)**

- Mama nitarudi
- nitarudi
- kizuizini

(1 x 1 = 1)

(b) Tambua nafsineni katika shairi hili (ala. 2)
Nafsineni ni mfungwa aliye kizuizini. Anauliza iwapo mamake angali anasimama na kusubiri akitazama kule kizuizizni aliko nafsineni (2 x 1 = 2)

(c) Eleza toni katika shairi hili (ala. 2)

- Toni ya masikitiko/uchungu wa moyoni/huzuni. Anasikitikia hali yake ya kuvaa matambara, njaa kufanyishwa kazi tele n.k.
- Toni ya matumaini mshairi ana matumaini kwamba siku moja atatoka kizuizini.

(d) Taja mambo manne ambayo mshairi analamikia (ala. 4)

- Kuachwa njaa
- Kufungwa
- Kufukuzwa
- Kutopewa nafasi ya kupumzika, kulala na kuwaza
- Kuvaa matambara
- Kufanyshwa kazi kama mnyama

(e) Fafanua dhamira kuu katika shairi hili (ala. 2)

- Mshairi anadhamiria kulalamika /kukashifu namna anatumiwa vibaya kizuizini

- Mshairi anakashifu madhila na mateso ambayo wafungwa hutendewa.
- Kumpa mamake matumaini kwamba atatoka kizuizini siku moja

(f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (ala. 2)
- Mistari mishata
- Idadi ya mishororo inabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine
- Idadi ya mizani inabadilika kutoka mshororo hadi mshororo.

(g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (ala. 2)
- Ni mwenye kulalamika – analalamikia hali yake ya kuwa na njaa , kupigwa
- Ni mwenye matumaini – anatumai kuwa siku moja atatoka kizuizini
- Mwenye mapenzi- anampenda mamake na kumwita mama mpenzi (2 x 1 = 1)

(h) Fafanua mbinu tatu za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (ala. 3)
- Takriri – neno nitarudi limerudiwa rudiwa
- Mdokezo – nitarudi mama mpenzi……….
- Taswira
- balagha

(i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili (ala. 2)
(i) Hayawani - mnyama
(ii) Nadhari - fikira

**MAJIBU YA SWALI YA PILI - CHOZI LA HERI**

(a) (i) Ni maneno ya Mwangeka
(ii) Anamwambia Ridhaa
(iii) Wamo katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Rubia
(iv) Ni baada ya kuyakumbuka maneno ya Tila kuwa haifai kucheza na uwezo wa vijana katika jamii.

(b) (i) Tashbihi - wao ni kama nanga
(ii) Jazanda - merikebu inasimamamia taifa la wahafidhina
(iii) Taswira - picha ya merikebu inayozamishwa (zozote mbili 2 x 2 = 4)

(c) Vijana hawapati nafasi ya kushiriki kikamilifu katika uzalishaji wa mali na raslimali k.m. Elimu wanayopata haiwasaidii kujipatia kazi
- Hawawezi kujiajiri kwa kuwa hawana mtaji wa kuanzisha biashara, jambo ambalo linafanya maisha kuwa magumu zaidi
- Wanahimizwa kurudi mashambani ili kuzalisha mali huko lakini baadhi yao hawana mashamba.
- Wana jukumu la kuelimishana kuhusu nafasi ya kila mmoja katika kuboresha uongozi uliopo kwa kuzalisha nafasi za kazi.
- Wana jukumu la kutambua kwamba wanatumiwa na viongozi kwa minajili ya kutimiza matakwa yao ya kisiasa.
- Wana jukumu la kutambua kwamba hawafai kujihusisha na maswala ya mapenzi katika umri mdogo ili kujiepusha na madhara yake k.v ujauzito. (zohali)
- Wanatafuta njia za kuyamaliza/ kuyapunguza matatizo yanayowakumba k.m. chaurembo anafanya kazi katika shamba la majanichai ili kumpunguzia mfadhili wake mzigo.
- Wanafuata utamaduni wa jamii zao k.m Toama na wenzake wanashiri mila za tohara za jamii yao.
- Wanakumbwa na mabadiliko mengi wanapoendelea na kukua (kimwili na kimaumbile) Sare za awali za pete zinapoanza kukataa mwili kutokana na kukua ananunuliwa nyingine na mamake.
- Vijana wanalaghaiwa kwa urahisi na watu wenye tama ya kujitajirisha kwa kuahidiwa kazi k.m Bi Kangara anawauza ng'ambo bila ufahamu wao.
- Vijana wana uhuru wa kujichagulia wake au waume. Nyanyake pete anataka ajichagulie mume.
- Ni wasomi k.m Mwangeka, umu n.k (2 x 10)

**MAJIBU YA SWALI YA TATU - CHOZI LA HERI**

(a)
- Watu walichukua silaha kupigania uhuru wao
- Mlio wa bunduki ulikuwa ukisikika
- Vilio vilijaa hewani
- Vyombo vya dola vilitumiwa kudumisha amani
- Misafara ya watu ilionekana

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

– Mazao yalichomwa mashambani
– Watu waliuana
– Majumba yaliteketezwa

Hoja zozote nne 4 x 1 = 4

(b) Mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri amewaumbua wanawake kabisa. Thibitisha ukweli wa kauli hii (alama 16)

– Sauna anawatorosha wana wa Lunga (Dick na Mwaliko) badala ya kuwajibika kuwalea kama alivyomwahidi /kulinda usalama wao
– Sauna na Bi Kangara wanashirikiana kuwalangua watoto wa wenyewe wanaohusishwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya mfano Dick.
– Subira anaitoroka familia yake na kwenda mjini. Huko anabugia kinywaji kikali (sumu) na kufa
– Pete anajihusisha na ukahaba kwenye baa alikokuwa akiuza pombe. Anaambulia uja uzito baada ya kuwahiwa na mlevi mmoja nishai zikiwa zimemlemea.
– Pete anajaribu kuavya mimba ya Nyangumi (mara nne) bila kufanikiwa na pia ya mtoto wa tatu (ya mlevi). Hafanikiwi
– Wanawake wanawatupa watoto mfano Naomi anaokota kitoto kilichokuwa kimetupwa jalalani.
– Mama yake zohali kutomtetea dhidi ya dhuluma za babake licha ya kujua uchungu wa kulea mimba.
– Baadhi ya wanawake wanakubali kuwa waasherati mfano, Pindi tu Bi. Kimai anapoenda mashambani, Bwana Tenge analeta wanawake wengine nyumbani. Annette anadai kumwachia kiriri vimada wake
– Sauna anawahudumia walevi kwa njia zote anakouza pombe (ukahaba).
– Naomi anamtoroka Lunga baada ya kufilisika, anamsababishia kihoro kingi, kinachomzidishia shirikizo la damu. Anaishia kufariki.
– Annette anamwacha Kiriri na kwenda ng'ambo anakojiunga na wanawe. Hili linamsababisha Kiriri Kihoro na upweke. Kihoro pamoja na kufilisika kunasababisha kifo chake.
– Mamake Sauna ananyamaza na kutochukua hatua yoyote hata baada ya kugundua kuwa bwana Maya amekuwa akibaka mtoto wake. Anamwonya Sauna dhidi ya kusema unyama huo kwa yeyote.
– Tauma anajificha na kupaswa tohara kisiri licha ya kukanywa na babake.
– Rehema anamtelekeza mwanaye Chandachema kwa kumpeleka kwa nyanyake.
– Sally anamwacha Billy kwa madai kuwa chumba alichomjengea ni kiota. Anasaliti penzi lao
– Mamake Pete kuridhia kuozwa kwake kwa mzee Fungo jambo linalosababisha kukatiziwa masomo yake
– Jamii ya wanawake kumtenga Mwekevu kwa kuwania uongozi ati kwa sababu amepanda kwenye ulingo wa wanaume
– Mamamkwe kumwonea gere subira anamwona kama aliyekuja kumbwakura mwanawe na daima kumchukua kama mgeni. Alimbagua, kumfitina na kumsingizia wizi wa mayai ya kuku (aliowafuga)
– Mamake Sauna anampeleka bintiye kuavya mimba aliyopagazwa na babake wa kambo, bwana Maya.
– Wanawake kushirikiana na mabwana zao kuwabagua watoto waliozaa nje ya ndoa mfano. Mamake Pete kumpagaza nyanyake malezi yote ya Pete baada ya kisingizio kwamba alikuwa mtoto wa nje.
– Bi. Kangara anawauza wasichana katika madanguro.
– Wanawake wa kiafrika kufunga ndoa na vikongwe ama wanaume wengine waendapo g'ambo anashangaa ikiwa Annette amekuwa mmoja wao (16 x 1 = 16)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MAJIBU YA SWALI LA NNE**

(a) Haya ni maneno ya Sasa akimwambia Mbura katika sherehe baada ya kula. Wanazungumzia ile hali ya matumbo yao kushiba ilhali wengine wanadhikika tu (1 x 4 = 4)

(b) Mbinu ya kimtindo
(i) Jazanda/ sitiari/ istiari
(1 x 2 = 2)
(ii) Swali la balagha
Tanbihi: kutaja (1)
Mfano: (1)

(c) Fafanua ukweli kwamba wahusika wachache wanakula vibaya (ala. 10)
– Mzee Mambo anapokea mshahara mkubwa lakin hana kazi yoyote – Yeye ni waziri kivuli.
– Wizara moja inaendeshwa na mawaziri wawili , Wizara ya Mipango na Mipangilio.
– Mzee Mambo halipwi mshahara, yeye huchota kwa sababu ya cheo chake.

- Wafanyakazi wanafika tu kazini na hawafanyi lolote, wanapokea mishahara
- Sasa na Mbura wanaendesha wizara kwa namna ya kujifaidi. Wao huadai wizara ni ya kuwaendesha tu.
- Sasa na Mbura wanafakamia chakula jinsi wenye uwezo wanavyopapia mali ya umma

(zozote 6 x 1 = 6)

**4. TUMBO LISILOSHIBA**

**MAJIBU**

- Wananchi wengine badala ya kuchukua hatua mwafaka dhidi ya wanyakuzi, hungojea wakati wao wanyakue k.v Sasa na Mbura
- Viongozi wananyakua mali ya mabilioni kwa hila na hawajali mf. Mzee Mambo anaandaa sherehe kubwa kwa sababu mtoto ameingia nasari na mwingine kuota vijino
- Watu walio karibu na viongozi kupewa vyeo ilhali wanyonge hawana kazi mf. Mzee Mambo ana vyeo viwili.
- Wanyonge kufanya kazi ngumu na nzito kwa malipo duni, sasa na Mbura
- Viongozi kutowajibika katika kuchunguza utenda kazi wa wafanyakazi wao kwani hushikiriza kwenda kazini na sio kufanya kazi jambo linalohujumu taifa kiuchumi.
- Wananchi kuchangia kuzorotesha uchumi wananchi kwa kufumbia macho unyakuzi unaoendelezwa na viongozi mf. Sasa na Mbura.
- Magari ya serikali kutumika katika sherehe za kibinafsi badala ya kuwahudumia wananchi. Mf. Kubeba mapambo nk.
- Viongozi kutochunguza ubora wa vyakula vinavyokuja shereheni. Vinaweza kuwa hatari kw binadamu
- Watu kunyongana na kuuana ili wapate shibe hasa mataifa yanayoendelea.
- Wenye hadhi ya chini kuruhusiwa kutwaa vyao baada ya mabwanyenye kujinyakulia vyaomf. Sasa na Mura
- Viongozi wa mataifa yanayoendelea kutowajibikia kazi zao. Wanakubali bidhaa duni kurundikwa katika mataifa yao mf. Mchele wa basmati.
- Mali ya umma kunyakuliwa . Dj anafungua duka la dawa zilizotolewa katika bohari ya serikali huku wanyonge wakiteseka .
- Serikali kuwalipa watu ambao hawafanyi kazi mishahara mikubwa hivyo kudhoofisha uchumi mf. Mzee Mambo
- Kituo cha televisheni ya taifa kupeperusha matangazo ya sherehe ambazo hazina umuhimu wowote katika ujenzi wa taifa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MAJIBU YA TUMBO LISILOSHIBA**

**Jadili jinsi maudhui ya umaskini yalivyoshughulikiwa katika hadithi ya Tulipokutana tena.**

**5.** **(a)** watoto kukosa elimu mfano: wazazi wa Bogoa wailishindwa kumwelimisha

- Wazazi kishindwa kuwalea watoto wao.
- Kudharauliwa kwa watoto maskini
- Watoto wa maskini kufanyishwa kazi za sulubu
- Maskini kukosa mavazi
- Kukosa nauli
- Watoto wa maskini kudhulumiwa
- Maskini kubaguliwa (Pogogo ni ya watu wa chini)
- Watoto kuwalaumu wazazi wao – Bofoa hapendi wazazi
- Maskini wanalaumiwa bila hatia - waliokosa kuenda shule walidhaniwa watoto
- Ukosefu wa upangaji uzazi unazidisha umaskini.

Mame Bakari

(b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na changamoto nyingi. Tetea (alama 10)

- Tukio la kubakwa linampotezea fahamu na anaaibika anapozinduka na kujipata akiwa uchi
- Mwanamke kujeruhiwa – Sara anavuna damu nyingi
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa
- Kukatizwa masomo
- Kukejeliwa – mwalimu mkuu
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara ana mawazo mengi
- Mwanamke kubebeshwa mimba katika umri mdogo
- Kuogopa kutoa habari ya kubakwa kwa wazazi kwa zababu hawangemwamini
- Kuishi maisha ya kimaskini

– Kulaumiwa hata kama ni yeye aliyebakwa

**KIGOGO - PAULINE KEA**
**MAJIBU**

6. (a) Haya ni maneno katika fikra za Majoka
   - Ni babu anayeongea
   - Babu anamwambia Majoka kuwa lazima aisome bahari na kusonga mbele kwa mpango (yaani aangalie hali iliyoko nchini kutokana na utawala wake mbaya) kwani hana budi kuishi
   - Majoka ako hospitalini kwenye chumba cha wagonjwa ambapo anahudumiwa na daktari na nesi.

   (3 x1 )

   (b) (i) Takriri - ajali , ajali
   (ii) Jazanda/ istiari - ajali - mabaya (kumng'oa mamlakani)

   (c) Babu - Amezinduka
   - Mkweli
   - Mshauri mwema
   - Mwenye tahadhari
   - Mwenye hekima
   - Mwenye matumaini uk 81/82 hatuna budi kuishi Zozote 4 x 1

   (d)
   - Majoka aliua Jabali – kifo hiki kinamwandama (asema wanaililia damu yangu)
   - Majoka hakujali furaha ya kuoa mtu apendaye alioa Husda kutimiza wajibu ajutia kumwoa mnafiki.
   - Majoka alifungulia biashara ya ukataji wa miti watu wakaathirika na kuusumbua uongozi wake
   - Majoka alikosa kushughulikia suala la mihadarati ikaangamiza mwanawe Ngao junior.
   - Majoka alipuuza kesi ya babake Tunu hivyo Tunu akasomea uanasheria na baadaye kuongoza maasi dhidi yake.
   - Majoka aruhusu kemikali kumwagwa sokoni – wachuuzi wanaunga kumpiga
   - Raia walibugia pombe waligeuka kuwa vipofu na hata wengine kufa.
   - Mama Pima aliuzia watu pombe bila kujali ikawadhuru vilevile ajutie kuuza pombe
   - Ngao junior anaamua kutumia mihandarati ambayo mwishowe inamfisha.
   - Husda kuongozwa na tama ya mali kuolewa na Majoka – baadaye anahuzunika wakati Majoka anamwambia ukweli kuwa yeye alipenda mali yake si Majoka (8 x 1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TAMTHILIA YA KIGOGO**

7. (a) Kinaya cha maneno yaliyopigiwa mstari
   - Uchaguzi wa mazingira - majitaka kuelekezwa wanakofanyia kazi wanyonge
   - Kusherekea mwezi mzima uhuru badala ya kufanya kazi.
   - Kupujua thamani ya elimu na kutobuni nafasi za kazi. Vijana wanahitimu chuoni na kufanya kazi duni k.v kuchonga vinyago.
   - Wanyonge kufungiwa soko la Chapakazi.
   - Maandamano kukabiliwa kikatili – Polisi kuwatawanya kwa risasi.
   - Wafanyakazi katika kampuni ya majoka hawana bima ya afya.
   - Kuendeleza ubaguzi – watu kupata uongozi kutokana na ukoo. Ngao Junior anatarajiwa kurithishwa uongozi na majoka.
   - Mwanamke kutopewa nafasi ya uongozi. Majoka anapinga Tunu.
   - Unyanyasaji wa kijinsia - Majoka kumdharau kewe kwa kumwita mwanamke.
   - Kuwaangamiza wapiganiaji haki. Jabali anauwawa.
   - Majoka kuvipangaza vizazi vya kesho deni kutoka kwa wafadhili. Anatumia msaada huo kuchonga sanamu.
   - Kuwatekeleza vijana kwenye matumizi mabaya ya vileo – Shuleni vijana wanadungana dawa na kuwa makabeji
   - Kuwapiga na kuwaumiza wapigania haki. K.v Tunu.
   - Kuongeza mshahara na hapo hapo kuongeza kodi ya walimu na wauguzi.
   - Kupandishwa bei ya chakula katika kioski cha kampuni.
   - Wanasagamoyo kulipa kodi na hali soko halisafishwi.
   - Kuwarithisha mbinu hasi za uongozi k.v matumizi ya hongo Majoka anamgawia Kenga ardhi.

- Uharibifu wa mazingira mfano ukataji miti.
- Serikali kutoa kibali cha kuuza pombe haramu kwa Asiya.
- Baadhi ya raia wanalazimika kula uroda ili wapewe kandarasi ya kuoka keki k.v Asiya.
- Baadhi ya wanasagamoyo wanatishiwa wahame kwa kutupiwa vijikaratasi.

(c)

- Kutoa tonge kinywani - Husda anatumia jazada kumaanisha kuwa mumewe ambaye anashuku kuwa tayari amenyakuliwa na Ashua. Ni kutokana na hali ambapo yuko tayari kumshambulia mwanamke huyu.
- Kuku na kanga (uk 28) – Husda anatumia kama njia ya kuonyesha kuwa, kama Ashua ameshindwa kumtuza mumewe, ataweza kumtuza Majoka ambaye ni wa kiwango cha juu akilinganishwa na mumewe Ashua, bwana Sudi.
- Vidhibitimwendo (uk. 33) – hii ni ishara ya kuwazua Tunu na wengine wanaoongoza maandamano kukomesha tabia hii yao, na hatimaye kumaliza kabisa
- Kuweka mahali pao (uk. 34) – hapa Kenga anamaanisha yuko tayari kuwau wote wanaoongoza maandamano na wanaopinga utawala wa Majoka mmoja baada ya mwingine hadi waishe.
- Kuota mizizi, kukita na kumea pembe (uk. 35) – Kenga anatumia kumwonyesha Majoka kwamba Tunu na wapinzani wengine wa mzee Majoka walianza mambo polepole kisha baadaye wakapata nguvu zaidi hadi sasa wanatekeleza vitindo vinavyonda kinyume na matakwa ya Majoka bila woga wowote kama vile kuandaa maandamano.
- Kutotumia bomu kuulia mbu (uk. 35) – Majoka anamfahamisha Kenga kwamba hakuna haja ya kutumia nguvu nyingi kupambana na wapinzani wake kama vile akina Tunu. Kwake anawaona wakiwa watu wadogo sana ambao wanahitaji nguvu kidogo kuwaangamiza.
- Kucheza na simba anayenyonyesha (uk. 37) – samba ni ishara ya Majoka ambaye ni hatari kama samba, huku kutia mikono katika mdomo wa samba ni ile hali ya Tunu kuingilia uongozi wa Majoka kwa namna ya kutaka kuuporomosha. Hapa Majoka anamwonya Tunu kwamba ni hatari sana kuingilia utawala wake kwa njia hii.
- Bahari mchafukoge – ni jazanda ya mambo kumwendea mrama Sudi. Kenga anamaanisha Sudi atakumbwa na matatizo au changmoto kali za kimaisha iwapo hataacha kuingilia maswala ya uongozi mbaya wa mzee Majoka.
- Keki ya taifa – ni raslimali za nchi ambazo zinanuiwa kuwanufaisha watu wote katika jamii ya sagamoyo. Raslimali hizi zinawafaidi watu wachache kama vile Majoka na vibaraka wake.
- Makombo ya keki ya uhuru – (uk. 17) ni jazanda ya raslimali chache wanazopata watu kutoka kwa viongozi.
- Asali – ni jazanda ya mapenzi kuja kwa Ashua kunamfanya majoka kumwona mwanamke huyu kama mtu anayetaka maswala ya mapenzi kutoka kwa Majoka.
- Kutafuta nyuki – ni jazanda ya kutafuta mapenzi/mwanamume ili amkidhie mahitaji yake ya kimwili
- Ala moja haikai panga mbili – ala inaashiria Ashua nazo panga mbili ni Sudi na Majoka. Majoka anamfahamisha Ashua kuwa wanaume wawili hawawezi kuwa na mwanamke mmoja. Kwa hivyo Ashua achague kuishi na mmoja wao.
- Milango i wazi – (uk. 23) Majoka anatumia kwa Ashua kama mbinu ya kumwonyesha kwamba, ingawa ameolea yuko tayari kumchukua na kukaa naye.

8. (a)
   - Gharama kubwa ya utafiti
   - Kushukiwa na wanajamii
   - Mafanani wanaweza kudai malipo
   - Ukosefu wa usalama
   - Upungufu wa wakati
   - Vikwazo vya kimawasiliano /lugha
   - Kutojitolea kwa wanajamii kushiriki utafiti
   - Mtafiti kukataliwa na wanajamii (alama 8)

   (b)
   - kuhifadhi siri
   - Kukuza uhusiano
   - Kukuza utangamano
   - Kutambulisha kundi
   - Kutafsidi lugha



for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Kukuza lugha
- Kuongeza ladha katika lugha
- Kuhifadhi historia ya utamanduni
- Kuondoa urasmi katika mazungumzo
- Kusawiri mpangilio wa jamii kiuchumi (alama 6)

(c)
- Kuwasilisha ujumbe mzito
- Kutenganisha matukio
- Kuondolea hadhira ukinaifu
- Kushirikisha hadhira
- Kurefusha hadithi ( kuendeleza hadithi)
- Kipumuo, kupunguzia hadhira uchovu wa huzuni
- Kuipa hadhithi toni Fulani
- Kuangazia maadili katika hadithi (alama 6)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA – MECS II**
**102/1**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 1**
**Insha**
**Muhula Wa Pili**

1. Lazima
   Wewe ni kiongozi wa wafanyakazi (wasio walimu) katika Shule ya Upili ya Baraka. Wengi wao wamejiingiza katika visa vya utovu wa nidhamu wakiwa shuleni. Waandikie memo kuwaonya dhidi ya tabia hii.

2. Kukaa nyumbani kwa muda mrefu sana bila kwenda shuleni kulileta athari mbaya kwa wanafunzi. Eleza.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
   Daraja ukilibomoa ujue kuogelea.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Nilitoa simu yangu mfukoni na kuipokea bila kuangalia ni nani alikuwa akinipigia. Nilipoipokea, ilinidondoka……

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA – MECS II**
**102/2**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 2**
**Muhula wa Pili - 2020**
**Muda: Saa 2½**

1. **UFAHAMU :** (Alama 15)
   *Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.*

Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inafaa na inayopatikana kwa urahisi. Isitoshe , mtoto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile: iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo.Mtoto hapaswi kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Vile vile , mtoto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia mtoto ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali. Pamoja na hayo anastahili kupendwa na kuheshimiwa kimawazo na kihisia.

Haki za watoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababu serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi husika.Yeyote anayezikiuka anapasa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria .Walakini , haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi wa hawa wamejipata wakiselela kwenye mitaa na hata majaa ya mji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula: licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi: kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusitikisha ni kwamba wale wanaotarajiwa kuwa **vigogo** wa kuzilinda haki hizi ndio wanaoongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kinjinsia, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasi huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile mjomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

Madhila yanayowapata watoto hayatokei tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru. Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana.Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi ambayo **huwa nanga kwao** kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kijinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni. Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi na walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapojitahidi kujinyanyua na **kujikuna wapatapo** kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasi hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. **Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kama kwamba ni waota ndoto za mchana.**

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe ttufanye hima tuungane mikono na kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Twapaswa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma , mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati.

(a) Huku ukitoa mifano **minne**, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. (alama 4)

(b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

(c) Kwa kurejelea aya ya nne , onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (alama 3)

(d) "Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatayo kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) Vigogo…………………………………………………………………………………………

(ii) Huwa nanga kwao………………………………………………………………………………

(iii) Kujikuna wajipatapo……………………………………………………………………………

**2.** MUHTASARI (Alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha,kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa Fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huadhirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwana methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upizani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watuwengine wengi pasiwe na upizani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa.kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo Fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano kitabu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele Fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano , neno ‘mwerevu ‘huweza kuwa na maana kwa kuweka katika muktadha wa ‘mjinga’, ‘mjanja’, ‘hodari’, na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknologia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kianachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali Fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia Fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55-60) (alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

Nakala safi

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100-110) (alama 10, 2 za utirriko)

Matayarisho

.**Nakala safi**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

(a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

(i) /t/ /s/

(ii) /h/ /gh/

(iii) /o/ /u/

(iv) /b/ /a/

(b) (i) Mzizi ni nini? (alama 1)

(ii) Toa mfano wa kitenzi chenye mzizi huru. (alama 1)

(c) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

N+RH+t+E

(d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 2)

Kiokoteni

(e) Andika katika ukubwa. (alama 1)

Paka hawa wamemfukuza mbwa wetu.

(f) Taja matumizi mawili ya kiambishi /e/ (alama2)

(g) Andika upya ukifuata maagizo. (alama 3)

(i) Maji ambayo wanakunywa ni hatari. (Andika katika hali ya mazoea bila kutumia amba)

(ii) Watu wengi <u>walihasirika</u> bomu <u>lilipolipuka</u> katika jengo hilo. (Tumia nomino badala ya vitenzi vilivyopigwa mstari.)

(iii) Pombe hiyo ilimfanya kuwa <u>kipofu.</u> (Tumia kitenzi badala ya neno lililopigiwa mstari)

(h) Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi kinachofanya kazi ya kielezi. (alama 2)

(i) Bainisha aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Wao si wahalifu ingawa walikuwa msituni walipokamatwa.

(j) Tunga sentensi ukitumia nomino <u>waya</u> pamoja na kivumishi cha pekee cha kusisitiza. (alama 2)

(k) Andika katika usemi halisi. (alama 2)

Hamisi alimwambia nyanya yake kuwa siku hiyo hakuwa na nafasi lakini angemtembelea siku ambayo ingefuata.

(l) Changanua kwa jedwali. (alama 2)

Mwenye njaa hana miiko.

(m) Taja matumizi mawili ya parandesi. (alama 2)

(n) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu / dhamira yake. (alama 1)

Rais amepiga marufuku ukataji miti nchini.

(o) Andika katika umoja. (alama1)

Hao wameharibu nyua zilizotengenezwa kwa mbao.

(p) Andika katika wakati uliopita hali timilifu (alama 1)

Miti katika msitu huo inakauka.

(q) Andika upya ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
<u>Nyanya</u> <u>alisomba</u> taka na kuitia katika <u>jaa</u> lililo <u>shambani.</u>
(r) Huku ukitoa mifano mwafaka taja miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U/I (alama 2)
(s) Tunga sentensi ukitumia **<u>na</u>** kama: (alama 2)
(i) Kihusishi
(ii) Kuonyesha umilikaji
(t) Onyesha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Polisi ambao walikuja juzi waliwakamata majambazi wote jana jioni.
(u) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana mbili za neno **<u>muhali.</u>** (alama 2)
(v) Andika methali inayoafiki maelezo yafuatayo .
Ni afadhali kupata matatizo madogo kwa sasa ili kuyaepuka mengi baadaye.

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha
(i) Mazingira (alama 2)
(ii) Mada (alama 3)
(iii) Hali (alama 2)
(b) Fafanua sera tatu ambazo zimepitishwa na serikali zinazochangia kuimarika kwa lugha ya Kiswahili. (alama 3)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA – MECS II**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

**<u>SEHEMU A: USHAIRI</u>**

1. **LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

**Wanaume ni wanyama**

1. Nakumbuka vyema sana,sisahau siku ile
Nilipoitwa na nina,akanipa ya kivyele
Mwanangu umsichana,nakuasa usikile
Si watu waone,wanaume ni wanyama.

2. Kuwa umevunja ungu,ni hali ya maumbile
Bora uwapo na bongo,anasa uzikimbile
Ukijitia maringo,utatungwa mimba mbele
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

3. Ngawa waje na manoti,"Nakupenda"wakwambile
Wakuvalie makoti,usiwaachie mbele,
Hata wapige magoti,wambile mna kelele
Si watu waone vile,wanaume ni wnyama.

4. Ngono ni tendo la suna, Amina sikimbilile
Wala miguu halina,kwamba lingekukimbile
Muhimu kwako Amina,kwanza uthamini shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

5. Kuzurura mitaani,si tabia njema ile
Unapotoka nyumbani,fululiza hadi shule
Si kwenda vichochoroni,kuwaona kina wale

Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

6. Uwe mwana msikizi,yano uyazingatile
Mengine kuhusu penzi,mwanangu taonywa shule
Kama marneyo mzazi,nimekuonya kimbele
Si Watu waone vile,wanaume ni wanyama.

7. Wakaja kina Hamadi ,mwana wa Mzee sule
Kwangu wakapiga hodi,hata mkuu wa shule
Ila nikajitahidi,kukwepa mitego ile
Si watu waone vile,wanaume ni wanyama.

8. Na kuna huyo Karisa, mwanafunzi kule shule
Akawa hunipapasa, name pia ile vile
Mwishowe ikatupasa,tugawe tunda tule
Si watu waone vile,wanaume ni wanyama.

9. Nani akachovya uto,wa asali tamu vile
Na kisha aape kuto, kula asli milele
Kuwa ni mjamzito,wamenifukuza shule
Si watu waone vile, wanaume ni wanyama.

10. Karisa yu vilevile,angali yuwaenda shule
Na mie kitumbo mbele,ninajikuna upele
Yameshatimia yale,niloonywa siku ila
Si watu waone vile,wanaume ni wanyama.

**MASWALI**

a) Tambua nafsineni katika shairi. Thibitisha. (ala. 2)
b) Eleza mambo **sita** ya nafsineni kama ushauri kwa msemewa. (ala. 6)
c) Fafanua umuhimu wa aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (ala.2)
d) Andika mifano ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (ala. 3)
   i) Jazanda/sitiari
   ii) Swali la balagha
   iii) Tashihisi/uhaishaji
e) Eleza mbinu **tatu** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (ala. 3)
f) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari (ala. 2)
g) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (ala. 2)
   i) Mpangilio wa vina katika beti
   ii) Idadi ya vipande katika mshororo.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B: RIWAYA**
**A.matei:Chozi la Heri**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. " Alishagaa jinsi ulimwengu unavyoweza kummeza binadamu,akawa hata hawawazii vifaranga wake.
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
   ii) Bainisha mbinu ***mbili*** za kimtindo ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (ala. 2)
   iii) Eleza sifa ***nne*** za anayerejelewa na dondoo hili. (ala. 4)
   iv) kwa kutolea mifano ***kumi*** kutoka riwayani,thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari. (ala. 10)

3. a) Onyesha jinsi matumizi ya majazi katika "chozi la Heri' yanaafiki na vilevile kinyume (kinaya) ukirejelea maeneo na wahusika hawa. (ala. 15)
   i) Wahafidhina
   ii) Subira
   iii) Mwanaheri
   iv) Msitu wa Heri

b) Changanua aina za taswira katika dondoo lifuatalo. (ala 5)
"Ridhaa alisimama kwa maumivu makali,mikono kairudisha nyuma ya mgongo wake uliopinda kwa uchungu....akawa anatazamana ana kwa ana na tanuri la moto….anakumbuka kupepesa kwa jicho lake kulia…Anakumbuka anguko ambalo alianguka sebuleni mwake,akatafuta kilichochomfanya kujikwaa…Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba yake ya nyumbani adhuhuri ya juzi ile.Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: TAMTHILIA**
**P. KEA: Kigogo**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. a) "Nafikiri mimi nawe twasoma kurasa tofauti sana."
   Eleza tofauti baina ya wahusika wanorejelewa. (ala.10)
   b) Majoka bin Marara ni kiongozi mwenye hila. Fafanua. (ala. 10)
5. "…huwezi kujipeleka kwenye pango la joka katika hali hii yako."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
   b) Eleza mbinu ya kimtindo iliyotumika hapa. (ala. 2)
   c) Eleza umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (ala. 4)
   d) Thibitisha namna wahusika mbalimbali walivyojipeleka kwenye pango la joka. ( ala. 10)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
**A. Chokocho na D. Kayanda(Wah): Tumbo Lisiloshiba**
**na Hadithi Nyingine**
**Jibu swali la 6 au la 7**

**D. Kayanda: Mwalimu Mstaafu.**

6. a) "Samahani mwalimu,nimekuumbulia jina bilashi.Uniwie radhi sana. Samahani sana" " Kwani kulikoni?"
   i) Eleza muktadhaa wa dondoo hili. (ala. 4)
   ii) Tambua mbinu ***mbili*** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (ala. 2)
   iii) Eleza namna wahusika mbalimbali walivyoumbuliwa katika hadithi hii. (ala 7)
   b) Eleza jinsi maudhui ya malezi yanavyojitokeza katika hadithi. "Tulipokutana Tena." (ala. 7)

**E. Kimaliro: Mtihani wa Maisha**

**7.** a) "Mpita njia huyu anabaini punde kwamba pana mambo na mambo ni kangaja huenda yakaja."
   Thibitisha ukweli wa dondoo hili ukirejelea hadithi ya "Mtihani wa maisha" (ala, 8)
   b) Onyesha madhara ya ubakaji ukurejelea hadithi ya " Mame Bakari' (ala. 12)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Mjukuu wangu kumbuka mtoto mzuri siku zote huwa ni mfano manga katika nyumba; hupendeza kila mtu, si mkubwa mdogo. Hatendi mambo ambayo huleta mregemrege kwa yeyote. Pia hafanyi mambo yaendayo upogo kwani hukuna sana kichwa chake kabla ya kutenda. Binadamu mzuri hapendi kubwatabwata maneno,huficha siri kama kaburi. Jaribu kuwa mvumilivu ambaye mwisho hula mbivu. Tendea wenzako mema kwa kuwa wema hauozi. Pendana na watu wa viwango vyote huenda wakakufaa,wakikutenga utateseka, jifya moja kumbuka haliinjiki chungu. Jaribu kuwa msamehevu na ulinde mdomo wako. Kumbuka ni heri kujikwaa dole kuliko kujikwaa ulimi. Ukisema ovyo na ukitenda maovu utakuwa kama mtu apandaye upepo na kuvuna tufani.Penda au taka kwa kiasi, usivuke mipaka kwani tamaa nyingi mwisho ni mauti. Ya nini kutaka vitu vya ufahari kwa vishindo? Kupata kuna Mungu na pia ukitia bidii na ukiwa muaminifu kazini utafanikiwa mwisho kabisa,tii wazazi wako,radhi ni bora kuliko mali. Maombi yao yatasaidia kufungua milango yote ya heri na utaishi kwa furaha ghaya hata mpaka majirani wakuonee gere.

## Maswali

a) Ainisha kipera hiki cha mazungumzo kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (ala.2)

b) Eleza mambo ***manne*** anayoambiwa msemewa na nafsineni. (ala. 4)

c) Bainisha mbinu ***nne*** za kimtindo katika mazungumzo haya. (ala. 4)

d) Mbali na matumizi ya lugha fasaha, Eleza mikakati ***minne*** ambayo mzungumzaji angetumia kufanikisha uwasilishaji. (ala.4)

e) Unanuia kutumia hojaji kufanya utafiti kuhusu mazungumzo ya aina hii. Eleza sababu ***sita*** za kuchagua mbinu hii. (ala 6)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA -MECS** II
**Muhula wa Pili - 2020**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 1**

1. **Swali la lazima**

Vipengele viwili vikuu vya insha hii ya kiuamilifu vishughulikiwe.
- a) Muundo/sura
- b) Maudhui

**a) Muundo**

Mtahiniwa azingatie vipengele vifuatavyo:

i) Nembo na anwani ya shule ya Baraka (iandikwe juu katikati mwa karatasi)
ii) Nambari ya marejeleo/kumbukumbu ya marejeleo
iii) Tarehe – inaweza kuandikwa pambizoni kwenye mstari mmoja na nambari ya marejeleo.
iv) Mtajo
- a) Kutoka kwa : Kiongozi wa wafanyikazi
- b) Kwa : Wafanyakazi wote.

v) Mada/kuhusu: Utovu wa nidhamu.
vi) Utangulizi- mtahiniwa atangulize kiini cha memo.
vii) Mwili – Hoja zijadiliwe na ziwekwe ki-aya
viii) Hitimisho
Ahitimishe insha yake k.m. kujumuisha hatua ambazo zitachukuliwa kwa atakayeendelea kuwa mtovu wa nidhamu shuleni.
ix) Kimalizio
- a) Sahihi
- b) Jina
- c) Cheo (ingawa si lazima)
- d) Nakala kwa

**b) Maudhui**

Mtahiniwa aandike hoja zinazohusiana na nidhamu kazini. Mifano.
- i) Wizi wa vitu vya shule.
- ii) Kuchelewa kufika kazini.

iii) Kuondoka kazini mapema.
iv) Kuzembea kazini.
v) Kukosa kufika shuleni bila ruhusa.
vi) Kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.
vii) Kuletea wanafunzi dawa za kulevya.
viii) Kutoa siri za shule.
ix) Matumizi mabaya ya mali ya shule.
x) Kuchochea wanafunzi kugoma.
xi) Kutumia vileo wakiwa kazini.
xii) Kuweka mafuta ya taa katika chakula cha wanafunzi.
xiii) Kufanya biashara haramu na wanafunzi km kuwapa simu zao waongee na marafiki zao kwa malipo.

**Hitimisho**

Ihusiane na mada. Inaweza kujumuisha hatua za kinidhamu kulingana na sheria za shule. Anaweza pia kuwahimiza wafanyakazi kuzingatia nidhamu kazini – ili kuboresha utendakazi wao.

**Tanbihi**

1. Mtahiniwa asipokuwa na sura ya memo aondolewe alama 4S.
2. Akiwa na sura bila maudhui atuzwe D+ 04/20
3. Mtahiniwa anastahili kutumia lugha yenye toni kali au kuhimiza nidhamu kazini.
4. Anaweza kufafanua kosa na wakati uo huo ataje hatua ya kinidhamu.
5. Anaweza kufafanua makosa kisha ataje hatua za kinidhamu

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

6. Athari mbaya kwa wanafunzi kutokana na kukaa nyumbani kwa muda mrefu sana

Baadhi ya hoja ni:
i) Wasichana wengi walipata mimba.
ii) Wengine kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.
iii) Wengine kusahau masomo.
iv) Kujiingiza katika ndoa za mapema.
v) Ajali na vifo kutokana na ukosefu wa ulinzi mzuri nyumbani.
vi) Kujiingiza katika vikundi haramu.
vii) Baadhi yao kuamua kufanya vibarua kuliko kurudi shuleni.
viii) Kuwa na migogoro nyumbani na kulazimika kutoroka nyumbani.
ix) Kujiingiza katika maovu ya kila aina km ukahaba.

**Tanbihi**
Mtahini atathmini hoja za mtahiniwa.

7. Hii ni insha ya methali

Mtahiniwa abuni kisa kinachodhihirisha maana ifuatayo: Ukiharibu au kupoteza kitu ambacho kinakufaa, utafute namna ya kujisaidia ukipata shida ya kitu hicho. Mfano:

- Kuharibu kazi Kisha ukafutwa kazi na kukosa riziki.
- Kuvunja uhusiano na familia au ukoo hatimaye wakakutenga.
- Mwanafunzi kuharibu uhusiano na walimu au wazazi wake wanaomsaidia.
- Nchi kuvunja uhusiano na nchi zingine zinazoisaidia kueneza utalii au kufanya biashara.
- Mtu kuharibu uhusiano wa kirafiki na marafiki zake waliokuwa wakimwelekeza au kumsaidia.
- Kuchoma shule na unahitaji kusoma.

**Tanbihi**

1. Kisa kionyesha hali/pande mbili:
   i) Kubomoa daraja (kuharibu uhusiano)
   ii) Kujua kuogelea (kutafuta/ kuwa na namna ya kujisaidia ukihitaji mtu au kitu hicho)
2. Mtahiniwa atakayerejelea upande mmoja tu amepungukiwa kimaudhui.
3. Atakayeandika kisa kisichohusiana kamwe na methali hii amepotoka kimaudhui.

4. Mtahiniwa abuni kisa kinachoanza na kuafikiana na maneno aliyopewa.
   Kisa kionyeshe tukio ambalo linasababisha hali ya simu kumdondoka km Mshtuko au mshangao kutokana na majonzi au furaha.

**Tanbihi**

- Mtahiniwa baada ya kuandika kauli ya kwanza anaweza kutumia mbinu rejeshi.
- Kisa kinaweza kusimuliwa katika nafsi ya kwanza, ya tatu au mchanganyiko wa nafsi zote tatu.

**MTIHANI WA PAMOJA – MECS II**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**102/2**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 2**
**Muhula wa Pili – 2020**

**1. UFAHAMU :** (Alama 15)

(a) Huku ukitoa mifano **minne**, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. (alama 4)

- ***Watoto wananyimwa haki licha ya katiba kulazimu haki hizi kutimizwa***
- ***Mojawapo ya haki za kimsingi ni makazi. Ilihali watoto wanalala mitaani***
- ***Watoto hawapati chakula ilhali wanapaswa kupata lishe bora***
- ***Wanaotakiwa kulinda haki za watoto ndio wanaozikiuka(vigogo)***
- ***Wazazi na jamaa wa karibu wanashiriki katika unyanyasaji wa watoto.***

***Alama 4x1=4***

(b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

- ***Watoto hutekwa na kutumikishwa vitani***
- ***Watoto wanageuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana***
- ***Watoto huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili***
- ***Hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi/ kubeba bunduki nzito***

***Alama 3x1=3***

(c) Kwa kurejelea aya ya nne , onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (alama 3)

- ***Serikali / viongozi walikuwa na shabaha ya elimu kwa wote***
- ***Serikali kubuni sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi***
- ***Utekelezaji wa sera hii unaendelea***
- ***Kunao wanaopigania haki ya kuwa na elimu bila malipo licha ya matatizo yaliyopo ambao wanaonekana kama waota ndoto mchana***

***Alama 3x1=3***

(d) "Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

- ***Asilimia ya watoto na watu wazima wasiojua kusoma ni kubwa***
- ***Kuwepo kwa idadi ya watoto wasioenda shuleni***
- ***Wazazi wapojitahidi kujinyanyua hujipata katika kinamasi cha ulitima***
- ***Watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia katika kiza cha ujinga***

***Alama 2x1=2***

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatayo kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) Vigogo

- ***wabingwa/ wenye mamlaka/ wanaopenda kuendeleza elimu ya watoto***
- ***viongozi / watetezi/ washika dau/ wanaopigania haki/ wakereketwa/ vinara/ walo mstari wa mbele/ watawala/ waopigania haki za watoto***

***Alama 1x1=1***

(ii) Huwa nanga kwao

- **Mazito/ mzigo/ uzani mkubwa/ kuwa mzigo kwao** ***Alama 1x1=1***

(iii) Kujikuna wajipatapo

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- **Kujitahidi kadri ya uwezo wao/ kujizatiti kulingana na uwezo/ kujaribu kujinyanyua kulingana na uwezo wake**
- **Lazima aweke uwezo**

***Alama 1x1=1***

**2.** MUHTASARI (Alama 15)

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55-60) (alama 5, 1 ya utiririko)

Nakala safi

1. **Maarifa huyadhibiti , huyaendesha, huyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu**
2. **Anayekosa maarifa huathirika pakubwa**
3. **Maarifa ni utajiri anaotumia binadamu kujifaidisha pamoja na wanajamii/ elimu ni mali/ msingi wa utajiri na maendeleo ni maarifa**
4. **Elimu ni chimbuko la maarifa**
5. **Maarifa hayana upizani**
6. **Kila mtu ana uhuru wa kutumia maarifa kuzalisha maarifa mengine**
7. **Utumiaji wa maarifa hauyamalizi**
8. **Maarifa hayagusiki** **Alama 8x1/2 =4**

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100-110) (alama 10, 2 za utirriko)

**Nakala safi**

- **Maarifa huingiliana na maarifa mengine/ maarifa aliyonayo mtu mmoja huweza kuhusishwa nay a mwingine**
- **Maarifa yanaweza kuhamishwa/ maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine**
- **Maarifa yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo mingine ya kidhahania**
- **Maarifa yanaweza kugeuzwa / kubadilishwa na kuwa ishara ambazo hufanywa / huyafanya kuwasilishwa kwa njia ya nyepesi**
- **Yana sifa ya uhusianaji**
- **Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana**
- **Hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa yasisambae / huenea haraka**
- **Huepuka pingu za watu kuwadhibiti wenzao**
- **Maarifa ni nguvu inayoshinda nguvu zote**

**Alama 8x1=8**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

(a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

(i) /t/ /s/
- ***/t/ kipasuo /s/ kikwamizo***

(ii) /h/ /gh/
- ***/h/ hutamkiwa koromeo /gh/ kaakaa laini***

(iii) /o/ /u/
- ***/o/ irabu ya wastani /u/ irabu ya juu***

(iv) /b/ /a/
- ***/b/ konsonanti /a/ irabu***

***Alama 4x ½ =2***

(b) (i) Mzizi ni nini? (alama 1)
- ***Sehemu ya neno inayobeba maana kuu na ambayo haibadiliki***

***Alama 1x1=1***

(ii) Toa mfano wa kitenzi chenye mzizi huru. (alama 1)
- ***Hini , subiri , samehe n.k*** ***alama 1x1=1***

(c) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

N+RH+t+E

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| – **<u>Mtoto</u>** | ***<u>wa Juma</u>*** | **<u>yumo</u>** | **<u>chumbani</u>** | |
| **N** | **RH** | **t** | **E** | ***alama 4x1/2 =2*** |

(d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 2)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiokoteni | ***Ki-*** | ***okot-*** | ***e-*** | ***ni*** | |
| | ***Ngeli*** | ***mzizi*** | ***himizo*** | ***wingi*** | ***alama 4x ½=2*** |

(e) Andika katika ukubwa. (alama 1)

Paka hawa wamemfukuza mbwa wetu.

– ***Majipaka / mapaka haya yamelifukuza jibwa letu***

***Alama 1x1=1***

(f) Taja matumizi mawili ya kiambishi /e/ (alama2)

– ***Kauli somea, chomea, ombea***
– ***Rai/ himizo kasomeni ,mpikie, niambie***
– ***Kiambishi cha uundaji wa nomino mpambe, mshinde,***

***Alama 2x1=2***

(g) Andika upya ukifuata maagizo. (alama 3)

(i) Maji ambayo wanakunywa ni hatari. (Andika katika hali ya mazoea bila kutumia amba)

– ***Maji wayanywayo ni hatari***

***Alama 1x1=1***

(ii) Watu wengi <u>walihasirika</u> bomu <u>lilipolipuka</u> katika jengo hilo. (Tumia nomino badala ya vitenzi vilivyopigwa mstari.)

– ***Watu wengi walipata <u>hasara</u> kulipotokea <u>mlipuko</u> wa bomu katika jingo hilo***

***Alama 1x1=1***

(iii) Pombe hiyo ilimfanya kuwa <u>kipofu.</u> (Tumia kitenzi badala ya neno lililopigiwa mstari)

– ***Pombe hiyo ilimpofusha.*** ***Alama 1x1=1***

(h) Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi kinachofanya kazi ya kielezi. (alama 2)

***Mfano ;***

– ***Wezi walitoroka <u>walipowaona askari.</u>***

***Alama 2x1=2***

(i) Bainisha aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Wao si wahalifu ingawa walikuwa msituni walipokamatwa.

– ***Wao <u>si</u> wahalifu ingawa – t- kipungufu***
– ***<u>Walikuwa</u> msituni – t – kikamilifu***
– ***<u>Walipokamatwa</u> –halisi*** ***Alama 3x1=3***

(j) Tunga sentensi ukitumia nomino <u>waya</u> pamoja na kivumishi cha pekee cha kusisitiza. (alama 2)

***Mfano;***

– ***Waya wenyewe ndio uliotumiwa kufungia vitu hivyo***

***Alama 2x1=2***

(k) Andika katika usemi halisi. (alama 2)

Hamisi alimwambia nyanya yake kuwa siku hiyo hakuwa na nafasi lakini angemtembelea siku ambayo ingefuata.

– ***"Sina nafasi leo. Nitakutembelea kesho." Hamisi akamwambia nyanya yake.***

***Alama 1/3 x6=2***

(l) Changanua kwa jedwali. (alama 2)

Mwenye njaa hana miiko

| | | | |
|---|---|---|---|
| **S** | | | |
| **KN** | | **KT** | |
| **W** | **N** | **t** | **N** |
| **Mwenye** | **njaa** | **hana** | **miiko** |

***Alama 4x1/2 =2***

(m) Taja matumizi mawili ya parandesi. (alama 2)

– ***Hutumiwa kutoa maelezo zaidi***
– ***Hutumiwa katika maandishi ya kitamthi /Kufungia ufafanuzi***
– ***Kufungia herufi ama nambari***

***Alama 2x1=2***

(n) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu / dhamira yake. (alama 1)

Rais amepiga marufuku ukataji miti nchini.

– ***Sentensi ya taarifa***

***Alama 1x1=1***

***(o) Andika katika umoja. (alama1)***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

***Hao wameharibu nyua zilizotengenezwa kwa mbao.***

– ***Huyo ameharibu ua uliotengenezwa kwa ubao*** ***Alama 1x1=1***

(p) Andika katika wakati uliopita hali timilifu. (alama1)
Miti katika msitu huo inakauka

– ***Miti katika msitu huo ilikuwa imekauka.*** ***(alama 1x1=1)***

(q) Andika upya ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
<u>Nyanya</u> <u>alisomba</u> taka na kuitia katika <u>jaa</u> lililo <u>shambani</u>.

– ***<u>Bibi aliokota/ alizoa</u> taka na kuitia katika <u>jalala</u> lililo <u>kondeni</u>***
***(alama 4x ½ =2 )***

(r) Huku ukitoa mifano mwafaka taja miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U/I (alama 2)

– ***Mwamvuli- miavuli ( mw-mi)***
– ***Mti-miti (m-mi)***
– ***Muwa-miwa (mu-mi)*** ***alama 2x1=2***

(s) Tunga sentensi ukitumia na kama: (alama 2)
***(i)*** Kihusishi ***Alishambuliwa na wezi.*** ***alama 1x1=1***
(ii) Kuonyesha umilikaji –***Yeye ana mali nyingi.*** ***(alama 1x1=1***

(t) Onyesha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Polisi ambao walikuja juzi waliwakamata majambazi wote jana jioni.
***Polisi ambao walikuja juzi-kiima***
***Majambazi / majambazi wote –shamirisho***
***Jana jioni-chagizo*** ***alama 3x1=3***

(u) Eleza maana mbili za neno muhali. (alama 2)

– ***Kutowezekana kwa jambo***
– ***Ghasia/ fujo (sharti atunge sentensi mbili)*** ***(alama 2x1=2)***

(v) Andika methali inayoafiki maelezo yafuatayo:
Ni afadhali kupata matatizo madogo kwa sasa ili kuyaepuka mengi baadaye

– ***Heri nusu shari kuliko shari kamili***
– ***Heri ya mrama kuliko ya kuzama***
– ***Heri kuwa kibichi kuliko kuungua*** ***(alama 1x1=1)***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha
(i) Mazingira (alama 2)

– ***Mazingira hudhibiti ishara zinazotumika.***
– ***Mazingira huathiri toni/ kiimbo***
– ***Mzungumzaji huchota msamiati kutoka anakozungumzia***
– ***Mazingira hudhibiti urasmi wa lugha***
***(alama 2x1=2)***

(ii) Madhumuni (alama 3)

– ***Mada huathiri uteuzi wa msamiati***
– ***Mada hudhibiti toni inayotumika***
– ***Usanifu wa lugha hutegemea kule kunakozungumziwa***
***(alama 3x1=3)***

(iii) Hali (alama 2)

– ***Hali ya mtu huathiri toni au kiimbo k.m. mtu mwenye huzuni hutumia toni ya chini***
– ***Muundo wa sentensi huathiriwa na hali ya mtu***
– ***Hali ya mtu yaweza kuathiri usanifu wa lugha.***
***(alama 2x1=2)***

(b) Fafanua sera tatu ambazo zimepitishwa na serikali zinazochangia kuimarika kwa lugha ya Kiswahili. (alama 3)

– ***Kiswahili kufanywa lugha rasmi***
– ***Kiswahili kuwa lugha ya taifa***
– ***Kiswahili kuwa somo la lazima shuleni***

– *Kiswahili kutumiwa bungeni kama lugha rasmi*
– *Kiswahili kutumiwa katika machapisho ya serikali*

(alama 3x1=3

**MECS II**
**FASIHI YA KISWAHILI NOV.2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. USHAIRI**

a) Mama yake mshauriwa (al.1)
"Kama mameyo mzazi, nakuonya ukimbilie." (al.1)

b) (i) akimbie anasa
(ii) asijitie maringo
(iii) asitungwe mimba
(iv) wanaume wakimwambia wanampenda awakimbie
(v) akitoka nyumbani afululize
(vi) asifanye ngono
(vii) asizurure mitaani
(viii) asitembee vichochoroni
(ix) ajiepushe na wanaume, ni wanyama

***(za kwanza 6 x 1=6 )***

c) (i) urudiaji wa silabi -k.m le,na,ti
Kujenga ridhimu /kulipa shairi muonjo/mdundo wa kimuziki/kuleta urari wa vina
(ii) urudiaji wa mistari/mishororo –k.m kibwagizo cha shairi. Kusisitiza wazo kuu/kuonyesha mtazamo wa nafsineni/kuchimuza toni ya shairi.

***(2 x 1=2) (Aina ½, Umuhimu ½)***

d) (i) Jazanda/Sitiari – wanaume ni wanyama.
(ii) swali la balagha – nani akachovya uto wa asali tamu vile?
(iii) Tashihisi/uhaishaji – wala miguu halina kwamba lingekukimbile
– "Ngono" inazungumziwa kama dude hai. ***(3 x 1=3)***

e) (i) Inkisari/kufupisha – ngawa- ingawa, mameyo- mama yako, taonywa- utaonywa
(ii) Tabdila - ukimbile- ukimbie, usikile- usikie, uzingitile- uzingatie.
(iii) kuboronga/kufinyanga/kubananga sarufi k.m kuzurura mitaani, si tabia njema ile – Ile tabia ya kuzurura mitaani si njema.

***(3 x 1=3)***

f) Uwe mwana unayesikia/msikivu wa kuzingatia unayoambiwa. Mambo kuhusu mapenzi utaonywa shuleni lakini nikiwa mama yako mzazi ninakuonya kimbele ujihadhari na wanaume kwa sababu ni wanyama.

***(4 x ½ = 2)***

g) (i) Ukara
(ii) Mathnawi

***(2 x 1=2)***

**2. CHOZI LA HERI**

a) (i) Msemaji ni mwandishi/msimulizi
(ii) Msemewa/ anamrejelea Dick
(iii) Dick yuko katika uwanja wa ndege wa Rubia
(iv) Anakumbuka jinsi mama yake alivyowaacha wakiwa wadogo. ***(4 x 1 =4)***

b) (i) Jazanda/Sitiari – hawawazii vifaranga wake.
(ii) Tashihisi/uhuishi – ulimwengu kummeza binadamu.

***(2 x 1=2)***

**c) Sifa za Dick**

– Mwenye bidii – anasafiri ng'ambo kuuza vifaa vya simu ; anajiendeleza kitaaluma.
– Mwenye msimamo imara – anapoamua kuacha uhalifu anafanya uamuzi wa mkataa.
– Mwenye busara – anaamua kubadilika na kuacha ulanguzi wa dawa za kulevya ; anaanzisha biashara ili kujikimu.
– Jasiri – anakabiliana na hali ya ulanguzi ; fikra za kwao zinapomjia na kutaka kulia anazidhibiti.



for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Mwenye matumaini – hata anapoingilia biashara ya ulanguzi, ana matumaini ya kupata mbinu ya kujinasua.
- Mwoga.
- Amewajibika
- Mshauri bora
- Mwenye shukrani
- Msomi

*(za kwanza 4 x 1=4)*

**d) <u>Vifaranga wanaweza kuwa</u>;**

- Mtu aliye chini ya mamlaka ya mwingine k.v. mwana kuwa chini ya mzazi wake.
- Mwenye umri mdogo kuliko mwingine.
- Maskini au mtu wa tabaka la chini.
- Asiye na mamlaka/cheo cha chini
- Anayehitaji msaada.
- Wafanyikazi.
- Wakimbizi/maskwota.
- Aliye na hali Fulani kama vile ugonjwa.
- Mtu aliyekumbwa na changamoto/udhaifu/ulemavu
- Aliye na kitembo duni cha elimu.
-

i) Kuwatoroka wanao/familia - Naomi anapomwachia lunga wanawe watatu wakiwa wadogo. Subira anawaacha wanawe wawili – Lime na mwanaheri

ii) kutelekeleza majukumu yao - Rehema mamake (chandachema) anamwacha aishi na bibi yake Fumba anapomwachia mamake jukumu la kumlea Chadachema na kupata familia nyingine/anahamia ng'ambo/Babake pete/Bw. Tenge.

iii) <u>Mapuuza</u> - Babake Kairu hashughuliki kukidhi mahitaji ya Kairu ilhali anajiweza.

iv) K<u>uwatumikisha</u> –wazazi wake Zohali wanampa kazi ya kuwa kijakazi baada ya kupata mimba.

v) <u>Kudhulumiwa</u>/kubakwa - Sauna anafanyiwa unyama na babake mlezi/mamake hamtetei

vi) <u>Kulanguliwa</u>/kutekwa nyara – Buda anamtumia Dick kama mlanguzi wa dawa za kulevya licha ya umri wake/ Sauna anatumiwa na Bi. Kangara kuteka watoto.

vii) <u>Kubaguliwa</u> – mamake Kaizari kumwona kama mgeni wa kumlaumu kumbwakura mwanawe/Selumu/Pete kudhalilishwa na wake wenza.

vii) <u>Kuachishwa masomo mapema</u> – Pete anaachishwa masomo ili kaka zake waelimishwe/kukatizwa

xi) <u>Kuozwa bila hiari</u> –Pete anaozwa na wajombaze na mamake bila hiari yake

x) <u>Kuavywa/kutupwa</u> – kitoto Riziki Immaculata kinatupwa na mamake na Neema anakiokota/pete anajaribu kuavya mimba

x) <u>Kuwakana wanao</u> – k.m Babake Kipanga/Babake Kairu/Babake sauna

xii) <u>Kufukuzwa</u> – Pete anafukuzwa na Nyangumi mkewe anaporejea/Fungo anamfukuza Pete.

xiii) <u>Kukosa kazi</u>/malipo duni – k.m Shamsi/wafanyakazi/hawaongezewi mishahara

xiv) Kutishwa – k.m Dick anatishwa na Buda

xv) Kupokwa mashamba yao k.m waafrika

xvi) Kudanganywa – km Pete anadanganywa na Nyangumi

xvii) Kupitia dhiki ya kisaikolojia – k.m chandachema, Ridhaa, Kaizari

xix) kuuawawa – k.m Lemi anauawa bila hatia

xx) Kufisidiwa – k.m wakimbizi wanafisidiwa na familia ya Bw. Kute.

xxi)Kuharibiwa mali yao – k.m Ridhaa anabomolewa nyumba yake

xxii) Kujazwa hofu – k.m akina Kairu,Kaizari

*(zozote 7 x 1 = 7)*

3. **a) <u>Mbinu ya majazi inavyoafiki na pia kinyume/kinaya</u>.**

**i) <u>Wahafidhina</u>**

Hili ni jina la kimajazi linaorejelea jamii isiyotaka kubadili mtazamo wa mambo au hali ya mtu kutopendelea kubadili. Jina hili ***linaiafiki*** wahafidhina kwanza. (ala. 2)

- Raia hawataki kiogozi wa kitaifa wa kike – Bi Mwekevu
- Raia wanashikilia tamaduni k.v upashaji tohara. - Tuama
- Mzee mwimo anaamini kwamba kukutana na mwanamke asubuhi ni nuksi.
- Kwamba mwanamume hastahili kulia – Mamake Ridhaa
- Wanategenea wakoloni hata baada ya miaka hamsini ya uhuru

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

- Kuna uhasama wa kiukoo k.v Anyamvua na waombwe
- Wasichana kama pete wanaozwa mapema/wanakatiziwa masomo. n.k

***Kama kinaya*** ***(alama. 2)***
- Wahafidhiwa wanamchagua kiogozi mwanamke.
- Wazee kama mzee msarifa wanapinga tohara ya wasichana

**ii) <u>Subira</u>** - ***ina maana ya kuvumilia*** ***(ala. 2)***
Inavyoafiki
- Anavumilia kuonewa gere na mama mkwe
- Anavumila unyama aliotendewa na vijana mabarobaro/anavumilia majeraha

***kama kinaya*** **(ala. 1)**
- Anashindwa kuvumilia katika ndoa yake na Kaizari na anaamua kuondoka

***iii) <u>Mwanaheri</u> – Heri ni afadhali*** ***(ala. 2)***
***Limemwafiki*** kwa njia zifuatazo;
- Anamfaa Umu pale shuleni na kumfanya aone mzigo wake kwa mwepesi
- Yeye na ndugu yake Lime wanarudi shuleni mlemle kijijini mwao.
- Anawafaa wanafunzi wenzeke kwa kipawa chake cha kughani mashairi.
- Anapedwa na wanafunzi wenzake
- Anapokea ushauri na nasaha baada ya kubakwa.

***Kama Kinaya*** ***(ala. 1)***
- Anabakwa akiwa pamoja na dadake Lime
- Mamake anaondoka na kuwaacha na baba yao.
- Anashuhudia mamake akidhalilishwa na wakweze.

***iv) <u>Msitu wa Heri</u> – ni baraka,neema, utulivu au fanaka.*** ***(ala 1)***
***Linaafiki kwani***
- Mzee Mwimo anasuluhisha migogoro ya familia kwa kuwahamishia wake wawili wa mwisho
- Huku kunampa Ridhaa marafiki wapya
- Ndiko Ridhaa anakoolea
- Ndiko Ridhaa anafanya bidii masomoni na kufanikiwa kielimu na kitaaluma.
- Ridhaa anawaletea heri wakazi kwa kuwaletea maji ya mabomba na kubadilisha mazingira

***<u>Kama Kinaya</u>*** **<u>(alama. 2)</u>**
- Ridhaa anatengwa shuleni
- Ridhaa anaitwa mfuata mvua
- Ridhaa anachomewa nyumba na familia yake
- Kaizari anavamiwa na mkewe kujeruhiwa na mabinti zake kubakwa.

b) **<u>Aina za taswira</u>**
i) Taswira hisi - …"mgongo wake uliopinda kwa uchungu.
ii) Taswira ya uoni – akawa anatazamana ana kwa ana na tanuri la moto/ anakumbuka kupepesa kwa jicho lake la kulia
iii) Taswira ya mwendo – anakumbuka anguka ambalo alianguka subuleni mwake.
iv) Taswira ya mguso – akatafuta kilichomfanya kujikwaa/jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba yake ya nyumbani
v) Taswira ya usikivu - anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama.

***(5x1=5;Aina - ½,Mfano - ½)***

**<u>4. KIGOGO</u>**
a***)Wahusika wanaorejelewa ni Tunu na Majoka wanatafautiana kama ifuatavyo. Msemaji ni tunu na msemewa na Majoka.***

| TUNU | MAJOKA |
|---|---|
| i) Ni mzalendo-analitetea jimbo lake kwa dhati dhidi ya dhuluma za Majoka<br>ii) Ni mwenye utu/huruma – anawahurumia Sudi,pendo na pili<br>**iii)** Msema kweli/mkweli – anamkabili Majoka na kumwambia ukweli kuhusu uogozi wake | **i)** Ni msaliti – anawanyanyasa Wanasogamoyo badala ya kuwaogoza vyema.<br>ii) Katili –anawaua wapinzani wake k.v Jabali<br>**iii)** Mwongo/Mnafiki – anajifanya kuwa na huruma huku akishirikiana na vikaragosi wake kuwadhulumu wananchi<br>**iv)** Mbinafsi/mwenye tamaa –anafunga soko ili ajenge |

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

| | |
|---|---|
| **iv)** Anajali – anawajali wanasagamoyo kwa kutetea masilahi yao<br>**v)** Jasiri –anamkabili Majoka ofisini bila kumwogopa<br>**vi)** Ni mwadilifu – anakataa vishawishi vya majoka k.v kujitenga na sudi,kuolewa na ngao Junior.<br>**vii)** Mtetezi wa haki – anawatetea wanyonge waliofugiwa soko.<br>**viii)** Mwenye msimamo thabiti anataka kuozwa kwa ngao Junior.<br>**xi)**Mwenye maadili mema- Hana uhusiano wowote na Sudi kama majoka alivyodai<br>**x)** Mwajibikaji –anawapeleka pili na pendo kwa mamake ili watunzwe kwa muda.<br>**xi)** Msamehevu – anakubali msamaha wa Mamapima.<br>**xii)** Mwenye hekima/busara –anagundua vishawishi vya Majoka kuvikataa.<br><br>**xiii)** Ni mnyenyekevu – anakubali kina Kenga Kingi na Asiya bila kuwakamata/kuwashutumu. | hoteli ya kifahari<br>**v)** Mwoga-anamwambia Mwango akae nae Tunu na Sudi wanapokuja kumwona.<br>**vi)**Ni fisadi –anafuja pesa za kusafisha soko/ananyakua kiwanja cha soko.<br>**vii)** Ni dikteta/mnyanyasaji – anaamrisha kufungwa kwa kituo cha habari cha habari cha Mzalendo.<br>**viii)** Mwepesi wa kusahawishika –anayaamini maneno ya Kenga<br>**ix)** Mwasherati/ mzinzi – anamtaka Ashua kimapenzi licha ya kuwa na mke<br>**x)** Mtelekezaji majukumu/asiyewajibika Hajali maslahi ya watawaliwa k.v kumpa Mamapima kibali cha kuuza pembe haramu.<br>**xi)** Mwenye kisasi – anamtia Ashwa jela ili kumwaadhibu sudi<br>**xii)** Ni mpumbavu/mjinga – hatambui kuwa anapotashwa na Mzee Kenga<br>**xiii)** Nu mjeuri/ mwenye majivuno anajilinganishana mashujaa katika Bibilia na mighani ya Waswahili<br>***(zozote 10x1=10)*** |

***Tanbihi: Ni sharti mtahiniwa atoe sifa zinazo kinzana moja kwa moja.Asipofanya hivyo asituzwe***

**b**)

- Anamwangamiza Jabali kisha anaeneza fununu kuwa alikufa na ajali ya barabarani
- ii) Anawatumia wahuni kama Ngurumo na kumlemaza Tunu.
- iii) Anatumia lugha ya kitamathali kutekeleza hila zake.k.m Chopi anapewa amri ya 'kuukata mguu" wa Tunu,yaani , kumwangamiza kabisa.
- Anapanga hila ya kuwafurusha wafadhili wa waandamanaji ili kukata nguvu za Tunu.
- Anatumia vyombo vya habari kutia Wanasagamoyo uzalendo bandia –anarekodi sauti yake,nyimbo za kizalendo
- Anatumia Ngao Junior kama chombo cha kumnasia Tunu.
- Anapanga kumrithisha mwanawe Ngao Junior uongozi kwa kumtangaza rasmi katika sherehe za kuadhimisha kuzaliwa kwake ingawa jambo hili linashindikana.
- Majoka alipanga njama ya kufunga Runinga ya Mzalendo na kubakia na moja tu ile tiifu ya Sauti ya Mashujaa
- Majoka akiwa na Mzee Kenga wanapanga njama za kuwakutanisha Ashua na Hussda ili kuzua mtafaruku baina yao na kumtia Ashwa kizimbani
- Anamtia Ashua jela ili ajaribu kumshawishi Sudi amchongee kinyago.
- Anatumia hila kumpa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu ilia pate uungawaji mkono na walevi k.v.Ngurumo.
- Anatumia pesa za ufadhili kama vichocheo vya kutekeleza mradi wake.
- Anapanga namna ambavyo angepata faida kubwa katika vioski vilivyomo katika viwanda vyake –bei ya vyakula inapanda
- Majoka anatumia ujanja kunyakua ardhi ya soko la Chapakazi kwa kuwahadaa kuwa limefungwa kwa kipindi cha mwezi mzima.
- Anafanya ujanja wa kuajiri binamu yake, Kenga ili kumsaidia kutekeleza miradi yake ya kihila.
- Majoka anatumia hila kumwoa Husda japo hakumpenda ili kutimiza wajibu wake katika jamii kama kiongozi.
- Majoka anatumia hila kwa kusambaza vijibarua vinavyosema jamii ya akina Siti ihame Sagamoyo ili awatie hofu
- Majoka anajaribu kuwapiganisha Sudi na Ashua kwa kumwambia Ashua kuwa Sudi anauhusiano wa kimapenzi na Tunu
- NMajoka anajaribu kumshawishi Tunu kuwa Sudi na Asha wanaiwinda roho yake.

(***zozote 10x1=10)***

**5. a)**

**(i) Msemaji ni <u>Bi. Hashima</u>**
(ii) Msemewa ni Tunu akiwemo Siti.
(iii) <u>Nyumbani</u> kwa kina Tunu.
(iv) Baada yaTunu kusema anataka <u>kwenda</u> kukutana namajangili waliomjeruhi/waliomvunja mguu.

***(4 x 1=4***)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**b) (i) MsemoNahau – pango la joka.**
(ii) Jazanda/sitiari – kujipeleka kwenye pango la joka – waliopo mahasimu.

**c) Umuhimu wa Hashima;**
i) Ni kielelezo cha uwajibikaji – baada ya kifo cha mumewe anajifunga kibwebwe mpaka anafidiwa.
ii) Anaonyesha masaibu/shida za raia – wanaishi kwa hofu
iii) Kuendeleza maudhui ya utetezi wa haki – anajifunga kibwebwe hadi anafidiwa/ Majoka kugharamia masomo ya Tunu.
iv) Kiwakilishi cha masaibu ya wajane- Majoka hataki kumlipa fidia ya kifo cha mumewe/anataka kumrithi.
v) Anaonyesha sifa za Majoka – jinsi anavyowadhulumu raia.
vi) Mfano wa malezi mema – anamlea Tunu hadi anapokamilisha elimu ya kiwango cha uzamifu.
vii) Anaonyesha hali ngumu wanayopitia wakulima kutokana na ukosefu wa mvua/ mito kukauka /miti kukatwa/mavuno kupungua.

***(zozote 4 x 1=4)***

d)
- Ashua kujipeleka kwa Majoka kuomba msaada wa chakula. Majoka anamhangaisha.
- Tunu kupinga uongozi wa Majoka, kisha anatumiwa wahuni wanaomuumiza mguu.
- Tunu kujipeleka kwa Mamapima,anatusiwa na kusimangwa na walevi.
- Jabali alipinga uongozi wa Majoka, akauwawa.
- Ngurumo aliropokwa Mangweni , akauwawa.
- Chopi alisemekana kujua mengi hivyo akauwawa.
- Ashua kushambuliwa na Husda alipomkuta ofisini mwa Majoka
- Siti wanatupiwa vijikaratasi za kuwafurusha Sagamoyo
- Kombe licha ya kuunga mkono chama cha Majoka, ni miongoni ya wanaotupiwa vijikaratasi.
- Sudi anakataa kuchonga kinyago cha shujaa, mkewe Ashua anatiwa ndani na Majoka.
- Kingi anakataa amri ya Majoka ya kuwapiga risasi raia, anafutwa kazi.
- Walevi kuathirika na pombe hadi wengine kuwa vipofu na wengine kufariki.
- Ngao Junior alikufa kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya.
- Ashua anafungwa gerezani na Majoka ili amshawishi Sudi kumchongea kinyago.
- Husda anatambua kuwa Majoka hampendi wakati anapomuuliza maswali kwenye ambulensi.
- Wanafunzi wa Majoka Academy wanaishia kuwa makabeji.
- Majoka anasalitwa na waliomuunga mkono k.v Kenga licha ya kukataziwa kuwahutubia raia pale sokoni.
- Watu wnataka kumpiga Majoka anapowatusi.
- Vijana watano wanuawa wanapoandamana kufungwa kwa kioski katika Majoka and Majoka Company.
- Boza anagudua kuwa Ngurumo anakula uroda na mkewe baada ya kulewa kuropokwa.
- Boza anapuuzwa na Kenga kuhusu uchongaji wa vinyago licha ya kujipedekeza kwake.
- Runinga ya Mzalendo inafungwa baada ya kupeperushwa habari kuhusu Tunu.
- Tunu anatoneshwa kidonda kuhusu babake baada ya Majoka kumkumbusha alipojipeleka ofisini mwake
- Majoka anatusiwa na Tunu baada ya kumpendekezea aolewe na Ngao Junior.
- Babake Tunu anaaga dunia katika Kampuni ya Majoka. Hawakuwa na bima.

6. **HADITHI FUPI**

**a) i)**
i) Msemaji wa kauli ya kwanza ni Jairo
ii) Msemaji wa kauli ya pili ni mwalimu Mstaafu Mosi
iii) Nyumbani kwa mwalimu mstaafu.
iv) Jairo anapokuja kwa Mwalimu Mosi na upanga akidhani kuwa mwalimu Mosi amemuoa binti yake
***(4x1=4)***

**ii)**
i) Msemo/Nahau – uniwie radhi
ii) Swali la balagha – kwani kulikoni? ***(2x1=2)***

**iii) Namna wahusika mbalimbali wanavyoumbuliwa**
i) Jairo anawasuta wanafunzi waliosoma naye kuwa walikuja kuwatishia na magari yao makubwa.
ii) Watu waliohudhuria sherehe wanasonya na kumtusi Jairo wanapoambiwa wamsihi apite.
iii) Mwandishi anapotoa taswira ya jinsi Jairo alivyokuwa amevaa –fulana nyekundu iliyochanika vibaya vibaya.
iv) Jairo anapowakejeli waliosoma naye kuwa wote hawakujui kupenga kamasi wala kuhesabu vidole vya mikono yao.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

v) Jairo anapowakashifu waliofuja pesa zilizochangishwa na rais alipokuja kwenya Shule ya Upili ya Wagwani
vi) Jairo anasema Mwalimu Mstaafu Mosi alikuwa kikwazo kikubwa kwake. Anasema hakuna mtoto wa mtu mwingine atakayekatishwa tamaa na Mwalimu Mosi kwani anastaafu.
vii) Jairo pia anasema Mwalimu Mosi alimpotezea muda wake bure shuleni.
viii) Jairo anawaita waliosoma naye wenye magari mazito kuwa ni wakora.
ix) Jairo anamlaumu mwalimu Mosi kwa kumsihi kuepukana na ufuska ilhali kinyume chake ndio utamu wa uhondo wa maisha, kwamba Mosi hajui haramu ni tamu na maisha ni mafupi.
xii) Jairo anamfokea Mwalimu Mosi kwa kumletea zawadi kwake. Anasema Mosi amemuaibisha.
xiii) Wambeya wanamwambia Jairo kuwa mwalimu Mosi na bintiye Jairo walighairi nia ya kutafuta vitabu madukani na kuanza kuishi pamoja. Jairo aliyaamini haya.
***(zozote 7x1=7)***

**MALEZI**

b)

- Baadhi ya watoto wanaelewa katika hali ya kimaskini. Kwa mfano, wazazi wake Bogoa hawakuwa na uwezo wa kununua sabuni Bogoa anasema kuwa sabuni kwao ilikuwa kitu cha anasa kwa familia yao.
- Baadhi ya wazazi wanasaidiwa kuwalea wanao. Wazazi wake Bogoa wanampeleka kwa rafiki yao Bi. Sinai ili awasaidie kumlea.
- Wazazi wanawalazimisha watoto kufanya wanavyotaka/wamewanyima fursa ya kujieleza Licha ya Bogoa kukataa kutengana na familia yake ili kuenda kuishi mjini na rafikiye babake. Babake anampuuza na kumpeleka huko.
- Walezi wanawatesa watoto. Bi Sinai anamtesa Bogoa kwa kumfanyiza kazi ngumu kama vile kuamka alfajiri kuchoma maandazi ya kuuza shuleni ilahali alikuwa na miaka mitano tu.
- Walezi wanawanyima watoto fursa ya kusoma. *Bi Sinai anamfanyiza Bogoa kazi badala ya kumpeleka shuleni. Anadai kuwa watoto wa kimaskini hawastahiki kusoma shuleni.*
- Baadhi ya wazazi wameonyesha uwajibikaji kwa mfano,Sebu anawashukuru wazazi wake kwa kumfanyia mengi aliyoyataka kama vile kumuelimisha
- Baadhi ya wazazi wanawapotosha wanao kwa mfano Bi Sinai anawahimiza wanawe kuwabagua watu wengine kwa kuwazuia kutocheza na Bongoa ingawa waliishi katika nyumba moja.
- Wazazi wengine wanawafunza wanao kuwanyanyasa maskini,kwa mfano,watoto wa Bi. Sinai wanapomuuliza kwa nini Bogoa haendi shuleni kusoma anawambia kwamba watoto wakimaskini hawakustahiki kusoma;walistahili kutumwa

**7. a) Mambo ni kangaja huenda yakaja – ni mambo ambayo yanatokea na labda hayakutarajiwa.**

- Samwueli anadhani kuwa atakapopokea matokeo ya mtihani atakuwa akitembea kama fahali lakini mambo yanakuwa kinyume.
- Samueli alidhani kuwa mwalimu mkuu atampa hongera atakapoingia ofisini mwake lakini anaishia kutupiwa matokeo ya mtihani wake.
- iii) Samweli anadhani amepewa matokeo mazuri na kuamua ayaonee mbele Baadaye anaona matokeo yake yenye safu ya D na E
- Mamake Samueli alijua kuwa mustakabali wa familia nzima ulitegemea mafanikio ya Samueli. Ataikwamua familia toka kwenye ulitima akishafanikiwa masomoni, hilo halikutendeka.
- Samueli anauona uso wa mama jinsi ulivyobadilika toka kwenye furaha hadi jitimai baada ya kupokea matokeo
- Babake samueli, ingawa anayaona fahari mafanikio ya binti zake, aliwaona wnawake tu, Fahari yake imo kwa Samueli akifua dafu.
- Samueli alijua ndiye nguzo ya familia yake kwa kudumisha jina la ukoo. Sasa mawazo yanamwadhibu.
- Samueli hana uhakika kuhusu mustakabali wa mahusiano yake na Nina. Kwake Nina, Samueli alikuwa bingwa masomoni kama alivyojipendekeza.
- Baba Samueli alitarajia kupata matokeo ya mtihani pundi samueli atakapofika nyumbani Samueli anamdanganya kuwa hakupokea mateo yake.
- Samueli hakutarajia kuwa babake angerauka asubuhi na mapema kuelekea shuleni kushauriana na mwalimu mkuu ili kubaini kulikoni.
- Samueli alitarajia kuwa angejitumbukiza bwawani afe mara moja lakini anaokolewa.
- Samueli kumbe huwa alikuwa pekee yake pale bwawani kumbe kulikuwa na mpita njia aliyejaribu.
- Wanakijiji wanamuomba babake Samueli amsamehe lakini anampa kamba ajimalize.
- Samueli anashtukia mamake akimshika mkono na kumwambia waende zao nyumbani

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Samueli anaponyanyua kichwa anamuona muhibu wake Nina kwenye umati wa wanakijiji ,hatujui hisia zipi zinampitia Nina akilini. ***(zozote 8 x 1 = 8)***

b)

- Ubakaji umemwacha Sara na kovu ambalo haliwezi kufutika maishani mwake. Kila wakati sara hukumbuka unyama aliofanyiwa usiku huo.
- Ubakaji mara nyingi humfanya mwathiriwa kuachwa na majeraha. Sara anatokwa damu katika sehemu za uzazi.
- Sara anaathirika kisaikolojia. Sara ameathirika sana kiasi cha kujiuliza kwa nini Mungu akaiumba dunia iliyoja udhalimu uliopita mipaka dhidi ya jinsia ya kike.
- Baadhi ya wanawake huishia kuavya mimba zinazotokana na ubakaji. Sara alikuwa na mawazo kama haya lakini akashauriwa na rafikiye sarina.
- Humfanya mwathiriwa kulipiza kisasi. Sara alitaka kumtupia tofali mbakaji aliyetumiwa akitaka kumbaka msichana mwingine lakini akaghairi kwa sababu alikuwa karibu kukata roho.
- Huweza kumfanya mwathiriwa kuwa mjamzito. Sara anaambulia ujazito bila mpango.
- Huweza kumfanya msichana afukuzwe shule kwa sababu ya ujauzito. Sara alihofia kwamba angefukuzwa shule kwani wasichana ndio husoma sio mama/wajawazito.
- Baadhi ya waathiriwa hujitia kitanzi kwa kujiona hawana maana yoyote maishani. Sara alikuwa na mafikira yakujiua lakini akalitupilia mbali wazo hilo kwa kuwa si njia nzuri ya kutatua taizo lake
- Humwacha mwathiriwa na huzuni na kilio kisicho na mpaka. Sara anahuzunika na kulia akumbukapo dhuluma aliyotendewa na janadume lililombaka.
- Kutengwa – Sara anaona kuwa angetengwa na jamii kutokana na kosa lisilokuwa lake.
- Baada ya msichana kubakwa ni vizuri kupata ushauri nasaha. Sara alishauriwa na rafikiye Sarina. Wote wawili walikubaliana kuficha ujauzito, jinsi atakavyojifungua, jinsi ya kupata matibabu hasa wakisaidiwa na dadake Beluwa.
- Waathiriwa wanastahili kuonyeshwa mapenzi na marafiki walionyesha mapenzi kwake. Babake aliandaa sherehe kubwa ya kumkaribisha mtoto.

- Kusutwa na kukashifiwa – ujauzito ungeiaibisha jamii
- Sara anaona angefukuzwa nyumbani na babake

**(zozote 12 x 1=12)**

**8. Fasihi Simulizi**

a) Mawaidha – Baba anamtolea mjukuu wake nasaha/mafunzo/kutahadharisha.

***(Kipera 1, Maelezo – 1) (2 x1=2)***

b)

- Mtoto mzuri siku zote hupendeza kila mtu.
- Hatendi mambo yanayoudhi yeyote.
- Hafanyi mambo yaendayo kombo kwa yeyote
- Hapendi kuropoka maneno,huficha siri.
- Awe mvumilivu,mwishowe atafaulu
- Atendee wenzake wema
- Awapende watu wa viwango vyote.
- Awe msamehevu.
- Alinde mdomo wake
- Asiwe na tamaa
- Atie bidii
- Awatii wazazi wake ***(za kwanza 4 x 1 = 4)***

c)

- Tashbihi - ni mfano wa mango katika nyumba/huficha siri kama kaburi
- Msemo/Nahau - yaendayo upogo/milango ya heri/furaha ghaya
- Methali – mvumilivu hula mbivu/wema hauozi/jifya moja halinjiki chungu/heri kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi/radhi ni bora kuliko mali.
- Jazanda/sitiari –mtu apandaye upepo na kuvuna tufani/yatafungua milango ya heri.

***(za kwanza 4x1=4)***

d)

- Awe mbaraza
- Awe mfaragazi/kubadilisha/kuigeuza mawaidha

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- kuielewa hadhura.
- Kuielewa lugha ya hadhira yake
- kuwa mbunifu
- Kuwa mcheshi
- Kutumia viziada lugha
- Kubadilisha toni
- Kuigiza/udramatishaji
- Kushirikisha hadhira
- Kuuelewa utamaduni wa jamii yake.

*(za kwanza 4x1=4)*

**e) Umuhimu wa hojaji/manufaa**

- Data haiwezi kufisidiwa
- Ni rahisi kupata habari za kutegemewa/kuaminika na kuondoa hofu/uoga kwa wahojiwa;
- Huokoa muda – kwa sababu hojaji nyingi zinaweza kutumwa
- Inaweza kutumika katika mahojiano kama mwongozo
- Jambo moja huweza kuelezwa na wengi.
- Mtafiti anaweza kufikia idadi kubwa ya watoaji habari
- Humpa mhojiwa muda wa kuwazia maswali na kuyafanya uchuguzi kabla ya kuyajibu
- Huwa ni njia iliyo na gharama ya chini Zaidi
- Hazina athari za mtafiti kwa sababu aghalabu mtafiti hayupo zinapojazwa.
- Hojaji inaweza kubadilishwa kulingana na kiwango cha wajazaji/wahojiwa. *(za kwanza 6 x 1=6)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA KIDATO CHA NNE - 2020**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI – KIRINYAGA**

**102/1**
**Kiswahili**
**Karatasi 1**
**(Insha)**
**DESEMBA 2020**
**KIDATO CHA NNE**

1. **Swali la lazima.**
   Wewe ni mkurugenzi mkuu katika kampuni ya Tononoka ambapo pameripotiwa visa kadhaa vya ugonjwa wa uviko - 19 (korona) baada ya kupuuzwa kwa kanuni zilizowekwa na wizara ya Afya nchini. Waandikie wafanyikazi wako memo ukiwaonya dhidi ya jambo hili.

2. Dhuluma katika asasi ya ndoa haiathiri tu wanajamii husika nyumbani bali elimu ya watoto wao pia. Fafanua.

3. Andika kisa kitakachothibitisha maana ya methali ifuatayo:-
Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.

4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa kauli ifuatayo:-
... walipofungua mlango huo hatimaye, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao waliangua vilio kwa maafa waliyoshuhudia.

**JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA KIDATO CHA NNE - 2020**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI – KIRINYAGA**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2**
**(Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimu Jamii)**
**DESEMBA 2020**

1. **UFAHAMU**.(alama 15)
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Takwimu zilizotolewa na Wizara ya Afya katika wiki moja iliyopita zinahofisha kwa kuweka rekodi ya idadi kubwa zaidi ya vifo vya wathiriwa wa korona kuwahi kupatikana tangu janga hili litue humu nchini.

Bali na waliopoteza maisha yao, idadi ya maambukizi ya Covid-19 imepaa zaidi kiasi kwamba wataalamu wameanza kukisia kwamba huenda hizi ni dalili za mkumbo wa pili wa maambukizi haya hatari kuanza kushika kasi.

Wataalamu pia wameelezea sababu ya janga hili kukithiri ni kutokana na wananchi kutowajibika hata kutozingatia maangizo ya serikali ya kuzima maambukizi ya gonjwa hili. Maagizo haya yaliyopuuzwa ni kama kuvaa barakoa kwa njia ifaayo, kuzingatia umbali wa mita moja na nusu, kutogusagusa macho, pua na midomo pamoja na kunawa mikono ipasavyo. Mambo yalienda segemnege wakati kafyu ililegezwa, vilabu kufunguliwa huku ibada, harusi na mazishi yakirejelewa kama kawaida.

Suala la mapuuza limedhihirika wazi wazi kwenye mikutano ya kisiasa ambapo viongozi huwakusanya wananchi bila kujali uzingatiaji wa kanuni hizi za wizara ya Afya. Baadhi ya viongozi wameonekana wakitoa mifano mibaya ya kutovalia barakoa na hata kutowashauri wafuasi wao kuzingatia maagizo hayo. Suala hili limeghadhabisha viongozi wa kidini na wa wizara ya Afya ambao wametoa wito mikutano yote hasa ya kisiasa nchini izimwe kote nchini ili kunusuru hali iliyopo kwa sasa.

Hata ingawa hali ya siasa nchini imechochewa na uzinduzi wa ripoti ya Mpango wa Maridhiano (BBI) ambayo kampeni zake zimeanza kwa kasi, serikali inafaa kufanya maamuzi ya busara kati ya siasa na thamani ya uhai wa raia wake. Rais anapojiandaa kutoa mwelekeo kuhusu mbinu mwafaka za kipaumbele suala la mikutano ya kisiasa ambayo inafaa kuzimwa kabisa kando na mbinu zingine faafu kukomesha janga hili linalokondolea macho maisha ya wakenya.

Kaimu katibu mkuu wa chama cha madaktari nchini (KMPDU) alisima tayari msambao wa korona uko kila mahali na marufuku ya kutoingia wala kutoka baadhi ya kaunti hakutadhibiti hali hiyo.

Naye mkurugenzi mkuu wa shirika la utafiti wa kimatibabu Afrika (Amref), alisema marufuku ya usafiri italeta madhara zaidi kwa uchumi wa nchi. “Kile ambacho serikali inapasa kufanya ni kuimarisha masharti ya kupunguza mtugusano wa wananchi na hivyo kudhibiti kiwango cha mambukizi,” akasema kwenye mahojiano ya simu.

Kwingineko makamishina wa kaunti tofauti wanapendekeza maafisa wa polisi waendelee kushika doria ili kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafuata kanuni za kukabiliana na kusambaa kwa virusi vya Covid-19 vinavyosababisha ugonjwa wa korona.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali.**

a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka. (alama 2)
b) Eleza sababu **nne** ambazo zimechangia kusambaa haraka kwa ugonjwa wa korona. (alama 4)
c) Viongozi wa kisiasa ni kizingiti cha vita dhidi ya ueneaji wa virusi vya Covid-19. Thibitisha
d) kauli hii. (alama 3)
e) Ni hatua gani zinazoweza kuchukuliwa ili kukomesha janga hili kwa mujibu wa taarifa hii? (alama 3)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)
i) takwimu

ii) mtagusano
iii) doria

2. **UFUPISHO (alama 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Roho nyingi za waja zimeangamizwa na kudhulumiwa kwa kukatiwa aushi kwa sababu ya ajali za barabara. Nchi yetu ni moja ya nchi ambazo hurekodi idadi kubwa ya ajali barabarani la kushangaza ni kuwa idadi ya ajali imeendelea kuongezeka licha ya kuimarika kwa miundo misingi. Barabara zilizokarabatiwa na kuwa za kisasa ndizo zinazoongoza kwa idadi ya ajali.

Serikali ilichukua hatua za kukabiliana na ongezeko la ajali hizi. Juhudi za kuleta vifaa vya kupuliza hewa ili kubaini wale wanaoendesha magari wakiwa wamelewa ni hatua moja muhimu sana. Mlevi mmoja akipatikana na kushtakiwa ikakuwa funzo kwa wengine walio na tabia kama hiyo. Takwimu za

idara ya polisi inayoshughulikia usalama barabababarani zinaonyesha kuwa ulevi ndio unaongoza katika kusababisha ajali. Hatua hii itasaidia kwa kuwa dereva mlevi hukosa makini anapoendesha gari kwa sababu ya ukadiriaji na uamuzi wake huathirika kwa hewa ni wa polepole sana.

Serikali imekatiza safari za usiku za magari ya abiria yanayosafiri masafa marefu. Magari haya yalilazimika kukatiwa leseni mahususi inayokubalia kusafiri usiku. Magari haya lazima yakaguliwe kila wakati na kuhakikisha kuwa yako katika hali nzuri ya kuwa barabarani. Lazima yawe na madereva wawili ambao watasaidiana kuliendesha gari kwa zamu. Madereva hawa wawe wameidhinishwa na mamlaka inayosimamia usalama barabarani.

Kwa kupewa leseni hii idhibati inatolewa kuwa dereva atakuwa akiendesha gari kwa saa zisizozidi nane na kuwa atakuwa akipumzika kwa muda huo kabla ya kuliendesha gari tena. Barabarani nako, anatakiwa kupumzika kwa muda wa dakika thelathini kila baada ya saa tatu. Hayo magari sharti yawe na magurudumu sawasawa na sio yale yanayonyesha upara na kukosa kudhibiti barabara njema. Nazo taa, breki na honi viwe timamu. Basi iwapo magari mabovu yatapatikana barabarani, mwenyewe ashtakiwe na gari kupigwa marufuku njiani.

Usalama barabarani utaimarika ikiwa magari ya umma yatakuwa na vidhibiti mwendo ili kupunguza kasi barabarani. Baadhi ya wenye magari na madereva huwa na tamaa ya fulusi. Huawalazimu abiria kukataa katakata mwendo huu wa kiwazimu kwa kuwatahadharisha na kuwaonya madereva wanapokiuka agizo hili, polisi wapashwe habari ili sheria iwaandame. Hali kadhalika magari yote lazima yawe na mikanda ya usalama kwa madereva na abiria. Mikanda hiyo husaidia wakati wa ajali kwa kuwazuia wasafiri kurushwarushwa ndani au nje ya gari. Isitoshe, mikanda hiyo huwapa abiria starehe katika usafiri kwa sababu hakuna misongamano garini. Magari ya umma, mithili ya matatu na mabasi yanahitajika kubeba idadi ya abiria iliyokubalika. Iwapo dereva atapatikana amezidisha idadi, dereva na abiria hao ziada watozwe faini papohapo.

Idara ya polisi wa trafiki haiwezi kuachwa nje katika juhudi za kudumisha usalama barabarani. Idara hii ina jukumu la kukagua magari na kuthibitisha kwamba yanafaa kwa usafiri au uchukuzi. Pia kuhakikisha kuwa magari hayasheheni uzito kupita kiasi kilichokadiriwa.

Idara hii inafaa kuwanasa wanaoendesha magari kwa mwendo wa kasi au wanaovunja sheria za barabarani. Polisi watazamiwa kujepusha wasitiwe dosari kwa kutwaa hongo. Yeyote atakayefanya kosa hili ashtakiwe kisha adhabu kali itolewe dhidi yake.

Watumiaji wengine bali na madereva wanalo jukumu la kulinda usalama barabarani. Waendeshaji baiskeli na wanaoenda kwa miguu wanafaa kuwa waangalifu wanapokuwa barabarani wanapaswa kuelewa na kufuata sheria za barabarani ili kudumisha usalama wao na wa wengine pia. Ni wajibu wa serikali kuhakikisha kwamba barabara ni bora na zitawawezesha madereva na abiria kufurahia safari zao.

Usalama barabarani utaimarika ikiwa tutayazingatia haya yote. Ikumbukwe kuwa magari yameundwa ili kusaidia mwanadamu maishani wala si kumhiliki.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali.**

(a) Fafanua hatua ambazo serikali imechukua ili kudhibit ajali barabarani. (maneno 80 - 85) (alama 10)

Nakala chafu
Nakala safi

(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya mwisho. (maneno30 - 40) (alama 5)
Nakala chafu
Nakala safi

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

(a) Eleza sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo:- (alama 2)
(i) /g/
(ii) /z/

(b) Andika neno lenye miundo ifuatayo ya silabi. (alama 1)
IKIKI

(c) Andika sentensi ya neno moja yenye viambishi vifuatavyo. (alama 2)
(i) kiambishi cha nafsi / ngeli (umoja)
(ii) wakati
(iii) kirejeshi
(iv) kitendwa / ngeli
(v) mzizi \\

(d) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia neno lililopigwa mstari kama nomino. (alama 2)
Maria alicheka hadi akawashangaza wengi.

(e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:- (alama 1)
Ua uliokauka ni wa bawabu

(f) Tunga sentensi ukitumia kivumishi kisisitizi cha wastani pamoja na nomino katitika ngeli ya i - i (alama 2)

(g) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 1)
Ndege huyu ana miguu midogo.

(h) Unganisha sentensi zifuatazo ili uwe na sentensi yenye kishazi tegemezi. (alama 2)
Kembo ataimba vizuri.
Kembo atatuzwa zawadi.

(i) Alama za mtajo hutumiwa kufungia usemi halisi onyesha matumizi mengine mawili ya alama hii katika sentensi. (alama 2)

(j) Kanusha sentensi ifuatayo wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
Kuli alipakia shehena katika meli.

(k) Changanua sentensi zifutazo kwa vielelezo vilivyo katika mabano.
(i) Omari angali anacheza soka. (jedwali) (alama 2)
(ii)Atanishughulikia vizuri. (matawi) (alama 2)

(l) Tambua matumzi ya kiambishi kwa katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
(i) Juma alipata alama moja kwa kumi.
(ii)Wageni walitembea kwa utaratibu.

(m) Andika sentensi Ifuatayo upya ukibadilisha yambwa tendewa kuwa kiima. (alama 2)
Mwalimu atawasimulia wanafunzi hadithi.

(n) Tambua kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Wazee hao wanne walikuwa watumwa.

(o) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 3)
KN(W) + KT(T) + RN(N+RH)

(p) Aila ni kwa familia ndoa ni kwa ________________________________ ilhali ____________________ ni kwa himila (alama 2)

(q) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia neno lililopigwa mstari kama kitenzi. (alama 2)
Mzee alionyesha ukarimu kwa wanakijiji.

(r) Taja hisia zinazodhihilishwa na vihisishi vilivyopigwa mstari. (alama 2)
(i) Inshallah! Mola atakuongoza
(ii)Simile! Nimeangata mzigo mzito.

(s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya fuka na vuka. (alama 2)

(t) Mzee Juma huwadekeza wanawe. Wanapokosa hawaadhibu. Wanapokomaa wanakaidi amri zake
Andika methali inayoweza kutumiwa kuelezea hali hii. (alama 1)

(u) Mbuzi walipopotea mchungaji alikuwa na wasiwasi. (alama 2)
Anza kwa: Kupotea ...

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)

Wananchi hoyee! Kiti juu! Kiti thumps up! Leo ni ile siku tuliyoingojea kwa hamu na ghamu. Imefika haijafika? Naona hamjadanganywa na huyo jamaa atembeaye na kupaka matope jina langu. Ni nani hajaona maendeleo niliyoleta hapa tangu mnichague nyinyi wenyewe? Sasa hii ni time nyingine naomba, nawasihi, nawanyenyekea mnikabidhi votes zenu ili niwatumikie.

(a) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)
(b) Eleza sifa **nane** za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 8)

**JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA KIDATO CHA NNE - 2020**
**HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI – KIRINYAGA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**FASIHI**
**DESEMBA 2020**
**KIDATO CHA NNE**

**SEHEMU A: TAMTHILIA**
**Pauline Kea : Kigogo.**

1. **Swali la lazima.**

"Huoni kisima kimeingia paka na maji hayanyweki tena."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondoo hili. (alama 2)
(c) "Kuyaopoa mataifa machanga ya Afrika kutoka kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake." Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthilia ya kigogo. (alama 14)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**Assumpta K. Matei: Chozi la Heri.**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "... wewe hujui kwamba umaskini unaweza kuupujua utu wa mtu akatenda hata asiyokusudia kutenda."

(a) Eleza sifa **nne** za anayerejelewa. (alama 4)
(b) Onyesha vile utu wa mtu ulivyopujuliwa kwa kurejelea Riwaya ya Chozi la Heri. (alama 16)

Au

3. "... inasikitisha kwamba badala ya kuliongoa jahazi letu wameligongesha mwamba bila kujua."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha tamathali mbili za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili na ufafanue dhima yake. (alama 2)
(c) Jadili jinsi wahusika wafuatao walivyoliongoa jahazi lao katika kukabiliana na hali yao ya maisha.
   (i) mwangeka (alama 5)
   (ii) pete (alama 5)
   (iii) selume (alama 4)

**SEHEMU C : HADITHI FUPI**
**Alifa Chokocho na D. Kayanda : Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "... mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni udunishwaji, ni ushabiki usio na maana ... ni ugonjwa usio na dawa!"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi ya masharti ya kisasa. (alama 7)
(d) Onyesha vile unyonge wa mwanamke unavyojitokeza katika hadithi ya mame Bakari. (alama 7)

Au

5. (a) Eleza jinsi maudhui ya umaskini yanavyojitokeza katika hadithi ya Ndoto ya Mashaka. (alama 12)
(b) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo. (alama 8)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Waridi ni moja kati yao. Kati ya maua. Ua maarufu ingawa maua mengi yapo. Baadhi yao mazuri na baadhi ya mengine mabaya. Lakini ukiniuliza maua yapi mazuri au mabaya zaidi, sitakuwa na jibu la swali lako. Natambua tu yapo mengi. Mengi maua Mashaallahu! ... kila nitazamapo Waridi, sikosi kuonja chagizo za uzuri wake. Sifa za Waridi hizo ... na harufu yake je? ilipekecha hurufu yake nzuri, harufu ya Waridi .... baada ya dhiki faraja!... ua langu lilikwanyuka kwanyu na kikonyo chake, likapeperushwa na dhoruba kali.

**SEHEMU D: USHAIRI**
**Jibu swali la 6 au la 7**

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Watalamu muwe macho, vuani moto muenge,
Muenge hicho ambacho cha watu wenye mawenge,
Mawenge yenye kijicho, Kiswahili wakivunge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Sichafue Kiswahili, barakala tuwapinge,
Tuwapinge kila hali, wasiguse tuwainge,
Tuwainge wende mbali, Kiswahili tujijenge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Sichafue yetu lugha, waharibu wabanange,
Wabanange iwe nyagha, waiweke tengetenge,
Lugha kuitwa ulugha, lafidhi watia denge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Tuichangie heshima, na ulugha tuupinge,
Tuhifadhi kwa salama, na kisingio unyonge,
Kelele za maamuma, sio watu ni visinge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Kasema Sheikh Amri, Kiswahili tukisenge,
Kisitawi kinawiri, kitumike kwenye bunge,
Hii ni yetu farari, lugha yetu tuichunge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

Kikipatwa na maradhi, kwa sindano tukidunge,
Kila jama kukitidhi, kipatwe hapo tupunge,
Tukitia mfawadhi, kama kunde na kihenge,
Barakala tuwapinge, sichafue Kiswahili.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Bainisha mapendekezo **manne** yanayodokezwa na mshairi kuhusu kuhifadhi na kuimarisha lugha ya Kiswahili. (alama 4)
(b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
(c) Bainisha nafsi nenewa na kinacholengwa akitekeleze. (alama 2)
(d) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
(e) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 2)
(f) Bainisha bahari mbili za ushairi zinazojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili\ Kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:- (alama 4)
  (i) Pande katika ushairi
  (ii) Mpangilio wa maneno
(g) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika ushairi. (alama 2)
  (i) mfawadhi
  (ii) Barakala
  (iii) maaamuma
  (iv) muenge

Au

7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo,
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo,
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tuyasikiayo,
Nayo, visa na mauko, wanyonge wayakutayo,
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo,
Naandika!
Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo,
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo,
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo,
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo,
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo,
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo,
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo,
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo,
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo,
Naandika!

**Maswali.**

(a) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2)
(b) Bainisha bahari tatu zinazojikita katika ushairi. (alama 3)
(c) Fafanua sifa tatu za kiarudhi zilizotumika katika ubeti wa tano. (alama 3)
(d) Eleza aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumika. (alama 2)
(e) Andika mifano ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 4)
  (i) Kinaya
  (ii) Swali la balagha
  (iii) Takriri
  (iv) Taharuki
(f) Andika aina mbili za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
(g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alaam 4)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Sasa Susa
Utapikiwa na nani?
Jiko tumelitwaa
Utapakuliwa na nani?
Kijiko tumetwaa

Hatuna shida
Makoo tunao chungu tumbi
mchukueni huyo
Tumewakabidhi
Nyie dhaifu
Msio na wa kuwatunza
Msio na wapishi!
Pia mitamba mepokelewa tayari
na wazee kwa furaha.

**Maswali.**

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 2)
(b) Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa huu ni utungo wa aina ya ngonjera. (alama 2)
(c) Andika sifa mbili za jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)
(d) Tambua sifa za ushairi simulizi zinazoweza kujitokeza kwenye utungo huu. (alama 6)
(e) Unanuia kutumia hojaji kukusanya habari kuhusu tungo za aina hii:-
(i) Eleza manufaa manne ya kutumia mbinu hii. (alama 4)
(ii) Eleza changamoto nne za kutumia mbinu hii. (alama 4)

**KIRINYAGA**
**KIDATO CHA NNE - 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI FASIHI 102/3**

1. (a) Muktadha wa dondoo.

Msemaji : Babu
Msemewa : Majoka
Mahali : Hospitalini
Sababu : Babu anampa Majoka usia. Anaukosoa uongozi wa Majoka kwa kumuusia kuwa atende wema kwa raia wa Sagamoyo.

*(al 4 x 1 = al 4)*

(b) Tamathali za usemi.

i) Jazanda - kisima kimeingia paka.
ii) Swali la balagha - Huoni maji hayanyweki tena? *(zakwanza 2 x 1 = al 2)*

(c) Kuyaopoa mataifa machanga ya Afrika kutokana na kinamasi cha madhulumu kwa kuna gharama yake.

i) Vitisho - Sudi anatishwa na Kenga kuwa ulimi wake ungemtuma kwenye bahari mchafukoge.
ii) Kukabiliwa na taasubi ya kiume - Tunu anapuuzwa na baadhi ya watu kwa kuwa ni mwanamke. Ngurumo anasema heri ampe paka kura lakini si mwanamke.
iii) Kupigwa marufuku kwa maandamano - Kenga anamshauri Majoka kutangaza kuwa maandamano yote ni haramu.
iv) Kuuawa - Wapinzani wa uongozi Sagamoyo wanauawa katika jitihada za kusaidia Sagamoyo. Jabali aliuawa.
v) Vifungo - Ashua anafungwa kwa kukataa matakwa ya Majoka. Kufungwa kwake kulikuwa na nia ya kumshinikiza Sudi amchongee Majoka kinyago.
vi) Umaskini - Ashua anavamiwa na uhitaji kiwango cha kumwendea Majoka kutafuta usaidizi. Watoto wao Pili na Pendo wanalala njaa.
vii) Kushambuliwa na vijana - Vijana walitumiwa kumvamia Tunu, nia ikiwa kumuua. Aliishia kuumizwa vibaya kiasi cha kumfanya atumie kiti cha magurudumu.
viii) Kukatiziwa vyanzo vya riziki. Sudi na ashua wanaachwa bila namna ya kupata riziki baada ya Soko kufungwa na Majoka.
ix) Watu kufurushwa makwao - Jamii ya kina Siti inaandikiwa vibarua vya kusema wahame Sagamoyo. Hii inatokana na wao kutounga mkono ungozi wa Majoka.
x) Kudhihakiwa - Tunu anadhihakiwa na waliomuunga mkono Majoka. Alipokwenda Mangweni, anadhihakiwa kwa kuambiwa kwanza aolewe.
xi) Kugobanishwa - Tunu na Sudi wanachochewa kukosana ili waachane na harakati za ukombozi. Tunu anachochewa dhidi ya Sudi kwa kuambiwa kuwa yeye na Ashua ndio walikuwa wakiwinda roho yake.
xii) Matusi - Sudi anarejelewa na Majoka kama Zebe. Majoka ananuia kumdunisha machoni pa mkewe Ashua.
xiii) Kukabiliwa kwa nguvu wanapoandamana - Polisi wanatumia nguvu kupita kiasi kuwakabili waandamanaji. Vijana watano wanauwawa.
xiv) Usaliti kutoka kwa wenzao -Juhudi za kuleta ukombozi zinapingwa na baadhi ya wanasagamoyo kama vile Ngurumo, Asiya na Boza.
*xv)* Ndoa zao kuingiliwa - Majoka anapania kuisambaratisha ndoa yao Sudi na Ashua. Anamshawishi Ashua aachane na Sudi na akubali kuolewa naye.

*(zozote 14 x 1 = al 14)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

2. (a) <u>Eleza sifa za Lunga</u>. (al 4)

i) Mwenye bidii - Alifanya kazi kwa bidii mpaka akakwea na kuwa mkurugenzi wa shirika la maghala la na nafaka.
ii) Mkweli - Alizuia mahindi ya sumu yauziwe raia.
iii) Ana mapenzi ya dhati - Aliaga baada ya kuachwa na mkewe Naomi.
iv) Msimamo dhabiti - Alikataza mahindi ya sumu yauziwe raia hadi akafutwa kazi.
v) Ni mlezi - Anawalea wanawe vizuri hata baada ya mkewe Naomi kumwacha.*( za kwanza 4 x 1 = al 4)*

(b) <u>Vile utu wa mtu ulivyopujuliwa.</u>

i) Uharibifu wa mali - Jumba la Ridhaa la kifahari linateketezwa bila huruma na waandamanaji.
ii) Mauaji - Polisi wanakabiliana kikatili na uhalifu wa vijana, wanapigwa risasi. Familia ya Ridhaa inachomewa ndani ya nyumba.
iii) Kupigwa - Subira mkewe Kaizari anapigwa na kukatwa na wanaharakati kwa madai kwamba Kaizazi alimuunga mkono Mwekevu.
iv) Unyanyasaji wa kimapenzi - Vijana wanawabaka Lime na Mwanaheri. Sauna anabakwa na Bwana Maya.
v) Dhiki ya kisaikolojia - Mabarobaro wanawabaka mwanaheri na Lime mbele ya baba uap. Walimwachia Kaizai kuuguza donda la kihisia.
vi) Kutengwa - Mavyaa wa Subira anamchukulia kama mgeni. Anamwona kama aliyesababisha kuhujumika kwa mali yao.
vii) Kutelekeza wana - Subira anawaacha watoto wake bila kujali huzuni anayowasababishia.
viii) Ulanguzi wa watoto - Sauna anashirikiana na Bi. Kangara - Wanaendeleza wizi wa watoto. Mfano Dick na Mwaliko.
ix) Ajira ya watoto - Mzee Buda anawaajiri watoto. Anamtumia Dick kulangua dawa za kulevya ughaibuni.
x) Unyanyasaji wa kijinsia - Bwana Maya anampiga mama Sauna na hali mama huyu anakubali chochote anachoambiwa.
xi) Ukiukaji wa haki za wagonjwa. Dawa zinazonunuliwa kwa matumizi ya wagonjwa zinaishia kwenye maduka ya dawa ya msimamizi wa hospitali.
xii) Ukiukaji wa haki za wafanyakazi. Selume analalamikia ukosefu wa vifaa vya kimsingi hospitalini k.v glavu.
xiii) Kimondo analalamikia ujira duni unaopewa wafanyakazi katika shamba la kahawa - wafanyakazi hawana bima ya matibabu.
xiv) Kunyimwa haki ya elimu - Pete anaozwa licha ya rai za nyanya yake kwamba aachwe afuatilie elimu.
xv) Kesi kukawia kwa muda mrefu bila kusikilizwa. Tila anamatumaini kuwa jaji atasikiliza kesi ile ambazo zinaselelea mahakamani kwa miongo miwili, zisikilizwe kwa kuamuliwa.
xvi) Ukiukaji wa haki za wafungwa - Wanawekwa rumande kwa muda mrefu, miongo miwili huku wakingojea kusikilizwa kwa kesi.
xvii) Wanyonge kwenye msitu wa mamba kupewa hatimiliki bandia. Viongozi walikuwa wanajua ardhi hii ni marufuku.
xviii) Uongozi unaruhusu ujenzi wa nyumba kwenye maeneo yaliyotengewa ujenzi wa barabara na baadaye kuwasababishia wenyewe hasara.
xix) Kufutwa kazi kikatili - Lunga anafutwa kazi kwa sababu alipinga kuuzwa kwa mahindi duni kwa raia.

*(zozote 16 x 1 = al 16)*

3. (a) <u>Muktadha wa dondoo.</u>

Msemaji : Mwangeka
Msemewa : Ridhaa
Mahali : Katika uwanja wa kimataifa wa Ndege wa Rubia.
Sababu : Mwangeka anasikitika kuona kwamba, vijana wanatumiwa na wanasiasa vibaya kuzua fujo na kuvuruga mshikamano wa kijamii. *(4 x 1 = al 4)*

(b) <u>Tamathali za usemi na dhima yake.</u>

(i) Jazanda - Jahazi
- imetumika kurejelea nchi ya wahafidhina na mshikamano wa kijamii uliopo.

(ii)Nahau / msemo - gongesha mwamba.
- imetumika kuonyesha vile vijana walivyo uharibu mshikamano wa kijamii kwa kutumiwa na wanasiasa kuzua vurugu.

*(Kutaja $^1/_2$ Mfano / maelezo $^1/_2$ Kwanza 2 x 1 = al 2)*

(c) <u>Jinsi wahusika walivyoliongoa jahazi lao.</u>

<u>Mwangeka</u>

i) Alijitenga na mazingira - Mwangeka anaondoka nyumbani kwa babake mzazi ili kujiondolea adha ya kumpoteza mkewe aliyechomwa moto.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

ii) Kubadilisha msimamo wa awali - Mwangeka aliapa kutooa tena Nyamvula alipouwawa. Anapokutana na Apondi, anabadilisha msimamo na kumwoa.
iii) Kuchukua msimamo imara - Mwangeka aliiacha taaluma yake ya uhandishi na kuiingia katika kitengo cha usalama ili awahudumie raia wengi.
iv) Kujitegemea - Mwangeka alitafuta kiwanja cha kujengea nyumba yake bali na kitovu cha babake.
v) Kujiendeleza kielimu - Kutokana na kichapo cha babake alipoigiza mbolezi ya Dede, Mwangeka aliwajibika zaidi masomoni na kuhitimu katika chuo kikuu.
vi) (vi) Kulia ili kupunguza mwemeo wa kupoteza aila yake - Mwangeka anaposhuhudia kiunzi cha mkewe aliyechomwa moto, analia - Jambo hili lilimpa utulivu na amani. *(zozote 5 x 1 = al 5)*

(ii) Pete

i) Pete anamwaga dukuduku kuwasimulia selume na meko kisa chake ili kupunguza mwemeo wa matatizo yake.
ii) Kutumia mbinuishi kukabiliana na changamoto za maisha - Pete anapokosa Sado anatafuta kanzu kuukuu kujifadhilia.
iii) Kuchukia jaala ili kupunguza madhila yake - Pete anachukia nguvu za maumbile zilizomweka kwenye jinsia ya kike.
iv) Kuvunja mikatale na tamaduni zilizopitwa na wakati - Pete anatoroka kwa mzee Fungo kwani hawalingani kiumri.
v) Kujiendeleza kiuchumi - Pete alitafuta kibarua ili kujikimu kimaisha. Anaajiriwa katika kiwanda cha kutengeneza sare za shule.
vi) Pete anatathimini matunda yake na kuwazia athari za matendo yake kama vile kujaribu kujitia kitanzi na kuavya mimba - Anasema hawezi kuishi kwa kujidhalilisha tena.

*(zozote 5 x 1 = 5)*

(iii) Selume

i) Amewajibikia kazi yake - Selume anawahudumia wagonjwa katika kituo cha Afya cha Mwanzo Mpya - Jambo linalomfanya kuridhika zaidi maishani mwake.
ii) Kupinga tamaduni zilizopitwa na wakati - Selume anamwelekeza Tuama dhidi ya kupashwa tohara na kufuata mila bila tahadhari.
iii) Kujiuzulu kazi - Selume anajiuzulu kazi katika hospitali ya umma kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vya kimsingi kama vile glavu.
iv) Kuwa na msimamo dhabiti - Selume aliondoka kwa mumewe kwa sababu ya kuhitilafiana kimsimamo na wakwe zake - Anamuunga mkono mwanamke kwani alitaka mabadiliko.
v) Kukataa kudhulumiwa - Selume anahiari kuishi kambini badala ya kuishi kwenye kasri la dhuluma la mumewe.

*(zozote 4 x 1 = al 4)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

4. (a) Muktadha wa dondooo.

| | | |
|---|---|---|
| Msemaji | : | Kauli ya mwandishi. *(al 1)* |
| Mrejelewa | : | Dadi *(al 1)* |
| Sababu | : | (i) Dadi anapitia hali ngumu katika ndoa yao na Kidawa. *(al 1)* |
| | : | (ii) Dadi anakosa kumwelewa mkewe kidawa na fasiri ya ndoa ya kisasa. *(al 1)* |

*(4 x 1 = 4 mks)*

(b) Mbinu mbili za kimtindo.

(i) Jazanda - dawa
(ii) Nidaa - dawa!

*(kwanza 2 x 1 = al 2)*

(c) Ukweli wa kauli kwenye dondoo. *(al 7)*

i) Dadi ndiye mchuma riziki - Yeye ni muuza samaki na apatacho kinatumiwa kuilisha jamii yake. Pesa za mkewe ni za kununua fasheni mpya na mapambo.
ii) Dadi anapoamua kuzua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu - Alianguka na kuumia vibaya sana.
iii) Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa za kuwauzia wateja - Kila mara mkewe anapofanya hivyo, anaumia sana. Anaiona hiyo kama fursa ya mkewe kuhusiana na wanaume wengine.
iv) Kila mara Dadi alitarajiwa kuwa baada ya kula angeviondoa vyombo mezani na hata kuvisafisha.
v) Kidawa hakubali kuwa mwanaume kazi ni za nje si za ndani na kuwa Dadi kufanya kazi za ndani ni hisani tu.
vi) Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashindwa kumweleza.
vii) Dadi analazimika kushika shughuli za upishi kama vile kukuna nazi kutia mboga tui.
viii) Wanandoa kujiwekea masharti ya uzazi - Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu kutokana na athari za usasa.
ix) Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashindwa kumweleza.

*(zozote 7 x 1 = al 7)*

(d) Unyonge wa mwanamke katika hadithi ya mama Bakari.

i) Kila mara mwanamke anapobakwa, anayelaumiwa ni mwanamke na hata huonwa kama shetani - mfano ni Sara.
ii) Kuishi maisha ya kimaskini - Msimulizi anaeleza kuwa Sara angekunjiwakunjiwa matambaara yake na kurushiwa nje.
iii) Kuogopa kutoa taarifa ya kubakwa - Sara anaona kuwa wazazi wake hawangemwamini.
iv) Kuogopa adhabu ya wazazi - Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.
v) Tukio la kubakwa linampotezea Sara fahamu na anaaibika sana anapozinduka na kujipata akiwa uchi.
vi) Mwanamke kujeruhiwa - Baada ya Sara kubakwa na janadume lile, anaharibiwa na kuvuja damu.
vii) Mwanamke anateseka kisaikolojia - Sara anaingiwa na mawazo mengi jinsi atakavyoukabili ule ujauzito. Anafikiria hata kuavya mimba, kuhama kwao au kujiua.
viii) Sara alivunjiwa ujanajike na utu wake na janadume.
ix) Masomo ya Sara kukatizwa - Mwalimu mkuu alimkabidhi Sara barua ya kumfukuza shule.
x) Mwalimu mkuu kutomsikiliza Sara wala kumhurumia - Badala yake aliongoza kumkeijeli na kumweleza haikuwa shule ya wazazi bali ya wasichana.
xi) Twisheni inayofanyika usiku inahatarisha usalama wa wanafunzi. - Hili ndilo linasababisha kubakwa kwa Sara. *(zozote 7 x 1 = al 7*

5. (a) Umaskini katika hadithi ya ndoto ya mashaka.

i) Waridi alimwacha mashaka kwa sababu hakuweza kuikimu familia yake; yeye na watoto wao saba.
ii) Wazazi wa Waridi walikoseshwa raha na ndoa ya kimaskini ya Mashaka na Waridi - walihamia Yemeni kujiepushia aibu.
iii) Umaskini unamfanya mashaka kuota ndoto za ufanisi wake. Anajuta anapojipata katika hali ile ile ya umaskini.
iv) Wasakakatonge wanafanya maandamano wakitaka mabadiliko katika maisha yao - Wanasema bora wafe badala ya kuishi maisha ya umaskini.
v) Waridi alimwacha mpenziwe mashaka na kukimbilia Yemeni - Hii ni kutokana na umaskini wa Mashaka.
vi) Mashaka alipoachwa na Waridi alikuwa hana chakula wala maji. Hakuona thamani ya maisha tena.
vii) Mashaka alitafuta vijikazi na vibarua ili kuweza kujikimu na kumlea Biti Kidebe aliyeugua.
viii) Mashaka na Waridi waliishi chumba duni cha kupanga.
ix) Maskini wengi waliishi katika mtaa wa Tandale ambako nyumba hazikujengwa kwa mipango na mpangilio maalumu.
x) Chumba cha Mashaka kilijengwa kwa madebe na kilikumbatiana na choo cha jirani.
xi) Wakazi wa Tandale waliishi maisha duni - walikosa hata vifaa vya kimsingi kama vile misala.
xii) Umasikini wa Mashaka unadhihirika pale aliposhindwa kuwapa wanawe malazi - wavulana walilala kwa jirani jikoni.
xiii) Binti zao Mashaka walibanana na mama yao kwenye kijichumba chao kidogo - Hii inaashiria umaskini.
xiv) Chumba cha mashaka hakikuwa na vitu vingi. Hakikuwa na meza wala kiti.
xv) Umasikini uliwabadilisha sura Mashaka na Waridi - Zilitosha kuwa kurasa za kusomea.

*(zozote 12 x 1 = al 12)*

(b) Mtindo katika dondoo.

i) Jazanda - Waridi, dhoruba kali.
ii) Uradidi - Kati ya maua ... ingawa maua mengi yapo.
iii) Tanakuzi / ukweli kinzani - maua yapi mazuri au mabaya zaidi.
iv) Swali balagha - na harufu yake je?
v) Tanakali ya sauti - lilikwanyuka kwanyu.
vi) Nidaa - mengi maua mashaallahu!
vii) Taswara oni - kila nilitazamapo Waridi.
viii) (viii)Methali - Baada ya dhiki faraja.
ix) Usambamba - na harufu yake je? ilipekecha harufu yake nzuri, harufu ya waridi.
x) Chuku - kila nilitazamapo waridi, sikosi kuonja chagizo cha uzuri wake.

*(zozote 8 x 1 = al 8)*

6. (a)

i) Barakala wapigwe vikali.
ii) Kizazi cha sasa wasiige wenye kutaka kugandamiza Kiswahili.
iii) Sindano kipigwe kikipatwa na maradhi.
iv) Kiswahili kifanywe lugha murwa.
v) Kitumike rasmi bungeni.
vi) Wataalamu wawe macho ili Kiswahili kilindwe.

*(za kwanza 4 x 1 = al 4)*

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

(b)
i) Ushauri / kuelimisha
ii) chuki / hasira / huzuni
iii) (iii) kuhamasisha *(yeyote 1 x 2 = al 2)*

(c) Nafsi nenewa - kizazi cha kisasa.
(i) Kinahimizwa kukitunza, kukitukuza na kulinda Kiswahili.
(ii) Kuhifadhi lugha ya Kiswahili kwa njia mwafaka. *(2 x 1 = al 2)*

(d) (i) inkisari : watalamu - wataalamu
sichafue - usichafue
kasema - akasema
kuleta urari wa mizani
(ii) kuboronga sarufi / kubananga sarufi
Kiswahili wakivunge - wakivunge Kiswahili
Barakala tuwapinge - tuwapinge barakala
Kwa sindano tukidunge - tukidunge kwa sindano
Kuleta urari wa vina
(iii) mazda / mazida - kisitawi - kistawi
kuleta urari wa mizani
*(za kwanza 2 x 2 = al 4)*

(e)
i) Mishororo minne
ii) Kila mshororo umegawika katika pande mbili.
iii) Mizani nane katika ukwapi na nane katika utao.
iv) Mshororo wa mwisho unarudiwa rudiwa katika kila ubeti.
v) Idadi ya beti ni sita. *(zozote 4 x $^1/_2$ = al 2)*

(f) (i) mathnawi - kila mshororo wa kila ubeti umegawika katika pande mbili.
(ii) pindu - neno moja au maneno ya ubeti wa kwanza kutumiwa kama ukwapi wa ubeti unaofuatia.
*(2 x 2 = al 4)*

(g) (i) mfawadhi - jitihada
(ii) Barakala - wanaoiga desturi za kigeni
(iii) maamuma - watu
(iv) muenge - kujitayarisha
*(zozote 4 x $^1/_2$ = al 2)*

7. (a) kuwahimiza watu hasa wanyonge wainuke na kupinga maovu na maonevu wanayofanyiwa na mabwenyeye wenye uwezo
*(1 x 2 = al 2)*

(b) (i) msuko : kibwagizo kimefupishwa
(ii) kikwamba : katika beti 3, 4 na 5 neno moja ndilo linaanza kila mshororo.
(iii) sakarani : kuna bahari kadhaa katika shairi
(iv) ukawafi : una vipande vitatu (ukwapi, utao na mwandamizi) katika mishororo ya kwanza mitatu ya kila ubeti isipokuwa kibwagizo.
*(za kwanza 3 x 1 = al 3)*

(c) (i) mishororo minne
(ii) vipande vitatu katika mishororo ya kwanza mitatu na kimoja katika kibwagizo.
(iii) mshororo wa mwisho kurudiwarudiwa
(iv) mizani 2 - 6 - 8
2 - 6 - 8
2 - 6 - 8
4
*(za kwanza 3 x 1 = al 3)*

(d) (i) Tabdila : mamiya- mamia

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(ii) inkisari : vumiliyo - kuvumilia ; naandika - ninaandika
(iii) kuboronga sarufi : maudhi tuyasikiayo - tuyasikiayo maudhi.

*(za kwanza 2 x 1 = al 2)*

(e) (i) Kinaya - watukufu wenye nayo
(ii) swali la balagha - kwa hayo uyaonayo?
(iii) Takriri : hawa ; bado ; mamiya
(iv) Taharuki: Naandika!

*(4 x 1 = al 4)*

(f) (i) Neno -awa ; naandika ; bado
(ii) Silabi - ya ; yo
(iii) kikundi cha maneno / kirai - mamiya mamiya

*(za kwanza 2 x 1 = al 2)*

(g) Hawa wanaotulimia wanavumilia dhiki
wao ni wengi na ndio huzalisha mali
wao ndio wanaoumia na kupata mateso / taabu
wanayokumbana nayo hivyo ninaandika / ninasema

*(4 x 1 = al 4)*

8. (a) Kuainisha wimbo kwa kuzingatia maudhui.
(ii) Wimbo wa harusi - mchukueni huyo tumewakabidhi
- msio na wapishi

*Kutaja - al 1* *mfano al 1*

(b) Sababu ya utungo huu kuwa ngonjera.
(i) Kuna mazungumzo ya kulumbana na kujibizana kati ya upande wa bwana harusi na wa bibi harusi.

*(1 x 2 = al 2)*

(c) Sifa za jamii.
(i) Ulipaji mahari - Mitamba imepokelewa.
(ii) Wazee kuwa na nafasi katika ndoa - mitamba imepokelewa na wazee.

*(kwanza 2 x 1 = al 2)*

(d) Sifa za ushairi simulizi katika utungo huu.

- Utungo huu huwasilishwa kwa njia ya mdomo mbele ya hadhira kwa kukaririwa, kughaniwa au kuimbwa.
- Huweza kubuniwa papo hapo na kuwasilishwa kwa hadhira hai au tungo za awali huwasilishwa kutoka kwa kumbukumbu za mwasilishaji.
- Utungo huu hutolewa ukiambatana na ala za muziki k.v njuga na marimba.
- Utungo huu ni sehemu ya utamaduni wa jamii na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Hutumia lugha yenye mvuto mkubwa; yenye mapigo yaliyopangwa kwa muwala na urari.
- Huweza kuwasilishwa na mtu mmoja au kundi la watu.
- Hubadilika kulingana na anayeuwasilisha, hadhira na wakati. Wimbo mmoja unaweza kuimbwa kwa mahadhi mbalimbali kulingana na mwimbaji.
- Mwimbaji anaweza kushirikisha hadhira yake katika uimbaji kwa kupiga makofi.
- Huandamana na uigizaji mwimbaji, kwa mfano, huambatanisha maneno yake na vitendo kama vile ishara za uso, ishara za mkono.
- Hufungamana na shughuli au muktadha kama vile nyimbo za harusi huimbwa wakati wa harusi.
- Hutumia lugha ya kitamathali kunaweza kuwa na misemo, nahau, jazanda na istiara.

*(zozote 6 x 1 = al 6)*

(e) (i) Manufaa manne ya hojaji.

- Hojaji huwa na gharama ya chini.
- Mtafiti anaweza kufikia idadi kubwa ya watoaji habari kwa kipindi kifupi kwa sababu hojaji nyingi zinaweza kutumwa hata kwa njia ya posta.
- Inaweza kutumika katika mahojiano kama mwongozo. Mhoji anaweza kuitumia katika mahojiano kufidia udhaifu wa mhojiwa.
- Humpa mhojiwa muda wa kuwazia maswali na kuyafanyia uchunguzi kabla ya kuyajibu.
- Hojaji kwa kawaida hazina athari za mtafiti kwa sababu, aghalabu mtafiti hayupo zinapojazwa . Mhojiwa hujaza habari za kweli bila kushinikizwa kuchukua mtazamo fulani kutokana na kuwepo kwa mtafiti.

*(za kwanza 4 x 1 = al 4)*

(f) (ii)Changamoto nne za hojaji.

- Maswali yenye utata husababisha fasiri mbalimbali ambazo hufanya matokeo yasitegemeke.
- Huenda watu wakakosa kuijaza hojaji kwa kikamilifu kwa sababu mbalimbali kama vile kuhofia lawama au watu wakakataa kujaza kabisa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Hojaji ikiwa ndefu sana huenda baadhi ya watu wakakataa kujaza kabisa.
- Hojaji wazi huwa ngumu sana kwa mtafiti kuchanganua data. Uchanganuzi hichukua muda mrefu.
- Huenda wahojiwa wasijaze mambo ya kweli si rahisi kwa mtafiti kudhibisha iwapo habari ni za kweli.
- Wahojiwa wanaweza kuchelewa kutuma hojaji zao, hasa hojaji zilizotumwa kwa posta.
- Baadhi ya wazee, japo wana habari za kutegemewa, hawajui kusema na kuandika.
- Kwa vile mtafiti hakabiliani ana kwa ana, hawezi kupata sifa za uwasilishaji wa vipera vya fasihi simulizi kama vile toni na kidatu. *(za kwanza 4 x 1 = al 4)*

**KIRINYAGA**
**KIDATO CHA NNE - 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI - INSHA 102/1**

1. Huu ni utungo amilifu. Vipengele viwili vikuu vya utungo wa aina hii vishughulikiwe.
   (a) Maudhui
   (b) Muundo

(a) Muundo wa memo.
- Mtahiniwa azingatie muundo wa juu (sura) wa memo.
- Vipengele vifuatavyo vya kimsingi vizingatiwe.

i) Nembo na anwani ya kampuni ya Tononoka iandikwe juu, katikati ya karatasi wala si pambizoni.
ii) Nambari ya marejeo / kumbukumbu ya marejeleo kwa mfano:- kumb /Rej.J.K / Jumla/
iii) Tarehe - Inaweza kuandikwa pambizoni kwenye mstari mmoja na nambari ya kumbukumbu.
iv) Mtajo -
   (a) Kutoka kwa : Mkurugenzi
   (b) Kwa : wafanyikazi wote
(v) Mada / kuhusu: Maenezi ya ugonjwa wa uviko - 19
(vi) Utangulizi : Mtahiniwa atangulize kiini cha memo.
(vii) Mwili - Hapa ndipo hoja zitakapojadiliwa.
   - Hoja zipangwe kiaya.
(viii) Hitimisho:
   Mtahiniwa ahitimishe utungo wake.
   Hapa anaweza kujumuisha hatua ambazo zitachukuliwa kwa wasiozingatia kanuni za wizara ya afya.
(ix) Kimalizio -
   Muundo wa mwisho wa memo udhihirike kama ifuatayo:-
   (i) Sahihi
   (ii) Jina
   (iii) Cheo (si lazima)
   (iv) Nakala kwa k.m
      (a) Mkurugenzi
      (b) Wakuu wa vitengo. (si lazima)

(b) <u>Maudhui.</u>
- Mtahiniwa aibue hoja zinazohusiana na kutozingatia kanuni za kuzuia ueneaji wa ugonjwa wa uviko - 19.
- Kanuni za kuzuia uenezaji wa uviko - 19
   (a) Nawa mikono kila mara.
   (b) Kuvaa barakoa.
   (c) Epuka kugusa uso na pua.
   (d) Safisha / takasa sehemu za umma.
   (e) Epuka mikusanyiko ya watu.
   (f) Funika mdomo na pua unapopiga chafya .
   n.k

<u>Hitimisho.</u>
Hitimisho inaweza kujumuisha hatua ya kinidhamu kulingana na wizara ya afya.
   (i) Kupewa likizo ya lazima pengine bila malipo.
   (ii) Faini
   (iii) Kufungwa jela.
   (iv) Kushushwa hadhi kwenye kampuni.
- Mtahiniwa anaweza pia kuwahimiza wafanyikazi kuzingatia kanuni za wizara ya afya (bila kutoa onyo)
<u>Tanbihi.</u>
(i) Kwa vile hili ni onyo, mtahiniwa anahitajika kutumia lugha yenye toni kali au inayohimiza.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

2. Athari za dhuluma katika asasi ya ndoa.
   (i) Huweza kusababisha mauti / kifo / mauaji miongoni mwa wanandoa.
   (ii) Baadhi ya vita vya ndoa husababisha ulemavu wa viungo vya mwili kutokana na kujeruhiwa katika vita.
   (iii) Huzalisha talaka.
   (iv) Uharibifu wa mali na pia stakabadhi za elimu. Mfano, hasira kumfanya mmoja kutekeza stakabadhi, kurarua.
   (v) Athari za kisaikolojia kwa wahusika. Hupata msongo wa mawazo na mafadhaiko.
   (vi) Malezi ya watoto huathirika hivi kwamba watoto hutelekezwa kutokana na ugomvi mwingi wa vita vya wazazi.
   (vii) Huweza kuathiri maisha ya baadaye ya ndoa kwa watoto (watakapooa / kuolewa)

   *(Tathimini hoja zingine za mtahiniwa)*

   Athari kwa elimu ya watoto.
   (i) Watoto husheheneza utovu mwingi wa nidhamu kutokana na malezi mabaya nyumbani. Hii huchangia matokeo hasi masomoni.
   (ii) Watoto hulala sana nyakati za masomo shuleni. Hili hutokana kwa mfano na kutolala nyumbani kwa sababu ya vita vya wazazi usiku kucha.
   (iii) Watoto hukosa muda wa kudurusu na kufanya kazi ya shule wakiwa katika mazingira ya nyumbani.
   (iv) Watoto wengi huathiriwa na ukosefu wa karo kwa sababu wazazi hawana wasaa wa kupangia elimu ya watoto wao.
   (v) Kutelekeza watoto huathiri masomo ya watoto kwa kukosa ushauri nasaha wa wazazi.
   (vi) Watoto kugeuka dhulumati shuleni na kuishia kuadhibiwa mara kwa mara huathiri masomo yao.

3. Hii ni insha ya methali.

   Maana:-

   Kuwafanyia wema watu ni sawa na kujiwekea akiba. Huenda nao wakakutendea wema utakapouhitaji.

   Funzo: Usidhani unafanya kazi ya bure unapomfaa mtu fulani.

   Matumizi: Inaweza kuhimizwa anayefikiria kuwa wema autendao ni wa bure na kuwa hatafaidika hata akiendelea.

   Mtahiniwa aandike kisa kitakachodhihirisha pande zote mbili.

4. Hii ni insha ya mdokezo.
   - Mtahiniwa abuni kisa kitakachomalizia kwa maneno aliyopewa.
   - Kisa kionyeshe majuto ya mwandishi kwa kutofuata maagizo / sheria au ushauri wa wazazi na walimu.
   - Kisa kidhihirishe machungu, maafa, mashaka na magumu yaliyomkumba mtahiniwa maishani kutokana na kutofuata ushauri wa walimu na wazazi.
   - Kudinda kufuata maagizo na hatimaye kuingia au kupata hasara kukuzwe vizuri katika utungo wa mwanafunzi.
   - Sababu ya kujuta kwake ionekane wazi katika hadithi yake.

   Tanbihi.
   i) Kisa kizingatie nafsi ya kwanza umoja.
   ii) Mwandishi ajihusishe katika usimulizi la sivyo atakuwa amejitungia swali.
   iii) Wakati uliopita uzingatiwe.
   iv) Mtahiniwa asibadili mdokezo kwa namna yoyote.
   v) Mtahiniwa atakuwa amepotoka kimaudhui pale tu kitakosa kuoana na kimalizio hivyo kuandika yasiyohusiana na swali.
   vi) Atakayekosa kumaliza kwa kauli hii, na kisa kisioane na kiini cha swali atakuwa amejitungia swali.
   vii) Mtahiniwa akikosa kumalizia kwa kauli aliyopewa lakini kisa chake kioane na kiini cha swali, atakuwa hajapotoka kimaudhui, amepungukiwa kimtindo. Akadiriwe kulingana na masimulizi yake.

   - Watakaojadili upande mmoja wasituzwe zaidi ya alama kumi.

   Hoja za kuunga mkono.
   i) Kuondoa ufisadi kati ya walimu wakuu na wachapishaji.
   ii) Kuhakikisha kuna usawa kati ya wanafunzi wote.
   iii) Ufunzaji umerahihishwa.
   iv) Kuinua kiwango cha elimu.
   v) Kukomesha wizi wa vitabu.
   vi) Kuondolea wazazi mizigo.

   Hoja za kupinga.
   i) Shule kupokea vitabu kama wamechelewa.
   ii) Kuua biashara za kuuza vitabu vya kusoma.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

iii) Ushuru kupanda.

3. Maana ya methali ni kwa samaki aanzapo kuoza huanza kichwani.
Methali hii yaweza kutumiwa kupigia mfano jamii ambayo imeharibika au iliyozama katika uozo kwa kuwa viongozi wake wameharibika. Kwa mfano nchi ambayo haiendi vizuri kwa kukosa uongozi ufaao.
Mtahiniwa aandike kisa kimoja ambacho kinadhihirisha kuwa asasi yoyote ya jamii ambayo imepotoka huanzia kwa viongozi. k.m Iwapo watoto hawana maadili wazazi ndio waliotangulia kuyakosa.
4. Insha lazima iwe na kichwa.
Kisa lazima kioane na maneno aliyopewa.
Lazima mtahiniwa amalizie insha yake kwa maneno aliyopewa.
Asipomalizia kwa maneno hayo amekosa dondoo.
Kisa cha mwanafunzi kionyeshe hatari fulani ambayo mhusika anaepuka.
Mwanafunzi lazima ajihusishe katika kisa hicho.
Asipojihusisha basi amejitungia swali.

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA 2019.**

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtihiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa.
Kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yeye mawazo swali, ubunifu mwingi na hati nadhifu. Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hoja, msamiati na mtindo ili aweze kuikadiri kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyopendekezwa. Viwango vyenyewe ni A., B, C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**VIWANGO MBALI MBALI**
**KIWANGO CHA D - MAKI 01 - 05.**

1. Insha ya aina hii haieleweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika,uakifishaji usiofaa na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo, kimtindo n.k.
5. Kujitungia swali na kulijibu.
6. Insha ya urefu \.warobo ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**
**D - (Kiwango cha chini) Maki 01 - 02.**

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
4. Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
5. Kunakili swali au kichwa tu.

**D (Wastani)**
**Maki 3**

1. Mtiririko wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
3. Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+ (D YA JUU) MAKI 04 - 05**

1. Insha huwa na makosa mengi ya kila aina, lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.

**KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06 -10.**

1. Mtahiniwaanajaribu kushughulikia mada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.
2. Mtahiniwaanawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia / hana ubunifu wa kutosha.
3. Mtahiniwa anaakifisha sentensi vibaya.
4. Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
5. Insha ina makosa mengi ya sarufi. ya msamiati na ya tahajia (hijai)
6. Insha yenye urefu wa nusu ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C**
**C - (C YA CHINI MAKI 06 - 07**

I. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha haieleweki kwa urahisi.

**C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.
5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa.
6. Ana shida ya uakifishaji.
7. Anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka.

**C+ (C YA JUU) MAKI 09 -10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyokuwa na mvuto.
2. Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Ana shida ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi ya msamiati na ya hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.

**KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11-15.**

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
2. Mtahiniwa anatumia miundo tofautitofauti ya sentensi vizuri.
3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
4. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu. Hoja zisipungue nne katika kiwango hiki.
5. Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA B.**
**B -(B YA CHINI) MAKI 11-12**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofautitofauti akizingatia mada.
2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
4. Makosa yanadhihirika / kiasi.

**B WASTANI MAKI 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Mawazo yake yanadhihirika akizingatia mada.
3. Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Makosa ni machache.

**B+ (B YA JUU) MAKI 14 -15**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika waziwazi.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri. .

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

5. Uakifishaji wake wa sentensi ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa na pale.

**KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKI 16 - 20.**

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
2. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
3. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa urahisi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo
5. Insha ina urefu kamili.

**MAUDHUI.**

1. Maudhui hoja au mambo yanayozungumziwa,kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa. }
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

**MSAMIATI.**

- Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika.
- Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule.
- Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi.
- Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano maneno mapya yanaibuka kila uchao.

**MTINDO.**

Mtindo unahusu mambo yafuatayo:
. Mpangilio wa kazi kiaya. .
. Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
. Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
. Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano, methali, misemo, jazanda na kadhalika.
. Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika.
. Sura ya insha.
. Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

**SARUFI.**

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:
(i) Matumizi ya alama za uakifishaji. .
(ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa.
(iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
(iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
(v) Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
(vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
(vii) Matumizi ya herufi kubwa: .
(a) Mwanzo wa sentensi.
(b) Majina ya pekee.
(i) Majina ya mahali, maji, nchi, mataifa na kadhalika.
(ii) Siku za juma, miezi n.k.
(iii) Mashirika, masomo, vitabu n.k.
(iv) Makabila, lugha n.k.
(v) Jina la Mungu.
(vi) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa.- Foksi, Jak, Popi, Simba, Tomi na mangineyo.
(vii) Majina halisi ya watu k.m Maria, Rutto.

**MAKOSA YA HIJAI / TAHAJIA.**

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika;
(a) Kutenganisha neno kwa mfano ‘aliye kuwa’.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Kuunganisha maneno kwa mfano 'kwasababu'.
(c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile 'ngan-o' badala ya nga-no.
(d) Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano 'ongesa' badala ya 'ongeza'.
(e) Kuacha herufi katika neno kwa mfano 'aliekuja' badala ya 'aliyekuja'.
(f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile 'piya' badala ya 'pia'.
(g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j, i.
(h) Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
(i) Kuacha ritifaa au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom'be, ng'ombe, ngo'mbe n.k
(k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27- 08- 2013.

**ALAMA ZA KUSAHIHISHA.**

== Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.
___ Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokea kwa mara ya kwanza tu.
✓ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilikia pambizoni kushoto.
Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno / maneno.
✓ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.
X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofa. Alama hutiwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya✓ chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.
Maelezo yaonyeshe: Urefu wa insha k.v robo, nusu, robo tatu au kamili na udhaifu wa mwanafunzi.

**UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA.**

| | |
|---|---|
| Maneno 9 katika kila msitari. | Ukurasa mmoja na nusu |
| Maneno 8 kaitka kila msitari. | Ukurasa mmoja na robo tatu. |
| Maneno 7 katika kila msitari. | Kurasa mbili. |
| Maneno 6 katika kila msitari. | Kurasa mbili na robo. |
| Maneno 5 katika kila msitari. | Kurasa mbili na robo tatu. |
| Maneno 4 katika kila msitari. | Kurasa tatu na robo tatu. |
| Maneno 3 katika kila msitari. | Kurasa nne na nusu. |

**JUMLA YA MANENO.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) Kufikia maneno | 174 | lnsha robo asizidi alama | 05/20 |
| (b) Maneno | 175 - 274 | Insha nusu asizidi alama | 10/20 |
| (c) Maneno | 275 - 374 | Insha robo tatu asizidi alama | 15/20 |
| (d) Maneno | 375 - 400 | Insha kamili. | 20/20 |

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KIRINYAGA**
**KIDATO CHA NNE - 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI 102/2**

1. Ufahamu.
(a) Ugonjwa wa korona / maambukizi ya ugonjwa wa korona / Janga la korona.
*(1 x 2 = al 2)*

(b)
- Wananchi kotovaa barakoa kwa njia ifaayo.✓
- Kutozingatia umbali wa mita moja na nusu kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine.✓
- Watu kushikashika macho, pua ana midomo.✓
- Watu kutonawa mikono ipasavyo.✓

*(4 x 1 = al 4)*

(c)
- Viongozi wanawakusanya wananchi katika mikutano yao ya kisiasa. ✓ Hawazingatii kanuni za wizara ya afya katika mikutano hii.✓

- Baadhi hawavai barakoa na wanakosa pia kuhimiza wafuasi wao kuzivaa.✓
- Walilegeza kafyu,✓ walifungua vilabu.✓
- Waliruhusu ibada, mazishi na shughuli za harusi kurejelewa. ✓

*(3 x 1 = al 3)*

(d)
- Wananchi wote pamoja na viongozi wazingatie kanuni zilizowekwa na wizara ya afya.✓
- Kuzima kabisa mikutano ya kisiasa.✓
- Kupunguza mtagusano wa wananchi.✓
- Maafisa wa polisi waendelee kushika doria kuhakikisha wananchi wanafuata kanuni za wizara ya afya.✓

*(3 x 1 = al 3)*

(e) (i) takwimu -maelezo ya kihesabu yanayoeleza idadi ya vifo kutoka na korona.
(ii) mtagusano - mwingiliano wa watu katika shughuli mbalimbali.
(iii) doria - ulinzi wa zamu ili kuhakikisha sheria zilizoweka zinafuatwa.

*(Adhibu makosa sita ya hijai 6 x $^1/_2$ = al 3, ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi, usiadhibu zaidi ya alama uliyotuza)*


2. <u>Mwongozo wa ufupisho.</u>

(a)
- Vifaa vya kupuliza hewa ili kubainisha wanaoendesha wakiwa wamelewa.✓
- Serikali ilikatiza safari za usiku za magari na abiria.✓
- Magari yalilazimika kutwaa leseni mahsusi.✓
- Magari haya lazima yakaguliwe kila wakati.✓
- Magari yawe na madereva wawili watakaosaidiana.✓
- Madereva wawe wameidhinishwa na mamlaka ya usalama barabarani.✓
- Magari yawe na magurudumu sawasawa.✓
- Taa na breki ziwe timamu.✓
- Magari yanayopatikana na hatia, mwenyewe kushtakiwa na kupigwa marufuku njiani.✓
- Magari ya umma yawe na vidhibiti mwendo ili kupunguza kasi.✓
- Magari yawe na mikanda ya usalama.✓
- Magari yanahitaji kubeba idadi ya abiria iliyokubalika.✓
- Dereva na abiria iwapo watapatikana wamezidisha idadi watozwe faini papohapo.✓
- Idara ya polisi ina jukumu la kukagua magari na kuhakikisha hayasheheni uzito kupita kiasi.✓
- Kuwanasa wanaoendesha mwendo wa kasi na kuvunja sheria barabarani.✓
- Polisi wanatazamiwa kujiepusha na hongo.✓

*(Hoja 10, mtiririko 1)*

(b)
- Bali na madereva watumiaji wengine wanalo jukumu la kulinda usalama barabarani.✓
- Waendeshaji baiskeli na wana oenda kwa miguu wawe waangalifu.✓
- Wanapaswa kufuata sheria barabarani.✓
- Ni wajibu wa serikali kuhakikisha kuwa barabara ni bora.✓
- Usalama barabarani utaimarika ikiwa sheria zitazingatiwa kwa kuwa magari yameundwa ili kusaidia wala si kuhini.✓

*(Hoja 5, mtiririko 1)*
*Adhibu makosa 6 ya hijai 6 x $^1/_2$ = al 3*
*makosa 6 ya sarufi 6 x $^1/_2$ = al 3*
*maneno ya ziada : maneno 10 1Z*



a = 9
b = 4
u = <u>2</u>
15

3. Matumizi ya lugha.

(a) (i) /g/ - kipasuo
- hutamkiwa kwa kaakaa / laini

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

/z/ - kikwamizo / kikwaruzo / kikwamizwa

*(4 x $^1/_2$ = al 2)*

(b) Ajapo
alapo
ajaye n.k

*(1 x 1 = al 1)*

(c) Aliyekisahau
Tanbihi - mzizi uwe wa kitenzi cha asili ya kigeni. *2/0*

(d) Kucheka kwa Maria kuliwashangaza wengi au
Kicheko cha Maria kiliwashangaza wengi. *2/0*

(e) Nyua zilizokauka ni za mabawabu. *1/0*

(f) Mifano ya nomino katika ngeli ya l - l
Kama vile sukari, petroli, chumvi.
Sukari iyo hiyo ilimwagika. n.k *2/0*

(g) Kidege hiki kina viguu vidogo. *1/0*

(h) Kembo akiimba vizuri atatuzwa zawadi.
Kembo aimbapo vizuri atatuzwa zawadi.
Iwapo Kembo ataimba vizuri atatuzwa zawadi.
Ikiwa Kembo ataimba vizuri atatuzwa zawadi. *2/0*

(i) (i) Kubainisha maneno ya lugha nyingine yanayoingizwa katika lugha ya Kiswahili.
(ii) Kufungia majina ama anwani za vitabu, nyimbo, filamu. n.k *2/0*
(iii) Kufungia maneno yasiyozoeleka au ambayo hayajakubalika kama msamiati wa lugha fulani . Mambo yakiwa "poa".
(iv) Kufungia neno lenye maana tofauti na iliyokusudiwa yeye ni "karimu" ukimaanisha ni bahili.

*(2 x 1 = a 2)*

(j) Kuli hatakuwa amepakia shehena katika meli. *2/0*

(k) Omari angali anacheza soka.

(i) S✓

KN✓ KT✓

N✓ Ts✓ T✓ KN✓

N✓

Omari angali anacheza soka✓

*(8 x $^1/_4$ = al 2)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Atanishughulikia vizuri

S✓

KN✓ KT✓

O✓ T✓ E✓

atanishughukia vizuri □ *(6 x $^1/_3$ = al 2)*

(l) (i) Sehemu ya kitu kizima / akisami.
(ii) Kuonyehsa namna /hali. *(2 x 1 = al 2)*

(m) Wanafunzi watasimuliwa hadithi na mwalimu. *2/0*

(n) watumwa

*(1 x 1 = al 1)*

(o) mfano:
Yeye atawaimbia wageni wa rais. *3/0*

(p) nikahi / nikaha
mimba / ujauzito
*(2 x 1 = al 2)*

(q) kirimu / mzee aliwakirimu wanakijiji. *2/0*

(r) (i) Ishallah! kutakia heri.
(ii) Simile - Kutoa ombi la kupishwa.
*(2 x 1 = al 2)*

(s) Fuka - toa moshi
- sababisha kunukia
Vuka - toka upande mmoja hadi mwingine.
- zidi kiasi
- potoka
- kuwa uchi / toka nguo *2/0*

(t) Mchelea mwana kulia hulia yeye
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. *1/0*

(u) Kupotea kwa mbuzi kulimtia mchungaji wasiwasi. *2/0*

*(Adhibu makosa sita ya hijai 6 x $^1/_2$ = al 3, ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi, usiadhibu zaidi ya nusu ya alama uliyotuza)*

4. (a) *(al 2)*

(b) (i) Kuvutia / changamfu - ohee!
(ii) Maswali / udadisi - imefika, haijafika
(iii) Chuku - nyuso zinatangaza ushindi.
(iv) Mafumbo / misemo - kupaka tope
(v) Msamiati - ushindi
uchaguzi / siku mliongojea.
(vi) Swali balagha - Ni nani hajaona.
(vii) Kutozingatia sarufi - imefika, haijafika.
(viii) Kuchanganya ndimi - 'tyme
(ix) Utohozi - vote
(x) Ushawishi - Nawasihi , naomba
(xi) Urudiaji - ona
(xii) Mbinu rejeshi - Ni nani hajaona ... *(zozote 8 x 1 = al 8)*

Tanbihi. Hoja sharti iandamane na mfano au maelezo.

*(Adhibu makosa manne ya sarufi 4 x $^1/_2$ = al 2)*

*(Adhibu makosa manne ya hijai 4 x $^1/_2$ = al 2*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**

**SWALI LA LAZIMA.**

1. Umeteuliwa kama katibu wa kamati iliyochunguza suala la unyanyasaji wa wanawake na jinsi ya kukabiliana na hali hiyo katika wilaya yako. Andika ripoti kuhusu matokeo ya uchunguzi huo.

2. Ujenzi wa reli mpya hapa nchini utaleta faida kuliko hasara. Jadili.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Mbaazi ukikosa kuzaa husingizia jua.
4. Kamilisha insha yako kwa maneno …..Kuanzia siku hiyo mtazamo wangu wa maisha ukabadilika.

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA**
**MTIHANI WA NOVEMBA/DESEMBA**
**Cheti cha shule ya sekondari Kenya**
**Kiswahili – Karatasi ya 2**
**Lugha**
**KISWAHILI 102/2**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(Ufahamu,ufupisho,matumizi ya lugha na isimujamii)

**1.UFAHAMU (alama 15)**

***UFAHAMU (ALAMA 15 )***

***Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.***

Tutakuwa tunajidanganya tukianza kujitanua vifua na kusema kwamba Kiswahili hakina matatizo. Ni kweli kwamba Kiswahili kina hadhi kubwa kitaifa na kimataifa. Rais anaweza kuapishwa kuchukua wadhifa wake kwa Kiswahili. Mjumbe anaweza kuamka na kuhutubia kongamano la Muungano wa Afrika kwa Kiswahili. Unaweza kusoma Kiswahili kwenye mtandao wa wavuti au kukisikiliza katika idhaa za kitaifa na kimataifa. Unaweza kufundisha Kiswahili Marekani, Marakani, Uholanzi au Uingereza. Lakini huwezi kufumbia macho matatizo chungu nzima yanayoikabili lugha hii.

Usambazaji wa lugha huenda sambamba na uwezo wa wasemaji wa lugha. Wakoloni walikuwa na uwezo mkubwa. Walikuja na lugha zao wakatushikia shokoa tuzijue na tuzitumie; tupende tusipende. Ndiyo maana Afrika inakabwa koo na Kireno na Kiarabu au lugha nyingine za wenye nguvu. Walikuwa na uwezo na walitumia mtutu wa bunduki kuhakikisha wanatusemesha lugha zao. Kwa bahati mbaya, Kiswahili hakina wasemaji wenye uwezo wa kutumia mtutu wa bunduki kuwalazimisha watu kukisema. Hatusemi kwamba Kiswahili ni lugha ya wanyonge. La hasha! Tunasema kwamba wale waitwao Waswahili sio tabaka au kabila la watu au taifa lenye uwezo wa kuwadhibiti watu wengine na kuwamezesha ustaarabu wao. Hoja hapa ni kwamba wale wasemao Kiswahili huonwa kama wanyonge.

Kuna mwelekeo mbaya sana uliokithiri unaoshikilia. Kiswahili ni lugha ya ombaomba. Hapana shaka mwelekeo huo una dosari kubwa. Lakini upo. Kutokana na hilo wapo watu wenye heshima zao na akili zao razini ambao wanaona soni kuzungumza Kiswahili. Hawataki kuonekana hawakusoma au kisomo chao ni duni. Vile vile kuna wale ambao watakisema Kiswahili lakini hawaoni aibu kuzivunja kanuni zake za kisarufi. Wanaweza kuaibikia kubananga sarufi ya Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu lakini hawana haya na ndio wanaosema kuwa Kiswahili ni pungufu na hakiwezi kufundisha masomo changamano kama vile hisabati na sayansi, kana kwamba masomo hayo ni lugha sio taaluma. Yamkini wanaandama falsafa inayosema, "Mnyonge mnyongeni." Kama hili si tatizo labda itolewe fasili nyingine ya neno "tatizo" Kwa miaka nenda miaka rudi vyombo vya habari vimesaidia katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa miaka nenda miaka rudi vyombo vya habari vimesaidia katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hadhira vyombo hivi huwa ni ruwaza na vielelezo vya ufasaha wa lugha si hoja kama ni

redio, runinga au magazeti. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vya habari vimetepetea mno kiasi kwamba vimekuwa adui mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Inashangaza jinsi wamiliki wa vyombo hivi wanavyowapa ajira watu ambao kwa kweli umahiri wao wa lugha ya Kiswahili ni mdogo au haupo kabisa. Kuna wale waitwao wanahabari wanaohudumu katika vyombo vinavyotumia Kiswahili lakini ambao ni vielelezo vya vile Kiswahili kisivyopaswa kusemwa au kuandikwa. Hii ni tanzia kwa maendeleo ya Kiswahili. Tunadahili kwamba vyombo vya habari vinachangia katika "kukinyonga" Kiswahili.

Kwa hakika "wanyongaji" wa Kiswahili ni wengi. Miaka ya mapema ya themanini palizuka kilugha cha vijana kilichopewa jina la Sheng. Nimcheshi mmoja aliyesema urefu wa Sheng ni "Shemeji Hakuna Elimu, Gura." Sheng ndiko walikohamia au kuguria vijana kilugha nje ya mawanda ya elimu. Walitaka kujificha kwenye kwapa za vijineno visiyoeleweka na wazazi wao. Sasa ajabu ni kwamba waliokuwa wakisema Sheng zama hizo, wenyewe wamekuwa wazazi. Na bado wanasema Sheng. Hatimaye Sheng imekuwa lugha ya taifa isiyo rasmi. Inazungumzwa nyumbani, arusini, matangani, kanisani, redioni na kuandikwa magazetini. Kwa sababu sheng "imeiba" maneno mengi kutoka kwenye Kiswahili sanifu na kuyasongoa, inakuwa taklifu kujua tofauti. Wanafunzi wanatatizika kupambanua baina ya Sheng na lugha sanifu katika insha na maandishi yao.

Ipo hatari kwamba Sheng ikishamiri sana kama inavyoendelea kushamiri, watu wachache sana wataweza kuzungumza na kuelewa Kiswahili sanifu. Kiswahili sanifu kinaweza kujikuta kimeenguliwa kutoka kwa hadhi ya lugha ya taifa hadi kuwa lugha ya kigeni. Hata pengine hilo limeanza kutokea tayari. Si ni kweli kwamba kwa baadhi ya maashiki wa Sheng Kiswahili ambacho ni Kiswahili kweli kinawatanza kama vile wanavyotanzwa na Kichina au Kiyunani? Wanapotazama habari za Kiswahili kwenye runinga wanabaki kutumbulia macho picha pasi kuelewa msamiati unaotumiwa. Kiswahili kinastahimili makuruhu mengi, na mengine hutoka vyanzo visivyotarajiwa. Asasi zinazohusika na Kiswahili pia huchangia kudorora kwa hali ya Kiswahili. Kosa kubwa lilipo ni ukosefu wa ushirikiano. Kuna ukosefu wa ushirikiano kati ya watengenezaji wa bidhaa au watoaji huduma wa matangazo ya kibiashara. Kila uchao kiwango cha Kiswahili kwenye matangazo ya kibiashara kinaendelea kudidimia.

Mathalani, unaposoma au kusikia kauli kama vile "net iliyotibiwa" kama tafsiri ya treated mosquito net, unajiuliza kama kitu kinachorejelewa kilikuwa kinaugua ugonjwa gani. Si vigumu kushuku kwamba watu wengi wanaotafsiri matangazo ya kibiashara ni malimbukeni wasiojue mbele wala nyuma ya tafsiri. Labda wapo Wakenya wengine wenye uwezo mkubwa wa tafsiri lakini ambao ushauri na uhusika wao haukutafutwa. Ukweli huu ndiyo tanzia ya lugha hii. Kuna watu waliojiambika ubingwa na kuaminiwa ni mabingwa na kupewa majukumu ambayo si kiasi chao kuyatekeleza. Tokea ni tafsiri zenye taksiri. Hili linatuleta katika swala zima la ushirikiano. Kwa sababu Kenya ina wasomi wengi waliotaalamika katika Kiswahili mbona hawashirikiani kuunda chombo mahsusi kukiendeleza Kiswahili? Ni kweli kwamba vyama kadha vimekuwa vinabuniwa na kujiita vyama vya Kiswahili, lakini aghalabu shabaha ya waasisi wa vyama hivyo ni kujifaidi wenyewe. Huu ubinafsi unahujumu juhudi za ushirikiano na asasi nyingine za ndani na nje ya nchi kukiendeleza Kiswahili.

Ni fedheha kwamba ingawa Kenya huhesabiwa kuwa nchi inayozungumza Kiswahili, wanafunzi wa kigeni wanaotaka kujifunza Kiswahili sanifu husafiri hadi Tanzania kufaidi uhondo wa Kiswahili hicho. Dar es Salaam imegeuzwa Makkah ya Kiswahili, ambako wanaokiwania wanakimbilia kuhiji. Matatizo yanayokitanza Kiswahili yasipotanzuliwa Kenya itaendelea kuwa tanbihi tu katika kurasa za matini ya lugha azizi ya Kiswahili.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

1. Taja matatizo manne yanayokumba Kiswahili. ( alama 2 )
2. Pendekeza njia nne za kuyashughulia matatizo haya. (alama 4 )
3. Unafikiri hoja ya mwandishi kwamba hatimaye Sheng itakuwa lugha ya taifa ni kweli? Eleza (alama 2)
4. Vyombo vya habari vimechangia kiasi kikubwa kwa matatizo yanayokumba lugha ya Kiswahili. Eleza. ( alama 4 )
5. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye kifungu: (alama 3)
   (a) Taksiri
   (b) Tanzia
   (c ) Wakatushikia shokoa

**2. UFUPISHO (alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Kuna haja ya serikali ya Kenya kuwa na sera mwafaka ya ukuzaji wa Kiswahili, ili kiweze kukabiliana na maendeleo ya teknolojia. Jambo hili limepuuzwa siku nyingi. Ni vyema ifahamike kwamba umilisi wa lugha unawezesha mawasiliano yenye ufanisi kwa sababu mwasiliniaji anaweza kujieleza kwa ufasaha. Kwa jinsi anaweza kuhusiana na hadhira vizuri na kufanikisha mawasiliano yaliyo na tija katika maendeleo.

Ingawa kwa sasa Kiswahili kinatumika katika nyanja mbalimbali za maendeleo sehemu za mashambani, ufanisi mkubwa zaidi utapatikana ikiwa Kiswahili kitapewa uzito zaidi kupitia michezo ya kuigiza, hadithi na sarakasi zilizo na dhamira ya maendeleo. Mtindo huu unapendelewa sana na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulika na maswala ya idadi ya watu katika kuhamasisha umma kupanga uzazi na kupunguza idadi ya watu. Iwapo mtindo huu utatumiwa na watalamu wanaowahamasisha wananchi kuhusiana na maswala ya maendeleo huku lugha ya Kiswahili ikitumiwa bila shaka lugha hii itakuwa na nafasi kubwa ya kufanikisha maendeleo.

Kuna haja ya kutumia Kiswahili katika vyombo vyote vya habari kama redio, majarida na hata kanda za video kusambaza habari zinazohusiana na maendeleo. Kwa sasa idhaa za redio ndizo hutumia Kiswahili kwa wingi ilhali runinga zinatumia lugha hii kwa kiasi tu. Lugha ya Kiswahili haijatumika kuandika majarida ya kilimo, afya au uchumi ilhali Kiingereza ndicho kilichotawala katika uwanja huu. Matokeo ya mwelekeo huu ni kwamba idadi kubwa ya watu wasio na elimu katika sekta zote za maendeo hawaelewi mambo mengi ambayo yangewafaa kujiendeleza kwa vile Kiingereza hakieleweki kwao.

Vilevile kuna haja ya kutafsiri matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini Kenya na kwingineko kwa lugha ya Kiswahili ili maarifa ya tafiti hizo ziwafikie walio wengi na wanaoelewa Kiswahili. Hili likifanyika tafsiri hizi zinapaswa kuwekwa katika sehemu maalum za maktaba za kitaifa na vituo vya kijamii vinavyowahamasisha wananchi kuhusu maswala ya maendeleo. Kwa jinsi hii, maarifa mapya yatawafikia Wakenya wengi. Maarifa tunayoyazungumzia hapa ni pamoja na yale yanayopakuliwa kutoka kwenye tovuti. Katika mustakabali huu, mradi wa kampuni ya Mikrosoft wa kufikisha teknolojia ya mawasiliano hasa kwa tovuti sehemu za mashambani hauna budi kuigwa na kuungwa mkono na serikali ya Kenya. Iwapo utafanikiwa, utawezesha watu ambao wana elimu kupakua maarifa hasa maafisa wanaohamasisha maendeleo, na kuyaeneza kwa watu wengine kwa kutumia Kiswahili.

Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza uenezaji wa Kiswahili na matumizi yake hasa katika maeneo ya mashambani. Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wana jukumu la kufanya hivi ili kupendekeza hatua za kufanikisha lugha hii.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 90 – 100 (alama 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika aya ya nne. (Maneno 40 – 50) (alama 5, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

**a)** Akifisha

huenda serikali ikawazia kusimamia uagizaji wa bidhaa zinazotumiwa kuthibiti maenezi ya janga la korona hatuwezi kuwaruhusu matapeli wachache kuendelea kujinufaisha kwa njia zisizofaa alisema waziri wa usalama rasilmali nyingi za serikali zinatumiwa vibaya na watu wachache (alama 4)

b) Andika umoja

Kusoma huku kutachukua muda mrefu kuliko kiasi. (alama 1)

c) Tunga sentensi kwa kutumia nomino inayotokana na kitenzi ‘durusu’ (alama 2)

d) Andika sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi -li- (alama 4)

e) Tumia kihusishi katika sentensi hii. (alama 1)

Wanafunzi wamo darasani

f) Andika sentensi mbili kuonyesha maana mbili tofauti za neno,**kina** (alama 2)

g) Ipambanue sentensi hii kwa njia ya mistari

Agnes na Amina ndio waliokuwa wakisaidiana masomoni. (alama 4)

h) Andika sentensi moja moja ukitumia vitenzi hivi. (alama 2)
la
fa

i) Andika upya ulivyoagizwa kwa maneno yaliyo mabanoni.
Mtoto wa miaka kumi na miwili alilazimishwa kuolewa kwa jizee lile. (tendwa) (alama 2)

j) Tumia **-ndi-** pamoja na viambishi vya ngeli kujaza nafasi zilizoachwa. (alama 1)
Hapo ___________liangaziapo mwezi nuru..
Viwavi _______________ waharibuo mimea.

k) Onyesha iliko shadda katika maneno yafuatayo. (alama 1)
Mbu ________________________________________
Fadhaika ______________________________________

l) Andika sentensi kwa viunganishi hivi vifaavyo. (alama 2)
Isije ikawa
Huenda ikawa

m) Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)
Jua nisemalo ni muhimu kwetu.

n) Tumia kiashiria kisisitizi kuikamilisha sentensi hii. (alama 1)
Aliivaa nguo _________________jana.

o) Tambua sauti ambazo si vikwamizo /l/,/th/,/j/,/s/,/ny/,/f/,/a/ (alama 1)

p) Ainisha viambishi katika neno **'kujidhiki'** (alama 2)

r) Andika tofauti iliyomo katika sentensi hizi. (alama 1)
Ningejua ningetia juhudi masomoni.
Ningalijua ningalitia juhudi masomoni.

s) Kanusha (alama 1)
Mumetambua umuhimu wa masomo sasa.

t) Andika sentensi yenye visehemu vifuatavyo. (alama 1)
Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja
Kiambishi cha wakati ujao
Kirejeleo
Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu wingi (kitendwa)
Mzizi wa kitenzi
Kauli ya kutenda

u) Taja na ubainishe viwakilishi katika sentensi hii. (alama 2)
Huyu anataka kuona chako ulichoandika.

v) Andika katika usemi halisi.
Mwalimu alipotuuliza ikiwa tulitaka kusoma riwaya wakati wa alfajiri tulimjibu kwamba tungefurahia kufanya Hesabati kwa kuwa hali ya anga ilikuwa bado tulivu. (alama 2)

w) Onyesha kishazi huru katika sentensi hii. (alama 1)
Mwalimu aliyeingia darasani akihema hakutusalimu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**4. ISIMUJAMII (alama 10)**

Wewe ni daktari katika hospitali ya kifahari zaidi katika kaunti ya Kakamega. Umealikwa kuwashauri wanafunzi wa Shule ya Upili ya Tujizatiti kuhusu tahadhari wapaswazo kuzingatia kujilinda dhidi ya maambukizi ya virusi vya COVID- 19.Fafanua sifa kumi za sajili utakayotumia.

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**NOVEMBA/DESEMBA 2020**

**SEHEMU A: USHAIRI.**

**1. LAZIMA.**

*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**SABUNI YA ROHO.**

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Ndiwe suluhu za zama, waja wakukimbilia,
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani,
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Matajiri wanakujua, wema wako wameonja
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja
sura zao 'mefufua, wanazuru kila nyanja,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, onana na maskini,
Watazame mayatima, kwao kumekua duni,
Wabebe waliokuwa, wainue walio chini,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, wapi kapata uwezo,
umezua uhasama, waja kupata mizozo,
Ndiwe chanzo cha zahama, umewatia vikwazo,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Umevunja usuhuba, familia zazozana,
waliokuwa mahabuba, kila mara wagomabana,
Roho zao umekaba, majumbani wachinjana
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,
Sinilipue jabomu, sije kawa marehemu,
Niondoe jahanamu, ya ufukara wa simu
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika,
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,
Nichekeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI.**

a) Taja nafsi nenewa. Thibitisha. (al.2)
b) Eleza toni ya nafsi neni. (al.1)
c) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili. (al.4)
d) Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika mleo wa ubeti wa sita? (al.1)
e) Ukitoa mfano eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (al.3)

f) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (al.4)
g) Jadili jinsi mshairi anatumia idhini ya mshairi. (al.2)
h) Kwa kurejelea mpangilio wa vina eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa. (al.1)
i) Fafanua maana ya: (al.2)
   i) Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.
   ii) Jehanamu.

**SEHEMU B: TAMTHILIA**
**Pauline Kea: Kigogo**
**Jibu swali la 2 au 3.**

2. "Tunajivunia kuwa na Kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji sumu ya nyoka barani."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
   b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (al.2)
   c) Kwa kutumia mifano mwafaka, onyesha kwa hoja kumi na nne jinsi sumu ya nyoka ilivyoathiri eneo la sagamoyo katika tamthilia ya kigogo. (al.14)
3. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi.
   a) Jazanda (al.10)
   b) Majazi (al.10)

**SEHEMU C: RIWAYA**
**Assumpta K. Matei: chozi a heri**
**Jibu swali la 4 au 5.**

4. "Mustakabali wa ukuaji wetu kiuchumi uligonga mwamba wakati sheria ya mkoloni ilipompa mzungu kibali cha kumiliki mashamba…."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
   b) Kwa kutolea mfano, tambua tamathali ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (al.2)
   c) Bainisha na ueleze maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (al.4)
   d) Jadili jinsi ambayo sheria za mkoloni za kumiliki mashamba zilivyowaathiiri waafrika katika Riwaya hii. (al.10)
5. "Baba umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusima dede?
   a) Jadili umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili. (al.10)
   b) Kwa kutolea mifano mwafaka onyesha ukweli wa kauli iliyotajwa hapo juu kwa mujibu wa Riwaya ya chozi la Heri. (al.10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: HADITHI FUPI.**
A. Chokocho na D. Kayanda: Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine.
Jibu Swali la 6 au 7
6. "………Wanafunzi wa chuo kikuu si kama watoto vikembe wa shule ya chekechea…."
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
   b) Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotumiwa katika dondoo hili. (al.2)
   c) Eleza sifa mbili za msemaji wa maneno haya (al.4)
   d) Hadithi hii inadhihirisha utegemezi wa binadamu. fafanua. (al.12)

7. "…..Naapa na mola wangu sitafanya tena biashara hii."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
   b) Biashara inayorejelewa ilikuwa na athari hasi kwa jamii. Huku ukirejelea hadithi ya Mkubwa, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja nane. (al.16)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.**

Lala toto lalax2
Mama anakuja lala
Atakuletea ndizi
lala toto lala….
Mama akupenda lala,
Ameenda sokoni lala.

a) Huu ni wimbo wa aina gani? thibithsa. (al.2)

b) Kando na aina hii ya wimbo taja na ufafanue aina mbili za nyimbo. (al.2)
c) Dondoa na ueleze maudhui yoyote mawili katika wimbo huu. (al.2)
d) Tambua shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii husika ukitoa sababu zako. (al.4)
e) Ni tamathali gani ya lugha iliyotamalaki katika wimbo huu. Toa mfano. (al.2)
f) Eleza majukumu manne ya nyimbo katika jamii. (al.4)
g) Eleza njia nne ambazo ungetumia katika kukusanya kipera hiki cha fasihi simulizi katika jamii. (al.4)

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA KWANZA**
**INSHA 102/1**
**MWEZI WA NOVEMBA/DESEMBA 2020**

**1. <u>RIPOTI.</u>**
- ✓ Mwanafunzi azingatie muundo/sura ya ripoti. Kichwa kionyeshe ripoti ya nani/kamati gani, kuhusu nini n.k

**<u>Utangulizi.</u>**
Mtahiniwa aleze.
i. Dhamira ya kamati
ii. Wanakamati pamoja na vyeo vyao.
iii. Muda ambao kamati ilichukua kufanya uchunguzi.
iv. Mbinu za ukusanyaji data.

**<u>matokeo ya Uchunguzi.</u>**
Mtahiniwa azingatie;
- ✓ Kutorithi mali ya wazazi
- ✓ wanawake wajane kunyang'anywa mali na kufukuzwa
- ✓ kupashwa tohara/kukeketwa
- ✓ kutoelemishwa
- ✓ Ndoa za mapema
- ✓ Kubakwa
- ✓ kupigwa na kutusiwa
- ✓ kutalikiwa bila hiari
- ✓ kulaumiwa kwa utasa
- ✓ kufanyishwa kazi za nyumbani kama mtumwa.
- ✓ Kunyimwa ajira kwa vile akipata mimba atajikokota kazini na atahitaji likizo baada ya kujifungua.
- ✓ Ajira ya mtoto wa kike ambapo anafanyishwa kazi ya sulubu na kupewa mshahara duni.

(hoja zingine zozote)

**<u>Mapendekezo/suluhu.</u>**
- ✓ Hatua kali za kisheria kwa wanaopiga, wanaowabaka na wanaotekeleza mila ya tohara na ndoa za mapema.
- ✓ kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochangia udunishaji wa wanawake.
- ✓ Kuwashauri watoto wa kike badala ya kuwapasha tohara.
- ✓ kuelimisha mwanamke kuhusu haki zao
- ✓ kuwapa wanawake nafasi sawa za ajira na katika uongozi.
- ✓ kubuni sheria za kuwawezesha kumiliki mali.
- ✓ Kuanzisha makao ya watoto wa kike wanaotishiwa na mila mbaya.

**<u>HITIMISHO.</u>**
- ✓ Mtahiniwa atoe maoni, kauli, msimamo mradi yahusiane na mada husika.
- ✓ Insha ikikosa sura ifaayo akadiriwe ifaavyo kisha aondolewe alama 4 za sura.

2. Hii ni insha ya mjadala hivyo mwanafunzi aunge au apinge mjadala kwa kueleza faida na hasara.

**<u>kuunga – faida.</u>**
- ✓ Kuimarika kwa uchumi na biashara hapa nchini kwani bidhaa zitasafirishwa kwa haraka.
- ✓ muda mwingi wa usafiri utaokolewa
- ✓ Barabara zitaweza kudumu kwa muda mrefu kwa vile malori mazito yabebayo mizigo yatapungua barabarani.
- ✓ Nafasi za kazi zitaongezeka hasa kwa wanojenga reli hii.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- ✓ Gharama ya usafiri itapunguza hivyo kupungaza bei ya bidhaa.
- ✓ Mwingiliano baina ya watu utaimarika.

**Kupinga- Hasara.**

- ✓ Waendeshaji malori yabebayo mizigo na mabasi ya abiria watakosa nafasi za kazi.
- ✓ Wanaomiliki mabasi na malori wataathirika kwa kukosa au kupungukiwa na kipato.
- ✓ Gharama kubwa ya ujenzi itaathiri hata vizazi vijavyo kwa vile ni deni la kulipwa miaka mingi.
- ✓ Kuathirika kwa watu wanaohamishwa kutoka mashamba yao ili ujenzi ufanyike.
    - Mtahiniwa asiwe na hoja chini ya tano. Aliye na tatu asipite kiwango cha C+, hoja moja au mbili asipite kiwango cha C-.
    - Hoja zote zijadiliwe kikamilifu
    - Akishughulikia upande mmoja tu bila kugusia upande wa pili asipite kiwango cha C+.

3. Mbaazi ukikosa kuzaa husingizia jua.

- ✓ Kisa kidhihirishe hali ya mtu anayeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo kisha kumlaumu mwenzake kwa makosa au kutofaulu kwake mwenyewe.
- ✓ Atunge kisa kimoja tu, na wala sio visa
- ✓ Kisa kiwe na urefu ufaao na kioane na methali.
- ✓ Kisa kisichooana na methali, apate 03
- ✓ Akiegemea upande mmoja tu wa methali, asipite kiwango cha C+

4. Kisa cha mtahiniwa kimalizikie kwa maneno ya mdokezo aliyopewa.

- ✓ Atakayeanza na maneno ya mdokezo atakuwa amepotoka na atuzwe kiwango cha D.
- ✓ Asipomalizia kwa mdokezo aliopewa na kisa chake kihusiane na mdokezo, atakuwa hajapotoka kimaudhui bali amepungikiwa kimtindo.
- ✓ Ajihusishe na kisa (atumie nafasi ya kwanza).
- ✓ Asiyejihusisha amelemewa kimtindo.

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA**
**MTIHANI WA NOVEMBA /DESEMBA 2020**
**MWONGOZO WA UTAHINI WA KISWAHILI 102/2**
**DISEMBA 2020**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Majibu ya ufahamu – Matatizo yanayokumba Kiswahili.

1. Matatizo yanayokumba Kiswahili.

i) Kuwepo kwa kasumba ya kikoloni miongoni mwa baadhi ya watu kuhusu matumizi ya Kiswahili.
ii) Kutowepo kwa sera madhubuti au imara kuhusu matumizi ya Kiswahili.
iii) Ukosefu wa mwongozo kuhusu uendelezaji wa misamiati na istilahi za Kiswahili.
iv) Kutopendelewa kwa Kiswahili kunakotokana kwa lugha nyingine kama Kiingereza, Kijerumani, Kifaransa, n.k
v) Ukosefu wa wataalamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili.
vi) Ukosefu wa wataalamu wa kutosha humaanisha kuwa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia ifaayo unakabiliwa na tatizo kubwa.
vii) Kutokuwepo na waandishi wa kutosha wanaoandika katika lugha ya Kiswahili.
viii) Kuzuka na kuenea kwa lugha ya Sheng miongoni mwa wanajamii.
ix) Ukosefu wa vitabu bora vya kuwasaidia wanaojifunza lugha hii.
x) Mashirika ya uchapishaji kuelekea kukipa Kiingereza kipaumbele katika uchapishaji wao.
xi) Uhaba wa magazeti au majarida ya Kiswahili ambazo ni msingi muhimu wa uzambazaji wa lugha.
xii) Kuendelea kutumiwa kwa lugha ya Kiingereza katika shughuli nyingi nyingi za kitaifa.
xiii) Ukosefu wa chombo cha kuiendeleza lugha ya Kiswahili kama taasisi ya Kiswahili n.k.
xiv) Kutokuwepo msukumo wa kutosha miongoni mwa wanasiasa au wanaopanga sera kuihusu lugha ya Kiswahili.
xv) Ukosefu wa utafiti wa kutosha kuhusu tofauti za lugha ya Kiswahili.

2. Jinsi ya kuyashughulikia matatizo yanayokumba Kiswahili.

i) Kutilia mkazo ufundishaji ufaao wa ya Kiswahili
ii) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika nyanja nyingi za maisha yetu.

iii) Kupitishwa kwa sera nzuri inayoweka wazi malengo ya serikali kuihusu lugha hii na kuota mwongozo ufaao hatima (destiny) ya lugha yenyewe.
iv) Kuhimiza kuwepo kwa idara za Kiswahili taasisi za juu ili kuendeleza utafiti wa Kiswahili
v) Kuwepo kwa sheria ambazo zinazohimiza wazi majukumu na nafasi ya Kiswahili nchini.
vi) Kubuniwa kwa vyombo vya kukiendeleza Kiswahili kama taasisi ya utafiti wa lugha hii.
vii) Raia kuhamasishwa na kukumbushwa umuhimu wa kuionea fahari lugha ya Kiswahili.
viii) Wachapishaji wanahimizwa kuchapisha machapisho ya lugha ya Kiswahili. Serikali inaweza kuzuka na vituo vya kuwafanya wachapishaji hao wasichelewe kuchapisha vitabu hivyo.
ix) Serikali kutoa au kutenga kasima (kiasi fulani cha fedha ) fulani ambayo inaweza kutumiwa kusaidia ukuzaji wa Kiswahili katika taasisi ya elimu.
x) Kuanzishwa kwa tuzo zinazowatunza waandishi wanaoandika kazi nzuri zinazosaidia ukuzaji wa Kiswahili.
xi) Kuhimizwa kuwepo kwa magazeti ya Kiswahili ambayo yatauzwa kwa bei inayowafanya wengi kuyamudu.
xii) Kuifanya lugha ya Kiswahili msingi muhimu katika taasisi za elimu. Kwa mfano, daktari asiweze kuwa daktari bila kuonyesha umilisi (uwezo) mzuri wa lugha ya Kiswahili.
xiii) Kuwepo kwa vipindi vya redio na runinga ambavyo vinahimiza matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili.
xiv) Kuhimiza raia kutambua kuwa Kiswahili ni msingi muhimu wa kujitambulisha kama raia wa nchi hii.

3. La. Haiwezi kuwa lugha ya taifa kwa kuwa haina sarufi na inabadilika kila uchao. Ndio, iwapo itiatumiwa na wengi na kusambaa kwa namna ambavyo itatumiwa kwa mapana na marefu katika maisha ya jamii.
4. Vyombo vya habari na matatizo ya Kiswahili.
   (i) Baadhi ya vyombo vya habari vimetepetea kwamba vimekuwa adui mkubwa wa lugha ya Kiswahili.
   (ii) Baadhi ya vyombo vya habari vimewapa ajira watu ambapo umahiri wao wa lugha ya Kiswahili ni mdogo au haupo kabisa. Kuna wale waitwao wanahabari wanaohudumu katika vyombo vinavyotumia Kiswahili lakini ambao ni vielelezo vya vile Kiswahili kisivyopaswa kusemwa au kuandikwa. Hii ni tanzia kwa maendeleo ya Kiswahili. Kwa hivyo, vyombo vya habari vinachangia katika "kukinyonga" Kiswahili.
   (iii) Kuna ukosefu wa ushirikiano kati ta watengezaji wa bidhaa au watoaji huduma na waundaji wa matangazo ya kibiashara. Kila uchao kiwango cha Kiswahili kwenye matangazo ya kibiashara kinaendelea kudidimia.
   (iv) Tafsiri zipatikanazo katika vyombo vya habari ni za hali yachini na zinazodunisha hadhi ya Kiswahili na kukikoroga. Si vigumu kushuku kwamba watu wengi wanaotafsiri matangazo ya kibiashara ni malimbukeni wasiojua mbele wala nyuma ya tafsiri.

5. (i) Taksiri – kuwa na walakini, makosa.
   (ii) Tanzia – ukweli mbaya au mchungu.
   (iii) Wakatushikia shokoa – wakatulazimisha tuzije.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**2. UFUPISHO**
**Majibu**
(a) 1.Kuna haja ya serikali kuwa na sera mwafaka ya Kiswahili.
2.Umilisi wa lugha unawezesha ufanisi katika mawasiliano.
3. Mwasilianaji anaweza kuhusiana na hadhira na kufanikisha mawasiliano yaliyo na tija katika maendeleo.
4. Ufanisi mkubwa unapatikana ikiwa Kiswahili kitapewa uzito zaidi kupitia michezo ya kuigiza, hadithi na sarakasi.
5. Mtindo huu unapendelewa na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulikia maswala ya idadi ya watu.
6. Kuna haja ya kutumia Kiswahili katika vyombo vya habari.
7. Idhaa za redio hutumia Kiswahili zaidi kuliko runinga.
8, Lugha ya Kiswahili haijatumiwa katika majarida ya kilimo, afya na uchumi.
9. Watu wengi hawaelewi mambo amabyo yangewafaa kujiendeleza.
(hoja 8 x 1 = 8 utiririko alama 1)

(b) 1. Kuna haja ya kutafsiri matokeo ya tafiti zilizofanyika kwa lugha ya Kiswahili.
2. Tafiti hizi ziwekwe katika sehemu maalum ya maktaba ya kitaifa.
3. Kupitia hatua hii maarifa mapya yatawafikia wakenya.
4. Mradi wa Mikrosoft unapaswa kuungwa mkono.
5. Utawawezesha watu kupakua maarifa na kuyaeneza kwa wengine.
hoja 5 x 1 = 5 (utiririko = alama 1)

**i) Adhibu makosa ya hijai hadi 6. ½ alama kwa kila kosa.**
**ii) Adhibu makosa ya sarufi hadi 6 (½ alama kwa kila kosa.)**

**iii) Adhibu kosa mara moja tu, litokeapo kwa mara ya kwanza .**

**Tanbihi: jumla ya makosa iangaziwe katika sehemu zote mbili.**

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

**a)** Akifisha
**huenda serikali ikawazia kusimamia uagizaji wa bidhaa zinazotumiwa kuthibiti maenezi ya janga la korona hatuwezi kuwaruhusu matapeli wachache kuendelea kujinufaisha kwa njia zisizofaa alisema waziri wa usalama rasilmali nyingi za serikali zinatumiwa vibaya na watu wachache**
**(alama 4)**

**" H**uenda serikali ikawazia kusimamia uagizaji wa bidhaa zinazotumiwa kuthibiti maenezi ya janga la korona**.** **H**atuwezi kuwaruhusu matapeli wachache kuendelea kujinufaisha kwa njia zisizofaa**,**" **a**lisema **W**aziri wa **U**salama. **"R**asilmali nyingi za serikali zinatumiwa vibaya na watu wachache."

Tuza kwa kila viakifishi 2-4=alama 1; 5-7=alama 2; 8 -10=alama 3; 11-12= alama 4

b) **Andika umoja**
**Kusoma huku kutachukua muda mrefu kuliko kiasi.** **(alama 1)**
Kusoma huku kutachukua muda mrefu kuliko kiasi.

**c)** **Tunga sentensi kwa kutumia nomino inayotokana na kitenzi '**durusu' **(alama 2)**
Atumie mojawapo ya maneno haya; udurusu,kudurusu,

**d)** **Andika sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi -li- (alama 4)**
i) Liliiva vizuri-li- kiambishi cha ngeli
ii) Alisoma riwaya hiyo.-li- kiambishi cha wakati uliopita
iii) Linalala darasani-li- ya ukubwa

**e)** **Tumia kihusishi katika sentensi hii.** **(alama 1)**
**Wanafunzi wamo darasani**
Wanafunzi wamo ndani ya darasa.
Wanafunzi wamo katika darasa.

**f)** **Andika sentensi mbili kuonyesha maana mbili tofauti za neno,**kina **(alama 2)**
i) Kina Mariamu wametuzwa.
ii) Kitabu hiki kina makosa mengi.
iii) Ziwa Turkana lina kina kirefu.
iv) Bainisha kina cha ukwapi katika shairi hili.

**g)** **Ipambanue sentensi hii kwa njia ya mistari**
**Agnes na Amina ndio waliokuwa wakisaidiana masomoni.** **(alama 4)**

S- KN+KT
KN- N + U + N
N- Agnes
U- na
N- Amina
KT- s+T + E
s-ts+ts
ts- ndio
ts-waliokuwa
T-wakisaidiana
E- masomoni

**h)** **Andika sentensi moja moja ukitumia vitenzi hivi.** **(alama 2)**
la -Twala wali.
fa – Hajafa,nimemwona yu hai.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**q)** **Andika upya ulivyoagizwa kwa maneno yaliyo mabanoni.**
**Mtoto wa miaka kumi na miwili alilazimishwa kuolewa kwa jizee lile.(tendwa)(alam 2)**
Mtoto wa miaka kumi na miwili aliozwa jizee lile.

**r)** **Tumia -ndi- pamoja na viashiria vya ngeli kujaza nafasi zilizoachwa. (alama 1)**
Hapo ndipo liangaziapo mwezi nuru.
Viwavi ndio waharibuo mimea.

**s)** **Onyesha iliko shadda katika maneno yafuatayo. (alama 1)**
'mbu
fadha 'ika

**t)** **Andika sentensi kwa viunganishi hivi vifaavyo. (alama 2)**
**Isije ikawa**
Sentensi ionyeshe kuwa hatarajii/hatazamii/hali ya kuwa na hofu
**Huenda ikawa**
Sentensi ionyeshe hali ya kutokuwa na hakika

**u)** **Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)**
**Jua nisemalo ni muhimu kwetu.**
i) Gimba litoalo nuru angani
ii) Elewa / fahamu kuwa

v) **Tumia kiashiria kisisitizi kuikamilisha sentensi hii. (alama 1)**
**Jana aliivaa nguo __________aliyonayo.**
Jana aliivaa nguo ii hii aliyonayo.

**w)** **Tambua sauti ambazo si vikwamizo /l/,/th/,/j/,/s/,/ny/,/f/,/a/ (alama 1)**
/l/,/j/,/nya/ na /a/

**x)** **Ainisha viambishi katika neno 'kujidhiki' (alama 2)**
Ku- - kiwakilishi ngeli
-Ji- -kirejeshi nafsi
-i- kauli ya kutenda

**r)** **Andika tofauti iliyomo katika sentensi hizi. (alama 1)**
**Ningejua ningetia juhudi masomoni.**
Haiwezekani
**Ningalijua ningalitia juhudi masomoni.**
Yawezekana

**s)** **Kanusha (alama 1)**
**Mumetambua umuhimu wa masomo sasa.**
Hamjatambua umuhimu wa masomo.

**t)** **Andika sentensi yenye visehemu vifuatavyo. (alama 1)**

**Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja**
**Kiambishi cha wakati ujao**
**Kirejeleo**
**Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu wingi (kitendwa)**
**Mzizi wa kitenzi**
**Kauli ya kutenda**

Nitakapowaita
Nitakaowaita

**u)** **Taja na ubainishe viwakilishi katika sentensi hii. (alama 2)**
Huyu anataka kuona chako ulichoandika.
Huyu –kiashiria/kionyeshi
Chako –kimilikishi

**v)** **Andika katika usemi halisi. (alama 2)**
**Mwalimu alipotuuliza ikiwa tulitaka kusoma riwaya wakati wa alfajiri tulimjibu kwamba tungefurahia kufanya Hesabati kwa kuwa hali ya anga ilikuwa bado tulivu.**
"Mwataka kusoma riwaya alfajiri hii ? " Mwalimu aliuliza.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

"Tunafurahia kufanya Hesabati kwa kuwa hali ya anga ni tulivu." Tulimjibu.

w) **Onyesha kishazi huru katika sentensi hii.** **(alama 1)**
**Mwalimu alipoingia darasani akihema hakutusalimu.**
Kishazi huru- Mwalimu hakutusalimu.

4. **ISIMUJAMII (alama 10)**
Wewe ni daktari katika hospitali ya kifahari zaidi katika kaunti ya Kakamega. Umealikwa kuwashauri wanafunzi wa Shule ya Upili ya Tujizatiti kuhusu tahadhari wapaswazo kuzingatia kujilinda dhidi ya maambukizi ya virusi vya COVID- 19.Fafanua sifa kumi za sajili utakayotumia.

Sifa za sajili ya hospitalini zizingatiwe.
1. Lugha rasmi itatumiwa.
2. Maswali ya kudadisi yataulizwa na dakatari kuibua majibu ya mgonjwa.
3. Msamiati maalum wa hospitalini.
4. Lugha ya upole/yenye unyenyekevu itatumiwa
5. Lugha ya mgonjwa hudhihirisha maumivu/unyonge
6. Lugha ya kutumainisha wagonjwa hutumiwa.
7. Kauli fupi fupi zinazoeleweka kwa urahisi hutumiwa.
8. Maagizo hutolewa kuhusu jinsi ya kutumia madawa.
9. Maneno yaliyotoholewa hutumiwa kwa mfano,stethoskop,virusi,baktiria na kadhalika.
10. Huwa ni ya moja kwa moja bila kuwepo kwa mafumbo.
11. Aghalabu humtaja Mungu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KAMATI YA ELIMU YA JIMBO LA KANISA KATOLIKI LA KAKAMEGA MTIHANI WA KUKOMOA MTIHANI WA NOVEMBA/DESEMBA 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA TATU.**

**USHAIRI.**

a) Nafsi nenewa ni pesa/fulusi – waja wanazitumia kusuluhisha matatizo mbalimbali kama vile kununulia vifaa, kulipa madeni. (kutaja – 1, Maelezo 1)

b) Toni ya nafsi neni ni ya kulalamika. Analalamika kuwa pesa zimemkimbia.
Toni ya kusifia – Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima. (al.1)

c) <u>Arudhi</u>.
- Beti nane
- Mishororo minne katika kila ubeti
- Vina vinabadilika katika kila ubeti isipokuwa kibwagizo.
- Mshororo wa mwisho ni kibwagizo- sabuni ya roho ndiwe mvunja mlima.
- vipande viwili katika kila ubeti. (4x1=4)

d) Pesa zimeteka nyara roho za wapendanao na kuwafanya kuuana majumbani mwao. (al.1)

e) Balagha – ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Tashbihi – sinilipue ja bomu.
Jazanda – Jehanamu ni tatizo
Tashhisi- Nguo zao umefua, sura zao umefufua, roho zao umekaba.
-fulusi zinazoombwa kumwondoa mnenaji jehanamu, zina uchoyo.
Takriri- Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.
zozote (3x1=1)

f) Mshairi anamsihi mvunja mlima (pesa) kuwasaidia maskini na mayatima ambao hali zao duni. Awabebe waliokwama na kuwainua walio chini. Ndiye sabuni ya roho na mvunja mlima. (mtimiza yote). (al.4)

g) Idhini
- Inkisari – mfano; 'sinilipue – usinilipue
  'mefuta- umefuta
- Kuboronga sarufi – mfano, wema wako wameonja badala ya wameonja wema wako. (2x1=2)

h) Bahari ya:
Ukaruguni – kila ubeti una vina tofauti na vya ubeti mwingine. (1x1=1)

Maana ya
i) Ni wewe ambaye hufurahisha na kusuluhisha matatizo yote.
ii) tatizo.

**SEHEMEU YA B: TAMTHILIA.**

2. Ni sauti ya mtangazaji/mjumbe katika redio ya rununu ya Sudi. Wanaosikiza redio ni Sudi, Boza na Kombe wakiwa kwenye karakana yao sokoni- chapakazi
Tangazo ni kuhusu sherehe za uhuru ambazo zitachukuwa muda na mwezi mzima. (4x1=4)

b) Jazanda- sumu ya nyoka
Utohozi – kampuni. (kuitaja -1, maelezo -1=2)

c) Vifo mfano ngao junior
- Watu wanageuka vipofu
- Ukengeushi mf. ngurumo
- kuanguka chini ovyo ovyo na kugaragara.
- wanafunzi katika shule ya majoka wamegeuka vichwa maji.
- Hawatambui athari za ulevi
- hawaoni athari ya soko kufungwa.
- Kuvunjika kwa ndoa
- Kupotoka kwa maadili
- Utepetevu (uzembe) wanashinda ulevini
- Kuwaunga mkono viongozi wasiowajibika baada ya kupewa vipeni.
- Kutumia lugha chafu/matusi mfano Ngurumo kumtusi Tanu.
- Kukosa wachumba/ukapera mfano Ngurumo
- Kuvuja pesa
- Waathiriwa wanatumiwa na viongozi kutekeleza maovu mfano Ngurumo.
- Kutofuata maagizo - chopi hakufuata maagizo ya kumuua Tunu.

(za kwanza kumi na nne 14x1=14)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

3. a) Jazanda/Sitiari
Maana: maelezo ya kimafumbo yanayoashiria jambo Fulani au hali Fulani inayofahamika kubeba hali nyingine tofauti.
- Uvundo uliohanikiza katika eneo la soko la chapakazi unashiria uozo wa kijamii kama vile utepetevu wa viongozi.
- Uchongaji wa kinyago kizuri cha mwanamke ambaye ni Tunu akiwa na kinasa sauti ni kuangazia nafsi ya mwanamke katika jamii: ana uwezo wa kuwa kiongozi.
- Uchongaji wa kinyago cha mhenga Fulani wa Boza unaashiria uhafidhina na ubarakala unaoendelezwa katika jamii na baadhi ya watu.
- Kombe anaposema kwamba keki ya uhuru imeliwa kwingine kisha wao waletewa masazo kuonyesha utabaka na ukoloni mamboleo unaoendelezwa na viongozi na vibaraka wao anaojifaidi pekee.
- Majoka anapomwambia Ashua kuwa hangeacha kula mkate kwa kuchelea kiungulia. Hali hii inaashiria uendeshaji wa anasa na uozo wa viongozi wanaotaka kutumia madaraka ya kutimiza ufuska wao hata kwa wake wa watu bila hofu yoyote.
- Kenga anaposema kuwa ukitaka kuwafurusha ndege kata miti kwa maana ya kuangamiza viongozi wa makundi pinzani inadhihirisha maudhui ya ukatili na siasa za mauaji.
- Sudi anapomwambia Ashua kuwa siasa yao imesukumiza kwenye chombo wasichotaka kuabiri anamaanisha imebidi washiriki katika harakati za ukombozi. Aidha, maudhui ya asasi ya ndoa yanaangaziwa kupitia mzozo wao. (Sudi na Ashua)

- Chopi anawaambia Sudi kuwa shamba likimshinda kulima aseme anamaanisha pengine Sudi ameshindwa kumkidhia Ashua mahitaji yake kama mke hivyo kuendeleza maudhui ya ndoa na mapenzi.
- Babu nasema kuwa chombo chenye rubani imara huhimili vishindo na hasira ya mawimbi kumaanisha uongozi mzuri hutegemea kiongozi aliyeimara na mwajibikaji.
- Babu naporejelea mshumaa kuwaka na kuasha mishumaa mingine anamaanisha kiongozi anastahili kuwafaa raia. Aidha, anadokezea umuhimu wa umoja na ushirikano katika jamii.
- Ashua anamwambia Majoka kuwa ushahidi hauwezi kupatikana ikiwa kipanga ndiye hakimu katika kesi ya kuku kumaanisha ukiukaji wa haki katika jamii.
- Babu anamwambia Majoka kuwa labda chombo chake kinakwenda kinyumenyume badala ya kwenda mbele kumaanisha utawala wa Majoka haujaonyesha mabadiliko yoyote yaliyoleta manufaa bali umeendelza ukoloni mambo leo. (za kwanza 10) 10x 1=10)

**MAJAZI.**

b)

- Majoka- Nyoka kubwa kupita kiasi. Ana tabia ya nyoka kubeba fimbo ya nyoka na maumbo ya nyoka. Kutengeneza sumu ya nyoka. Kufuga nyoka. (swila)
- Tunu – kitu cha dhamana (zawadi) ni mwanamke wa kipekee anayekabiliana na viongozi dahlimu.
- Sudi-bahati njema. Ni bahati njema kwa Sagamoyo. Anajitolea kupigana na uongozi mbaya.
- Kenga – kumfanya mtu aamini jambo lisilo la kweli (uongo)
- Husda- kuonea mtu gere/kijicho/wivu. anamwonea Ashua wivu kwa sababu amesoma, mrembo na apendwa na Majoka.
- Kombe –mmea unaotambaa ambao utomvu wake ni sumu inayopakwa katika kigumba cha mshale. ana tabia ya kutoonyehsa msimamo dhabiti.
- Ngurumo- sauti ya mvumo inayosikika angani wakati wa mvua. Anahusika kuwaua na kuwapiga wapinzani wa Majoka.
- Chopi-kulewa chopi/chakari. Hakufuata maagizo anayopewa na Majoka kwa sababu ya kulewa.
- Mama pima- kazi yake ni kupima na kuuza pombe.
- Asiya-sehemu ya kitu au mbaki. Mfano Majoka anamuona kama mbaki linalostahili kuondolewa baada ya kifo cha Ngurumo.
- Boza-mjinga/mpumbavu. Mfano anaunga mkono serikali kijinga, mkewe azini na Ngurumo.
- Hashima- mwenye heshima, anawafundisha wengine kuwa na heshima.
- Saga moyo- kufanya kitu kiwe unga unga (saga). Watu wanaosihi katika jimbo hili wanapitia maumivu makali ya moyo.
- Chapakazi-mahali pa kufanyia kazi kwa bidii.

(za kwanza kumi 10x1=10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA C RIWAYA.**

4.a) Ni maneno ya **Ridhaa** kupitia mawazoni mwake akimweleza binti yake **Tila**. Alikuwa kando ya gofu la jumba lake lililokuwa linavuka moshi. Ni baada ya mjadala kuhusu mafanikio ya baada ya uhuru. (4x1=4)

b)i) Nahau/msemo – gonga mwamba. (kutaja -1, maelezo -1)

c) Ukoloni/dhuluma- mashamba ya wenyeji yanamilikiwa na walowezi. (kutaja-2, Maelezo-2=4)

d) Waafrika walilalzimika kupoteza mashamba yao katika sehemu fulani. mfano mzee Msubili.

- Waafrika walilazimika kuwa, ama vibarua katika mashamba yao.
- wengi walilazimika kuwa maskwata.
- wale waliobahatika kuwa na makao yao walipata sehemu ambazo hazingeweza kutoa mazao.
- watoto wadogo walilazimishwa kutoka kwenye susu zao, hata vifua havijapanuka.
- waliokosa pesa za kununua mashamba walikosa mahali pa kuishi.
- Kupuuzwa kwa sera za mwafrika za umiliki wa ardhi, ulivuruga mshikamano wa kijamii.
- Maisha ya waafrika wengi ilibaki kuwa ya kutegemea wazungu.
- wale waliokuwa na pesa za kununua mashamba walionwa kama wageni wasiopasa kuaminiwa.

5b) (Maelezo “mtoto wa miaka hamsini.” Ni nchi za bara la Afrika ambazo baada ya kupata uhuru bado hazijapiga hatua katika kuboresha uchumi na mambo mengi ya kimsingi katika nchi zao, zimebaki nyuma kimaendeleo kwa kunyanyaswa , kuelekezwa, kuamuliwa na kutegemea mataifa yaliondelea kama watoto.)

**Hoja.**

- Mashamba ya waafrika ya Theluji nyeusi yalinyakuliwa na kumilikiwa na wakoloni kabla ya uhuru.
- Baada ya uhuru mashamba ya waafrika yalimilikiwa na watoto wa walowezi. Mfano katika maeneo ya 'Kisiwa Bora"
- Waafrika/wenyeji wa mashamba waligeuzwa kuwa maskwata katika vitovu vya usuli wao.
- Baada ya uhuru waafrika wamebaki kuwa wategemezi wa wakoloni kwa chakula.
- Waafrika vile vile wamebaki kuwategemea wakoloni kwa ujira.
- Waafrika hawana uwezo kuamua wanachotaka kukuza katika ardhi yao.
- Nchi za kiafrika zimebaki nyuma kimaendeleo haswa katika uchumi. hazina viwanda vya kusagia kahawa au chai.
- wakoloni ndio wenye uwezo wa kuamua cha kukuza katika mashamba ya waafrika. mfano chai na kahawa.
- Mimea inayokuzwa barani Afrika husafirishwa ng'ambo kumfaidi mkoloni.
- Waafrika hawana uwezo wa kujisagia kahawa na chai.
- Baada ya mazao- kahawa na chai kwenye viwanda vya ng'ambo na kusagwa chai hiyo inarejeshwa na kuuzwa kwa bei ghali.
- Waafrika waligeuzwa na kuwa hazina ya wafanyikazi wa wazungu na kupalilia mazao yao.

(10 x1 = 10)

5.a) Mrejelewa ni Ridahaa.

- Kielelezo cha viongozi waliowajibika. Anakwenda hospitalini kumhudumia mgonjwa aliyeumia.
- Anachangia kuendeleza tabia za wahusika. Tunao na ucheshi wa Terry na ukakamavu wa Tila.
- Kupitia kwake mwandishi amekuza maudhui mbalimbali kama vile uwajibikaji, utu, uongozi, ndoa n.k.
- Kupitia kwake maisha ya maskini na matajiri yanalinganishwa. Mtaa wa Afueni kuna majumba ya kifahari. Mtaa wa kazikeni una mabanda mengi.
- Ametumiwa kuangazia juhudi za viongozi katika kuendeleza jamii, kukabiliana na magonjwa, ufadhili wa elimu n.k.
- Anachangia katika kujenga ploti. Kuanzia kituo cha afya cha mwanzo mpya na kubadilisha mkondo wa maisha ya Selume.
- Anaonyesha athari za kutokuwa na uthabiti wa kisiasa.
- Kupitia kwake tunaona migogoro inayosababishwa na tofauti za kiusuli. Wanafunzi wenzake shuleni wanamtenga kwa sababu yeye ni mgeni.
- Ni kielelezo cha watu wanaopenda mshikamano wa watu katika jamii. Anawasaidia wapwa wa mzee Kedi, Mwangeka anawasaidia Umulkeri na Dick licha ya kutokuwa na uhusiano wowote.
- Ni mmoja wapo wa wasimulizi wa matukio ya hadithini. Anasimulia kisa cha kupoteza majumba yake mawili. (zozote kumi (10x1=10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: HADITHI FUPI.**

6 a)

- Msemaji ni Daktari Mabonga
- Msemewa ni wanafunzi wa somo la fasihi.
- Mahali ni ukumbi wa mhadhara
- sababu – Dkt Mabonga anasuta wanafunzi kwa kuwa vitegemezi baada ya mwanafunzi kutaka kueleza namna fasihi inavyoelekeza. (4x1=4)

b) Tashbihi – si kama watoto wakembe. (kutaja-1, maelezo -1=2)

c) i) Msomi- Ni mhadhiri wa fasihi katika chuo kikuu cha kuvukoni.

ii) Mkweli – Hasiti kusema yale yaliyomo moyoni hata kama yataleta maudhi. Anawakashifu wanafunzi kwa kutaka kufanyiwa kila kitu. (2x2=4)

d)

- Dennis Machora na Penina wanaishi katika mtaa wa Newzealand na kodi ilikuwa inalipwa na wazazi wake penina.
- Penina alisema kuwa hangeweza kuolewa na mwanamume asiye na kazi yenye mshahara duni.
- Dennis Machora aliona kuwa Penina angekuja kulalamika kuwa Dennis machora amekuwa kupe. Penina alikuwa anatumiwa kshs.5000/= kila wiki na wazazi wake kwa matumizi.
- Msichana mmoja alisema kwamba mchumba wake ni katibu katika wizara ya habari, mawsiliano na teknolojia, kwa hivyo karibuni watafunga ndoa aondokewe na adha ya masomo.

- Aidha Dennis Machora alikuwa anategemea mkopo wa shule kujikimu. Pesa hizo zinapoisha anahangaika.
- Dkt. Mabonga alisema kuwa binadamu hatafuti chakula
- Dkt. Mabonga alisema kuwa binadamu wanapiga ubwete na kugeuka kupe.
- Wanafunzi wengine wanaonelea waache masomo waende kusimamia biashara za wazazi wao.

(zozote kumi na mbili 10x1=10)

7.a)

i) Ni maneno ya Mkumbukwa
ii) Anamwabia Mkubwa
iii) Wamo nyumbani mwa Mkumbukwa
iv) Ni baada ya kubadili nia na kutotaka kutumiwa na Mkubwa kusambaza unga/dawa za kulevya kwa wateja. (4x1=4)

b)

- Kufungwa – Mkumbukwa anatiwa mbaroni na kufungwa kwa siku tatu baada ya kupatikana na begi la unga.
- Kusinzia- Mkumbukwa anadai kwamba vijana wanatumia unga wanasinzia saa zote, hivyo kuishia kutofanya kazi.
- Vifo- Mkumbukwa anadai kwamba vijana wengi wamekufa kutokana na matumizi ya unga.
- Ufisadi- biashara ya unga inaendeleza ufisadi katika jamii, Mkubwa anamhonga mkuu wa polisi Ng'weng;we wa Ngagu ili amfungulie Mkumbukwa.
- Wizi- vijana mateja wanaibia watu mitaani.
- Fujo-vijana mateja wanazua fujo wakitumia visu na bisibisi.
- Kudhoofika kwa afya- Afya ya vijana mateja imedhoofika kutokana na matumizi ya unga.
- Tunaambiwa kwamba hawana nguvu. Wengine wanadondokwa na udenda.
- Kujitoga mwili – vijana mateja wanajitoga mwili ambao umejaa matundu kama jahazi la mtefu.
- Kupujuka kwa maadili-vijana mateja wanawatusi wengine. Wanamwita Mkubwa Makande/mavi ya bata.
- Uzembe-vijana mateja wamekuwa wazembe hawafanyi kazi wanalaliana vichochoroni baada ya kutumia unga.
- Vitisho –unga umewasababisha vijana mateja kuwa wenye vitisho. wanamtishia Mkubwa kwamba wangemtoa chango.
- Magonjwa- dawa za kulevya zinawasababishia vijana mateja magonjwa kama vile kifua kikuu na kutokana na kujitoga mwilini. (zozote nane 8x2=16).

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**.

a) Bembezi/Bembea/Bembeleza. Msimulizi anambembeleza mtoto alale sababu mamake ameenda sokoni. (kutaja-1, maelezo-1=2)

b)

- Hodiya- za watu wanapofanya kazi.
- sifo – za kutoa sifa kwa wahusika Fulani katika jamii.
- wawe- za wakulima wakiwa shambani
- mbolezi- za kuomboleza.
- Nyiso-huimbwa katika sherehe za tohara.
- Kimai-huimbwa na wavuvi wakiwa baharini. (kutaja-1, maelezo-1=2)

c) i) Malezi – analea mtoto.
ii) Mapenzi- Hataki mtoto alie. (2x1=2)

d) i) Biashara – kuna soko
ii) Ukulima/kilimo- wanalima ndizi (kutaja-1, Maelezo -1 (2x2=4()

e) i) Takriri – lala lala
ii) Mdokezo - lala…… (2x1=2)

f)

- Kumburudisha
- Kuliwaza
- Kuelemisha
- Kuhifadhi utamaduni
- Kufikirisha

- Kuweka kumbukumbu ya histroia. (4x1=4()

g)

- Utazamaji/kuchuuza – kutazama kwa makini yanayotokea na kuandika.
- Kusikilia wasanii wakiwakilisha tungo zao- ili kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
- Kuhoji wanaofahamu mengi kuhusu fasihi simulizi
- kurekodi katika kanda za sauti – kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
- Kurekodi kwa filamu na video –kuonyesha uhalisi wa mandhari. (4x1=4)

`

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA – 2020**
**Machi/Aprili 2020**
**102/1**
**KISWAHILI – INSHA- Karatasi ya 1**

1. Wewe ni mwandishi wa habari katika gazeti la Mzalendo. Umetembelewa na profesa wa masuala ya Historia na Serikali kwa minajili ya kumhoji kuhusu namna ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa katika taifa lenu la Utengano. Andika mahojiano yenu.
2. Kufaulu kwa Mfumo Mpya wa Elimu ya Umilisi hakutegemei juhudi za serikali tu, bali pia jamii kwa ujumla. Jadili
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Atafutaye hachoki na akichoka keshapata.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno haya: Ingawa sikuwa ninamwamini, sikutarajia angetenda kitendo cha kiuhayawani kama hicho.

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2020**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**UFAHAMU (Alama15)**
**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Uchumi ni mfumo wa mapato, na matumizi ya watu katika nchi fulani. Uchumi huu huhusisha sekta mbalimbali kama vile utalii, kilimo, sanaa miongoni mwa sekta nyingme muhimu. Ukuaji wa kiuchumi hutegemea mambo kadhaa ili kuzaa matunda. Katika nchi zote ulimwenguni, sera za kisiasa huamua jinsi uchumi utakavyokua na kunawiri. Kama siasa hazitilii maanani sera za ukuaji wa kiuchuini, basi mapato ya nchi hiyo hugubikwa katika wingu kubwa la uchochole.

Nchini Kenya, kwa mfano, kuna ulinganifu mkubwa kati ya siasa na ukuaji wa kuichumi. Ukuaji wa kiuchumi hutegemea uteuzi wa maafisa wanaosimamia asasi muhimu sana katika usimamizi wa uchumi. Asasi hizi ni kama vile wizara ya fedha, Wizara ya Mipango ya kitaifa na Ruwaza ya 2030, Mamlaka ya Ukusanyaji wa ushuru ( KRA), Benki kuu ya Kenya (CBK). na tume ya kupambana na ufisadi (KACC). Usimamizi wa asasi hizi huwa muhimu sana katika kuamua hatima ya uchumi wa nchi hii.

Katika mwezi wa Juni kila mwaka, Waziri wa fedha husoma bajeti kwa' Wabunge. Katika maelezo yake yaitwayo nakisi ya bajeti hujitokeza. Kabla ya bajeti kuandaliwa Wizara ya Mipango huandaa hati iitwayo Usoroveya wa kiuchumi. Baada ya kusomwa kwa bajeti ni jukumu la Wabunge kupitisha mswada wa kifedha unaohusisha wizara zote au kuutupilla mbali. Jukumu hili linafaa kutekelezwa kufikia tarehe 31 Oktoba ya kila mwaka kulingana na sheria.

Wakati huo huo, afisa anayejulikana kama Mhasibu Mkuu wa serikali huwa na jukumu la kuchunguza na kutathmini matumizi ya fedha ya Wizara mbalimbali na kutoa ripoti yake kwa kamati ya Uhasibu wa Umma bungeni (PAC). Kamati hii hutoa mapendekezo yake kwa mkuu wa sheria na pia kwa Tume ya kupambana na ufisadi ili haki iweze kutekelezwa mahakamani iwapo dosari za kifedha zimefanyika.

Benki kuu ya Kenya kupitia kwa Gavana wake huwa na jukumu la kutoa ushauri kwa serikali kuhusu usimamizi wa kifedha, kuchunguza nguvu za shillingi ya Kenya dhidi ya sarafu za kigeni, kutoa sarafu za Kenya kwa umma. na usimamizi wa benki zote nchini miongoni mwa majukumu mengine.

Kwa upande mwingine, mamlaka ya Ukusanyaji ushuru nchini huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa malengo ya ushuru yamefikiwa na pia kuhakikisha kuwa hakuna mtu binafsi au kampuni yoyote inayokwepa kulipa ushuru.

Iwapo kuna udanganyifu wowote, basi swala hili linafaa kuangaliwa na mahakama zetu na haki kutekelezwa.

Kwa ujumla, sisi kama wananchi tunafaa kusaidia asasi hizi zote kufikia malengo yake ili tupate ukuaji wa kiuchumi utakaofaidi watu wote. Jambo hili litahakikisha kuwa pengo lililo kati ya walalahai na walalahoi limezibwa. Sisi kama wananchi, tunafaa kuonyesha uzalendo wetu kwa nchi yetu kwa kulipa ushuru inavyotakikana , tukifuata mwito kuwa KULIPA USHURU NI KUJITEGEMEA. Mwisho, tusaidie viongonzi wetu katika kuendeleza sera mwafaka za kiuchumi ili nchi yetu ipige hatua kubwa katika ukuaji wa kiuchumi. Iwapo afisa yeyote atatuhumiwa kushiriki katika kashfa yoyote ya kuhujumu nidhamu ya kifedha basi anafaa kukabiliwa vilivyo kisheria bila kujali hadhi yake ya kijamii au kisiasa.

**Maswali**

a. Ipe habari hii kichwa mwafaka. (alama 1)
b. Ukuaji wa kiuchumi nchini Kenya hutegemea nini? (alama 2)
c. Benki kuu ya Kenya ina majukumu yepi? (alama 4)
d. Mhasibu mkuu ana dhima ipi serikalini? (alama 2)
e. Pendekeza hatua tatu za kufufua uchumi kulingana na taarifa (alama 3)
f. Ni vipi Wakenya wanaweza kuonyesha uzalendo? (alama 1)
g. Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ufahamu. (alama 2)
   (i) hatima …………………………………………………………………………………
   (ii) wahalahai

**2. UFUPISHO (alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Inaaminika kuwa majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au kuathirika vibaya zaidi kutokana na hali mbaya ya uokoaji. Watu wengi ambao hujitolea kutoa majeruhi baada ya ajali kama za barabarani, maporomoko ya ardhi au nyumba huwa hawang'amui hata chembe jinsi ya kukabiliana na uokoaji. Hatima ya juhudi zao ambazo hulenga kutenda mema ni kuathirika zaidi kwa majeruhi.

Hali ya uokoaji inaweza kurekebishwa kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma. Elimu hii yahitajika na kila Mkenya kwani mikasa ya ajali za barabarani na nyinginezo inaendelea kutokea kila siku.

Ajali zinapotokea si ajabu kuona makundi ya waokoaji wakibeba majeruhi hobelahobela bila kuzingatia madhara wanayoweza kuwaongezea kutokana na ubebaji wao. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumbabatisha na hata kusababisha kifo.

Kuna mambo mbalimbali ambayo makundi ya waokoaji yanatakiwa kuzingatia wakati yanatoa huduma ya kuokoa. Kwanza ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza ikatokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini zaidi. Makundi ya waokoaji yameweza kwa kuliingilia eneo la ajali mbumbumbu kama mzungu wa reli.

Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi. Pana uwezekano wa majeruhi kutupwa mbali na eneo la ajali.Vivyo hivyo, kuna majeruhi ambao huweweseka baada ya ajali na kuanza kutembea wasijue wanakoelea. Wengi wao huanguka karibu na eneo la ajali au wakaenda mbali.

Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua. Ili kuhakikisha kuwa majeruhi anapumua, mwokoaji atazame kama kifua kinapanda na kushuka. Hali kadhalika, mwokoaji anaweza kusikiliza au kuguza kifua na kuona kama kuna ishara za kupumua. Iwapo majeruhi anapumua, muokoaji amweke katika hali ambayo itaimarisha kupumua kwake. Anaweza akamlaza chali au kumgeuza kwa pamoja na kichwa chake ili kufungua mkondo wa hewa. Pia mwokoaji ahakikishe hamna chochote kinywani kinachoweza kumsakama. Ikiwa hapumui, mwokoaji anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake.

Fauka ya hayo, upulizaji wa hewa utahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.

Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejeruhiwa. Chunguza kama majeraha ni vidonda tu au kuna kuvunjika kwa mfupa na kubainisha ni mfupa upi. Haya yatamwezesha mwokoaji kujua jinsi ya kumbeba majeruhi. Pakiwa na kuvunjika kwa mfupa, ni muhimu kutotumia kiungo kilichovunjika anapobebwa.

Pia kuchunguza vile majeruhi amejeruhiwa, humwezesha mwokoaji kujua huduma ya dharura atakayoitumia. Majeruhi akiwa anavuja damu sana, ni muhimu kuzuia uvujaji huu. Iwapo ni kidonda kidogo, kinahitaji kufungwa ili kuzuia uambukizaji. Mwokoaji anaweza kutumia kifaa chochote kilicho karibu kutolea huduma hizi. Kwa mfano, anaweza kupasua nguo ya majeruhi ili apate kitambaa cha kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu au kumfunga kidonda.

Hatua inayofuata ni kumhamisha majeruhi toka eneo la ajali hadi hospitalini. Mwokoaji anaweza kuwatumia watu wengine kutafuta msaada. Wanaweza kupiga simu wakitumia nambari za simu za dharura kama zile za polisi, wazimamoto au makundi ya wataalamu wa shughuli za uokoaji. Nambari hii ya simu huwa 999 popote na huwa haina malipo. Wanaopiga simu ni vyema kutoa maelezo ya mahali ambapo ajali imetokea, ama ya ajali na huduma za dharura zinazohitajika.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Ikiwa makundi ya wataalamu wa uokoaji hayakupatikana, ni jukumu la mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini. Majeruhi wakiwa wengi ni bora kuanza na wale waliozimia au wenye matatizo ya kupumua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana. Baadaye mwokoaji awasaidie waliovunjika mifupa huku akimalizia na wenye majeraha yasiyohatarisha maisha. Ni muhimu kuwabeba majeruhi kwa kutumia machela. Hii hupunguza kuathirika zaidi kwa majeruhi. Iwapo hamna machela karibu, mwokoaji anaweza kuunda moja kwa kutumia vipande viwili vya mbao, blanketi shuka au makoti.

Ujuzi wa huduma ya kwanza ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo kila mtu anapaswa kuwa nayo.

**<u>MASWALI</u>**

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 50 tu. (Alama 5, utiririko 1)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza kwa kutumia maneno 90-100, hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji.(Alama 10, utiririko 1)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) Huku ukizingatia jinsi hewa inavyozuiliwa, ainisha sauti zifuatazo: (alama 2)
   i) /y/ ..........................................................................................
   ii) /sh/.........................................................................................
   iii) /h/.........................................................................................
   iv) /ny/.......................................................................................

b) Andika neno lenye muundo ufuatao. (alama 2)
   i) irabu, irabu, irabu ..........................................................................................................
   ii) irabu, konsonanti, konsonanti, konsonanti, irabu

c) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo: (alama 2)
   i) mwanao
   ii) azingatiaye

d) Onyesha aina za vielezi katika sentensi zifuatazo: (alama 2)
   i) Barabara ndefu zaidi ilisakafiwa barabara.
   ii) Kiplagat alianza kula alipoambiwa asishike chakula hivi hivi.

e) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa. (alama 2)
   Mwanamke huyu alibeba ndoo hizi hadi sokoni.

f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
   KN(RH + RH) + KT(t + V)

g) Tunga sentensi ukitumia neno **alikuwa** kama:
   i) kitenzi kishirikishi kikamilifu (alama 1)
   ii) kitenzi kisaidizi (alama 1).

h) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa: (alama 3)
   Mwanasiasa alisema, " Mkinipigia kura nitawajengea zahanati kabla mwisho wa mwaka huu."

i) Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani? (alama 1)
   i) ufizi ..........................................................................................................
   ii) firigisi ......................................................................................................

j) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama 1)
   Waziri anasoma hotuba yake.

k) Andika sentensi ifuatayo katika hali kanushi: (alama 1)
   Nzige wengi walikuwa wanavamia maeneo hayo kabla ya serikali kuchukua hatua.

l) Bainisha kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
   Mama alimpikia mgeni wetu nyama ya kuku.

m) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
   Mwalimu aliyetuzwa jana alifundisha shairi lililotungwa na Kezilahabi.

n) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **daka** na **taka**. (alama 2)

o) Tunga sentensi **mbil**i kuonyesha matumizi **mawili** ya kiambishi **ka**. (alama 2)

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari. (alama 4)
   Genge la wezi lilituvamia.

q) Bainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
   Pikipiki iliyonunuliwa jana iliharibika karibu na mto.

r) Eleza majukumu ya sentensi ifuatayo: (alama 1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Nipe kalamu yangu mara moja!

s) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)

Kazi hii imekuwa (tendea) ngumu sana lakini siwezi kufa (tendeshwa) moyo.

t) Taja methali inayoafiki maelezo yafuatayo: (alama 1)

Mtu anayetegemewa katika jamii akiondoka wanaomtegemea huwa mashakani.

**ISIMUJAMII (alama 10)**

‘’Mwenye sikio amesikia. Usiwe kama mimi. Wapurukushe wote wakupotoshao. Fuata ruwaza ya wanaokujali. Kwangu nimejishika sikio baada ya laiti nyingi. Macho yamefumbuka. Usiseme nitazeekea huku. Lengo langu ni kuwahi uzamili na hata uzamifu. Kwani kuitwa profesa ni kosa? Niwafae wengine kimasomaso na kihali’’

a) Taja na kuthibitisha sajili ya mazungumzo haya. (alama 2)

b) Tambua mazingira ambamo mazungumzo haya yanatokea. (alama 1)

c) Eleza sifa zozote **saba** za lugha zilizotumika kwenye mazungumzo haya. (alama 7)

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA**
**NOVEMBA - 2020**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA A - FASIHI SIMULIZI**

**1.** Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kwenye friji lakini haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia *“My friend kunywa soda”.*

(a) Taja na ueleze maana ya kipera hiki **(alama 2)**

(b) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita. **(alama 6)**

(c) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Tetea kauli hii. **(alama 4)**

(d) Ni changamoto gani zinaweza kumkabili mwanafasihi nyanjani? **(alama 4)**

(e) Dokeza umuhimu wa kukusanya data nyanjani. **(alama 4)**

**SEHEMU YA B - TAMTHILIA: KIGOGO** na *Pauline Kea*

**2.** “Udongo tungeliuwahi uli mbichi. Limekuwa donda ndugu sasa. Waliota ikakita na wakamea hata pembe.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Taja na kueleza tamathali moja ya usemi inayojitokeza kwenye dondoo hili. **(alama 2)**

(c) Eleza sifa zozote nne za msemaji wa kauli hii. **(alama 4)**

(d) Dondoo hili linadhihirisha jinsi baadhi ya Wanasagamoyo walivyoshiriki kuivunja jumuiya yao. Fafanua. **(alama 10)**

**3.** “Wananchi katika mataifa ya Afrika wanakumbwa na tatizo la uongozi mbaya.” Thibitisha ukweli wa kaui hii kwa mujibu wa Tamthilia . **(alama 20)**

**USHAIRI**

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

1. Sikilizeni wimbo huu:
Niliokuwa mtoto nilitwa chacha
Kwa matamshi yangu ya sasa
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure.

2. Huu utakuwa wimbo wako
Utakapostaafu urudipo nyumbani
Umelewa kangara na nyayo zako

Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini.
Utakuwa kichekesho cha watoto
Watakaoukuita, Ticha! Popote upitapo.

3. Kumbuka mwalimu utakapostaafu,
Mijusi watataga mayai ndani ya viatu
Vyako vilivyokwisha visiginino.
Na ndani ya sidiria chakavu
Zilizoshikizwa Kamba kwa pini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu
Za marashi na za bia.

4. Na manyigu yatajenga ndani ya kofia
Zilizosahaulika kutani
Utakapokufa nge watazaliana
Chini ya jiwe juu ya kaburi lako,
Na mlevi fulani akipita atapenga
Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke
Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

5, Lakini wakati ungali hai
Unaweza kubadilisha mkondo wa maji
Lakini kwanza mzungumze. Wewe na mimi.
Acha mioyo yote izungumzwe
Baada ya kunyanyaswa
Na kisha nusu mshahara.

6. Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi?
Utafundisha tena ngonjera?
Utapeleka tena wanafunzi asubuhi
Wakajipange barabarani kusubiri
Mgeni afikaye saa kumi na apitapo
Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe
Na huku nyuma mwasambaa na njaa?

7. Tazama hilo runda madaftari mezani
Utalimaliza kwa mshahara mkia wa mbuzi?
Tuzungumze. Ninyi na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze
Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo
Mtawekwa kwenye vijiti na kutupwa
Nje ya ua, ndani mtawaacha
Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya

8. Sikilizeni walimu,
Anzeni kufundisha hesabu mpya
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini
Ni sawa na sifuri. Hapana utawala
Fundisheni historia historia mpya
Hapo zamani za sasa
Hapakuwa na serikali.

9. Sikilizeni kwa makini
Umoja hatuna
Twasambaratika kama nyumba
Tulicho nacho ni woga,
Na kinachotuangusha ni unafiki.
Lakini tusikate tamaa kama mbuni.
Tukiupata umoja bado tunayo silaha.
Kura.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Thibitisha kwamba hili ni shairi huru. **(alama 5)**
(b) Eleza jinsi maudhui ya utamaushi yanavyojitokeza ukimrejelea nafsi-nenwa. **(alama 4)**
(c) Nafsi-nenwa anapaswa kujilaumu kwa masaibu yake. Thibitisha. **(alama 2)**
(d) (i) Bainisha nafsi-neni katika shairi hili. **(alama 1)**
(ii) Jadili toni ya shairi hili. **(alama 2)**
(e) Eleza matumizi mawili mawili ya usambamb na jazanda katika shiri hili. **(alama 4)**
(f) Eleza maana ya kufungu kifuatacho:
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri. **(alama 2)**

**5. USHAIRI**

Leo ‘mekuita,
Kwa upole nitanena,
Tabiya hii yako mwana

Uli wa kulaza damu,
Pahala nawe hudumu,
Hutufai nawe humu,

Wapendani naumi,
Hulimi na walimi
Haya sijaona mimi,

Mwiza kazi yu wa chira
Asiyeta ajira
Ndiye muja wa hasara,

Unavitaka vya bure
Lako ndizo hamurere
Uchao ‘wa ‘tuza bure.

La mno lako ni ung’are
Uturi ujirashire
Hukosi kuzua ghere

Unazani utaoa?
Jasho nalo hujatoa,
Utaithibiti ndoa?

Unafaa kujitoa,
Na mali ukayazoa,
Ndipo utapopoa

Si mambo ya kutanga,
Chunga utajikaanga
Mchumba chumbiya mwenga

Utafanyani kiwatunga
Na hilo likawe janga,
Mwanangu hutochenga

Kisomo ndiyo unayo,

Nikupe ya moyo
“Kayatiye masikiyo
Si yetu tujuwapo

Na uzembe uzidiyo
Uchaoni mbiyombiyo
Na hiyo shambiroyo

Uniizia gange
wataka ukajitenge
Nakuasa ujichunge

Ni andewaye tenge
Wala hashiki shilange
Hubomoa asijenge

Huitoa jasho lako
Umebaki mitiko
Sizo zetu nyendo zako

Uzirembe nyele zako
Ukatembee kwa deko
Na marashi ya mnuko

Utamwoa wa nani?
Utachokishika nini?
Wa kukubali nani?

Fanye kazi kwa manani
Hamadi i kibindoni
Ukamtafute mwendani

Fi na huhu fi na yule
Umetujile uwele
Na yule ukamuole

Himila wakahimile
Na lije likulemele
Na wote wakikujile

Shahada umejitwaliya

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Ujuzi unao kocho, hutaki kuutumiya
Upate ukitakacho Kile cha kukufaiya

Mwana wa 'ntiya kichocho Kwona umejiachiya
Umekuwa kitumiwacho Kidhani wawatumiya
Unawapa wapendacho Na wanachokutakiya

Komu mwanangu ukome Usinifishe mveyeleo
Usombombi uukome, Ukome kwanzia leo
Sitakwita te'niseme Ishapita hii leo

Ukware si kuwa dume Dume ni ajira
Wa itaha ndiye dume Anakheshimu nafseo
Muungwana ja kimeme Fikira nokwelezeo

Mradi unayo masikizi Haya umenisikiya
Kazituwe nyendo hizi, Ukawe wa kutuliya
Ukasuhubiye kazi, Halafu itakufaiya

Nakoma zaidi s'ezi Yametosha mekwambiya
Nimekuweko na juzi, Miyaka menipitiya
Nimejizolea ujuzi, Na ndiyo ha 'nakupa haya

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

1. Fafanua sifa za shairi hili. **(alama 3)**
2. Kando na kigezo cha idadi ya mishororo, chambua bahari nyingine tatu za shairi hili. **(alama 3)**
3. Huku ukitolea mifano mwafaka, fafanua mambo mawili aliyofanya mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama 2)**
4. Andika ubeti wa nane kwa mtindo tutumbi. **(alama 3)**
5. Tambua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa na mshairi. **(alama 2)**
6. Eleza dhamira ya shairi hili. **(alama 1)**
7. Tambua nafsi-nenewa katika shairi hili. **(alama 1)**
8. Ni nini toni ya shairi hili? Eleza. **(alama 2)**
9. Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama iliyotumika katika shairi hili. **(alama 2)**
   (i) ghere
   (ii) sitaha

**<u>SEHEMU YA D</u> - RIWAYA YA CHOZI LA HERI**

**6.** "Msamehe ….., hakuna mja aliyekamilika."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
   (b) Eleza umuhimu mnenewa katika dondoo hili. **(alama 4)**
   (c) Kwa kurejelea wahusika mbalimbali riwayani, thibitisha kuwa hakuna mja aliyekamilika. **(alama 12)**

**7.** Jadili jinsi mwandishi wa riwaya hii alivyofaulu kutumia mbinu ya kinaya na sadfa. **(alama 20)**

**<u>SEHEMU YA E</u> - TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

**8.** Safari ya elimu ni kama ua la waridi ambalo licha ya upendezaji wake, huzingirwa na miiba. Jadili adha za safari hii kwa hoja tano tano kutoka kwa kila mojawapo wa hadithi fupi zifuatazo: Mapenzi ya Kifaurongo, Mame Bakari, Mwalimu Mstaafu na Mtihani wa Maisha.

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA – 2020**
**Machi/Aprili 2020**
**Mwongozo wa usahihishaji**
**102/1**
**Swali la kwanza**

1. Hili ni swali la mahojiano. Mtahiniwa atimize vigezo vifuatavyo vya sura.
2. Kichwa – kionyeshe ni mahojiano baina ya fulani na fulani (vyeo) na au mahojiano kuhusu mshikamano wa kitaifa.
3. Wahusika waweze kutambuliwa na kushiriki katika mazungumzo ya kimapokezano. Usemi halisi utumiwe.
4. Mwandishi wa habari ndiye mhoji ; aulize maswali, profesa wa Historia ndiye mhojiwa; ajibu maswali.

Baadhi ya hoja:

1. Matumizi ya lugha ya taifa kuimarishwa/ kusisitizwa.
2. Kupiga vita ukabila na unasaba.
3. Kuhusisha tamasha za kitaifa katika uimbaji na uigizaji.
4. Kuwashirikisha Wanautengano katika mashindano nas michezo ya aina mbalimbali.
5. Kuwahusisha wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya Utengano katika mfumo wa aina moja ya elimu.
6. Kuimarisha uzalendo wa Wanautengano kupitia uimbaji na wimbo wa taifa na nyimbo nyingine za kizalendo.
7. Kuhimiza ndoa za mseto zinazohusisha Wanautengano kutoka maeneo mbalimbali na makabila mbalimbali.
8. Kuhimiza usawa katika ugavi wa rasilimali za nchi pasi na kuzingatia umenke, tofauti za kitabaka, rangi au kabila la mhusika.
9. Wanautengano kuhimizwa kuwekeza, kuishi na kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya Utengano mbali na kule iliko asilia yao/kitovu chao.
10. Kuwepo na siku maalum ambapo Wanautengano wanaonyesha tamaduni zao kwa wengine ili kuwafanya kuthamini tofauti hizo na kujiepusha kuzidunisha.
11. Kuwashirikisha Wanautengano wote katika uongozi wa nchi kama vile katika uchaguzi wa kiongozi wa nchi na waandamizi wake.

**Tanbihi:**

1. Hoja zozote tano zilizoelezwa kikamilifu zinaafiki.
2. Hoja zote ziibuliwe na kuelezwa na mhojiwa. Hoja zinazotoka kwa mhoji zisikubaliwe.
3. Mkwaju wa wima utolewe kwa mtahiniwa pembezoni kushoto mwa karatasi ya majibu hoja inapokamilikia.
4. Atakayeandika mahojiano lakini akose maudhui (hoja) atuzwe alama 4 za sura.
5. Atakayeandika insha yenye maudhui lengwa lakini akose sura ya mahojiano akadiriwe vilivyo na kuondolewa alama 4S (za sura) baada ya kutuzwa.
6. Kaida nyingine za utahini wa insha kama vile urefu, sarufi, hijai, mtindo na msamiati zizingatiwe kikamilifu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Swali la pili**

(a) Hili ni swali la mjadala.
(b) Mtahiniwa ajadili pande zote; juhudi za serikali na vilevile juhudi za jamii kwa ujumla.
(c) Atakayezingatia upande mmoja atakuwa amepungukiwa kimaudhui hivyo basi asipite C+ 10/20

Baadhi ya hoja za kuunga mada (juhudi za jamii)

1. Wazazi kuwahimiza wanao kuenda shule.
2. Wanafunzi kuwa na ari / moyo wa kusoma – kujitolea
3. Wazazi kuchangia katika ufadhili wa masomo.
4. Wazazi kuwahimiza wanao kuenda shule.
5. Viongozi kuhakikisha watoto kutoka maeneo yao wanahudhuria masomo.
6. Walimu kujibidiisha na kuwajibikia kazi zao.

Juhudi za serikali

1. Mafunzo kwa walimu kuhusu mfumo mpya.
2. Serikali kuchapisha vitabu vya kutosha vinavyoafikiana na mfumo mpya.
3. Vifaa vinavyohitajika kufanikisha shughuli ya mafunzo.
4. Kuongeza idadi ya walimu wenye ujuzi

5. Kupiga kampeni (kupigia debe) za kuufanikisha mfumo huu.
6 Kueleza umuhimu/ manufaa ya mfumo huu wa elimu kwa jamii.

**Swali la tatu**
Hili ni swali la methali.
Mtahiniwa asimulie kisa kitakachothibitisha uamilifu wa methali hii.
Mtahiniwa anaweza kuzingatia taswira zifuatazo;

a. Mtoto ambaye anatoka katika familia ya kichochole anakosa karo lakini kwa bahati nzuri akampata mfadhili anayempa ruzuku ya masomo. Anajibidiisha kimasomo na anafaulu kujiunga na chuo kikuu.

b. Mtoto ambaye anapoteza wazazi wake analazimika kukatiza masomo yake kwa ukosefu wa karo. Baada ya muda mrefu wa kukaa nyumbani, anapata mhisani anayejitolea kumlipia karo yake baada ya masaibu yake kuangaziwa katika vyombo vya habari. Anasoma kwa kujituma na hatimaye anafaulu.

c. Mtu aliyekuwa na maono ya kuwa pengine daktari, mwalimu au rubani anajikakamua kimasomo na kufaulu kusomea taaluma aliyokuwa akiitamani.

d. Mfanyikazi fulani ambaye alitaka atambuliwe kazini, anafanya kazi yake kwa juhudi kuu na hatimaye anafaulu kupandishwa cheo pengine kuwa meneja mkurugenzi au mkurugenzi msimamizi wa masuala ya wafanyikazi.

e. Mkulima ambaye alijituma katika shughuli za kilimo. Licha ya vizingiti vingi alivyokumbana navyo ikiwemo ukosefu wa pembejeo na hata halianga isiyotabirika, hatimaye jitihada zake kuzaa matunda.

f. Kijana kutoka familia iliyolemazwa na ukata anadhamiria kuoa kutoka katika familia fulani inayojiweza. Posa yake inakataliwa kutokana na hali yake ya kiuchumi. Anajikakamua kwa kufanya vibarua vya hapa na pale na kutunduiza fedha kiasi cha haja. Anapopeleka posa kwa mara ya pili inakubaliwa na hivyo anapata barafu ya moyo wake.

**Tanbihi ~** Sharti kisa cha mtahiniwa kionyeshe hali zote mbili: yaani mhusika ambaye alikuwa katika hali fulani ya uhitaji na namna avyofanya ili kijiopoa kutokana na hali hii tete. **AU** Mhusika anayewania kitu fulani maishani na mbinu anazotumia kufikia tamanio lake.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Swali la nne**
Hii ni insha ya mdokezo.
Mtahiniwa ahitimishe kwa maneno aliyopewa.
Usimulizi ujitokeze katika nafsi ya kwanza hali ya umoja.
Msimulizi anaweza kuwa alishuhudia maovu yaliyotendwa  na mnenwa yaliyomfanya asimwamini na hatimaye huyu mhusika kutenda jambo baya zaidi ambalo linamshtua msimilizi. Mnenwa amekuwa akitenda maovu kwa kiasi fulani ingawa kwa sasa ametenda jambo baya zaidi ambalo linamwajabisha msimulizi.
Kitendo hiki cha kiuhayawani kinaweza kumwathiri msimulizi moja kwa moja au wahusika wengine.
Kuna uwezekano wa mhusika (mnenwa) kutenda mambo yanayomdhuru yeye mwenyewe na hata tujitendea hiki kitendo cha kiuhayawani.

**Baadhi ya mikondo**
a) Mhusika (mnenwa) awe mtumizi wa mihadarati kwa muda mrefu na mwishowe kujitia kitanzi.
b) Mhusika amekuwa kibaka kwa muda mrefu. Anapindukia kuwa mwizi/jambazi sugu. Anaenda kuiba kwenye benki na kuwapiga risasi walinzi wote.
c) Mhusika kufanya mambo akiwa mlevi, kwa mfano, kuwatusi watu, kuwapiga na hata kuwajeruhi. Katika hali yake ya ulevi, anaendesha gari vibaya na kusababisha ajali mbaya.
d) Mhusika kuwa laghai. Kuwasingizia wenzake shuleni/kazini kila wakati. Aendeleze ulaghai huo kwa kuwasingizia wenzake jambo baya zaidi linalowasababishia maafa kama kufukuzwa shule, kufutwa kazi au hata kufungwa jela.

**TANBIHI**
a) Jambo/tendo analolitenda mwishowe liwe baya zaidi kuliko matendo yake ya awali.
b) Asipoonyesha jambo/tendo baya zaidi (la kiuhayawani), atakuwa amepungukiwa kimaudhui. Asipite **C** 08/20
c) Asipoonyesha kilichomfanya msimulizi kutomwamini atakuwa ameshughulikia swali upande mmoja. Asipite **C**+10/20

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA**
**MACHI 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/2**

**UFAHAMU**

a) Kuimarisha uchumi (alama 1)

b) Hutegemea sera za kisiasa hasa katika uteuzi wa maarifa wanaosimamia asasi muhimu sana nchini.
   i) Kutoa ushauri kwa serikali kuhusu usimamizi wa fedha.
   ii) Kuchunguza nguvu ya shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu za kigeni.
   iii) Kutoa sarafu za Kenya kwa umma.
   iv) Usimamizi wa benki zote nchini. (alama 4)

c) i) Kuchunguza matumizi ya fedha.
   ii) Kutathmini matumizi ya fedha ya wizara mbalimbali.
   iii) Kutoa ripoti yake kamati ya uhasibu wa umma bungeni. (alama 2)

d) i) Kuhakikisha ushuru umelipwa.
   ii) Kuziba pengo baina ya walalahai na walalahoi.
   iii) Kusaidia viongozi wetu kuendeleza sera mwafaka za kiuchumi. (alama 3)

e) Ni vipi Wakenya wanaweza kuonyesha uzalendo?
   Kulipa ushuru inavyotakikana. (alama 1)

f) i) Hatima – mwisho/tamati
   ii) walalahai- matajiri/ wenye uwezo mkubwa (alama 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**UFUPISHO**

**a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 50 tu. (Alama 5, utiririko 1)**

1. Majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au kuathirika vibaya zaidi kutokana na hali mbaya ya uokoaji
2. Watu wengi hawang'amui hata chembe jinsi ya kukabiliana na uokoaji.
3. Hali ya uokoaji inaweza kurekebishwa kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma.
4. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha na hata kusababisha kifo.

**b) Eleza kwa kutumia maneno 90-100, hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji. (Alama 10, utiririko 1)**

1. Kwanza ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza ikatokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini zaidi.
2. Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi.
3. Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia , moyo unapiga jinsi anavyopumua.
4. Iwapo majeruhi anapumua, mwokoaji amweke katika hali ambayo itaimarisha kupumua kwake.
5. Ikiwa hapumui, mwokoaji anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake.
6. Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejeruhiwa – kama majeraha ni vidonda tu au kuna kuvunjika kwa mfupa na kubainisha ni mfupa upi.
7. Hatua inayofuata ni kumhamisha majeruhi kutoka eneo la ajali hadi hospitalini.
8. Ni jukumu la mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini.
9. Ni bora kuanza na majeruhi waliozimia au wenye matatizo ya kupumua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana.
10. Ujuzi wa huduma ya kwanza ni muhimu kwa kila mtu.

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) /y/ kiyeyusho **½ alama**
   /sh/ kikwamizo **½ alama**
   /h/ kikwamizo **½ alama**
   /ny/ king'ong'o **½ alama**

b) i) irabu, irabu, irabu mf aoa, aua, aue **alama 1**
   ii) irabu, konsonanti, konsonanti, konsonanti, irabu mf ombwe, imbwa, umbwa **alama 1**

c) (i) Mwanao
   Mw- ngeli
   an – mzizi
   o – umiliki **1/0**

   (ii) azingatiaye

a- nafsi ya tatu umoja
zingati – mzizi
a- kauli tenda
ye – kirejeshi **1/0**

d) (i) Barabara – zaidi – namna hali
Barabara – namna hali **alama 1**
(ii) kifisi – namna mfanano
hivi hivi – namna vikariri **alama 1**

e) Janajike hili lilibeba madoo haya hadi sokoni. **2/0**
**Mf. Mtoto wa mama ni mrefu.**

f) KN (N + RH) + KT( t + V)
Mf. Mtoto wa mama ni mrefu. **2/0**

g) i) Kitenzi kishirikishi kikamilifu
mf. Mama **alikuwa** analala **alama 1**
ii) Kitenzi kisaidizi
mf. Mtoto **alikuwa** analala sbuleni. **alama 1**

h) Mwanasiasa alisema kuwa iwapo wangempigia kura angewajengea zahanati kabla mwisho wa mwaka huo.
**½ x 6 = 3**

i) ufizi U – ZI ½
firigisi - I – ZI ½

j) Waziri atakuwa amesoma hotuba. **alama 1**

k) Nzige wengi hawakuwa wanavamia maeneo hayo kabala serikali kuchukua hatua.
**1/0**

l) **Kiima – mama**
**Mgeni wetu – yambwa tendewa**
**Nyama ya kuku – yambwa tendwa** **3 x 1**

m) Mwalimu aliyetuzwa jana - kishazi tegemezi **½ alama**
Alifundisha shairi - kishazi huru **alama 1**
Lilotungwa na Kezilahabi - kishazi tegemezi **½ alama**

n) Tathmini jawabu la mwanafunzi
Daka – shika/kamata
Taka – uchafu, kusudia/penda **(alama 2)**

o) Ka –amri km. Kaeni chini! Kamwambie aje
Ka – kitendo kitafanyika wakati ujao, km. Ata**ka**yesoma, wata**ka**oshiriki
Ka – wakati usiodhihirika, km. Waziri **ka**jiuzulu **(alama 2)**

p) Genge la wezi lilituvamia
S ---- KN + KT
KN ---- N + KH/KV
N ----- Genge
KH----- H +N /KV ---V + N
H/V ---- la
N ---- wezi
KT -----T
T -------lilituvamia **½ X 8 = 4**

q) RN – pikipiki iliyonunuliwa jana
RT – iliharibika karibu na mto
RH – karibu na mto **alama 3**

r) Amri **alama 1**

s) Kazi hii **imeniwia** ngumu sana lakini siwezi **kufishwa** moyo. **alama 2**

t) **Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.** **alama 1**

**ISIMUJAMII**

**a) Taja na kuthibitisha sajili ya mazungumzo haya.** **(alama 2)**
Sajili ya mawaidha/ushauri/ wosia/ nasaha
Mzungumzaji anamtolea msikilizaji nasaha asifuate mkondo mbaya wa maisha aliyofuata.

**b) Tambua mazingira ambamo mazungumzo haya yanatokea.** **(alama 1)**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Shuleni/chuoni/taasisi ya elimu – anaiotoa nasaha hii kwa wenzake akiwa chuoni kwa sababu anasema wasidhani atazeeka huko, lengo ni kupata shahada.

**c) Eleza sifa zozote saba za lugha iliyotumika kwenye mazungumzo haya. (alama 7)**

- Lugha iliyojaa matumini-anawania kupata uzamili na uzamifu
- Utohozi-profesa-professor
- Swali balagha-kwani kuitwa professor ni kosa.
- Iv) Lugha ya kuonya-mwenye sikio amesikia
- Nahau-nimejishika sikio-nimejirekebisha
- Lugha sanifu-Kifungu kizima kimetumia lugha ipasavyo
- Lugha ya maelezo- wapurukushe wote wakupotoshao fuata ruwaza ya wanaokujali
- Msemi-macho yamefumbika-amezinduka
- Matumizi ya msamiati wa taaluma ya kiusomi-uzamili,uzamifu na profesa
- Matumizi ya sentensi fupi fupi-Usiwe kama mimi.
- Lugha inayotumia taswira-anapotolea nasaha anasema usiwe kama mimi picha ya pengine jinsi alivyoathirika anajitokeza akilini.
- Lugha imejaa hekima-anasema fuata ruwaza ya wanaokujali(Ushauri anatoa unaongozwa na busara kwa yule hataki msikilizaji ahasirike)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA**
**MACHI 2020**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/3**

**1. Fasihi simulizi**

Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kwenye frijilakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazungukz tu . Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia ‘’ *My friend, kunywa soda”*

**a) Taja na ueleze maana ya kipera hiki. AL 2**

Kichekesho

Ni mchezo mfupi ambao hupitisha ujumbe kwa njia au namna ya kuchekesha.

**b) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita AL 6**

- Huburudisha watazamaji na waigizaji wenyewe. Burudani hii mara nyingine hupumbaza.
- Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii kama vile upashaji tohara, matambiko, majigambo, ngoma, miviga na michezo ya watoto hudumishwa kupitia maigizo.
- Ni kitambulisho cha jamii; kila jamii ina Sanaa ya maigizo ya jamii husika. Miviga na sherehe za arusi na mazishi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
- Hukuza umoja na ushirikiano wa watu wanapojumuika kushiriki katika maigizo. Hao hujitambulisha kama jamii moja.
- Ni nyenzo za kupitisha maarifa na amali za jamii kupitia michezo ya jukwaani. Husawiri mtazamo wa jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile woga, wizi na usaliti.
- Hukuza ubunifu madhalan watoto wanaposhiriki michezo ya watoto, hujifunza kubuni michezo wakiwa wachanga na pia Sanaa ya uigizaji.
- Hukuza kipawa cha uongozi katika michezo, huweza kujifunza stadi za uongozi
- Ni njia ya kuimarisha urafiki. Kwa vile mizaha na utani katika malumbano hukuza urafiki na uhusiano bora
- Huongoza jamii kupambana na na mazingira wanamojipata. Kutegemea imani ya wanajamii,matambiko yanaweza kuondoa matatizo katika jamii kama vile njaa, ugonjwa na ukame kwa kuomba Mungu
- Maigizo huelimisha kupitia maudhui na hulka za waigizaji na kushauri nafsi zao, kuiga au kukashifu hulka hizo.

**Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategenea fanani. Tetea kauli hii. (Alama 4)**

- Huwa mchangamfu na mcheshi kwa hadhira yake ili kuwafanya wapendezwe na hadithi
- Anafahamu utamaduni wa jamii yake.
- Anaifahamu hadhira yake vizuri na kusimulia kulingana na mapendeleo yao. wasichana au wavulana? vijana au wazee?
- Huwa na uwezo wa ufaraguni - uwezo wa kubadilisha sehemu fulani za sanaa bila kujifunga na muundo asilia.
- Mwenye kumbukumbu nzuri - uwezo wa kukumbuka

- Mwenye uwezo wa kuigiza kwa kutumia viungo vyake, uso (ishara-uso) na sauti(kiimbo)
- Mwenye uwezo wa kujenga taharuki kwa kusita kidogo ili kuvuta nadhari ya hadhira yake.
- Hushirikisha hadhira yake katika nyimbo n.k
- Mtambaji hodari na mkwasi wa lugha.

**Ni changamoto gani zinaweza kumkabili mwanafasihi nyanjani?( Alama 3)**

- Gharama ya utafiti-huenda gharama ikwa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu. Baadhi ya mafanani au wahojiwa huenda wakadai walipwe kabla ya kutoa habari zozote.hivyo ikiwa mtafiti hana hela basi utafiti wake utakwamizwa.
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji wa hojaji huenda ukawafanya wengi wao kutojaza hojaji zao. Wanajamii wengine huweza kushuku kwamba mtafiti anawapeleleza na wakakataa kutoa habari.
- Vizingiti vya kidini amabavyo hutokea pale ambapo baadhi ya wahojiwa wanaamini kwamba matendo ya fasihi simulizi k.v matambiko na uimbaji wa taarabu yanaenda kinyume na imani yao ya kidini.
- Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi ,kukosekana kwa wazee wanaoweza kutamba ngano ama kueleza vipera vingine k.v vitendawili.
- Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi ikiwa mkusanyaji analazimika kwenda mbali kukusanya habari,hasa katika sehemu kame itakuwa vigumu iwapo hana gari.
- Ukosefu wa usalama ,huenda mkusanyaji wa fasihi simulizi akavamiwa ,baadhi ya watu si wakarimu na huenda wakamshuku mtafiti na kuvamiwa.

**Dokeza umuhimu wa kukusanya data nyanjani. (Alama 3)**

- Ukusanyaji husaidia kurekodi na kuhifadhi tamaduni za jamii mbalimbali kwa nia ya kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
- Ukusanyaji huiendeleza fasihi simulizi kwa kurekodi vipera vya fasihi simulizi
- Husaidia kuziba pengo la utafiti liliopo.
- Ukusanyaji zaidi wa data za fasihi simulizi hutumiwa kama kiunzi cha uchunguzi wa kulinganisha fasihi simulizi za jamii mbalimbali.
- Humwezesha mwanafunzi kupata maarifa au stadi za kufanya utafiti katika taalima nyingine za kijamii kama vile sosholojia.
- Humpa mwanafunzi nafasi ya kushuhudia na kuathiriwa moja kwa moja na utendaji wa fasihi simulizi

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TAMTHILIA : KIGOGO** na *Pauline Kea*

2. “Udongo tungeliuwahi uli mbichi. Limekuwa donda ndugu sasa. Waliota mizizi ikakita na wakamea hata pembe.”
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Taja na kueleza tamathali moja ya usemi inayojitokeza kwenye dondoo hili. (alama 2)
   (c) Eleza sifa zozote nne za msemaji wa kauli hii. (alama 4)
   (d) Dondoo hili linadhihirisha jinsi baadhi ya Wanasagamoyo walivyoshiriki kuivunja jumuiya yao. Fafanua. (alama 10)

**Majibu**

(a) Kueleza muktadha
- Msemaji ni Kenga
- Anamweleza Majoka
- Walikuwa ofisini mwa Majoka
- Walikuwa wakizungumzia jinsi ya kuwakomesha watetezi wa haki
- Majoka anaahidi kuwanyamazisha anaposema dawa yao anayo.
  (4x1=4)

(b) Tamathali iliyotumumiwa
- **Methali-** udongo uwahi uli mbichi- kumaanisha wangewakomesha wapinzani walipoanza utetezi wao (kabla ya kupata nguvu zaidi)
- **Msemo-** ndonda ndugu- kumaanisha tatizo ambalo haliishi (anarejelea jinsi kuna Tunu wanang’ang’ania kupigania haki za wanyonge)
- **Nahau-** ota mizizi na mea pembe- nahau hizi zimetumiwa kuonyesha jinsi watetezi walivyo imara katika utetezi wao
  **( Ya kwanza 1x2=2) (kutambua ni alama 1, maelezoalama 1)**

(c) Sifa za Kenga

- Mbabedume/mwenye taasubi ya kiume - anaamini mwanamke hawezi kuwa shujaa Sagamoyo. Anashangaa sana Sudi anapomwonyesha kinyago cha shujaa wa kike alichokuwa akichonga.
- Mpyaro - anamtukana Tunu kuwa yeye ni hawara.
- Dhalimu - yeye na Majoka wanapanga vifo vya watu. Mfano ni mauajiyaJabali. Anapanga kuwaumiza watu kwa kutumia wahuni.
- Fisadi – anajaribu kumhonga sudi kwa zawadi nyingi kutoka kwa Majoka. Aidha anapokea kipande cha ardhi ya pale sokoni alichomegewa na Majoka.
- Mshauri mbaya - amnamshauri Majoka vibaya hasa kuhusiana na kutumia nguvu zaidi dhidi ya waandamanaji. Aidha anazua mpango wa kumtia Ashua kizuizini ili kumlazimisha Sudi kumchongea Majoka kinyago cha Ngao.
- Mwenye majuto - anapozinduka, anakiri makosa yake ya kuwanyanyasa raia na kujiunga na wanasagamoyo
- Msaliti - anamwacha Majoka na kujiunga na wanasagamoyo anapoona raia wanakaribia kufanya mapinduzi
  (Hoja 4x1=4)

d) Jinsi Wanasagamoyo walivyoivunja jumuiya yao
- Ngurumo na wahuni wenzake kumshambulia Tunu na kumjeruhi vibaya.
- Ngurumo kumsaliti Boza kwa kuzini na mkewe.
- Kenga kumpa Majoka ushauri mbaya. Mfano, kufunga soko na kulipa kisasi dhidi ya wapinzani.
- Majoka kumiliki kiwanda kikubwa zaidi cha kuzalisha sumu ya nyoka (dawa za kulevya zinazowahasiri vijana vibaya)
- Majoka kuidhinisha ukataji wa miti- matokeo yake ni ukame na ukosefu wa chakula.
- Majoka kutoa kibali kwa Asiya cha kutengeneza na kuuza pombe haramu inayowapofusha na kuwaua watu.
- Majoka kuwafurusha wachuuzi sokoni. Ananyakua ardhi hiyo ili ajenge hoteli ya kibinafsi.
- Majoka kuwapa wafanyakazi nyongeza ndogo ya mshahara huku akipandisha kodi
- Uongozi wa Majoka kuwasaliti vijana kwa kutowapa ajira baada ya kufuzu mfano ni Tunu, Ashua na Sudi.
- Viongozi kama Kenga kuwa na makundi haramu kama vile Kenga kuonekana akiwahutubia wahuni chini ya mbuyu.
- Majoka kukopa pesa kutoka nje na badala ya kuendeleza maendeleo, anafuja pesa hizo kwa mradi wa kibinafsi wa uchongaji vinyago. Pesa hizo zitalipwa na umma kwa kipindi cha miaka mia moja.
- Kampuni ya majoka kupandisha bei ya chakula kwenye kioski. Hii ni baada ya kulifunga soko.
- Wizi wa kura- Majoka anazua mbinu za wizi wa kura kwa kuhofia ushindani na aendelee kusalia mamlakani.
- Majoka kuwagawia wandani wake raslimali za umma. Mafano, Kenga anapewa kipande cha ardhi ya sokoni.
- Ngurumo na walevi wenzake pale mangweni wanamdhalilisha Tunu. Anamweleza hawezi kumpigia kura, heri amchague paka kama si Majoka.
- Majoka kuwatamani wanawake wengine licha ya kuwa na mke.
- Majokma kuvitumia vyombo vya dola kudhulumu raia. Anawatumia polisi kuwaua vijana watano waliokuwa wanaandamana ili kupinga nyongeza ya bei ya chakula kwenye duka la kampuni.
- Majoka kumchochea ashua dhidi ya mumewe Sudi- nia yake ni kuwatenganisha.
- Majoka kupanga kukifunga kituo cha Runinga ya Mzalendo kinachowazindua wanasagamoyo kuzifahamu haki zao. (Hoja zozote 10x1=10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. <u>Tamthilia ya Kigogo</u>**

1. Unyakuzi wa mali ya umma – Majoka anaamua kulifunga Soko la Chapakazi ili kujenga hoteli ya kifahari.
2. Ubinafsi – Majoka anavibomoa vibanda vya Wanasagamoyo na kupanga kujenga hoteli yake ya kifahari.
3. Utepetevu/ukosefu wa uwajibikaji – wananchi wanalipa kodi lakini wanakosa huduma kusafishiwa soko na huduma za maji taka.
4. Vitisho – Majoka anatisha kumfuta Kingi kazi
5. Viongozi wamekosa maadili ya kikazi – Majoka anamrai Ashua mkewe Sudi ili aendeleze ufuska naye.
6. Kuwatesa wapinzani – Tunu na Sudi wanateswa lakini wanaendelea kupigania mageuzi
7. Kuvunja sheria – Majoka anampa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu ambayo ni kinyume na katiba
8. Wizi wa kura –Majoka anasema kuwa hata wasipompa kura atashinda
9. Ubaguzi katika utoaji wa kandarasi - kandarasi ya kuoka keki inatolewa kwa Asiya ambaye ni mke wa Boza

10. Matumizi mabaya ya pesa za umma – pesa zinatumiwa katika shughuli za kuchonga vinyago
11. Utawala wa kiimla na wa kutojali – Wanasagamoyo hawana usemi wowote; Majoka anasema kuwa atajenga hoteli watu wapende wasipende
12. Mauaji ya kikatili – watu wasio na hatia wanauawa; Jabali
13. Kuzwazulia watu wasio na hatia - Ashua anazuiliwa na Majoka bila kosa lolote
14. Wanasagamoyo wanakabiliwa na unyonyaji – bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni imepanda maradufu tangu soko lilipofungwa
15. Kuwanyima wanasagamoyo haki ya kaundamana – wanaharamisha maandamano
16. Unasaba – Majoka anamwajiri Kenga ambaye ni binamuye kama mshauri wake mkuu
17. Viongozi wanatumia nafasi zao kuwaangamiza vijana - matumizi ya dawa za kulevya – wanfunzi katika shule ya Majoka Academy wadungana sumu ya nyoka
18. Utapeli - Kuwaongezea walimu mshahara na wauguzi na kuongeza kodi
19. Kurithisha uongozi – Majoka anapanga kutambulisha Ngao Junior kuwa kiongozi mpya mpya badala ya Wanasagamoyo kumchagua kiongozi wao
20. Kuruhusu biashara ya ukataji wa miti -
Matumizi mabaya ya vyombo vya dola – polisi wanatumiwa kuwatawanya waandamanaji4.

**4. USHAIRI**

(a) Hili ni shairi huru kwani :
1. Lina idadi tofauti ya mishororo katika ubeti ; kwa mfano, ueti wa kwanza ni sita na wa tatu ni saba.
2. Lina idadi tofauti ya mizani katika kila mshororo ; mshororo wa kwanza ni tia na wa pili ni kumi na nne katika ubeti wa kwanza.
3. Lina idadi tofauti ya vipande katika mishororo yake. Kwa mfano, lina vipande viwili katika mishororo mingi ila vipande vitatu katika ubeti wa pili mshororo wa sita, vipande viwili mshororo wa tatu ubeti wa tano.
4. Lina matumizi mengi ya alama za uakifishaji has aya kuulizia na mshangao kwa mfano, watakaokuita, Ticha ! … zilizoshikizwa kamba kwa pini
5. Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi ?
6. Utafundisha tena ngonjera ?
7. Silabi za mwisho wa kila mshororo zinatofautiana.
8. Lina matumizi ya mishata kwa mfano, kumbuka mwalimu utakapostaafu – mijusi watataga mayai ndani ya viatu vyako vilivyokwisha visigino – Na ndani ya sidiria chakavu – zilizoshikizwa kamba kwa pini.

(zozote 5 x 1=05)

(b) **Maudhui ya utamaushi**
1. Mwalimu anakuwa bure/ hana chochote.
2. Mwalimu atakapostaafu akilewa atashindwa kutembea vizuri hivyo kuwa kichekesho cha watoto.
3. Mwalimu atavaa vyatu vilivyokwisha visigino.
4. Mwalimu atavaa sidiria chakavu zilizoshikizwa kamba kwa pini.
5. Mwalimu atakosa bia au marashi mpaka mende watazaliana kwenye chupa tupu.
6. Mwalimu apungukiwa tu mkono na mgeni kiongozi anayewaacha njaa licha ya kumwimbia sifo na kumsubiri kwa muda mrefu.

(maelezo manne 4x1=04)

(a) Nafsi – nenwa ni mwalimu/ walimu –anapaswa kujilaumu kwa sababu:
1. Hana umoja (ushirikiano) na walimu wenzake hata wanasambaratika kama nyumbu.
2. Mwalimu ni mwoga. Anajikunja kama jongoo.
3. Mwalimu anafundisha nyimbo na ngonjera za kuwasifia viongozi wasiomfaidi.
4. Mwalimu anafanya kazi nyingi (kusahihisha rundo la madaftari) kwa mshahara mdogo. (mshahara wa mkia wa mbuzi)
5. Ni mnafiki.

(d) (i) Nafsi – neni ni mwalimu anayewazindua walimu wenzake waambae woga na kuanza kufundisha mambo mapya ya kuukosoa uongozi uliopo.
(ii) Toni ya kukejeli/ kushutumu / kudhihaki walimu kwa kukubali kila aina ya madhila na kwa woga wa kupindukia.
Anakejeli mwalimu atakavyostaafu akawa maskini wa kupindukia.
Toni ya kushauri / kunasihi walimu kujiunga pamoja, kufundisha mambo yanayohusiana na mabadiliko na kuasi uoga.

(Yoyote 1x2=02)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(e) (i) **Matumizi ya usambamba /urudiaji**

**Urudiaji wa miundo sawa ya mistari/ vipande**

1. Nilipokuwa mtoto niliitwa Chacha
2. Nilipokuwa kijana niliitwa Chaupele
3. Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
4. Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure

**Urudiaji wa maneno**

Nilipkuwa, niliitwa,n utakapostaafu, utafundisha, sikilizeni

**Urudiaji wa mistari**

Acha mioyo yetu izungumze

(2x1=02)

(ii) **Matumizi ya jazanda**

1. Mende kuzaliana ndani ya chupa tupu za marashi na za bia – hali ya ufukara atamojipata mwalimu aliyestaafu.
2. Kuwekwa kwenye vijiti na kutupwa nje ya ua – kuondolewa katika nafasi za kuibua sera.
3. Wacheza ngoma – viongozi
4. Mjinga mmoja – kiongozi mkuu
5. Wezi ishirini viongozi waandamizi / mawaziri
6. Historia mpya – elimu mpya ya kimapinduzi (2 x 1= 02)

(f) Maana ya mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri – kiongozi mkuu mmoja ambaye hana busara / hekima aiandamana na baraza lake la washauri waliojaa ufisadi ni sawa na hali ya kutokuwa na kiongozi (1x2=2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**5. Shairi la pili**

a)
- Lina mishororo mitatu katika kila ubeti
- Lina vipane viwili,ukwapi na utao
- Vina vya ndani/kati na nje vinabadilikabadilika kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.
- Lina mizani kumi na sita katika kila mshororo kwa kila ubeti
- Lina beti 16

b)
- Mshororo wa mwisho unabadilikabadilika katika kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho
- Mathnawi.Lina vipande viwili,ukwapi na utao
- Ukaraguni,Vina vya kati na nje vinabadilikabadilika kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho
- Sabilia.Mshororo wa mwisho wa unabadilikabadilika
- Mandhuma.Ukwapi unatoa wazo kisha utao unakamilisha

c)
- Inkisari.mifano,kayatiye
- Kuboronga sarufi/kufinyanga lugha/kubanga lugha.Mfano,"nikupe yangu ya moyo " badala ya "nikupe ya moyo yangu"
- Tabdila.Mfano' masikiyo' badala ya `masikio'

d)
- Unafaa kujitoa ufanye kazi kwa bidii/maanani
- Ukayazoe mali yako na ukishapata/ukishatia kibindoni,
- Ndipo utakapomtafuta mwandani/mwenzio/mke/mchumba

e)
- Mubalagha/maswali ya balagha.Mfano "utamwoa wa nani?"
- Msemo.Mfano kulaza damu
- Tashbihi.Mfano "muungwans ja kimeme"
- Taswira.Mfano "na marashi ya mnuko"

f) . Ni kumshauri/kumwonya mwana aliyepata masomo dhidi ya uvivu/uzembe.Mzee/mzazi anamwonya mwanawe aepuke uzembe na starehe na afanye kazi kwa bidii ili awe na maisha mema siku za usoni.

g) Mwana.Anaonywa na mzaziwe dhidi ya uvivu/uzembe wa kutofanya kazi.

h) .
- Kushauri
- Kuonya

i) i) ghere
Kukera/kufedhehesha/kusumbua
ii) sitaha
Heshima/ustaarabu/uungwana

ii) Jadili toni ya shairi hili. (alama 2)

(a) Eleza matumizi mawili mawili ya usambamba na jazanda katika shairi hili. (alama 4)

**6. CHOZI LA HERI**

**(a) Muktadha**

1. Ni maneno ya mamake Sauna
2. Anamzungumzia Sauna
3. Ni katika kumbukizai za Sauna
4. Ni baada ya Sauna kutendewa unyama na babake mlezi
5. Sauna anabakwa na kuambulia ujauzito, hali inayobainisha mkondo wa maisha ya Sauna.

**(b) Mnenewa ni Sauna**

1. Dhulumakwawatotokatikandoa/ familia. Anabakwa na babake mlezi.
2. Kikulacho ki nguoni mwako. Anawaiba wanawe Lunga ilhali aliaminiwa kuwatunza.
3. Anaendeleza maudhui ya usaliti. Anatumia furs aya uaminifu wa watoto kuwaiba na kuenda kuwauza.
4. Ukatili wa mamake. Mamake anamshurutisha kuavya mimba na kujificha tukio hilo kuwa siri.

**c) Hakuna mja aliyekamilika**

*(Walakini wa binadamu katika Chozi la Heri)*

1. Sauna
Ulanguzi wa watoto
Biashara haramu , kuwauzia watu maji machafu
2. Mamake Sauna
kumshurutisha mwanawe Sauna kuavya mimba.
Kuficha maovu ya mumewe
Anatoroka mumewe (Bwana Kero) baada ya kufutwa kazi
3. Bwana Kero
mlevi kupindukia hali inayomsababishia kufutwa kazi.
4. Bwana Maya
kumpiga makonde mkewe kila wakati,
Kumtisha na kumtusi mkewe
Kumbaka mwanawe – Sauna
5. Lunga
Tamaa ya kuwa mkulima. Kuharibu misitu
Kujigamba kuwa alitoka katika ukooo wa Kiriri
6. Naomi
Anamtoroka mumewe na kumwacha katika upweke.
Alipenda kufanya nongwa na kulalamikia maisha duni baada ya kutolewa Msitu wa Mamba.
7. Sally
Anakataa usuhuba wa Billy
Dharau, anaita jumba la Billy kiota. Hawezi kuishi kwenye kiota.
8. Bwana Kalima
Laghai, anamfuta kazi Lunga kwa kisingizio cha kustaafisha wafanyikazi ili kupunguza gharama.
9. Annette
Katili/ saliti ; anamwacha Kiriri katika ukiwa baada yao kufilisika
Alipenda kumsimanga mumewe kwa kuwaita watumishi wake ; vimada.
10. Mzee Kedi
Katili,saliti ; anamchomea Ridhaa nyumba yake na kuingamiza ailayake.
11. Zohali
Tamaa na ulimbukeni wa ujana unamsababishia ujauzito.
12. Fumba
Anamringa Rehema mwanafunzi wake.
Anamtelekeza Chandachema kwa kumwachia bibiye malezi.
13. Bwana Tenge
Mzinifu/asherati ; aliwaleta wanawake kwa nyumba wakati Bi.Kimai alikuwa shamba.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

14. Tindi
    Kaidi ; anakosa kufuata ushauri wa mamake wa kurejelea nyumbani mapema – kabla ya saa kumi na moja magharibi.
15. Mzee Buda
    Mlanguzi wa mihadarati
    Vitisho ; kumtishia Dick kusingiziwa wizi ili auawe.
16. Shamsi
    Mlevi kupindukia
    Kuwapigia watu kelele usiku
17. Subira
    Kutamauka ; anashindwa kuvumilia nongwa na masimango ya mavyaa wake.
    Anatoroka na kuwaacha wanawe na mumewe – Kaizari
18. Kipanga
    Mraibu wa dawa za kulevya
    Ananusurika kifo kutokana na kangaara iliyowaua watu sabini.

**7 CHOZI LA HERI**

Jadili jinsi mwandishi wa Riwaya hii alivyofaulu kutumia mbinu ya kinaya na sadfa . **Alama 20**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KINAYA**

- Kinaya ni maelezo ya mambo kinyume na yalivyo.
- Mwangeka anashiriki udumishaji wa amani Katika Mahariki ya kati huku familia yake ikiangamia nyumbani kutokana na ukosefu wa amani.
- Mzee Kedi anaua familia ya Ridhaa ilhali ni yeye aliyethamini masomo ya wapwaze.
- Ni kinaya wenye maduka kufunga milango wakati jumba la Ridhaa lilipochomeka badala ya kuyaacha wazi watu wotorokee .
- Ni Kinaya Lunga Kirir kuachishwa kazi baada ya kutetea wanyonge wasiuziwe mahindi yaliyokuwa na sumu.
- Ni kinaya Sauna kujifanya mzuri ilhali anawaiba watoto
- Ni kinaya Neema kupeleka mtoto kwa makazi ya watoto na mwishowe kwenda kupanga mtoto huko
- Ni kinaya Naomi kutoroka mmewe nawanawe ilhali hapo baadaye anajilaumu
- Ni kinaya nchi ambayo ¡na miaka hamsini kuonekana kama mtoto wa mika hamsini
- Ni kinaya kuwa wafrika wanakuwa wafanyikazi katika mashamba yao chini ya wakoloni
- Ni kinaya watu walioishi na Ridhaa kwa amani wanawageukia na kuchoma nyumba yake pamoja na familia yake
- Ni kinaya vijana kumbaka lime na Mwanaheri mbele ya wazazi wao
- Ni kinaya mamakwe kufukuza subira kwa kuwa hawakuwa wa jamii moja
- Ni kinaya mzee Maya kumbaka mwanawe Sauna
- Ni kinaya wazazi wa Zohali ambao ni wasomi kumtesa Zohali kwa ajili ya ujauzito
- Ni kinaya Tuama kusifu utamad uni wa tohara za kike iIhali ndio sababu ya kuwa hospitalini
- Ni kinaya watu wan chi ya Wahafidhina kumkataa kiongozi wa kike na ndiye anayewafanyia kazi
- Ni kinaya kwa pete kutaka kujia kwa kuwa na watoto watatu akiwa umri wa chini ya mia ishirini na moja

**Hoja zozote 10 X1=10**

**SADFA**

- Sadfa ni kuwaleta wahusika kadhaa pamoja bila kukusudiwa.
- Selume kufikiria kustaafu katika hospitali ya uma wakati Ridhaa alikuwa anamalizia ujenzi wa hospitali ya Mwanzo Mpya
- Umu kukutana ana Hazina alipokuwa akimtafuta.
- Safari ya Umu kuchelewa inamfanya akutane na Dick katika uwanja wa ndege.
- Mwangeka kukutana na Apondi katika karakana ni sadfa.
- Ni sadfa Umu, Dick na Mwaliko kukutana katika Hoteli ya Majaaliwa.
- Inasadifiana kuwa wakati Selume anapotaka kiacha kazi katika hospitali ya umma ndio Ridhaa anama liza kujenga hospitali ya mwanzo mpya
- Siku ya kuzaliwa kwa Umu inasadifiana nay a Mwangemi
- Inasadifiana wakati Neema akienda ofisini ana kiona kitoto kilichokuwa kimetupwa
- Umu na Dick wanakitana kisadfa katika uwanja wa ndege
- Ni sadfa Mwaliko kupangwa na binamuye mwangeka aliyempanga nduguye
- Inasadifu kuwa Dick alipokuwa akiwaza juu ya nduguye Umu alikuwa nyuma yake
- Kukutana kwa wana wa Lunga katika hoteli ya Majaliwa ni sadfa

- Ni sadfa kuwa Umu anapowaza sana juu ya maisha yake wenzake wana matatizo kumliko
**Hoja zozote 10 X1=10**

**8. Safari ya elimu ni kama ua la waridi ambalo licha ya upendezaji wake, huzingirwa na miiba. Jadili adha za safari hii kwa hoja tano tano kutoka kwa kila mojawapo wa hadithi fupi zifuatazo: Mapenzi ya Kifaurongo, Mame Bakari, Mwalimu Mstaafu na Mtihani wa Maisha.**

***Tanbihi: swali hili linamhitaji mtahiniwa kuonyesha changamoto zinazoikumba elimu***.

**1. <u>Mapenzi ya Kifaurongo</u>**

i) Ugumu wa kuelewa mambo shuleni – Dennis Machora na wenzake wanapata kugumiwa na mambo wanayofunzwa katika mhadahara chuoni. Kauli za Daktari Mabonga hazieleweki upesi.
ii) Utabaka shuleni – Dennis mwenye jadi ya kimaskini anatatizwa na maisha chuoni anakojipata akitagusana na wenzake kutoka familia za kitajiri.
iii) Kejeli za walimu – Daktari Mabonga anawajekeli wanafunzi wake kwenye mhadhara kila wanapomwuliza maswali .
iv) Kuchekwa na wanafunzi wengine – Wanafunzi wanamcheka sana Dennis anapomwomba Daktari Mabonga kutumia lugha nyepesi katika mhadhara.
v) Kutamauka shuleni – Dennis anakatizwa tamaa na masomo anapoyaona kama madubwana ambayo hakujua yalitoka wapi.
vi) Utashi /Umaskini huwakumba baadhi ya wanafunzi – Dennis anajipata na uhitaji wa vitu muhimu vikiwemo malazi bora, chakula n.k. Analazimika kulalia shuka zilizozeeka na kuchanikachanika na pia kunywa uji anapokosa chakula.
vii) Upweke/Ubaguzi shuleni – Wanafunzi wa familia za kitajiri huona haya hujinasibisha na wenzao wasio na chochote. Dennis anajipata katika upweke kutokana na hili.
viii) Anasa/ Mapenzi shuleni – Wanafunzi katika Chuo cha Kivukoni wanatumbukia kwenye anasa na masuala ya mapenzi , Dennis anawaona wenzake wakitembea huku wameshikana wawili wawili.
ix) Kukosa kazi baada ya kusoma – Dennis anatafuta kazi bila ya mafanikio licha ya kuhitimu na shahada ya uanahabari kutoka kutoka chuoni.

**2. <u>Mame Bakari</u>**

i) Mimba za mapema kwa wasichana – Sara anajipata na ujauzito unaomtatiza kimawazo akiwa mwanafunzi.
ii) Kubakwa kwa wanafunzi wa kike – Sara anabakwa na janadume asilolijua majira ya saa tatu unusu akitoka 'twisheni'.
iii) Kutengwa kwa wanafunzi wajawazito – Sara anawazia kutengwa na watu wote wa kando na wa karibu.
iv) Wanafunzi kukosa wa kuwasikiliza wanapopatwa na balaaa mishani - Sara anawaza jinsi ambavyo hakuna mtu ambaye angemwelewa baada ya kubakwa.
v) Kufukuzwa shuleni kwa wasichana wajawazito/ kukatiziwa masomo – Sara anawazia jinsi ambavyo mwalimu mkuu angemfukuza kwa kusema shule ni ya wanafunzi sio wamama.
vi) Msongo wa mawazo/ Shinikizo za akilini – Sara anajiwa na wazo la kujitoa uhai, hata hivyo nalikomesha wazo hilo.
vii) Uavyaji mimba – Wanafunzi wa kike huweza kulazimika kuavya mimba ili wafiche hali zao. Wazo hili liliwahi kumjia Sara na akalitupilia mbali.
viii) Kuaibishwa – Sara anawazia ambavyo mwalimu mkuu angemwita mama hadharani.

**3. <u>Mwalimu Mstaafu</u>**

i) Ubaguanaji kwa misingi wa wepesi wa kupata mambo darasani – Jairo alibaguliwa katika sherehe ya kustaafau kwa mwalimu Mosi kwa kuwa hakuwa hodari masomoni hivyo hakutajirika baada ya shule.
ii) Dhana potovu ya baadhi ya wanafunzi – Jairo alikuwa na dhana ya kwamba mwalimu Mosi kwa kuendelea kumpa matumaini shuleni alikuwa anamharibia wakati.
iii) Mtazamo hasi dhidi ya masomo – Jairo hakupenda masomo. Kwake waliosoma na kufanikiwa ni wakora.
iv) Baadhi ya wanafunzi huwa na uwezo wa chini wa kuelewa mambo darasani – Jairo alipata sufuri ambazo mwalimu Mosi alimpa matumaini kwamba zingepisha mia mia.
v) Walimu kupata lawama kutokana na upungufu wa wanafunzi – Jairo anamlaumu Mwalimu Mosi kwa mapungufu yake shuleni.
vi) Baadhi ya wanafunzi huzipuuza nasaha za walimu – Jairo alipuuza kabisa ushauri alioupata kutoka kwa Mwalimu Mosi kuhusu kuepuka ufuska, ulevi n.k.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**4. <u>Mtihani wa Maisha</u>**

i) Wasi wasi utokanao na matokeo ya mtihani – Samueli anajipata moyo ukimtuta anapokwenda kuyapokea matokeo ya mtihani wake wa kidato cha nne.
ii) Walimu kuwadunisha wanafunzi – Samueli anasema vile ambavyo Mwalimu mkuu hakuwahi kumwamini.
iii) Dharau kutoka kwa walimu – Mwalimu mkuu anamwonyesha dharau Samueli anapoingia ofisini kuyapokea matokeo yake. Anamtupia matokeo yake badala ya kumpa kwa njia nzuri.
iv) Wanafunzi kupumbazwa na sifa wanazopaliwa na wenzao – Samueli alipokuwa akisoma, alipumbazika na umaarufu kutoka kwa wanafunzi wengine akasahau kutia bidi. Wenzake walimtambua kama 'rasta' shuleni.
v) Kuvunjwa moyo na matokeo duni ya mtihani – Samueli anavunjika moyo anapopata matokeo duni ya mtihani.
vi) Mapenzi ya mapema – Samueli anaingilia uhusiano wa kimapenzi na msichana kwa jina Nina.
vii) Udanganyifu wa wanafunzi kwa wazazi wao – Samueli anamdanganya babake kuwa hakupata matokeo ya mtihani kwa kuwa hakukamilisha kulipa karo.
viii) Baadhi ya wanafunzi huwakosea heshima walimu- Samueli anamrejelea mwalimu mkuu kama 'hambe'.
ix) Wanafunzi kwenda mbali kupata elimu – Samueli alilazimika kusomea shule iliyokuwa mbali na nyumbani.
x) Kusalitika kwa wazazi – Wazazi wa Samueli wanahisi kusalitika baada ya mtoto wao mvulana, waliyemtegemea sana kufeli mtihani wa kidato cha nne.
xi) Elimu ya msichana kutodhaminiwa sana – Babake Samueli aliona fahari kumwona mtoto wa kiume akifanikiwa, licha ya kuwa binti zake wawili Bilha na Mwajuma walifaulu katika mtihani ya sekondari na walikuwa vyuoni.

**Tanbihi***: Mwanafunzi anaweza kupendekeza hoja nje ya zilizotolewa kwenye mwongozo huu. Hivyo, mtahini atathmini hoja za mwanafunzi.*
***Hoja tano kutoka kwa kila hadithi ( 5 × 4 = 20)***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET**
**102/1**
**KISWAHILI INSHA**
**KARATASI YA KWANZA**
**DECEMBER, 2020**

1. Wewe ni mwanahabari wa runinga tajika nchini. Matatizo ya kilimo katika Nchi yako yameshamiri kwa kiwango cha juu mno. Andika mahojiano baina Yako na afisa wakilimo nchini, mkiangazia njia mwafaka za kutahia Vizingiti hivyo.

2. Vijana ndio viongozi wa kesho kama wakinasihiwa kwa njia mwafaka; kwa muda wa miaka kumi vijana wamekumbwa na matatizo chungu nzima. Onyesha matatizo haya na jinsi yananvyoweza kutatuliwa.

3. Thibitisha ukweli wa methali‘ Mchumia juani hulia kivulini.’ Kwa kusimulia kisa cha kusisimua.

4. Tunga kisa cha kusisimua na kimalizike kwa … nahapo ndipo nilipong’amua kuwa maisha yangu yalikuwa hatarini.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA LANJET - 2020**
**102/2**
**KISWAHILI**
**DECEMBER - 2020**

**1. <u>UFAHAMU[ALAMA 15]</u>**

**<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>**
Uchumi wa mapato na matumizi ya watu katika nchi Fulani.uchumi huu huhusisaha sekta mbali mbali kama vile utalii,kilimo,sanaa,miongoni mwa sekta nyingine muhimu.ukuaji wa kiuchumi hutegemea mambo kadhaa ili kuzaa matunda.katika nchi zote ulimwenguni,sera za kisisasa huamua jinsi uchumi utakavyokuwa na kunawiri.kama siasa hazitilii maanani sera za ukuaji wa kiuchumi,basi mapato ya nchi hiyo hugubikwa katika wingu kubwaa la uchochole.

Nchini Kenya,kwa mfano,kuna ulinganifu mkubwa katika siasa na ukuaji wa kiuchumi.ukuaji wa kiuchumi hutegemea uteuzi wa maafisa wanaosimamia asasi muhimu sana katika usimamizi wa uchumi.asasi hizi ni kama vile wizara ya mipango ya kitaifa na ruwaza ya 2030,mamlaka ya ukusanyaji wa ushuru(KRA),benki kuu ya Kenya (CBK),na tume ya kupambana na ufisadi (KACC).usimamizi wa asasi hizi huwa mhimu sana katika kuamua hatima ya uchumi na nchi hii.

Katika mwezi wa juni kila mwaka,waziri wa fedha husoma bajeti kwa wabunge.katika maelezo yake dhana iitwayo nakisi ya bajeti hujitokeza.kabla ya bajeti kuandaliwa,wizara ya mipango huandaa hati iitwayo usoroveya wa kiuchumi.baada ya usomwa bajeti,ni jukumu la wabunge kupitisha mswada wa kifedha unaohusisha wizara zote au kuutupilia mbali.jukumu hili linafaa kutekelezwa kufikia tarehe 31 oktoba ya kila mwka kulingana na sheria.

Wakati huo afisa anayejulikana kama mhasibu mkuu wa serikalli na jukumu la kuchunguza na kutathimini matumizi ya fedha ya wizara mbalimbali na kutoa ripoti yake kwa kamati ya uhasibu wa umma bungeni(PAC).kamati hii hutoa mapendekezo yake kwa mkuu wa sheria na pia kwa tume ya kupambanma naufisadi ili haki iweze kutekelezwa mahakamani iwapo dosari za kifedha zimefanyika.

Benki kuu ya Kenya kupitia kwa gavana wake huwa na jukumu la kutoa ushauri kwa serikali kuhusu usimamizi wa kifedha,kuchunguza nguvu za shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu za kigeni,kutoa sarafu za Kenya kwa umma na usimamizi wa benki zote nchini miongoni mwa majukumu mengine.

Kwa upande mwingine,mamlaka ya ukusanyaji ushuru nchini huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa malengo ya ushuru yamefikiwa na pia kuhakikisha kuwa hakuna mtu binafsi au kampuni yoyote inayokwepa kulipa ushuru.iwapo kuna udanganyifu wowote,basi swala hili linafaa kuangaliwa na mahakama zetu na haki kutekelezwa.

Ka jumla,sisi kama wananchi tunafaa kusaidia asasi hizi zote kufikia malengo yake ili tupate ukuaji wa kiuchumi utakaofaidi watu wote.jambo hili litahakikisha kuwa pengo lililo kati ya walalahai na walalahoi limezibwa.sisis kama wananchi,tunafaa kuonyesha uzalendo wetu kwa nchi yetu kwa kulipa ushuru inavyotakina,tukifuata mwito kuwa KULIPA USHURU NI KUJITEGEMEA.mwisho tusiadie viongozi wetu katika kuendeleza sera mwafakla za kiuchumi ili nchi yetu ipige hatua kubwa katika ukuaji wa kiuchumi.iwapo afisa yeyote atatuhumiwa kushiriki katika kashfa yoyote ya kuhujumu nidhamu ya kifedha,basi anafaa kukabiliwa vilivyo kisheria bila kujali hadhi yake ya kijamii au kisiasa.

**Maswali**

a) Ipe habari hii kichwa mwafaka (alama1)
b) Uchumi ni nini) (alama 1)
c) Benki kuu ya Kenya ina majukumu yapi? (alama2)
d) Mhasibu mkuu ana dhima gani serikalini? (alama1)
e) Pendekeza hatua mbili za kufufua uchumi (alama 2)
f) Ufisadi umehujumu vipi ukuaji wa kiuchumi? (alama 3
g) Eleza maneno yafuatayo kama kama yalivyotumika katika ufahamu
   i) Nakisi ya bajeti (alama 1)
   ii) Usoroveya wa kiuchumi (alama1)
   iii) Bajeti (alama 1)
   iv) Hatima (alama 1)
   v) Walalahai na walalahoi (alama 1)

**2. UFUPISHO[ALAMA 15]**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

**HAKI ZA MKENYA KIKATIBA**

Kumnyima mtu nafasi na kufanya mikutano popote ni kinyume cha sheria za Kenya hasa zinavyopatoikana katika katiba.kila mwnanch ana haki ya kutangamana na uhuru kuhudhuria mikutano yoyote.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Ningetaka kurejelea baadhi ya haki hizi ili ziweze kueleweka na wakenya wengi.itauwa kwamba sheria ya haki za binadamu inamhakikishia mtu haki na uhuru bila khusisha kabila,makazi maoni ya kisiasa,imani ya sisa,rangi au jinsia yake(mke au mume).haki zinazolinda katiba ya Kenya ni nyingi.

Katuiba ya Kenya inasema kuwa kila mtu ana haki kuwa hai na hakuna mtu anaeza kupoteza uhai wake makusudi,isipokuwa katika utekelezaji wa hukumu ya kifo iliyopitishwa na mahakma.

Hata hivyo,kuuwa kwa mtu yeyote hakuchukuliwi kuwa uvunjaji wa haki za kimsingi ni:katika kujitetea au katika kutetea mali,au:wakati wa kutiwa nguvuni kisheria,kuzuiwa aliyezuiliwa kisheria kutoroka au katika kukomesha ghasia,maasai au mgomo,au:ili kuzuia mtu ana uhalifu,au:katika tukio la vitu vilivyotangzwa kisheria,hata mwizi sugu sugu analindwa na katiba na haki zake zote.

Kitu cha kusikitisha ni kwamba wananchi wengi hawana imani na Mahakam zetu,na kwamba hujichukulia sheria mikononi pindi wanapokumbana na wezi.hapo ndipo hutokea kitendo cha hawa wananchi wenye hamasa na wezi huopigwa na kuuawa popo hapo.

Uwezekano wa kumuuumiza mtu asiyekuwa na hatia ni wa kweli.aghalabu,raia wapiti njia huchukuliwa kama wezi n ahuweza kuumia bure bilashi.

Haki nyingine inayolindwa na katiba ni haki ya uhuru wa mtu binafsi.hii ina maaana ya uhuru wa mtu kutofungwa jela au kutiwa kizuizini bila sababau yoyote.mtu anapokamatwa au kuzuiwa mujibu wa sheria,hapo mtu huyo ananyang'anywa haki hii.

Kwa mujibu wa sheria,mtu hatatiwa nguvuni au kuzuiliwa isipokuwa:kupitia utekelezaji hu au amri ya utekelezaji wa hukumu au amri iliyotolewa kwake kwa mujibu wa amri ya mahakama kwa madhumuni ya kupelekwa jela ya mahakama au kisheria,au:kukiwa na tuhuma ya kutosha kwa ametenda au alikuwa karibu kutenda kosa la uhalifu.

Kadhalika,mtu hukamatwa au kuzuiliwa akiwa mwenye umri wa miaka chini ya 18 kwa madhumuni kumpeleka shuleni,au:kwa madhumuni ya kuzuia usambazaji wa ugonjwa wa kuambukiza au kuml na kumtibu mtu ambaye ana sababu ya kutosha la uhalifu.

Atashikwa pia akiwa ni mraibu wa dawa za kulevya au pombe,au mzururaji asiyekuwa mahali maaalumu pa kuishi au katika kumzuia kuingia Kenya kinyume cha sheria au katika kutekeleza amri ya kumfukuza,kumrudisha kwao ili afikishwe mahakamani au kumwondoa nchini Kenya.

Mtu aliyetiwa nguvuni au kuzuiliwa lazima ajulishwe upesi iwezekanavyo sababu ya hatua hiyo.katiba inatoa uhakika wa kesi kuendeshwa haraka,haki ya kuwasiliana na mahakimu na haki ya dhamana.

Kwa bahati mbay,tunajua hii huvunjwa panapotumika sheria zinazokandamiza.mara kwa mara tumesikia wananchi wengi hutiwa nguvuni na kuzuiliwa kwa muda mrefu bila kufikiswa mahakamani.

Mbinu mojawapo itumikayo ni kuwahamisha washukiwa kutoka kitua kimoja ch apolisi hadi kingine.kitendo hiki ni kinyume kabisa na katiba.

Isitoshe,tunajua polisi wameweza kuwafungia watu na kuwatesa kwa muda mrefu.mtu aliyeshikwa ili aletwe mahakamani au kwa sababu kuna tuhuma tosha ya kuwa ametenda au alikuwa karibu utenda kosa la uhalifu ni lazima afikishwe mahakamani upesi iwezekanavyo katika muda wa saa 24 tangu anaswe au katika muda wa siku 14 tangu atiwe nguvuni,endapo amekamatwa kutokana na tuhuma tosha ya kuwa ametenda au alikuwa karibu kutenda kosa la uharifu,uuuaji au wizi wa kutumia nguvu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali.**

a) Eleza haki zinazorejelewa katika taarifa hii (maneno 25-35)
(Alama 6+1mtiririko)
Matayarisho

b). Eleza sababu zinazofanya haki ya mtu kukiukwa (maneno 50-55)
(alama 7+1mtiririko)
Matayarisho

**3.MATUMIZI YA LUGHA [ALAMA 40]**

a. Bainisha mofimu katika neno lifuatalo (alama 2)
Zisizosukika

b. Tambua aina za vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mstari (alama 2)
Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya yeye ndiye mwizi.

c., Andika vinyume vya maneno yaliypigiwa mstari (alam 2)
**i) Alipofika nilimlaki**
**ii) Aliponiona alitabasamu**

d. Bainisha vishazi huru na vishazi vitegemezi katika sentensi ifuatayo. [alama 2]
Hurafa ni hadithi zenye wahusika wanyama na visasili huhusu chanzo cha jambo Fulani.

e. Bainisha virai katika sentensi (alama 1)
Metobo alimtaka kulipa deni lote.

f. Andika katika usemi wa taarifa. (alama 3)
"Vileo havipaswi kupewa matangazo ya kuvutia,"akasema hatibu

g. unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo (alama 1)
a) punga
b) tunza

h. Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha visanduku. [alama 3]
Mwalimu aliyepanda mbegu amevuna mazao mengi.

i. Tunga sentensi sahihi katika kauli ya kufanyia (al 2)
i) -fa-

ii) -cha-

j. Andika kwa umoja. [alama2]
Uovu waliotuonyesha hautasahaulika

k. Kanusha sentensi ifuatayo. [alama 2]
Kuchora kwake kulitunufaisha

l. Geuza sentensi ifuatayo ukitumia 'O' rejeshi katika hali ya mazoea. [alama2]

Jino ambalo lilingolewa liliota tena.

m. Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa. [alama 2]
Kigoma chake kilipigwa hadi kikapasuka.

o. Eleza matumizi ya kiungo –ki-katika sentensi ifuatayo (al 1)
Lydia amekuwa akisoma vitabu hivi tangu asubuhi.

p. Andika kisawe kimoja kwa neno ulilopewa (al 1)
i) nikahi

q. Tunga methali moja kutokana na taarifa ifiuatayo:- [alama 2]
Mtoto akidekezwa sana tabia yake itakua mbaya akiwa mtu mzima.

r. Eleza maana mbili katika neno lifuatalo (al 1)
Furuka

s. Unda majina mawili kutokana na vivumishi ulivyopewa (al 2)
i) jahili
ii) cheshi

t. Akifisha kifungu hiki;- (ala 4)
Mungu wangu ona umelitia doa shati langu jeupe metobo alifoka.

u. Tofautisha katika ya sentensi hizi. [alama 3]
i) yambwa tendewa
ii) yambwa tendwa

**ISIMU JAMII(ALAMA 10)**

a. Eleza maana ya usanifishaji wa lugha ya kiswahili(alama 2)
b. Taja na ueleze matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili(al 4)
c. Tofautisha kati ya lugha ya kimataifa na lugha ya taifa. (alama 4)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA LANJET - 2020**
**102/3**
**KISWAHILI FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**DICEMBA, 2020**

.

**SEHUMU YA A**
**TAMTHILIA: KIGOGO**
(Pauline Kea)

1. "Ni laghai siwaamini. Wanasema wanakwenda huku na mara…"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b) Eleza mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (Alama 2)
c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji. (Alama 6)
d) Fafanua jinsi wanaorejelewa na mzungumzaji walivyo laghai. (Alama 10)

**SEHEMU YA B**
**RIWAYA: CHOZI LA HERI**
(Assumpta K. Matei)
Jibu swali la ***Pili*** au la ***Tatu***

2. "Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alalama 4)
b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (alama 6)
d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. (alama 8)

*Au*

3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:
(a) Hotuba (alama 10)

(b) Uozo katika jamii (alama 10)

**SEHEMU YA C**

**HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

(Alifa Chokocho na Dumu Kayanda- Wahariri)

Jibu swali la ***Nne*** ama la ***Tano***

**NDOTO YA MASHAKA**

4. “Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi.”
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Mzungumzaji alikuwa na haki ya kuradua kufa. Thibitisha. (alama 12)

*Au*

5. Ukirejelea hadithi zozote nne katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, eleza jinsi maudhui ya Mapenzi na ndoa yanavyojitokeza (alama 20)

**SEHEMU YA D**

**USHAIRI**

***Jibu swali la sita ama la saba***

***6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

Naogopa, kukupa wangu mtima, sitaki mie nilie
Naogopa, kutoa yangu kalima, eti wewe utulie
Naogopa, ninashindwa kusimama, wewe pete unitie
Naogopa, wanaume wanauma, ja panya wapulizie.

Naogopa, kwita wako mama mama, nami anikaripie
Naogopa, sipendi nyingi dhuluma, za wanaume nilie
Naogopa, kushinda nimeinama, goti mume nipigie
Naogopa, za mkemwenza hujuma, matusi anipatie.

Naogopa, uchungu ukiniuma, mwana nikakuzalie
Naogopa, kupigwa kama ngoma, ndiposa nikatulie
Naogopa, kila kitu kunisoma, ndo hela unipatie
Naogopa, kuitwa mwizi wa sima, ila nikuandalie.

Naogopa, dadazo kuwaandama, udaku wakanitie
Naogopa, kuuleta uhasama, mimi mnipiganie
Naogopa, koritini kusimama, mali tukashindanie
Naogopa, kumwaga wenu mtama, kuku niwamiminie,

Naogopa, naogopa ninasema, yabidi uvumilie
Naogopa, nawe babu kusimama, eti ndoa niingie
Naogopa, ndoto zangu kuzizima, hili doa nijitie
Naogopa, <u>taa yangu kuizima</u>, mwingine jitafutie.

***(Meja S. Bukachi- Uketo wa Ushairi uk 24)***

**MASWALI**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)
b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 1)
c) Nani nafsi nenewa katika shairi hili? (Alama 1)
d) Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili. (Alama 2)
e) Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga. (Alama 2)
f) Weka shairi hili katika bahari mbalimbali. (Alama 3)
g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)
h) Kwa nini nafsi neni anasita kuchukua hatua? (alama 4)
i) Vifungu vifuatavyo vina maana gani katika shairi? (alama 2)
   i. Taa yangu kuizima
   ii. Dhuluma

***Au***

***7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Ee mpwa wangu,
Kwetu  hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisha kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mume,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. (alama 2)
(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ? (alama 2)
(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi ya kiume (alama2)
(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (alama 4)
(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (alama 2)
(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili (alama 4)
(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (alama 4)
  (i) Mbari
  (ii) Msununu
  (iii) Ngariba
  (iv) Uvundo

**SEHEMU YA E**
**FASIHI SIMULIZI**

***Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali***

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye niliompa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu na waone chozi langu, wasikie kilio changu,
Mizimu na waone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!

***(Kutoka: Assumpta K. Matei- Fani ya Fasihi Simulizi, uk 145)***

**Maswali**

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 2)
(b) Jinsia ya nafsi neni ni gani? (alama 2)
(c) Eleza sifa zozote sita za kipera hiki cha fasihi simulizi. (alama 6)
(d) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii. (alama 4)
(e) Fafanua njia sita jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi. (alama 6)

For more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET**
**KISWAHILI KARATASI YA 1**
**INSHA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**
**DESEMBA, 2020**

1. a. Ni sharti insha hii iwe na kichwa.
   b. Utangulizi ni sharti uwepo.
   c. Mahokiano huwa na hitimisho.

Hoja za kuangaziwa. (matatizo)
1. Wakulima kununua mbegu duni.
2. Uchechefu wa fedha za kuendelea kilimo.
3. Ukosefu wa elimu tosha ili kuendeleza kilimo cha kisasa.
4. kupata mbegu na mbolea kwa wakati usiofaa. (kama zimechelewa)
5. Magonjwa ya mifugo na mimea.
6. Kiangazi.
7. Njia mbovu za kusafirishia mazao ya wakulima.
8. Ukosefu wa wawekezaji nchini.
9. Ukosefu wa soko mwafaka.
10. Wezi wa mifugo.

Suluhu.
a. Serikali kuhakikisha mbegu na mbolea ni za kiwango cha juu.
b. Serikali kuwapa wakulima mikopo.
c. Maafisa waelekezi kutolewa na serikali za gatuzi tofauti.
d. Maafisa wa kuwatibu mifugo kuajiriwa na serikali za gatuzi tofauti.
e. Serikali kuona kwamba wakulima wamepata maji kwa wingi.
f. Serikali kurekebisha barabara ili magari ya kusafirisa mazao kufika vijijini.
g. Serikali kuwapa wakulima ulinzi na kurai wawekezaji.

1. Matatizo.
    a. Ukosefu wa kazi.
    b. Matumizi ya dawa za kulevya.
    c. Uigaji wa hulka za kigoni mitandaoni.
    d. Kuna utepetevu miongoni mwa washika dau kazini.
    e. Ukosefu wa vielelezo wema.
    f. Malezi mabaya
    g. Shinikizo la rika
    h. Kuzorota kwa maadili.
    i. Ubaguni kazini. (uhaba wa tajriba)

Suluhu
    a. Ni sharti serikali ibuni nafasi za kazi.
    b. Sheria kali kuwekwa.
    c. Vijana kupewa mawaidha mara kwa mara, na kuelimishwa.
    d. Washika dau kukumbushwa majukumu yao, ili wawe vielelezo wema.
    e. Kutokana na malezi mabaya vijana waelimishwe upya.
    f. Vijana wapewe nafasi kazini waache kuanguliwa kwa sababu ya uhaba wa tajriba.
    g. Matatizo katika nambari 8 na 9 vijana wanahitaji kufunzwa upya.

2. Maana ya methali ni sharti iwekwe bayana.
    Ni lazima mtahiniwa aangazie pandi mbili za methali

    Kuchumia juani, changamoto alizozipata alipokuwa akifanya kazi.
    Kulia juani; ufanisi uangaziwe kwa kina.
    Methali ione na kisa kitachosimuliwa.

3. Ni sharti kisa kione na kipengele mtahiniwa apewa.
    Kisa kiwe cha kusisimua msomaji.
    Kisa chenyewe kitamatike kwa kipengele kilichotolewa.
    Mtahiniwa asipokitumia kipengele hicho atuzwe.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET</u>**
**<u>102/2 KISWAHILI</u>**
**<u>DECEMBER, 2020</u>**
**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA</u>**

**1. Ufahamu**
Maswali
a) Ipe habari hii kichwa mwafaka (alm1)
– Mfumo wa uchumi nchini
b) Uchumi ni nini) (alama 1)
– Ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi Fulani
c) Benki kuu ya Kenya ina majukumu yapi? (alama2)
– Kutoa ushauri juu ya usimamizi wa fedha/kuchunguza nguvu ya shilingi ya Kenya/usimamizi wa benki zote.
d) Mhasibu mkuu ana dhima gani serikalini? (alama1)
– Kuchunguza na kutadhimini matumizi ya pesa katika wizara.
e) Pendekeza hatua mbili za kufufua uchumi (alama 2)
– Kukusanya ushuru.
– Kuendeleza sara mwafaka.
f) Ufisadi umehujumu vipi ukuaji wa kiuchumi? (alama 3)
– Kutokua na maafisa waaminifu.
g) Eleza maneno yafuatayo kama kama yalivyotumika katika ufahamu
    i) Nakisi ya bajeti (alama 1)
    – Upungufu wa fedha.
    ii) Usoroveya wa kiuchumi (alama1)

– Kusoroteka katika uchumi

iii) Bajeti (alama 1)
– Makadirio ya matumizi ya pesa
iv) Hatima (alama 1)
– mwisho
v) Walalahai na walalahoi (alama 1)
– Matajiri na maskini

TAHADHARI
- Ondoa nusu maki kwa kila kosa la sarufi litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita
- ondoa nusu maki kwa kila kosa la hijai litokeapo mara ya kwanza hadimakosa sita
- jumla ya makosa ya sarufi nay a tahajia yaondolewe baada ya kupitia maswali yote

**2. <u>Ufupisho</u>**
soma makala yafuatayo kisha ujibu

**HAKI ZA MKENYA KIKATIBA**

Kumnyima mtu nafasi na kufanya mikutano popote ni kinyume cha sheria za Kenya hasa zinavyopatoikana katika katiba.kila mwnanch ana haki ya kutangamana na uhuru kuhudhuria mikutano yoyote.

Ningetaka kurejelea baadhi ya haki hizi ili ziweze kueleweka na wakenya wengi.itauwa kwamba sheria ya haki za binadamu inamhakikishia mtu haki na uhuru bila khusisha kabila,makazi maoni ya kisiasa,imani ya sisa,rangi au jinsia yake(mke au mume).haki zinazolinda katiba ya Kenya ni nyingi.

Katuiba ya Kenya inasema kuwa kila mtu ana haki kuwa hai na hakuna mtu anaeza kupoteza uhai wake makusudi,isipokuwa katika utekelezaji wa hukumu ya kifo iliyopitishwa na mahakma.

Hata hivyo,kuuwa kwa mtu yeyote hakuchukuliwi kuwa uvunjaji wa haki za kimsingi ni:katika kujitetea au katika kutetea mali,au:wakati wa kutiwa nguvuni kisheria,kuzuiwa aliyezuiliwa kisheria kutoroka au katika kukomesha ghasia,maasai au mgomo,au:ili kuzuia mtu ana uhalifu,au:katika tukio la vitu vilivyotangzwa kisheria,hata mwizi sugu sugu analindwa na katiba na haki zake zote.

Kitu cha kusikitisha ni kwamba wananchi wengi hawana imani na Mahakam zetu,na kwamba hujichukulia sheria mikononi pindi wanapokumbana na wezi.hapo ndipo hutokea kitendo cha hawa wananchi wenye hamasa na wezi huopigwa na kuuawa popo hapo.

Uwezekano wa kumuuumiza mtu asiyekuwa na hatia ni wa kweli.aghalabu,raia wapiti njia huchukuliwa kama wezi n ahuweza kuumia bure bilashi.

Haki nyingine inayolindwa na katiba ni haki ya uhuru wa mtu binafsi.hii ina maaana ya uhuru wa mtu kutofungwa jela au kutiwa kizuizini bila sababau yoyote.mtu anapokamatwa au kuzuiwa mujibu wa sheria,hapo mtu huyo ananyang'anywa haki hii.

Kwa mujibu wa sheria,mtu hatatiwa nguvuni au kuzuiliwa isipokuwa:kupitia utekelezaji hu au amri ya utekelezaji wa hukumu au amri iliyotolewa kwake kwa mujibu wa amri ya mahakama kwa madhumuni ya kupelekwa jela ya mahakama au kisheria,au:kukiwa na tuhuma ya kutosha kwa ametenda au alikuwa karibu kutenda kosa la uhalifu.

Kadhalika,mtu hukamatwa au kuzuiliwa akiwa mwenye umri wa miaka chini ya 18 kwa madhumuni kumpeleka shuleni,au:kwa madhumuni ya kuzuia usambazaji wa ugonjwa wa kuambukiza au kuml na kumtibu mtu ambaye na asababu ya kutosha lauhalifu.

Atashikwa pia akiwa ni mraibu wa dawa za kulevya au pombe,au mzururaji asiyekuwa mahali maaalumu pa kuishi au katika kumzuia kuingia Kenya kinyume cha sheria au katika kutekeleza amri ya kumfukuza,kumrudisha kwao ili afikishwwwe mahakamani au kumwondoa nchini Kenya.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Mtu aliyetiwa nguvuni au kuzuiliwa lazimna ajulishwe upesi iwezekanavyo sababu ya hatua hiyo.katiba inatoa uhakika wa kesi kuendeshwa haraka,haki ya kuwasiliana na mahakimu na haki ya dhamana.

Kwa bahati mbay,tunajua hii huvunjwa panapotumika sheria zinazokandamiza.mara kwa mara tumesikia wananchi wengi hutiwa nguvuni na kuzuiliwa kwa muda mrefu bila kufikiswa mahakamani.

Mbinu mojawapo itumikayo ni kuwahamisha washukiwa kutoka kitua kimoja ch apolisi hadi kingine.kitendo hiki ni kinyume kabisa na katiba.

Isitoshe,tunajua polisi wameweza kuwafungia watu na kuwatesa kwa muda mrefu.mtu aliyeshikwa ili aletwe mahakamani au kwa sababu kuna tuhuma tosha ya kuwa ametenda au alikuwa karibu utenda kosa la uhalifu ni lazima afikishwe mahakamani upesi iwezekanavyo katika muda wa saa 24 tangu anaswe au katika muda wa siku 14 tangu atiwe nguvuni,endapo amekamatwa kutokana na tuhuma tosha ya kuwa ametenda au alikuwa karibu kutenda kosa la uharifu,uuuaji au wizi wa kutumia nguvu.

**Maswali.**

b) Eleza haki zinazorejelewa katika taarifa hii (maneno 25-35)
(Alama 6+1mtiririko)
matayarisho

- **Kufanya mikutano popote**
- **Kutangamana/kuhudhina mikutano**
- **Kuwa hai**
- **Mtu binafsi/kutofungwa jela/kutiwa kizuizini bila sababu.**
- **Anayetiwa kizuizini aambiwe sababu.**
- **Kesi iendeshwe haraka.**
- **Haki ya kuwasiliana na mahakama.**
- **Haki ya dhamana.**

Jibu

c) Eleza sababu zinazofanya haki ya mtu kukiukwa(maneno 50-55)
(alama 7+1mtiririko)
Matayarisho

- **Akiwa chini ya miaka 18 anweza kukamatwa na kupelekwa shuleni**
- **Kumlinda na kumtibu mtu ambaye kuna sababu ya kutosha kushukiwa kwamba hana akili timamu**
- **Kumzuia kuingia Kenya kinyume cha sheria au kutekelezwa zmri ya kumfukuza.**
- **Utekelezaji wa hukumu ya kifo iliyofishwa na mahakama**
- **Kuwa mtu katika kujitetea/ kutetea mali.**
- **Kuzuia mtu kutoroka akiwa amezuiwa kisheria.**
- **Mtu anapokamatwa au kuzuiliwa kwa mujibu wa sheria.**

Jibu

TAHADHANI UFUPISHO

- Ondoa nusu makii kwa kila kosa la sauti litokeapo mara ya kwanza hadi makosa 12.
- Ondoa nusu maki kwa kila kosa la tahajia litokeapo mara ya kwanza hadi makosa 6.
- Maneno yakizidi kwa 5 (odoa nusu maki) ; 10 ondoa maki
- Makosa yatolewe baada ya kujumulisha maki zote

**<u>SARUFI</u>**

a. Bainisha mofimu katika neno lifuatalo (alama 2)

Zi-ngeliu
Si- kikanushi
Zo- kirejeshi
Suk- mzizi/shina la kitenzi
Ik- kauli
a- Kiishio

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b. Tambua aina za vitenzi katika sentensi hii kwa kuvioigia mistari (alama 2)
Sisi tulikwisha kutambua alikua na nia mbaya yeye ndiye mwizi.
Tukikwisha –saidizi
Kutambua- kikuu
Alikuwa- saidizi
Ndiye- kishikishi kipungufu

c. Andika vinyume vya maneno yaliypigiwa mstari(alam 2)
iii) Alipofika nilimlaki
**Jibu;alipoondoka,nilimwaga**
iv) Aliponiona alitabasamu
**Jibu;aliponiona alinuna**

d. Bainisha vishazi huru na vishazi vitegemezi katika sentensi ifuatayo.
Hurafa ni hadithi zenye wahusika wanyama na visasili huhgusu chanzo cha jambo Fulani.
- Hurafa ni hadithi zenye wahusika wanyama- kishazi huru
- Visasili huhusu chanzo cha jambo Fulani- kishazi huru

e. Bainisha virai katika sentensi (alama 1)
Metobo alimtaka kulipa deni lote.
**Jibu**
- Metobo- kirai nomino
- Deni lote- kirai nomino

f. Andika katika usemi wa taarifa.(alama 3)
"Vileo havipaswa kupewa matangazo ya kuvutia,"akasema hatibu
– Hatibu alisema kwamba vileo havikupasa kupewa matangazo ya kuvutia

g. I) unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo(alm 1)
a) punga
– punga, mpungwaji
b) tunza
– tunzo, mtunzaji, utunziji

h. Changanua sentensi ifutayo kwa kielezo cha jedwali/visanduku.
Mwalimu aliyepanda mbegu amevuna mazao mengi.
**Jibu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S | | | | |
| KN | | KT | | |
| N | S | T | KN | |
| | | | N | V |
| mkulima | Aliyepanda mbegu | amevuna | mazao | mengi |

i. Tunga sentensi sahihi katika kauli ya kufanyiza (al 2)
i)-fa-
– Fia- mwalimu ahakiki jibu la mwanafunzi
ii)-cha-
– Chea –mwalimu ahakiki jibu la mwanafunzi
Tanbihi: bila sentensi mwanafunzi asipate alama.

j. Andika kwa umoja
Uovu waliotuonyesha hautasaulika
– Uovu alionionyesha hautasahaulika

k. Kanusha sentensi ifuatayo.
Kuchora kwake kulitunufaisha(al 2)
– Kuchora kwake hakukutunufaisha

l. Geuza sentensi ifuatayo ukitumia 'O' rejeshi ya mazoea.
Jino lililongolewa liliota tena.
– Jino ling'olewalo huota tena

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Jino linalong'olewa huota tena

m. Andika wingi wa sentesi hii katika hali ya ukubwa
  - Magoma yao yalipigwa hadi yakapasuka

n. Eleza matumizi ya kiungo –ki-katika sentensi ifuatayo(al 1)
  Mwalimu amekua akisoma vitabu hivi tangu asubuhi.
  - Kitendo kimekuwa kikiendelea kwa muda Fulani.

o. Andika kisawe kimoja kwa neno uilopewa(al 1)
  i) Nikahi
  - Ndoa/harusi/akidi

p. Tunga methali moja kutokana na taarifa ifiuatayo:-
  Mtoto akidekezwa sana tabia yake itakua mbaya akiwa mtu mzima.
  - Mtoto umleavyo ndivyo akuwavyo.
  - Mwacha mwana kulia hulia yeye mwenyewe.
  - Usipo ziba ufa utaziba ukuta

q. Eleza maana mbili mbili katika neno lifuatalo(al 1)
  Furuka
  - Kuwa mkubwa; kua
  - Kuwa na furaha; changamka

r. Unda majina mawili kutokana na vivumishi ulivyopewa(al 2)
  i) jahili
  - Ujahili, majakili

  ii)cheshi
  - Ucheshi, mcheshi

s. Akifisha kifungu hiki;-(ala 4)
  Mungu wangu ona umelitia doa shati langu jeupe metobo alifoka.
  - "mungu wangu! Ona umelitia doa sharti langu jeupe." Metoko alifoka

t. Tofautisha katika sentensi
  i) yambwa tendewa
  - Shangazi alimnunulia <u>mtoto</u> gari.

  ii)yambwa tendwa
  - Shangazi alimnunulia mtoto <u>gari</u>

    <u>TAHADHARI</u>
    <u>-Ondoa makosa ya sarufi [s] nay a tahajia [h] kama yatokeapo</u>
    <u>-Ondoa nusu maki kwa kila kosa litokeapo mara ya kwanza liwe la sarufi ama la tahajia</u>
    <u>-Usiondoe zaidi ya nusu alama zilizotolewa kwa kila swali</u>

**ISIMU JAMII(ALAMA 10)**

d. eleza maana ya usanifishaji wa lugha ya kiswahili(alama 2)
  - ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo wa lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana, kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi
  - kusanifisha ni utaratibu wa kuondoa tofauti zote za lugha ambazo hutokana na kimaeneo na tabaka.

e. taja na ueleze matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili(al 4)
  - kuwapo na wananchi wengi wanaolonea fahari lugha ya kiingereza kuliko ya Kiswahili.
  - Kasumba kuwa lugha ya Kiswahili ni ya watu ambao hawajaelimika.
  - Vipindi zaidi kutoka redio na runinga hupeperushwa kwa kingereza kuliko kwa lugha ya Kiswahili.
  - Lugha za kikabila kushamili zaidi kimatumizi kuliko Kiswahili miongoni mwa jamii mbalimbali.
  - Kuzuka na kuenea kwa sheng mionggoni mwa vijana kunakunakwadhini usanifu na ueneaji wa Kiswahili.
  - Magazeti na majarida mengine yanayochapishwa ni ya kiingereza.
  - Hakuna sera maalum na imara kuhusu matumizi ya Kiswahili.
  - Uhaba wa utafiti wa Kiswahili.
  - Wanasiasa wengi kutopigia upatu ukuzaji na utumizi wa lugha ya Kiswahili.
  - Upungufu wa wataalamna imara kuhusu matumizi ya Kiswahili kama vile walimu.
  - Wengi wa wanafunzi hujikita tu katika kufundisha yale ya mitalaa badala ya kupanua mawanda ya wanafunzi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

f. Tofautisha kati ya lugha ya kimataifa na lugha ya taifa. (alama 4)
- Lugha ya kimataifa inaweza kutumika katika mawasiliano nje ya mipaka ya nchi husika kwa masuala ya kisiasa, kidiplomasia, kibiashara na kitamaduni.
- Lugha ya taifa ni lugha iliyoteuliwa kama kitambulisho na ustaarabu wa taifa zima.

**MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**
**102/3**
**KISWAHILI FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**DISEMBA 2020**

**SEHUMU YA A**
**TAMTHILIA: KIGOGO**
(Pauline Kea)

**1. “Ni laghai siwaamini. Wanasema wanakwenda huku na mara…”**

**a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)**
Haya ni maneno ya Majoka. Anamwambia Babu anapokuwa amezimia. Yupo katika chumba cha wagonjwa. Majoka analalamika kuwa chombo kinaenda kinyume na matarajio yake. Babu anamtaka Majoka asilalamike kwani yeye ni mmoja wa marubani. (4×1= 4)

**b) Eleza mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (Alama 2)**
Kinaya- Majoka analalamika kuwa hawapendi marubani ilhali yeye ni mmojawapo wa marubani. (1×2= 2*)*
*lazima maelezo yawe sahihi ndiposa mtahiniwa apate alama zote mbili. Moja ya kutaja na moja ya kueleza. Bila maelezo sahihi kwa jibu sahihi tuza 0*

**c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji. (Alama 6)**
**Sifa za Majoka**
- Ni Katili. Anawaua wapinzani wake. Anamwangamiza Jabali na chama chake cha Mwenge kwa kuhofia upinzani. Aidha, anapanga njama za uuaji wa Wanasagamoyo wengine, kama Tunu, Chopi na hata Sudi (uk 34).
- Mwepesi wa kushawishika. Anakubali bila kudadisi athari za ushauri mbovu wa Kenga kuwa wamwangamize Chopi. Aidha, anautumia ushauri wa Kenga wa kumnasa Ashua ili kulipa kisasi kwa Sudi aliyekataa kumchongea kinyago (uk 29).
- Ni mwingi wa tamaa. Ana tamaa kubwa ya mali. Ananyakua shamba la soko la Chapakazi ili aweze kujijengea hoteli kubwa ya kifahari. Ana mali mengi ikiwemo Majoka and Majoka Company, Majoka and Majoka Academy, Majoka and Majoka Mordern Resort na bado haridhiki.
- Ni mwenye uchu. Ana tamaa za kimwili. Anatamani kushiriki mapenzi na Ashua licha ya kuwa Ashua ameolewa naye mwenyewe ana mke (uk 29).
- Mwenye taasubi. Hawathamini wanawake. Anaamini kuwa mwanamke ni mwanamke tu. Anatishia kumchafua Husda.
- Ni fisadi. Ananyakua mashamba ya umma kwa manufaa yake mwenyewe. Anamgawia Kenga kipande cha shamba huko sokoni kwa kigezo kuwa anashirikiana vyema naye.
- Mkware/Mzinzi. Hamwamini mkewe tu. Anataka kushirikiana mapenzi na Ashua ambaye si mke wake wa ndoa (uk 28). (3×1= 3)

*Kila hoja ifafanuliwe ndiposa mtahiniwa atuzwe alama moja*

**Umuhimu wa Majoka**
- Ni kielelezo cha viongozi wabaya na katili wanaowanyanyasa wananchi.
- Ametumiwa kupigia darubini viongozi wa mataifa huru ya Afrika na jinsi wanavyowanyanyasa wananchi kwa kufuata uongozi mbaya wa vibaraka wao.
- Ni kiwakilishi cha viongozi wanaokengeuka pindi tu baada ya kupewa uongozi na wananchi ili kukidhi tama zao. (3×1= 3)

*Hoja za umuhimu ziwe na ulinganifu fulani na sifa*

**d) Fafanua jinsi wanaorejelewa na mzungumzaji walivyo laghai. (Alama 10)**
**Wanaoreewa ni viongozi.**
Viongozi hawa ni laghai kwani:
- Hawahifadhi mazingira. Maji machafu (uchafuzi wa mazingira) yalipita mtaroni na kueneza harufu mbaya kila mahali bila uongozi wa Sagamoyo kuliona hili kuwa tatizo (uk 2).

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Wanahatarisha maisha ya wananchi. Soko la Chapakazi limebadilishwa na kufanywa uwanja wa kumwagia kemikali (uk 2).
- Wanawadhulumu wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanahangaishwa na wanaosanya ushuru kwa kuwaitisha kitu kidogo na wengine kitu kikubwa (uk 2–3).
- Hawajali maendeleo ya kesho. Serikali kutangaza mwezi mzima wa kusherehekea uhuru bila watu kufanya kazi ilhali haijali watakachokula watu (uk 4).
- Hawana sera bora za maendeleo. Serikali ya Sagamoyo haina mipango maridhawa ya kimaendeleo. Majoka anamiliki kampuni kubwa ya sumu ya nyoka badala ya miradi muhimu (uk 4).
- Wanaruhusu na kuendeleza ufisadi. Kuna ufisadi unaomfanya Asiya kupata kandarasi ya uokaji keki ya uhuru kwa kujuana na Husda bali si kwa kufuzu na kufaulu (uk 7).
- Wanaendeleza udikteta. Utawala wa Sagamoyo ni wa kimabavu. Kenga anamlazimisha Sudi amchongee Majoka kinyago cha Ngao licha ya kujua kuwa uongozi wa Majoka ni wa udhalimu (uk 9).
- Wanatazama mambo nchini yakiendelea kuharibika. Kombe, mshiriki wa karibu wa Kenga anakiri kuwa mambo yameenda kombo Sagamoyo (uk 15).
- Hawajali maslahi ya wananchi. Uongozi unafunga soko la Chapakazi. Soko hili ndilo kitegauchumi pekee kwa Wanasagamoyo (uk 25).
- Wanawachochea wananchi kuandamana. Kuna maandamano ya mara kwa mara na yasiyotatuliwa katika jimbo la Sagamoyo, wanachi wanapigania haki zao.
- Wanaendeleza matumizi mabaya ya asasi za kijamii. Majoka anawatumia polisi wake vibaya ili kujidumisha uongozini. Polisi wanawanyanyasa na kuwadhulumu wananchi bila Majoka kujali.
- Wana ubinafsi mwingi. Sagamoyo kuna uongozi wa ubinafsi. Majoka anataka kuendeleza ubinafsishaji wa uongozi wa Sagamoyio kwa kumtangaza rasmi Ngao Junior kuwa mrithi wake (uk37).
- Wanaendeleza unyakuzi wa ardhi. Kuna unyakuzi wa mali ya umma. Majoka analifunga soko na kuinyakua sehemu hiyo ili ajenge hoteli ya kifahari (uk 45).

(10×1= 10)

*Kila hoja ifafanuliwe kikamilifu*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>SEHEMU YA B</u>**

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

(Assumpta K. Matei)

Jibu swali la ***Pili*** ama la ***Tatu***

**2. <u>“Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…”</u>**

**a) <u>Eleza muktadha wa maneno haya (alalama 4)</u>**

Haya ni maneno ya Kaizri. Anamwambia Ridhaa. Wapo katika Msitu wa Mamba. Ni baada ya kufurushwa kutoka Mlima wa Simba baada ya vita vya baada ya uchaguzi kuzuka. Anarejelea usawa kiasi uliokuwa ukionekana kuwepi pale kambini. (4×1= 4)

**b) <u>Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili (alama 2)</u>**

Kinaya- watu hawawi sawa ila kifoni (1×2= 2)

**c) <u>Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya (alama 6)</u>**

***Sifa za Kaizari.***

- Ni mwenye busara. Anaelewa kuwa hakuna usawa wakati wa kifo kati ya maskini na matajiri ikizingatiwa wanavyokufa na wanavyozikwa (uk 14- 15).
- Ni maskini. Matone mazito ya mvua yalianguka kwenye ngozi ya wanawe, Lime na Mwanaheri. Hana uwezo wa kuwasaidia. Hata tambara hana (uk 15- 16).
- Ni mcha Mungu. Anamshukuru Mungu kuwa wangali hai licha ya hali ngumu (uk 16).
- Mwenye huruma. Aliwahurumia vijana waliouwawa kwa risasi na polisi wa Penda Usugu Ujute (uk 24).
- Mzalendo. Aliihurumia nchi yake ambayo ilielekea kushindwa kuwashawishi watu wake kuelewa umuhimu wa usalama (uk 24- 24).
- Mwenye mapenzi ya dhati. Alijaribu sana kuwaokoa wanawe waliokuwa wakibakwa ila akashindwa (uk 25).
- Mwenye tahadhari. Siku za kwanza kambini hakuweza kutumia vyoo vya kupeperushwa (uk 29).
- Mshawishi. Aliwasihi wakimbizi wenzake kuchimba misala (long drop) (uk 29). (3×1= 3)

*Kila sifa ifafanuliwe. Sifa zisianze kwa vinyume kama: hana utu, si mwenye tahadhari n.k.*

***Umuhimu wa Kaizari***

- Anawakilisha watu wenye busara katika jamii.
- Ametumiwa kuonyesha matatizo wanayokumbana nayo wakimbizi.
- Anawakilisha athari zinazotokana na vita vya kikabila.
- Ametumiwa kuwajenga wahusika wengine kama Ridhaa. (3×1= 3)

**d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu (alama 8)**

- Sheria za kikoloni zilimpa mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao na umilikaji wa ardhi na Waafrika sehemu hizi kupigwa marufuku (uk 7).
- Hata katika kifo hamna usawa. Kuna wanaokufa wakipepewa na wauguzi katika zahanati za kijijini. Wengine hulala maumivu yao yakiwa yamefishwa ganzi kwenye hospitali za kifahari (uk 14).
- Pia kuna tofauti katika mitindo ya mazishi ya matajiri na maskini. Matajiri huvishwa mavazi ya kifahari tofauti na maskini (uk 15).
- Mwalimu aliwaambia kina Tila kuwa utawala huteuliwa maksudi kuendeleza mfumo uliopo wa kiuchumi kwa maslahi ya watawala na tabaka ambalo linazimiliki nyenzo za uzalishaji mali (uk 39).
- Bwana Kangata na jamii yake walilowea kwa shamaba la mwajiri wao ambaye alikuwa akiishi jijini (uk 64).
- Kimondo alimweleza Lunga kuwa kuishi kwao wanyonge kuliamuliwa na matajiri (uk 69).
- Waafrika wafanyakazi maskini walinyimwa matibabu kwa kukosa *Medical Scheme* kama alivyoeleza daktari mwafrika (uk 70).
- Baada ya wakimbizi kuishi katika Msitu wa Mamba kwa kipindi fulani, jamii ilianza kutwaa uchangamano wa mtu kutambua kuwa yeye alitokana na ukoo mtukufu na jirani yake alikopolewa na ukoo wa mlalaheri (uk 75).
- Katika wimbo wake, Shamsi anaeleza kuhusu matajiri wanaomchungulia na kumcheka wakiwa kwenye roshani zao wakipunga pepo baada ya kujaza matumbo yao (uk 130).
- Ridhaa alihamia mtaa wa Afueni. Mtaa wa watu wenye kima cha juu kiuchumi. Daraja kubwa limeutenga mtaa huu na mtaa wa Kazikeni, mtaa wa watu wenye maisha ya kubahatisha (uk 137- ***138).*** (8×1= 8)

Au

**3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:**

**(a) Hotuba (alama 10)**

Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya watu. Pia huitwa hutuba. Mwandishi wa riwaya hii ametumia hutuba kwa ustadi mkuu kupitisha ujumbe mbalimbali. Hotuba hizi ni:

1. *Hotuba ya Racheal Apondi kwa maafisa waliohudhuria warsha* kuhusu jukumu la vikosi vya askari katika
- kudumisha usalama, amani na maridhiano nchini (uk 112- 113). Katika hotuba hii, Racheal Apondi anasisitiza kuwa:
- Suala la usalama haliwezi tena kupuuzwa. Usalama umekuwa mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu.
- Anasema kuwa bila usalama, binadamu hawezi hata kushiriki katika shughuli za kuzalisha mali, hivyo hata mahitaji yake mengine ya kimsingi kama vile chakula, malazi na makazi hayawezi kukidhiwa.
- Kila binadamu ana jukumu la kudumisha amani na usalama.
- Wafanyakazi wa umma, hasa polisi na wanajeshi wana jukumu kubwa zaidi la kudumisha usalama na amani.
- Kila mmoja wetu anastahili kuhakikisha kuwa ameepuka vitendo vya kihalifu.
- Ni vyema mtu kuwaangaza wahalifu wakati wote.
- Vikosi vya polisi na wanajeshi vimefunzwa maarifa ya kukabiliana na kadhia za jinai na upelelezi.

(4×1= 4)

2. *Hotuba ya Lunga Kiriri- Kangata kwa walimu na wanafunzi* gwarideni (uk 68-69). Hotuba hii ilisisitiza
- umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Anasisitiza kuwa:
- Suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu.
- Misitu ilikuwa imevamiwa na viongozi wenye mate ya fisi.
- Baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali za umma wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kuwapoka makazi yao.
- Maelfu ya maekari ya misitu yamefyekwa na kujengwa viwanda.
- Badala ya mibambakofi na miti mingine inayosafisha hewa, michai imetwaa nafasi yake.
- Wanaohusika na matendo haya wanapoulizwa hudai kuwa michai si adui ya mazingira!
- Wengine wanasema kuwa misitu haina budi kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula, kwani jamii lazima ijitosheleze kwa chakula.
- La kuhuzunisha ni kwamba hawa hawa wanaosema hivyo ndio wanaokita majengo ya kifahari katika sehemu ambazo zinastahili kutengewa upanzi wa chakula!
- Wengine wamediriki kunyakua hata madhababu kwenye Mlima wa Nasibu ili kujenga hoteli kubwa za kitalii.
- Wazee wetu hata hawana mahali pa kuchomea kafara!
- Tunakata miti bila kupanda mingine.
- Hata mabustani ya maua tunashindwa kuyastawisha.
- Tukiendelea kuharibu mazingira sehemu yetu itazidi kuwa jangwa. (2×1= 2)

3. *Hotuba ya Umu katika hoteli ya Majaliwa*siku yake ya kuzaliwa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Umu anawashuku Mwangeka na Apondi kwa kuwa wazazi wake wema.
- Anawashukuru kwa kumsomesha.
- Anawashukuru kwa kumsaidia Dick kujiendeleza kimasomo.
- Mwangeka na Apondi wanamshukuru Umu kwa kuwapa furaha.
- Apondi anamshukuru kwa kumlea mdogo wao kwa maadili bora. (2×1= 2)

4. *Hotuba ya Dick katika hoteli ya Majaliwa* siku ya kuzaliwa kwa Umu.

- Dick anamshukuru Umu kwa msaada wake na ahadi ya kumlea.
- Anamkumbusha siku walipokutana katika uwanja wa ndege na ilivyokuwa muhimu kwake.
- Anamshukuru Umu kwa kumwelekeza kwa wazazi wao wale.
- Anawashukuru Apondi, Mwangeka na wanawe kwa ushauri wanaompa. (2×1= 2)

*Mtahiniwa ataje hotuba kisha aeleze masuala muhimu yanayoibuliwa na kila moja.*

**(b) <u>Uozo katika jamii (alama 10)</u>**

- Uozo ni hali ya kuzorota na kutozingatiwa tena kwa maadili mema katika jamii. Ni hali ambapo milazote na desturi njema huvurugwa na wanajamii wanaofanya mambo yaliyo kinyume nahali halisi ya maisha. Mwandishi amejadili suala hili kwa undani kama ifuatavyo;
- Jamii inaendeleza ubakaji. Genge la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini Lime na Mwanaheri na kuwabaka mbele ya baba yao (uk 25).
- Kuna ulanguzi wa dawa za kulevya. Dick alipotoroshwa na Sauna alipelekwa kwa tajiri mmoja aliyemwingiza katika kusafirisha dawa za kulevya kutoka nchi moja hadi nyingine (uk 119- 120).
- Wanajamii wanaendeleza uporaji na wizi wa mali. Vijana wanawavamia watu, kuwaua na kupora katika maduka ya kihindi, kiarabu na ya waafrika wenzao.
- Jamii inaendeleza ufuska/ ukahaba. Sauna aliiba watoto na kuwapeleka kwa mama mmoja aliyewatumia kwa biashara ya nipe nikupe (uk 84).
- Biashara haramu inaendelezwa. Bi. Kangara alifanya biashara ya kuwauza watoto na vijana- Safari yake ilipata mkondo mwingine baada ya polisi kupata fununu kuhusu njama ambazo yeye na Bi. Kangara walikuwa wakiendesha. Mabibi hawa walikuwa na mtandao ambao kazi yake ilikuwa kuwauza watoto na vijana (uk 84).
- Kuna tatizo la mimba za mapema. Vijana wana mazoea ya kukumbatia mtafaruku wa kuhisia unaowapata na mara hujipata wameambulia ujauzito kama alivyofanya Zohali (uk 98).
- Baadhi ya wanajamii wanaendeleza uavyaji mimba. Sauna alijaribu awezavyo kuavya mimba na mwishowe, baada ya kushindwa, anaamua kujiua.
- Kukiuka maadili ya kikazi. Fumba (mwalimu) anakiuka maadili ya kazi na kujihusisha kwa mapenzi na mwanafunzi wake, Rehema, na hatimaye kumpachika ujauzito (uk 102).
- Wazazi wanawabaka wana wao. Babake Sauna anafanya mapenzi na mwanawe kila apatapo nafasi, na mwishowe, Sauna anapata mimba.
- Starehe na anasa kwa vijana. Vijana wa vyuo vikuu wameshindwa kutofautisha usiku na mchana. Tindi anasahau kumrejesha Lemi nyumbani kutokana na muziki (uk 121).
- Wazazi wanakwepa malezi na kuwatupa wanao wakiwa wachanga. Neema anampeleka mtoto aliyemwokota kwa polisi (uk 162).
- Vijana kuwaiga wazee. Mwangemi na Mwangeka walikuwa na tabia mbovu ya kumuiga babu yao (uk 186). (10×1= 10)

*Mtahiniwa afafanue kwa mifano kutoka katika riwaya.*

**<u>SEHEMU YA C</u>**

**HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

(AlifaChokocho na Dumu Kayanda- Wahariri)

Jibuswali la ***Nne*** ama la ***Tano***

**NDOTO YA MASHAKA**

4. **<u>“Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi.”</u>**

**(a) <u>Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)</u>**

Haya ni mawazo ya Mashaka. Yuko chumbani mwake. Anakumbuka hali yake ngumu ya maisha na mashaka tele. Anamkumbuke mkewe, Waridi, alivyomtoroka na wanawe. Anayaona maisha kutokuwa na thamani tena kiasi kwamba anaona kifo kingemfaa. (4×1= 4)

**(b) <u>Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hii (alama 4)</u>**

Takriri- nimechoka

Uzungumzi nafsi- sasa nimechoka… (2×2= 4)



for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**(c) <u>Mzungumzaji alikuwa na haki ya kuradua kufa. Thibitisha (alama 12)</u>**

***Mashaka alikuwa na haki ya kuradua kufa kwani alikuwa amepitia matizo mengi:***

– Mamake mzazi, Ma Mtumwa, aliiaga dunia punde tu baada ya kumkopoa.
– Baada ya kifo cha mamake, babake alishindwa kuvumilia naye akaaga dunia.
– Mashaka alilelewa na Biti Kidebe asiyekuwa mamake mzazi.
– Mamake mlezi, Biti Kidebe naye alihitaji kulelewa. Daima alilalamikia miguu yake.
– Mashaka alilazimika kufanya vijikazi ili kumsaidia mamake mlezi kupata chohcote cha kutumia.
– Mashaka na Biti Kidebe walipanda mabokoboko ambayo wengi waliamini si ndizi.
– Biti Kideba aliendа jongomeo pindi tu Mashaka alipomaliza chumba cha nane.
– Mzee Rubeya na Shehe Mwinyimvua wanawafungisha Mashaka na Waridi Ndoa ya Mkeka bila kupenda kwao.
– Mzee Rubeya wanawakimbia Mashaka na Waridi na kurudi kwao Yemeni ili Mashaka wasije kuwaaibisha.
– Kazi ya Mashaka ilikuwa ya kijungu meko- ya kupigania tumbo.
– Mashaka na Waridi waliishi sehemu kuchafu kule Tandale, Kwatumbo, eneo la Uswahilini.
– Walikosa vyoo wakawa wanatumia karatasi kwa haja zao zote.
– Mashaka na Waridi walipata watoto wengi, saba, ambao wanawashinda kuwakimu.
– Mashaka alilazimika kuomba jikoni kwa jirana yake, Chakupewa, ili wanawe wa kiume wapate mahali pa kulala.
– Chumba chao kiliingiza maji mvua iliponyesha.
– Mashaka alifanya kazi ya usiku katika Shirika la Zuia Wizi Security (ZWS).
– Waridi anamtoroka Mashaka maisha yanapokuwa magumu. (12×1= 12)

*Kila hoja ifafanuliwe kikamilifu*

*Au*

**5. <u>Ukirejelea hadithi zozote nne katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, eleza jinsi maudhui ya Mapenzi na ndoa yanavyojitokeza (alama 20)</u>**

**<u>Masharti ya Kisasa</u>**

*Ndoa ya Dadi na Kidawa*

– Ndoa imedhibitiwa na masharti.
– Kuna kugawana majukumu katika ndoa.
– Ndoa zinazingatia mno kupanga uzazi.
– Ndoa inaruhusu mwanamke kufanya kazi. Kidawa alikuwa Metroni.
– Baadhi ya watu huingilia ndoa za wenzao ili kuvunja mapenzi ya wanandoa. (5×1= 5)

**<u>Mapenzi ya Kifaaurongo</u>**

– Ndoa iliyotarajiwa kati ya Dennis na Penina ilijaa unafiki. Penina anamfukuza Dannis kwa kukosa kazi.
– Ndoa imetawaliwa na kuhimiliana.
– Ndoa imejaa kukata tamaa. Penina anamfukuza Dennis baada ya kukosa kazi.
– Ndoa imezingirwa na utabaka.
– Mepenzi humea, hukua, huugua na kufa baadaye. (5×1= 5)

**<u>Ndoto ya Mashaka</u>**

– *Ndoa ya Mashaka na Waridi*
– *Ndoa ya Mtumwa na Mzee Rubeya*
– Ndoa ni ya kulazimishwa- Mashaka na Waridi
– Utabaka umetawala ndoa- Waridi ni wa tabaka la juu
– Ndoa inakumbwa a tatizo la malezi bora.
– Kuna mateso na kutengana kwa wanandoa.
– Ndoa zinakumbwa na matatizo mengi.
– Ndoa za mapema ni chanzo cha aibu. (5×1= 5)

**<u>Mtihani wa Maisha</u>**

– Wazazi wa Samueli wanampenda sana mwanao. Wanampeleka shuleni ili apate elimu.
– Samueli anampenda sana Nina.
– Nina anamwamina sana Samweli na kuamini kuwa ni bingwa.
– Mamake Samueli anampenda sana mwanawe. Anamtaka asijiue.
– Ndoa humwitaji mwanamke kumheshimu mumewe.
– Motto wa kike anachukuliwa kuwa si bora kama alivyo wa kiume. Babake Samueli aliamini kuwa motto wa kike akiolewa mambo yake huwa yameisha. (5×1= 5)

*Mtahiniwa asirudie hoja moja katika hadithi zaidi ya moja. Kila hoja ifafanuliwe kikamilifu.*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA D**
**USHAIRI**
***Jibu swali la sita ama la saba***
***6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

**MASWALI**
a) **Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)**
Naogopa (1×1= 1)
b) **Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 1)**

Mtunzi alidhamiria kuonesha baadhi ya matatizo wanayoyapitia wanawake baada ya kufunga ndoa. (1×1= 1)
c) **Nani nafsi nenewa katika shairi hili? (Alama 1)**
Nafsi nenewa ni mwanamume (mzee) anayetaka kufunga ndoa. (1×1= 1)
d) **Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili (Alama 2)**
Takriri- naogopa
Tashbi- wanauma ja panya
Msemo- wanauma ja panya wakipulizia
Taswira- naogopa nawe **babu** kusimama (2×1= 2)
e) **Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga (Alama 2)**
Tabdila- mie- mimi
Inkisari- kwita- kuita
Kikale- mtima- moyo
Kufinyanga sarufi- matusi anipatie- anipatie matusi (2×1= 2)
f) **Weka shairi hili katika bahari mbalimbali (Alama 3)**
Ukawafi- lina vipande vitatu katika kila mshororo
Kikwamba (zivindo)- neno 'naogopa' linarudiwa mwanzoni mwa kila mshororo.
Mtiririko- vina vya ndni na vya nje vinafanana kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. (3×1= 3)
g) **Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)**
Naogopa uchungu utakaoniuma ili nikuzalie mwana. Naogopa kupigwa kama ngoma ndiposa nitulie. Naogopa kuchunguzwa ndipo unipe pesa. Naogopa kuwa nitaitwa mwizi wa sima ilhali nakuandalia. (4×1= 4)
h) **Kwa nini nafsi neni anasita kuchukua hatua? (alama 4)**
Hataki alie
Anaogopa wanaume kwani wanauma kama panya.
Anaogopa kuita mama ya mumewe mama naye amkaripie
Anaogopa dhuluma za wanaume
Anaogopa kushinda ameinama goti mume ampigie
Anaogopa mkemwenza amhujumu na kumtusi.
Anaogopa uchungu wa kujifungua.
Anaogopa kupigwa kama ngoma.
Anaogopa kusomwa kabla ya kupewa pesa.
Anaogopa kuitwa mwizi wa sima anayoandaa.
Anaogopa udaku wa dada za mume.
Anaogopa uhasama wa kupiganiwa
Anaogopa kushindania mali kortini
Anaogopa kufichua siri za kina bwana.
Anaogopa ndoto zake kuzizima na doa ajitie
Anaogopa kuizima taa yake (8× ½ = 4)
i) **Vifungu vifuatavyo vina maana gani katika shairi? (alama 2)**
i) Taa yangu kuizima- kupoteza matarajio/ malengo yake
ii) Dhuluma- mateso (2×1= 2)
***Au***
7. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali
**Maswali**
(a) **Hili ni shairi la aina gani ? Thibitisha (alama 2)**
Shairi huru- Halijazingatia kanunu zote za utunzi wa mashairi wa kuzingatia arudhi (2×2= 2)

(b) **Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ? (alama 2)**
Anayeimba ni mjomba

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Anayeimbiwa ni mpwawe (2×1= 2)

**(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume (alama 2)**

Anaambiwa uoga ukimtikisa huenda ni wa akina mamaye
Alichinjiwa fahali ili awe mwanamume (2×1= 2)

(d) **Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (alama 4)**

Chuku – wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo
Takriri – kikali
Isitiari – upweke ni uvundo
Tashhisi – uoga ukifikia (2×2= 4)

**(e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (alama 2)**

Wakulima – Atapewa shamba la mahindi
Wafugaji – Atapewa mbuzi (2×1= 1)

**(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili (alama 4)**

Tabdila – aamushwe – aamshwe
Inkisari – Mme – mwanamume
Kuboronga sarufi – Fahali tulichinja- tulichinja fahali (2×2= 4)

(g) **Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili ?(alama 4**)

i) Mbari- ukoo
ii) Msununu- anayenuna
iii) Ngariba- mtahirishaji
iv) Uvundo- harufu mbaya (4×1= 4)

**SEHEMU YA E**

**FASIHI SIMULIZI**

***(Kutoka: Assumpta K. Matei- FaniyaFasihiSimulizi, uk 145)***

Maswali

**(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 2)**

Maapizo- miungu na wakuone/ laana wakumiminie (1×2= 2)
*Kutaja al 1- kufafanua al 1*

**(b) Jinsia ya nafsi neni ni gani? (alama 2)**

Mwanamke/ jinsia ya kike- ndimi nilompa uhai mwana unoringia (1×2= 2)
*Kutaja al 1- kufafanua al 1*

**(c) Eleza sifa zozote sita za kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 6)**

– Maapizo yalitolewa kwa watu ambao walienda kinyume na maagizo ya jamii zao; wabakaji, waliowatusi wazazi wazee na wengineo.
– Katika baadhi ya jamii za Kiafrika, maapizo yalitolewa kabla ya ulaji wa kiapo.
– Maapizo yanaweza kutolewa moja kwa moja na yule aliyeathirika.
– Kidini, Mungu, miungu au mizimu huweza kutoa maapizo kuhusu mustakali wa mtu fulani.
– Maapizo huaminiwa kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema.
– Maapizo hutumia lugha fasaha. Lugha ya ulumbi.
– Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidi ya maovu. (6×1= 6)

**(d) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii (alama 4)**

– Hutumiwa kama nyenzo ya kuwaonya wanajamii dhidi ya matendo hasi.
– Hutambulisha jamii. Kila jamii ina namna yake ya kuapiza.
– Hukuza umoja katika jamii. Kuwapo kwa kaida na miiko sawa huwafanya watu kujihisi kuwa kitu kimoja.
– Huadilisha. Wanajamii hujifunza kutenda mema ili kuepuka laana. (4×1= 4)

*Mtahiniwa afafanue hoja zake ili zilingane na kipera cha maapizo.*

**(e) Fafanua njia sita jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi (alama 6)**

– Wanafunzi hukariri, hughani na kuimba mashairi katika tamasha za muziki.
– Mawaidha na vipera vingine vya fasihi simulizi hupitishwa katika sherehe za harusi, jando, mazishi na matambiko.
– Utegaji na uteguaji vitendawili kupitia redio na runinga.
– Michezo ya kuigiza katika runinga na redio.
– Sarakasi zinazofanywa na wasanii huhifadhi kipera cha vichekesho.
– Watafiti wanatafiti na kuhifadhi kwa kurekodi au kuandika vipera vya fasihi simulizi.
– Utambaji wa hadithi bado hufanyika katika baadhi ya jamii, hasa katika sehemu za mashambani.

(6×1= 6)

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/1**
**KISWAHILI (INSHA)**
**NOV/ DEC 2020**
**KARATASI YA KWANZA**

1. Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa kuchunguza chanzo cha ukosefu wa usalama nchini. Andika ripoti mliyowasilisha.

2 Jadili njia za kupunguza utovu wa nidhamu miongoni mwa vijana.

3 Andika insha itakayoafikiana na methali. 'Baniani mbaya kiatu chake dawa'

4 Endeleza kisa kifuatacho

Mambo yalianza kama mzaha...

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Watu wengine hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari. Wanatumia sukari kwa hamu na ghamu bila kutambua kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule waungwana kutengenezea vitu kama keki, mahamri, vitumbua na kadhalika na akina yahe hawangeweza kuigharamia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotayarishwa viwandani sasa haina virutubishi vyovyote . Halikadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini. Umuhimu wa sukari wakausaza kwa kutia ladha tamu tu. Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masalio ya asidi mwilini yenye sumu inayoathiri siha.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya meno kuuma. Pili, sukari nyeupe imehusishwa na ongezeko la maradhi ya kisukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi holela ya sukari huleta kipandauso au ugonjwa wa gahfla wa kuumwa upande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pia ,sukari huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kemikali iitwayo kolestroli, ambayo ni ufuta unaonata na ambao unatokana na kutoyeyuka kwa mafuta yote mwilini. Kemikali hii ya kolestroli inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa myembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda moyo ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa sukari, ingawa ni tamu, ni sumu mwilini. Wataalamu wa lishe wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia.

Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi kwa mwili wa mwanadamu.
Asali huwa na sukari asilia,vitamini, madini na amino asidi. Hivi vyote huwa na manufaa mbalimbali mwilini. Mathalani, asali huupa mwili nishati inayohitajika kuendesha shughuli za viungo.Licha ya hayo, asali huuchangamsha mwili.Asali huwa na kemikali ambazo husaidia watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango

cha himoglobini, hivyo kupunguza uwezekano wa watoto kuwa na anemia ( upungufu wa damu ) . Halikadhalika, asali husaidia katika usagaji wa chakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya magonjwa ya kukohoa.Asali husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani. Asali pia inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii, hutunza ngozi na kuifanya ing'are, huondoa vipele na ugumu wa ngozi ,pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika . Halikadhalika, asali hutibu vidonda. Viwanda vingi vya vipodozi vilevile hutumia asali kama malighafi muhimu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

**MASWALI**

a) Kutokana na taarifa hii, kwa nini wazee wa zamani waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko watu wa siku hizi? (alama 1)

b) Taja matumizi **mawili** ya sukari nyeupe. (alama 2)

c) Onyesha madhara **matatu** ya sukari nyeupe mwilini. (alama 3)

d) Taja aina ya sukari iliyo na manufaa mwilini mwa mwanadamu au ueleze ni kwa nini. (alama 2)

e) Eleza manufaa ya asali: (alama 2)

i) Ndani ya mwili

ii) Nje ya mwili

f) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa: (alama 4)

i) Hamu na ghamu………………………………………………………….………

ii) Akina yahe.………………………………………………………………….

iii) Sugu………………………………………………………………………..…

iv) Vipodozi:……………………………………………………………………

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA B: UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana hukopa msamiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa.Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile ‘shule’ ulikopwa na kutoholewa kutokana na neno *schule*. Msamiati kama vile *‘leso’, ‘karata’ na ‘mvinyo’* yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina ‘balozi’ na ‘bahasha’ yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha hazuka.Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaba yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasibisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindio yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo sahili wa lugha ili kufanikisha mawasiliano. **Pijini** ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.

Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo.Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo ianyopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani,

kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku lugha nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia au zitakufa na kusahaulika kabisa.

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu. **(Maneno 50) (alama 6, 2 za mtiririko)**.
   **MATAYARISHO**
   **JIBU**

2. Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani? **(Maneno 30)**

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) i) Eleza dhana ya kiambishi (alama 1)
   ii) Ainisha viambishi na utoe mifano (alama 2)
b) Taja vitamko vyenye sifa zifuatazo: (alama 2)
   i) Vokali ya nyuma, juu
   ii) Nazali ghuna cha mdomo
c) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili. (alama 2)
d) Tunga sentensi ya masharti yasiyowezekana. (alama 2)
e) i) Taja sifa mbili za nomino za pekee. (alama 2)
   ii) Dhihirisha nomino ya pekee katika sentensi. (alama 1)
f) Ainisha kiunganishi katika sentensi hii. (alama 2)
   Japo Kiptoo ni dereva hodari, hana leseni ya kuendesha gari
g) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili tofauti za neno 'bana' (alama 2)
h) Fuata maagizo kwenye mabano. (alama 2)
   Tafadhali hakikisha Jane ameelimika vizuri (andika katika kauli ya kutendesha)
i) Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)
   "Kamau alimkimbilia Chati"
j) 'Kwa' imetumika vipi katika sentensi zifuatazo? (alama 2)
   i) Tumealikwa kwa Chebet.
   ii) Alipata alama ishirini kwa mia.
k) Tunga sentensi kubainisha muundo ufuatao. (alama 2)
   KN(W+V)+KT(T+E)
l) Andika kwa ukubwa wingi. (alama 2)
   Mwizi aliiba nguo na kiti
m) i) Tofautisha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo. (alama 2)
   ii) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi moja. (alama 2)
n) Tunga sentensi ukitumia kirejeshi 'O' kuonyesha uzoefu. (alama 2)
o) Eleza matumizi ya kiambishi /ji/ (alama 1)
   Alijikata mguu.
p) Andika sentensi ifuatayo katika hali isiyodhihirika. (alama 1)
   Kibofu hupaa angani.
q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
   "Kwa nini unampiga ndugu yako? Nyanya alimuuliza.
r) Pambanua kwa kielezo cha matawi. (alama 4)
   Mkufunzi hodari amepita mtihani rahisi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII**

a) Eleza mambo matano yaliyochangia maendeleo ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano nchini Kenya kabla ya Uhuru. (alama 5)
b) Kwa nini watu huchanganya msimbo wanapozungumza. Toa hoja tano. (alama 5)

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi 3**
**Nov/Dec 2020**

**Swali la lazima**
**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**1.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Hivi leo nimesonya, swali ninaulizia
Kila tunapowakanya,ndivyo mnakimbilia
Tangia tumewaonya,mmegoma kusikia
Mwataka tufanye nini,muache kuvuta bangi.

**Wosia** mewatolea,**nudhumu** tukatungani
Mikutano kuandaa,yote tukajadilini
Shere mnatuchezea,mwajificha vichakani
Mwataka tufanye nini ,muache kuvuta bangi

Mwatwambia hamvuti,kumbe mnatuhadaa,
Mwatwambia hamvuti, na macho mmekodoa
Mwatwambia hamvuti,na harufu mnatoa
Mwatakatu fanye nini ,muache kuvuta bangi

Hamwezi kutufichani,sisi tunawatambua,
Hata nywele hamchani,kama dengu zimekaa
Mnakaa kama nyani,darasa mmezubaa
Mwataka tufanye nini ,muache kuvuta bangi,

Kisha vuta hiyo ngwai,mwasumbua wasichana
Ati mmepata rai,mistari kwa ngushia
Mnaanza kujidai,jinsi mlivyokomaa
Mwataka tufanye nini,muache kuvuta bangi.

Mabinti na nyinyi pia,leo nimeshawapata
Mbona mnapendelea,machali wanaovuta!
Ni moshi wawavutia, bangi wakishaivuta
Mwataka tufanye nini,muache kuvuta bangi.

Wone walotangulia,jinsi walivyochakaa
Dawa zimewatibua,vichaa wamesalia
Meshindwa kujitambua,pakubwa **wamesinyaa**
Mwataka tufanye nini,muache kuvuta bangi.

Nambieni kazi gani,ambayo imetangazwa
Hata kwenye gazetini,ambayo imeelezwa
Ati  ili ufanyeni, bangi imependekezwa
Mwataka tufanye nini ,muache kuvuta bangi.

Kadi tamati natia,jibu ninalingojea
Nawaombea Jalia, laana kuiondoa
Aje kuwaghofiria,motoni sijeingia
Mwataka tufanyenini ,muache kuvuta bangi.*(Utunzi wa kabiduka)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

1) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama1)
2) Taja nafsi neni na nafsi nenewa (alama 2)
3) Ni nini kinachomkera malenga kwa mujibu wa ubeti wa kwanza (alama1)
4) Ni nini athari za bangi kwa mujibu wa mshairi huyu (alama3)
5) Liweke shairi hili katika bahari mbili kwa kuzingatia:
   i) Idadi ya vipande ii) Vina (alama 2)
6) Eleza umbo la shairi hili . (alama1
7) Andika ubeti wa pili kutoka mwisho kwa lugha ya nathari. (alama 3)
8) Toa mifano ya uhuru wa kishairi iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)
9) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili (alama 3)
   i) Wosia
   ii) nudhumu
   iii) wamesinyaa

**SEHEMU YA B :TAMTHILIA KIGOGO**

1 Utawala wa Majoka ni Sumu ya nyoka fafanua kwa kutolea mifano mwafaka katika Tamthilia(alama 20)

**AU**

2 Fafanua mbinu alizozitumia Majoka ili kubakia mamlakani. (alama 20)

**SEHEMU YA C: FASIHI SIMULIZI**

1. "Mwanangu nakuona unakua vyema kila uchao.Najua hivi karibuni utaanza kutafuta jiko,hakikisha unajiamini,piga moyo konde katika kukumbatia tamu na shubiri ya maisha ya ndoa.Hakuna binadamu aliye kamilika kama Mungu hivyo usitarajie mke aliyekamilika kwani ni binadamu si Mungu''

**Maswali**

a) Tambua kipera cha fasihi simulizi kinachohusishwa na kifungu hiki . (alama 2)
b) Taja sifa za kipera hiki. (alama 8)
c) Taja umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 8)
d) Matumizi ya kipera hiki huwa na lengo gani katika maisha ya kila siku katika jamii? (alama 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA**
**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda:**
**Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine**
**Jibu swali la 1 au la 2.**

1. i) Sekta ya elimu inachangamoto nyingi.Thibitisha kwa kurejelea hadithi zifuatazo : (alama 20)
   a) Mapenzi ya Kifaurongo
   b) Shogake dada ana Ndevu
   c) Mwalimu Mstaafu
   d) Mtihani wa maisha

**au**

2) '' Hakikubakia hata chakula kidogo cha sadaka ya mwenye njaa… ''
i) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja kumi ukirejelea hadithi yaTumbo Lisiloshiba (alama 10)

ii) Jadili uhalisia wa hadithi yaTumbo Lisiloshiba katika jamii ya leo kwa kutoa hoja kumi . (alama 10)

**SEHEMU E: RIWAYA CHOZI LA HERI**

1. Eleza masaibu yanayowakabili watu wasiokuwa "wenyeji" katika Riwaya ya Chozi la Heri

AU

2. Fafanua migogoro inayojitokeza katika Chozi la Heri (alama 20)

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/1**
**KISWAHILI (INSHA)**
**Mwongozo wa insha**

1. **Swali la Lazima**
   Sura

- Anwani – Herufi kubwa
- Utangulizi
- Njia za utafiti
- Matokeo – Angaahojatano.
- Mapendekezo – Yaoanena matokeo / matatizo.
- Hitimisho
- Jina
- Cheo
- Sahihi

**Majibu / Hoja**

a. Ukosefu wakazi kwa vijana.
b. Idadi chache ya maafisa wa usalama.
c. Matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana.
d. Ufisadi
e. Utepetevu wa uongozi.
f. Ukosefu wa motisha kwa walinda usalama.
g. Vifaa / zanaa duniza usalama.
h. Teknolojia – mtandao.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**2 Swali la pili.**
1. kufungwa jela.
2. kutozwa faini.
3. ushauri na saha
4. sheria kali dhidi ya wale wanao wahusisha vijana katika ukiukaji wamaa dili - panografia.
5. kuwajibika kwa wazazi - malezi bora.
6. dini – kutoa ushauri.
7. kuandaa warshana kuhamasisha vijana katika shughuli zinazokuza maadili.
8. Tamaduni – kuhifadhi tamaduni zinazo unga maadili.
9. Kupunguza umaskini unaochochea vijana kukosa vitu vya.
   Kimsingi na kujiingiza kwenye maovu.
10. Wakubwa kwa mifano bora miongoni mwa vijana.
12. Walimu kusisitiza nidhamu miongoni mwa vijana.
13. kudhibiti uhuru usiona mipaka-matumizi ya simu n.k.
    Tanahahi
    Mtahini wa lazima ataje visa vya utovu wa maadili na kuoanisha hoja yake na suluhisha lenyewe. Asipofanya vile asituzwe zaidi ya C. maki 8.

3. **Baniani mbaya kiatu chake dawa.**
- Hii ni inshayamethali.
- Maana kiatu cha baniani ni kitu au kundi la watu linalo chukia / kudharau kitu.
- Dawa:Kitu husika huenda kikawa ndicho jibu au jawabu suluhisho kwa tatizo fulani maishani mwa mtu katika jamii.
- Mtahini waaandike kisa kuthibitisha matumizi haya ya methali.
- Mtahini waazingatie pande zote mbili.
- Methali nyingine yenye maana sawa ni

Matikiti na malango ndio maponyanjaa.

**Utunzaji**

- Pande zote za methali zishughulikiwe.
- Anayeshughulikia upande mmoja asipite alama ya C /08/20
- Anayekosa kulenga katika kisa chake kimaudhui – apate alama D/03/20.

**Insha ya kuanzia**

- Kisa kioanena mwanzo uliotolewa.
- Mtahiniwa asiongeze maneno
- Kisa kiwe cha kuvutia na liwe ni tukio la kusikitisha.

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/2**
**KISWAHILI (INSHA)**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Wazee hao hawa kutumia sukari nyeupe, kwa hivyo hawa kujiongezea sumu mwilini au waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. (yoyote 1 x 1 = alama 1)

(b) (i) Hutumika katika vinywaji kama uji na chai.
(ii) Hutumika kupika vyakula kama keki au mahamri. (1 x 2 = alama 2)

(c) (i) Huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya menokuuma.
(ii) Husababisha maradhi ya kisukari, moyo na hipoglisimia.
(iii) Huleta maradhi ya ngozi, figo na ongezeko la kolestroli, ambayo nikemikali Hatari mwilini.

(iv) Huleta kipanda uso; ugonjwa wa ghafla wa kuumwa na kichwa upande mmoja.
(zozote 3x1 = alama 3)

(d) Sukari yenye manufaa ni ya asili aitokanayonavyakulakamanafaka, matunda, mboga na miwa na asali kwa sababu huwana virutubishi (vimejaa sukari asilia) (1 x 2 = alama 2)

(e) (i) Ndani ya mwili
- Huupa mwili vitamini, madinina amino asidi.
- Huupa mwili nishati.
- Huchangamsha mwili/husaidia usagaji wachakula /husaidia mwili kujikinga na maradhi kama homa/huzidisha kiwango cha himoglobini na kupunguza uwezekano wa watoto wadogo kupata anemia / husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani. (1 x 2 = alama 2)

(ii) Nje ya mwili
- Hufanya ngozikung'ara/huondoa vipele na ugumu wa ngozi/ hutibu kule ngozi imekatikakatika / navidondavilivyotokananakuchomeka(kujipaka kutibu vidonda).
(yoyote 1 x 1 = alama 1)

(f) (i) Hamu na ghamu – Kutarajia ukiwa na tama kubwa, shauku, uchu.
(ii) Akinayahe – Watu wa kawaida, watu wa tabaka la chini, maskini, fukara, Wakata walahoi.
(iii) Sugu – ngumu
(iv) Vipodozi – vitu au bidhaa za kurembesha k.m. mafuta na poda.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1. MAJIBU YA UFUPISHO**

(a) Hoja za kuzingatia

- Mita gusano ya kijamii hufanya lugha kuathiriana.
- Ukopaji wa vipengele vya lugha ni moja ya athari hizo.
- Msamiati hukopwa ili kueleza dhanangeni.
- Lugha zote hukopa.
- Kiingereza kimekopa kutoka kilatini, kifansana Kiswahili.
- Kiswahili nacho kimekopa kutoka kiingereza, kiarabu, kireno, kituruki na kijerumani.

(b) Hoja za kuzingatia

- Kuzuka kwa hali ya uwingi – lugha.
- Ukuaji wa lugha.

- Kuzuka kwa lugha mpya.
- Kudunishwa kwa lugha.
- Kufa kwa lugha.

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a)

i) Ni sehemu ya neon ambayo huambatanishwa kwenye mzizi wa neon ili kulipa neno maana mbalimbali
Ni silabi ambazo huambiswa kwenye mzizi wa neon ili kulikamilisha ki maana 1 x 1 = alama 1

ii) Viambishi√ awali√ hutokea kabla ya mzizi
Mfano :alimpiga

Viambishi√ tamati hutokea baada ya mzizi
Mfano: alituchezea

Kutaja – ½ mfano – ½
Hoja 2 x 1 = alama 2

b)

i) /i/ alama 1
ii) /m/ alama 1

c) Sentensi sahihi
Ni sentensi iliyo na wazo moja kuu/ maana iliyo kamili
Ni sentensi yenye kitenzi kimoja halisi
Ni sentensi inayojitosheleza kimuundo – inakiimana kitenzi
Mfano: Mtoto analia
Walitutembelea
Wageni walifika asubuhi
Maana alama – 1
Mfanowasentensi – alama 1

d) Sentensi ya masharti yasiyowezekana
Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani.
Alama 2

e)

i) Sifa za nomino pekee
Huanza kwa herufi kubwa hati katikati ya sentensi.
Hutaja majina ya vitu maalum au halisi kama vile watu, mahali, vyeo, n.k
Hojazote 2 x 1 = alama 2

ii) Nomino ya pekee katika sentensi
Mama alimuita Hasani kwa sauti.
Yeye ni Waziri Mkuu nchini Kenya.
Atunge sentensi moja alama 1

f) Kuainisha kiunganishi
Japo – cha kuonyesha kinyume alama 2

g) Sentensi moja kuonyesha maana mbili za 'bana'

h) Tafadhali elimisha Jane vizuri. alama 2

i) Maana mbili: (i) Alienda ili aone chati
(ii) Alitoroka alipoona chati alama 2

j) Maana mbili za 'kwa'
Kuonyesha mahali alama 1
Kuonyesha akisami/ sehemuya alama 1

k) Sentensi kuonyesha muundo ufuatao
KN (W + V) + KT (T + E)
Wale√ wawili √wanaimba√ vizuri√
Atunge sentensi 4 x ½ = alama 2

l) Ukubwawingi
Majizi√ yaliiba√ maguo√ namajiti√
4 x ½ = alama 2

m) Tofautisha
Shamirisho kipozi– nomino inayotendwa

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

– Nomino inayopokea kitendo moja kwa moja kutoka kwa kiima
  Shamirisho kitondo - nominoinayotendewa
– Nomino ambayo haipokei kitendo moja kwa moja kutoka
  Kwa kiima alama 2


n) Kirejeshi 'o' cha uzoefu
  Waumini waimbao kanisani ni hawa.
  Mtoto aliaye ni huyu. alama 2

o) Matumiziya /ji/
  Alijikatamguu - kirejeshi cha nafsi ya tatu(umoja) (yeye)
– Kirejeshi cha ngeli (umoja) alama 1

p) Haliisi yodhihirika
  Kibofu chapa ambinguni

q) Usemi wa taarifa
  Nyanya alitaka kujua kilichosababisha ampige ndugu yake. alama 2

r) Kupambanua kwa matawi
  Mkufunzi hodari amepita mtihani rahisi.




## ISIMU JAMII (alama 10)

a) Yaliyochangia maendeleo ya Kiswahili kabla ya uhuru
– Biashara – Kiswahili kilifanywa lugha ya biashara kati ya pwaninabara.
– Dini - Kiswahili kilitumiwa kusambaza uislamu na ukristo.
– Siasa - Wapiganiaji uhuru walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.
– Elimu - Kiswahili kilitumiwa na wamisheni kufundisha na kuandika.
– Vyombo vya habari – magazeti mengi ya Kiswahili yalizukanya kati za mkoloni.
– Vita vikuuuvya kwanza na vya pili vya dunia vilichangia kueneza Kiswahili.
  Kilitumiwa kama lugha ya mawasiliano.
  Zozote 5 x 1 = alama 5

b) Sababu za watu kuchanganya msimbo wanapozungumza.
– Athari za lugha zote
– Kukosa msamiati wa kutumia
– Upungufu wa kimsamiati katika lugha moja
– Kuficha ujumbe
– Kutaka kuonyesha ujuzi katika lugha nyingi
– Kutaka kushirikisha watu katika mazungumzo
– Mazoea
– Mtu anapokuwa na hasira, mshtuko, furaha, n.k
  Zozote 5 x 1 = alama 5

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA GARISSA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi 3**
**Mwongozo wa kusahihisha Fasihi**

**1) Ushairi**

1 Uvutaji bangi,mwataka tufanye nini mwache kuvuta bangi,athari zabangi(kichwa chochote mwafaka kisizidi maneno sita)yoyote 1x1

2 Nafsi neni-mshauri,mwalimu (1x1)
nafsi nenewa –wanafunzi,wavulana,vijana ( 1x1)

3 Kila wanapokanywa ndivyo wanavyozidi kutumia bangi (1x1)

4 Kusumbua wasichana, -Kuchakaa -Kuwavichaa -Kuzubaa darasani-Kusinyaa,kuzorota afya (zozote 3x1)

5 i) Idadi ya vipande mathnawikwasababulina vipande viwili katika kila mshororo (1x1)
ii) Vinaukaraguni –kila ubeti una vina vinavyo tofautiana na ubeti mwingine 1x1 (alama 2)

6 Lina beti tisa
– Kila ubeti una mishororo minnne
– Lina vipande viwili kwa kila mshororo
– Lina kibwagizo
– Mizani kumi na sita kwa kila mshororo (zozote 3x1)

7 Mshairi anataka aambiwe ni kazi gani ambayo imewahi kutangaazwa hata kwenye gazeti inayohitaji watu nao vuta bangi ili wafuzu kuifanya au kuajiriwa,anauliza watafanya kitu gani ili wavuta bangi waache kuvuta\
. ( Alama 3)

8 Kubananga/kuborongasa rufi vichaa wamesalia badala ya wamesalia vichaa
Inkisari –nambiebadalayaniambie (zozote 2x1)

9) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili (alama 3)
Wosia –ushauri/nasaha,mawaidha
nudhumu –mtungo,shairi
wamesinyaa-wamedhoofika afya (zozote 3x1)

**2 MajibuTamthilia**

1 Sumu ya nyoka husababisha kifo na madhara makubwa, imetumia kuashiria dawa za kulevya. Aidha uovu unaotendwa na utawala wa Majoka ni mfano wa sumu kali yanyoka .

- Wanafunzi katika Majoka Academy wanaangamia kwa kudunga na sumu ya nyoka ambayo inaaminika kuwa dawa za kulevya.
- Masomo katika shule ya Majoka Academy hayawafaidi wanafunzi,yanakuwa kama sumu ya nyoka kwao kwani Ashua anasema kuwa hawafuzu.
- Ngao Juniour anaaga dunia kutokana na kuumwa na nyoka
- Ngurumo anaua wakwa kuumwa na nyoka
- Majoka ana kiwandakikubwachakutengenezeasumuyanyoka
- Utawala unakataa kusafisha soko na kuacha kemikali na uchafu kuwasababishia watu maradhi yasiyokuwa na tiba
- Soko la Chapakazilinafungwa na kusababishia wanasaga moyo wanaolitegemea dhiki kubwa ya kupata riziki(Watoto wa Ashua na Sudi (Pili na Pendo )wanakosachakula)
- Utawala wa Majoka unatuma wahuni kumshambulia Tunuiliasileteu pinzani na kuendeleza harakati za ukombozi.
- Utawala wa Majoka unamwua Jabali
- BabayeTunu anakufaa kimfanyia Majoka kazi
- Vijana wanauawa wakiwa katika maandamano ya kutetea haki zao kutokana na kudhulumiwakazini.
- utawala wa Majoka unawapa leseni watu kuuza pombe haramu inayosababisha madhara mabaya kwa watumiaji.
- Ufafanuzi wa swali 2x1= 2Hoja zozote 9x2=18

1. **Fafanua mbinu alizozitumia Majoka ili kubakia mamlakani**.
Majibu:

- Askari kuwapiga na hata kuwauwa waandamanaji kama wanavyoagizwa na Kenga.
- Vitisho, vikaratasi vya kuwatishia watu kuhama vinatupwa ili kuwatia hofu watu kwa kuwaambia wahame.
- Vyombo vya dolak.m Gereza linatumiwa kuwatenga na kuwatesa wazalendo. Mfano ni Ashua anayefungiwa ili ayakubali mapenzi ya Majoka.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Hongo inatumiwa, mfano, Sudian abembelezwa na Kenga kukitengeneza kinyago cha Majoka. Anaahidiwa pesa tele na safari zang'ambo.
- Ujanja mfano ndoa ya tunu kwa ngao junior ili Tunu awache upinzani anapokuwa katika familia ya Majoka.
- Kupigwa, Tunu anapigwa sana na kuvunjwa miguu
- Vifo vya viongozi wanaopigania haki mfano, Jabali, Tunu alijaribu kuuwawa na Majoka.
- propaganda kutumia mitandao ya kijamii na stesheni moja tu ya kitaifa
- Kuzima vyombo vya habari vingine vyote ili visitoe taarifa za kweli kuhusu yale yanayoendelea Saga moyo
- Kuhakikisha wananchini maskini kwa kukosa ajira. Hali hii inahakikisha kuwa hao ni wategemezi hivyo wanadanganywa na misaada na pesa kidogo ili wawapigie kura viongozi waovu kama Majoka. Kwa mfano, inasemekana kuwa Chakula cha msaada kingetolewe. Pia keki ndogo inawafurahisha watu kama BozanaKenga.
- Pombe na vileo hutumika kuwalevya vijana hivyo wasifikirie zaidi. Vijana kama ngurumo na wenzake wanatumi wanaviongozikuzuarabshanakuwauawanaopiganiahakizao. Kutokanana ule zihuu, vijana wanashindwa kuuelewa ukweli juu ya hali yao,hivyo wanajazwa mawazo duni na viongozi wabaya.
- Uongo na hila, mfano, kuwa ongezea watu mishahara kidogo kasha kuwatozako dihivyo, wananchi wanaonakuwa uongozi unawajali kumbe unawanyanyasa bila kujali.

**3Fasihi Simulizi**

a) Mawaidha (alama 2)

b)
- Ni mawazo mazito kuhusu maisha k.vunyumba, urithi, mapenzi, malezin.k
- Mawaidha hulenga hadhira maalum
- Hulenga maudhui maalum
- Huibua maadili yanayohitajika kuzingitiwa
- Ujumbe katika mawaidha hujitokeza moja kwa moja.
- Hutolewa na mtu mmoja anayeaminika kuwa mjuzi waanayezungumziwa
- Hutumia lugha ya kipekee yenye maana kina na yakuvutiahadhira
- Tamathalinyingizausemhutumiwa zozote (4x2=8)

c)
- Ni njia moja wapo ya kuendeleza utamaduni wa jamii
- Huwapinda watu kushiriki ipasavyo katika shughuli za utamaduni
- Huelekeza jamii inapotoka
- Hujasirisha waoga na kuwapa ukakamavu wasionao
- Huelimisha
- Huwaondolea ujinga wengine katika jamii
- Husaidia katika uchanganuzi wa mambo na hali zinzoikabili jamii
- Huamrisha uadilifu katika jamii. (zozote 4x2=8)

d)

---Kuonya -Kushauri ---Kuelekeza ---Kutahadharisha-----Kuelimisha (zozote 2x1=2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: HADITHI FUPI.**
**TUMBO LISILOSHIBA**

**4. a) Mapenzi ya Kifaurongo.**

i) Mapenzi: Kuna mahusiano ya kimapenzi miongoni mwa wanafunzi,Penina anamwendea Denis kutaka kuwa mpenzi wake.
ii) Utabaka chuoni: Denis Machora anajihurumia anapojilinganisha na wanafunzi wengine kutokana na hali yake ya umaskini.
iii) Kutamauka kwa wanafunzi kutokana na ugumu wa masomo.
iv) Umaskini –Denis Machorahanamahitajiyakimsingikama vile chakula.
v) Ukosefu wa ajira baada ya kukamilisha masomo – Denis.
vi) Wahadhiri kutowajibika: Dkt. Mabonga anafunza vitu ambavyo haieleweki.
vii) Uzembe – Wanafunzi katika chuo kikuu hawatilii maanani masomo yao. (zozote tano)

**b) Shogake dada ana ndevu.**

- Mapenzi ya kiholela: Safia na Kimwana ni wanafunzi wa shule ya msingi ilhali wana uhusiano wa kimapenzi.
- Mimba za mapema – Wanafunzi kupata mimba wakiwa bado shuleni. Safia alipata mimba akiwa darasa la nane.

- Uavyaji mimba – Wanafunzi wanaopata mimba wakiwa shule wanakata shauri kuavya mimba – Safia.
- Vifo vya mapema–Wanafunzi wanaopata mimba wanapojaribu kuavya mimba na kuishia kufa – Safia.
- Kutowajibika kwa wazaz katika malezi ya watoto wao: Wazazi hawajihusishi katika masomo ya watoto wao.Wazazi wake Safia hawakujua walichokuwa wakifanya chumbani Safia na Kimwana walikodai kudurusu masomo yao. (zozote tano)

**c) Mwalimu Mstaafu.**

- Kutamauka:Wanafunzi kujiona zuzu wasiposhika masomo,mfano,Jairo.
- Ubaguzi: Kufeli katika elimu kunachukuliwa kama ni kufeli maishani. Hata hawapewi nafasi ya kuzungumza mbele ya watu.Mwalimu Mosi anawashinikiza wasimamizi katika sherehe ya kustaafu kwake kumpa Jairo nafasi ili naye aihutubie hadhira.
- Umaskini: Watoto kufukuzwa shule kwa kukosa vitabu vya kaida – Sabina bintiye Jairo.
- Mfumo wa elimu: Haushughulikii wasioshika masomo darasani- Jairo.
- Mapenzi ya kiholela:Wanakijiji walishuku kuwa huenda Mwalimu Mosi alikuwa amemtorosha shule Sabina bintiye Jairo. (zozote tano)

**d) Mtihani wa Maisha.**

- Mapuuza ya wasimamizi wa elimu: Mwalimu Mkuu anamtupia Samueli matokeo yake kama mtu anayemtupia mbwa mfupa.Alipuuza uwepo wake ofisini mwake.
- Wanafunzi kutembea mwendo mrefu kwenda shule za kutwa.
- Ukosefu wa nidhamu shuleni; Samueli alipokuwa shuleni aliitwa ,'Rasta' kutokana mahoka yake.Anawaita mahambe kama mwalimu wao mkuu.
- Kufeli mitihani: Matokeo ya Samueli ni D na E katika masomo yote.
- Kutamauka baada ya kufeli mtihani: Samueli anataka kujiua.
- Mapuuza ya wanafunzi: Samueli alidhani kuwa ni mwerevu ilhali hajui chochote.
- vii) Taasubi ya kiume: Samueli alitarajiwa kufanya vyema kuliko dada zake. (zozote tano)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**5. ''Hakikubakia hata chakula kidogo cha sadaka ya mwenye njaa...''**

**i) Kauli hii inarejelea unyanyasaji wa Wanamadongoporomoka..**

- Jitu linamaliza chakula chote kwenye Mkahawa Mshenzi bila kuwajali wateja waliokuwa pale.
- Vibanda vya Wanamadongoporomoka vinabomolewa bila kujali watapokwenda wenye vibanda.
- Wakubwa wanaweka vikwazo katika sheria kwa makusudi ili kuwazuia watu wadogo kutetea mali zao.
- Wanamadongoporomoka hawahusishwi katika mipango ya maendeleo katika eneo lao.
- Askari wa baraza la mji na jeshi la polisi wanatumiwa kuwafurusha Wanamadongo wenye njaa katika makazi yao badala ya kuwahakikishia usalama wao.
- Majengo mengi yanajengwa katikati ya jiji kiwango cha mtu kukosa nafasi ya kuvuta pumzi.
- Wanasheria kukosa kuwa waaminifu wanapokabiliwa na sheria ngumu.''siku wanasheria waaminifu ni adimu kama haki yenyewe!''
- Wakubwa wanataka kunyakua ardhi ya wasiokuwa na nguvu kwa lazima baada ya
- Wakubwa wanataka kuwahonga kwa visenti vyao vichache ili waondoke ilhali hawana pa kwenda.
- Mazingira chafu- Madongoporomoka ndiko kunako pachapacha za kila kitu;tope na uchafu unaonyekenya,makaro na uvundo unaopasua mianzi ya pua.

Hoja zozote kumi (1x10=10) Hakiki majibu ya wanafunzi.

**ii) Ukweli wa kauli.**

**Watahiniwa walinganishe yanayotokea katika hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na ulimwengu wa kisasa.Asipolinganisha asituzwe alama.**

a) Ubinafsi- Kuna ubinafsi na ulafi katika jamii ya kisasa kama ilivyo katika hadithi.Jitu linamaliza chakula chote kwenye Mkahawa Mshenzi bila kuwajali wateja wengine.

b) Unyakuzi- Wakubwa wanataka kunyakua ardhi ya watu wadogo kama ilivyo katika jamii ya leo ambapo viongozi hunyakua ardhi ya watu maskini.

c) Dhuluma- Wananchi hukandamizwa kwa kubomolewa vibanda/makazi yao hata bila ilani na kuachwa wakihangaika jinsi ambavyo inafanyikia Wanamadongoporomoka.

d) Ufisadi- Wakubwa wanataka kuwahonga na vijisenti vidogo ili wahame makazi yao jinsi viongozi katika jamii ya leo huwahonga wananchi maskini na kunyakua mali yao.

e) Sheria zenye vikwazo- Katika jamii ya leo,sheria huwapendelea matajiri na viongozi kwani wao huweka vikwazo makusudi ili kuwazuia maskini na wasio na nguvu kutetea haki zao.Hali ni hiyo hiyo katika hadithi ya Tumbo Lisiloshiba.

f) Kutengwa- Wananchi hawahusishwi Na viongozi kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya maeneo yao.Wanamadongoporomoka hawahusishwi katika mipango ya maendeleo.

g) Mazingira chafu- Hali katika mtaa wa Madongoporomoka ni mbaya,viongozi hawasafishi mtaa wao,kama ilivyo katika mitaa duni nyingi katika jamii ya leo.

h) Wanasheria wasio waadilifu- Jinsi inavyokuwa vigumu kupata wanasheria waadilifu katika jamii ya leo, ndivyo ilivyokuwa adimu kuwapata wanasheria waaminifu kama haki yenyewe katika jamii ya hadithi ya Tumbo Lisiloshiba.

i) Msongamano mijini- Jiji lilikuwa limejaa limejaa kila mahali;mall,majumba ya muziki,maduka makuu,shule, vyuo,hospitali,mahakama,majumba ya ofisi,n.k. Jinsi ilivyo katika miji mikuu mingi leo.

j) Matumizi mabaya ya vyombo vya dola- Askari wa baraza la mji na jeshi la polisi walitumiwa kuwafurusha wanamadongoporomoka badala ya kuwahakikishia usalama wao,Vyombo vya dola vinatumiwa vibaya na viongozi wa sasa.

k) Maendeleo- Kuna maendeleo yaliyopiga kasi katika jamii ya sasa kama ilivyo katika jamii ya hadithini.Jiji limejaa majumba ya mikahawa,malls,deparmental stores,casinos,n.k.

l) Ushirikiano- Kuna ushirikiano na umoja wa wananchi wanaonyanyaswa katika jamii ya sasa jinsi Mzee Mago alivyowakusanya wanamadongoporomoka ili kutetea haki zao.

Hoja zozote kumi (1x10=10) Hakiki majibu ya wanafunzi

Chozi la Heri

1 Eleza masaibu yanayowakabi liwatu wasiokuwa “wenyeji” katika Riwaya ya Chozi la Heri

- Kubaguliwa kwa mfano Ridhaa anabaguliwa na kufanyiwa dhihaka na watoto wenzake shuleni
- Nyumba zao zinachomwa pamoja na mali zao nyumba za Ridhaa zinateketezwa
- Baadhi wanauawa kwa mfano familia ya Ridhaa inateketezwa katika moto
- wanalazimika kutembea mwendo mrefu kutafuta makao ya muda
- Baadhi wanakabiliwa na magonjwa katika harakati ya kutorokea usalama
- wanakosa chakula wakiwa katikaka mbiya wa kimbizi
- Wengine wanakufa kwa magonjwa
- wanakosa maji safi ya kunywa katika kambi ya wa kimbizi
- wanalazimika kula matund ana mizizi ya mwitu
- wanakosa vyoo na kulazimika kutumia vile vya kupeperusha. Zozote 10x2

Fafanua migogoro inayojitokeza katika Chozi la Heri alama 20

- Migogoro baina ya wafuasi Mwekevu na wale wanao muunga mkono mwanamume
- mgogoro wa kimaoni baina ya Tila na Ridhaa
- Mgogoro baina ya Umulkheri na askari kuhusu watoto waliopotea
- Mgogoro baina ya Mwangeka na mkewe Lilly Nyamvula
- Mgogoro baina ya askari na waandamanaji
- Mgogoro baina ya watoto shuleni

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA LAINNAKU**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**

**Maswali**

1. Wewe ni mwakilishi wa vijana katika kaunti yenu ya Tupamoja. Andaa barua pepe utakayomtumia waziri wa masuala ya vijana na jinsia katika serikali kuu ukimfahamisha kuhusu changamoto wanazopitia vijana eneoni.

2. Sekta ya kilimo nchini imeendelea kukumbwa na matatizo chungu nzima. Thibitisha.

3. Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji.

4. Andika insha itakayotangulizwa kwa maneno yafuatayo:
   Siku yenyewe ilikuwa njema. Niliamka alfajiri na mapema ili kuanza shughuli zangu za kila siku. Mara nikapata ujumbe…

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>TATHMINI YA PAMOJA YA LAINNAKU I - 2020</u>**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**Machi 2020**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma. Wanafunzi wengi nchini, wakiwemo wanangu bado hawajaripoti shuleni. Watenda nini? Juhudi za wanafunzi wengi nchini ambazo hufananishwa na za mchwa wajengao vichuguu kutwa kuchwa huenda zikazama kwenye bahari yenye kina kirefu.

Hii si kwa kupenda kwa wanafunzi hao bali kwa majaliwa ya Mungu anayewapa waja viti na kumbi. Hakuna mja aliyezaliwa na hela mkononi wala umaskini kinywani. Wewe uliyenacho shukuru Mungu.

Wapo wanaoamka wakinywa chai ya mkandaa kwa kiporo baridi cha ugali na wapo wanaoshtaki njaa kwa **matobosha** na sambusa kwa mikate ya mofa kila asubuhi. Wewe ni wa tapo gani? Kupata kwa maskini au mnyonge ni kwa mwenye nguvu kupenda, na ili maskini apate njia lazima tajiri ampe nafasi. Wangapi wamepata nafasi ilhali matajiri wanalilia zaidi haki za kutajirika?

Zaidi ya wanafunzi asilimia thelathini wanakabiliana na umaskini ana kwa ana. Wengi wao walihitimu kujiunga na shule za mikoa na wengine za kitaifa lakini ng'o! Kuendelea kwao kusoma kumegeuka jinamizi ya kighafla!

Wakuu wa shule kadhaa tulizotembelea mapema wiki iliyopita **walilimatia** kuzungumzia suala hili ambalo ni nyeti kutoka kwa wanafunzi wa jamii fukara nchini.

Wengine walidai kwamba ulipaji karo wa wanafunzi hao pindi waingiapo shuleni huwa kizungumkuti kwao. Japo mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yakiwemo benki na asasi mbalimbali hujitokeza hadharani na kujitwika mzigo wa gharama zote, mambo huenda **tenge tahanani** pindi kufuatiliwa kwa ada kunapoanza.

Hii husababishwa na ithibati nyingine za uongo baina ya jamii watokako wanafunzi hao na uhalisia wa stakabadhi za wanafunzi waathirika, zinazowasilishwa baada ya matokeo yao kuwasilishwa kwa wadhamini. Namaanisha stakabadhi bandia. Hii si kumaanisha kuwa kila mhusika wa kudhaminiwa hawi mkweli, hasha! Njia za kibinafsi na mikato wakati mwingine hukwamiza ndoto za wanafunzi wanaodhamiria kuukwea mlima wa masomo kwa minajili ya kujikimu na kuzifaa familia zao siku za usoni. Wengine huuza mifugo wao kwa minajili ya kupata angalau nusu ya karo ya mwaka mzima. Umewahi kuwaona wenzetu kutoka kwa makabila ya Kimaasai, Wapokoti, Wasamburu na Waturkana wakisherehekea kwa nderemo pindi mtoto wao anapohitimu katika chuo kikuu kwa cheti fulani kama vile; stashahada, shahada ya uzamili au uzamifu?

Anzia mavazi hadi masomo…wanafunzi husomea taabu, hula taabu na kumeza taabu lakini siku yao ya mavuno huwaacha wenzao nusu vilio na wengine nusu vicheko. Huimba na kurukaruka kwa furaha ya ndama wanywao maziwa huku machozi ya raha yakiwatoka mbonini.

Kuna wanafunzi wengi wanalilia misaada ya karo na udhamini hasa wale watokao katika jamii maskini. Eti! Wanaisaka ndoto! Mwenye uwezo ajitokeze kufuta machozi yao jamani. Hongera zangu ni kwa mashirika yanayojifunga nira kuimarisha na kuitimiza ndoto ya wanafunzi hawa wenye malengo timamu maishani bila kubagua. Sio tu mashirika pekee bali watu binafsi (ambao Mungu huwapa uwezo wa kula na kusaza) ambao wanaweza kufadhili yeyote.

Kwa yakini, kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Misukosuko yoyote ya kiuchumi nchini huanza na mzalendo mwenyewe.

Umeitendea haki gani nchi yako? Ama warudisha maendeleo nyuma? Nafasi uliyoiwania ukitoa ahadi nyingi, umeitumiaje kuwasaidia wanyonge? Sidhani hela za CDF zingali zinatumika sawasawa katika kila kaunti nchini. Ukila kwa vijiko na uma wakumbuke walao kwa vidole kwani vijiko hawajaviona kwao tangu kuzaliwa!

**Maswali**

a. Ipe anwani mwafaka habari uliyoisoma. (alama 2)

b. Nini maana ya, 'huenda juhudi za wanafunzi wengi nchini zikazama kwenye bahari yenye kina kirefu ? (alama

c. Kuneemeka kwa mkata kwategemea mambo mawili. Yataje. (alama 2)

d. Mashirika yanayojitolea kuwafadhili wanafunzi kutika jamii fukara hukumbwa na changamoto ipi? (alama 2)

e. Kufikia mwisho wa taarifa hii mwandishi anatoa rai gani? (alama 4)

f. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyovyotumiwa katika kifungu: (alama 3)

i) Matobosha……………………………………………………………………….

ii) walilimatia..................................................................................................

iii) tenge tahanani…………………………………………………………………….

**2) MUHTASARI**

Maendeleo ya taifa hutegemea jinsi wananchi wanavyojitolea katika kulibiringisha gurudumu la uchumi wao. Kila mwanajamii anahitajika kujibidiisha katika kazi au taaluma yake . Mzalendo yeyote yule hupata motisha ya kufanya kazi iwapo anaweza kupata ile kazi aliyokuwa akitamani.

Kumakinika katika taaluma fulani si jambo jepesi na huchukua muda kutengenea. Kwa mfano , ili mhazili apate staha ya uhazili sharti apitie ngazi mbalimbali. Mwanzo kabisa lazima ahitimu vyema katika masomo rasmi ya darasani . Masomo hayo pamoja na cheti huweza kumpa fursa nzuri ya kujiunga na vyuo mbalimbali vya uhazili. Anapojiunga na vyuo hivyo ndipo safari inapoandaliwa.Kukamilisha safari hii anahitaji muda wa miaka minne-mitano. Anapohitimu huwa tayari ameimudu shughuli hiyo.Hata hivyo , anatakiwa afanye mazoezi kila mara ili asisahau yanayohitajika katika taaluma hiyo. Wengi waliokwishapata ujuzi huo wa uhazili huona kuwa hawatapata kazi nzuri yenye mshahara mkubwa. Baadhi yao hujilinganisha na wale wenzao ambao katika masomo wana utaalamu kama wao. Ijapokuwa wote ni wahazili ,viwango vyao ni tofauti na mishahara pia hutofautiana. Tofauti hapa ni daraja zao za vyeo. Baada ya kuhitimu na kupata vyeti vya uhazili ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia. Anayefanikiwa ana safari ya kujikakamua hasa kwa upande wa uzingatifu wa kazi kikamilifu na kutunza hadhi ya ofisi yake.

Kuna mashirika makubwa yanayojiweza kiuchumi, ambayo rasilimali yake ni imara. Mashirika madogo huwa yana rasilimali yenye kuyumbayumba . Mashirika haya yana wahazili na wafanyikazi ambao hupata mishahara duni. Wafanyikazi wote hao hufanya kazi kwa kutokuwa na uhakika wa kulipwa mwishoni mwa mwezi.Watu kama hao hawawezi kutilia maanani kazi zao. Mashirika mengine hutegemea utu wa mkurugenzi. Baadhi ya wakuu hao huwa wabanizi na huwapunja wafanyakazi wao.Hili ni swala nyeti ambalo linahitaji kutatuliwa kwa kuwa na chama cha kupigania haki za wafanyikazi. Wakati wanapotafuta kazi wahazili wengi huwa ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.

Wale waliobahatika kupata kazi ya ajira katika kampuni kubwa za kimataifa , mishahra huwa ni ya kutia moyo. Katika dunia hii ,wahazili wana vibarua vigumu kwa sababu lazima wapate tajriba na uzoefu wa taaluma inayoendelezwa na shirika fulani.Mhazili sharti azoee istilahi zinazotumiwa. Wakurugenzi aghalabu huwa hawana subira . Mhazili

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

anapotumia msamiati usioenda sambamba na shughuli za kiofisi hawasiti kufoka.Wavumilivu miongoni mwao hula mbivu. Hawa hawafi moyo bali hujitahidi zaidi ili wasikumbwe na kimbunga cha kufokewa . Kuna wengine ambao humwaga unga.

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 60-70. (Alama 7,1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho , eleza mambo muhimu yanayoshugulikiwa na mwandishi . ( maneno 60 – 70) (alama8,1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40 )**

a) Taja na utofautishe **vipasuo** vya ufizi. (alama4)

b) Tumia **shadda** kubainisha maana mbili za neno: **walakini .** (alama2)

c) Andika sentensi ifuatayo katika **udogo-wingi**: (alama2)
Mbuzi alikimbizwa na mbwa mkali.

d) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **dalili na dhalili**. (alama2)

e) Andika upya kwa kutumia **kiwakilishi-nafsi huru** badala ya nomino zilizopigiwa mstari. (alama 2)

i) Siti, Kadzo na Kisia ni wafuasi maarufu.
ii) Mimi na ndugu zangu ni waimbaji hodari.

f) Alama za mtajo hutumiwa kufungia maneno halisi ya msemaji. Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mengine mawili ya **alama za mtajo**. (alama2)

g) Badilisha vitenzi vifuatavyo viwe katika hali ya **kutendama**. Kisha uvitungie sentensi (alama4)
i) ganda
ii) ficha

h) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa **jedwali**: (alama 4)
Wanafunzi werevu watafadhiliwa ilimradi wadumishe nidhamu.

i) Bainisha **shamirisho** katika sentensi hii. (alama 3)
Auma amekatiwa muwa na Ouma kwa kisu kipya.

j) Eleza maana inyokusudiwa na kiambishi **-po-** kama kilivyotumika katika sentensi zifuatazo (alamal 2)
i) Kila tusikiapo wakiimba, sisi hutulia kuwasikiza.
ii) Tunaposikia wakiimba, sisi hutulia kuwasikiza.

k) Nomino zifuatazo ziko katika **ngeli** gani ? (alama 2)
i) mjusi
ii) mate

l) Tambua **viambishi** awali na tamati katika neno alaye (alama 2)

m) Andika **vitenzi** vinavyotokana na nomino zifuatazo: (alama 2)
i) mfuasi
ii) kifaa

n) Eleza matumizi ya **kwa** katika sentensi zifuatazo : (alama 2 )
i) Alisifiwa kwa kuibuka mshindi.
ii) Daktari **Mabonga** aliwatibu wanakijiji kwa miongo kadhaa.

o) Tunga **sentensi** yenye muundo ufuatao: (alama 2)
KN (V+N) + KT(t+V)

p) Eleza hali katika sentensi zifuatazo: (alama2)
i) Obadia anasimama akasome.
ii) Karoli asoma kitabu cha Kiswahili.

q) Toa maana ya **nahau**: (alama 1)
Kuwa na mizungu.

**4. ISIMUJAMII (AL 10)**

a. Fafanua sifa zozote tano za sajili ya mazungumzo ya afisini. (alama 5)

b. Thibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (alama5)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA LAINNAKU 2020**
**102/ 3 KISWAHILI – Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**Muda: Saa 2 ½**

**SEHEMU YA A: TAMTHILIA**
**P. KEA: KIGOGO**
**1. LAZIMA**

" Siafu huwa wengi. Si rahisi kuwamaliza…. Hawawezi kuliziba kwa ungo!"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(ii) Bainisha tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (alama 4)
(iii) Jadili mbinu **kumi na mbili** ambazo "Siafu" wanatumia kupigana na utawala dhalimu. (alama 12)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**
**A: MATEI :CHOZI LA HERI.**

*Jibu swali la 2 au la 3*

2 a) "Alikumbuka jinsi rafiki yake … alivyofishwa kwa njia hii. Akili yake ilimtambia kisa chenyewe kana kwamba inataka kumuonya"
  i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  ii) Bainisha tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
  iii) Fafanua umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili katika kujenga riwaya hii. (alama 4)
 b) Kwa kutolea hoja **kumi** jadili changamoto zinazowakumba vijana wengine katika riwaya "Chozi la Heri". (alama 10)

3. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika kukuza maudhui katika riwaya Chozi La Heri.
  a) Mbinu rejeshi. (alama 10)
  b) Kinaya. (alama 10)

**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI**

*Jibu Swali 4 au la 5.*

A. Chokocho na D. Kayanda (Wah); Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.
A. Chokocho: "Masharti ya kisasa"

4. "Au huelewi wanawake wana uhuru? *My dress, my choice*!"
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza mbinu **mbili** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Jadili dhana ya "Mwanamke wa kisasa" kama ilivyoshughulikiwa katika hadithi "*Masharti ya kisasa*". (alama 7)
(d) Hakiki jinsi maudhui ya uozo wa kijamii yanavyojitokeza katika hadithi "*Mame Bakari*." (alama 7)

5 a) Onyesha jinsi ubadhirifu unavyoshugulikiwa katika hadithi, "*Shibe inatumaliza*." (alama 8)
 b) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 12)

"Ee, dunia hii ina mambo. Haya! Hivi vyeo vyangu maana yake nini hasa? Umuhimu wake ni upi? Na majukumu yake je? Mungu wangu we, ni muda sasa natoka kwangu Kombora. Narudi kulala unono. Lakini akitokea mtu akaniuliza kazi zangu zipi hasa, sitakuwa na jibu zaidi ya mikogo na madaha yangu tu. Nitakaza meno na kulegeza ulimi wa kumbabaisha kwa kizunguzungu. Tamko langu litakuwa "*huku third world bwana eee…yah! Yah let me tell you mhh! Yah!*"

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

*Jibu Swali La 6 au la 7*

6. **Soma Shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

***Dhamiri yangu*.**

Dhamiri imenifunga shingoni.
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwishachora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula.
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: kamba, kamba.

Oh! Nimefungwa kama mbwa.
Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Kuifikia na hapa nilipofungwa
Nimekwisha pachafua na kuhama siwezi.

Kamba isiyoonekana haikatiki,
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
Aliharibu na mbwa aliuma watu.
Ninamshukuru aliyenifunga hapa
Lakini lazima nitamke kwa nguvu "Hapa nilipo sina uhuru"

a) Taja mambo **manne** ambayo mshairi analalamikia. (alama 4)
b) Kwa nini mshairi haoni haja ya yeye kuwa huru? (alama 2)
c) Eleza maana ya mshororo ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. "Kamba isiyoonekana haikatiki." (alama 2)
d) Taja na utoe mifano ya aina **mbili** za tamathali zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
e) Kwa kutoa mifano **miwili**, eleza jinsi matumizi ya mishata yanavyojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
f) Andika ubeti wa **pili** kwa lugha nathari. (alama 4)

7. **Said A. Mohamed:** *Mbele ya Safari*

1. Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

5. Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili. (alama 2)
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (alama 6)
c) Taja na ueleze bahari **mbili** za shairi hili ukizingatia: (alama 4)
 (i) Mizani;
 (ii) Vina.
d) Andika ubeti wa **saba** kwa lugha ya nathari. (alama 4)
e) Eleza umuhimu wa aina **mbili** za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (alama 4)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI</u>**

**8.** *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***.**

Ndimi Mwimo mdumishaji ukoo
Ndimi ndovu mtetemesha ardhi
Aliyepigana vita, ukoo kuauni
Ziliporidima zangu nyayo
Adui alinywea, mafahali na mitamba akatukabidhi
Kwenye misitu sikuwa na kifani
Paa na hata visungura
Vilijikabidhi kwangu
Kwa kuinusa tu mata
Nani aliyewahi
Ngomani kunipiku?
Makoo hawakunisifu, wakalilia nikaha?
Kwenye Nyanja za michuano
Nani angethubutu, ndaro kunipigia?
Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi, hata kabla hatujavaana?

i) Andika aina ya sifo hii. (alama 1)
ii) Bainisha shughuli **mbili** za kiuchumi na **mbili** za kijamii zinazoendelezwa na jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)
iii) Eleza mambo **manne** ambayo yanaweza kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 4)
iv) Eleza faida **tatu** za matumizi ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano. (alama 3)

b) Unanuia kutumia hojaji kukusanya habari kuhusu kipera hiki:
 i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. (alama 5)

ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. (alama 5)

**TATHMINI YA PAMOJA YA LAINNAKU I 2020**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI**
**INSHA – 102/1**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**

1. **Ni barua pepe**
   Kazi ya mtahiniwa idhihirishe vipengele viwili vikuu vya kisura
   a) Utangulizi:
      - Kutoka kwa:
      - Kwenda kwa:
      - Tarehe:
      - Kichwa/anwani/mada
   b) Mwili
      - Maudhui au kiini cha barua kishughulikiwe hapa
      - Hoja zipangwe kwa kuzingatia mtindo wa aya

**Baadhi ya hoja**

a) Ukosefu wa nafasi za kazi kwa waliosoma na kuhitimu taaluma mbalimbali
b) Umaskini katika jamii – wengi wameshindwa kwendelea na masomo yao licha ya kufuzu katika ngazi tofautitofauti za elimu
c) Matumizi ya dawa za kulevya
d) Kukosa vielelezo katika jamii
e) Ahadi hewa kutoka kwa wanasiasa wanaowatumia katika harakati za kujitafutia vyeo na baadaye kuwatema vijana.
f) Makundi ya kihalifu yanayowashawishi vijana kujiunga nayo.
g) Wazazi wasiotelekeza wajibu wao wa malezi – wasiogharimia karo na mahitaji mengine ya malezi kwa vijana.
h) Shinikizo la rika – wengi hupotea baada ya kupokezwa ushauri mbaya.
i) Kukosa mashirika yanayoweza kufadhili miradi inayoweza kuwafaa vijana.
j) Wenye vipawa kupuuzwa na kukosa uungwaji mkono na serikali.
k) Kupuuzwa na kunyimwa nafasi ya kujieleza.
l) Kutopewa nafasi katika ngazi mbalimbali za uongozi.

**Tuza hoja nyingine mwafaka**

2. **Matatizo yanayokumba sekta ya kilimo.**

a) Vifaa duni vya kulima kv. Wengi wa wakulima hutumia viserema.
b) Ukosefu wa maghala ya kuhifadhia mavuno – hasa kwa wakulima wa nafaka
c) Mashamba madogo yasiyoruhusu matumimzi ya tekinolojia ya kisasa kv. Trekta na mashine nyinginezo.
d) Kukosa wataalamu wenye ujuzi wa kutosha ili kuwaelekeza wakulima ipasavyo.
e) Vijana wenye nguvu kuhamia mijini ili kutafuta kazi za ofisi; hivyo kuachia wazee wasio na nguvu shughuli za kilimo.
f) Wakulima kukosa ufadhili au uungwaji mkono na serikali.
g) Bei duni kwa bidhaa zinazouzwa katika masoko ya dunia kv; kahawa, majanichai n.k
h) Mabadiliko ya misimu ambayo yameleta ukame.
i) Uvamizi wa wadudu hatari kama vile nzige.
j) Umaskini – wakulima wengi hawatumii pembejeo au mbegu zilizoidhinishwa kwa kukosa hela.
k) Ukosefu wa elimu – wakulima wasio na ujuzi wa kutumia mitindo ya kisasa ya kulima huishia kutumia mbinu za kale.
l) Wamiliki wa mashamba makumbwa yasiyotumika katika shughuli za kilimo.
m) Mafuriko yanayoharibu mazao kwa wakulima wengi.
n) Vijana kudhalilisha kilimo.

**Tuza hoja nyingine mwafaka**
**Hoja zote ziwe za kuunga mkono kauli**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. Ni methali**

Mtu akisifiwa sana kwa wema wake hatimaye hujiona bora zaidi na kuharibu wema huo. Methali nyingine yenye maana sawa na hii ni; ngoma ikilia sana hupasuka.

Methali hii ni onyo kwa wanaopenda kuwatunuku na wanaotunukiwa sifa kemukemu.

Kisa cha mwanafunzi kidhihirishe pande zote mbili; kusifiwa sana na kulitia tembo maji

**Tanbihi: Si lazima pande zote mbili zishughulikiwe kwa upana sawa**

**4. Ni insha ya mdokezo**

Mdokezo huu utumike mwanzo wa insha ya mtahiniwa.

Kisa cha mwanafunzi chaweza kulenga ujumbe wa kutamausha alioupokea au ujumbe wa kutia moyo au wenye kuashiria bahati njema

**MWONGOZO WA KUSAHAHIHISHA**
**KISWAHILI 102/2**
**TATHMINI YA PAMOJA YA LAINNAKU 1-2020**

**1. UFAHAMU**

a. Umaskini / Elimu / Matatizo yanayoathiri masomo ya maskini 1x2

b. Wanafunzi huenda wakakatiza masomo yao kutokana na umaskini 1x2

c. (i) majaliwa ya Mungu
(ii) kupatiwa nafasi na matajiri
2x1

d. Wafadhiliwa huwasilisha stakabadhi bandia 1x2

e. (i) watu binafsi wenye uwezo wasaidie maskini
(ii) Watu waonyeshe uzalendo wao kwa kusaidia maskini
(iii) Kutumia pesa za CDF vizuri 2x2

f. (i) mahamri au ndazi
(ii) walikawia kuzungumzia jambo hilo
(iii) fujo au ghasia isiyorekebishika 3x1

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**kuadhibu**

**1**. sarufi (s) : Ondoa nusu alama kwa kila kosa litokeapo kwenye kijisemu mahususi mradi tu pana alama nzima,

2. hijai (h): Ondoa nusu alama hadi upeo wa alama tatu kwa kila kosa litokeapo kwa mara ya kwanza.

**2. MUHTASARI**

a.

i) Maendeleo ya taifa hutegemea bidii ya wananchi kazini/ wanavyojitolea kazini.
ii) Mzalendo hupata motisha apatapo kazi aliyoitamani.
iii) Kumakinika katika taaluma fulani huchukuwa muda kutengenea/ taaluma yoyote huchukuwa muda kutengenea
iv) Mhazili lazima ahitimu darasani / katika masomo darasani.
v) Anapojiunga na vyuo vya uhazili huchukuwa muda kuhitimu.
vi) Anatakiwa afanye mazoezi kila mara ili asisahau.
vii) Wengi huona kuwa hawatapata kazi nzuri/ ya mshahara mzuri/ wengi hujilinganisha na wenzao wenye viwango / mishahara tofauti/ ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia.
viii) Anayefanikiwa ni lazima /sharti /hana budi kujikakamua kazini. (6x1)

b)

- Mashirika makubwa yanajiweza kiuchumi kuliko madogo
- Mashirika madogo hulipa mishahara duni isiyotegemewa.
- Wafanyakazi hawawezi kutilia maanani kazi zao.
- Baadhi ya wakurugenzi ni wabanizi na huwapuja wafanyakazi wao/
- ulipaji wa mishahara hutegemea utu wa mkurugenzi/
- mashirika mengine hayana utaratibu maalumu wa kulipa mishahara/

- Kuna haja ya kuwa na chama cha kupigania masilahi ya wafanyikazi.
- Wahazili wengi ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.
- Wanaoajiriwa katika mashirika /kampuni za kimataifa hulipwa mishahara mikubwa.
- Wahazili lazima wapate tajiriba/uzoefu na wawe wavumilivu.
- Wakurugenzi wasio na subira huwafokea/ huwafuta kazi wahazili wasiomakinika .

(7x1)

M
(a) 6
(b) 7
(ut) 2

15 – hs – z

**Maelezo**

- Zingatia idadi ya maneno yaliyotolewa katika swali.
- Jibu liandikwe kwa lugha nathari.
- Makosa ya sarufi na hijai yaadhibiwe hadi upeo wa makosa 6 (Alama 3) kwa kila mojawapo.

**3. Matumizi ya lugha (alama 40)**

a)
i) t - nyepesi /sighuna/haitingizi nyuzi za glota/haina mrindimo/H
ii) d- nzito /ghuna/hutingiza nyuzi za glota /hutetemesha nyuzi za glota/ina mrindimo /GH
(kutaja 1, tofauti 1 ) x2

b)
i) wa'lakini – kasoro/ dosari/ upungufu/ nomino
ii) wala'kini – hata hivyo/ kiunganishi
2x1

c) vibuzi√ vilikimbizwa√ na vijibwa√ vikali√. 4x½

d) dalili - ishara/alama
dhalili – kalili/ duni /pungufu/dhaifu
Sentensi: Askari dhalili alionyesha dalili za ugonjwa wa homa ya ndege. 1x2

e) i) wao
ii) sisi 2x1

f)
i) Kuonyesha maneno ya lugha geni. Tulikula "mbuta" tulipofika mjini.
ii) Hutumika kubainisha anwani ya filamu, vitabu, mjarida au vipindi vinapotajwa katika sentensi. Mfano: Kipindi cha "vioja mahakamani" huwaburudirisha wengi nchini Kenya.
iii) Kuonyesha dhana/ maneno ambayo hajatumikai sana / hayajakubalika rasmi/ yenye maana fiche.Mfano: Japo wanasiasa wanasema kuhusu "kung'atuliwa ", wengi hawajafahamu maana yake . 2x1

g)
i) gandama – Maji yamegandama na kuwa barafu.
ii) fichama - walipohisi hatari nyumbani, waliingia kichakani kujifichama humo. 2x2

h)

| | | | S | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | U | S2 | | |
| KN | | KT | | KN | KT | |
| N | V | T | | ɵ | T | N |
| Wanafunzi | werevu | watafadhiliwa | ilimradi | ɵ | wadumishe | nidhamu |

16x ¼= 4

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

i) Auma - kitondo
Muwa - kipozi
Kisu kipya - ala
3x1

j)
i) wakati wowote/ mazoea
ii) wakati maalumu/wakati mahususi 2x1

k)
i) A – WA
ii) YA – YA 2x1

L)
i) 'a' – kiambishi awali 1x1
ii) 'a' na 'ye' – viambishi tamati 2x½
iii) Tan: atakayeunganisha a na ye asipate

m)
i) fuata
ii) faa 2x1

n)
i) sababu / kusudi/nia
ii) wakati/msimu/muda 2x1

o) Yule mgeni ni machachari/Hawa walimu ni shujaa. 1x2

p) i) mfululizo wa vitenzi/ vitendo katika wakati uliopo
ii) hali isiyodhihirika. 2x1

q) Pata maarifa mengi; kuwa na ujuzi/ufahamu mwingi 1x1

**kuadhibu**

a) Hijai (h): Ondoa nusu alama kwa kila kosa litokeapo mara ya kwanza kufikia upeo wa alama tatu (makosa 6)
b) Sarufi (s): ondoa nusu alama kwa kila kosa litokeapo mara ya ya kwanza mradi pana alama kamili katika kijisehemu husika.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**4. ISIMUJAMII**

a.

- Huwa na matumizi ya lugha rasmi. Mfano: Lugha ya mwajiri na mwajiriwa hudumisha urasmi
- Huwa na adabu. Afisa wa cheo cha chini hamrejelea afisa wa cheo cha juu kwa heshima. Mfano: "Bwana mkurugenzi"; Mwalimu Mamboleo na kadhalika.
- Matumizi ya lugha sanifu hudumishwa. Stakabahi na mawasiliano rasmi hufunywa kwa lugha sanifu kama vile Kiingereza sanifu au Kiswahili sanifu.
- Msamiati huteuliwa kulingana na mada inayoshughulikiwa. Kwa mfano,ikiwa ni kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha, istilahi za uhasibu hutumiwa.
- Ubadilishanji na uchanganyaji msimbo unaweza kutokea, hasa mazungumzo yakiwa kati ya maafisa wa cheo sawa.
- Lugha nyepesi
  Afisa wa ngazi ya juu anapozungmuza na maafisa wa ngazi za chini huenda akatumia lugha nyepesi wanayoielewa ili wasimwone kuwa mwenye kiburi.
- Lugha ya kiswahili inaweza kutumika katika afisi za utawala wa mikoa. Aidha, lugha ya mama huweza kutumika katika afisa za machifu. Pia wakuu wa vijiji hutumia.
- Upashanaji zamu hutegemea wazungumzaji. Ikiwa mawasiliano ni kati ya afisa wa ngazi za juu na afisa wa ngazi ya chini, afisa wa ngazi ya juu ndiye atakayeelekeza upashanaji wa zamu.

5x1

**Baadhi ya hoja:**

b.

- Hutumiwa kufunzia vyuoni.
- Hutumiwa katika mawasiliano katika mikutano ya kimataifa.
- Ni nyenzo ya kutangazia kwenye idhaa mbalimbali.
- Hutumiwa katika maandishi ya majarida au magazeti.
- Hutumika katika utafiti.

- Ni chombo cha ajira.
- Hutumiwa kutafsiria sanaa maarufu za kimataifa.
- Hutumiwa kusambaza na kukuza utamaduni wa mwafrika
- Hutumika katika burudani.
- Hutumika katika teknohama /maendeleo ya kiteknolojia.
- Huchangia katika kukuza lugha zingine.
- Hukuza amani baina ya nchi mbalimbali.
- Ni kitambulisho cha watu wa Afrika Mashariki.
- Husawazisha watu wa mataifa mbalimbali.
- Hukuza michezo.
- Huendeleza biashara.
- Hutumika kama lugha rasmi katika umoja wa Afrika.
- Hutumika katika Bunge hasa bunge la Afrika Mashariki.
- Huunganisha mataifa hasa wa Afrika Mashariki.

Tan:
a) Si lazima mwanafunzi ajirejelee kuhusiana na dhana ya kimataifa kwa kila mstari.
b) Kadiria jibu la mwanafunzi.

(Kutaja ½ mfano/maelezo ½ )

**Kuadhibu**
S : Adhibu kosa litokeapo kwa mara ya kwanza hadi upeo wa alama 2 (makosa 4)
H: Ondoa nusu maki kwa makosa yatokeapo kwa mara ya kwanza hadi upeo wa alama 2(makosa 4)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**
**KISWAHILI KARATASI YA TATU (FASIHI) LAINNAKU 1, 2020**
**SWALI LA KWANZA – LAZIMA – KIGOGO**

1. a) Msemaji – Bi. Hashima kwa Siti wakiwa kwake Bi. Hashima. Siti amewatembelea kuwajulia hali. Anajuza Bi. Hashima kuwa walitupiwa vijikaratasi vya kuwataka kuhama Sagamoyo.
4 x 1 = 4

b) Tamathali
i) Jazanda/istiari Siafu – wanyonge.
ii) Msemo – kuliziba kwa ungo. 2 x 2 = 4

c)
- Kuanza harakati za ukombozi. Tunu na Sudi.
- Kukataa ushawishi. Sudi.
- Kuwatia hofu viongozi dhalimu – Sudi kuwajuza wanachunguzwa.
- Kuwazindua wanyonge.
- Kuchunguza mienendo ya viongozi dhalimu.
- Kuwaita/kukusanya na kuwaongoza kukabili viongozi dhalimu.
- Migomo ya wauguzi na walimu.
- Kuwakabili viongozi dhalimu moja kwa moja.
- Maandamano.
- Mikutano ya hadhara.
- Kuamua kuunga mkono uongozi ufaao
- Kukataa ajira – Ashua.
- Kususia mikutano ya Majoka.
- Matumizi ya vyombo vya habari. Runinga ya Mzalendo.
- Upelelezi kutoka nje.
- Ufadhili kutoka nje wa wapiganiaji haki.
- Kusomea uanasheria – Tunu.

(funge za kwanza 12 x 1 = 12)

**SEHEMU YA B: RIWAYA : CHOZI LA HERI**

2 a

(i) Maneno ya msimulizi, yanahusu Dick akikumbuka rafikiye Lemi aliyeuawa na umati. Anakumbuka anapotishwa na Buda angetupwa nje na kusingiziwa wizi. Hofu hii inamchochea kuingilia ulanguzi wa dawa za kulevya. 4 x 1 = 4

(ii) Tamathali
- Tashihisi – akili ilimtambia kisa.
- Chuku – si kawaida hadithi kutamba kisa.
- Mbinu rejeshi – alikumbuka.

(za kwanza 2 x 1 = 2)

(iii) Umuhimu wa Dick
- Kuonyesha nafasi ya familia katika malezi
- Kukashifu ufisadi. Maafisa wa usalama.
- Kukashifu matumizi ya madawa ya kulevya.
- Anachimuza maudhui ya mabadiliko – Anabadilika.
- Anaonyesha nafasi ya vijana kuboresha maisha katika jamii zao.
- Anajenga wahusika wengine k.m. Mwangeka.
- Kuendeleza ploti/mkondo wa hadithi. Kisa cha Lemi.
- Anakashifu suala la ulanguzi wa watoto.
- Kuonyesha ukatili wa jamii.
- Anasawiri ukatili wa Sauna.
- Umuhimu wa ujasiriamali – biashara.

Zozote 4 x 1 = 4

b) Changamoto zinazowakumba vijana wengine.
- Madawa ya kulevya – Kipanga
- Kurandaranda mitaani – Hazina
- Mimba za mapema - Zohali
- Tohara - Pete
- Kubakwa – Sauna na babake mlezi.
- Umaskini – Pete kutumia tambara kama sodo
- Uavyaji mimba – Pete anajaribu.
- Gharama ya juu ya maisha vyuoni – Kijana mmoja analalamika
- Ahadi za uongo.-wanasiasa
- Kuadhirika kisaikolojia – Chandachema kwa Bw. Tenge.
- Vijana kutopewa ruzuku chuoni.
- Tamaduni potovu – Tuama kujipeleka kupashwa tohara
- Ubaguzi shuleni - Ridhaa
- Utengano wa kifamilia – Dick, Mwaliko na Umu
- Kutumiwa na viongozi kuanzisha vurugu-Hitman
- Ukosefu wa ajira – Shamsi anabugia vileo
- Malipo duni Pete kwa Patel. Shilingi mia mbili.

(za kwanza 10 x 1 )
Kadiria jibu la mwanafunzi

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

3. Mbinu

a) Mbinu rejeshi
- Ridhaa anakumbuka matukio kabla ya kuchomeka kwa nyumba na familia yake.
- Mazungumzo kati ya Ridhaa na bintiye Tila.
- Mandhari ya nyumba ya Mwangeka.
- Mazingira shuleni Tangamano ambako mwalimu Dhahabu anafunza.
- Visa vya Kairu, Mwanaheri, Zohali, Chandachema wanasimulia masaibu yao.
- Visa vya Pete, Sauna na Neema.
- Kisa cha Lemi ambacho Dick anakitamba.
- Kisa cha Mwangeka, Mwangemi na babu yao.
- Mzee Kedi alivyohusika kuteketeza mali ya Ridhaa.
- Mamake mwangeka alivyokuwa mbabedume.

- Mwangeka walivyohusiana na mjukuu wake Becky.
- Mwangeka anakumbuka bibi yake baada ya hotuba ya Apondi.

(zozote 10 x 1)

b) kinaya

- Ridhaa anamwambia bibi yake aache fikra za kijadi ilhali yeye anatishwa na Milio ya kerengende na bundi.
- Mwangeka kwenda kudumisha amani familia yake inaangamia kutokana na ukosefu wake.
- Ingawa Ridhaa ana ujuzi katika taaluma ya utabibu anashindwa kuokoa familia yake.
- Hata baada ya wahafidhina kupata uhuru miaka hamsini iliyopita bado wanawategemea hao hao walowapa uhuru.
- Ridhaa anakwenda kufanyia mgonjwa upasuaji kuyaokoa maisha yake anaporejea familia yake imeangamia.
- Wahafidhina wanakuza kahawa badala ya kuisaga wanawauzia wageni na kisha kuinunua kwa bei ya juu.
- Majirani wa Ridhaa waliomuita 'Ndugu' ndio wanaokuja kumchomea nyumba.
- Kedi kuchoma nyumba ya Ridhaa aliyedhamini masomo ya wapwa wake wawili.
- Kedi kumsaidia Ridhaa kupata shamba baadaye anahusika kumchomea.
- Mkewe Kedi amekuwa rafiki wa mke wa Ridhaa hali anamwacha achomekee jumbani mwake.
- Ridhaa amehusika kuleta maendeleo kijijini mwake ilhali bado wanamwona kama mgeni.
- Vijana wanawapigia kura viongozi dhalimu kila baada ya miaka mitano huku wakijua hawakutimiziwa ahadi za hapo kabla.
- Viongozi badala ya kuwaelekeza vijana wanawatumia kendeleza njama zao.
- Hazina ya Jitegemee inayonuiwa kuwainua vijana inaishia kuwanufaisha familia za viongozi.
- Maafisa wa usalama badala ya kudumisha amani wanawatazama raia wakiuana.
- Lunga analalamikia uharibifu wa mazingira ilhali babake anashiriki kuyaharibu.
- Watoto wa Kangata kujinasibisha na mwajiri wa babayao ilhali baba yao yuko.
- Mwalimu Fumba kumwendea kinyume mwanafunzi wake Rehema badala ya kumwelekeza.
- Polisi kumuuliza Umu ndugu zake walimwambia wanaenda wapi ilhali amewaambia walipotea.
- Mamake Sauna badala ya kumwelekeza anamlazimisha kutungua mimba.

(zozote 10 x 1 = 10)

Tathmini jibu la mwanafunzi.

**SEHEMU YA C. HADITHI FUPI.**

4 a) Maneno ya Kidawa, kwa mumewe Dadi wanapita njiani pale Kidawa anamwona Dadi akiwatumbulia macho wanawake waliovaa nguo fupi. 4 x 1 = 4

b) mbinu mbili za kimtindo

i) balagha – wa uhuru?
ii) kuchanganya/kuhamisha ndimi My dress, my choice
iii) Kejeli – Kidawa kumkejeli Dadi.

(za kwanza 2 x 1= 2)

c) Mwanamke wa kisasa

- Huvaa mavazi ya kisasa.
- Hutangamana na wanaume.
- Amesoma.
- Hufanya kazi hata ya usiku.
- Humgawia mumewe kazi za nyumbani.
- Hupanga uzazi.
- Hujipondoa.
- Anadai apewe uhuru.
- Si lazima ajifunike gubigubi.
- Hufanya kazi zaidi ya moja.
- Ana bidii kazini.
- Lazima apelekewe posa.
- Hufanyisha mtihani mwanamume anayemtaka na lazima apite.
- Ana uhuru wa kuonyesha ukaidi au utukutu.

zozote 7 x 1 = 7

d) Uozo wa kijamii – Mame Bakari

- Janadume linampachika mimba.
- Kufukuzwa nyumbani.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Kuadhibiwa na wazazi.
- Kutoaminiwa na wazazi.
- Kutengwa na mjomba, ndugu na hata mama.
- Kufukuzwa shuleni.
- Kutengwa na jamii.
- Kusemwa na majirani.
- Mauaji – kuavya mimba.
- Mauaji – janadume linauawa na umati.
- Masumbuko ya kisaikolojia.
- Uoga kwa wazazi.
- Hisia za kujiua.
- Janadume linambaka Sara bila huruma.
- Linamwacha uchi akiwa amepoteza fahamu.
- Linamvunja ubikira.

(zozote 7 x 1 = 7 )

5 a) Ubadhirifu "Shibe inatumaliza."

- Ingawa Mzee Mambo ni waziri hana wizara yoyote.
- Anatatoka kwake Kombora na kurejea kulala bila kufanya kazi yoyote.
- Anapata mshahara bila kufanya kazi yoyote.
- Wao hupakua mshahara.
- Waliobarikiwa wanaamini wamebarikiwa na hawawezi kupokonyeka.
- Sherehe kubwa inaandaliwa kusherehekea kifungua mimba kuingia nasari na mnuna wake kuota meno mawili.
- Sherehe ya kibinafsi kupeperushwa katika runinga ya taifa
- Matukio yale kuwekwa katika mitandao ya kijamii.
- Magari ya serikali kutumika katika shughuli za kibinafsi
- Watu shereheni kula kutoka asubuhi.
- Kuna vyakula vya kila aina katika sherehe hii.
- Hakuna upishi pale ila watu wanaendelea kula bila kujali.
- Matumbo ya Sasa na Mbura yanashindana kunguruma.
- Sasa na Mbura wanakurupuka na kupiga foleni kupata chakula wanachokila kilafi.
- DJ anacheza wimbo wa "Sijali Lawama."
- DJ na wenzake wanachota mabilioni ya pesa za serikali.
- Duka la DJ kuiba madawa kutoka bohari la serikali
- DJ anapata maji na umeme bila kulipia.
- Watu wanakula vyao na vya wenyewe.
- Watu wanakula wanachokijua na wasichokijua.
- Wanakula bila kujua vilikotoka wala vilikopikiwa.

(zozote 8 x 1 = 8 )

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) mtindo

- uzungumzi nafsi – wa Mzee Mambo.
- balagha – maana yake nini hasa?
- kinaya – kurudi kulala bila kufanya kazi yoyote.
- msemo – kulegeza ulimi.
- kuchanganya ndimi –huku third world.
- kuhamisha ndimi – let me tell you.
- Taswira/uoni – ya Mzee Mambo
- Takriri – Yah, Yah!
- majazi – Kombora – alfajiri kubwa.
- chuku – Mzee Mambo kutoweza kabisa kuelezea kuhusu kazi zake.

(Zozote 6 x 2 = 12)

Kumbuka: katika kujibu maswali ya tamthilia, riwaya na hadithi fupi lazima mtahiniwa ahusishe kitabu hicho. Kwa kutoa mifano maalum.

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

6. Dhamiri yangu.

(a)

i) kufungwa kama mbuzi.
ii) kunyimwa uhuru.
iii) alipofungwa pameharibika.
iv) angependa kuhama lakini hawezi.
v) kuna chakula/majani mengi mbele yake lakini hayafikii.
vi) ufupi wa kamba.
vii) upungufu wa chakula/njaa.

(Za kwanza 4 x 1 = 4)

b) Amekwishazoea hali yake/hapendi kuonekana tofauti/hana msimamo wake/hataki kuleta madhara

( 1x2)

c) Dhamiri iliyo akilini mwake ndiyo iliyomfunga.hajafungwa na yeyote/amejifunga na nafsi yake.

(1x2)

d) Tamathali

– Tashbihi – kama mbuzi.
– istiara – sahani ya mbingu.
– jazanda – mti wa utu.
– Tasfida – nimekwisha pachafua.
– Takriri/uradidi – kamba kamba.
– Nidaa/siahi – Oh!
– Tashihisi/uhuishi – Dhamiri imenifunga.
– Taswira – kamba fupi.
– Tanakuzi – anataka kufunguliwa lakini hataki.
– kinaya – Namshukuru aliyeifunga.

(Za kwanza 2x2 = 4)
(atoe mifano mwafaka)

e) Mishata: Mishororo ambayo maana yake haijakamilika bali hukamilika katika mshororo unaofuata k.m.

– Nami kwa mbaya bahati, katika
– Nimepiga teke na nigusapo kwa mdomo
– Nami sitaki ikatike maana
– Mbuzi wa kamba alipofunguliwa mashamba
– Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena (zozote 2x2 = 4)

f) Nimefungwa kama mbwa na kwa bahati mbaya katika kutaka kuondoka pale nimeipiga teke sahani ya mbingu ambayo imeenda mbele na siwezi kuifikia na pale nilipofungiwa ni pachafu. (4 x 1 = 4)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

7.

a) kupigania uhuru/haki/kujiendeleza kiuchumi.
walishiriki/walisimama/walitaka milki pamoja

(Kutaja 1) (Kueleza 1) (1x2 = 2)

b) kinaya

– viongozi kujinufaisha – raia maskini.
– viongozi raha – raia dhiki.
– viongozi kudharau raia – kuwatemea mate.
– raia kupigania uhuru – kutofaidika.
– kutoafikia maazimio – milki ya haki.
– walianza safari pamoja – mwishowe wanabaguliwa . (6 x 1 = 6)

c) (i) mizani – msuko – mshororo wa mwisho umefupishwa.
(ii) vina – ukara – vina vya kati vinabadilika vya tamati vinatiririka.

(Kutaja 1 kueleza 1 (2x2=4)

d) Mshairi analalamika kuwa viongozi walipofikia hali nzuri ya maisha tamaa ilizidi huku wakiwa na starehe za kila aina huku wakiwasahau waliowapa nafasi za uongozi ili kufikia hali yao ya sasa. (4 x 1 = 4)

e)

i) Inkisari – Tukawa`chia – Tukawaachia – kutosheleza mizani.
ii) Kuboronga sarufi – kialeni wadiriki – wadiriki kialeni – urari wa vina.
iii) Tabdila – shaki – shaka – urari wa vina.
iv) (iv) Lahaja/kikale – kialeni - kileleni – upekee wa msamiati/mapigo ya kimziki.
(za kwanza 2 x 2 = 4)

8 a

- majigambo/kivugo (1 x 1)
- Shughuli za kiuchumi
- Usasi – kwenye misitu sikuwa na kifani.
- Ufugaji – mafahali na mitamba.
- Wizi wa mifugo . (2 x ½ = 1)

Shughuli za kijamii

- Wizi wa mifugo.
- Uchezaji ngoma.
- Upiganaji mieleka.
- Ndoa – makoo kulilia nikaha. (2 x ½ = 1)

(iii) Ili kufanikisha uwasilishaji anayejigamba

- Avae maleba.
- Abadilishe toni.
- Kuigiza vitendo.
- Kupandisha na kushusha kidatu, sauti.
- Kuhusisha hadhira.
- Kuimba kwa kasi au wastani.
- Kutumia ishara.
- Kutumia ala zinazoafikiana na ujumbe.
- Kutumia miondoko.
- Sauti inayosikika. (4 x 1)

(iv)

- Huchangia ngano iburudishe zaidi.
- Husisitiza dhamira/wazo.
- Ni kipumuo kwa hadhira.
- Huondoa uchovu/.ukinaifu.
- Hufumbata baadhi ya maudhui.
- Hurefusha au kufupisha matukio hadithini.
- Kuhusisha hadhira.
- Kutenga matukio/migogoro.
- Huchochea hisia anazonuia mtambaji kupata.
- Kusawiri baadhi ya tabia/sifa za mhusika katika ngano.

(za kwanza 3 x 1 = 3)

b) (i) Hojaji

- manufaa/umuhimu
- Gharama ya chini.
- Kufikia idadi kubwa kwa kutuma hojaji.
- Mwongozo katika mbinu ya mahojiano.
- Mhojiwa hupata fursa ya kuwazia majibu ya maswali.
- Haziathiri mtafiti mara nyingi hayupo nyanjani.
- Inaweza kubadilishwa kulingana na kiwango cha elimu cha wahojiwa.

(Za kwanza 5 x 1 = 5)

(ii) Changamoto

- Maswali tata huleta utata kuyafasiri.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Watu kukosa kujaza hojaji kwa kikamilifu.
- Ikiwa ndefu watu wanaweza kukataa kuijaza.
- Hojaji wazi huwa ngumu kuchanganua data.
- Wahojiwa kudanganya.
- Wahojiwa kuchelewa kurejesha hojaji zao.
- Haiwezi kujazwa na wasiojua kusoma na kuandika.
- Baadhi ya sifa za fasihi simulizi k.v. toni na kidatu hupotea.

(Za kwanza 5 x 1 = 5)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO**
**MTIHANI WA KUHITIMU SHULE ZA SEKONDARI**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA, 2020**
**KISWAHILI-KARATASI YA 1**

**1.LAZIMA**
wewe ni katibu wa kamati inayochunguza jinsi ya kupunguza tatizpo kuu la uhaba wa kazi kwa vijana nchini Kenya. Andika ripoti ukitoa mapendekezo ya kamati.

2. ushauri-nasaha una manufaa kwa wanafunzi wa shule sekondari. Eleza
3. Andika insha itakayodhihirisha methali ifuatayo:
   Mchumia juani hulia kivulini.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo:
   ………….nilielewa fika kuwa "mgagaa na upwa hali wali mkavu."

**KIGUMO**
**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA 2**

1.**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Pindi jamii inapoendelea kupiga hatua kimaendeleo ndivyo mabadiliko yanavyotokea katika nyanja za maisha. Baadhi ya mabadiliko haya ni chanya ilhali mengine ni hasi. Kati ya mabadiliko hasi katika sekta ya afya ni kukithiri kwa idadi ya watu wenye unene wa kupindukia.

Unene wa kupindukia unaweza ukasababishwa na mambo mengi. Mojawapo ni watoto kurithi jeni za hali hii kutoka kwa wazazi. Kuna familia ambazo zinatambulikana kuwa na hali hii ya unene ambayo watoto huweza kurithi.

Hata hivyo mchango mkubwa wa hali hii ni tabia ya kupapia lishe yenye wanga mwingi au chakula kinachoupa mwili joto, na chakula kisicho na virutubishi vyenye thamani, hasa asusa zilizotayarishwa na kupakiwa.

Matumizi ya vyakukla na vinywaji vyenye sukari nyingi pia huchangia unene huu. Hulka za anasa kama vile ubugiaji pombe kupindukia na ulaji nyama, hasa zenye mafuta mengi, huchangia kuleta unene wa kupindukia. Ukosefu wa mazoezi ya kunyoosha viungo na utegemezi wa magari na mashine katika utenda kazi nao huchangia kuongeza unene wa kupindukia.

Aghalabu wanawake hupata unene wa kupindukia wawapo wajawazito na wanaponyonyesha. Jamii huwahimiza wajawazito kula sana, hasa vyakula vya kuongeza uzito mwilini. Mama huonekana kuwa anahitaji kula maradufu kwani anahitaji chakula chake na cha kiumbe aliye tumboni. Vivyo hivyo, huhimizwa kula sana anapojifungua ndipo apate maziwa ya mtoto anayemnyonyesha. Matokeo ya haya ni unene wa kupindukia.

Unene wa kupindukia hauna mipaka. Hutokea kwa watoto, vijana na wazee. Lakini unafahamika kujikita zaidi katika jamii ambazo zaimeinukia kiuchumi. Hii ni kwa kuwa kundi hili ndilo hushikilia hulka za maisha ya kisasa ambazo huchangia kuleta unene wa kupindukia. Watu wengi siku hizi huwa na shughuli nyingi ambazo zinawazuia kupata muda wa kunyoosha viungo. Wengi hulaza damu na hawajui thamani ya kunyoosha viungo kiafya. Wengi nao hushughulikia mambo yasiyo na manufaa kama kushinda na kukesha katika baa.

Watu wengi siku hizi wanategemea magari hata kwa masafa mafupi ambapo mtu angeenda kwa miguu. Kuenda kwa miguu kunasaidia kupunguza uwezekano wa kupata unene wa kupindukia. Hata kuosha vyombo siku hizi kunafanywa na mashine ambazo zimewapunguzia watu utendaji wa kazi za sulubu.

Unene wa kupindukia huhushiswa na matatizo mengi ya kiafya. Unene huambatana unyounyo na mpumuko wa shinikizo la damu, maradhi ya moyo na ugonjwa wa kisukari. Aliye na shinikizo la damu anaweza kupata kiharusi kwa urahisi.

Huu ni ugonjwa unaosababisha kupooza kwa mwili. Kuna kupooza kunakoweza kutibiwa, kwingine kunamlemaza mtu na kuna kunakoweza kuleta kifo cha ghafla.

Aghalabu, mwenye unene wa kupindukia hushindwa kutembea na hata kufanya kazi. Akitembea kwa masafa mafupi, atahema na utadhani amevunja rekodi ya masafa marefu ya mbio za nyika. Kulala kwao nako ni kwa shida kwani wengi hushindwa kupumua vizuri. Zaidi ya haya miguu wakati mwingine hulemewa na uzito mkubwa. Watu kama hawa hupata ajali za kuvunjika mifupa kwa urahisi. Hata ufanyaji kazi wao hutatizwa. Wengi huhisi uchovu kila wakati.

Matabibu huwashauri watu walio na unene wa kupindukia kupunguza uzito huo iwapo watataka kujinusuru na hatari zote zinazoletwa na unene huu. Hata hivyo, kupunguza unene si jambo rahisi na huhitaji kujitolea na uangalifu mwingi ili kudumisha kiasi ambacho si hatari kiafya.

Njia moja ya kupunguza unene ni kupitia kwa lishe, wataalamu wa lishe bora huweza kushauri aina za vyakula na kiasi ambacho kitamwezesha mtu kupunguza unene. Mara nyingi, mtu hupendekezewa kutokula chakula chenye wanga kwa wingi. Hukatazwa pia kula vyakula vilivyosindikwa na nyama zenye mafuta mengi. Pamoja na haya, ni kupunguza matumizi ya vyakula na vinywaji hivi kwani huzidisha uzani.

Hali kadhalika, wataalamu hushauri mtu kufanya mazoezi ya kunyoosha viungo. Mazoezi haya yana mchango mkubwa katika kupunguza unene. Hata hivyo, wengi huona ugumu kwa kuwa hawajazoea haya. Ushauri hutolewa pia dhidi ya watu kukaa kwa wakati mrefu katika tarakilishi, televisheni na utegemeaji wa magari sana.

Wataalamu hushauri kuwa kupunguza unene si jambo la mtu kujiadhibu kwa kujinyima chakula wala kuzingatia baadhi ya vyakula visivyo na ladha. Husema kuwa kula kiasi kidogo cha lishe bora na kufanya mazoezi kunatosha.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) " Asilimia kubwa ya vyanzo vya unene wa kupindukia hutokana na mienendo ya binadamu." Tetea kauli hii kwa mujibu wa kifungu. (alama 4)

b) "Unene wa kupindukia unafahamika kujikita katika jamii ambazo zimeinuka kiuchumi." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hoja nne kutoka kwa kifungu. (alama 4)

c) Eleza madhara ya unene wa kupindukia (alama3)

d) Bainisha sababu tatu zinazoonyesha kuwa kupunguza unene si jambo rahisi na huhitaji kujitolea na uangalifu mwingi. ( alama 3)

e) (i) Andika kisawe cha **bugia pombe**. ( alama 1)

(ii) Andika maana ya **lishe** **(alama1)**

**1. UFUPISHO ( ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Marundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tishio kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka ni makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya sandarusi, huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali.Mifuko ya sandarusi ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati wa mvua za gharika. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa na mifuko hii. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa pori na majini.

Kwa sababu zitokanazo na taka, pana haja ya kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na rasilimali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano, maji ni rasilimali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Rasilimali hii inaweza ikatumiwa kwa njia endelevu. Kwa mfano, badala ya kutumia bafu ya manyunyu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu. Wengi, kwa kukosa hela za kununulia mipira ya viwandani,

hutumia karatasi na mifuko ya sandarusi kutengeneza mipira wanayoitumia kucheza. Hii ni teknolojia endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu kwa ada. Kisha huzipeleka taka hizi kule zitakapobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya sandarusi hupelelekwa katika viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki kama matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengeneza bidhaa nyingi.

Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyovigeuza na kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengeneza bidhaa kama vitabu, kotoni shashi za choo na magazeti.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka, kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazolishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mijini katika maeneo ya biashara kama mikahawa na hospitali.
Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira na yenye manufaa kemkemu. Kwanza, hugeuzwa taka ambayo huweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo, hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumika kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Aghalabu watu wengi  wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule na hospitali. Badala ya kupoteza moto huu bure bilashi, inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemsha maji. Maji haya yanaweza yakatumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuvitupa vifaa katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo.

Kwa vyovyote vile, si jambo muhili kwa watu popote wapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utumiaji huu huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 70. ( alama 9 ,1 ya mtiririko)
**Matayarisho**
Jibu

b) Eleza jinsi taka zinavyoweza kutumiwa kwa manufaa ya waja. (alama 6,1 ya mtiririko)
**Matayarisho**
**Jibu**

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ( ALAMA 40)**

a) Linganisha sauti zifuatazo ( alama 2)
i) /m/ na /ng'/ ……………………………………………………………………………………………
ii) /j/ na /gh/
iii) (iii) /t/ na /f/
iv) /th/ na /z/

b) Andika neno lenye silabi inayochukua muundo wa konsonanti,konsonati,nusu irabu na irabu. ( alama 1)

c) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo. ( alama 2)
i) Lililokunjwa
ii) Mikate

(d) Andika sentensi ifuatayo kwa **wingi** ( alama 2)
Lililosemekana kuwa ni lake limeharibiwa na binamuye.

(e) Onyesha miundo miwili ya nomino katikla ngeli ya **U-I** ( alama 1)

(f) Onyesha majukumu yanayotekelezwa na kiimbo katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Toka nje haraka!
ii) Nipikie wali tafdadfhali.

(g) Bainisha matumizi ya ' ni' katika sentensi ifuatayo. ( alama 2)
Mkamateni Omondi ambaye ni mtoto wangu niliyempeleka shuleni.

(h) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani ?
i) chai ……………………………………………..
iii) nyasi……………………………………………….

i) Kwa kutunga sentensi, bainisha matumizi mawili ya alama ya mshazari katika uakifishaji. (alama 2)

(j) Ainisha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwanafunzi mtiifu atanunuliwa kitabu kipya na babake kesho jioni.

(k) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. ( alama 2)
Alisema angeenda kwao.

(l) Ainisha **virai** vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. ( alama 2)
<u>Tuwachague viongozi wazuri</u> <u>wenye bidii na uadilifu</u>.

(m) Tambua vishazi katika sentensi zifuatazo. (alama2)
i) Maina hucheka anaponiona.
ii) Endapo atafika atanipata nyumbani.

(n) **Changanua** sentensi ifuiatayo kwa kutumia **jedwali**. (alama 2)
Angali anafunzwa na mwalimu.

(o) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: **gari** na **ghali** (alama 2)

(p) Tumia '**kwa**' katika sentensi kuleta dhana zifuatazo (alama 2)
i) Pamoja na ……………………………………………………………………
ii) Sababu ya kutenda jambo.

(q) Andika upya sentensi ifuatayo katika **usemi halisi**. (alama 2)
Mtahini alisema kuwa kujibu maswali kwa usahihi kungewahakikishia matokeo bora katika mtihani huo wao.

(r) Jaza pengo ukitumia maneno yaliyo katika parandesi katika hali inayofaa; (alama 2)
Mwanafunzi mwenye………………(buni) huwafanya ………… (elimu) wake kufurahia.

(s) **Yakinisha** sentensi hii katika **umoja.** (alama 2)
Msipohama hapa hamtapewa makazi mapya.

(t) Unganisha sentensi hizi ukitumia **kiunganishi cha kukubali**. (alama2)
i) Wananchi walikabiliwa na hatari.
ii) Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

(u) Andika **kinyume** cha: (alama 2)
Mwanamume aliyejasirika kuangua bendera haraka amesifiwa.

(v) Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo. (alama 2)
Ng'ombe watatu waliibiwa na wezi hao.

**ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**.

Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa, mahakama imethibitisha kuwa una shtaka la kujibu…

(a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mifano miwili kwenye makala. (alama 2)

(b) Eleza sifa nyingine **nane** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO**
**MTHANI WA SHULE ZA SHULE ZA UPILI**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**
**KARATASI YA 3**

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

**1 a.**

Umepewa jukumu la kutafiti kuhusu michezo ya watoto katika jamii yako.

(i) Taja eneo ambalo utafanyia utafiti wako. (alama 2)

(ii) Fafanua mbinu ambazo utatumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za uteuzi wako. (alama 10)

b. Jamii ya waluo wana ohangla,
Waluhya wana Isukuti,
Wakikuyu wana mwomboko
Wakamba wana wathi na kilumi
Waswahili wana chakacha

(i) Tambua kipera kinachorejelewa katika maelezo haya (alama 2)

(ii) Fafanua dhima ya kipera hiki (alama 6)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**
**Jibu swali la 2 au 3**

**2.** "Vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Tambua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)

**c)** Jadili sifa tatu za msemaji. (alama 3)

**d)** Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya. (alama 11)

**Au**

**3.** Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)

**SEHEMU YA C TAMTHILIA; KIGOGO NA PAULINE KEA**
**Jibu swali la 4 au 5**

4 Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (alama 4)

(c) Eleza matatizo yanayoikumba safari inayorejelewa. (alama 12)

5. Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. Ukirejelea tamthilia ya Kigogo, ipatie nguvu kauli hii. (alama 20)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
**Jibu swali 6 au 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo! Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mweyewe!

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya shairi hili (alama.2)
b) Tambua njia **mbili** anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (alama 2)
c) Taja na utoe mifano ya aina **nne** za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (alama 4)
d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha nathari/tutumbi (alama 4)
e) Kwa kutoa mfano **mmoja mmoja** onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili (alama 4)
f) Bainisha toni ya shairi hili (alama 2)
g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi (alama 2)
   i) mstahiki
   ii) hupuliki

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nikiwa na njaa na matambara mwilini
Nimehudumika kama hayawani
Kupigwa na kutukanwa
Kimya kama kupita kwa shetani
Nafasi ya kupumzika hakuna
    Ya kulala hakuna
    Ya kuwaza hakuna
Basi kwani hili kufanyika
Ni kosa gani lilotendeka
Liloniletea adhabu hii isomalizika?

Ewe mwewe urukaye juu angani
Wajua lililomo mwangu moyoni
Niambie pale mipunga inapopepea
Ikatema miale ya jua
Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?
Je nadhari hujitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?
Mpenzi mama, nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama maiti yangu imekatikakatika
    Vipande elfu, elfu kumi
    Nitarudi nyumbani

Nikipenya kwenye ukuta huu
Nikipitia mwingine kama shetani
Nitarudi mpenzi mama...
Nitarudi hata kama kifoni.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Tambua nafsineni katika shairi hili (alama 2)
c) Eleza toni katika shairi hili (alama 2)
d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (alama 4)
e) Fafanua dhamira katika shairi hili (alama 2)
f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (alama 2)
g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (alama 2)
h) Fafanua mbinu tatu za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (alama 3)
i) Eleza maana ya maneno yafuatoyo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (alama 2)
   i) hayawani
   ii) nadhari

**SEHEMU YA E: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA.**
**Shibe inatumaliza: Salma Omar Hamad**

**8.** "Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine?"
**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b)** Eleza sifa za msemaji. (alama 6)
**c)** Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

**KIGUMO**
**MWONGOZO WA KUTAHINI INSHA(102/1)**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA 2020.**

**1.** Hii ni insha ya ripoti vipengele vya:
(a) Kimuundo vya utungo wa aina hii vidhihirike kama ifuatavyo:

(i) Kichwa kionyeshe:
- Kamati au kundi la wachunguzi
- Mada ya ripoti
- Kipindi cha wakati
- Kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(ii) Utangulizi uhusishe:
- Uelezee kwa muhtasari jambo linaloandikiwa ripoti
- Orodha ya wanajopo waliohusika
- Muda uliotumika kufanya uchunguzi/ utafiti
- Tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti

(iii) Mbinu za ukusanyaji data m.f
- Utafiti wa nyanjani
- Mahojiano
- Hojaji
- Upelelezi
- Kurejelea na kusoma ripoti na makala mengine kuhusu ripoti husika

(iv) Mwili
- Hufafanua matokeo ya utafiti/ uchunguzi
- Huandikwa mada ndogondogo
- Kila mada izungumzie mada moja pekee
- Hitimisho

Aandike chini ya kijianwani cha hitimisho.

(v) Mapendekezo
- Yaorodheshwe kwa nambari.
- Yapendekeze suluhisho/ hatua za kuchukuliwa.

(vi) Hitimisho/ kimalizio
m.f ripoti imeandaliwa na kuandikwa na

Sahihi ______________
Jina _________

Wadhifa ____________
Tarehe ______________

**MAUDHUI**

- ✓ Kuongezea/ kujenga viwanda zaidi/ kubuni nafasi za kazi
- ✓ Kuanzisha taasisi za kufunza kazi za kifundi
- ✓ Kutoa ufadhili wa kifedha kwa vijana m.f mikopo ili kuanzisha biashara
- ✓ Kuimarisha kilimo nchini kwa kuongezea bei za mazao shambani ili kuwavutia vijana katika kilimo
- ✓ Kupunguza umri wa kustaafu
- ✓ Kuhimiza vijana kutumia teknolojia ya kisasa ili kujiajiri m.f simu
- ✓ Kutambua na kukuza vipawa/ talanta za vijana.
- ✓ Kuhamasisha vijana kuhusu umuhimu wa kujiajiri

2. Utungo udhihirishe manufaa ya ushauri-nasaha katika shule za sekondari.

- Kukuza/ kudumisha nidhamu kwa wanafunzi.
- Kuadilisha/ kufunza maadili/ kujenga wanafunzi waadilifu
- Kusaidia katika kuifanya maamuzi mema katika maisha
- Kuepuka mtumizi ya mihadarati
- Kusaidia kukabiliana na changamoto za kimaisha
- Kusaidia kukuza mahusiano mema kati ya jinsia tofauti yaani ya kike na kiume.
- Kusaidia kuepuka ndoa za mapema
- Kusaidia kuepuka mimba za mapema
- Kusaidia kupita mitihani
- Kusaidia katika uteuzi wa masomo na mafunzo ya baadaye.
- Kukabiliana na unyanyapaa katika jamii
- Kufuata kanuni za afya
- Kukabiliana na changamoto za ukuaji m.f kubaleghe

3. Mtahiniwa atunge kisa kitakachodhihirisha maana ifuatayo:

- Mhusika kufanya kazi ngumu( juani) na mwishowe kufurahia matunda ya kazi yake(kivulini)
- Idhihirishe kuvumilia hali ngumu kazini na mwishowe kupata malipo mema
- Idhihirishe kufanya kazi kwa bidii na kuvumilia shida na baadaye kufurahia faida ya jasho la mhusika.

Hali zifuatazo zinaweza kuijtokeza:

- ✓ Mkulima kulima kwa shida na mwishowe kufurahia mavuno mengi/ mazuri
- ✓ Mwanabiashara kuvumilia hali ngumu ya kiuchumi na mwishowe kupata faida kubwa biasharani
- ✓ Mwanafunzi kusoma kwa shida na mwishowe kufurahia matoke mema
- ✓ Ndoa kupitia matatizo mengi na baadaye kudumu baada ya kushauriwa na kusherehekea kufanikiwa kwa ndoa
- ✓ Mwathiriwa wa ulevi/ mihadarati kupitia wakati mgumu katika harakati za kuacha/ kubadilika na hatimaye kufurahia kuacha kabisa
- ✓ Watoto kulelewa katika uchochole na baadaye wakasoma na kuajiriwa na kijikomboa kutoka uchochole

**TANBIHI:** sehemu zote mbili za methali zijitokeze.

4. Hii ni insha ya mdokezo:

*Mtahiniwa abuni kisa kitakachoafiki:*
*Mhusika anayejitahidi na hatimaye kupata.*
*Kisa kionyeshe juhudi ambazo zinapelekea kupata.*
*Kisa kionyeshe hali kujitahidi na kifanikiwa.*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**
**KISWAHILI 102/2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**UFAHAMU**

**(a)**

i) Kupapia lishe yenye wanga mwingi
ii) Matumizi ya vyakula vyenye sukari nyingi
iii) Ubugiaji wa pombe kupindukia
iv) Ulaji wa nyama hasa zenye mafuta mengi
v) Ukosefu wa mazoezi ya kunyoosha viungo
vi) Utegemezi wa kazi na mashine katika utendaji kazi 4x1

**(b)**

- Kundi hili hushikilia hulka za maisha ya kisasa ambazo huchangia unene
- Hutegemea magari hata kwa masafa mafupi
- Huosha vyombo kwa mashine kwa sababu ya kuwa na pesa
- Wao hushinda na kukesha katika baa
- Huwa na shughuli nyingi zinazowazuia kupata muda wa kunyosha viungo
- Wengine hulaza damu na hawajui thamani ya kunyoosha viungo kiafya 4x1

**(c)**

- Shinikizo la damu
- Maradhi ya moyo
- Kisukari
- Kiharusi
- Hushindwa kutembea na kufanya kazi
- Kutoweza kulala vizuri
- Miguu kulemewa na uzito mkubwa
- Kuvunjika mifupa kwa urahisi
- Kuhisi uchovu kila wakati 3x1

**(d)**

- Mtu hupendekezewa kutokula chakula chenye wanga kwa wingi
- Hukatazwa kula vyakula viliyosindikwa na nyama zenye mafuta mengi
- Kupunguza matumizi ya vyakula na vinywaji vyenye sukari na pia pombe
- Mtu huhitsjiks kufanya mazoezi ya kunyosha viungo
- Watu hushauriwa kutokaa kwa wakati mrefu katika tarakilishi televisheni na utegemeaji wa magari
  3x1

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**(e)**

- Piga maji 1x1
- Chakula chenye virutubisho kamili 1x1

**2.**
**UFUPISHO**

**(a)**

- Marundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji ni tishio kwa siha ya umma na mazingira
- Taka huwa ni makazi ya wadudu na wanyama waharibifu ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani
- mifuko ya sandarusi huziba mitaro ya maji
- Majitaka na mifuko ya sandarusi huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa
- maji hukosa njia na kusababisha mafuriko yaletayo hasara ya mali na uhai
- sandarusi huwasakama tumboni wanyama wa nyumbani na porini
- pana haja ya kutafuta njia na teknolojia ya kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya umma
- njia mojawapo ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na raslimali ili kupunguza uzalishaji wa taka 8x1

**(b)**

- ✓ vijana hutumia karatasi na mifuko ya sandarusi kutengeneza mipira wanyoitumia kuchezea
- ✓ hutumiwa kutengeneza bidhaa za plastiki kama matangi na mitungi
- ✓ hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu kotovu, shashi na magazeti
- ✓ taka hugeuzwa kuwa mboji
- ✓ hutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani
- ✓ hutumiwa kuchemshia maji ya kutumiwa nyumbani kwa kutumia tanuri 5x1

## 3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** i) nazali/ ghuna
ii) ghuna
iii) sighuna
iv) vikwamizo 1/2x4

**(b)** ngwena/ ndwele/ ngwafua/ chinjwa/ jengwa 1x1

**(c)**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| – Li - | li- | lo- | kunj- | w- | a |
| ngeli | wakati | kirejeshi | mzizi | kauli | kiishio |
| – Mi- | kate | | | | |
| wingi | mzizi | | | | 2x1 |

**(d)** Yaliyosemekana kuwa ni yao yameharibiwa na binamuze. 1x1

**(e)**
- mw-mi—mwavuli-miavuli
- m-mi—msumari-misumari 1/2x2

**(f)**
- amri
- ombi/rai 2x1

**(g)**
- mkamateni-wingi
- ni-kitenzi kishirikishi kipungufu
- ni liyepeleka- nafsi
- shule**ni- mahali 4x1/2**

**(h)** chai---I-I
nyasi—U-ZI 2x1/2

**(i)**
- kuandika tarehe 9/03/2020
- Maneno yenye maana sawa
- Kuonyesha au/ ama 2x1
- Kutenga shilingi na senti

**(j)**
- Mwanafunzi mtiifu- kitondo
- kitabu kipya- kipozi
- babake- kiima
- kesho jioni_ chagizo 4x1/2

**(K)** (i) Ataenda kwa mtu mwingine
(ii) Yeye ataenda alikozaliwa 2x1

**(l)** Tuwachague viongozi wazuri wenye bidii na uadilifu.
RT RV 2x1

**(m)** Maria hucheka-huru
anaponiona-tegemezi
endapo atafika-tegemezi
atanipata nyumbani- huru 4x1/2

**(n)**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **S** √ | | | |
| **KN** √ | **KT** √ | | | |
| O | **TS** | **T** | **H** | **N** √ |
| sss | **Angali** | **anafunzwa** | **na** | **mwalimu** |

4x1/2

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**(o)** Gari lake Habwe lilinunuliwa kwa bei ghali. 1x2

**(p)** (i) Wazee kwa vijana wamefika mkutanoni.
(ii) Aliadhibiwa kwa utukutu wake. 2x1

**(q)** **"** Kujibu maswali kwa usahihi ku**ta**wahakikishia matokeo bora katika mtihani **huu wenu**,"mtahini akatuambia/ akasema. 4x1/2

**(r)** ubunifu, walimu 2x1

**(s)** Ukihama hapa utapewa makazi mapya. 1x2

**(t)** Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi japo walikabiliwa na hatari. 1x2

**(u)** Mwanaume aliyeogopa kuangika bendera polepole alikashifiwa. 4x1/2

**(v)** Magombe matatu yaliibwa na majizi hayo. 1x2

**4. ISIMUJAMII**

**(a)** Sajili ya mahakamani/ kortini. Kuna kutajwa kwa maneno ushahidi, mahakama na shtaka. 1x2

**(b)**

- ✓ Kunukuu/ kurejelea vifungu vya sharia za nchi ili kuthibitisha ukweli wa mambo
- ✓ Kudadisi/ kuuliza na kujibu maswali ili kuthibitisha ukweli wa mambo m.f. mshtakiwa kutakwa ataje majina yake/ aeleze tukio Fulani
- ✓ Lugha ya unyenyekevu, heshima na adabu hususan upande wa hakimu na mshtakiwa mf. Mheshimiwa jaji, samahani/ kunradhi
- ✓ Matumizi ya lugha ya kukopwa kutoka lugha zingine ili kuhifadhi maana asilia ya neno km. amicus curiae( kilatini)
- ✓ Lugha shawishi hasa wakili anapomtetea mshtakiwa ili asihukumiwe k m. mteja wangu
- ✓ Lugha ya ishara hutumiwa kudhihirisha uhalisia/ ukweli wa mambo k.m shahidi kuashiria tukio aliloshuhudia
- ✓ Msamiati wa kawaida huwa na maana maalum unapotumiwa katika muktadha wa kisheria k.m my learned friend- mwanasheria mwenzangu
- ✓ Urudiaji ili kuondoa utata m.f unaweza kurudia uliyoyasema yaani mshukiwa aliiba
- ✓ Utohozi ili kudumisha maana katika msamiati wa mahakama m.f jaji-judge
- ✓ Kuzozana na kukatizana kauli hasa mawakili wanapowatetea wateja wao k.m mteja wangu hakuwa katika eneo la tukio
- ✓ Upishanaji zamu/ kupokezana zamu ili maelezo ya ushahidi yaeleweke kikamilifu
- ✓ Kuhamisha ndimi hususan wanapotaja vifungu vya katiba na sharia
- ✓ Kuchanganya ndimi m.f my learned friend **( za kwanza 8x1)**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO**
**MWONGOZO**
**MTIHANI WA KISWAHILI FASIHI**
**KIDATO CHA NNE**
**FASIHI SIMULIZI**

**1. (a)**

(i) Mandhari ambapo pana watoto wachanga wanaocheza uwanjani/darasani (1x2=2)

(ii) Fafanua mbinu ambazo utatumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za uteuzi wako. (alama 10)

- Kusikiliza-mtafiti anaweza kuwasikiliza Watoto wanapocheza na kusimulia visa vyao.
  Mtafiti atapata ujumbe asilia na halisi kwa sababu Watoto hawatatia chuku michezo yao
- Kushiriki-mtafiti anaweza kujiunga na Watoto katika michezo yao na kujirekodia anachokibaini katika ushirika huo.
  mtafiti huja karibu na Watoto na kupata habari za kuaminika moja kwa moja.
- Kurekodi-mtafiti anaweza kutumia vinasasauti, kanda za video, filamu au upigaji picha.
  mtafiti hupata habari za kutegemewa na anaweza kuzirejelea baadaye/kumbukumbu
- Uchunzaji/kutazama-mtafiti anashuhudia kwa macho michezo ya Watoto inapoendelezwa.

mbinu hii ni bora kwani utendaji hautaadhiriwa kwani wachezaji/washiriki hawatajua kuwa wanatazamwa.

- Kutumia Hojaji-mtafiti anaweza kutayarisha hojaji ambayo ataipelekea mhojiwa ambaye anapaswa kuijaza. mbinu hii ni bora kwani mtafiti anaweza kuwafikia watoaji wengi wa habari kwa wakati mmoja.
- Mahojiano-mtafiti anaweza kukabiliana ana kwa ana na waahusika anaonuia kupata maarifa kutoka kwao. mbinu hii inamwezesha mtafiti kupata ufafanuzi wa papo kwa hapo

**Zozote 5x2=10**

*Tan: Mtahini atoe mbinu, aifafanue kisha atoe sababu ili apate alama 2 katika kila hoja.*

(b). (i) kipera cha ngoma alama 2

(ii) Dhima ya Ngoma

- Kuburudisha
- Ni kitambulisho cha jamii
- Kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika
- Huleta utangamano katika jamii
- Huelimisha
- Hukuza uzalendo
- Kuhifadhi historia ya jamii zozote 6x1

**2.** "Vipi binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"

a)

- Haya ni maneno ya Mwanaheri
- Akimwambia Kairu na Umu
- Walikuwa katika shule ya Tangamano
- Ni baada ya kukutana na kuanza kusimuliana kuhusu yaliyowafika hadi wakakutana pale

zozote4x1

b) Swali balagha - vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?
Methali-Maji yakimwagika hayazoleki.
Jazanda-maji yaliyomwagika kutaja-1, 2x1
*Maelezo-1*

c) Sifa tatu za msemaji (Mwanaheri)

- Mwenye mawazo mapevu. Mama yake angetafuta suluhu kwa mgogoro kati yake na wakwe zake badala ya kujiua
- Mwenye busara - anaamini kuwa hakuna haja ya kushughulikia mambo ambayo hawezi kuyabadilisha
- Mwenye bidii - anatia bidii shuleni. Anafuata ushauri wa mwalimu Dhahabu kwamba elimu itamletea mabadiliko
- Mshauri za kwanza 3x1

d) **Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya**

- Lunga kumwagikiwa na maji pale anapoachwa na mkewe Naomi
- Umu na nduguye wanamwagikiwa na maji kwa kuachwa mayatima wakati Lunga anapoaga
- Ridhaa anamwagikikwa na maji wakati anapoipoteza aila yake yote isipokuwa Mwangeka
- Mwangeka anamwagikiwa na maji kufuatia kifo cha mkewe na mtoto wake
- Zohali anamwagikiwa na maji pale anapotungwa mimba katika umri wa ujana na kupelekea afukuzwe shuleni na kuteswa na wazazi
- Waafrika wanamwagikiwa na maji pale wanapokatazwa na wakoloni kulima mazao yaletayo fedha huku ikiwalazimu kufanya vibarua kwao
- Baadhi ya vijana wa rika la Tuama wanakufa baada ya kupashwa tohara
- Hospitali inamwagikiwa na maji pale Selume analalamikia ukosefu wa mwangaza, ukosefu wa glavu na deni kutokana na usimamizi duni
- Wakaazi wa msitu wa mamba wanaharibikiwa pale wanapofurushwa huku vyakula walivyolima vikiibiwa na viongozi
- Vijana barobaro wanaotumiwa na wanasiasa kuandamana wanamwagikiwa wa maji pale wanapomiminiwa risasi vifuani wa walinzi huku wakiuawa
- Kitoto kinachookotwa na Neema kilimwagikiwa na maji pale kilitupwa na mama mzazi badala ya kukilea
- Ridhaa anasimulia mwanawe Mwangeka vile walivyobomolewa nyumba zao kwenye mtaa wa Zari, hawakupewa fidia yoyote nao wale waliowauzia viwanja hivi waliingia mitini
- Lunga kufutwa kazi na mkurugenzi kwa kupinga mradi wa ununuzi mahindi

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

*zozote 11 x 1 = 11*

**3. Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika riwaya ya Chozi la Heri**

- Matusi na vitisho - Bwana Maya alipoulizwa maswali na mkewe alimpiga makonde, kumpa vitisho na matusi. Aidha, anaselea kumwuliza sababu za kuhusiana ngono na bintiye Sauna
- Kubakwa - Sauna anabakwa na babake wa kambo Bwana Maya. Mamake naye anamsaidia kuavya mimba hiyo
- Ndoa za mapema - Pete baada ya kupashwa tohara anaozwa kwa mzee Fungo kwa lazima. Nyanyake anajaribu kumtetea lakini hakufaulu
- Kukatizwa elimu - kiu yake Pete ya kuendelea kusoma inakatizwa baada ya ndoa ya lazima kwake bwana Fungo
- Waume zao kukosa uaminifu katika ndoa - Mfano Bwana Tenge anashiriki ngono na wanawake wengi wakati Bi Kimai yuko kijijini
- Uongozi / ushindi wake kudunishwa - ushindi wake Mwekevu unadhalilishwa na mpinzani wake kuandaa maandamano ili kupinga kuchaguliwa kwake
- Kutelekezwa - mfano ni Chandachema anayeondoka kwa jirani yake baada ya kulalamikia vitu vidogo vidogo kuonyesha kutoridhika kuishi naye. Aidha Zohali anatelekezwa na wazazi wake na kuishia kuwa ombaomba mjini
- Mazingira duni ya kazi - Subira anafanya kazi katika mazingira duni yasiyo na nguvu za umeme pia kukosa vifaa muhimu vya kufanyia kazi
- Kufukuzwa shuleni - Zohali anafukuzwa shuleni baada ya kupata mimba
- Tamaa ya maisha ya juu - mfano ni Sally mpenziwe Billy anayemtaliki kwa kujengewa chumba kama tundu la ndege. Aidha Naomi mkewe Lunga anamtaliki kwa kuona uduni wa maisha yao baada ya Lunga kufutwa kazi
- Kujitia kitanzi - Subira baada ya kumtoroka mumewe anakunywa sumu kwenye chumba huku amejifungia
- Utasa - Neema, mkewe Mwangemi anakosa mtoto hivyo kumpanga Mwaliko
- Ujane - Rachael Apondi ni mjane wa Mandu. Hivyo anaposwa na Mwangeka baadaye
- Kifo - Lilly Nyamvula, Anatila, Becky na mkewe Ridhaa wanaangamia katika mkasa wa moto kwenye jumba kubwa lake Ridhaa baada ya ghasia za uchaguzi kuzuka
- Simango la wanafamilia - jamaa zake Kaizari hawakukoma kumwita Subira mwizi wa mali yake mumewe na jamaa zake. Hivyo anamtaliki Kaizari.
- Umaskini - Umaskini wake Chandachema unamfanya kufanya kazi duni. Aidha, kutokana na umaskini wake Sauna, unamfanya ashiriki biashara mbovu ya utekaji nyara kwa watoto na kuwa kijakazi
- Taasubi ya kiume - Jinsia ya kiume inalenga kudhibiti mwanamke kwa njia zifuatazo:
- Kumposa mapema - Pete kwa Fungo
- Kumbaka mwanamke mfano: Maya kwa Sauna
- Kutodhamini ushindi wa mwanamke - mfano ushindi wake Mwekevu kudhalilishwa
- Kupata watoto nje ya doa - mfano ni Kairu anazaliwa nje ya ndoa na babake ni tajiri
- Kushiriki ngono nje ya ndoa - Bwana Tenge anashiriki ngono na wake wengi wakati mkewe yuko mashambani
- Walimu kushiriki ngono na wanafunzi wa kike - mfano mwalimu Fumba kwake Rehema na kumzaa Chandachema
- Mwanamume mmoja mpita njia kumsimanga Neema aache kujishughulisha na kile kitoto kwenye biwi kwani wamepata wengi pale

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Askari kumuuliza Umu maswali yenye kuudhi kwenye kituo cha polisi
- Mzee Fungo kutoonekana akijishughulisha naye Pete baada ya kurudi kwa mke wa kwanza. Anampa uhuru wa kuondoka. Anamwita 'Mwanakwenda'
- Kaango kumuoa Akelo Kiriri pindi tu anapokamilisha masomo yake ya kidato cha nne
- Bi Kangara na mumewe kufanya biadhara haramu ya kuwateka nyara mabinti na kuwapeleka ndanguroni
- Biashara duni - baadhi kama vile Sauna wanafanya biashara duni ya utekaji nyara na ujakazi. Aidha, Chandachema anachuna majani chai ili kulipa karo na mahitaji ya kimsingi. Pete anashiriki ukahaba jijini

zozote 20x1

**TAMTHLIA YA KIGOGO.**

4 a) i) Msemaji ni majoka.
ii) alikuwa anamwambia babu katika ndoto.
iii) walikuwa katika chumba cha wagonjwa.

iv) hii ni baada ya kupata habari ya kifo cha mwanawe Ngao Junior.
(zozote4x1=4)

b) i) Jazanda – safari
- uongozi

ii) msemo – dhahiri shahiri.

iii) nidaa – dhahiri shahiri babu! (zozote4x1=4.)

v) taswira

c) Mauaji - jabali aliuawa na uongozi wa Majoka.
- kufungwa kwa soko la Chapakazi.
- njaa
- Ufisadi
- Kufungwa jela kiholela.
- vikuchapwa na askari.
- uchafuzi wa mazingira.
- migomo
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.
- Kutowajibika kwa viongozi.
- Ubadhirifu wa mali ya umma
- Kudhibiti vyombo vya habari
- Usaliti
- Ulipizaji wa kisasi.

Utabaka. (zozote12 x1= 12.)

5. Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. Ukirejelea tamthilia ya kigogo, ipatie nguvu kauli hii.

(i) **Kuuawa**
Wapinzani wa uongozi Sagamoyo wanauawa katika jitihada za kuisaidia Sagamoyo. Jabali aliuawa kwa kuwa mpizani wa majoka.

(ii) **Kushambuliwa na vijana.**
Vijana walitumwa kumvamia Tunu, nia ikiwa kumuua. Aliishia kuumizwa vibaya kiasi cha kufanya atumie kiti cha magurudumu.

(iii) **Kudhihakiwa**
Tunu anadhihakiwa na waliouunga mkono uongozi wa Majoka. Alipokwenda Mangweni, anadhihakiwa kwa kuambiwa kwanza aolewe.

(iv) **Vifungo**
Ashua anafungwa kwa kukataa matakwa ya majoka. Kufungwa kwake kulikuwa na nia ya kumshinikiza Sudi amchonge Majoka kinyago.

(v) **Kugotanishwa**
Tunu na Sudi wanachochewa kukosana ili waachane na harakati za ukombozi. Tunu anachochewa dhidi ya Sudi kwa kuambiwa kuwa yeye na Ashua ndio walikuwa wakiwinda roho yake.

(vi) **Kukatiziwa vyanzo vya riziki.**
Sudi na Ashua wanaachwa bila namna ya kupata riziki baada ya soko la chapakazi kufungwa na majoka.

(vii) **Vitisho**
Sudi anatishwa na Kenga kuwa ulimi wake ungemtoma kwenye bahari mchafukoge.

(viii) **Umaskini**
Ashua anavaliwa na uhitiaji kiwango cha kumwendea Majoka kutafuta usaidizi. Watoto wao na Sudi (Pili na Pendo) wanalala njaa.

(ix) **Watu kufurushwa makwao**
Jamii ya kina Siti inaandikiwa vibarua vya kusema wahame Sagamoyo. Hii inatokana na wao kutouunga mkono uongozi wa Majoka.

(xi) **Matusi**
Sudi anarejelewa na Majoka kama Zebe. Majoka ananuia kumdunisha machoni pa mkewe Ashua.

(xii) **Ndoa zao kuingiliwa**
Majoka anapania kuisambaratisha ndoa ya Sudi na Ashua. Anamshawishi Ashua aachane na Sudi na akubali kuolewa naye.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(xiii) **Vyombo vya habari kufungwa**
Baadhi ya vyombo vya habari kama vile runinga ya Mzalendo inafungwa kwa kupeperusha habari kuhusu watetezi wa haki.

(xiv) **Kupigwa marufuku kwa maandamano**
Kenga anamshauri Majoka kutangaza kuwa maandamano yote ni haramu.

(xv) **Kukabiliwa kwa nguvu wanapoandamana.**
Polisi wanatumia nguvu kupita kiasi kuwakabili waandamanaji. Matumizi haya ya nguvu yalipelekea kuumizwa kwa watu na kuuawa kwa vijana kiwandani.

(xvi) **Usaliti kutoka kwa wenzao.**
Juhudi za kuleta ukombozi zinapingwa na baadhi ya Wanasagamoyo kama vile Ngurumo, Asiye na Boza.

(xvii) **Kutimuliwa kwa wafadhili wa watetezi wa haki**
Majoka anatoa pendekezo la wafadhili wa harakati za ukombozi kuvunja kambi.

(xviii) **Kukabiliwa na taasubi ya kiume**
Tunu anapuuzwa na baadhi ya watu kwa kuwa ni mwanamke. Ngurumo anasema, "Heri nimpe paka (kura)…lakini si mwanamke."

(xix) **Kupumbazwa kwa baadhi ya wananchi**
Baadhi ya wananchi wanapinga harakati ya ukombozi kwa kuwa walipumbazwa na Majoka na watu wake kwa kuachiwa kitu pale mangweni.

(xx) Kutenganishwa wakati mikutano muhimu
Wakati Tunu na Sudi wanaenda kwa Majoka kusema naye, majoka anawatenga ili aweze kukabiliana na kila mmoja.

(xxi) Kuishi kwa hofu na wasiwasi
Bi. Hashima anaeleza jinsi ambavyo wanaishi kwa wasiwasi kutokana na dhiki wanazokutishwa na uonghozi wa Majoka.

(xxii) Kukosa muda wa kuwa na familia
Sudi alikuwa na shughuli nyingi za kiukombozi, zilizomfanya kukosa muda wa kuwa familia yake.

(Zozote 20x1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

***SHAIRI***

***6.***

a) Eleza dhamira ya shairi hili (zozote 2x1)
- Kueleza madhara ya kutofuata mawaidha
- ushauri wa baba na mama
- Kuonyesha hasara/shida zinazowapata watu walio na kiburi, majivuno, tamaa

***2 x 1 = 2***

b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake.
- Matumizi ya kibwagizo…… uliyataka mwenyewe
- kurejelea methali…. "majuto ni mjukuu huja kinyume,mchimba kisima huingia…
- kutumia nidaa….. ngoo! (za kwanza 2 x 1)

c) Taja na utoe mifano ya aina zozote nne za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi.(al.4)
- Swali la balagha – ya nini kushangaa?
- Jazanda – umelichimba la kukuzika handaki/ulijidharia samba
- Taswira
- methali (za kwanza 4 x 1)

d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari/tutumbi (al.4)
- Yale uliyoyaona kuwa bora ndiyo sasa yamekuletea shida. Mamia ya matatizo hayaishi kwako. Iwapo ungetambua hapo awali basi hungekuwa ukitatizika. Wewe mwenyewe ndiwe chanzo cha haya.

(zozote 4 x 1)

e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili

- Inkisari – alikuamba badala ya alikwambia
- Kuboronga sarufi – alikwambia huko mama badala ya alikwambia mama yake
- Lahaja – huaziriki / hupuliki (zozote2 x 2)

f) Bainisha toni ya shairi hili
  i) Toni ya majuto – anashangaa mambo yanavyomwendea
  ii) Toni ya masikitiko – anasikitika mishikeli haitoki kwake (matatizo yameganda)

(Zozote 2 x 1)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi
  i) mstahiki - mheshimiwa
  ii) hupuliki - husikii / ***husikizi*** ***2 x 1 = 2***

**7.**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.1)
– Mama nitarudi
– Nitarudi
– Kizuizini 1 x 1 = 1

b) Tambua nafsineni katika shairi hili (al.2)
– Nafsineni ni mfungwa aliye kizuizini. Anauliza iwapo mamake angali anasimama na kusubiri akitazama kule kizuizini aliko nafsineni 1 x 2 = 2

c) Eleza toni katika shairi hili (al.2)
– Toni ya masikitiko / uchungu wa moyoni/huzuni. Anasikitikia hali yake ya kuvaa matambara, njaa, kufanyiswha kazi tele n.k
– Toni ya matumaini. Mshairi ana matumaini kwamba siku moja atatoka kizuizini `2 x 1 = 2

d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia
– Kuachwa njaa
– Kufungwa
– Kufukuzwa
– Kutopewa nafsi ya kupumzika, kulala na kuwaza
– Kuvaa matambara
– Kufanyizwa kazi kama mnyama (za kwanza 4 x 1 = 4

e) Fafanu dhamira katika shairi hili
– Mshairi anadhamiria kulalamikia/kukashifu namna anatumiwa vibaya kizuizini
– Mshairi anakashifu madhila na mateso ambayo wafungwa hutendewa
– Kumpa mamake matumaini kwamba atatoka kizuizini siku moja

2 x 1 = 2

f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru
– Mistari mishata k.m ya kulala hakuna
– Idadi ya mishororo inabadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi nyingine
– Vina kutofautiana
– Mizani tofauti 2 x 1 = 2

g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi
– Ni mwenye kulalamika – analalamikia hali yake ya kuwa na njaa, kupigwa
– Mwenye matumaini – anatumai kuwa siku moja atatoka kizuizini
– Mwenye mapenzi – anampenda mamake na kumwita mama mpenzi

(za kwanza 2 x 1

h) Fafanua mbinu 3 za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu
– Takriri – neno 'nitarudi' lilmerudiwarudiwa au sauti "ni"
– Mdokezo – nitarudi mama mpenzi
– Tashibihi – "kupitia mwingine kama shetani"
– Taswira-ubeti wa mwisho
– Jazanda-shetani
– Usambamba-nitarudi (za kwanza 3x1)

i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shiari hili (al 2)
  i) Hayawani - ***mnyama***
  ii) Nadhari - ***fikira***

**8.** a) Maneno haya yanasemwa na Mbura
– alikuwa anazungumza na Sasa
– walikuwa kwenye sherehe iliyoandaliwa na mzee Mambo
– walikuwa wanazungumza kuhusu 'kula kwao'

*4 x 1 = 4*

b) **<u>Sifa za Mbura</u>**
– ni mzalendo - anafanya kazi kwa bidii katika wizara yake kama njia ya kuonyesha uzalendo
– mwenye tamaa - anajaza sahani kwa chakula na kukila chote

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- mwenye utu - anataka wananchi wale kwa niaba ya viongozi kama vile wao wamekuwa wakila kwa niaba yao
- Mfisadi - amepokea kazi kwa afisi ya serikali kwa njia isiyo halali
- mzembe - baada ya kula sahani tatu za vyakula kwenye sherehe analala usingizi mzito badala ya kwenda kazini
- mtetezi wa haki
- mvumilivu
- mpyaro -
- msema kweli *zozote 6 x 1 = 6*

c) **<u>Jinsi viongozi walivyo wabadhirifu</u>**

- hulipwa mishahara mikubwa sana na serikali jambo linalochangia ubadhirifu wa mali ya umma
- sherehe kubwa za viongozi wa kiserikali huchangia pakubwa ubadhirifu
- viongozi hutumia raslimali za nchi kwa manufaa yao ya kibinafsi - magari ya serikali
- raslimali zilizotumiwa katika kuvinunua vyakula na vinywaji vingetumika katika kuendeleza asasi tofauti za kijamii
- DJ na wenzake wanapata mabilioni ya fedha kutokana na kuwatumbuiza wageni katika kama hizi
- viongozi wanawachukua baadhi ya watu wao wa karibu na kufanya juu chini kuona kwamba wanajifaidi na mali na raslimali za wananchi pasipo kuzitolea jasho kamwe
- upeperushaji wa matangazo katika vyombo vya habari ya sherehe za kiongozi binafsi ni njia ya kuendeleza ubadhirifu wa raslimali za umma
- Mbura ana Sasa wanaendeleza ubadhirifu pale wanapoamua kuchukua vyakula kupita kiasi katika sherehe za mzee Mambo
- kuwaajiri viongozi wawili wenye nyadhifa sawa katika sekta tofauti za umma
- vibaraka na vikaragosi kupewa mali ambayo ingewafaidi wananchi

*zozote 10 x 1 = 10*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya kwanza**
**Insha**

1. **Lazima.**
Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi. **(Alama 20)**
2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili. **(Alama 20)**
3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa. **(Alama 20)**
4. Andika insha itakayomalizikia kwa;
…walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. **(Alama 20)**

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**

**1 UFAHAMU (alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.
Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (alama 1)
(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (alama 2)
(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (alama2)
(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
(h) (i) inasigana..........................................................................
(ii)yameghoshi……………………………………………
(iii)vighairi…………………………………………………

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**2 UFUPISHO (alama 15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'
Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.
Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.
Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.
Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.
Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.
Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a ) Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**3 MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Taja vipasuo sighuna (alama 2)

(b) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi (alama 2)

(c ) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama 2)
Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

(d) Sahihisha
Mwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. (alama 2 )

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Hakuwapiga wala kuwalaghai.

(f) Eleza viambishi katika neno lifuatalo (alama 3)
Walichokilalia

(g) Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
Wanafunza wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao.

(h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale (alama 4)
Yohana na Otieno hucheza kandanda.

(i) Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. (alama 3)

(j) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)
Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)
IK+KI+KI+KI

(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. (alama 2)
(i) kibainishi
(ii) parandesi

(m) Tumia neno –baya kama: (alama 2)
(i) kiwakilishi
(ii)kielezi

(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi ‘la’ katika kauli ya tendewa. (alama 2)

(o) Badlisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi. (alama 2)
Yunis amepata <u>faida</u> kutokana na <u>ukulima</u>.

(p) Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (alama2)
Tinga amewafanya ng’ombe wake wanywe maji.
(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie ‘amewafanya’)

(q) Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. (alama 2 ).

(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. (alama 2)
Umu alimwandikisha mkewe.

(s) Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. (alama 1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**4. ISIMUJAMII** (Alama 10)

(a) Lahaja huainishwa katika makundi mawili. Yataje (alama 2)
(b) Eleza sifa zozote nne za lugha ya taifa. (alama 4)
(c ) Tolea ushahidi namna nne kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (alama 4)

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**Karatasi hii ina kursa nne zilizopigwa chapa.**

***SEHEMU YA A: RIWAYA***
***Assumpata K. Matei: Chozi la Heri***

***LAZIMA***

1. "Haiwezekani! Hili haliwekazi! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza kwa kifupi yaliyowapata wahafidhina baada ya usemi huu. (alama.4)
   (c) Riwaya ya chozi la heri inaonyesha maovu yanayotamalaki katika jamii.Thibitisha. (alama 12)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B: TAMTHILIA**
***Kigogo.Pauline Kea.***
***Jibu swali la 2 au la 3***

2. Tatizo la uongozi katika bara la Afrika ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kwa kurejelea matukio kwenye tamthilia ya kigogo, jadili ukweli wa kauli hii (alama 20)

**AU**

3. "Mtalipa kila tone la damu mlilomwaga sagamoyo ;wewe na watu wako."
   a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)
   b) Eleza sifa za mzungumzaji (alama 4)
   c) Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa maisha ya anayezungumziwa yametawaliwa na dhuluma. (alama 12)

***SEHEMU YA C: HADITHI FUPI***

4. Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo, onyesha jinsi jamii imegawanyika kitabaka kuegemea.
   i) Kielimu
   ii) Kikazi
   iii) Kiuchumi (alama 20)

***SEHEMU D: SHAIRI***
**<u>WASIA</u>**

5. Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msije juta laiti, mkamba sikuwambia
Si hayati si mamati, vijana hino dunia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msije andama baa, makaa kujipalia
Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapo yyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI:**

a) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. (alama 4)
b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. (alama 2)
c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)
   i) idadi ya vipande katika mshororo
   ii) mpangilio wa vina katika beti.
d) Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (alama 4)
f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
g) Tambua: (alama 2)
   i) Nafsi neni
   ii) Nafsi nenewa
h) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. (alama 2)
i) Eleza maana ya msamiati: 'aula' (alama 1)

***SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI***

6. a) Eleza maana ya miviga. (alama.2)
   b) Eleza sifa tano za miviga. (alama.5)
   c) Miviga ina udhaifu gani. (alama.3)
   d) Fafanua umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama.6)
   e) Eleza vizingiti viwili vinavyokumba ngomezi. (alama.4)

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**Mtihani mwigo2020 majibu**
**102/1**
**Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)**

1. Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi. (Alama 20)

**(a) Muundo wa barua rasmi - yenye anwani 2**

i) Ina anwani ya kwanza: - Mwandishi - mtahiniwa abuni anwani yake – Iwe wima (Alama1)
ii) Tarehe - Chini ya anuani ya kwanza (Alama½)
iii) Anwani ya pili Mwandikiwa- mkurugenzi wa shirika la uchapishaji (Alama1)
iv) Maamkizi - Kwa Bwana/ Bibi, (Alama½)
v) Mtajo / mada - <u>KUH/MINT/ YAH: KUOMBA KAZI YA UHARIRI</u> (Alama2)
vi) Mwili wa barua –
- Utangulizi _ Asili ya habari kuhusu nafasi ya kazi – tangazo
- Maelezo ya kibinafsi kwa kifupi.
- Ufaafu wake kwa hiyo nafasi (Alama4)
- **Maelekezo kwa wasifu kazi kwa maelezo zaidi.**

vii) Hitimisho - Sahihi ya mwandishi , jina na cheo kama anacho. (Alama1)

**(b) Wasifu kazi/ Tawasifu kazi**

(i) Habari za kibinafsi – Jina
- Jinsia
- Umri / Tarehe ya kuzaliwa
- Ndoa – ameolewa au la /Hadhi
- Anwani - Barua pepe, meme/webu nambari ya simu.
- Dini
- lugha uzijuazo (Alama2)

(ii) Elimu – Orodha ya shule – Aanze kwa kiwango cha juu zaidi na kumalizia shule ya msingi. Ataje hadhi na jina la taasisi, kipindi cha wakati, cheti alichohitimu. (Alama2)
(iii) Tajriba – Ujuzi wa kikazi/ maarifa. Ataje tajriba aliyonayo katika utendaji kazi anayoiomba. Ujuzi alionao uonyeshe shirika au kampuni alipofanya kazi. (Alama2)
(iv) Ufanisi - Ataje na aeleze ufanisi wake. (Alama1)
(v) Uraibu - Ataje mambo ambayo anapenda kufanya wakati wa ziada au anapokuwa hayumo kazini. K.m. kusoma, kusaidia jamii n.k. (Alama1)
(vi) Wadhamini/ Warejelewa wa wili au zaidi.
Habari zifuatazo kuhusu wadhamini zitolewe.
- Wawe wawili au watatu.
- Jina /majina
- Vyeo/ Taaluma/ kazi
- Anwani
- Nambari ya simu
- Kipepesi. (alama2)

2. *Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili.*
<u>Jinsi ametelekezwa</u>
Kukosa waelekezi
Kuwachwa kujikidhi pekee.
Kutopigiwa debe kama msichana.
Kutwikwa majukumu angali mchanga.
Kutoajariwa na mashirika ya ufadhili.
Vyama vya kupigania mvulana kutowajibika.
Kunyimwa nafasi ya masomo.
Kukosa mashirika ya utafiti kuhusu wavuluna.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

<u>Janga</u>
Anaacha masomo
Anaingilia dawa za kulevya na anasa.
Anaungana na vikundi vya ugaidi.
Wanakosa hadhi ya mwanamume.
Kuchangia kuporomoka kwa misingi ya kifamilia.
Kukosa viongozi wa kesho.

<u>TANBIHI</u>
1. *Lazima aonyeshe pande mbili, asipo atuzwe nusu ya alama.*
2. *Kuwe na kichwa au mada.*
3. *Atimize maneno kati 350 – 400*
4. *Kadiria hoja nyinginezo.*

3. *Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.*

**Maana.**
*kiatu* cha baniani ni kitu au kundi la watu ambalo limechukiwa au kudharauliwa.
*Dawa*: Kitu husika huenda kikawa ndicho jibu au jawabu au suluhisho kwa tatizo fulani maishani mwa mtu au katika jamii
Mtahiniwa aandike kisa kuthibitisha matumizi haya ya methali
Mtahiniwa anaweza kutumia methali nyingine zenye maana sawa kama;
- Matango na matikiti ndio maponya njaa
- Wembamba wa reli gari moshi hupita
- Nyumba nzuri si mlango fungua uingie

Utuzaji
(i) Pande zote za methali zishughulikiwe.Anayeshughulikia upande moja asipite alama C 08/20
Anayetaja tu upande wa pili bila maelezo kikamilifu achukuliwe kuwa amelenga lakini ana udhaifu wa maudhui
(ii) Anayekosa kulenga katika kisa chake amepotoka kimaudhui alama D 03/20

4. *Andika insha itakayomalizikia kwa;*
*…walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia.*

- Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa
- Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa
- Kisa kilenga tukio lililozua taharuki miongoni mwa wahusika
- Tukio lenyewe lazima lidhihirishe maafa /maangamizi
- Lazima litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba,katika gari n.k
- Mtahiniwa atumie *nafsi ya tatu hali ya wingi*(warejelewa)
- Atumie *wakati uliopita.*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**KISWAHILI KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

## 1 UFAHAMU

(a) Kukichuza/kupima/kukadiria/kuchunguza kipindi cha mahusiano.(alama1)
(b) Ni wa kudumu/ni wa muda mrefu/hautavunjika/ni wa milele. (alama 1)
(c) (i) Huwezesha watu walio mbali kuwasiliana.
(ii) Ni nyenzo ya kudumisha uhusiano.
(Mojawapoalama 2)
(d) (i) Talaka
(ii) Maisha ya mjini ambayo yanabadilikabadillika.
(iii) Mfumo wa maisha ya kibepari/ubinafsi mwingi.
(iv) Uhamaji
(v) Ufutwajikazi
(vi) Ubadilishaji kazi
(vii) Hali zisizotegemewa
(viii) Mifumo ya kimataifa
(ix) Mifumo ya kisiasa
(Zozote 4 x1 = 4)
(e) Hujiri katika muktadha wa huduma fulani/Ni uhusiano wa chembe chembe/Ni uhusiano ulio tovukwa na hisia za utu.
(Mojawapoalama 2)
(f) Aina tofauti za mahusiano/mahusiano katika jamii/Tuhakiki /tuchunguze , mahusiano ya jamii.
( Mojawapoalama 2)
(g) (i) inasigana – inatofautina/inapingana/inakinzana/inahitilafiana (alama 1)
(ii) yameghoshi – yamejaa/yamesheheni/yamebeba/yametawaliwana/yameseta/ yamerundika/yazidisha/yameongeza (alama 1)
(iii) vighairi – kinyume/tofauti (alama 1)

***Kukosoa – h – 6 x ½ =al.3***
***s- ½ kwa kila kosa. Asikosolewe zaidi ya ½ ya alama alizotuzwa.***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

## 2 UFUPISHO

(a)
– Maarifa huyadhibiti, huyatawala, huyaendesha na kuyaongoza maisha ya binadamu.
– Anayekosa maarifa huathirika pakubwa.
– Maarifa ni utajiri mkubwa ambao binadamu huutumia kwa faida yake na wanajamii wenzake/Elimu ni mali/Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu ni maarifa.
– Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.
– Maarifa hayana upinzani.
– Utumiaji wa maarifa hauyamalizi.
– Kila mtu ana uhuru wa kutumia maarifa kuzalisha maarifa mengine./Anaweza kunyumbua maarifa na kuyatunza kwa namna tofauti.
– Maarifa hayagusiki. 8 x ½ =4

(b)
– Maarifa huingiliana na maarifa mengine.
– Hayawezi kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
– Yaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo ya kidhahania.
– Huweza kubadilishwa/kugeuzwa na kuwa ishara.
– Yana sifa ya uhusianaji.
– Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo.
– (vii)Hayawezi kudhibitiwa/kuzuiliwa mahali fulani yasisambae/Huenda haraka sana.
– Huepuka pingu za watu kudhibiti wenzao.
– Ni nguvu inayoshinda nguvu zote.

***(Zozote 8 x 1=8)***

**3 MATUMIZI YA LUGHA**

(a) /p/, /t/, /j/, /k/ 4 x ½

(b) (i) kazi – shamirisho
(ii) haraka ipasavyo – chagizo
(2 x ½ )

(c) K. m. Mtoto yule aliadhibiwa vikali na mama yake.

(d) Mwalimu aliyekuja juzi anafundisha Kiswahili vizuri.
(4 x ½ =2)

(e) Aliwapiga na kuwalaghai. (alama 2)

(f) Wa – nafsi/ngeli
li - wakati
cho – kirejeshi
ki – kitendwa
i – kauli/kinyambulishi
a –kiishio
(6 x ½ =3)

(g) wote – kivumishi cha pekee
wenye – kivumishi cha pekee
kubwa – kivumishi cha sifa
wao – kivumishi kimilikishi
(4 x ½ =2

(h) S – KN + KT
KN – N + U + N
N – Yohana
U – na
N – Otieno
KT – T + N
T – hucheza
N – kandanda (8 x ½ =4

(i) (i) Huwa na kirejeshi.
(ii) Huwa na vitenzi viwili au zaidi.
(iii) Huwa na vishazi viwili; huru na tegemezi.
(3 x 1=3)

(j) Askari jela alimwuliza Kendi, ‘’Unadhani hapa ni kwenu? Kuja kwangu mara moja.
(2 au 0)

(k) K.m. Alhamisi, alfajiri n.k.

(l) (i) K.m. ng’ombe, ’14, n’taenda n.k. (al. 1)
(ii) Mwalimu (wa Historia) ametuzwa n.k. (al.1)

(m) (i) K.m. Kibaya kimetupwa. (al. 1)
(ii) K.m. Alicheza vibaya. (al. 1)

(n) liwa
K.m. Chakula chote kililiwa na paka. (al. 2)

(o) Yunis alifaidika kwa kulima.
Yunis alifaidika kutokana na kulima.
(Yoyote 2 x 1=2)

(p) Mifugo wangu wamenyweshwa maji na Tinga. (al. 2)

(q) (i) werevu, wema, wokofu, wivu n.k. (al.1)
(ii) uovu, ulevi, uwongo,uchungu n.k (al. 1)

(r) (i) Umu alimfanya aajiriwe.
(ii) Umu alimfanya aandike.
(iii) Umu alisababisha kitendo cha jina lake kuandikwa.
(iv) Aliyeandikwa ni mke wa Umu.
(v) Aliyeandikwa ni mke wa mtu mwingine.
(Zozote 2 x 1=al. 2)

(s) K.m. Kerich acheza vizuri. (al. 1)
***Kukosoa - h -6 x ½ =3***
***s- Kilakosa ½ - Asikosolewe zaidi ya nusu ya alama***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

***alizotuzwa.***

**4 ISIMUJAMII**

(a) (i) Kijamii
(ii) Kijiografia/kimaeneo (2 x 1=2)

(b)
- Huwa na wazungumzaji wengi.
- Huwa ni lugha ya kwanza ya kikundi cha watu inayokiwezesha kikundi husika kupokezana utamaduni.
- Huwa na muundo wakiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu wa nchi husika.
- Lazima iwe mojawapo wa lugha asilia (4 x 1=4)

(c)
- Kiswahili kinazungumzwa na watu wa Afrika Mashariki na Kati.
- Kiswahili hufundishwa katika shule za Kenya, Uganda na Tanzania.
- Kiswahili hufundishwa katika vyuo vya Afrika Mashariki, Marekani na Ujerumani.
- Hutumika katika mikutano ya kimataifa kama vile Umoja wa Afrika.
- Kiswahili hutangazwa katika idhaa za Kimataifa kama vile B.B.C, Redio China na Idhaa ya Kijerumani.
- Kwa sasa hutumika katika mtandao.

(Zozote 4 x 1=4)
***Kukosoa – h -4 x ½ =2***
***s- 4 x ½ =2***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SUKEMO JOINT EXAMINATION TEST 2020**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**LAZIMA**

**1. (a)**
- Maneno ya Tetei, Mwanaharakati
- Anawaambia wananchi/wapiga kula.
- Baada ya mwekevu kutawazwa/ Kiogozi mwanamuke
- Watu walishukuwa silaha kupigania uhuru wao.

(b)
- Watu walishukuwa silaha kupigania uhuru wao.
- Mlio ya buduki ilisikika.
- Vilio vilijaa hewani.
- Vyombo vya dola vilitumwa kudumisha amani.
- Msafara ya watu ilionekana ikimaha kwao.
- Mazao yalichomwa mashambani
- Majumba yalichomwa
- Watu waliuliwa.

Zozote nne (1 x4)

(c)
- Nyumba ya Ridhaa inateketezwa
- Luga anafutwa kazi bila sababu.
- Mwanaheri kunajisiwa
- Fumba kuringa mwanafunzi wake mamba
- Familia ya ridha kuteketezwa majirani.
- Pete kuozwa
- Subira kubaguliwa Kwa sababu za kiukoo.

- Naomi kuwatelekeza wanawe.
- Uharibifu wa mazingira – serikali inakata miji.
- Chandachema chema anadhumiwa kimapenzi na mwalimu wake fumba.
- Shamba lao shamusi linanyakuliwa.
- Pete anakeketwa.
- Ndoa za mapema/pete
- Uuzaji wa pombe haramu
- Ulaguzi wa madawa ya kulevya
- **Ulaguzi wa watoto.**
  **<u>TANBIHI</u> Kadiliria jawabu la mwanafunzi zozote kumi na mbili. (12x1)**

<u>2. KIGOGO</u>

Ufisadi

- Wafanyabiashara wanalazimishwa kutoa hongo kombe anasema lazima tutie tonge kinywanina tuwape wenye nchi kitu kidogo
- Mapendeleo ya kinasaba
- Majoka anamteua Kenga binamuye kuwa mshauri wake mkuu (maneno ya sudi uk 9)
- Majoka anapanga kumtambulisha Ngao Junior kama mrithi wake (uk 36)
- Usaliti/ukiukaji wa majukumu
- Watawala wanasaliti wapiga kura kuwa kutotokeleza majukumu yao. Soko linanuka uvundo kutokana na maji machafu ya taka. Wanachojua viongozi ni kukusanya kodi (uk2)
- hawatekelezi majukumu yao ya kusafisha soko

Udhalimu/ukatili

- Viongozi kutumia vitisho na kuwanyang'anya wafanyabiashara kilicho chao (sudi anasema katika uk 3)
- Vijana watano waliokuwa wakifanya maandamano wanauawa na wachuuzi sokoni wanaumia uk 16
- Chuki za kikabila
- Vijikaratasi vinaenezwa kuwatia woga watu kutoka kabila Fulani. Wanaambiwa kuhama (uk.51-52)

Unafiki

- Majoka anasema kuwa wanasagamoyo wasiruhusu watu wachache waliojazwa kasumba za kiloloni kuwarejesha katika utumwa. Pia anadai kuwa hatuwezi kukubali kutawaliwa tena yeye anatenda mambo yayo hayo anaokashifu.
- Ubadhirifu
- Serikali inakopa pesa nyingi na kuziweka katika miradi isiyofaa (pesa inakopeshwa na kutumiwa katika mradi wa kuchonga kinyago cha hayati Marala Bin Ngao
- Unyakuzi wa ardhi ya umma
- Ardhi ya soko inanyakuliwa na majoka anajenga hoteli ya kifahari katika ardhi hiyo nakuwagawia wendani wake kama vile kenga baadhi ya sehemu ya ardhi hiyo
- Matumizi mabaya ya mamlaka
- Kenga anamshauri majoka kutumia uwezo wake kuharamisha maandamano na kuwaamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi kuwatawanya waandamanaji (uku 34)
- Dawa za kulevya na pombe haramu

  Tunu anasema kuwa juzi walizika watu waliokufa kutokana na pombe haramu. Wenginewamegeuka kuwa vipofu (ku 63
- Umaskini umekidhiri katika jamii hii wafanyabiashara katika soko la sagamoyo ni watuwenye elimu na talanta kochokocho kama vile Sudi. Wangali wanaishi katika umaskini licha ya bidii zao. Boza anasema kijirununu cha pesa nene.. maskini akipata (uk 7
- Vijana wanatumiwa kumvamia Tunu na wapinzani wengineo (zozote (alama 20)
- Tamaa, Majoka ana tamaa ya mali ya umma kwa sababu analifunga soko la chapakazi iliajenge hoteli ya kifahari. Vilevile yuko na tama ya wake za wengine m.f Ashua
- Uozo, Mamapima anapewa kibali na serikali ya majoka kuwauzia watu pombe haramuinayowaua na kuwafanya vipofu. Vilevile majoka yuko na kampuni kubwa ya uzalishajisumu ya nyoka barani (dawa za kulevya) ambayo inauzwa katika shule ya majoka na majoka academy
- Ubarakala: Kuna vibaraka ambao wanamshauri Majoka isivyofaa m.f. Kenga anamshauri Majoka kulipiza kisasi kwa Ashua.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Tenga Utawala: Majoka anawatenga wasiomuunga mkono k.v. Tunu na Sudi na kuwaleta karibu wanaoukubali ungozo wake m.f. ni mama pima na Ngurumo na pia Kenga.
- Matumizi ya vyombo vya dola: Polisi wanatumika kuwatawanya wananchi kutumia vitoza machozi. Hali hii inwafanya wanasagamoyo kufa na wengine kuwa walemavu.
- Kuotkuwa na uhuru wa vyombo vya habari: Majoka anasema Sagamoyo kitabaki kituokimoja tu Sauti ya Mashujaa.
- Hali ngumu ya maisha: Wananchi wanoishi katika mazingira machafu, Kombe anasemawamegeuza soko kuwa uwanja wa kemikali na taka. Wanasagamoyo wengine hawana hatachakula.
- Ukosefu wa uwajibikaji: mama pima anawauzia watu pombe haramu licha ya kuwa nikinyume cha sheria. Pombe hiyo inawaua watu na kuwapofusha vilevile mama pima anamgawia Ngurumo uroda ili amsaidie kupata kandarasi ya kuoka keki ya uhuru. (1 x 20 =20)

3. <u>KIGOGO</u>

a)
- maneno ya Tunu
- anamwabia majoka
- ofisini mwa majoka
- Ashu alikuwa gerezani

b) Sifa za Tunu
- Mwanamapiduzi
- Msomi
- Mtetezi wa haki
- Jazili
- Mzalendo
- Mwajibikaji
- Mzindushi
- Mwenye mhawalaka mwema

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**c)** Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa Maisha ya Majoka yametawaliwa na dhuluma.
- Dhuluma ni kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake; ni uonevu, ni tendo lisilo la haki. Majoka alidhihirisha dhuluma maishani mwake binafsi na katika uongozi mwake.
- Serikali yake hutoza wanabiashara kodi lakini wanafanyia kazi katika mazingira machafu. Uvundo umekithiri. Sudi anasema. “Ni jukumu lao kuhakikisha soko ni safi si kukusanya kodi pekee….. (uk 3).
- Bali na kulipa kodi isiowaletea huduma yoyote wafanyakazi wa soko wanalalamika kuwa wanadaiwa pesa zaidi. Kombe asema kuwa ni lazima wpate chakula na pia wawape wenye nchi kitu kidogo.
- Shua asema mahali wanapofanya kazi wanadaiwa kitu kikubwa au kitu chote.
- Utawala wake unawanahangaisha wafanyakazi, hawafanyi kazi kwa amani Ashua asema “…na kuhangaishwa na wenye nguvu ndiyo hewa tunayopopumua…” (uk2). Sudi anathibitisha hilo anapolalamika kwamba, “si haki kuchukua kilicho chetu na kututishatisha”(uk3).
- Anadhulumu raia kwa kutumia raslimali za Sagomoyo kujinufaisha pamoja na wachache, wanaomunguka. Wao ndio hula ile keki kubwa, huku raia wakitaabika. Sudi anamwambia Boza, “Hapo basi – kijikeki. Kwa nini wewe upate kidogo? Sagamoyo ni kwenu, shrehe ni zenu.. na keki kubwa ni ya kina nani”(uk 14)
- Ni dhuluma pia kwa serikali ya majoka kufunga soko la Chapakazi mahali ambapo watu wengi hufanya biashara ili kupata chakula chao cha kila siku.
- Katika kiwanda chake wafanya kazi wanapujwa. Soko la Chapalazi lilipofungwa bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni ya Majoka and Majoka ikapanda maradufu. Wafanyakazi hawawezi kugharimia chakula. Hii ni dhuluma dhidi ya wafanyakazi. Majoka kuendelea kujitajirisha huku wafanyakazi wake wakiumia (uk 17)
- Maandamano yanayokumba jimbo la Sogamoyo si walimu, si wauguzi, si wafanyakazi wa kampuni, si wafanyakazi wa soko ni ithibati tosha kuwa watu wanadhulumiwa.
- Ni dhuluma pia kuwaua watu.
- Alimuua Jabali kuwa mshindani katika siasa.
- Wale vijana watano wa Majoka and Majoka Company waliuawa wakidai haki yao kwenye maandamano.
- Tunu alikuwa auawe kwa kukashifu vitendo vyake vya kidhalimu.
- Kingi alionywa kuwa angevunjwavunjwa na chatu kwa kukaidi amri ya Majoka ya kuwapiga watu risasi.

- Majoka anawaua hata washirika wake wa karibu akihofia kuwa wangetoa siri zake. Kwa mfano Ngurumo aliuawa ilhali alikuwa mfuasi wake sugu. Chopi alipangiwa kuuawa pia kwa kijua 'mengi'. Hii ni dhuluma iliozidi. Majoka anasema anaona ziwa kubwa ajabu lililofurika damu… kuna kilio cha ndani kwa ndani na machozi mengi humo yasiyoonekana… (uk 73) na kwamba mikono yake ilikuwa imefungwa nanga humo damuni. (uk 73).
- Serikali yake imewahini wananchi raha, wanaishi kwa hofu. Heshima anakiri kwamba yeye na Tunu wake wanaishi kwa hofu nyingi. Wanaogopa kwamba wanaweza kuvamiwa wakati wowote hasa akitilia maanani kuwa mwanawe nusura auawe. Tunu anapopiga nduru kwa kuota mamake anafikiri wameshambuliwa.
- Isitoshe serikali ya Majoka inawahangaisha watu kuwatupia vijikaratasi vya kuwashurutisha wahame Sagamoyo si kwao. Siti anasema, "Jana walitutupia vijikraratasi… Tuhame Sagamoyo si kwetu" (Uk 52-53).
- Anaamuru polisi kusambaratisha kikatili maandamano raia ambao hawakuwa na hatia. Walikuwa wakidai haki yao tu.
- Anwawadhulumu raia waliochagua kwa kutowapa huduma muhimu kama vile hospitali, barabara, maji safi, vyoo, nguvu za umeme, elimu na hata ajira kwa vijana waliokamilisha masomo. Viogozi wasiowajibika hawatilii maanani mahitaji ya umma.

**4. HADITHI FUPI.**

Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo onyesha jinsi jamii imegawika kitabaka kuegemea

(a) Uchumi
(b) Kazi
(c) Elimu

➢ Tabaka ni kundi la watu katika jamii linalojitofautisha na kundi jingine kwa misingi ya kiuchumi, kielimu, kikazi n.k. katika hadithi hii matabaka haya yamedhihirika.

(a) Kiuchumi, kuna tabaka la juu matajiri na la chini la maskini. Watu wenye fedha nyingi wanaweza kununua magari makubwa ya kibinafsi, kujenga majumba ya ghorofa, kununua matatu na mabasi.

- Matajiri wanaweza kuwapeleka watoto wao shule za mikoa na kitaifa maana wanau wezo wa kulipa karo ya huko.
- Watoto wa matajiri wakifuzu kwenda chuo kikuu wanahahikisha wanaishi maisha ya kifahari. Mavazi yao ya kutoka nchi za nje wamenunuliwa simu za bei ghali, vipakatalishi na Ipad
- Wazazi hawa ni msaada kwa watoto wao, wanawapa pesa za kutosha za matumizi chembilecho Penina, babake humtumia elfu tano kila wiki.
- Watoto wa matajiri hawasumbuki hata baada ya kufuzu vyuoni na kukosa kazi. Penina analipiwa kodi na wazazi wake na nyumbani mwake mna runinga na kochi. Bila shaka amenunuliwa na wazazi wake.
- Utajiri wa wazazi ndio unawafanya baadhi ya wanafunzi wa chuo cha kivukoni kutokuwa makini sana. Masomo yakiwa magumu, wengine wanahiari kuyaacha. Wanajua wanaweza ungana na wazazi wao katika biashara zinazowaletea mapato makubwa, kwa mfano magari ya uchukuzi na nyumba za kupanga.
- Shakila anatafutiwa kazi na mamake kwa sababu ana cheo kikubwa kazini mwake. Ni mkurugenzi mkuu.
- Tabaka la maskini linawakilishwa na Dennis na wazazi wake. Dennis mara nyingi anabaki kutamani/kumezea mate magari makubwa yanayoendeshwa na wenye pesa.
- Dennis anakiri kuwa "kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani." (uk 20) Haya ndio maisha amezoea"Dennis, hata chuoni anakosa chakula, anakosa pesa za kununua na anakosa kwa kukopa,asema, pesa zangu zimekwisha na sina kwingine ninakoweza kukopa kwa"(uk 18.)
- Maisha ya watu maskini ni ya hadhi ya chini; ya kunywa uji mweupe bila sukri, mavazi ya bei ya chini yakilinganishwa nay a matajiri ambayo ni ya kutoka nchi za nje.
- Chumba cha Dennis kinaonyesha anatoka katika tabaka la chini. Hakina vitu vya thamani. Kuna kijiredio ambacho kinaimba kwa sauti ya chini, shuka za kitandani ni kuu kuu zimechanikachanika n.k. hakika kuna utengano wa wazi kati ya maskini na matajiri.
- Watoto kutoka jamii maskini wanasomea shule za hadhi ya chini, shule za vijijini. Watoto kama vile Dennis huishi wakiwazia umaskini wao katika jamii uliowakossha nafasi ya kusomaa katika shule za kifahari.
- Tabaka la maskini hufikiri kuwa elimu ni njia moja ya kuwanasua kutoka umaskini. Dennis anasoma kwa bidii ili awe daktari, mhadhiri, mtangazaji au mwandishi msifika.
- Anatamani kuwa ataweza kununua gari kubwa na hata kuwasaidia wazazi wake. Anawaza moyoni hivi, "Maskini nitawalipaje wazazi wangu wema wlionitendea? Nani atawafidia nguvu na jasho lao…uk 25. Kwa hivyo ni jambo la kutamausha mno Dennis anaposaka kazi kwingi na anakosa. Miaka mitatu baada ya kufuzu chuoni na bado alikuwa akifanya 'tarmacking' yaani kutafuta kazi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Watoto kutoka jamii maskini hawapati msaada wa kupata ajira kutoka wazazi. Maasa wazazi hawajulikani na hawana uwezo. Hii ndio sababu Shakila anapata kazi katika kampuni ambamo mamake anafanya kazi naye Dennis anakosa.

5. LAZIMA: SHAIRI

a)
- Kujitahadhari na vyote vinavyong`ara sababu zitawadhuru
- Kujiepusha na zinaa
- Wasiandame baa.
- Wasifikirie wanaovalia kinadhifu na kujipondoa ndio wazuri na kuwaandama.
- Wasiandame/ wasipapie anasa
- Kumcha Jalia
- Kuvumilia na kujikaza Zozote 4 x 1 = 4

b)

I) Tabaini – si hayati si mamati ub 1
ii) Msemo - makaa kujipalia ub 2
kaza kamba.
iii) Methali - si mlamgo nyumba nzuri…ub 4
iv) Tashbihi- wamepita ja umeme ub 5
kufa kama nyani ub 6 Zozote 2 x 1 = 2

c) Mathnawi – migao miwili kila mshororo.
ii) Ukara – vina vya ndani vinatofautiana lakini vya nje vinafanana kila ubeti. ( 2 x 1= 2)

d i) Tabdila - huno - huo ubeti 1
ii) Inkisari – mkamba - mkaamba ubeti 1
juta – kujuta ubeti 1
alo – aliye ubeti 8
ngia – ingia ndani
iii) utohozi - sitoria ub 5
iv) Lahaja -hino – hiyo ubeti 1
v) kuborogha sarufi – makaa kujipalia
Madhara kukadiria zozote 2 x 1= 2

e) i) Ingawa vitu vitaonekana bora na kuvutia machoni.
ii) Dunia ina udhaifu na maovu mengi.
iii) Vijana ninawasarifu / nawasihi iwapo mtanisikia.
iv) Tahadhari na vyote vinavyong`ara kwani vinaweza kukudhuru. 4 x 1= 4

f) Toni ya ushairi- mshairi anawashauri vijana dhidi ya kutotahadhari na ya dunia. 1x 1= alama 1

g) Nafsi neni – mshauri/ mzazi/ mhenga alama 1
Nafsi pokezi – vijana alama 1

h) i) Balagha – wawapi leo madume, anasa walopapia?
Umuhimu – kuibua hisia za nafsi nenewa kuhusu kupapia anasa na raha.
ii) Bora/ zuri (alama 2)

<u>FASIHI SIMULIZI</u>

6. Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalumu cha mwaka. *(1x2=alama2)*

b) Sifa za miviga
- Miviga huandamana na matendo Fulani k.m kucheza ngoma, kupioga magoti
- Huongozwa na watu mahususi k.m kuna wanaongoza kafara
- Huandamana na utoaji mawaidha/ulumbi
- Maleba huvaliwa na wanaohusika
- Hufanyiwa katika mazingira maalum
- Huambatana /hufungamna na utamaduni wa jamii husika
- Hufanya katika kipindi/wakati maalum
- Huwa na kutolewa kafara
- Sadaka hutolewa

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Kuna kula viapo – wahusika huweka ahadi kutenda wema *(zozote 5x1=alama5)*

c) Udhaifu
- Husababisha kudorora kwa maendeleo
- Huleta utengano kati ya jamii/majirani
- Huasi mabadiliko ya kiwakati (nyingine zimepitwa na wakati)
- Madhara yaweza kutokea hasa vifaa butu vinapotumika
- Huleta utengano wa kijinsia, kumtukuza mwanaume na kudunisha mwanamke k.m jando na unyango *(zozote 3x1=alama3)*

d) Umuhimu wa ngomezi
- Ni njia ya kuwasiliana katika jamii husika
- Hudumisha usiri wa jamii husika
- Hutumiwa kutangaza matangazo muhimu kuhusu shughuli maalum
- Huendeleza utamaduni wa jamii
- Huisaidia jamii kuionea fahari historia yao
- Hutahadharisha kuhusu matokeo ya dharura
- Hudhihirisha ufundi wa kisanaa (kutumia zana Fulani za muziki)
- Hutekeleza majukumu ya maandishi katika jamii zisizojua kuandika
- Huburudisha *(zozote 6x1 = alama 6)*

e) Vizingiti
- Mwingiliano wa makabila tofauti hauruhusu tena matumizi ya ngomezi
- Maendeleo ya teknolojia hayaruhusu ngomezi k.m barua, simu
- Watu wamekuwa wabinmfsi – hawawezi kuitika ngoma ikipigwa
- Ukosefu wa usalama – watu kushambiliwa wakiitikia wito wa ngomezi *(zozote 2x1=alama 2)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**

1) Kumezuka ugonjwa hatari katika nchi yako unaoitwa virusi vya korona. Wewe ukiwa mkurugenzi mkuu wa afya, mwandikie waziri wa afya barua pepe ukimwelezea kuhusu athari na njia za kukabiliana na ugonjwa huo.
2) “Mitandao ya kijamii ina faida na hasara. Jadili
3) Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
Nazi mbovu harabu ya nzima
4) Andika insha ambayo mwisho wake utakuwa:
Lo! Sikuamini kuwa ni yeye alitenda kitendo nilichokiona. Waama ni kweli, umdhaniaye ndiye siye.

**MURANGA SOUTH**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI 2**
**(Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimu Jamii)**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

1. **UFAHAMU**.(alama 15)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalau, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu kwa kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kiwango cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii inasagana na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilika badilika. Isitoshe kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari yameghoshi ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na mazingira zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa, pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya

kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko na anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo kuna vighairi hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mapito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni, Je tunahusiana vipi na jamaa zetu, taaisisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

**Maswali.**

a) Bainisha ujumbe mkuu unaujitokeza katika kifungu hiki. (alama 1)
b) "Binamu hawezi kuishi bila mahusiano". Thibitisha kwa kurejelea hoja **nne** katika kwenye kifungu. (alama 4)
c) Fafanua athari za teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)
d) Bainisha changamoto **nne** zinazotokana na kuharibika kwa mahusiano. (alama 4)
e) Eleza mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika kifungu. (alama 1)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
   (i) Inasigana
   (ii) yameghosi
   (iii) vighairi

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

2. **MUHTASARI (alama 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**

Sisi vijana wa Kenya inatuwajibikia kufanya kazi kwa bidii, na kwa dhati ya moyo wetu tuweze kupata ufanisi, na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke " ajizi ni nyumba ya njaa" kwa hivyo hatufai kulaza damu tukiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani Zaidi elimu ya vijana na ya watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo. Tupende, tusipende lazima tuzidishe mazao ya mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu nchini inaongezeka. NI sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo pia lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba lazima kila mmoja aajiriwa maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya mwananchi wa Kenya badala ya kuwaachia ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayoyapata majumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele, sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu lazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja, "utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kitatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu, wakati tunapokosea lazima tukubali tumekosea na kufanya masahihisho mara moja, kwani "usipoziba ufa utajenga ukuta". Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi. Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu mashuleni na majumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, Amani na upendo. Lazima tuwe na bidii na ushirikiano mwema kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni lwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo atokao ama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi, tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba kubwa ya utajiri.

**Maswali**

a) Fupisha aya ya kwanza ( maneno 60—70) (alama 7 na 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**
**JIBU.**

b) Eleza mambo muhimu anayoibua mwandishi katika aya ya pili . (maneno 90 - 100) (alama 6 na 1 ya mtiririko)
**Matayarisho**
**JIBU**

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

(a) Taja zinapotamkiwa sauti mwambatano zifuatazo. (alama 1)
i) /ng/
ii) /bw/
iii) Jaza mapengo katika sentensi zifuatazo. (alama 1)
i) Kikwamizo kizito cha kaakaa laini.--------------------
ii) Irabu ya mbele juu--------------------------

(b) Andika maneno yenye miundo ifuatayo. (alama 2)
(i) KIKKIKI
(ii) IIKKI

(c) Ainisha mofimu katika neno. (alama 3)
Lilililimia

(d) Wanafunzi walifanya <u>bidii</u> katika somo la Hisabati. (alama 2)
(Geuza neno lililopigiwa mstari kuwa kitenzi)

e) Tunga sentensi kudhihirisha dhana tatu za kiimbo. (al.3)

(f) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati uliopita hali timilifu. (alama 2)
Nyundo hii imevunjika mpini wake.

(g) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia kinyume cha neno lilopigiwa mstari. (alama 1)
Nyanya <u>aliomboleza</u> kwa siku kadhaa wakati wa matanga ya bintiye.

(h) Tunga sentensi ukitumia:- (alama 2)
(i) Kihusishi cha mtenda.
(ii) Kihisishi cha majuto.

(i) Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-ZI (alama 2)

(j) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
KN (N + V) + KT (T + RH + RE)

(k) Andika upya sentensi ifuatayo ukianzia kwa yambwa tendewa. (alama 2)
Wafugaji waliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo.

(l) Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana mbili tofauti. (alama 2)
Julius ngeno mwanawe Kallu na Fatuma walikiletea kijiji chao sifa.

(m) Andika katika udogo wingi. (alama 2)
Nyoka yule mrefu aliingia katika nyumba.

(n) Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)
Mama aliwaendea watoto wale.

(o) Changanua sentensi zifuatazo kwa kuzingatia maagizo uliyopewa mabanoni.
(i) Haya yao yalikuwa yameiva lakini hawakujua. (Tumia kielelezo cha mstari) (alama 2)
(ii) Tunda li mtini. (Kielelezo cha matawi) (alama 2)

(p) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya shombo na chombo. (alama 2)

(q) Geuza sentensi ifuatayo iwe na kishazi tegemezi. (alama 2)
Mzee alifika jana na ataondoka kesho.

(r) Unda nomino dhahania kutokana na kitenzi zembea. (alama 1)

(s) (i) Jino linapong'oka huacha pengo, hali jeraha linapopona huacha __________ (alama 2)
(ii)Bumba ni kwa nyuki ______________________ ni kwa nyota na __________________ ni kwa nzige

4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)

Abdii: Unafikiria hii kesi tutaimanage?
oketch: Labda tukisweet talk huyo resident magistrate.
Hassan: What if tukimchotea something small?

(a) Mtindo uliotumika katika mazungumzo haya ni upi? Toa sababu. (alama 1)
(b) Eleza sababu **nne** zinazopelekea wazungumzaji kutumia mtindo huu? (alama 4)
(c) Serikali inafanya juhudi kukiendeleza Kiswahili sanifu nchini Kenya, eleza juhudi zozote **tano**. (alama 5)

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

**MURANGA SOUTH**
**102/3**
**KARATASI YA 3**
**KIDATO CHA NNE**
**FASIHI**

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

1) Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Nani kama Shivachi?
Shivachi wa Tetei
Tena mwanamberi wake
Ni mimi niliyeshika ngao
Nikaongoza kikosi maalum
Tukawapiga maadui na kuwarudisha kwao
Mimi ni mwamba
Thabiti kama Ikhongo Murue
Jiwe kuu la Ilesi
Shivachi mwenye mundu uliong'aa kwa makali
Uliopita katikati ya Ulweso Aliyejifanya kiongozi
wa maadui Sasa yu wapi?
Nani kama Shivachi?

a) Taja kipera cha kifungu ulichosoma cha ushairi simulizi. (ala 2)
b) Eleza sifa za kipera ulichotaja. (ala 5)
c) Maudhui na fani ya maigizo hutegemea mwigizaji. Thibitisha kauli hii kwa hoja tano (ala 5)
d) Eleza majukumu matano ya miviga katika jamii (ala 5)
e) Taja njia tatu za kukusanya data katika fasihi simulizi (ala 3)

For more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B TAMTHILIA: KIGOGO**

2) "Acha lakini zako, nikumbatie kipenzi"
   a) Weka dondoo hii katika muktadha wake (ala 4)
   b) Onyesha hulka mbili za msemaji zinazojitokeza katika dondoo hili (ala 4)
   c) Jadili maudhui ya ukandamizaji wa mwanamke kwa kuzingatia tamthlia nzima (ala 12)

3) a) Tamthilia ya Kigogo inaangazia maisha halisi ya jamii za Kiafrika.Jadili. (ala 10)
   b) Kwa kurejelea tamthilia nzima ya Kigogo jadili nafasi chanya alizopewa mwanamke . (ala 10)

**SEHEMU C: RIWAYA: CHOZI LA HERI**

4) "Kipi kilimpa mama uyabisi wa moyo hata akawaacha wanawe?"
a) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. (ala 4)
b) Tambua tamathali ya usemi katika dondoo hili (ala 2)
c) Eleza masaibu yanayowapata wanajamii kutokana na uyabisi wa wanawake ukirejelea riwaya nzima. (Hoja 14 x 1 = 14)

5) Fafanua jinsi mwandishi wa chozi la Heri alivyofaulu katika matumizi ya mbinu zifuatazo
   **a)** Taswira (ala 10)
   **b)** Majazi (ala 10)

**SEHEMU D: USHAIRI**

Soma shairi hili kisha ujibu maswali
Sinusubuwe akili, nakusihi e mwandani
Afiya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende siptalini Sisi tokea azali,
twende zetu mizimuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani Tuna dawa za asili,
hupati sipitalini
Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
Dawa yake ni subili, au zogo huauni
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumba
Japo maradhi dhahili, kuteguliwa
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Waambiwa damu, kalili ndugu msaidieni
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mizimu wakupa kweli, wakueleza undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wa majano na wa kijani
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi mlangoni?

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Andika anwani inayofaa kwa shairi hili. (ala 1)
b) Kwa nini mshairi hataki kwenda hospitali: (ala 3)
c) Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi (ala 4)
d) Tambua bahari zilizotumika katika shairi hili (ala 2)
e) Eleza nafsineni katika shairi hili (ala 1)
f) Tambua toni ya shairi hili (ala 1)
g) Eleza muundo wa shairi (ala 4)
h) Fafanua idhini ya mshairi inavyojitokeza katika shairi hili (ala 2)
i) Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili (ala 2)
   i) Mwandani   ii) Ndwele

**SEHEMU E: HADITHI FUPI : TUMBO LISILOSHIBA**

"…si hamhitaji ndege mnapotaka kusafiri au siyo? Mnaruka tu hewani kama ndege"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala 4)
b) Tambua mbinu za tamathali za usemi zilizotumika katika dondoo hili (ala 2)
c) Eleza sifa na umuhimu wa msemaji (ala 6)
d) Kwa kurejelea hadithi nzima thibitisha maudhui yaliyokuwa yanazungumziwa na wahusika katika dondoo hili (ala 8)

**<u>MURANGA SOUTH</u>**
**<u>KISWAHILI KARATASI YA KWANZA INSHA</u>**
**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA</u>**

1) Huu ni utungo amilifu. Muundo wake wa kipekee ni lazima udhihirike. Vipengele viwili vikuu vya insha ya aina hii ni lazima vishughulikiwe.
   Vipengele hivi ni:-
   a) Muundo
   b) Maudhui

a) **Muundo**
Mtahiniwa azingatie muundo au sura ya barua pepe.

Vipengele vifuatavyo vya kimsingi Viweze kuzingatiwa:

i) Anwani ya barua pepe ya anayeandika barua kwa mfano:

Kutoka kwa: Awani ya mwandishi

ii) Anwani ya barua pepe ya anayeandikiwa barua. Kwa mfano:
Kwa: Anwani ya mwandikiwa

iii) Mada: kwa mfano
Athari za ugonjwa wa virusi vya korona na njia za kukabiliana nao.

iv) Tarehe ya kutumiwa kwa barua

v) Utangulizi

vi) Mwili. Hapa ndipo hoja zitakapojadiliwa
Hoja zipangwe ki –aya huku zikifafanuliwa.

vii) Hitimisho. Mtahiniwa ahitimishe utungo wake.

viii) Kimalizio
Muundo wa mwisho wa barua pepe udhihirike. Kwa mfano pawe na:
Sahihi
Jina
Cheo

b) Maudhui
Mtahiniwa aweze kuibua hoja ambazo zinahusiana na athari za ugonjwa wa virusi vya korona na njia za kukabiliana nao.
Hoja ni kama vile:

Athari

1) Watu kuaga dunia
2) Biashara nyingi kusambaritika
3) Uchumi wa nchi kuporomoka
4) Pesa nyingi kutumika katika kuuguza wagonjwa
5) Taasisi za elimu kufungwa
6) Sekta kama vile usafiri na utalii kuathirika
7) Mizozo ya kifamilia kuongezeka
8) Athari za kisaikolojia

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Njia za kukabiliana na ugonjwa huu

1) Kuzingatia usafi kama vile kunawa mikono mara nyingi na kutukasa kila mahali.
2) Kuvalia barakoa
3) Kuepukana na sehemu zilizo na watu wengi
4) Wahudumu wa afya kuvalia mavazi ya kujikinga
5) Kula matunda ya kuongezea nguvu za kujikinga na magonjwa
6) Kukaa nyumbani ukihisi dalili zozote za ugonjwa
7) Kusalia nyumbani ikiwa hauna shughuli ya lazima.

Tanbihi
Mtahiniwa atachukuliwa amejitosheleza kimaudhui iwapo atakuwa na angaa hoja tano na zaidi zilizofafanuliwa kwa mapana.
Akizitaja tu atakuwa amepungukiwa kimaudhui
Mtahiniwa akikosa sura ya barua pepe aadhibiwe kwa kutolewa alama nne za sura s4

2) Hii ni insha ya mjadala. Hili ni swali la hoja ambapo mtahiniwa anaweza kutaja faida na hasara za mitandao ya kijamii. Hoja hizi zinafaa kuwa zimefafanuliwa ili mtahiniwa awezee kujitosheleza kimaudhuni.

Faida za mitandao ya kijamii

a) Utangamano. Huunganisha watu bila kujali asili yao.
b) Watu huburundika kupitia mitandao, sinema na vichekesho

c) Husaidia katika biashara
d) Huwezesha maingiliano ya watu
e) Hurahisisha mawasiliano duniani
f) Huimarisha utafiti
g) Nchi hupata ushuru unaolipwa kupitia biashara za mitandao
h) Watu wengi hupata ajira kutokana na mitandao ya kijamii.

Hasara za mitandao ya kijamii

a) Vijana kuzembea kuwa kushinda mitandaoni ya kijamii
b) Wizi kupitia mitandao
c) Uenezaji wa picha chafu
d) Kugharimu pesa nyingi zinazoweza kutumika katika kuboresha maisha
e) Kutumiwa kuingilia maisha ya watu binafsi

3) Hii ni insha ya methali kisa ambacho mtahiniwa atatunga kidhihirishe maana ya methali. Maana ni kuwa mtu mwovu akiwa katika kundi la watu anaweza akawambukiza watu darasa lenye wanafunzi waadilifu. Kukija mwanafunzi mgeni ambaye ni mtovu wa maadli anaweza kuwaharibu waliokuwa waadilifu.

Kisa kinaweza kudhihirisha hali zifuatazo

i) Mwanfunzi mgeni kuwaharibu wanafunzi waliokuwa waadilifu
ii) Muumini mgeni kanisani awaharibu waumini waliokuwa wacha Mungu.
iii) Katika taasisi yoyote ile wafanyikazi wazuri wanaweza kuharibiwa na mfanyikazi mmoja.

TANBIHI

Methali mara nyingi huwa na sehemu mbili . Kisa cha mtahiniwa kiweze kudhihirisha sehemu mbili za methali.
Mtahiniwa aonyeshe uovu wa mhusika na jinsi uovu huo uliambukizwa wengine.
Hata hivyo pande zote mbili si lazima zitoshane.
Wale ambao wataandika kisa kisichohusiana na methali watakuwa wamepotea kimaudhui.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

4) Hii ni insha ya mdokezo. Maneno kiini katika mdokezo huu ni kutoamini kuona alichokiona. Alishangaa kwa kuona kitendo kibaya alichokiona kikitendwa na mtu aliyemdhania kuwa ni mzuri. Kuna ile dhana ya kinaya kwa kuona kile hakutarajia.
Mtahiniwa anatarajiwa kutunga kisa kitakachooana na mdokezo aliopewa.
Anaweza kurudi nyuma kwa kutumia mbinu rejeshi akisimulia kisa hadi akafikia pale ambapo anashangaa kwa kile alikiona.
Kinaweza kuwa ni kitendo chochote kile kiovu kinachomshangaza.
Tanbihi

i) Mtahiniwa atakuwa amepotoka kimaudhui iwapo kisa chake hakitaoana na mdokezo.
ii) Kwa vyovyote vile lazima pawe na jambo ambalo linamshangaza
iii) Asipomalizia kwa mdokezo atakuwa amepungukiwa kimtindo, akadiriwe vilivyo MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**<u>MURANGA SOUTH</u>**
**<u>KISWAHILI KARATASI YA PILI</u>**
**<u>MWONGOZA WA KUSAHIHISHA</u>**

1. Ufahamu.

(a) Mahusiano katika jamii / aina za mahusiano katika jamii. (1 x 1 = al 1)

(b) (i) Kuna uhusiano wa kudumu wa mtu na jamaa yake.
(ii) Kuna mahusiano yanayohusisha washirika wetu wa karibu k.v marafiki na majirani zetu.
(iii) Kuna mahusiano ya muda mfupi ya huduma za kila siku k,v dukani, ibadani, kinyozini n,k
(iii) Mahusiano ya chembe ndogo ya watu inahusu huduma ndogo ambazo hazidumu kwa muda mrefu.
(4 x 1 = al 4)

(c) (i) Huwezesha watu au jamaa wako mbali kuwasiliana.
(ii) Hudumisha uhusiano wa kiijamii. (2 x 1 = al 2)

(d) (i) Talaka - huvunja uhusiano baina ya mke na mume.
(ii) Ubadilishaji wa kazi.
(iii) Mifumo ya kimataifa na kisiasa.

(iv) Mabadiliko ya maisha ya mjini.
(v) Uhamaji
(vi) Kufutwa kazi. (za kwanza 4 x 1 = al 4)

(e) Swali la balagha - Je uhusiano wetu na nchi ni wa mpito au ni wakudumu?
Kinaya - inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamii huweza yasiwe ya kudumu.
Jazanda / istiari - uhusiano wa chembechembe. (1 x 1 = al 1)

(f) inasigana - inapigana / inakinzana / inatofautiana/ inahitilafiana
yameghoshi - yamejaa / yamesheheni / yamerundika
Vighairi - vinyume / tofauti (3 x 1 = al 3)
Adhibu kosa la sarufi: litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita 1/2 x 6 = al 3
Adhibu kosa la tahajia litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita 1/2 x 6 = al 3

**2. MUHTASARI**

**(a)**

– Sisi vijana wa Kenya inatuwajibikia tujibidiishe kazini ili tufanikiwe na kuinua nchi yetu.
– haifai kulaza damu tukiwa matatizo yametuzonga.
– Lazima tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani.
– bila elimu itakuwa vigumu kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo.
– lazima tuzidishe mazao ya mashambani kwani idadi ya watu inaongezeka.
– Lazima tujishughulishe na biashara.
– Yatupasa kuleta uchumi mikononi mwa wakenya badala ya kuwaachia wasiohusika. (alama 7)

(b)

– Mafunzo tunayoyapata majumbani, shuleni na katika jamii lazima yatutambulishe na mbinu za kupitia.
– Elimu tambuzi inapaswa imfanye mwanakenya kujua wajibu wake.
– Elimu pumbao inatufanya tusione mbele.
– Vijana wanapaswa kuwa kielezo chema kwa wengine
– Lazima watu washirikiane na kuwa na umoja.
– Lugha ya taifa ndicho chombo kinachotuunganisha
– Tunapokosea, tukubali na kufanya masahihisho
– Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi kama wazalendo.
– Tujishughulishe na kuyangalia matatizo ya nchi na kuyatatua.
– Tuwe na nidhamu.
– Tuwe na bidii na ushirikiano kuwachagua viongozi wanaopenda maendeleo.
– Tusichague viongozi kwa kufuata ukoo au utajiri. (alama 8)

3 Matumizi ya lugha.

a) i Kaaka laini
ii) midomo
iii) /gh/
iv) /i/ 2×1/2

(b) Mifano: (i) Daftari, daktari n.k
(ii) aende n.k

(c) li-ngeli
li-wakati
li-kirejeshi
lim -mzizi
i-kauli
a-kiishio. Al 3

(d) Wanafunzi walijibidiisha katika somo la Hisabati.

c) i) swali
ii) kauli
iii) mshangao
iv) rai
v) amri 3x1

(f) Nyundo hii haikuwa imevunjika mpini wake.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(g) aliomboleza - alifurahia / alisherehekea

(h) (i) Mtoto amechapwa <u>na mamake</u>

(ii) Kwa mfano: laiti, lau, ole wangu, Afana / ek 2 x 1 = al 2

Tanbihi: Kadiria jibu la mwanafunzi.

(i) Mianzo: ufa –nyufa

Wimbo- nyimbo

Ukuta-kuta./ubao -bao

(j) Mifano:

Ndoo nyeupe iliokotwa kando ya barabara jana usiku.

Paka mweupe aliketi chini ya meza jana jioni.

Tanbihi: Kadiria jibu la mwanafunzi.

(k) Ng'ombe wote walikatiwa majani ya mti huo na wafugaji.

(l) (i) Julius, Ngeno, mwanawe Kallu na Fatuma walikiletea kijiji chao sifa.

(ii) Julius Ngeno, mwanawe Kallu na Fatuma walikiletea kijiji chao sifa.

(iii) Julius Ngeno. (mwanawe Kallu) na Fatuma walikiletea kijiji chao sifa. (zozote 2 x 1 = al 2)

(m) Vijoka vile virefu viliingia katika vijumba. (2 x 1 = al 2)

(n) Wakitie chakula tumboni.

kiashiria / kionyeshi watoto wale

o) S-S1KN(W+V)+KT(T+T)+U+KN()+KT(T)

S

KN KT

N T E

Tunda li mtini

Alienda kwa niaba yao. (zozote 2 x 1 = al 2)

(p) Chombo -kitu cha kufanyia shughuli fulani. Mfano-Arusi yake alipewa zawadi ya vyombo vya jikoni

- pambo la mwanamke kama kidani
- kifaa cha kutilia kitu kama vile ndoo na mtungi
- kitu cha kusafiria

Shombo – harufu isiyopendeza.chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka shombo

(q) Mzee aliyefika jana ataondoka kesho.

Mzee ambaye alifika jana ataondoka kesho. (zozote 2 x 1 = al 2)

(r) uzembe 1/0

(s) (i) kovu

1/0

(ii) Thurea

(iii) Wingu.2 x 1 = 2

Adhibu

hijai - makosa 6 (al 3)

sarufi - nusu ya alama zilizotengewa swali.

4. Isimujamii (al 10)

(a) Kuchanganya ndimi / kuchanganya msimbo. (al 1)

(b) Kificha siri.

Kutenga hadhira

Kuwa na umilisi wa lugha mbili au zaidi.

Kutoelewa lugha moja sawasawa.

Kuonyesha umahiri wao katika lugha zote

Kujihusisha na kundi fulani la wazungumzaji.

Kuonyesha hisia za kirafiki.

Kuathiriwa na malezi / mazingira / mazoea.

Uhaba wa msamiati wa wazungumzaji.

(c) Kukiingiza kwenye tarakilishi.

Kuunda majopo ya kiswahili ya wataalamu kutafiti.

Kufadhili utafiti.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Kinatumika bungeni
Katiba ya 2010 kutambua kiswahili kuwa lugha rasmi.
Kuhimiza uchapishaji wa vitabu / majarida.
Kufundishwa vyuoni / shuleni
Kiswahili kinatumika katika biashara.
Kiswahili kimeteuliwa kuwa lugha ya taifa.
Kiswahili kinatumika katika matangazo / taarifa / maabadini.

MURANGA SOUTH
KISWAHILI KARATASI YA TATU
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

FASIHI SIMULIZI
1) a) Majigambo / Vivugo (ala 2)
b) Sifa za majigambo
- Hutungwa na kughaniwa na mhusika
- Hutumia tamathali k.v. sitiari, ishara na takriri
- Aghalabu hughaniwa na wanaume
- Hutumia nafsi ya kwanza
- Anayeghani huweza kuvaa maleba na kuonyesha vifaa vya kazi
- Maudhui makuu ni ushujaa (zozote 5 x 1 = 5)

c)
- Sharti mwigizaji aigize kwa ujasiri ili aweze kupitisha ujumbe wake kwa ufasaha. ii) Awe na uwezo wa kufaragua yaani aweze kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake. iii) Aweze kutumia ishara za uso, za mwili na miondoko ambayo inaoana na hali anayoigiza (viziada lugha)
- Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha
- Aelewe hadhira yake ili abadilishe mtindo wa uigizaji kulingana na kiwango na matakwa yao
- Anafaa kuvaa maleba yanayooana na nafasi anayoigiza
- Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti tofauti za matukio anayoigiza
- Aweze kushirikisha hadhira kwa kuuliza maswali ili kuondoa uchovu (zozote 5 x 1 = 5)

d) Majukumu matano ya miviga katika jamii.
- Hukuza utangamano katika jamii
- Huwafunza wanajamii mila, kaida na desturi za jamii
- Hukuza na kuendeleza vipawa
- Ni njia mojawapo wa kuhifadhi utamaduni wa jamii
- Ni njia ya kurithisha vizazi vichanga utamaduni wa jamii vi) Huburunddisha jamii (zozote 5 x 1 = 5)

e) i) Mahojiano ii) Uchunzaji iii) Matumizi ya hojaji
iv) Kurekodi kazi za fasihi simulizi katika kanda za sauti na video
v) Kujihusisha moja kwa moja na uwasilishaji wa fasihi simulizi / mbinu ushiriki (zozote 3 x 1 = 3)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

TAMTHILIA : KIGOGO
2) a) Msemaji ni Majoka
Msemezwa ni Ashua
Mandhari ofisini mwa Majoka
Ashua amemtembelea Majoka ofisini ili kuomba msaada kwa sababu ya shida zinasomkumba.
Majoka naye anatumia nafasi hiyo kumdhulumu kimapenzi

b) i) Majoka
a) Ni mwenye tamaa ya mapenzi Anamdhulumu Ashua kimapenzi
b) Ni mwasherati / Mkware
Anamtaka Ashua kimapenzi ilhali ana mke kwake nyumbani

c)

1) Ashua kupigwa na askari akiwa gerezani
2) Kudhulimiwa kimapenzi. Majoka anamwambia Ashua amkumbatie
3) Kubezwa. Tunu anakejeliwa na Ngurumo na walevi wengine
4) Majoka anamtaka Ashua kimapenzi anapoenda kuomba msaada ofisini mwake
5) Kufanywa kijakazi nyumbani. Majoka anamtuma chopi kumwagiza mkewe kumpikia kuku na kumwokea chapati
6) Kutusiwa. Boza anamwambia Sudi kuwa asifikiri kuwa yeye anauza nyonga kama Tunu wake.
7) Ashua anafungwa na Majoka bila sababu
8) Wanawake wananyimwa uongozi.Ngurumo anamwambia Tunu kuwa kama hampi kura Majoka ni heri ampe paka wake Majoka lakini si mwanamke .
9) Wanawake wananyimwa ajira. Licha ya Ahsua kufuzu taaluma ya ualimu hakuajiriwa. Anaishia kuchuuza maembe sokoni
10) Kuozwa bila hiari. Majoka anataka kumwoza Tunu kwa mwanawe Ngao junior
11) Kunyimwa fidia. Majoka alitaka kumnyima fidia Hashima baada ya kifo cha mume wake.

3) a)
- Sera mbaya ya uongozi zinazosababisha umaskini
- Utabaka – Huwa pana mpaka mkubwa baina ya matajiri na maskini kama ilivyo Sagamoyo.
- Viongozi katili kuwaangamiza wapinzani wao k.m Jabali
- Viongozi wengi husahau wananchi waliowachagua na huendela kujilimbikizia mali k.m Majoka na vikaragosi wake. vi) Baadhi ya washauri wa viongozi wengi duniani huwapotosha k.m Kenga vii) Wananchi kulipa kodi bila kupata huduma wanazostahili
- Kuwepo kwa maandamano ya wanaharakati k.m madaktari na walimu. Pia Tunu anaongoza maandamano
- Kuwepo kwa urithishaji wa uongozi k.m Majoka anamwambia Kenga kuwa alikuwa na azma ya kumtangaza Ngao Junior kama mrithi wake Kisiasa.
- Utegemezi wa mikopo na misaada kutoka Ughaibuni (zozote 10 x 1 = 10)

b)
- Ni mkombozi k.m Tunu anatetea haki za wanyonge na kuleta mageuzi ii) Ni mtetezi wa haki k.m Ashua na Tunu wako mstari wa mbele kutetea haki za wanyonge iii) Mwenye utu k.m Tunu anamshauri Siti awapeleke watoto wa Sudi kwao.
- Ni jasiri k.m Ashua anamkosoa Majoka bila uoga. Tunu anamuweza Majoka kwa kumwita tapeli.
- Ni mcha Mungu k.m Hashima anaamini Mungu amekasirishwa na umwagikaji damu Sagamoyo
- Ni msomi – Ashua ana shahada ya ualimu – Tunu ni dakatari wa Uanasheria.
- Ni mwenye heshima k.m Siti anamsalimu mamake Tunu kwa heshima viii) Mwenye bidii k.m Ashua anatia bidii kazini kumsaidia mumewe kuikimu familia ix) Ni mwadilifu k.m Ashua anakataa kumvunjia Sudi heshima licha ya shinikizo za Majoka
- Mtiifu – Siti anakubali kuwapeleka watoto wa Sudi kwa akina Tunu
- Mwenye msimamo dhabiti k.m Tunu na Ashua wanakataa kushawishiwa na Majoka (zozote 10 x 1 = 10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

RIWAYA: CHOZI LA HERI

4) a)

i) Msemaji – Umulkheri / Umu
ii) Msemewa – nafsi yake / alijiuliza mwenyewe
iii) Sababu – Alimlaani mama yake ambaye aliwatelekeza. Sauna alikimbia na ndugu zake baada ya kifo cha baba yao.
iv) Mahali - nyumbai kwao (4 x 1 = 4)

b) i) Jazanda – uyabisi wa moyo ii)
Balagha – dondoo lote
Yoyote 1
m.f 1
Jumla ala 2

4) c)
- Uavyaji mimba. Mamake Sauna anamsaidia Sauna kuavya mimba
- Ndoa kuvunjika. Badala ya Subira kutatua mgogoro wake na mavya wake anaamua kuiacha familia.
- Ulanguzi wa watoto. Sauna anaudhika kwa kutotetewa na mamake alipobakwa na babake
- Uyatima - Subira anapojitia kitanzi anawaacha wanawe Lime na Mwanaheri kama mayatima
- Upweke – Naomi anawatoroka Umu na ndugu zake
- Vifo – Wanawake wengi wameavya mimba na kusababisha vifo vya watoto wachanga
- Magojwa - Lunga anpatwa na ugojwa wa shinikizo la damu
- Dhiki ya malezi – Lunga anaachiwa uchugu wa kuwalea watoto wake na Naomi
- Ukosefu wa malezi bora - Chandachema anakosa malezi bora.
  Ndoa za mapema –
- Mamake Pete alilazimishwa kuolewa na mzee Fungo akiwa darasa la sa saba.
- Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi Pete anatelekezwa na mamake na hivyo kukosa mahitaji.
- Utekaji nyara - Dick na Mwaliko walitekwa nyara na kijakazi Sauna
- Ajira za watoto - Sauna anaajiriwa kuwalangua watoto
- Ukosefu wa karo – Licha ya kuwa na mamake – Neema anakosa karo
- Kazi ya sulubu - Watoto wachanga wanafanya kazi ya sulubu kwa mfano Chandachema
- Dhuluma za kimapenzi – Pete anadhulumiwa kimapenzi na Nyangumi
- Mimba za mapema – Pete anozwa na mamake kwa mzee Fungo na kupata mimba za mapema.

5 a) Taswira
- Watu waking'ang'ania petroli kutoka kwa lori lililoanguka barabarani
- Maombolezi na maziko ya Dede
- Watoto wakiigiza maombolezi ya Dede
- Ridhaa akitoa mshipi kumcharaza Mwangeka kwa hasira
- Mwanafunzi aliyevaa sare mbele ya gwaride
- Picha ya makabiliano kati ya polisi na waakaji wa msitu wa Mamba
- Umu akiongea na askari wajeuri
- Umu akimsihi mamake ampe shilingi mia moja kisha anatoa shilingi mia mbili kwa ndangarizi yake na kumpa ombaomba
- Kundi kubwa la vijana mbele ya hoteli
- Majonzi ya mama Kairu na wanawe wakiuzika mwili wa mtoto kichakani
- Zohali akiwangukia wazazi wake miguuni
- Taswira ya Hitman
- Taswira ya Apondi akihutubu
- Picha ya Lemi akipigwa na umati
- Dick anapokutana na Umu kwenye uwanja wa ndege
- Shamshi na chupa yake mkononi (zozote 10 x 1 = 10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Majazi
- Ridhaa – maana ya kuridhika inambidi akubali familia yake imeangamia
- Kedi – linamaanisha kiburi – Anaaongoza uvamizi dhidi ya familia ya Ridhaa
- Waziri Tendakazi
  Anatimiza ahadi ya kubomoa nyumba katika eneo la Tononokeni.
- Nchi ya wahafidhina – Watu wasiopenda mabadiliko hasa ya kuongozwa na mwanamke
- Hazina – Kijana wa mta aliyepewa shilingi mia mbili na Umu. Inakuwa hazina kwa Umu
- Tangamano – wanafunzi wa shule hii wanatoka sehemu nyingi na kutangamana vii) Dhahabu – ni mwalimu wa thamani kwa wanafunzi wa thamani
- Zohali – Zohali ni uzito. Suala la kupata mimba lilikuwa zote kwa Zohali. ix) Shangazi Waridi – Alikuwa ua la kupendeza maishani mwa Chandachema
- Bwana Mwenge – anakuwa mwenge wa matumaini kwa Chandachema
- Mtaa wa Afueni – mataa wa kupata nafuu na pumziko
- Mtaa wa Kazikeni – mtaa wanakoishi maskini

- Hoteli ya Majaliwa – ni majaliwa ya kuwakutanisha Mwangeka, Dickson na Umukheri pamoja na mwangemi akiwa na Mwaliko.

Ushairi

6)

a) Nifuateni sipitali / dawa ziko nyumbani (1 x 1 = 1)

b) Tangu zamani wao huenda muzimuni masawa ya asili yapo
Hapendi upasuaji
Mtu anweza kupoteza maisha
Anafuata kielelezo cha mababu zetu (3 x 1 = 3)

c) Mtu akienda hospitali ni kwa kutojua vizuri kuwa daktari akiona mwili atasema ni saratani ya tumbo. Atavitia visu makali kujitayarisha kufanya upasuaaji. Operesheni atakukata viungo vya ndani. Kwa nini kwenda hospitalini iIlhali dawa ziko nyumbani (1 x 3 = 3)

d) i) mtiririko ii) mathnawi [ 2 x 2 = 2 ]

e) mgonjwa / anayeugua [ 1 x 1 = 1 ]

f) Huzuni / masikitiko / lawama / malalamiko [ 1 x 1 = 1] g)
- Beti sita
- Kila ubeti una mishororo mitano / takhimisa
- Kuna ukwapi na utao katika kila mshororo
- Kuna kibwagizo isipokuwa ubeti wa sita
- Kuna urari wa vina
- Kila mshororo una mizani 16 , ukwapi 8 utao 8 [ 4 x 1 = 4 ]

h) i) Inkisari- Taabani, waambiwa , sipitali ii)Tabdila- Afiya – Afya 2 x 1 = 2 ]

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA

a) Msemaji ni Kazu
Anamwambia Sebu
Wamo katika 'Hotel Rombeko'
Walikuwa wanazungumzia uchawi au ushirikina. Kazu ndiye aliyekuwa ameanzisha mada hii.

b) Swali la balagha – au siyo?
Tashibihi – Mnaruka hewani kama ndege

c) Sifa na umuhimu wa Kazu
- Mcheshi
- Mshirikina
- Mwenye mapenzi ya dhati
- Karimu
- Mpenda anasa

Umuhimu
Ni kiungo muhimu katika kuwaunganisha Sebu na Bogoa
Ametumika kuendeleza maudhui ya anasa na ushirikina

d) Maudhui ya ushirikina
- Inaaminika Wamate hawahitaji ndege kupaa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa mujibu wa Kazu. Wanaweza kuruka na kutua kwa kutumia uchawi.
- Kwa madai kuwa kulikuwa na chatu katika Seka aliyetambaa kutoka Mashariki hadi Magharibi huku akimeza maelfu ya watu
- Kuna madai kuwa huko Mate ukipiga pakacha teke usiku njiani linakwambia 'Bwana we, huoni kwamba unaniumiza?
- Sebu anopendekza uchawi kutambuliwa kama sayansi iliyofichama
- Sebu anaeleza kuwa kwao Mate mtu angerushwa kiuchawi kama ilivyofanyika kwa rafikiye Bogoa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**DAYOSISI YA KISII**
**HALMASHAURI YA MITIHANI, SHULE ZA JIMBO KATOLIKI, KISII**
**TATHMINI YA PAMOJA YA MTIHANI WA DEC. 2020**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1**
**INSHA**

1. **Insha ya lazima**
   Kumekuwa na matokeo mabaya ya Kiswahili kwa kipindi cha miaka mitatu mtawalia.
   Umeteuliwa kama mtaalamu katika kaunti yako kuchunguza kiini cha matokeo haya mabaya. *Andika ripoti ya uchunguzi wenu.*
2. Umaskini ni changamoto kubwa katika maendeleo ya magatuzi. Jadili.
3. Mchumia juani hulia kivulini.
4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Mlango wa nyuma ulibishwa mara mbili Ngo! Ngo! Kufungua tu, nikasikia sauti "lala chini…………………

**DAYOSISI YA KISII**
**HALMASHAURI YA MITIHANI, SHULE ZA JIMBO KATOLIKI, KISII**
**TATHMINI YA PAMOJA YA MTIHANI WA MWIGO DEC. 2020**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Alipokuwa akiukemea utamaduni na dhana za kikabila katika nyimbo zake, marehemu Bob Marley aliufananisha ubepari na "wanyama wala watu." Katika wimbo "Babylon System" (yaani mfumo wa kibepari), Marley alisema kuwa utamaduni huo ndio mzawa wa matatizo yote ya kiutawala ambayo yalikuwa yakiyakumba mataifa ya Weusi katika karne ya 20, wakati nchi zao zilikuwa zikitawaliwa na nchi za mataifa ya Ulaya.

Kwa mantiki hiyo, pengine Marley alikuwa na maono kuwa Afrika haingejikomboa kutoka kwa utumwa wa Kizungu, ikiwa ingeendelea kuziabudu na kuzishadidia tamaduni za Kimagharibi.

Utabiri huo nauoanisha na yanayoendelea nchini, ambapo serikali ya Jubilee imeonekana kushindwa kabisa kuikabili saratani ya ufisadi, ambayo inahatarisha kuliangamiza taifa hili lenye uchumi dhalili.

Donda hili linazidi kuyatandaza mabawa yake kutoka, tisho kuu likiwa ni uvamizi wa taasisi "takatifu" ambazo tunazitegemea kulikabili donda hilo.

Ni nani tutategemea kukabiliana na rushwa ikiwa taasisi kama Bunge, Tume ya Maadili na Kukabiliana na Ufisadi (**EACC**) kati ya zingine muhimu zimepakwa tope na saratani hiyo?

Kimsingi yote tunayopitia ni matunda ya uasi wa tamaduni za Kiafrika na uegemezi wa mifumo ya Kizungu kama mihimili ya jamii na nchi zetu.

Ndoto za watetezi wa Uafrika na nafasi ya Weusi kama marehemu Malcom X na Martin Luther King, zilikuwa ni kuona kuwa wameungana kabisa kukabiliana na matatizo yaliyowakabili bila kuzingatia mazingara waliyokuwemo.

Pindi tu baada ya mataifa mengi ya Kiafrika kujinyakulia uhuru wao katika miaka ya hamsini na sitini, viongozi wakuu walioziongoza nchi hizo kama Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta, Mwalimu Julius Kimbarage Nyerere kati ya wengine walianza harakati za kuliunganisha bara hili na kubuni Muungano wa Nchi za Kiafrika (**OAU**) japo ndoto hiyo haikufikia.

Kwa msingi huo, mhimili mkuu wa kiutawala ungekuwa ni mfumo wa kisosholisti, ambao ungekuwa nguzo kuu ya kuyaunganisha mataifa hayo.

Hata hivyo, migawanyiko mikubwa ilianza kushuhudiwa, huku baadhi ya mataifa yakianza kukabiliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutaasisika kwa maovu yote tunayoshuhudia sasa: ufisadi na tamaa ya kuogofya kutoka kwa viongozi wetu.

**Maswali**

a. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)
b. Onyesha mambo mawili makuu ambayo msanii aliyapinga. (alama 2)
c. Kwa nini ubepari umelinganishwa na "wanyama wala watu"? (alama 2)
d. Kwa mujibu wa taarifa eleza sifa za Bob Marley. (alama 2)
e. Swala linalozungumziwa limerejelewa kama "Donda".
   i) Eleza mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)
   ii) Ni kweli kuwa donda hili laelekea kuwa gumu? Thibitisha. (alama 2)
f. Tatizo hili la "donda" ni kama kujipalia makaa. Fafanua. (alama 2)
g. Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa taarifa. (alama 2)
   i) Mhimili…………………………………………………………………………
   ii) Taasisi…………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Nchi nyingi zimetia saini mkataba wa Umoja Wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kulindwa. Kwa kutia saini, nchi hizi zimetangaza kujitolea kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake wa kuwa watoto wote katika kinya zao wananufaika kutokana na haki hizi.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye viinilishe bora. Pili kila mtoto ana haki ya elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha kila mtoto ana haki ya kutopigwa, kutodunishwa kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kuzurutishwa. Hali kadhalika ana haki kuishi katika nyumba au makaazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe kufanya maamuzi. Fauka ya haya ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum, michezo, upendo na habari. Isitoshe anastahili kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwana jamii, hivyo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao

Walakini haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengine duniani bado wananyimwa haki zao. La kusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilinda haki hizi ndio wanaoongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje. Wengine hawapati chakula licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika nchi zenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wamegeuka mibaba ya kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanaotakiwa kuwa wamelindwa majumbani na shuleni na wazazi pamoja na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasionenda shule kwa sababu ya lindi la ufakara uliokithiri. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo wanang'ang'ania iwepo ni kama kwamba ni waota ndoto mchana. Jiulize, watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wako mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hivi ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kupitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati si kwa chati.

**Maswali**

a) Fupisha aya mbili za kwanza.( **maneno 65 – 70**) (alama 9, (1 utiririko)
   **Matayarisho**

**Jibu**

b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa. (**maneno 30 – 35**) (alama 4) (1, utiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Toa mfano wa sauti ambayo ni; (alama 2)
  i) Kikwamizo ambacho ni ghuna.
  ii) Kikwamizo ambacho sighuna.

b) Kwa kutoa mfano onyesha miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

c) Bainisha mzizi na viambishi tamati katika kitenzi kifuatacho. (alama 2)
Achezesha.

d) Tumia nomino zifuatazo katika sentensi ili zilete dhana zilizo kwenye mabano. (alama 2)
  i) Uchumi (Kielezi)
  ii) Mlevi (Kivumishi)

e) (i) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)
  (ii) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii. (alama 1)
  Mpira uliotoboka sana ulitengenezwa haraka.

f) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 2)
Mkihifadhi nafaka hizo vizuri maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha.

g) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 3)
basi mwanangu akasema daudi hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia vision 2030 wewe waonaoje

h) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati. (alama 1)
Beti alijishindia tuzo. Beti alishiriki katika utunzaji wa mazingira.

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 3)
Mvua ilinyesha tulipokuwa tukilima.

j) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa. (alama 2)
Malik alipuliza siwa akiwa kwa Shaka.

k) (i) Eleza maana ya sentensi ya masharti. (alama 1)
  (ii) Tunga sentensi moja ya masharti. (alama 2)

l) Tumia kiwakilishi cha **'a'** unganifu katika sentensi kuonyesha.
  (i) Umilikaji. (alama 2)
  (ii) Nafasi katika orodha au nafasi katika kundi. (alama 2)

m) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kistari kirefu. (alama 2)

n) Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja bila kurudia kitenzi. (alama 2)
Osoro amempigia Nyamoti simu. Nyamoti amempigia Osoro simu.

o) Andika maana tatu za neno: Kanda. (alama 3)

p) Andika visawe viwili vya nahau: enda kombo. (alama 2)

q) Andika sentensi hii katika hali ya ukubwa wingi. (alama 2)
Ng'ombe mnono atachinjiwa wachezaji.

r) Taja uamilifu wa neno lililopigiwa mstari. (alama 1)
<u>Hapa</u> ni pangu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

## 4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

**Mtu I**: Wewe njoo hapa! (Kwa sauti kubwa.) Fanya upesi!
**Mtu II**: (Anakimbia mbio.) Naja Sir.
**Mtu I**: (Anamtazama.) Unajifanya mwerevu?
**Mtu II**: Hapana Sir …eh … afande.
**Mtu I**: Jina?
**Mtu II**: Samwel Kibao
**Mtu I**: (Huku anaandika.) Lete kitambulisho.
**Mtu II**: Sina hapa Sir.
**Mtu I**: Huna kitambulisho? Utafanyiwa booking vipi?
**Mtu II:** Naomba …
**Mtu I**: Naomba! Naomba! Unaomba nini? Wazururaji kama nyinyi tunawajua. Mnajidai hamjui kuna curfew. Mnajiponza wenyewe na kuwahasiri wenzenu. Kisha , "Serikali saidia". Usiniharibie muda wangu. (Akiashiria.) Ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu leo. Tutakukirimu chakula na chumba.

(Anamsukuma ndani.)

**Maswali**

a) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 2)
b) Eleza sifa nane za sajili hii kwa kurejelea makala haya. (alama 8)

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA DAYOSISI YA KISII**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**LAZIMA**
**Soma mashairi haya kisha ujibu maswali**

**SHAIRI: A**
**MWANAMKE**

1. Namwona yu nyumbani,
Na jembe mikononi,
Analima,
Mavuno siyake,
Ni ya mume wake,

2. Namwona viwandani,
Pia maofisini,
Yu kazini,
Hamkani,
Anabaguliwa.

3. Namwona yu nyumbani.
Mpishi wa jikoni,
Yaya yeye,
Dobi yeye,
Hakuna malipo,
Likizo haipo,

4. Namwona kitandani,
Yu uchi maungoni,
Ni mrembo,
Kama chombo,
Chenye ushawishi,
Mzima utashi,

5. Namwona mkekani,
Yuwamo uzazini,
Apumua,
Augua,
Kilio cha kite,
Chapa mpiga pute.

6. Kwa nini mwanamke,
Ni yeye peke yake,
Anyimwaye,
Heshimaye,
Haki anakosa,
Kwa kweli ni kosa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SHAIRI B**
**WANAWAKE**

1. Wanawake ni wavyazi,
Na wao ndio walezi,
Kwetu sisi wapumbavu,
Kutupumbaza pumbaa

2. Ndio wao waadhamu,
Watutowao hamumu,
Tunaposhindwa na ghamu,
Ya mambo yakituvaa

3. Hakika ukiwatunda,
Huna budi kuwapenda,
Nawaendapo kuwadanda
Lazima utawavaa.

4. Kwa hakika mwanamke,
Ni kiumbe kilo pweke,
Na waume mupulike,
Wana mengi manufaa.

5. Kwa ufupi nakueleza,
Haya basi nisikiza,
La kwanza hututuliza,
Wapo nyumbani mwakaa
.

6. Chakula ukikileta
Mcheleo au nyata
Hupika pasi matata
Vikaiva kwa hawaa.

7. Au tuseme muhogo
Na vijisamaki ngogo
Uutuwapo mzigo
Kama huo kwa jamaa.

8. Huyo hufanya haraka,
Ikawa tahangaika
Kushughulikia kupika
Chakula kukiandaa.

9. Atafazaika sana,
Kukupikia kimwana,
Kwa sababu yako bwana,
Kwa kujuwa yako njaa.

10. Unapotoka kazini,
Au mwanawe shuleni,
Ajuwa wa taabani,
Kwa tumbo kukamaa.

11. Pili ndiye mkombozi,
Wa kuteta uzazi,
Wa kuongezea mizizi,
Udugu na ujamaa

12. Pindi unapouguwa,
Kwakowe hujisumbuwa,
Kukutafutia dawa,
Hana dakika kukaa.

13. Huitunza nyumba yako,
Hunadhifu nguo zako,
Na zaidi vilo vyako,
Ambavo vya manufaa

14. Yataka tuwaheshimu,
Mno sana tufahamu,
Yafaa tuwakarimu,
Kamba nipa wee twaa.

15. Kaditama wasalamu,
Zatosha niloazimu,
Kuwaletea muhimu,
Hapa basi ninakaa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(i) Yalinganue na kulinganisha mashairi A na B kimuundo (alama 4)
(ii) Kwa kurejelea kigezo cha mishororo eleza bahari za mashairi A na B (alama 2)
(iii) Eleza madhumuni ya mtunzi wa shairi A (alama 2)
(iv) Tofautisha toni katika mashairi haya mawili (alama 2)
(v) Suala la ubabedume limeangaziwa kwa kina katika shairi A. Fafanua. (alama 4)
(vi) Mwanamke wa shairi A anahitilafiana na wa shairi B. Jadili. (alama 2)
(vii) Shairi B ni wosia kwa wanajamii. Thibitisha dhana hii (alama 2)
(viii) Eleza maana ya kifungu 'vikaiva kwa hawaa' katika ubeti wa sita wa shairi B (alama 2)

**SEHEMU YA B:**

**TAMTHILIA; KIGOGO Pauline Kea**

2. "Ulitaka wahamie wapi siku kama hizi? Wamekuja kuuguza majeraha yao ya kufungiwa soko."
   a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Tambua mbinu mbili za lugha kwenye dondoo. (alama 2)
   c) Wanasagamoyo mbali na kufungiwa soko, wanayauguza majeraha yapi mengine. (alama 14)
3. 'Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba…… kuturejesha… hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena."
   a) Fafanua dondoo hili (alama 4)
   b) Kwa kurejelea mzungumzaji wa dondoo hili, fafanua unafiki unaojitokeza kwenye tamthilia. (alama 16)

**SEHEMU YA C:**

**RIWAYA : CHOZI LA HERI Assumpta K. Matei.**

*Jibu swali la 4 au 5*

4. "Na unadhani unakwenda wapi? Utaweza kujitunza … bibi yako ndiye huyo, hana hanani…''
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Fafanua masaibu yaliyomkumba mnenewa (alama 5)
c) Ulezi wa mwana ni jambo la shirika Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya chozi la heri. (alama 11)

5.
a) Kwa hoja kumi jadili jinsi mwandishi wa riwaya ya chozi la Heri alivyotumia mbinu ya majazi kufanikisha kazi yake. (alama 10)
b) Riwaya ya chozi la Heri imeyasawiri masaibu mengi yanayowakumba wafanyikazi. Thibitisha kwa kutoa hoja kumi ukirejelea riwaya yenyewe. (alama 10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA D:**

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE. Alifa Chokocho na Dumu kayanda

*Jibu swali la 6 au 7*

**Mtihani wa maisha**

6 "... ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)
c) Onyesha mawazo yanayomwadhibu anayerejelewa na dondoo hili. (alama 10)

**Tulipokutana tena**

7 " Mamangu siku iile aliniamsha mapema…"
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   ii) Tathmini umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuendeleleza dhamira ya hadithi hii. (alama 8)
   iii) Fafanua masaibu aliyopitia msemaji wa dondoo hili. (alama 8)

**SEHEMU YA E:**
**FASIHI SIMULIZI**

8. a) Ni matatizo gani yanayoweza kumkumba mtafiti wa data nyanjani? (alama 5)
   b) Eleza hatua anazoweza kuzichukua mtafiti wa kazi ya fasihi simulizi ili kujirahisishia kazi ya utafiti nyanjani (alama 5)
   c) fasihi simulizi ilihifadhiwaje zamani. (alama 1)
   d) Toa udhaifu wa jibu lako hapo juu (alama 1)
   e) eleza sababu za kufifia kwa fasihi simulizi katika jamii ya kisasa. ( alama 2)
   f) i.) miviga ni nini? (alama 1)
      ii.) miviga inafaa kupigwa marufuku katika jamii ya kisasa. Jadili (alama 3)
   g) Taja mifano ya ngomezi za kisasa ( alama2)

## DAYOSISI YA KISII

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**
**KARATASI YA KWANZA 2020 102/1 - INSHUmbo la ripoti lizingatiwe/sura**
**Sehemu zifuatazo zimulikwe.**

Anwani: Ripoti kuhusu matokeo mabaya ya Kiswahili katika kaunti …….

(a) Utangulizi: Lengo, aliyeitisha, kamati iliyoteuliwa na muda wa kuwasilisha ripoti.
Matokeo: aeleze vile matokeo haya yamekuwa yakishuka.

**(a) Hoja mbalimbali kuhusu:**
**Kiini cha matokeo hayo**

- Ukosefu wa walimu wa kutosha kumudu madarasa yote katika kila shule.
- Uhaba wa walimu wenye ujuzi.
- Fikra potovu kuhusiana na somo lenyewe/lugha ambayo ni ya hadhi ya chini.
- Watahiniwa kutofanya mazoezi ya kila mara.
- Ukosefu wa vitabu vya mazoezi na mitihani ya kudurusu.
- Baadhi ya walimu kuwa na madoido wanapofundisha badala ya kulenga mada.
- Watahiniwa kuathiriwa na lugha ya mama na sheng'.
- Vipindi vya Kiswahili ni vichache.

(b) **Suluhu/mapendekezo**.

- Walimu wenye ujuzi waajiriwe.
- Wakuu wa elimu waenda kwa warsha.
- Vitabu vinunuliwe na serikali.
- Kiswahili kipewe hadhi yake katika jamii.
- Walimu wajiandae kabla ya somo inavyostahili.
- Watahini kuwajuza watahiniwa sheria zinazozingatiwa kwa utahini ili kuwamakinisha.
- Vipindi vya Kiswahili shuleni viongezwe.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**(c) Sahihi na tarehe.**
**Jina na cheo**
Asipozingatia sura ya ripoti aondolewe 4 (s) sura.

2. **Umaskini ni changamoto kubwa katika maendeleo ya magatuzi**.
**Mtahiniwa aonyeshe: Vidokezi**.

- Hakuna rasilmali ya kutosha.
- Uhaba wa mvua sehemu kame.
- Ukosefu wa maji ya kutosha.
- Nafasi za kazi ni nadra.
- Miundo msingi bovu.
- Ukosefu wa wataalamu wa kutosha.
- Elimu duni.

**Kutuza**

Insha kamili iwe na hoja zisizopungua tano na zifafanuliwe vizuri.

3. **Aandike kisa kimoja kitakachodhihirisha ukweli wa methali hii:**
   ***Mchumia juani hulia kivulini.***

Mtahiniwa si lazima aeleze maana ya methali lakini akifanya hivyo bila kupotoka asiadhibiwe.
Maana : Mtu anayefanya kazi ngumu (juani) huishia kufurahia matunda ya kazi yake kwa raha (kivulini).

- ✓ Mtahini atunge kisa/visa vinavyoana na maana pamoja na matumizi ya methali husika.
- ✓ Ashughulikie pande zote mbili.
- ✓ Akishughulikia upande mmoja asipite C+ (10)
- ✓ Akipotoka atuzwe D wastani. (03)

(4) **Insha ya mdokezo**.

- ✓ Insha/mtungo ni lazima uanze kwa maneno aliyopewa mtahiniwa.
- ✓ Kisa chake kionyeshe namna mlango ulibishwa na kiwe ni kisa cha kutisha.
- ✓ Asiyeanzia kwa maneno aliyopewa atakuwa amepotoka.

**UTANGULIZI:**

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na mtahiniwa, asilia, ubanifu mwingi na hati nadhifu. Kwa kutegema maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutulia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hijai, hoja, msamiati na mtindo ili aweza kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyopendekezwa. Viwango vyenyewe ni A, B, C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**VIWANGO MBALIMBALI**

**KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01 – 05**

1. Insha haileweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile mtahiniwa anachojaribu kuwasilisha.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji haufai na insha ina makosa ya kila aina.
4. Kujitungia swali na kulijibu.
5. Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**

**D- (D YA CHINI) MAKI 01 -02**

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
4. Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
5. Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
6. Kunakili swali au kichwa tu

**D WASTANI MAKI 03**

1. Mtiririko wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
3. Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+ (D YA JUU) MAKI 4 – 5**

1. Insha ya aina hii huwa na makosa mengi ya kila aina. Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kikamilifu/mada haikukuzwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.

**KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06 – 10**

1. Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia mada japo hakuikuza na kuindeleza vilivyo.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia/hana ubunifu wa kutosha.
3. Mtahiniwa anaafikisha sentensi vibaya.

4. Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
5. Insha ina makosa mengi ya sarufi, ya msamiati na ya tahajia (hijai)
6. Insha yenye urefu wa nusu ikadiriwe hapa.
7. **NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C**

**C- (C YA CHINI) MAKI 06 – 07**

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.

**C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa uhafifu.
2. Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Ana shida ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi, ya msamiati na ya hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.

**KIWANGO CHA B JUMLA MAKI 11 – 15.**

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
2. Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
4. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.
5. Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA B**

**B- (B YA CHINI) MAKI 11 – 12**

1. Mtahiniwa awawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofauti tofauti akizingatia mada.
2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
4. Makosa yanadhihirika/kiasi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**B WASTANI MAKI 13.**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.
3. Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Makosa ni machache/kuna makosa machache.

**B+ (B YA JUU) MAKI 14 – 15.**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika waziwazi.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Sarufi yake ni nzuri.
4. Uakifishaji wa sentensi zake ni mzuri.
5. Makosa ni machache ya hapa na pale.

**KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKI 16 – 20**

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
2. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
3. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu kimawazo.
5. Insha ina urefu kamili.

**NGAZI MBALIMBALI KIWANGO CHA A**

**A- (A YA CHINI) 16 – 17**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anaishughulikia mada.
3. Ana mtiririko mzuri wa mawazo.
4. Msamiati wake ni mzuri na unaovutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Anatumia miundo tofautitofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa ni machache yasiyokusudiwa.

**A WASTANI MAKI 18**
1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kulingana na mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (A YA JUU) MAKI 19 – 20.**
1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughulikiwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu unaovutia zaidi.
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi.
6. Anatumia miundo tofautitofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

**VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI**

| KIWANGO | NGAZI | MAKI |
|---|---|---|
| A | A+<br>A<br>A- | 19 – 20<br>18<br>16 – 17 |
| B | B+<br>B<br>B- | 14 – 15<br>13<br>11 – 12 |
| C | C+<br>C<br>C- | 09 – 10<br>08<br>06 – 07 |
| D | D+<br>D<br>D- | 04 – 05<br>03<br>01 – 02 |

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**USAHIHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA**

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati mtindo, sarufi na hijai.

**MAUDHUI**
- Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
- Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
- Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

**MSAMIATI**
- Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika. Mtahiniwa anatarajia kutumia msamiati unaooana na mada teule. Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

**MTINDO**
- ✓ Mtindo unahusu mambo yafuatayo:
- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano, methali, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya isha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

**SARUFI**

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha.

**Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:**

- Matumizi ya alama za uakifishaji.
- Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa.
- Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
- Mpangilio wa maneno katika sentensi.
- Mnyambuliko wa kitenzi katika sentensi.
- Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
- Matumizi ya herufi kubwa.

**a) Mwanzo wa sentensi.**
**b) Majina ya pekee**

- Majina ya mahali, miji, nchi, mataifa na kadhalika.
- Siku za juma, miezi n.k
- Mashirika masomo, vitabu n.k
- Makabila, lugha n.k
- Jina la Mungu
- Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa – Foksi, Jak. Popi, Simba, Tomin na mengineyo.
- Majina halisi ya watu k.m Maria, Rutto.

**MAKOSA YA HIJAI/TAHAJIA**

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa ya kwanza tu.

Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

- Kutenganisha neno kwa mfano 'aliye kuwa'
- Kuunganisha maneno kwa mfano ' kwa sababu.
- Kukata silabi visivyo ajikapo pambizoni kama vile, 'n o'
- Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano 'ongesa' badala ya 'ongeza'.
- Kuacha herufi katika neno kwa mfano 'aliekuja' badala ya 'aliyekuja'.
- Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile 'piya' balada ya 'pia'
- Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j i.
- Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
- Kuacha tirifaa au kuindika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom'be, ngo'mbe n.k
- Kuandika tarakimu kwa mfano 27 – 08 – 2013.

Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.

Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokea kwa mara ya kwanza tu.

√ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilika pambizoni kushoto.

ʌ Hutumiwa kuonyesha kuacha kwa neno/maneno.

√ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii huitwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii huitwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya chini katikati kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

**UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA**

| | |
|---|---|
| Maneno 9 katika kila msitari | ukurasa mmoja na nusu |
| Maneno 8 katika kila msitari | ukurasa mmoja na robo tatu |
| maneno 7 katika kila msitari | kurasa mbili |
| maneno 6 katika kila msitari | kurasa mbili na robo |
| maneno 5 katika kila msitari | kurasa mbili na robo tatu |
| maneno 4 katika kila msitari | kurasa tatu na robo |
| maneno 3 katika kila msitari | kurasa nne na nusu |

| | | |
|---|---|---|
| kufikia maneno | 174 | Insha robo |
| maneno | 175 – 274 | Insha nusu |
| maneno | 275 – 374 | Insha robo tatu |
| maneno | 375 na kuen | |

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA DAYOSISI JIMBO LA KISII ,Dec. 2020**
**KARATASI YA PILI (2)**
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**1. UFAHAMU.**

a) Ufisadi **1x1 = 1**
b) i) Utamaduni
   ii) Dhana za kikabila. **2x1=2**
**c)** Ndiyo mzawa wa matatizo yote ya kiutawala**. 1x2=2**
d) i) Mwenye maono
   ii) Mtetezi **2x1=2**
e) i) Jazanda – ufisadi kurejelewa kuwa donda. **1x2=2**
   ii) Donda linatandaza mbawa zake kwenye 'taasisi takatifu' zinazopaswa kuupinga ufisadi. **1x2=2**
f) Uasi wa tamaduni za kiafrika.
   Kuegemea mifumo ya kizungu. **2x1=2**
g) i) Mhimili – nguzo/tegemeo/iliyo imara. **al.1**
   ii) Taasisi – kituo maalum cha kustawisha/ kutoa mafunzo. **al. 1**
   Adhibu sarufi popote patokeapo makosa na usiadhibu zaidi ya nusu alama aliyopata mwanafunzi.
   Hijai – hadi makosa sita.

**2. UFUPISHO**

a). i) Nchi nyingi duniani zinatia saini mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto.
   ii) Hii inahakikisha hakuna ukiukaji wake katika himaya zao.
   iii) Kila mtoto ana haki ya kuishi.
   iv) Kupata chakula cha kutosha na chenye lishe bora.
   v) Ana haki ya kupata elimu bila ada inayofaa, inayopatikana kwa urahisi.
   vi) Ana haki za kutopigwa/kutodunishwa kwa namna yoyote.
   vii) Kutolazimishwa kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa.
   viii) Kuishi katika nyumba/makaazi bora na salama.
   ix) Kutatizwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote ambayo inaweza kumhatarisha.
   x) Ashirikishwe katika kutoa maamuzi.
   xi) Kupata huduma za afya, mahitaji maalum, michezo, upendo na habari.
   xii) Anastahili kuheshimiwa na kila mwanajamii.
   xiii) Haki hizi zinatakiwa kuheshimiwa na kila mwanajamii.
   xiv) Serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi. ***Zozote 9x1=9***

**b).** i) Kuhimiza serikali kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni.
   ii) Tushirikiane kutoa huduma na kukomesha dhuluma.
   iii) Kupeleka miswada bungeni na kupitisha kuwa sheria.
   iv) Kubadilisha msimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda ipasavyo. ***(4x1=4)***

**a = 9**
**b=4**

mtiririko – 2

M — **a = 9**
**b=4**
**ut=2**
**15**

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) (i) v,dh,z,gh,h **1x1=1**
   (ii) f, th, s, sh **1x1=1**

b) (i) Silabi za irabu moja – oa, au, ua.
   (ii) Konsonanti za irabu – ki, ka, - ku – ta
   (iii) Konsonanti moja – M+tu, n+chi
   (iv) Konsonanti tatu na irabu – le + ngwa
   (Muundo ½ mfano ½ ) **x2 =2**


c) A - Kiambishi nafsi tatu umoja /Ngeli A – WA

Chez-mzizi **al.1**
esh – Mnyambuliko - viambishi **al.** ½
a-kiishio - tamati **al.** ½

d) (i) Nchi yetu itapiga hatua kubwa kiuchumi. **al.1**
(ii) Kiongozi mlevi husahau ahadi zake. **al.1**

**e)** (i) Kifungu cha maneno chenye muundo wa kiima na kiarifu. **(al.1)**
– Kundi nomino + kundi tenzi
– Tungo yenye kiima na kiarifu ambayo imo katika tungo kuu. **(1x1=1)**
(ii) Mpira uliotoboka jana – kishazi tegemezi. ½
Ulitengenezwa haraka – kishazi huru. ½

f) Ukihifadhi nafaka hiyo vizuri eneo hili litakuwa na chakula cha kutosha. **1x2=2**
g) "Basi mwanangu, "akasema Daudi. "hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia 'vision 2030'. Wewe waonaje?"
**6 x ½ = 3**
h) Beti alijishindia tuzo baada ya kushiriki katika utunzaji wa mazingira.
Majibu zaidi; kabla ya, kisha, halafu. **1x1=1**

i)



***6 x ½ = 3***

j) Siwa lilipuliziwa kwa shaka na Malik. **1x2=2**
k) (i) Ni sentensi inayoonyesha kutegemeana kwa matendo au hali.
(ii) Mvua ikinyesha mapema tutapata faida.
(Mwanafunzi atumie viambishi na maneno yanayoonyesha kuwa kufanikiwa au kutofanikiwa kwa tukio au tendo moja kunategemea kufanikiwa kwa tukio lingine)
**Mfano**: nge, ngali, ki, kama, iwapo.
✓ Wanafunzi wangefika mapema wangempata mwalimu.
✓ Kotu angalisoma kwa bidii angalifaulu.
✓ Iwapo unataka ufanisi lazima ujibidiishe.

l) (i) La kutanda linapendeza.
Tindi anataka cha mwenziwe. **1x2=2**
Au
(ii) Wa tatu atatuzwa shaba.
Mwalimu anamuita wa nne. **1x2=2**
(Atumie viwakilishi vya idadi halisi vinavyotumia '**a**' unganifu).
m) Kistari kirefu hutumiwa kutoa maelezo zaidi kufafanua au kuonyesha kusisitiza.
**Mfano**: Alinunua matunda ______ maembe, machungwa na matango.
✓ Hutumiwa kuonyesha kubadilika kwa maoni.
**Mfano**: Waite wale _____ hapana hawa.
✓ Hutumiwa kuonyesha msemaji katika usemi halisi.
**Mfano**: Utenga ni udhaifu ____ Duma.
n) Osoro na Nyamoti wamepigiana simu
(sentensi ionyeshe kauli/hali ya kutendeana) **1x2=2**
o) Eneo

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Kutomasa.
Aina ya mfuko.
Malipo ya mganga.
Makasia ya kuogelea.
Utepe au mshipi unaotumiwa kunasia sauti au picha. **3x1=3**

p) Enda mvange
Enda upago
Enda segemnege.
Enda arijojo
Enda shoro
Enda mrama
Enda tenge
Enda benibeni **2X1=2**

**q)** Magombe/majigombe manono yatachinjiwa wachezaji. **1x2=2**

r) W – kiwakilishi. **1x1=1**

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Sajili ni ya kituo cha polisi. Polisi, askari au mtu I anayerejelewa pia kama 'Afande' anamhoji mshukiwa au mtuhumiwa (Mtu II). **1x2=2**

b)
i) Msamiati maalum wa askari /polisi unaofungamana na sheria.
ii) Lugha yenye toni kali ya kutisha upande wa askari kwa mshukiwa ili kumfanya ashirikiane na polisi kusema ukweli.
iii) Lugha ya kudadisi au ya kuhoji ili habari kamili kupatikana.
iv) Lugha hii inazingatia urasmi kwa sababu uhusiano kati ya polisi na mshukiwa ni rasmi au wa kikazi.
v) Lugha ya unyenyekevu/heshima na upole hasa upande wa mshukiwa ili kudumisha uhusiano wa heshima uliopo baina ya polisi na mshukiwa.
vi) (vi)Kauli fupifupi kutumiwa kwa kuwa mahojiano huendeshwa kwa maswali ya kudadisi.
vii) Kuchanganya ndimi au kubadili msimbo kwa kuwa maneno mengine hueleweka vyema yanapoendelezwa kwa kimombo.

**Mfano**: curfew, sir.

viii) Huwa na lugha ya kuamrisha. Kuonyesha mamlaka na nguvu alizonazo polisi na kumfanya mshukiwa kutii.
ix) Kuna kukatwa kauli kwa mshukiwa.
x) Kuna kusitasita kwa mshukiwa anapozungumza na polisi kudhihirisha woga.
xi) Kuna lugha ya kejeli/dhihaka kuonyesha kuwa polisi anafahamu ujanja wa mshukiwa.
xii) Kuna uradidi ili kusisitiza ujumbe .
Naomba! Naomba.
xiii) Lugha inayovuta huruma.

**<u>Tanbihi</u>**

✓ Mtahini asieleze sifa zaidi ya nane.
✓ Asizungumzie nje ya makala.
✓ Kila hoja lazima itolewe maelezo na kutetewa kwa mifano.

Za kwanza **8x1=8**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**KISII DIOCESE SCHOOLS JOINT EVALUATION TEST 2020**
**KARATASI YA 3.**
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**SEHEMU YA A: USHAIRI**
**ULINGANUZI/ TOFAUTI**
**I) SHAIRI LA A**
**SHAIRI LA B.**

| SHAIRI LA A | SHAIRI LA B |
|---|---|
| – Lina beti sita | - lina beti kumi na tano |
| – lina mistari / mishororo sita kwa kila ubeti | -Lina mishororo minne katika kila ubeti |
| – Lina mpangilio wa silabi zinazohitilatiana katika mistari | -Lina mizani toshelezi katika mishororo mizani minne katika kila mshororo. |

***( Zozote 2 X 1 = 2)***

b) ULINGANISHAJI / USAWA
- Yote yana beti toshelezi
- Yote yana mseto wa mistari/mishororo mishata
- Na kituo
- Yote yana mpangilio wa beti
- Vina vinabadilika kila ubeti

***(Zozote 2 X1 = 2)***

II) Usita/Tasdisa – Mishororo 6
Tarbia/unne - Mishororo 4

***(2 x 1 =2)***

III) Kuangazia masaibu ya mwanamke – anavyodhulumiwa licha ya kuwa na manufaa au umuhimu sana maishan.

***(Hoja 1 x 2 = 2)***

IV) Shairi **A**: Toni ya huruma na masikitiko kwa sababu ya madhila anayetendewa mwanamke .
**B**: Toni ya ufahari kwa wema anaotenda mwanamke anatukuzwa kwa aadili yake.

***(zozote 2 x 1 =2 ) Shairi la A na B)***

V)
- Mwanamke anadhulumiwa na mwanamume
- Mwanamke huzalisha kiuchumi lakini hafaidi
- Huteswa kazini
- Anahudumishwa nyumbani kamapunda wad obi huku mume akistarehe.

***(Hoja Zozote 4 x1 = 4)***

VI) Mwanamke wa shairi A ni kiumbe mnyonge anayekandamizwa na mwanamume; Mwanamke wa shairi B amesawiriwa kuwa shujaa aliye huru na anaytegemewa na wanajamii.

***(Hoja 1 x 2 = 2)***

VII) Mtunzi anawashauri wanajamii wajiepushe na maovu mfano wizi ulevi.
VIII) Upesi au haraka / wepesi wa mapishi ***(Hoja 1x 2 = 2)***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TAMTHILIA**

2. a) “ **Ulitaka wahamie wapi siku kama hizi?
Wamekuja kuuguza majeraha yao ya kufungiwa soko.”**
- Msemaji ni ngurumo
- Anaambia Sudi
- Mangweni kwa Asiya
- Kuhusu vijana wengi waliokuwa wanashiriki ulevi mle.

***(4 x 1 = 4 )***

b) Swali balagha – ulitaka wahamie wapi?
Jazanda/stiara- Jeraha: huzuni /masikitiko ***( 2 x 1 = 2)***

***c)***
- Wapinzani kuuliwa, mfano jabali
- Wapinzani kujeruhiwa mfano Tunu
- Waandamanaji kupigwa na askari katika soko la chapakazi

- Kufungwa bila makosa, mfano Ashua kufungwa na utawala wa Majoka
- Walowezi kutishiwa kufurushwa – siti na Kombe wanarushiwa vijikaratasi ili wahame Sagamoyo
- Kukauka kwa mito na maziwa sababu ya ukataj misitu
- Njaa-pendo na pili, Hashima anasema mavuno ni haba
- Vijana waliosoma wamekosa kazi mfano Ashua
- Mazingira chafu pesa za kusafisha soko zimefisidiwa na soko kunuka
- Kuongezeka kwa bei ya bidhaa katika kiosk cha kampuni
- Walimu na madaktari kuongezewa mshahara ili hali utawala unaongeza kodi
- Wananchi kupewa makombo ilihali watawala wanakula keki kubwa.
- Mashamba ya umma yananyakuliwa na utawala ili kuendeleza biashara za kibinafsi
- Wafanyakazi kutolipiwa bima
- Kufungwa kwa vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

*(14 x 1= 14)*

3. **"Tusiwaruhu watu wachache waliojazwa kasumba………kuturejesha……hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena.**

**a)**

- Haya ni maneno ya Majoka / Sauti ya Majoka iliyorekodiwa katika redio.
- Anawahutubia wanaSagamoyo
- Anayasema maneno haya akiwa ikuluni
- Sauti hii imechezwa ili kuwafahamisha raia kuhusu kusherehekea miaka sitini ya uhuru.

**b)** ***<u>Unafiki katika kauli hii</u>***

**"Majoka anasema kuwa hawatakubali kutawaliwa kidhalimu kumbe ndiye anayetawala kidhalimu.**

- Kufunga soko –Anafunga soko la chapakazi hivyo kuwahini wafanyakazi k.m Ashua riziki yake
- Wahuni-Majoka ana kundi la wahuni liitwalo chatu analotumia kuwaua raia, kwa mfano mkuu wa polisi anapokataa kupiga raia risasi anatishia kumuvunjavunja.
- Mapenzi - anamtaka Ashua kimapenzi ndipo amsaidie lakini ameoa.
- Kukata miti -anafungulia biashara ya ukataji miti hivyo kutishia ukame Sagamoyo
- Kuwaua raia –Jabali anauwaa katika ajali iliyopangwa.
- Kuwafukuza walowezi –utawala wake unaeneza vijikaratasi vinavyowataka baadhi ya raia siti na kombe kahama Sagamoyo.
- Kupandisha bei ya vyakula-Anapandisha bei ya chakula katika kiosk mara dufu baada ya kufunga soko.
- Anawatusi raia –anawatusi raia wanaposusia mkutano wake na kuandamana ili kumshurutisha kufungua soko la chapakazi- Anawaita wajinga
- Kuharibu mustakabali wa wanafunzi-Anafungua shule ambayo inaharibu mustakabali wa wanafunzi sababu wanadungana sumu yanyoka shuleni(Makabeji
- Fidia –Babake Tunu alifia kwa kampuni yake lakini hakutaka kuwalipia fidia sababu hakuwa na bima –Bidii ya Hashima iliwaokoa.
- Kuumizwa Kwa Tunu – anawatumia wahuni kumvamia na kumuumiza Tunu. Anaumia Mwndi
- Kupandisha kodi-anawaongezea walimu na madaktari asilimia ndogo ya mshahara na kupandisha kodi wakati huo huo
- Kufunga Ashua-anamfunga aAshua licha ya Ashua kumwarifu kwamba ana mtoto anayenyonya
- Kufunga vyombo vya habari –Anafunga vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.
- Majoka anafaa kulinda rasilmali za umma lakini ananyakua ardhi soko la chapakazi na kujenga nchi za nje katika miradi ovyo mfano uchongaji wa vinyago
- Mauaji ya vijana –vijana waliogoma kulalamikia kufungwa kwa soko waliuawa na polisi.( 16 x 1 = 16)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA C. RIWAYA: CHOZI LA HERI**

4. **"Na unadhani unakwenda wapi?Utaweza kujitunza ………..bibi yako ndiye huyo,hana hanani."**

**a) Eleza muktadha**

i) Ni maneno ya Fungo yanayompitikia pete akilini /ni mawazo ya Pete
ii) Pete yuko katika hospitali ya Mwanzo Mpya
iii) Anapiga darubini kilichomleta hospitalini
iv) Pete alikuwa amejaribu kujiua kwa kunywasumu ili kujiua pamoja na kijusi chake.

***Zozote 4 x 1= 4***

**b) Fafanua masaibu yaliyomkumba mnenewa.**

- Alitelekezwa na wazazi wake na kulelelwa na nyanyake
- Pete alikosa kununuliwa sare mpya sababu mwili umeanza kuwanda
- Kukosa sodo wakati wa hedhi yake
- Kila mwezi nyanya akampa tambara la blanketi
- Pete alipashwa tohara akiwa shule ya msingi
- Anaozwa mapema kwa bwana Fungo akiwa mdogo
- Fungo alimtaliki akiwa na mtoto
- Pete alipata kazi ya kijungujjiko kule kwa mhindi
- Pete aliamka kabla ya jimbi la kwanza na kuondoka saa kumii na mbili jioni.
- Nyangumi anamdanganya na kumpa mtoto mwingine kusha akamuacha.
- Mmoja wa walevi tena anamringa kisha akajaribu kunywa sumu ili ajiue pamoja na kijusi chake.

***(Zozote 5 x 1 = 5)***

**c) Ulezi wa mwana ni jambo la shirika**

- Ridhaa alilelewa na babake mzee Msubili na mamake akapelekwa shule hadi akahitimu kuwa daktari
- Wanafunzi wenzake Rodha walipomwita mwizi mamake alimpeleke shule ambapo mwalimu aliwazumgumzia wenzake ana akasoma na kuhitimu
- Ridhaa alishirikiana na kedi kusomesha wapwaze wawili
- Ridhaa na Terry walishirikiana kuwalea wanao Anne, Dede na Mwangeka
- Lunga kiriri na Naomi walishirikiana kuwalea Dick, Umu na mwaliko hadi pale Naomi alipoenda mjini kutafuta maisha
- Sauna alimsaidia Lunga kuwalea akina Umu wakati Naomi aliwatoroka
- Mwangeka pamoja na Apondi wanampanga Umu kama mtoto wao na kumpa melezi mema.
- Apondi na Mwangeka wanawalea wanao Sofia na Ridhaa kwa mapenzi licha ya kuwa Sofia ni mwanawa Mandu.
- Mwangemi na Neema walimpanga mwaliko na kumpa malezi mema . Mwaliko anasomea isimu ya lugha
- Riziki Immaculata alitupwa kwenye jaa lakini Neema anamrokota na kumpeleka kwa kituo cha polisi ambapo anapelekwa kwa nyumba ya watoto
- Mamake Sauna na babake wa kombo walimlea lakini baba wa karibu alimbaka na kumringa jambo ambalo lilimfanya kutoroka.
- -Chandachema alilelewa na Bi kimai na Bwana Tenge wakati alikuwa mdogo. Chandachema babake ni Fumba na Rehema.
- Wazazi wa chandachema Fumba na Rehema baada ya kumzaa walimtelekezea nyanya yake. Nyanya mtu alimlea.
- Tindi na lemi walilelewa na mama yao hadi pale lemi anachomwa
- Dickson baada ya kukutana na Umu pale uwanjani wa ndege alipangiwa na Mwengeka na Rachel Apondi.
- Mwangeka na Mwangemi walipomuiga babu mwimo msubili, jioni hiyo walichapwa kwa makosa yao.

***(Zozote 11 x 1 = 11)***

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

***5. a) MAJAZI***

Ni mbinu ya kuvipa vitu, mahali, miji au wahusika majina kulingana na hulka zao.

- **HAZINA**-Umu aliwahi msaidia Hazina shilingi mia mbili akiwa mtoto wa kurandaranda mtaani baadaye Hazina anamfaa kwa kumwelekeza kwa nyuma ya watoto.
- DHAHABU-Ni mwilimu wa Umu na wanafunzi wengine. Ni dhahabu kwa wanafunzi hao sababu anawaelekeza vyema
- MSITU WA MAMBA-Msitu ambao wengi walikufa sababu ya njaa na magonjwa,walikosa chakula.
- MWALIKO-Alimwalika mwangemi kwenye dhofa ya kuzaliwa ikawa sadfa akaalikwa kwa dhifa ya umukusaliwa familia ilikutana.
- HOTELI YA MAJALIWA-katika hotel hii watoto wa lunga na Naomi wanakutana wote katika dhifa ya kusaliwa. Ilikuwa majaliwa Kwa watoto hewa kukutana nakupanga njia za kumtafuta mama yao.
- RIDHAA- Anaridhia hali zake zote
- Hali nzuri akiwa, anawalipia wapwaze masomo
- Aliasisha hospitali ya mwanzo mpya.
- UMU/KHERI-Ni majazi ,ana kheri njema kwa Dickson na na mwaliko, anawalea baba yao alipokufa.
- NEEMA.Neema zake zilimpeleka kumwokota riziki na kumlea mwaliko.

***zozote 5 x2=10***

***kutaja muhusika al.1***
***maelezo al.1***

b) **MASAIBU YANAYOWAKUMBA WAFANYIKAZI**

- Wafanyikazi wa kiafrika katika mashamba ya wazungu walipewa ujira mdogo
- Wafanyi kazi wa kiafrika walisukumwa kwenda sehemu hazina uwezo wa kuzalisha mimea.
- Lunga kiriri alifutwa kazi kwa kutetea wananchi wasilishwe chakula kibovu.
- Wafanyikazi wa majani chai wa shirika la chai la Tengenea walipewa vyiumba vidogo ambavyo vilikosa heshima.
- Watoto wa wafanyikazi -vigodoro ambavyo viliwekwa chini ya kitanda cha wazazi
- Wafanyikazi katika kampuni ya Patel waaingia kazi jogoo la kwanza na kutoka saa kumi na mbili jioni
- Wafinyikazi wanalipwa ujira mdogo wa shilling mia mbili kwa siku
- Wafanyikazi katika hospitali za umma wanakosa dawa za kuwapa wagonjwa
- Hospitali za umma zinakosa umeme sababu usimamizi wa hospitali haujalipia gharama.
- Wafanyaikazi wa hospitali za umma wanafisidi dawa za polio kwa kuwauzia maskini .
- wafanyikazi kupewa kazi ya kuhakikisha kazi imefanywa lakini ni wimbo tu.
- Watoto wa wafanyikazi hawatibiwi sababu wazazi wao wana ajira ya muda
- Wafanyikazi hawana bima(medical scheme)

***(zozote 10x 1=10)***

**6. SEHEMU D. HADIHI FUPI**

A.

- Ni kauli ya msimulizi wa hadithi
- Inamrejelea Samueli, mwanafunzi aliyehitimu kidato cha nne
- Samuel yuko katika faragha ya msalani pale shule alikoingia pasi na kusukumwa na haja.
- Hii ni baada ya kurushiwa, matokeo na mwalimu mkuu na kuona kuwa amefeli mtihani

***( 4 x 1 = 4)***

***b)*** Mwoga – Anapoingia afisi ya mwalimu mkuu anasitasita

- Anashindwa kuwakabili wazazi wake sababu amefeli mtihan
- Anatetemeka anapomwona babake pale bwagwani
- Mwenye majigambo: Anajigamba kuwa ana hakika amepita mtihani na kumshtua mwalimu mkuu
- Anajidai kuwa yeye simwerevu lakini anajua kupanga mambo yake na kile asomacho ndicho hutokea kwa mtihani
- Mwongo – Anadaa babake kuwa hakupata matokeo kwa kuwa hakukamilsha kulipa karo
- Mwenye bidii: Alitembea kilomita sita kwenda shule kila siku an kuwa alihudhuria madarasa yake vizuri.
- Mjinga:-Kutokana na majibu yake Samueli ni zuzu. Alifeli mtihani wa elimu

***Mcheshi:-***

Anachekesha kwa kauli zake kuhusu mwalimu mkuu na wazazi wake

Mwepesi wa kukata tamaa- Kufeli mtihani shuleni anaona kana kwamba amefeli maishani na kuamua kujiua.

***(zozote 6 x1 = 6)***

***c. Anasumbuliwa na kufeli mtihani***

- Anaona juhudi zakeza kutembea kilomita sita kuenda shuleni na kuhudhuria masomo zimeshindwa kuzaa matunda
- Analemewa ni vipi alifeli mtihani ilhali kuna mambo anayoyajua na alihudhuria masomo yyote.
- Anaona muda wa miaka minne, karo aliyolipiwa na babake zimepotea bure.
- Analemewa kuwa kuanguka mtihani ina maana hajui chochote/lolote
- Anaona kuwa babake hataelewa akimwambia kuwa ameanguka mtihani
- Anaona kuwa amewasaliti wazazi wake kwa sababu ndiye mwana wa kiume wa pekee hivyo ndiye tegemeo la kuwakwamua toka lindi la uchochole. (***zozote 5 x 2 =10)***

**7. "Manangu siku ile aliniamsha mapema….."**

(i)

- Haya ni maneno ya Bogoa Bakari
- Anawaambia mkewe Sakina, sebu ana mkewe Tunu, kazu na mkewe B Temu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

– Wamo club pogopogo
  Bogoa anawasimulia hadithi kuhusu jinsi alivyotolewa kwao nyumbani na kupelekwa kwa Bi Sinai aliyemtesa sana.

(ii) **Umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji**

– Kuchimuza suala la umaskini-wazazi wake Bogoa hawana uwezo wa kununua sabuni, Bogoa na babake kutembea kwa miguu bila viatu hadi mjini.
– Kuonyesha masaibu ya wanakijiji-walikuwa na tatizo la maji kwa maana yalikuwa hayapatikani karibu walitembea masafa marefu kuyatafuta
– Kumfumbulia Sebu fumbo alilotaka kufumbua. Amejua sababu ya Bogoa kutoroka nyumbani kwa Bi Sinai.
– Usimulizi unafichua aliyempeleka Bogoa kwa Bi Sinai ni babake
– Kusawiri maudhui ya mapenzi –mapenzi a Bogoa kwa nduguze, kwa wazazi wake yalimfanya kutotaka kutengana nao
– Kusisitiza kwamba Bogoa hakutaka kuishi na marafiki wa babake licha ya babake kusema ni wazuri –Alilia na kupiga ukwenzi
– Kusawiri maudhui ya elimu –Baba yake anamwambia angepelekwa shuleni kusoma
– Kuonyesha ukali wa baba yake Bogoa .Bogoa alipokataa kwenda kwa marafikize alimtishia kumchapa
– Kuendeleza maudhui ya ajira ya watoto-Bi Sinai alimtumia Bogoa kufanya kazi zote za nyumbani badala ya kumpeleka shule.
– Unachimuza suala la ukiukaji wa haki za watoto Bi Sinai anamtumia Bogoa kufanya kazi zote za nyumbani licha ya umri mdogo wa Bogoa hampeleki shule
– Kuanyesha maudhui ya utabaka- Bi Sinai anawaambia watoto wake kuwa watoto wa masini hawastahili kusoma bali kutumiwa nyumbani.
– Kufichua ukatili wa Bi Sinai-Anamchoma kwa kijinga cha moto baada ya kulala na kuacha mandazi kuungua
– Kuonyesha maudhui ya uwajibikaji- wazazi wa Bogoa wanamtembelea mjini kwa Bi Sinai kumsjulia hali.
– Kuendeleza maudhui ya siri-Bogoa aliteseka sana mikononi mwa Bi Sinai ila hakuwahi kumwambia rafikiye Sebu.
– Kubainisha masaibu a Bogoa –Bi Sinai hakumruhusu kutangamana na wazazi wake walipomtembea alikula makombo, anatusiwa, anakatazwa kucheza na watoto wengine, anatumikishwa nyumbani.

*( Zozote 8 x 1 = 8)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**iii) MASAIBU ALIYOPITIA BOGOA**

– Alikosa sabuni ya kuogea alipoamshwa siku ile mapema
– Alitembea kwa miguu bila viatu kutoka kwao hadi mjini.
– Amekosa mavazi bora, mamake alimpa shati kubwa lililompwaya
– Akiwa kwa Bi Sinai, alifanyishwa kazi nyingi za nyumbani kama kuchanja kuni, kupara samaki licha ya umri wake mdogo
– Hapelekwi shule bali alibaki nyumbani kufanya kazi za sulubu
– Bogoa hakuruhujiwa kucheza na watoto wengine
– Bogoa alichomwa kwa kijinga cha mto alipolala na kuache mandazi yakiungua
– Anakatazwa asitongamane na wazazi wake wakati wanakuja kumtembelea
– Bogoaanafiwa na wazazi wake na hata ,lezi wake Bi Sinai
– Bogoa alikua wa mwisho kula na tena alikula makombo. *(zozote 8 x 1 = 8)*

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8. a. MATATIZO YANAYOWEZA KUMKUMBA MTAFITI**

– Kushukiwa kuwa jasusi anayeipeleleze jamii na utamaduni wao unaweza kufukzwa
– Kunyimwa ruhusa na viongozi wa eneo unalotaka kutafiti
– Wanaotafitiwa kuomba malipo kabla ya kusimulia au kutoa habari
– Vikwazo vya kidini-wengi kudai fasihi simulizi inaenda kinyume na mafunzo ya dini.
– Kupotea/kufisidiwa vyombo vya utafiti
– Kuwepo kwa kupotea njia
– Ukosefu wa usalama mahali unaenda kutafiti

**(zozote 5 x 1= 5)**

b. Hatua za kutafiti/kurahisisha kazi yake(mtafiti)

– Kuwa mkarimu kadri inavyowezekana kwa kuwapatia marupurupu wanaomsaidia
– Kuwa mcheshi kwa watafitiwa ili kuwa na mlahaka mwema

- Kula na kunywa kinachopatikana katika jamii hiyo ili ujitambulishe na wenyeji
- Kuvaa mavazi ya kawaida yanayokubalika katika jamii anayotafiti
- Kutazama na kuandika anayoyasikia na kuona katika daftari- si lazima awe na kamera na video
- Ikiwezekana usiandike mbele ya msimulizi usije ukamkanganya,shuhudia andika baadaye.
- Ni busara kuepuka kubeba mitambo mikubwa ambayo inaweze kuleta shauku na wasiwasi.

**(zozote5x 1= 5)**

**c. FASIHI SIMULIZI KUHIFADHIWA ZAMANI**

- Ilihifahdiwa katika ubongo au akili ya watu hasa fanani walioisimulia

**d) TOA UDHAIFU WA JIBU LAKO HAPO JUU**

- Kumbukumbu za akilini zinaweza kufifia na kusahaulika
- Ajali inaweza kutokea na kuharibu ubongo asiweze kuhifadhi mambo
- Anayehifadhi anaweza kuyabadilisha mambo muhimu anayoyasimulia
- Fanani anaweza kufa. **(zozote 2 x 1 = 2)**

**e) SABABU ZA KUFIFIA FASIHI SIMULIZI**

- Kazi ya hati / maandishi imekuwa nyingi kiasi cha kufisha fasihi simulizi
- Uvumbuzi wa teknolojia ya kisasa umefanya kufifia kwa fasihi simulizi
- Wazee waliohifadhi na kuisimulia fasihi simulizi wamekufa
- Kutengana kwa wanajamii kwa sababu za kiuchumi imechangia kwa kufisa. **(zozote 2 x 1 = 2)**

**f) i) Miviga ni nini?**

Ni sherehe za kitamaduni zinazofanywa na jamii kwa kipindi Fulani.

**ii) Miviga kupigwa marufuku katika jamii**

- Miviga imeleta utengeno kati ya dini na wanafasihi simulizi
- Baadhi yamiviga huharibu mazingira
- Baadhi ya miviga huitilafiana na sheria za nchi
- Miviga inaweza kuchangia kusambaza kwa magonjwa ikiwa itahusu damu kutolewa/kunyoa
- Baadhi ya miviga inawatia hofu wanajamii
- Baadhi ya miviga imepitwa na wakati- mfano kutairi wanawake
- Baadhi ya miviga huleta hasara za kiuchumi **(zozote 3 x1=3)**

**g) Taja mifano ya ngomezi ya kisasa**

- Milio ya ambulensi
- Vingora vya magari ya rais
- Kengele shuleni au kanisani
- Honi kwenye magari
- Filimbi/firimbi michezoni **(Zozote 2x 1=2)**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**DAGORETTI/LANGATA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1**
**INSHA**
**DECEMBER 2020**

1. Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, uliweza kujiunga na kundi la vijana wa kaunti yenu wanaojaribu kuboresha maisha yao. Mwandikie gavana wa kaunti hiyo barua pepe ukimweleza changamoto mnazopitia na jinsi anavyoweza kusuluhisha.

2. Teknolojia ya kisasa ni kama sarafu yenye sura mbili. Jadili.

3. Umdhaniye ndiye siye. Onyesha ukweli wa methali hii.

4. Andika insha itakayomalizika kwa
………… tulijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi. Lakini jitihada zetu ziliambulia patupu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**DAGORETTI/LANGATA**
**TATHMINI YA PAMOJA YA MUHULA WA PILI - 2020**
**102/2**
**KISWAHILI (LUGHA).**
**DECEMBER 2020**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umasikini huu ni anuwai mathalan, ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaothiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni ya mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umasikini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tagemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

Maswali:
(a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)
(b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)
(c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umasikini ? (alama 4)
(d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)
(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)
   i) Kulitadarukia.
   ii) Kuatika.
   iii) Kuyaburia madeni.

**SEHEMU YA B: UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana hukopa msaimiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile 'shule' ulikopwa na kutoholewa kutokana na neno *schule*. Msamiati kama vile *'leso', 'karata' na 'mvinyo'* yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina 'balozi' na 'bahasha' yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha hazuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaba yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasibisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindio yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo sahili wa lugha ili kufanikisha mawasiliano. **Pijini** ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.

Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo ianyopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani, kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku lugha nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia au zitakufa na kusahaulika kabisa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1.** Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu. **(Maneno 50)** (alama8)
**Matayarisho**
**Jibu**

**2.** Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani? **(Maneno 30)** (alama 7)
**Matayarisho**
**Jibu**

3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

(a) Andika sifa za **kutambulisha** sauti zifuatazo. (alama 2)
(i) /d/ ________________________________________________
(ii) /th/ ________________________________________________

(b) **Fafanua** dhana ya **mofimu**. Bainisha **mofimu** katika maneno yafuatayo. (alama 2)
(i) Samaki ________________________________________________
(ii) Mtu ________________________________________________

(c) Ainisha **viambishi** kwa kurejelea **majukumu** ya kisarufi katika neno hili. (alama 3)
Alijipelekea

(d) Maneno **yaliyopigiwa** mstari yametumikaje? (alama 2)
Pahali pema pako si pema pa mwenzako.

(e) Andika sentensi **mbili** kutofantisha **vitate** hii. (alama 2)
(i) Apisha
(ii) Apiza

(f) Andika sentensi ifuatayo **upya** ukibadilisha neno **lililopigiwa** mstari kuwa kivumishi. (alama 2)
Mgeni alipewa dawati mpya.

(g) Unda nomino m**bilimbili** kutokana na vitenzi hivi. (alama 2)
(i) Kagua ________________________________________________
(ii) Hini________________________________________________

(h) **Kosoa** sentensi ifuatayo kisarufi. (alama 3)
Mahali kule pana siafu wengi.

(i) Tambua matumizi ya **'a'** katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Mwanafunzi acheza uwanjani.

(j) **Yakinisha** sentensi hii: (alama 2)
Usipofanya bidii hutapita mtihani.

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **kuamrisha**. (alama 2)
Tafadhali acheni kucheka ovyo.

(l) Andika kwa msemo wa **taarifa**: (alama 3)
"Sitakwenda sokoni leo ila nitakwenda kesho", Nikamjibu.

(m) Eleza matumizi **matatu** ya **kinyota**. (alama 3)

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 4)
Mlango umevunjwa na fundi aliyeujenga.

(o) Onyesha matumizi ya **chagizo** ya **mfanano** katika sentensi. (alama 2)
Alitembea kitausi kupokea zawadi.

(p) Andika sentensi ifuatayo kwa **udogo/wingi**. (alama 2)
Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.

(p) Tunga sentensi kuonyesha **matumizi** ya kiambishi **'ji'**.
(alama 2)

4. **ISIMU JAMII**:
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**
"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

**Maswali**
(i) Weka maneno haya katika sajili yake. (alama 2)
(ii) Nini kimekufanya uchague sajili uliochagua katika swali (i). (alama 1)
(iii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii. (alama 7)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**DAGORETTI/LANGATA**
**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA 3**
**DECEMBER 2020**

**SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI**
**LAZIMA**

1. A) i ) Taja aina mbili za maghani (Al.2)
ii) Eleza matatizo ya utafiti anayoweza kukumbana nayo mwanafasihi kule nyanjani (Al.8)
B) i) Misimu ni nini? (Al.2)
ii) Eleza umuhimu wa misimu. (Al. 8)

**SEHEMU B: Tamthilia**
**Kigogo : Na Pauline Kea**

2. " ……………Fungua macho uone. Keki ya uhuru imeliwa kwingine, mwaletewa masazo"
a) Eleza muktadha wa usemi huu. (Al. 4)
b) Thibitisha ukweli wa kauli kuwa keki ya uhuru imeliwa kwingine. (Al.8)
c) Eleza vizingiti vinavyomkabili mnenaji katika harakati za kusaka keki . (Al.4)
d) Jadili jazanda zinazojitokeza katika usemi huu. (Al.4)

**AU**

3. a.) Kwa kutumia mifano nane kutoka tamthilia, onyesha jinsi viongozi hutumia mamlaka yao vibaya (Al.8)
b.) Ukirejelea tamthilia, eleza nafasi sita chanya na nafasi sita hasi walizopewa wahusika wa kike (Al.12)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: RIWAYA.**
**Chozi la Heri: Na Assumpta Matei**

4. "………ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde, vitisho na matusi?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Al.4)
b) Taja mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili? (Al.2)
c) Fafanua umuhimu tatu wa msemaji wa maneno haya katika kuendeleza ujumbe wa riwaya (Al.6)
d) Jadili jinsi mbinu ya kinaya ilivyotumiwa na mwandishi katika riwaya hii kwa kutoa mifano nane. (Al.8)

**AU**

5. a) Kwa kutumia mifano kumi, dhihirisha ufaafu wa anwani "Chozi la Heri" (Al.20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
**Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine: Na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda – wahariri.**
**SHIBE INATUMALIZA**

6. "Ndugu yangu kula kunatumaliza"
"Kunatumaliza au tunakumaliza"
a) Fafanua muktadha wa dondo hili. (Al.4)
b) Jadili maana ya ndani/kitamathali katika kauli "kula tunakumaliza" (Al.10)
c) Ukirejelea mifano sita, onyesha ni kwa namna gani kula kunawamaliza watu wa jamii hii. (Al.6)

**AU**

7. a ) Kwa mujibu wa hadithi ya "Mame Bakari" ubahaimu unaotendewa mwanamke umekuwa na athari mbaya kwake. Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kutumia mifano mwafaka. (Al.10)
b.) Huku ukitumia mifano kumi, dhihirisha kuwa masharti ya kisasa ni anwani mwafaka kwa hadithi hii. (Al. 10)

**SEHEMU E: USHAIRI**

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Punda kalibeba gari, gari limebeba punda
Mwalimu anapakari, muashi vyuma adunda
Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda

Kinyume mbele.

SaramAla ahubiri, muhunzi tiba apenda
Mganga anaabiri, baharini anakwenda
Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
Kinyume mbele.
Wakili ana hiyari, biashara kutenda
Mtazame askari,akaza kaza kitanda
Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
Kinyume mbele
Apakasa daktari, ukili anaupinda
Saveya kawa jabari, mawe anafundafunda
Hazini wa utajiri, mali yote aiponda.
Kinyume mbele

Msemi huwa hasemi , wa inda hafanyi inda.
Fahali hawasimami, wanene walishakonda
Waliojitia utemi, maisha yamewavunda
Kinyume mbele.

Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
Tele haitakadiri huvia tulivyopanda
Mipango imehajiri, la kunyooka hupinda.
Kinyume mbele.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

**a)** Mtunzi alikuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? Taja matatu. (Al.3)

b) Licha ya tarbia, taja na ueleze bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. ( Al.4)

c) Jadili jinsi idhini ya mshairi ilivyotumiwa katika shairi hili kwa kutumia mifano minne (Al.4)

d) Uandike ubeti wa nne kwa lugha tutumbi (Al.4)

e) Eleza toni ya shairi hili. (Al.2)

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.
   i) Inda
   ii) Utemi
   iii) Imehajiri. (AL.3)

**LANGATA/DAGORETTI**
**MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MUHULA WA PILI 2020**
**<u>102/2</u>**
**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA</u>**

**2. UFAHAMU**

(a)
- Ufisadi
- Uongozi mbaya
- Turathi za kikoloni
- Uchumi kuegemezwa kwenya kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika.
- Idadi kubwa ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika.
- Ukosefu wa nyenzo na mali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini.
- Ukosefu wa elimu na nafasi za ajira. Zozote (4x1 = alama 4)

(b)
Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. (2x1 = alama 2)

(c)

- Kuibuka kuwa mikakati bora ya kupambana na umaskini.
- Pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini.
- Kuzalisha nafasi za kazi kwa dharura.
- Kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi.
- Kuendeleza elimu.
- Kuimarisha miundo msingi. (4 x 1 = alama 4)

(d)

Ni chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umasikini zaidi. (1 x 2 = alama 2)

(e)

- Kulitadarukia – kulishughulikia, kulitatua, kulikabili.
- Kuatika – kuanzisha kutia, kuzua.
- Kuyaburia madeni kuyasamehe madeni, kuyaondolea madeni. (3x1 = 3mks

**3. MAJIBU YA UFUPISHO**

(a) <u>Hoja za kuzingatia</u>

- Mitagusano ya kijamii hufanya lugha kuathiriana.
- Ukopaji wa vipengele vya lugha ni moja ya athari hizo.
- Msamiati hukopwa ili kueleza dhana ngeni.
- Lugha zote hukopa.
- Kiingereza kimekopa kutoka kilatini, kifansa na Kiswahili.
- Kiswahili nacho kimekopa kutoka kiingereza, kiarabu, kireno, kituruki na kijerumani.

(b) <u>Hoja za kuzingatia</u>

- Kuzuka kwa hali ya uwingi – lugha.
- Ukuaji wa lugha.
- Kuzuka kwa lugha mpya.
- Kudunishwa kwa lugha.
- Kufa kwa lugha.

**4. MAJIBU YA LUGHA**

(a) <u>Sifa za sauti / d /</u>

(i) Ni kipasuo.
(ii) Hutamkiwa kwenye ufizi
(iii) Ni sauti ghuna. (½ x 2)

<u>Sifa za / th /</u>

(i) Ni kikwaruzo / kikwamizo.
(ii) Hutamkiwa menoni.
(iii) Ni hafifu (si ghuna) (½ x 2)

(b) Ni kipashio kidogo cha neno ambacho hakiwezi kugawika zaidi na kina maana.

(i) Samaki (alama 1)
(ii) Mtu => m-tu.
(alama 1)

(c) alijipelekea

| a | - li | - ji - | pelek | - e | - a |
|---|---|---|---|---|---|
| nafsi ya umoja | wakati uliopita | mtendwa | mzizi | kauli | kiishio |


(6 x ½ = alama 3)

(d) Pema – kivumishi

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Pema – kiwakilishi (2 x 1 = alama 2)

(e) Apisha – kulitamka jina la Mungu kama njia ya uthibitisho.
Apiza – kutamkia mtu maovu. (2 x 1 = alama 2)
(f) Mwanafunzi mgeni alipewa dawati mpya. (2 x 1 = alama 2)
(g) Ukaguzi, mkaguzi, wakaguzi, kukagua. (½ x 2)
Mhini, uhini, kuhini , mhiniwa. (½ x 2)
(h) Mahali mle mna siafu wengi.
Pahali pale pana siafu wengi.
Mahali kule kuna siafu wengi.
(alama 3)
(i) Hali isiyodhihirika. (1 x 1 = 1)
(j) Ukifanya bidii utapita mtihani. (2 x 1 = 2)
(k) Acheni kucheka ovyo! (2 x 1 = 2)
(l) Nilimjibu kuwa singeenda sokoni siku hiyo ila ningeenda siku iliyofuata. (alama 5)
(m) (i) Maana zaidi ya neno fulani.
(ii) Neno limeendelezwa vibaya.
(iii) Sentensi ina makosa ya kisarufi. (alama 3)
(n)




(o) Mwanafunzi atunge sentensi akitumia vielezi vya namna mfanano kama Alitembea kitausi kupokea zawadi. (alama 2)
(p) Vitoto vikaidi viliiba vijitabu vya wenzao.
(alama 2)
(q) (i) Ukubwa
(ii) Kiambishi awali katika baadhi ya nomino katika ngeli ya LI-YA.
(iii) Kuonyesha uzoefu.
(iv) kujitendea (2x1 = alama 2)

**5. ISIMU JAMII**
(a) Hii ni sajili ya maabadini / dini.
(b) Sababu
(i) Matumizi ya maneno kama kutakasa nyoyo kabla ya kushiriki karamu ya Bwana.
(ii) Kumwendea Bwana atuondolee dhambi zetu. (Zozote 2x1 = 2)
(c) Sifa
(i) Matumizi ya msamiati maalum kwa mfano: Mungu asifiwe.
Alhadulillahi!
Shetani ashindwe!
(ii) Matumizi ya sentensi refu ili kuweza kueleweka vizuri na waamini.
(iii) Kudondoa kauli yaani kurejelea sehemu fulani katika maandiko matakatifu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(iv) Uradidi wa maneno kurudiarudia maneno kama:
Mungu yu mwema
Mwenyezi Mungu
Amina n.k.

(v) Matumizi ya ishara na miondoko.
Anapohubiri hutumia ishara na miondoko mfano kuinua mkono, Kuruka kutoka hapa na pale.

(vi) Kuchanganya nyakati sana kwa mfano: naye akaondoka hapo waende upande wa mashariki.

(vii) Matumizi ya maneno yenye asili ya kigeni kwa mfano: majina ya wahusika Sila na Petero.

(viii) Matumizi ya lugha maalum kama vile tamathali za usemi, taswira, jazanda n.k. (7x1 = 7)

**DAORETI/LANGATTA**
**Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari (K.C.S.E) 2020**
**KARATASI YA III - FASIHI**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. a) i) Aina za maghani
 i) Majigambo
 ii) Sifo
 iii) Tendi
 iv) Tondozi
 v) Rara
 vi) Pembezi Zozote 2 x 1 = 2

 ii)
- Ukosefu wa usalama
- Baadhi ya jamii haziruhusu watu kuingilia mambo yao
- Gharama ya usafiri
- Ukosefu wa vifaa
- Lugha inaweza kuwa changamoto
- Kutopata data ya kutosha (jamii zingine zilitupilia mbali mila zao)
- Kutokuwa na muda wa kutosha
- Hali mbaya ya anga
- Barabara zisizopitika *Zozote 8 x 1 = 8*

b) i) Misimu ni msamiati ambao huzuka katika kipindi fulani cha wakati na kutumika katika lugha na pengine baadaye hutoweka. *Al. 2*

 ii)
- Ni kitambulisho cha kundi fulani katika jamii.
- Hutumika kuhifadhi siri katika kundi fulani katika jamii.
- Inapokubaliwa huwa sehemu ya lugha fulani.
- Huondoa urasmi katika mazungumzo na kuleta uelewano wa haraka.
- Hukuza ushirikiano na uaminifu miongoni mwa watumizi.
- Huhifadhi historia ya jamii husika.
- Hutumiwa kuibua hisia za makundi mbali mbali katika jamii.
- Huongeza ladha katika mazungumzo na kuyafanya yavutie.
- Hutumiwa kufidia ukosefu wa msamiati. *Zozote 8 x 1 = 8*

2. a)
- Ni maneno ya Sudi
- Akimweleza Kombe
- Ni katika karakana iliyoko sokoni ya uchongaji wa vinyago ya Kombe, Boza na Sudi.
- Wameletewa keki (masalio) ya sherehe za taifa na Kenga.
- Sudi anapuuzilia mbali keki na kuiita kijikeki. *Zozote 4 x 1 = 4*
 *(mtahini lazima ataje msemaji)*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) (Mwanafunzi afasiri kuwa keki ya uhuru ni marufaa au faida ya uhuru huo).
- Soko linafungwa na bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni inapanda maradufu.
- Mtoto wa Sudi, Pendo analia kwa njia.
- Majoka anadai kuwa kuzaa ni kulea. (kwa vile ana uwezo wa kulisha watoto vizuri).
- Majoka ana kampuni kubwa ya Majoka na Majoka Academy ilhali anafunga soko la wachochole.
- Waandamanaji wanakabiliwa kwa nguvu na maandamano yao ya kudai haki yanaharamishwa.
- Viongozi chipukizi kama vile Tunu wanakandamizwa.
- Wafanyakazi wanaongezwa mshahara kwa asilimia ndogo na kisha kodi inapandishwa.
- Uongozi unazunguka tu katika nasaba ya Majoka; hata Majoka anataka kumtambulisha Ngao Junior kama mrithi rasmi.
- Runinga za Sagamoyo, hasa ya Mzalendo, zinafungwa huku ya Sauti ya Mashujaa pekee ikiruhusiwa kuendelea kuhudumu.
- Aila za kina Siti na Kombe zinatakiwa kuhama kutoka Sagamoyo ikidaiwa kuwa si kwao. *Zozote 8 x 1 = 8*

c)
- Sudi anasalitiwa na wenzake (Kombe na Boza wanashikirikiana na Kenga na Majoka).
- Mkewe Sudi, Ashua anatiwa mbaroni na Majoka.
- Majoka anamshawishi Ashua amuasi Sudi na uhusiane naye kimapenzi. Hata anafanywa kuamini ana uhusiano wa kimapenzi na Tunu.
- Watoto wa Sudi wanakosa chakula.
- Mshirika wa karibu wa Sudi, Tunu, anashutumiwa kwa kuuza nyonga na kina Ngurumo ambao wanasisitiza watampigia kura mzee Majoka. *Zozote 4 x 1 = 4*

d)
- Keki ya uhuru – manufaa/faida ya uhuru k.v chakula, usalama, elimu, mshahara n.k.
- Imeliwa kwingine – faida ya uhuru inawafikia viongozi wachache na vikaragozi wao k.v Majoka, Kenga, Asiya, Husda, Ngao Junior n.k
- Masazo – mabaki ya manufaa ya uhuru, keki anayopewa Boza haimtoshelezi na familia yake, mshahara wanaoongezewa wafanyakazi unatozwa kodi kubwa.
- Fungua macho – Sudi kuwa mwerevu na kubaini ukweli kuwa keki wanayopewa si halisi.

*Zozote 2 x 2 = 4 (kutaja jazanda – 1, kutaja maana – 1)*

3. a)
- Kutumia rasilmali za umma kugharamia sherehe za kibinafsi k.m Majoka kusherehekea siku ya kuzaliwa.
- Kuangamiza wapinzani wa kisiasa mf. Majoka kuua Jabali, Tunu kujeruhiwa vibaya.
- Ubaguzi mf. Majoka kuajiri watu wa uhusiano naye k.v Kenga, Asiya kupewa kandarasi ya kuoka keki kwa vile ana uhusiano na Ngurumo, rafiki wa Majoka.
- Majoka anaamrisha kufungwa kwa soko la Chapakazi kwa vile anataka kubomoa vibanda na kujenga hoteli ya kifahari.
- Serikali ya Majoka kulipisha kodi ya juu sana. Kombe anadai hawalipi kodi tu bali kodi na kitu juu yako.
- Majoka anaendeleza unyakuzi wa ardhi. Anapanga kumgawia Kenga kipande cha ardhi sokoni.
- Kutojali maslahi ya raia. Majoka anaidhinisha uuzaji wa pombe haramu kwa raia ambayo inawapofusha kuona wanywaji.
- Majoka anapata mikopo anayotumia kwa miradi duni kama vile uchongaji wa viwango vya marehemu babake.
- Kuchafua mazingira, Majoka anaruhusu ukataji wa miti ovyo ovyo na utupaji wa taka kutoka viwandani.
- Kutumia vibaya vyombo vya dola k.m Majoka kutumia polisi kupiga waandamaji na kuua wengine.

b) Nafasi Chanya
- Wenye bidii – Ashina anauza maembe sokoni na Tunu anashughulikia ukombozi na kufaulu.
- Watetezi wa haki – Ashua anatetea haki ya wanafunzi wa Majoka na Majoka Academy naye Tunu anatetea haki ya wanasagamoyo kutumia soko.
- Ni wanamapinduzi – Ashua anapinga hatua ya Majoka kunyakua uwanja. Tunu naye anaongoza watu kumtoa Majoka uongozini.
- Wazalendo halisi – Tunu anakataa kuolewa na Ngao Junior ili asipoe moto wa kutetea wanasagamoyo. Ashua anakataa kazi katika shule ya Majoka kwa vile inahusishwa na utumiaji wa dawa za kulevya.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Waadilifu – Ashua anakataa kujihusisha kimapenzi na Majoka licha ya Majoka kumshawishi. Tunu anatembea na Sudi lakini hajihusishi kimapenzi naye.
- Walezi bora – Hashina anamlea Tunu vyema baada ya mumewe kufariki na anakataa kuolewa na Majoka.
- Ashua anaenda kwa Majoka kuomba chakula na anapotiwa kizuizini, anawakumbuka watoto wake na kusema kuwa ananyonyesha.
- Wasalihina – Siti anaamini katika nguvu za Mungu kwani wanapotishwa, anasema "Tutamtegemea Mungu". Hashina pia anamwambia Tunu kuwa "kama ni lazima uende huko naona heri tuseme dua".
- Wenye msimamo thabiti – Siti anakataa kunywa pombe kwa mamapima, Tunu akataa kuolewa na Ngao Junior na Ashua anakataa kujihusisha kimapenzi na Majoka. *Zozote 6 x 1 = 6*

Nafasi hasi
- Wavunja sheria – mamapima anaendesha biashara yakuuza pombe haramu.
- Wenye mabezo – Husda anambeza Ashua akimuita kimada naye Ashua ansema Husda ni mdaku.
- Wafasiki – mamapima anashiriki mapenzi na Ngurumo na pia na walevi hapo nyumbani kwake.
- Wenye tamaa ya mali – Ashua anakosa subira na kumwambia Sudi kuwa wamemfungua macho na kuwa akiwa ameshindwa kumtunza aseme.
- Waoga – Ashua na Husda wanamwogopa Majoka wanapokabiliana ofisini mwake.
- Wenye mapendeleo – Husda anamsaidia mamapima kupata kandarasi ya kuoka keki kwa kuwa ni mkoi wake.
- Wapendaraha - Husda anaenda kuponda raha huko Majoka and Majoka Resort na kufurahia kuogelea na kuota jua. *Zozote 6 x 1 = 6*

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

4. a)
- Ni uzungumzi nafsia wa Sauna
- Sauna yuko nyumbani kwa Bi. Kangara.
- Anawaza kuhusu kilichomfanya aingilie biashara ya ulanguzi wa watoto.
- Anakumbuka jinsi alivyotoweka nyumbani baada ya kunajisiwa na babake mlezi, Bwana Maya.
- Alitoroka baada ya kukosa usaidizi wa mamake aliyemwogopa Bwana Maya sana.

*Zozote 4 x 1 = 4*
*(Lazima ataje msemaji)*

b) Balagha *Al. 2*

c) Umuhimu wa Sauna (Auntie Sauna)
- Anawakilisha wasichana katika jamii wanaodhulumiwa kimapenzi na baba walezi. Sauna alinajisiwa na Bwana Maya na kupata mimba.
- Anafichua ukatili wa baadhi ya wazazi wa kike katika jamii. Mamake alipogundua ana mimba, alimpeleka hospitali ili kuavya mimba hiyo.
- Anatumiwa kuendeleza maudhui ya ulanguzi wa watoto na dawa za kulevya.
- Ametumiwa kudhihirisha maudhui ya taasubi ya kiume. Sauna anasema Bwana Maya alitawaliwa na ubabedune.
- Anawakilisha vijakazi wanafiki wanaojifanya wazuri ilhali wana nia ya kutekeleza uhalifu.Sauna alijipendekeza kwa wajiri wake akiwa na nia ya kuwaiba watoto wao.
- Ametumwa kutoa funzo kuwa maovu yana mwisho. *Zozote 3 x 2 = 6*

d) Kinaya
- Vijana wanaosomea shahada ya uzamili katika chuo kikuu wanakunywa pombe haramu licha ya kushuhudia ikiwaangamiza watu wengine.
- Lunga Kiriri – Kangata anafutwa kazi badala ya kupongezwa alipowatetea wananchi kuhusu kula mahindi ya manjano yaliyohofiwa kuharibika.
- Shamsi na wenzake wanapoomba kuongezewa mshahara badala yake wanafutwa kazi.
- Walinda usalama wanatazama tu watu wakipora na kuteketeza mali ya Mzee Kaumu bila kufanya lolote.
- Ami zake Lucia wanapinga kuolewa kwake katika ukoo wa Waombwe ilhali Kiriri aliyetoka katika ukoo huo ndiye aliyeyadhamini masomo yake.
- Lunga Kiriri – Kangata anajishika tama mchana kutwa na huku amewaonya wanawe, Umukheri, Mwaliko na Dickson dhidi ya kujishika tama.
- Wanasiasa wanawahimiza vijana kurudi mashambani kulima wakisema hao ndio wenye nguvu ilhali ni wao waliowaahidi nafasi za kazi za kuandikwa mjini.

- Wahafidhina hawafaidiki kutokana na uchimbaji wa madini yanayopatikana nchini mwao kwa vile serikali yao inazipa nchi za kigeni kandarasi za kuchimbua madini.
- Ridhaa anaamini kuwa bundi na kereng'ende wanaolia waliashiria kutendeka kwa jambo fulani baya ilhali hapo awali amemwambia mkewe ajitenge na ushirikina kwa kuwa hufisha maendeleo.
- Viongozi wanawaahidi wakazi wa mandoporomoka kuwa watawajengea nyumba za hadhi kwa gharama nafuu lakini baadaye viongozi hao hao wanajichukulia hizo nyumba.
- Watoto kutoka familia zinazojiweza kiuchumi ndio wanaopewa mikopo ya kugharamia masomo huku watoto kutoka jamii maskini wakilazimika kufanya vibarua ili kujilipia karo. *Za kwanza 8 x 1 = 8*

5. a) Chozi la Heri ni hali ya machozi kutoka baada ya dhiki, aghalabu kuashiria faraja.

- Katika uwanja na ndege, Umukheri na Dickson wanapatana baada ya kupoteleana wakiwa wadogo. Wanalia machozi wakiambiana kimoyomoyo yaliyowakumba.
- Katika hoteli ya Majaliwa, Umukheri anakumbuka jinsi alivyopewa maisha mapya na malezi ya Mwangeka na Rachael Apondi. Pia wanadhamini masomo ya Dickson. Akumbukapo haya, anatokwa na machozi ya heri.
- Ridhaa anamwoza mwanawe, mwangeka, mke wa pili, Rachael Apondi baada ya kifo cha Lily huku machozi ya heri yakirovya kidari chake.
- Mwangeka anapoteza familia yake katika mkasa wa moto lakini mambo yanatengenea baada ya miaka mitatu anapopatana na Rachael Apondi. Anapata heri.
- Rachael Apondi anapojifungua mtoto wake, Ridhaa, anatokwa na machozi ya heri kwa vile anajua mtoto huyu ataunganisha uhusiano wake na Mwangeka.
- Mwangeka amemwambia Umukheri kuwa siku walipoenda kumchukua kutoka kwa mwalimu Dhahabu ilikuwa siku ya heri kwani alimkumbusha Becky aliyeaga dunia baada ya uvamizi.
- Mwanaheri anapoachwa na mamake, Subira, anaona maisha yamefika tamati. Hata hivyo yuko shuleni Tangamano ambapo ana nafasi ya kusoma ambapo anapata heri.
- Chandachema anaachwa mikononi mwa nyanyake. Baada ya kifo cha Nyanya, anaenda kufanya vibarua na kuishia katika makao ya mayatima. Sasa ana heri.
- Zoheri anajipata katika shida anapokuwa mjamzito. Hatimaye anapelekwa katika kituo cha watoto na kusaidiwa na mtawa Pacha. Sasa ana heri.
- Dickson anapitia matatizo mengi anapolangua madawa ya kulevya lakini baadaye anapata heri anapoanza kuuza vifaa vya umeme.
- Umukheri anateseka kutokana na kifo cha babake. Baadaye anasaidiwa kupata Rachael Apondi na Mwangeka wanaokuwa familia yake. Amekuwa na heri anaposoma hadi ng'ambo.
- Selume anafukuzwa kwa mumewe kwa tuhuma za kuunga mkono mpinzani wake wa kisiasa. Pia alipata shida afanyapo kazi katika hospitali za umma. Maisha yake yanapata heri anapoajiriwa katika kituo cha Afya cha Mwanzo Mpya.
- Kaizeri anakuwa na uchungu mkewe, Subira anapomwacha. Anakonda sana lakini baadaye anapata heri anapoajiriwa katika kituo cha Afya cha Mwanzo Mpya.
- Neema ambaye hakuwa na mtoto, alitokwa na chozi la heri alipoandamana na Mwangemi hadi kwenye kituo cha watoto ambapo anakabidhiwa Mwaliko.
- Mwaliko alihuzunika sana alipoachwa na wazazi wake lakini baadaye anapata heri anapopelekwa kituo cha watoto cha Benefacto, ambapo amechukuliwa na Neema na Mwangemi.
- Ridhaa anahuzunika familia yake inapoangamia katika mkasa wa moto. Hata hivyo kuna chozi la heri Ridhaa anapokumbuka kuwa mwanawe, Mwangeka amenusurika mkasa huo.
- Machozi ya huzuni yanawatoka wakaazi wa msitu wa Mamba kwa kukosa huduma, chakula na kusumbuliwa na magonjwa. Hawa wakimbizi wanapata heri, Selume anapoleta ujumbe kuwa wangejengewa nyumba mpya. Pia wanapata msaada wa chakula. *Za kwanza 10 x 2 = 20*

6. a)

- Kauli ya kwanza ni ya Mbura
- kauli ya pili ni ya Sasa.
- Walikuwa kwa Mzee Mambo.
- Mzee Mambo alikuwa ameandaa sherehe ya mtoto wake mmoja kusajiliwa katika shule ya nasari na wa pili meno yalikuwa yamepasua ufizi.
- Wanasema haya baada ya kula sana katika sherehe. *Zozote 4 x 1 = 4*

*(lazima amtaje msemaji)*

b)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Mzee Mambo kuwa waziri kivuli wa wizara zote – kupokea mshahara lakini hana kazi.
- wafanyakazi ni watepetevu – wanafika kazini lakini hawafanyi chochote.
- Vyeo vya mzee Mambo vinampa fursa ya kupakua mshahara (yeye anachota tu, hapewi).
- Wizara moja kuendeshwa na mawaziri wawili – Sasa na Mbura ni mawaziri wa wizara ya mipango na mipangilio.
- Wote wawili wanasimamia wizara kwa namna ya kujifaidi – wadai kuwa wizara ndiyo inawaendesha hasa.
- Magari ya serikali kutumiwa vibaya kama vile kuleta jamaa kwa sherehe pamoja na vyakula.
- Mbweo anayotoa Mbura ni ishara ya shibe. Ni dalili ya kiburi cha viongozi kuridhika kutokana na wizi wa mali ya umma.
- Jinsi Mbura na Sasa wanafakamia chakula upesi ni taswira ya jinsi viongozi wanapapia mali ya umma bila kuona haya.
- Matajiri hawajali lawama kutokana na wizi wanaofanya. DJ kwenye sherehe ya Mzee Mambo hajali lawama kwa kulipwa mabilioni ya pesa kutoka hazina ya umma.
- Pia DJ ana duka la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kubwa ya dawa za serikali.
- DJ na wenzake wanapata huduma za kimsingi k.v maji, umeme huku raia wakiumia. *Zozote 5 x 2 = 10*

c)

- Kuna magonjwa yanayosababishwa na kula chakula kisicho bora k.m sukari, seratani, presha n.k
- Kuna mauaji – watu wanauana kwa risasi na bomu na hata kunyongana kutokana na unyakuzi wa mali ya umma.
- Kuna uhalifu wa kunyang'anyana mali.
- Kutokuwa na utu/ukosefu wa heshima.
- Kutojirudi kutokana na makosa wafanyayo yaani kutokiri kosa na kuomba msamaha watendapo kosa.
- Kuna kuhalalisha wizi/unyakuzi – aliyepewa hapokonyeki.
- Kuna hali ya kuuana kifikira na kimawazo. *Zozote 6 x 1 = 6*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

7. a)

- Sara anapobakwa anapoteza fahamu na anaaibika anapozinduka na kujipata yu uchi.
- Kujeruhiwa – Baada ya Sara kubakwa, anaharibiwa na kuvuja damu.
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake.
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa.
- Masomo yake kukatizwa – Sarah anapewa barua ya kufukuzwa shule.
- Kukejeliwa – mwalimu hamsikilizi Sara bali anamkejeli na kusema hawafundishi wanawake hapo.
- Anateseka kiakili – Sara anaingiwa na mawazo jinsi atakavyoikubali hiyo mimba. Anawazia kuitoa, kuhama kwao au kujiua.
- Kubebeshwa mimba akiwa na umri mdogo. Mzigo huo unakuwa changamoto kutokana na umri wake mdogo.
- Kuishi kwa hofu ya adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.
- Kuogopa kutoa taarifa kwa wazazi kwa sababu wazazi hawangemwamini.
- Kuishi maisha ya kimaskini – tunaambiwa Sara angekunjiwakunjiwa matambara yake na kutupiwa nje.
- Kulaumiwa kila anapobakwa – Hata huonwa kama shetani na kulaumiwa. *Zozote 10 x 1 = 10*

b)

- Dadi ndiye mchuma riziki – anafaa kuuza samaki na kupata riziki huku pesa za mke zikitumiwa kununua fasheni.
- Dadi kusaidia kazi za nyumbani lakini bado kidawa, mkewe, hatosheki.
- Kidawa hakubali kuwa kazi za mume ni za nje bali za ndani ni hisani tu.
- Dadi analazimika kushika shughuli za upishi k.m kutia mboga tui.
- Dadi anaosha nyumba, anafagia, kufua na kupiga pasi nguo.
- Wanandoa kujiwekea mashati ya uzazi. Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu.
- Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa na kuuzia wateja.
- Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe lakini anaogopa kumweleza.
- Licha ya kuona ugumu wa masharti ya mkewe, Dadi hakuweza kuyakataa.
- Dadi kushuku mkewe ana uhusiano na mwalimu mkuu kunampa wasiwasi hadi ameshindwa kula.
- Kila mara Dadi alitarajiwa kuondoa vyombo mezani baada ya kula, na kuvisafisha.
- Dadi anapozua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu, jambo linalopelekea yeye kuanguka na kuumia. *Za kwanza 10 x 10 = 10*

8. a)

- Kuhimiza watu washikilie taaluma zao.
- Kukashifu/kushutumu ukosefu wa mwelekeo jinsi mambo yanavyoendeshwa.
- Kukuza msamiati wa wasomaji kuhusu watu na kazi zao. *Zote 3 x 1 =3*

b)
- Msuko – kibwagizo kimefupisha.
- Ukara – vina vya utao vinatiririka ilhali vya ukwapi vinabadilikabadilika. *Zote 2 x 2 = 4*

c) i) Inkisari – Walojitia – waliojitia, kiwapi – kiko wapi, kalibebe – akalibebe
ii) Tabdila – anahiyari – anahiari
Yamewavunda – yamewavunja
iii) Kuboronga sarufi
- Muashi vyuma adunda – muashi adunda vyuma
- Mhunzi tiba apenda – Mhunzi apenda tiba
- Baharini anakwenda – Anakwenda baharini

iv) Utohozi – Saveya – Soroveya
v) Lahaja – Yamewavunda, anafundafunda *Zozote 4 x 1 = 4*

d)
- Mwanasheria anaona heri afanye biashara.
- Askari naye anatengeneza kitanda.
- Mkulima wa kusifika naye anashindwa kulima.
- Kinyume ndicho kinapewa umuhimu. *Zozote 4 x 1 = 4*

e) Toni ya shairi – Masikitiko, mshangao.

f) i) Inda – Uchoyo, kiburi
ii) Utemi – Ukubwa, uongozi
iii) Imehajiri – imehama, imepotea, imeenda mrama

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MECS I**
**102/ 1 KISWAHILI INSHA**
**KARATASI YA KWANZA**

**Insha ya lazima**

1. Andika mahojiano baina ya waziri wa usalama wa kitaifa na waandishi watatu wa habari kuhusu hali ya usalama nchini.

2. Pendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa kukuza umoja wa kitaifa.

3. Mla cha mwenziwe na chake huliwa.

4. Tunga insha itakayoanzia kwa maneno yafuatayo.
   Alfajiri ya siku iliyofuata ilinipata nje ya mlango wa hospitali kuu ya kijito. Punde si punde milango ya wodi ikafunguliwa.Machozi yalinitiririka njia mbili nilipotupa macho kwenye kitanda alicholazwa mamangu.Hakuwepo............

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MECS I**
**102/2**
**Kiswahili**
**Karatasi ya 2**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA 2020**

**1. UFAHAMU - ALAMA 15**
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Mafisa wa ukaguzi wa abiria na mizigo alimrudishia cheti chake cha usafiri na kubofya tarakilishi yake kuashiria kuanza kumhudumia mteja mwingine. Duma alikichukua cheti chake cha usafiri kwa pupa, kana kwamba anamtarajia mtu kuja kukibwakura. Moyo wake ulitweta na kukiumiza kidari chake kikembe nusura kukipasua. Baada ya kukihifadhi cheti hiki ndani ya mfuko wake mdogo wa kusafiria, alichapuka moja kwa moja hadi chumbani ambamo wasafiri hungojea kuiva kwa safari.

Si kwamba Duma ni mwanagenzi wa safari za Ughaibuni. La! Hasha. Amekia vilele vya anga kwa muda wa miaka isiyopungua kumi sasa, tangu alipochukuliwa kijijini mwao akiwa na umri wa miaka kumi na miwili; mjomba wake anakuja kumtafutia kazi. Kazi aliyopata ilimtia tumbo joto mwanzoni, akataka kutoroka, atakomee kotote kule. Fikiria wewe, ndio sasa umetoka kwenye kazi ya kuvuna majani kwenye shamba kubwa la Bwana Mali, majani ambayo uapopata fursa ya kuyatafuna yanakufanya kujihisi kama tiari inayoelea angani! Kisha baadaye upagazwe kazi ya kuyauza majani hayo hayo, pamoja na unga unaohifadhiwa katika vifuko vidogo vya kuvutia, kwenye soko la siri na hata shuleni! Hata hivyo walisema wasemao kwamba papo kwa papo kamba hukata jiwe, na kinolewacho hupata.

Duma alipata walimu, akafunzwa jinsi ya kuyatumia majani na aina mbalimbali za unga ili kuituliza nadhari na dhamiri yake ambayo awali ikimsumbua sana. Polepole ule utu na ulimbukeni aliokuwa nao uliyeyuka, akatwaa moyo wa jiwe na kuikumbatia kazi hii kwa dhati ya moyo wake, moyoni akijiambia kuwa hayo ndiyo majaliwa yake. "Ikiwa huu si utashi was Mungu, kwa nini akalituma gonjwa kuja kuwaua wazazi wangu, mmoja baada ya mwingine?" "Kwa nini akawaacha akina ami kunipoka kidogo kilochobakizwa na matibabu ya wazazi wangu? Kwa nini asimtume mtu kuja kuniokoa nilipoingizwa kwenye biashara hii na mjomba Papa? " duma alijiuliza maswali haya mfululizo. Hatimaye aliihalalisha kazi yake kwa kusema, "Kazi mbi si mchezo mwema.

Duma alipopata tajiriba ya kutosha kupambana na walinda usalama wenye macho ya kipanga, mwajiri wake hakusita kumtumia kwenye safari za kusafirisha shehena kwenye masoko ya ng' ambo. Mara nyingi aliponea tundu la sindano kutiwa mbaroni. Wakati mwingine mashine za ukaguzi ziliweza kunusa shehena yake, akalazimika kulainisha viganja vya maafisa wakuu wa forodha. Kila mara alijiambia, "Hii kazi ni hatari, nikipata

pesa za kutosha kuufukuza uhawinde nitang'atuka." Hata hivyo, Duma tayari alikwisha kuwa sikio la kufa. Alikuwa amedidimia katika ulanguzi wa dawa za kulevya, ulanguzi ambao ulikuwa umemwingia kwenye mishipa jinsi dawa zenyewe zilivyokuwa zimegeuka damu inayousukuma moyo wake. Badala ya kuacha, yeye na mwajiri wake walizua mikakati mipya ya kusarisiha shehena.

Safari ya leo ilipoiva, Duma alifanya kama alivyoagizwa na mwajili wake. Asubuhi na mapema alibugia shehena yake, koo ikakubali kuisafirisa hadi tumboni ambapo uchango wake uliombwa kuihifashi hadi utakapofika wakati wa kuitapika shehena hiyo Ugaibuni. Fungu lililobaki lilitiwa ndani ya begi la kusaria, katikati ya nguo. Duma alitarajia kwamba atampata jamaa wake wa kawaida wkenye forodha. Akajiambia kwamba hata asipompata huyo jamaa anaweza kuitoa shehena hiyo hiyo kama kafara kwa maafisa was usalama. Duma alikuwa na bahati ya mtende kumpata huyo jamaa wake, pamoja na afisa wa usalama aliyejuana naye kwa vilembe, akafanikiwa kupitisha shehena zake bila kujua kwamba yake ya urubaini imefika.

Mara tu Dumma alipotua kwenye uwanja wa ndege wa Kamata, Polisi wa Kimataifa walimzingira. Mimweko ya kamera za wanahabari ilitishia kuyapofua macho ya mtumwa huyu ambaye alikuwa sharti auawe kwa kukubali kutumwa. Vikuku viwili vikubwa vilivirembesha viwiko vya mikono yake ambayo aliikabidhi kwa maafisa hawa kama anayekubali kuwajibikia kosa lake. Nchini mwake mwajiri wake alipiga kidogo alipotazama kadhaia hii kwenye runinga. Akasema, "Bloody coward! How could he allow himselft to be caught.?"

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>Maswali:</u>**

(a) Huku ukitoa mifano mitano, onyesha jinsi haki za kibinadamu zilivyokiukwa katika kifungu hiki. [alama 5]

(b) Andika vyanzo vinne vya maovu ya kijamii kwa mujibu wa taarifa. [alama 4]

(c) "Yaliyompata Duma ni mwiba wa kujichoma." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano minne. [alama 4]

(d) Eleza maaza za msamiati ufuatao kulingana na kifungu: [alama 2]

(i) wnye macha ya kipanga ____________________________________________

(ii) Zimegeuka damu inayousukuma moyo wake _______________________________

**2. UFUPISHO - ALAMA 15**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Katika ulimwengu huu tunaoishi wenye hekaheka nyingi, mwanadamu anaendeshwa na maisha mfano wa gurudumu la gari. Kwa watu wenye kufanya kazi katika mazingira ya ofisi ambapo wanaketi mchana kutwa, mazoezi ni muhimu sana. Baadhi ya watu huona fahari wapigapo tai na kuelekea au kutoka kazini kwa gari. Tabia hii ya mwanadamu inamshaulisha kuwa mwili wake ulidhamiriwa kufanya mazoezi ya viungo kwa kutembea au kufanya kazi zenye kuhitaji misuli kupashwa moto. Watu wengi hawana habari kuwa mazoezi yana faida tele kwao.

Wataalamu wa sayansi wamebainisha kuwa watu wanaodhiki miili yao kwa mazoezi ya mara kwa mara huishi zaidi kuliko wasiofanya mazoezi. Watu hawa huwa wamo katika hali nzuri ya afya na wenye nguvu kuliko wale ambao hawaishughulishi miiili yao kwa mazoezi au kazi zinazohitaji nguvu.

Ni dhahiri kwamba mazoezi huchochea kuundwa kwa seli mpya za ubongo. Utafiti wa kisayansi umebainisha kwa sehemu za ubongo zenye kusisimuliwa kwa mazoezi ndizo hutekeleza jukumu la kukumbuka na kujifunza. Bila mazoezi sehemu hizi zitashndwa kukumbuka au kujifunza maarifa mapya. Vile vile, imethibitishwa kwamba watu wanaoshiriki shughuli zenye kuwahitaji kutumia nguvu hutia fora katika mambo yanayowahitaji kukumbuka, kufanya maamuzi, pamoja na kusuluhisha matatizo.

Hali kadhalika, mazoezi huimarisha siha ya binadamu. Mathalani, matatizo ya moyo yanaweza kukabiliwa kwa kufanya mazoezi ya viungo. Kufanya mazoezi mara kwa mara huufanya moyo kuwa imara na kuuwezesha kutekeleza jukumu lake ipasavyo. Ifahamike kwamba moyo wenye siha huweza kupiga kiasi kikubwa cha damu bila ya juhudi kubwa. Hili bila shaka litamkinga binadamu dhidi ya kulemewa na kazi.

Isitoshe, kushiriki mazoezi au shughuli zenye kutumia nguvu mara kwa mara huuweka mwili katika hali nzuri ya kupambana na magonjwa. Utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa shughuli kiasi zinazomhitaji mtu kutumia nguvu, pamoja na upunguzaji wa uzito na uzingatiaji wa lishe bora, huweza kupunguza uwezekano wa hupata ugonjwa wa kisukari kwa baina ya asilimia 50 na 60. Mazoezi hayapunguzi tu shinikizo la damu, bali pia hatari ya kupata kiharusi. Aidha, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kudhibiti uzani wa mwili. Mtu

anapokula kiasi cha chakula kinachozidi mahitaji yake ya kimwili huweza kujinenepea na kushindwa kutekeleza majukumu ya kimsingi. Mazoezi husaidia kuzichoma kalori zisizohitajika mwilini. Hatua hii, licha ya kusaidia kupunguza uzani, huvisisimua viungo vya mwili. Matokeo ya haya ni utendakazi wa hali ya juu bila kuchoka. Vilevile mwili unaofanya mazoezi haudorori. Umbo la mtu anayefanya mazoezi hupendeza.

Juu ya hayo, kufanya mazoezi mara kwa mara husaidia kujenga misuli yenye nguvu. Misuli inapokuwa na nguvu tunaweza kulifanya jambo kwa muda mrefu bila kuchoka. Mbali na misuli kuimarika, mazoezi na shughuli zinazohitaji utumiaji nguvu husukuma hewa na virutubisho kwenye viungo mahususi vya mwili na kuvisaidia kufanya kazi vyema zaidi.

Hali kadhalika, mazoezi husaidia kujenga mifupa. Kadiri binadamu anavyoshiriki katika shughuli kama vile kuruka, ndivyo anavyoiimarisha mifupa yake. Shughuli ya aina hii huipa mifupa uzito ambao unaiweshesha kukua na kujengeka ikiwa na nguvu. Mazoezi pia hukawiza kudhoofika kwa mifupa.

Kunyooshanyoosha viungo nako huchangia kufanya mwili kuwa imara wenye kunyumbuka. Hali hii ya mwili hupunguza uwezekano wa kupata majeraha. Mwili usionyumbua hufanya mtu ashindwe kutekeleza hata shughuli zinazomhitaji kutumia nguvu. Si ibra kupata kwamba kuitekeleza shughuli ndogo tu humfanya mtu kupata maumivu.

Utulivu wa akili nao huweza kupatikana kwa kufanya mazoezi. Imebainishwa kwamba kufanya mazoezi kwa angalau dakika thelathini kwa muda wa baina ya siku tatu na tano kwa wiki hupunguza kwa kiasi kikubwa, dalili za unyong'onyevu. Na je, wajua kwamba kufanya mazoezi husaidia kupata usingizi? Mazoezi ni mfano wa bembea inayokutuliza na kukupa usingizi.

Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa. Nao mwili wa binadamu, kama mgomba, unahitaji kushirikishwa katika mazoezi ili kuuwezesha kuwa na hamu ya kutenda kazi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(a) Kwa kurejelea aya tano za kwanza, eleza matatizo ya kiafya yanayoweza kupatikana kwa kutofanya mazoezi. (maneno 100) (alama 9, 1 ya mtiririko)
Matayarisho
Nakala Safi

(b) Fupisha ujumbe wa aya tano za mwisho kwa maneno 80. [alama 6, 1 ya mtiririko]
Matayarisho
Nakala Safi

3. MATUMIZI YA LUGHA - ALAMA 40

(a) Linganisha sifa za sauti zifuatazo. [alama 2]
/k/ na /g/
/v/ na /dh/

(b) Andika maneno mawili tofauti yenye sauti mwambatano tofauti za ufizi. [alama 1]

(c) (i) Shadda ni nini? [alama 2]
(ii) Onyesha palipo na shadda katika neno lifuatalo: Muktadha. [alama 1]

(d) Eleza maana mbili za sentensi: Waite wale wale. [alama 2]

(e) Tumia kiunganishi cha masharti katika sentensi. [alama 2]

(f) Onyesha miundo miwili tofauti ya nomino katika ngeli ya U/ZI. [alama 1]

(g) Nukta pacha hutumiwa kuonyesha maneno ya msemaji katika tamthilia. Onyesha matumizi mengine mawili tofauti katika sentensi . [alama 2]

(h) Tambua aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo:
Mzee huenda anacheza kamari. [alama 2]

(i) Tunga sentensi katika wakati ujao hali ya kuendelea. [alama 2]

(j) Andika kwa usemi wa taarifa:
"Uchezeamo mna hatari," mama alinionya. [alama 3]

(k) Kanusha sentensi ifuatayo: Akisahau kuniamsha nitachelewa. [alama 1]

(l) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi ya kiambishi JI. [alama 2]

(m) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi:
Mwizi aliyeingia dukanai ameshikwa. [alama 2]
(n) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya vitate: ndoa na doa. [alama 2]
(o) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali:
Vililetwa nyumbani mapema. [alama 3]
(p) Tambua aina ya vishazi katika tungo lifuatalo.
Polisi wamemkamata mbakaji aliyehusika na ubakaji wa juzi. [alama 2]
(q) Nyambua vitenzi vifuatavyo kulingana na kauli zilizo kwenye mabano: [alama 2]
(i) fa (tendesha) ________________________________________________
(ii) La (tendeka) ________________________________________________
(r) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo.
Wazee na vijana walikuwa mkutanoni jana. [alama 1]
(s) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo:
Mtoto alipewa maziwa na mama kwa kikombe. [alama 3]
(t) Chakula ni kwa mlo, barabara ni kwa ____________________________ na afya ni kwa [alama 2]

**4. ISIMU JAMII - ALAMA 10**

(a) Kwa kutumia mifano, eleza sifa mbili mbili za sajili zifuatazo: [alama 6]
(i) Sokoni
(ii) Hospitalini
(iii) Uwanjani
(b) Taja na ueleze njia nne zinazoweza kutumiwa na serikali kuimarisha Kiswahili ikiwa lugha rasmi. [alama 4]

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MECS I**
**102/3**
**KARATASI YA 3**
**SEHEMU A: USHAIRI**

**1. Lazima**
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

**Nimeona**

Nimeona,milima na mabonde,misitu na nyika
Nimeona,majani na umande,uliotandazika
Nimeona,mkulima yuwenda shambani

Nimeona,uwanda na magugu,yalomkabili
Nimeona,wajibu na vurugu,'wiano mkali
Niimeona,mkulima akiwa tayari

Nimeona,kwa ari na juhudi,anatupa jembe
Nimeona,kakaza ukaidi,kwa nguvu achimbe
Nimeona,mkulima akiwa kazini

Nimeona,kijua kinawaka,kama jahanamu!
Nimeona,jembe lainuka,linapohujumu
Nimeona,mkulima akiwa mbioni

Nimeona,mvua yamiminika,naye hatohisi
Nimeona,kwa kani anatimka,bila wasiwasi
Nimeona,mkulima akiwa kazini

Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao
Na sioni, hadhiye kutukuka, ila kilio

Kwa nini? Nauliza mkulima: kwani?

a) Eleza ujumbe muhimu katika shairi hili. (Alama 4)
b) Fafanua arudhi zilizotumika kusarifu ubeti wa tatu. (Alama 4)
c) Onyesha uhuru wa mshairi shairini. (Alama 2)
d) Eleza mtindo uliotumika katika shairi hili. (Alama 5)
e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (Alama 3)
f) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 2)

**SEHEMU B:TAMTHILIA**

**Kigogo**: *Pauline Kea*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. ”Tunaangamia. Tunahitaji mtetezi anayeongozwa na hekima sio ubinafsi.”
   a) Onyesha mchango wa msemaji katika kutetea haki za wanasagamoyo. (Alama 10)
   b) Thibitisha kuwa kiongozi aliyekuwapo hakuongozwa na hekima. (Alama 10)
3. i) ”Mmetamauka nyinyi…Sagamoyo ni pazuri zaidi tangu soko lilipofungwa.”
   Jadili matokeo ya kufungwa kwa soko la Chapakazi. (Alama 12)
   ii) Onyesha vile mwandishi wa tamthilia ya Kigogo alivyotumia mbinu ya majazi kufanikisha kazi yake. (Alama 8)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: RIWAYA**

Chozi La Heri: *Assumpta Matei*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4 i). ”…mwanangu,walimwengu ni hasidi.Ndio walionisababishia uwele.Ishi mwanangu,utawaona.”
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
   b) Kwa kurejelea riwaya nzima,thibitisha kuwa walimwengu ni hasidi. (Alama10)
   ii) ”Usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu.Kwa hakika tunaweza kusema kuwa…”
   Fafanua mambo muhimu yaliyogusiwa katika hotuba hii. (Alama 6)

5. ”…haifai kucheza na uwezo wa vijana,wao ni kama nanga.Huweza kuzamisha na kuiongoa merikebu.Inasikitisha kwamba badala ya kuiongoa jahazi letu wameligongesha mwamba bila kujua.”
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
   b) Eleza mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo. (Alama 3)
   c) Anayeambiwa maneno haya ana umuhimu gani riwayani? (Alama 5)
   d) Kwa kurejelea matukio mbalimbali onyesha vile vijana wanavyoizamisha merikebu. (Alama 8)

**SEHEMU D:HADITHI FUPI**

Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine

*Jibu swali la 6 au la 7*

**Shibe Inatumaliza**: *Salma Omar Hamad*

6 i) ”lakini nakwambia tena,kula kunatumaliza.”
   Kwa kurejelea hadithi husika thibitisha ukweli wa kauli hii. (Alama 12)

**Mwalimu Msataafu**: *Dumu Kayanda*

ii) “Ajitose afilie mbali.Kutwa nzima siku hiyo kijiji kizima kilikuwa na sulubu kubwa ya kumzuia…”
   Jadili maudhui **manane** yanayoendelezwa na mrejelewa. (Alama 8)

**Ndoto ya Mashaka**: *Ali Abdulla Ali*

7. i) ”Ngoja ngoja huumiza matumbo! Nifanyeje lakini? Nimengoja na kungoja tangu na tama mpaka kutamauka.”
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (Alama 3)
   b) Eleza mbinu nne za lugha katika dondoo hili. (Alama 4)

c) Jadili mambo yaliyochangia mrejelewa kutamauka. (Alama 7)
d) Ukirejelea hadithi ya *Mame Bakari* fafanua maudhui ya udhalimu. (Alama 6)

**SEHEMU E:** FASIHI SIMULIZI

8. Ajenga ingawa hana mikono-ndege
 a Tambua aina ya kitendawili hiki. (Alama 1)
 b) Eleza tamathali iliyotumika katika kitendawili hiki. (Alama 2)
 c) Fafanua sifa nyingine **tano** za viitendawili. (Alama 5)
 d) Licha ya kuwa na umuhimu wake,miviga ina hasara zake.Zifafanue (Alama 5)
 e) Onyesha vile jamii ya sasa inavyoendeleza tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi. (Alama 7)

**MECS I**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**KARATASI YA KWANZA/INSHA**

**1.**

- Haya ni mahojiano
- Azingatie mtindo wa tamthilia k.m

Waziri:
Mwandishi 1:

- Ahusishe watu wane

Waziri
Mwandishi 1
Mwandishi 11
Mwandishi iii

- Azingatie mada

i. Hali ya usalama nchini - ni nzuri au ni baya
ii. Visa vya uhalifu / ukiukaji wa sheria – mauaji
 – Utekaji nyara
 – Visa vya kigaidi
 – Ajali barabarani
 – Uporaji wa pesa za umma.
iii. Hatua ambazo zimechukuliwa na:
 a) Polisi – kuwakamata wahusika
  Kuwashtaki na kuwahukumu.
 b) Umma – kushirikiana na polisi kuwafichua wahalifu
 c) Vyombo vya habari – kuelimisha umma kuhusu uhusiano mwema.
iv) Mipango ya baadaye
 – Wahusika wote washiriki kikamilifu.
 – Mwanafunzi asipozingatia sura ya mahonjiano (muundo) atolewe alama nne

2. jinsi ya kukuza umoja wa kitaifa
– kuhimiza matumizi ya lugha ya kitaifa
– kuhimiza uzalendo watu wajitambue kama wakenya.
– ndoa za maingiliano kati ya makabila tofauti
– shule ziwe za kitaifa ili mwanafunzi awe na uhuru wa kusomea kokote nchini.
– kuzuru sehemu tofauti nchini
– ugawi sawa wa raslimali za umma
– katiba
– michezo ya riadha.
– tamasha za muziki
– viongozi kuhubiri umoja

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- kukuza demokrasia
- kuheshimu haki za binadamu
- kumiliki mali kokote nchini.

3. Mla cha mwenzake na chake huliwa.
   Maana. Mtu anayekula vitu vya wenzake na vyake huliwa.
   Mtu anayewadhulumu wengine naye huja kudhulumiwana kuteswa
   Kisa kisipolenga maana ya methali atuzwe $^{02/}{}_{20}$
   Mwanafunzi azingatie pande zote mbili za methali.
   Akishughulikia upande mmoja atunzwe . x 10
4. 
- Hii ni insha ya mdokezo
- Mwalimu ahakiki utungo wa mwanafunzi
- Utungo uoane na mdokezo aliopewa
- Akibadili mdokezo atakuwa na udhaifu wa kimtindo.

**<u>Urefu</u>**
Maneno 375 + insha kamili $^{x/}{}_{20}$
Maneno kati ya 275 -374 robo tatu $^{x/}{}_{15}$
Maneno ya kati 175 – 274 nusu $^{x/}{}_{10}$
Maneno kati ya 1 – 174 robo $^{x/}{}_{5}$

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MECS**
**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA PILI</u>**

1. <u>UFAHAMU</u>
   i) **A**.
   ii) Kutengwa na mazingira ya nyumbani.
   iii) Kunyanyaswa mali na jamaa za wazazi.
   iv) Kufanyishwa kazi angali mtoto.
   v) Kulazimishwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya.
   vi) Kusababishiwa uraibu wa dawa.
   vii) Kusumbuliwa kisaikolojia- uoga, wasiwasi.
   viii) Kuhatarishiwa afya – kuzimeza dawa ili kuzisafirisha ughaibuni.
   ix) Kunyimwa malezi bora – anatolewa nyumbani akiwa mchanga –kabla ya ubwabwa wa shingo kumtoka.
   x) Kuhusishwa katika kutoa hongo. Zozote (5*1) al.5

**B.**
- Magonjwa – wazazi wa Duma wanatumia pesa nyingi kwenye matibabu –wanamwacha mnyonge hivyo kuwa windo la uraibu na ulanguzi wa dawa.
- Uyatima- Duma anakosa walezi hivyo kuinglia uraibu wa dawa.
- Tamaa/ ulafi- jamaa za Duma wanampoka mali kutokana na tama.Duma anaingilia ulanguzi wa dawa kutokana na tamaa.
- Ufisadi- maafisa wa usalama wanapokea hongo na kuendeleza ulanguzi wa dawa zaidi.
- Uraibu wa dawa za kulevya unamfanya Duma kutojidhibiti, anaendelea kuzitumia na kulangua kwa kupata nguvu mpya. (zozote 4*1 ) al.4

**C.**
- Duma anakubali kuziuza dawa shuleni na sokoni.
- Duma anajaribisha kutumia dawa hadi anakuwa mraibu sugu.
- Anakubali kumeza dawa ili kuzisafirisha.
- Badala ya kuwajibika kubadilika, anajiona kuwa mtendwa.

- Duma anahalalisha matendo yake hivyo kutoyarekebisha.
- Duma anawahonga polisi ili aachiliwe hivyo kudidimia zaidi katika maovu.
- Anashirikiana na mwajiri wake ili kuzua mbinu mpya kuendeleza uhalifu.Anakosa tahadhari na kuishia kukamatwa.
- Tamaa inamfanya asing'atuke kutoka kwenye uhalifu.

Zozote (4*1) al.4

**D**.

(i) Wenye makini / waangalifu / walio macho kupambana na uhalifu.
(ii) Ndizo zinazomwendeshea maisha / amekuwa mraibu sugu / ndizo zinazompa msukumo wa kuendelea na uhalifu. (alama 2)

**2.** **UFUPISHO**

**a**) Matatizo ya kiafya.

1. Sehemu za ubongo kushindwa kukumbuka au kujifunza maarifa mapya.
2. Kupatwa na ugonjwa wa Kisukari.
3. Kupatwa na shinikizo la damu.
4. Kupata kiharusi.
5. Kutodhibiti uzani wa mwili.
6. Kutopunguza uzani na kunenepa kupita kiasi.
7. Kuchoka na kutotenda kazi vizuri.
8. Kudorora kwa mwili.
9. Kutopendeza kwa umbo la mwili. Zozote 8,mtiririko 1

**b)**

1. Mazoezi hujenga misuli yenye nguvu.
2. Hewa husukumwa pamoja na virutubisho kwenye viungo vya mwili na kuvisaidia kufanya kazi vyema.
3. Husaidia kujenga mifupa yenye nguvu.
4. Pia hukawiza kudhoofika kwa mifupa.
5. Huchangia kufanya mwili kuwa imara bila kupata maumivu au majeraha.
6. Kupata utulivu wa akili. Mtu hupata usingizi wa kutosha.

Zozote 5,mtiririko 1

3. MATUMIZI YA LUGHA

**a**. (i) /k/ na /g/ - vyote ni vipasuo, hutamkiwa kwenye kaakaa laini.
(ii) /v/ na /dh/ - vikwamizo,ghuna. (alama 2)

**b**. Twika, twende ndwele,twiga,kwanza (kadiria kazi ya mtahiniwa) (alama 1)

**c**. (i) Shadda ni nini? Mkazo unaotokea kwenye silabi fulani katika neno wakati wa mazungumzo ili neno hilo liweze kutokeza maana yake halisi. (alama 2)
(ii) Muk'tadha. (alama 1)

**d**. (i) Watu Fulani wanaashiriwa wale chakula.
(ii) Msisitizo.
(iii) Kitendo cha viumbe Fulani kuvamia na kula wengine. (alama 2)

**e**. Ikiwa, iwapo, ukitaka, maadam,kama (kadiria kazi ya mwanafunzi). Mfano:Biashara yako itastawi iwapo utakubali ushauri wa wataalam. (alama 2)

**f**. Uzi - Nyuzi
Waraka - Nyaraka
Unywele - Nywele
Upanga- Panga (alama 1)

**g**. (i) Kuonyesha orodha.
Nilipokwenda sokoni nilinunua matunda: ndizi,mapera,machungwa na maembe.
(ii) Kutenganisha saa.
10:30:05
06:20:19 (alama 2)
(iii) Kutanguliza mifano inayoorodheshwa kutumia nambari. Kwa mfano:
(iv) Kutanguliza kifungu kirefu ambacho kimenukuliwa katika kitabu.
Mfano.Alitangulia kasha akaanza kusoma:

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**h.** Huenda – kitenzi kisaidizi (TS)
Anacheza –kitenzi kikuu (T) (alama 2)

**i.** Mwanafunzi atakuwa anasoma darasani.
Mkulima atakuwa analima shambani.
Mwalimu atakuwa akifundisha wanafunzi.
(kadiria na ki ) (alama 2)

**j.** Mama alinionya kuwa nilimokuwa nikichezea mlikuwa na hatari. (alama 3)

**k.** Asiposahau kuniamsha sitachelewa. (alama 1)

**l.** Matumizi ya ji.(Mtahiniwa atunge sentensi)
(i) Urejeshi katika nafsi zote tatu.
Nilijiumiza bure. (alama 2)
(ii) Hali ya ukubwa.
Mtu – jitu.
(iii) Uundaji wa nomino.
Msomaji
Usomaji
(iv) Nomino katika ngeli ya LI-YA .
Jino,jiko

**m.** Vijizi vilivyoingia vijichakani vimeshikwa. (alama 2)

**n.** Ndoa yake hamisi iliingia doa. (alama 2)
(kadiria kazi ya mtahiniwa)

**o.**

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | KT | | |
| Ø | T | RE | KE |
| | | E | E |
| | Vililetwa | Nyumbani | Mapema |

√ √ √

(alama 3)

**p.** Kishazi huru –Polisi wamemkamata mbakaji.
Kishazi tegemezi – aliyehusika na ubakaji wa juzi. (alama 2)

**q.** Fa – fisha
La – lika (alama 1)

**r.** Virai
(i) Kirai nomino – Wazee na vijana.
(ii) Kirai elezi – Mkutanoni jana. (alama 2)

**s.** Shamirisho kipozi –Maziwa
Shamirisho kitondo – Mtoto
Shamirisho ala – Kikombe (alama 3)

**t.** (i) Barabara – baraste au sawasawa (kadiria)
(ii) Afya – siha, ahueni,rai (kadiria) (alama 2)

4. ISIMU JAMII

**(a)** Sifa mbilimbili
(i) Sokoni (alama 2)
- Maelezo ya ubora wa bidhaa.
- Kupiga chuku.
- Ina ushawishi
- Hupuuza kanuni za sarufi
- Kuchanganya ndimi
- Hutumia lugha ya mkato
- Hujaa porojo
- Hutumia lugha nyepesi
- Uradidi
- Kauli fupi

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(ii) Hospitalini (alama 2)

- Hutumia lugha maalum – kitaaluma
- Huchanganya ndimi
- Kubadili msimbo
- Kudadisi
- Kutohoa
- Lugha ya usiri (madaktari)
- Majina ya vyeo –DKT
- Lugha ya hisia

(iii) Uwanjani (alama 2)

- Msamiati wa michezo
- Hupuuza kanuni za kisarufi
- Hutumia utohozi
- Hutumia lugha ya mkato
- Uradidi wa maneno
- Hutumia misimu
- Lugha ya taharuki
- Majisifu
- Majina ya wachezaji hutajwa (Taja $1/2$ Maelezo $1/2$ )

**b**. Kiswahili kama lugha rasmi

- Kipewe jukumu kuendesha shughuli zote katika ofisi za kiserikali.
- Kipewe hadhi kufundisha toka shule za msingi hadi vyuo vikuu.
- Kipewe hadhi kutumika katika hati zote za kiserikali.
- Kutoa mafunzo Kwa maafisa wa kiserikali ili kukielewa Kiswahili.
- Machapisho yaongezwe kwa wingi kutumia lugha ya Kiswahili.
- Kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa Kiswahili kama lugha. Zozote nne (4*1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJAGATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MUHULA WA PILI-DEC 2020**
**102/1**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**

**MASWALI**

1. Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo.
   Andika barua ya kuomba nafasi hii na uiambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.

2. Jukumu la kuzuia msambao wa virusi vya korona ni la mtu binafsi. Jadili.

3. Andika insha itakyothibitisha ukweli wa methali
   Mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe.

4. Anza kwa.
   Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa lakini chunga mabadiliko hayo yasikuzuzue….

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJAGATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MUHULA WA PILI-2020**
**KARATASI 102/2**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

**1. UFAHAMU (Alama 15)**

Huku ulimwengu unapoingia ya katika teknologia ya tarakilishi na sera ya utandaridhi, ukweli wa mambo ni kuwa akina mama wamezinduka. Suala la usawa wa kijinsia limeanza kushamiri kote duniani na ole wake mwanamume yeyote ambaye hajawa tayari kutembea na majira. Lakini hebu tuchunguze jambo hili kwa makini zaidi.

Usawa wa jinsia ni nini? Usawa wa kijinsia ni usawa wa binadamu wote; wawe wake au waume. Usawa huu unapaswa kudhihirika katika kugawa nafasi za kazi, utoaji wa elimu, nafasi za uongozi na Nyanja zinginezo zozote za maisha.

Ubaguzi wa aina yoyote ile hasa dhidi ya mwanamke ni jambo linalokabiliwa na vita vikali sana ulimwenguni kote.

Dahari na dahari, hasa katika jamii za kiafrika kumekuwa na imani isiyotingizika kuwa mwanamke ni kiumbe duni akilinganishwa na mwanaume. Kwa hivyo mwanamke amekuwa akifanyiwa kila aina ya dhuluma ikiwepo kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kunyimwa haki zake, kunyimwa heshima na mambo kama hayo, lakini je, ni kweli kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyefaa kutendewa haki?

Tukichunguza jamii kwa makini tunaweza kuona mara moja kuwa hivyo ni imani potovu isiyo na mashiko yoyote. Ukimulika familia yoyote ile iliyopiga hatua kimaendeleo, uwezekano mkubwa ni kuwa mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa. Mume anamthamini mke wake na <u>hadiriki</u> kufanya maamuzi muhimu yanayoweza kuathiri maendeleo ya familia bila kumhusisha mke. Mume kama huyo huketi na mkewe, wakishauriana na kufikia uamuzi bora.

Tukitoka katika muktadha wa kifamilia na kumulika ulimwengu wa kazi iwe ni katika afisi za serikali au kwenye makampuni binafsi, ukwerli ni kwamba kiongozi yeyote yule aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke nyumbani ambaye wanashauiriana kila uchao kuhusu kazi anayofanya hata kama mke hafanyi kazi mahali pale. Hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda asiyapate kwingineko kokote hata katika vitabu vya kupigiwa mifano. Hii ni mojawapo ya sababu ambayo huwafanya viongozi wa nchi mbalimbali kupenda sana kuwatambulisha wake na familia zao waziwazi kwa vile wanajua kuwa jamii inathamini sana msingi wa jamii. Kiongozi ambaye hana mke au familia au yule ambaye hana mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata

kama ni kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma.

Tukirudi nyuma kidogo na kupiga darubini mataifa ya mbali, tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri walio uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake mashuhuri waliotoa uongozini ambao hadi wa leo unapigiwa mfano. Wanawake hao walisimamia mojawapo ya mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa Zaidi duniani. Ingawa wengi wao sasa wameng'atuka, uongozi wao bado unakumbukwa hata baada ya miaka mingi ya wao kuamua kupumzika ,mfano ni kama :Bi Bandranaike wa Sri lanka, Golda Meir wa Israel na wengine wengi katika mataifa kama Indonesia, Ufilipino, Bangladesh, Pakistani na kwingineko.

Katika kufikia tamati, tunapozungumza kuhusu jinsia, hatuna budi kugusia kitafsili masuala nyeti. Kwanza,imani ya kushikilia kikiki tamaduni zisizofaa, ni jambo linalofaa kuchunguzwa kwa makini. Kwa mfano, kuna badhi ya jamii ambazo humlazimu mke kurithiwa baada ya kifo cha mumewe. Vile vile baadhi ya jamiii za kiafrika zinanshikilia kuwa mwanamke hana haki ya kurithi. Kutokana na Imani hii, wanawake wengi huishi maisha ya taabu baada ya kutengana na waume zao kwa vile hawana haki ya kurithi chochote kutoka kwa wazazi wao hata kama wazazi hao wana mali nyingi kupindukia. Mali ya wazazi ni haki ya watoto wa kiume wala si watoto wa kike! Hili ni jambo la kusikitisha mno.

Isitoshe, wanawake hukumbukwa na kizingiti kingine wanapojaribu kumiliki mali ya waumezao baada ya waume hao kukata kamba .sababu ni kuwa,baada ya hao wenda zao kuwekwa kaburini, vita vya umiliki wa mali huanza mara moja na mwishowe yule mke maskini hujikuta hana hata mahali pa kulala sembuse mali waliyochuma na mali yake yote kunyakuliwa na aila ya mumewe . Jambo hili linaonyesha namna tulivyoachwa nyuma na uhalisia wa mambo. Ni lazima jamii izuinduke na itoke kwenye kiza hiki chenye maki nzito.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a. Ina maana gani kusema kuwa wanaume hawana budi "kutembea na majira" (alama 2)

b. Kabla ya uzinduzi huu kuhusu usawa wa jinsia, wanawake wamekuwa wakitendewa dhuluma za kila aina. Taja tatu. (alama 3)

c. Je, ni kwa nini viongozi wengi hupenda kujitambulisha na familia zao? (alama 2)

d. Je, unaamini kuwa hisi na mawaidha anayatoa mke wa mume wake ni tunu na huenda yasipatikane kwingineko? Fafanua (alama 2)

e. Je, licha ya kunyimwa haki yake ya kujiamulia, ni matatizi yapi mengine yanayoweza kumkumba mke anayelazimishwa kurithiwa? (alama 3)

f. Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika hali muktadha. (alama 3)
Kushamiri
Hulka
Azma

**2. MUHTASARI**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Idadi kubwa ya wanafunzi huingiwa na wasiwasi wakaribiapo kufanya mtihani kwa sababu mbalimbali, kubwa likiwa ni hofu kwa jinsi ambavyo watafanya katika mtihani huo. Asilani mambo hayafai kuwa hivyo. Wataalamu wa masuala ya saikolojia na wale wa elimu wanashauri kuwa mtahiniwa anafaaa kupata muda mwingi wa mapumziko wakati anapokaribia kufanya mtihani ili aweze kuituliza akili asije akapatwa na mzongo wa akili.

Moja katika mashauri ni kuwa mtahiniwa anafaa kupata usingizi wa kutosha wakati akijiandaa na pia wakati akifanya mtihani. Hii ni kwa sababu mtihani wa mwisho si tofauti na mitihani mingine ambayo mtahiniwa amekuwa akifanya, pamoja na kuwa ni maswali ya jumla tu kutoka viwango vyote vya masomo. Hivyo basi, mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kudurusu na kufanya majaribio mbalimbali ya mtihani pamoja na kujikumbusha yale aliyofunzwa na mwalimu wake. Wale asimdunishe au kumdharau mwalimu hata kama stadi zake za kufundisha kazikumsisimua – alikupa kito cha thamani kitakachokufaa kama silaha wakati wa mtihani.

Mtihani unapokaribia, mtahiniwa anafaa kuwa amekwisha kutambua udhaifu wake na kutia bidii kuudhibiti kupitia udurusu, mijadala na mashauriano. Kumbuka kuwa bidii haiui ila hulipa. Hivyo basi, kila unaposhirikisha bidii na ujasiri wa wako na kuimarisha uelewe wako wa somo, na hatimaye ukaboresha matokeo katika somo hilo. Vilevile, kujadili au kufafanua mada unayoielewa vyema kwa m wenzio aiyeielewa kutakuwezesha kuielewa hata Zaidi na hivyo kuimarisha uwezo wako wa kuzoa alama nyingi katika mtihani endapo swali litatoka katika mada hiyo.

Pamoja na hayo, mtahiniwa anafaa kujihadhari na majuto ya kufanya kile ambacho hakupaswa kufanya. Anaweza kuhakikisha hili kwa kuyapitia maswali kwa makini Zaidi, na kuyatafakaria, kuyapangia na kuaandikia majibu sawasawa kasha kuyasoma tena majibu yake ili kuwa na uhakika kwamba hajapotoka.

Ikiwezekana (kwa sababu ya tofauti za kimapato na uwezo wa wazazi au walezi) mtahhiniwa anafaa kula visuri kabla kuenda kufanya mtihani. Vilevile, anapaswa kufika katika chumba cha mtihani kwa wakati unaofaa – mapema kabla ya muda wa kuanza kwa mtihani – na ahakikishe amebeba kila kifaa atakachokihitaji katika mtihani huo.

Ikiwa utashindwa kujibu swali Fulani, usipotezee muda mwingi. Baadala yake, enelea na swali linalofuatia kasha ulirejelee swali lile lililokutatiza baadaye ukishamaliza maswali yale mengine. Usipoteze muda kutafuta jibu ambalo huna kwa wakati huo. Juu ya yote, usidhubutu kuifanya hila katika mtihani kwa kuwa kitendo kama hicho kitasababisha matokeo yako kufutiliwa mbali, nayo bidii yako ya miaka mine itakuwa imeishia gizani, ukasalia kujuta.

**Maswali.**

a) Tumia maneno 60 kueleza ujumbe ulio katika aya mbili za mwanzo. (alama 6)

**Nakala chafu**

**Jibu**

b) Mwandishi anatoa ushauri gani kwa mtahiniwa katika aya ya tatu hadi ya mwisho? Eleza kwa maneno 100 (alama 9)

**Nakala chafu**

Jibu

**SEHEMU C - MATUMIZI YA LUGHA.**

a) Eleza ufauti ya kimsingi iliyopo kati ya irabu na konsonanti. (ala2)

b) Taja sifa tatu bainifu za irabu /O/ (ala 3)

c) Andika maneno yenye muundo ufuatao
  i) KKKIKI
  ii) KKIKI (ala2)

d) Andika tungo ya neno moja yenye viambishi vifuatavyo.
  i) Nafsi
  ii) Njeo
  iii) Kirejeshi
  iv) Shamirisho
  v) Mzizi
  vi) Kauli ya kufanyiza
  vii) Kiishio (ala3)

e) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana. (ala2)
  i) –la
  ii) – nywa

f) Andika sentensi ifuayo kulingana na maagizo. (ala2)

**Maagizo**

Mhalifu <u>alisamehewa</u> kwa sababu <u>alinyenyekea</u> .

Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino.

g) Andika kwa wingi

Kelele ya amchaye Mungu ni baraka. (ala1)

h) Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii

Utazawadiwa ukicheza vizuri. (ala2)

i) Tofautisha matumizi yapo katika sentensi hizi. (ala2)
  1. Alipomwona alimhoji.
  2. Amwonapo humhoji

j) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari. (ala2)

Ubaguzi <u>wa kijinsia</u> umekashifiwa mno na <u>viongozi wenye msimamo thabiti mno</u>.

k) Unda nomino kutokana na vitenzi (ala2)
  1. Jaribu
  2. Chuma

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

l) Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi
Wageni na wenyeji walikimbiliana (ala 2)

m) Andika katika msemo wa taarifa. (ala3)
"Nitakuarifu nikimwona" Maria alisema

n) Eleza maana mbili za sentensi (ala2)
Tuliitwa na Juma

o) Tumia "0" rejeshi katika sentensi ifuatayo
Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe. (ala 2)

p) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika tena sentensi ifuatayo.
Ukuta umemwuumiza mvulana alipokuwa akiuparaga. (ala3)

q) Changanua sentensi kwa njia ya jedwali.
Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri. (ala4)

**ISIMUJAMII**

Mtu 1: Wewe njoo hapa (kwa sauti kubwa) fanya upesi.
Mtu II : (anakimbia mbio) Naja Sir
Mtu I : (anamtazama) unajifanya mwelevu?
Mu II : Hapana Sir……eh…..afande
Mtu I : Jina
Mtu II : Samwel Kioko
Mtu I : (Huku akiandika) Lete kitambulisho
Mtu II : Sina hapa sir
Mtu I : Huna kitambulisho? Utafanyiwa booking vipi?
Mtu II : Naomba
Mtu I : Naomba ! naomba! Unaomba nini? Wazururaji kama nyinyi tunawajua. Mnajifanya hamjui kuna curfew. Mnajiponza, "zerikali saidia". Usiniharibie muda wangu (akiashiria) ingia ndani! Utakuwa mgeni wetu leo. Tutakukarimu chakula cha chumba.(anamsukuma ndani)

a) Bainisha sajili ya makala haya. (ala2)
b) Eleza sifa nne za sajili kwa kurejelea makala haya.(ala 8) __

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA GATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MUHULA WA PILI –DEC 2020**
**KARATASI YA TATU – 102/3**
**FASIHI**

**1. *FASIHI SIMULIZI: SWALI LA LAZIMA***

a) *Miviga ni nini?* *Al.2*
b) *Eleza sifa tano za miviga.* *Al.5*
c) *Fafanua hasara tatu za miviga.* *Al.3*
d) *Eleza changamoto tano ambazo mtafiti hukabiliana nazo anapokusanya data ya fasihi simulizi.* *Al.5*
e) *Eleza majukumu ya wimbo katika hadithi.* *Al.5*

***TAMTHLIA: KIGOGO***

**2. *Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!***

***a) Eleza muktadha wa dondoo hili.*** ***Al.4***
***b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki.*** ***Al.4***
***c) Eleza matatizo yanayokumba safari inayorejelewa.*** ***Al.12***

3. ***Tamthlia ya kigogo inazungumza kuhusu hali halisi katika mataifa mengi ya kiafrika. Jadili.*** ***Al.20***

**4. *RIWAYA: CHOZI LA HERI***

***"Alikumbuka jinsi rafiki yake……..alivyofishwa kwa njia hii. Akili yake ilimtambia kisa chenyewe kana kwamba inataka kumwonya (uk.120)***

a) *Fafanua muktadha wa dondoo hili.* *Al.4*
b) *Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili.* *Al.4*
c) *Tathmini nafasi ya anayelengwa na kauli hii katika kuijenga riwaya hii.* *Al.12*

5. a) *Fafanua namna mbinu ya majazi ilivyotumiwa katika riwaya.* *Al.10*
b) *Jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii ukirejelea riwaya ya Chozi la Heri.* *Al.10*

**6. *HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA***

a) *Eleza ufaafu wa anwani mapenzi ya kifuaurongo kwa kurejelea mhusika Penina.* *Al.10*
b) *Eleza nafasi ya elimu katika maisha ya wanajamii ukirejelea hadithi: Mtihani wa maisha.* *Al.10*

7. a) ***Mame Bakari***

***"Una nini? Umeshtuka mwanangu? Unaogopa? Uaogopa nini?***

a) *Weka dondoo hili katika muktadha wake.* *Al.4*
***b) Eleza sifa za mrejelewa.*** ***Al.6***
***c) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo.*** ***Al.2***
***d) Eleza umuhimu wa msemaji.*** ***Al.4***
***e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki.*** ***Al.1***
***f) Fafanua maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea hadithi nzima.*** ***Al.3***

**8. USHAIRI**

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupliiki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo h adaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Manchangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mwenyewe!

**MASWALI**

a) ***Eleza dhamira ya shairi hili.*** ***Al.2***
b) ***Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kusisitiza ujumbe wake.*** ***Al.2***
c) ***Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi.*** ***Al.4***
d) ***Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi.*** ***Al.4***
e) ***Bainisha toni ya shairi hili.*** ***Al.2***
f) ***Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili.*** Al.4
g) ***Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.*** ***Al.2***
   i) Mstahiki
   ii) Hupuliki

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA GATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**KARATASI YA KWANZA**
**KISWAHILI 102/1**

**1. LAZIMA**

a) Muundo wa barua rasmi – yenye anwani mbili
   i) Ina anwani ya kwanza: Mwandishi. (Mtahiniwa) abuni anwani yake – iwe wima Al.1
   ii) Tarehe : Chini ya anwani ya kwanza Al. ½
   iii) Anwani ya pili: Mwandikiwa – Mkurugenzi wa shirika la uchapishaji. Al.1
   iv) Maamkizi : kwa Bw/Bi Al. ½
   v) Mtajo/mada: KUH/MINT – KUOMBA KAZI YA UHARIRI Al.2
   vi) Mwili wa barua
      a) Utangulizi
      b) Maelezo ya kibinafsi kwa ufupi
      c) Ufaafu wake katika hiyo nafasi
      d) Maelekezo ya wasifu kazi kwa maelezo zaidi
      Al.4
   vii) Hitimisho: sahihi ya mwandishi, jina na cheo kama anacho. Al.1

b) Wasifu kazi/wasifu Taala

i) Habari za kinafsi – Jina
- Jinsia
- Umri/Tarehe ya kuzaliwa
- Ndoa/Hadhi
- Answani – Barua pepe/nambari ya simu
- Dini
- Lugha azijuazo.

Al.2

ii) Elimu – Orodha ya shule – aanze kwa kiwango cha juu zaidi.
- Ataje cheti alichohitimu. Al.2

iii) Tajriba – Ujuzi wa kikazi/maarifa. Al.2
iv) Ufanisi – Ataja na aeleze ufanisi wake. Al.1
v) Uraibu – Mambo anayopenda kufanya Al.1
vi) Wadhamini/Warejelewa wawili au zaidi;
- Jina la dhamini
- Vyeo/cheo cha mdhamini
- Amswani
- Nambari ya simu
- Barua pepe

2. **MIKAKATI YA KUZUIA**
i) Kunawa mikono
ii) Kutosalimiana
iii) Kuvaa barakoa
iv) Kutokohoa au kupiga chafya kiholela/kutumia karatasi shashi au kiwiko unapokohoa au kupiga chafya.
v) Kukaa mbali na watu wengine
vi) Kukaa nyumbani wakati ambapo mtu hana shughuli muhimu ya kufanya nje.
vii) Kuepuka mahali paolip na umati wa watu.
viii) Kutotumia pesa taslimu na badala yake atumie njia za kieletroniki kulipia
ix) Kutumia kieuzi wakati ambapo kuna ukosefu/uhaba wa maji
x) Kujitenga/kutafuta matibabu wakati ambapo viwango vya joto viko juu au anaonyesha dalili za maradhi.

Al.20

3 Mtu asiyetaka mwanawe alie huishia kulia yeye mwenyewe.
Huwanasihi wazazi wasichelee kuuaadhibu watoto wao wanapokosea ili waishie kuwa na tabia na menendo mizuri.

4. Mwanafunzi aweze kutunga kisa ambacho kinaonyesha ambacho kinaonyesha ni mambo gani ambayo yamefanya dunia kubadilika
Ni nani aliyekuwa akimpa ushauri na sababu za kumpa ushauri huo.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJAGATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA.**
**KARATASI 102/2**

**UFAHAMU**

(a) Lazima wakubali mabadiliko / kuwa swala la mabadiliko kuhusu jinsia haliwezi kupuuziliwa mbali. (alama 2)

(b) (i) Kutukanwa
(ii) Kudharauliwa
(iii) Kunyimwa haki
(iv) Kunyimwa heshima
(v) Kunyimwa nafasi za ajira, elimu, uongozi
*zozote tatu 3 x 1 = 3*

(c) (i) Jamii inathamini sana misingi ya familia / mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa
(ii) Kiongozi ambaye hana mke au familia au Yule ambaye mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma. (alama 2)

(d) (i) Kwa sababu yatalenga mafanikio ya familia na mume.
(ii) Kiongozi aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke ambaye wanashauriana.
(iii) Tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri waliotoa uongozi ambao hadi wa leo unapigiwa mfano (2×1 = alama 2)

(e) (i) kukosa urithi
(ii) Maisha ya dhiki.
(iii) Kubaguliwa
(iv) Magonjwa yanayoweza kuangamiza k.v ukimwi *zozote tatu 3 x 1 = 3*

(f) (i) Kushamiri - Kunawiri
(ii) Hadiriki –hafai / hastahili
(iii) Azma - Nia/ kusudi *3 x 1 = 3*

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**UFUPISHO: MAJIBU**

a) i) Wanafunzi wengi huhofia jinsi ambavyo watafanya katika mtihani.
ii) Wataal;amu wanashauri kuwa mtahiniwa anafaa kupata muda mwingi wa kupumzika.
iii) Mtahiniwa anaweza kupata mzongo wa akili kwa kukosa mapumziko.
iv) Mtahiniwa apate usingizi wa kutosha wakati akifanya mtihani.
v) Mtihani wa mwisho si tofauti na mwingine.
vi) Mtahiniwa afanye udurusu na majaribio ya mtihani mbalimbali. (6x1)

b) i) Awe ametambua udhaifu wake na kutia bidii . kaudhibiti kupitia udurusu, mijadala na mashauriano.
ii) Aulize maswali kuhusu mada asioielewa.
iii) Ajadili na kufafanua mada anayoielewa kwa mwenzake asieilewa.
iv) Ajihadhari na majuto ya kufanya kile hakupaswa kufanya.
v) Ayapitie maswali kwa makini saidi na kuyaafakari kuyapangia nakuyaandika majibu sawasawa.
vi) Ayasome tena majibu kuhakikisha kuwa hajapotoka.
vii) Ale vizuri kabla ya kwenda kufanya mtihani.
viii) Afike katika chumba cha mtihani kwa muda unaofaa na akiwa amebeba kila anachohitaji.
ix) Asipoteze muda mwing kwa swali linalomshinda bali alirejelee baadaye.
x) Asifanye hila katika mtihani kwani matokeo yake yatafutiliwa mbali. 9x1 =9

**MAJIBU YA MATUMIZI YA LUGHA.**

a) Wakati wa kuamka konsonanti sauti hubanwa ihali katika kutamka irabu sauti hainanwi. (ala2)

b)

- irabu ya nyuma
- Irabu ya wastani
- Irabu ya viringwa (ala 3)

c) I) Ndwele
ii) Pweza (ala2)

d) Niliowaimbisha, tunayemkimbiza, ninayempikisha. (ala3)

e) I) Liana
ii) nyweana (ala2)

f) Kusamehewa kwa mhalify kulitokana na unynyekevu wake. (ala2)
Msamaha ulitolewa kwa mhalifu kwa sababu ya unyenyekevu.
Kunyenyekea kwa mhalifu lulifanya msamaha kutolewa.

g) Kelele za wachao Mungu ni Baraka. (ala2)

h) Utazawadiwa - kishazi huru
Ukicheza vizuri - kishazi tegemezi (ala2)

i) Wakati maalum (uliopa)
Wakati wa mazoea (ala2)

j) Kwa kijinsia – RH
Viongozi wenye msimamo thabiti mno - RN (ala2)

k) I) Jaribio/kujaribu
ii) Uchumi/kuchuma
chumo/mchumi (ala2)

l) Na - kiunganishi
Na = kutendeana (ala2)

m) Maria alimwambia kuwa angemwarifu angewuona. (ala 3)

n) Juma alituhitaji kwenda kwake
Mimi pamoja na Juma tuliitwa na mtu Fulani.
Sisi pamoja na juma tuliitwa na mtu Fulani. (ala 2)

o) mtu anayejichafua mwenyewe ni yule atupaye tope.
Mtu ajichafuaye mwenyewe ni yule atupaye tope.
Mtu atupaye tope hujichafua mwenyewe
Mtu atupaye tope ndiye ajichafuaye mwenyewe. (ala2)

p) Ukuta - kiambaza/sera
Mvulana - mvuli/shababi/ghulamu
Akiuparaga – panda, mwea, paramia, somber (ala 3)

q)

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | | | | | | | |
| SI | | | U | S2 | | | |
| KN | KT | | | KN | KT | | |
| N | T | N | | N | T | E | |
| Ouma | alianguka | mtihani | ila | Kamau | alifuzu | vizuri | |

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MAJIBU YA ISIMU JAMII**

a) Kituo cha polisi, mtu I anarejelewa kama afande. Anamhoji mshukiea/mtu II

b) Msamiati maluum – booking, curfew
- Lugha yenye toni kali – usiniharibie muda wangu,! Ingia ndani!
- Lugha yenye unyenyekevu (mshukiwa) mtu II amrejelea mtu I kama sir, afande, anaomba
- Kauli fupi fupi – Jina , Samwel Kioko
- Kuchanganya/kubadili msimbo – sir, curfew
- Lugha dadisi – maswali
- Uradidi/takriri – naomba naomba
- Lugha yenye kejeli – serikali saidia, naomba baada ya kujiponza.

**TATHMINI YA PAMOJAGATUZI DOGO LA MERU YA KATI**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**
**KISWAHILI 102/3**
**FASIHI**

**LAZIMA**

**1. SWALI LA KWANZA**
**FASIHI SIMULIZI**

a) **Miviga ni nini?** **Al.2**
Ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi Fulani/maalum cha mwaka.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Sifa za Miviga. Al.5
i) Huandamana na matendo yanayofuata utaratibu maalum
ii) Huongozwa na watu mahususi
iii) Kuna utoaji wa mawaidha
iv) Maleba maalum huvaliwa na wahusika
v) Hufanyika mahali maalum panapofanyiwa sherehe hizi
vi) Huambatana na utamaduni wa jamii husika. (zozote 5)

c) Hasara ya Miviga. Al.3)
i) Baadhi ya miviga imepitwa na wakati kama tohara ya wasichana
ii) Baadhi ya miviga inakinzana na malengo ya taifa
iii) Hujaza watu hofu inapohusisha kafara za binadamu
iv) Ushiriki na unaweza ksababisha uhasama unapohusishwa
v) Baadhi hughalimu kiasi kikubwa cha pesa

d) Matatizo ya ukusanyaji data Al.5
i) Huenda gharama ya utafiti ikawa kubwa.
ii) Mtazamo hasi wa wanajamii, kuhusu ujazaji wa hojaji
iii) Wanajamii kushuku kwamba mtafit anawapeleleza
iv) Mbinu kama hojajo huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika
v) Wahojiwa hukataa kuhojiwa iwapo wanahisi baadhi ya matendo yanaenda kinyume na imani ya dini yao.
vi) Mtafiti huenda asiwe na wakati wa kutosha kuwahoji watu wengi.
vii) Huenda mtafiti akakosa usalama na hivyo kuvamiwa.

e) Majukumu ya wimbo. Al.5
i) Kuondoa uchavu/ukinaifu

ii) Ni njia ya kushirikisha hadhira
iii) Husukuma visa mbele – kipengele cha msuko/ploti
iv) Kukamilisha ujumbe au kuutilia mkazo
v) Kudhihirisha sifa za mhusika Fulani
vi) Huipa hadithi mnato/mvuto wa kipekee
vii) Kufanya hadithi kukumbukika.

**TAMTHLIA: KIGOGO**

2. a) Eleza muktadha — Al.4
Msemaji ni majoka
Alikuwa anamwambia babu katika ndoto
Walikuwa katika chumba cha wagonjwa
Hii ni baada ya majoka kupata habari ya kifo cha mwanawe Ngao Junior. (4x1)

b) Mbinu za uandishi katika dondoo. (Al.4)
i) Jazanda – safari kurejelea uongozi
ii) Msemo – Dhahiri shahiri
iii) Nidaa – Dhahiri shahiri babu! ( 2 x2 = 4)

c) Matatizo yanayoikumba safari. Al.1
i) Mauaji ya jabali na uongozi
ii) Kufungwa kwa soko la chapakazi
iii) Njaa
iv) Urisadi
v) Kufungwa jela kiholelea
vi) Kuchapwa na askari
vii) Uchafuzi wa mazingira
viii) Migomo
ix) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
x) Kutowajibika kwa viongozi
xi) Ubadhirifu wa mali ya umma
xii) Kudhirifu wa mali ya umma
xiii) Kudhibiti vyombo vya habari
xiv) Utabaka
xv) Ulipizaji kisasi
xvi) Usaliti (12 x 1 = 12)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

3. Tamthlia ya kigogo inazungumza kuhusu hali halisi kaitka mataifa mengi ya kiafrika. Jadili .
Hali halisi – hali kamili y mambo
i) Uongozi mbaya unaoendelezwa na majoka
ii) Unyakuzi wa ardhi majoka kipande cha ardhi palipokuwa soko la chapa kazi na kujenga hoteli ya kifahari majoka and majoka Resort.
iii) Mauaji – vijana waoandama wanauawa. Mpinzani k.m Jabali
iv) Vitisho wanasagamoyo wanaishi kwa hofu. Tunu kuvunjwa mguu.
v) Matumizi ya vyombo vya dola. Askari wanatawanya waandamanaji pasi kupata haki zao.
vi) Maandamano na migomo wafanyikazi wanagoma kutetea haki zao. Walimu na wauguzi.
vii) Uongozi wa kinasaba/ukoo familia ya Ngao inatawala Ngao bin Marara, Majoka bin marara aliyekusudia kumrithisha mwanawe Ngao Junior.
viii) Ufisadi wanasagamoyo wanatozwa kodi ya juu

ix) Ubadhirifu wa mali ya umma. Pesa za mkopo zinatumika kufadhili mradi wa uchongaji vinyago.
x) Umaskini Ashua anaenda kuomba msaada kwa majoka
xi) Ukoloni mamboloea
xii) Juhudi za mapinduzi
xiii) Ubaguzi wa wa kinjisia hasa kwa wanawake – Tunu alikejeliwa kuwa angereuliwa kama kiongozi wa sagamoyo.
xiv) Matumizi mabaya ya vyombo vya habari. 10x2 = 20

Hoja ( al.1)
Mfano mwafaka al.1

**CHOZI LA HERI**

4. Haya ni maneno ya msimulizi
Yanamhusu Dick akikumbuka rafiki yake lemi ambaye aliuawa na umati
Anakumbuka kisa hiki anapoitshwa kuwa angetupwa nje na mwajiri wake, Buda, kisha asingiziwe wizi na kuchomwa moto.
Hofu hii ndiyo iliyomchochea kuingilia ulanguzi wa dawa za kulevya. ( al.12)

b) Tamathali mbili za usemi
i) Tashihisi - Akili ya Dick ilimtambia kisa chenyewe kama kwamba inataka kumuonya.
ii) Chuku - Akili ilimtambia kisa

c) Umuhimu wa Dick Al.12
a) Ametumiwa kuonyesha nafasi ya familia katika malezi.
Kuondoka kwa mama yake kunaisambaratisha familia yake;Dick na mwalike wanaibwa na sauna.
b) Ametumiwa kukashifu ufisadi. Anasema kwamba maafisa wa usalama wanaingia kwa Buda kwa tabasamu na kutoka kwa vicheko.
c) Anaendeleza swala la matumizi mabaya ya dawa. Anatumia dawa na kuzilangua.
d) Anachimu za maudhui ya mabadiliko. Anaamua kuacha ulanguzi wa dawa, kujielimisha na kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya simu.
f) Anaonyesha nafasi ya vijana katika kuboresha maisha ya jamii zao. Anawaajiri vijana wenzake. Ni kielelezo cha vijana wanaotambua makosa yao na kujirekebisha.
f) Ametumiwa kujenga tabia za wahusika.
i) utu wa mwangeka. Anamchukua kama mwanawe na kumwelekeza.

ii) Ukakamavu wa Umu – umu anamwambia Dick kuwa yeye, umu, atawalea yeye Dick pamoja na mwaliko kwa viganja vyake japo umu ni mchanga wakati huo.

g) anaendeleza ploti kukutana kwake na umu kunabadilisha mkondo wa hadithi. Anaelekezwa na umu kwa mwangeka ambaye anamsaidia kuyatengeneza maisha yake zaidi.
6 x 2 = 12
Hoja (al.1)
Mfano ( al.1)

**5. a) Majazi katika riwaya ya chozi la heri**
i) Ridhaa – Kukubali ama kutosheka. Mhusika Ridhaa anakubali na kutosheka na makuruhu aliyofanyiwa ya kuteketezewa mali na familia yake.
ii) Bwana Tenge – Tenge ina maana ya fujo. Bwana Tenge anamfanyia mkewe fujo na vitimbi anamwendea kinyume mke wake, Bi. Kimai. Bwana Tenge anashiriki mapenzi na wanawake wengine.
iii) Mzee Kedi – Neno kedi lina maana ya mambo yasiyopendeza, mambo ya hila pia ni kiburi. Mzee Kedi anamfanyia ridhaa hila kwa kuhusika katika kuiangamiza familia yake.
iv) Bwana Mkubwa – Mkubwa ni neno lenye maana ya cheo au hadhi kubwa. Bwana mkubwa ana cheo kikubwa serikalini.
v) Tetei – ina maana ya kutetea. Bi. Tetei ni mwanaharakati anayetetea haki za wanaume.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

vi) Mwalimu Dhahabu ni madini yenye thamani. Mwalimu dhahabu ni mwalimu anayekuwa wa msaada kwa Umulkheri

vii) Hazina – Hazina ina maana mali iliyohifadhiwa. Mhusika Hazina anakuja kuwa kama hazina kwa Umukheri kwani anamfaa Umu jinsi alivyomfaa kwa kimpa noti ya shilingi mia mbili.

viii) Zohali – Neno hili lina maana ya ajizi. Mhusika Zohali anapachikwa mimba akiwa kidato cha pili ni dalili ya uzembe na kutomakinika masomoni.

ix) Chandachema – Chandachema ni jina lilil oundwa kutokana na Chanda kidole) chema ambacho huvikwa pete. Mhusika huyu ingawa anapitia changmoto tele maishani anaishia kupewa ufadhili wa masomo(kuvishwa pete) na shirika la kidini.

x) Bwana Mabavu – Mabavu ni nguvu. Bwana Mabavu anatumia nguvu kumpoka babake Shamsi ardhi yake.

xi) Mzee Maarifa- anatumia maarifa na hekima kuanzisha kituo cha kupigania hakiza kibinadamu.

xii) Neema ni mkewe Mwangemi. Neema ina maana ya Baraka. Mhusika huyu anakuwa Baraka kwa mume na pia kwa mwaliko.

xiii) Bwana Kimbaumbau ni mtu kigeugeu. Bwana Kimbaumbau anamsaliti Naomi kwa kutaka kufanya mapenzi naye.

b) Nafasi ya vijana katika jamii – chozi la heri

– vijana ni wasomi mf. Umu, tila.
– Ni walanguzi wa dawa za kulevya mf. Dick.
– Vijana wengine wa kike wakubali kukeketwa na wengine wanaaga dunia na kulazwa hospitalini mf. Tauma.
– Vijana ni wapenda fujo.
– Vijana hutumiwa na wanasiasa kutekeleza uovu na mauaji.
– Ni dhihirisho kama wasio na huruma. K.m kuua wenzao bila huruma.
– Wasio na msimamo dhabiti. Wanapotoshwa na wanasiasa bila kuwazia madhara waliosababisha.
– Vijana ni wenye bidii katika kazi zao mf. Dick.
– *(Tanbihi: kadilia hoja za wanafunzi.)* 10 x 1 = 10

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**HADITHI FUPI**

5. Ufaafu wa anwani " mapenzi ya kifaurongo' 10

Kifaurongo ni mmea wenye sifa ya kujifisha mara unapoguswa. Mwandishi akejeli mahusiano yaliyojengwa katika msingi wa unafiki.

– Penina anajifanya kumjali Dennis katika hali yake ya kunywa uji na kuonyesha huzuni. Anamtia Dennis mshawasha wa mapenzi ila si mapenzi kamili.
– Msimulizi anadai wavulana wengi wameangamia katika utandabui wa mapenzi baada ya kufanyiwa makuruhu na wasichana wenye tabia ya kifaurongo.
– Penina anadai atakuwa na Dennis kwa mazuri na mabaya lakini alimwacha alipokosa ajira.
– Penina asema kuwa hafanyi mzaha na kuwa hawezi kumchagua mpenzi kwa msingi wowote kama si mapenzi. Mwishowe alivunja ndoa yake kwa sababu Dennis alikuwa fukara. Hii ni tabia ya kifaurongo.
– Penina hataki kuitwa mpenzi wa Dennis na amtaka atafute msichana wa kufu yake akidai mgomba changaraweni haupandwi ukamea.
– Penina amfukuza Dennis nyumbani alipolosa kazi ilhali alikuwa ameapa hangemsaliti kwa vyovyote vile.
Hoja 5 x 2 = 10

b) Nafasi ya elimu katika maisha ya wanajamii – mtihani wa maisha .(10)

- Wanafunzi wanatarajiwa kufanya mtihani wa kidato cha nne ili kubaini hatima yao. Samueli awaza kuwa matokeao ya mthihani yangekuwa daraja ya ufanisi.
- Elimu ina daraja/viwango – Samueli anatarajia kuingia chuo kikuu anapokamilisha kidato cha nne.
- Katika masomo kuna kufeli.
- Wanafunzi wanahofia matokeo ya mtihani wa kidato cha nne k.m Samueli.
- Wanafunzi wanaojiamini kupindukia huathiriwa kisaikolojia wanapofeli.
- Wanakunzi lazima watimize matakwa Fulani kabla ya kupatiwa matokeo yao.
- Wanafunzi wengine wanaonea aibu matokeo yao.
- Jinsia ya kike inapiku jinsia ya kiume masomoni k.m Dada zake Samueli.
- Jinsia ya kike inabaguliwa masomoni. Babake Samueli ameweka matumaini yake kwa Samueli.
- Watoto wanatarajiwa kupita mtihani wanusuru familia zao.

- Wanafunzi wanaichukulia elimul na masomo kwa mzaha na kejeli.
- Samueli aliona shule kama jela. 10 x 1 = 10

6. Msemaji ni babake Sara. Akimwambia Sara. Wakiwa hospitalini kwenye chumba cha daktari. Sara alikuwa ameenda kufanyiwa vipimo vya ujauzito na Beluwa alipowakuta wazaziwe wakisubiri katika chumba hicho.

b) sifa za mrejelewa.(Sara)
   i) mpenda masomo
   ii) ni mwoga
   iii) mwenye busara
   iv) mwenye mapenzi ya dhati
   v) mwenye utu hakutaka kuavya mimba
   vi) ni msiri
   vii) mwenye maadili
   viii) mwenye majuto
   ix) ni mvumilivu.
   (kila sifa itolewe maelezo. Mwanafunzi akitaja sifa tu asituzwe)
   Hoja Zozote 6 (6x 1 = 6)

c) Mbinu za lugha
   i) Swali la balagha; una nini?
   ii) Takriri; unaogopa, unaogopa

d) umuhimu wa msemaji (babake Sara)
   i) Kupitia kwake tunapata habari ya ukali kupita kiasi kwa wazazi kwa wanao.
   ii) Ni kielelezo cha wazazi ambao hawako tayari kubadili msimamo wao mkali kwa watoto wao.
   iii) Anaonyesha umuhimu wa wazazi kushirikiana katika malezi.
   iv) Anaonyesha umuhimu wa kuweka siri katika masuala tata ya familia.
   v) Ni kielelezo cha wazazi wanaouenzi utamaduni wa jamii yao.

e)Maudhui : i) Malezi
   ii) mapenzi

g) ufafanuzi wa maudhi
   Babake Sara anakuwa mkali kwa sara. Babake Sara anadalika na kumwonyesha mapenzi.

   Mapenzi
   Kuna mapenzi ya dhati kati ya sarana salime.
   Salime anamsaidia sara anapokuwa mjamzito.
   Salime aidha anamsaidia sara kuweka siri ya ujauzito.

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

7. USHAIRI

a) Eleza dhamira ya shairi hili (Al.2)
   i) Kueleza madhara ya kutofuata mawaidha/ushauri wa baba na mama.
   ii) Kuonyesha hasar/shida zinazowapata watu walio na kiburi, majivuno, tama. 2 x 1 = 2

b) Tambua njia mbili analotimia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. Al.2
   i) Matumizi ya kibwagizo.
   ii) Kurejelea methali k.m maajuto ni mjukuu huja kinyume. 2x1=2

c) Mifano ya tamathali za usemi. Al.4
   Swali la balagha – ya nini kushangaaa?
   Jazanda - Ulijidhania Samba. 2x 2 = 4

d) Lugha ya tutumbi ( Nathari ) Al.4
   Yale uliyoyaona kuwa bora ndiyo sasa yamekuletea shida. Mamia ya matatizo hayaishi kwako/ wapo ungetambua hapo awali basi hungekuwa ukitatizika wewe mwenyewe ndiwe chanzo cha haya..
   (4 x 1 = Al.4)

e) Idhini ya kishairi katika shairi hili Al.14)

i) Inkisari – alikuamba badala ya alikwambia
ii) Kuboronga sarufi – alikwambia wako mama badala ya mama wako alikwambia
iii) Lahaja – huanziriki/hupuliki 2x 2 = 4

f) Bainisha toni ya shairi hili
i) Toni ya majuto – anashangaa mambo yanvyomendea
ii) Toni ya kusikitika – anasikitika mishikeli haitoki kwake (matatizo yameganda)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. Al.2
i) Mstahiki – mheshimiwa
ii) Hupuliki – Husikii/Husikizi

2 x 1 = 2

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KCNM AWAMU YA 2 KIDATO CHA NNE, MUHULA WA PILI**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA I**
**DISEMBA, 2020**

**Karatasi 1**

1. Andika barua kwa mwenyekiti wa Tume ya kupambana na ufisadi ikipitia kwa katibu wa tume hio, huku ukieleza madhara ya ufisadi na jinsi ya kukabiliana na ufisadi nchini. (alama 20)

2. Eleza mikakati ambayo serikali ya Kenya imeweka kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Kigaidi nchini. (alama 20)

3. Andika kisa kitakachodhibitisha maana ya methali
   Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. (alama 20)

4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno haya;
   ………………………baada ya hayo yote,alinikumbatia kwa huzuni huku akinishukuru kwa kujaribu kuiokoa hali. (alama 20)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KCNM AWAMU YA 2 KIDATO CHA NNE, MUHULA WA PILI**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**DISEMBA 2020**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata***

Wakati wananchi katika kila pembe ya dunia waliadhimisha siku ya wapendanao maarufu kama “Valentine Day,” kwa mitindo mbalimbali, hali hiyo ilikuwa tofauti kwa baadhi ya wanaume nchini Kenya, baada ya kulalamika kuhusu kunyanyaswa na wake zao.

Kulingana na mwenyekiti wa chama cha kutetea haki za wanaume nchini, idadi ya wanaume wanaopigwa na wake zao imeongezeka mno. Alisema juzi kuwa utafiti wa chama chake umeonyesha kuwa harakati za kumpa mwanamke uwezo zimeathiri maadili na kusababisha kuwadharau wanaume. Mwanaharakati huyo alidai kuwa tatizo hilo limechochewa zaidi na hali ya kuwa wanawake wengi sasa wana kipato kikubwa kuliko waume zao.

Mwishoni mwa mwezi polisi walimtia mbaroni mwanamke mmoja mjini Nyeri, baada ya kumshambulia mumewe na kumjeruhi kwa panga. Mwanamme huyo bado anapata matibabu hospitalini. Yeye alirudi nyumbani kama amevaa miwani ndipo akakatwakatwa usoni na uchunguzi kuhusu tukio hilo bado unaendelea.

Inadaiwa kuwa zaidi ya wanaume 460,000 walinyanyaswa na wake zao mwaka jana na kwamba utafiti wa shirika la kuwatetea wanaume umeonyesha kuwa kesi nyingi za wanaume kuteswa na wake zao zinaripotiwa katikakati mwa nchi.

Hata hivyo, baadhi ya wanaume katika eneo hilo wameunga mkono hatua ya wanawake kuwashambulia waume zao. Wanasema kuwa wanapigwa kwa sababu wamekosa kuwajibika kwa familia zao. Wanadai kuwa wanaume wengi <u>hawajulikani nyumbani kwao</u>. Wake zao wanawajua makasisi ambao huja kuwaombea kuhusu matatizo ya nyumbani huku mabwana zao wakizama katika ulevi. Wanawake na waume wa Nyeri wametaka serikali kukomesha uuzaji na unywaji wa pombe haramu ambayo imechangia sana katika ugomvi wa nyumbani.

**Maswali**

a) Yape makala haya anwani inayofaa (alama 1)
b) Eleza sababu za wanaume kupigwa na wanawake katika ndoa (alama 4)
c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa wanaume wengine hawajulikani nyumbani kwao? (alama 2)
d) Fafanua majukumu ya makasisi katika jamii kwa mujibu wa kifungu hiki (alama 2)
e) Ni mabadiliko yepi yametokea katika asasi ya ndoa kwa mujibu wa kifungu? (alama 3)
f) Eleza maana ya misamiati hii kama ilivyotumika kifunguni (alama 3)
   i) Mwanaharakati
   ii) Amevaa miwani
   iii) Waliadhimisha

**2. UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia hatua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumkinga mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha na walimu hasa ikizingatiwa kuwa gharama ya maisha imepanda mara dufu.

Hata hivyo, ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamuzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inaokana na ununuzi wa vitabu vya Kawaida na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha, kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama. Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanywe.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwango vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tujiulize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule katika maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inavyohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hili ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo hutofautiana. Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa.

Kwa mfano, programu za kutahini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula?

Sasa mbona fedha za ziada? Wanaotetea kupunguzwa kwa karo wanapunguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotisha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahi wanapopata matokea mema. Hali hiyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa huduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile, hutumiwa kuwajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu _maram‘ uliozoeleka katika shule nyingi ikumbukwe kuwe lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe.

Kwa marefu na mafupi yake, serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotozwa hasa katika shule za upili zinafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangekuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwaajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo. Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinafsi.

Naamini kuwa hatua ya Waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kujiunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kutoa mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yaliyopo kwa sasa.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 – 70)
(alama 8, 1 ya mtiririko)

Nakala ya matayarisho
Nakala safi

(b) Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 – 45)
alama 7, 1 ya mtiririko

matayarisho
Nakala Safi

1. **MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Toa **<u>maelezo</u>** ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. **(alama 2)**

i) /p/...........................................................................................................................................
ii) /ch/.........................................................................................................................................
iii) /m/..........................................................................................................................
iv) /r/............................................................................................................................

(b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. **(alama 1)**.
(c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. **(alama 3)**
(d) Tumia neno **<u>tausi</u>** kama **kielezi cha mfanano**. **(alama 1)**
(e) Onyesha **namna tatu** za kutumia kiambishi "ji" katika **sentensi moja**, kisha ueleze **matumizi** husika. **(alama 3)**..
(f) Ziweke nomino hizi katika **ngeli** zake. **(alama 2)**
i) waya ...........................................................................................................
ii) Kilembwe ...........................................................................................................
(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya **aina** gani kisha uonyeshe **miundo** yake. **(alama 4)**
(i) <u>Kikapu kilichofumwa juzi</u> kitauzwa marikiti.
(ii) Wenzetu <u>walikuwa wakijinaki kabla ya dimba</u>.
(h) Eleza **maana mbili** za sentensi**:** Zainabu alisema atakusaidia. **(alama 2)**
(i) Onyesha **majukumu** ya mofimu katika neno**:** awaliaye **(alama 3)**
(j) **Andika kinyume:** Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. **(alama 2)**
(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo <u>bila</u> kutumia kiambishi <u>ku</u>. **(alama 2)**
i) Tuma ......................................................................................................................
ii) Pinda ......................................................................................................................
(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya <u>ukanushaji na kinyume</u>. **(alama 2)**
(m) Andika kwa usemi wa taarifa: "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alilalamika. **(alama 2)**
(n) Tumia **visanduku** kuchanganua sentensi ifuatayo**:** Alipotuona alitupuuza, lakini sisi tulimsalimia. **(alama 4)**
(o) Tumia vitate vya <u>jua</u> , <u>toa</u> na <u>baka</u> katika sentensi **tatu tofauti.** **(alama 3)**
(p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka. **(alama 2)**
(i) Ameanguka .......................... matopeni.
(ii) Mlango ulibishwa.............................
(q) Tofautisha sentensi. **(alama 2)**
(i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.
(ii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

**2. ISIMU JAMII (Alama 10)**
**Maswali**

a) "........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa ........."
i) Bainisha sajili ya mazungumzo haya. (al.1)
ii) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (al.4)
b) Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa. (al.5)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KCNM**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasiya 3**
**FASIHI**
**DISEMBA 2020**
**SWALI LA LAZIMA**

**1.FASIHI SIMULIZI**

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali

**Sungura alivyokwepa kuliwa na samba**

Wanyama wa pori waliamua sikumoja kumtuma mnyama mmoja kila siku alikoishi samba kama chakula. Siku moja ilikuwa zamu ya sungura kwenda huko.Sungura alikuwa mjanja sana. Alipanga mpango mzuri wa kumwangamiza simba.
Alienda alikoishi samba muda mrefu baadaya muda wa chakula wa simba. Alimkuta samba akiwa na hasira kubwa sana.
``Kwa nini umechelewa jinsi hii?`` aliuliza kwa hasira.
'Bwana wee,`` alisema sungura kwa sauti ya upole.
``Nilichelewa kwa sababu samba mwingine alinikimbiza. Nilitaabika sana kabla ya kupata upenyuwa kutoroka.``
``Simba mwingine? Je, katikaporihili?`` aliuliza samba.
``Ndiyo bwana mkubwa. Najua anakoishi.Tuandamane nikakuonyeshe,`` alisema sungura.
Simba alijitayarisha kuandamana na sungura. Sungura aliongoza njiahadi walipofi kama hali palipoku wana kisimaki kubwa. Sungura alimgeukia na kusema, ``Anaishihapa. Tafadhali njoo umuone!``
Simba alisogea ulipokuwa ukingo wa kile kisima. Aliyatupa macho hukona kukiona kivuli chake. Alidhani kuwa huyo alikuwa samba mwingine.Kwa hasira kubwa alifungua kinywa na kunguruma. Alimwona huyo samba mwingine akikenulia meno.Simba hakuweza kusubiri, alijitosa kisimani apambane na samba huyo. Huo ulikuwa mwisho wake.Sungura aliondok aakicheka akifurahi kuwa sasa wanyama hawataliwa tena na simba.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) i) Andika aina ya hadithihii (Alama 2)
ii) Taja sifa tatu za kutambulisha aina hii ya hadithi (Alama 3)
iii) Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi kwa jamii (Alama 3)
b) Kwa kutoa mifano taja aina mbili ya fomyula ya: (Alama 4)
i) Kuanza hadithi
ii) Kumalizia hadithi
c) Eleza sifa nne za mtambaji bora katika fasihi simulizi (Alama 4)
d) Tofautisha kati ya vipera viwili vya fasihi simulizi.
i) Mighani na maghani (Alama 2)
ii) La kabuna misimu (Alama 2)

**SEHEMU YA B:**
**TAMTHILIA – KIGOGO - P – KEYA**
**Jibuswali 2 au 3**

2. Siwezimimi, siwezi, sita kikuwa gurudumu la akiba .....huja ya achahayo?
a) Eleza muktadha wa dondoo (al.4)
b) Eleza sifa nne za msemaji wa kaulihii (al.4
c) Tambua matumizi kumi na mawili **(12)**ya jazanda katika tamthilia (al. 12)

**AU**

3. Kuyaopo ama taifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. UkirejeleatamthiliayaKigogo, ipatienguvukaulihii. (al. 20)

**SEHEMU YA C:**
**HADITHI FUPI – TUMBO LISILOSHIBA – ALIFA C / DUMU K.**
**Jibuswali 4 au 5**

4. (a) "Mame Bakari"
Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwana athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka. (alama 10)

(b) "Masharti ya Kisasa"
"…mapenzi nimateso,niutumwa, niukandamizaji , niushabiki usiona maana."

**AU**

5. Ndoto ya mashaka: Ali Abdalla Ali
"Sasa nimechoka mja.Nimechoka hata na radua kufa kuliko kuishi.Hadiliniha ya mashaka ya kutengenezwa?Mashaka ya mashaka!
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika (alama 4)
c) Fafanua mambo sita ya nayo mfanya mrejelewa aradue kufa. (alama12)

**<u>SEHEMU YA D</u>**
**<u>RIWARA: CHOZI LA HERI: ASUMPTA MATEI</u>**

6 "…haifai kucheza na uwezo wavijana, wao ni kama nanga. Huweza kuzamisha na kuingoa merikebu."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika dondoo (alama 4)
c) Kwa kurejelea riwaya hii, onyesha jinsi vijana wamezamisha merikebu ya wahafidhina (alama12)

**AU**

7. Baadaya dhiki faraja. Onyesha vile ukweli wa methali hii unavyodhihirika kwenye riwaya. (alama20)

**SEHEMU YA E:**
**USHAIRI**

***8 Soma shairihilikishaujibumaswaliyanayofuata.***

Tunda ni **kuliangua**, chungwa liloninginia,
Tunda pia kuchumia, mbuga sima yowelea,
Jingine lo lipo?

Tunda kivuno shambani, limakisha **palilia**,
Tunda vinono nyumbani, kwa jasho shughulikia
Jingine lo lipo?

Tunda tokeo la kazi, na ujira jipatia,
Tunda matokeo wazi, jitihada jifanyia,
Jingine lo lipo?

Tunda pia ni kizazi, wana haoni liozaa,
Tunda tama yaulezi, wana wataponifaa,
Jingine lo lipo?

Tunda letu la uhuru, minyororo jikongoa,
Tunda sote kuwa huru, na mazao furahia,
Jingine lo lipo?

Tundani wetu uchumi, na chumo **kujichumia**,
Tunda mwenzangu huchumi, ukaweza kwendelea
Jingine lo lipo?

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Tunda bora utu mwema, yako roho kuilisha,
Tunda la roho nasema, mja kumkamilisha,
Jingine lo lipo?

**Maswali**

(a) Shairi hili lina bahari kadha zitaje na ueleze. (alama 4)
(b) Eleza vina na mizani ya ubeti wa sita na saba. (alama 4)
(c) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)
(e) Taja maana ya 'tunda' kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
(f) Eleza maana ya maneno haya kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)
 (i) Kuliangua
 (ii) Palilia
 (iii) Kujichumia.

**MTIHANI WA PAMOJA WA KCNM AWAMU YA 2 KIDATO CHA NNE, MUHULA WA PILI**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA I**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. Andika barua kwa mwenyekiti wa Tume ya kupambana na ufisadi ikipitia kwa katibu wa tume huku ukieleza madhara ya ufisadi na jinsi ya kukabiliana na ufisadi nchini. (alama 20)
 Hii ni barua rasmi na iwe na muundo ufuatao.

**a. Anwani ya mwandishi**
 Anwani ya mwandikiwa: mwenyekiti wa tume
 Kupitia kwa katibu wa tume na anwani yake.

b. **Mtajo: Kwa** Bw./Bi.

c. **YAH**: MADHARA YA UFISADI NA JINSI YA KUKABILIANA NAO NCHINI

**HOJA: MADHARA**

I. Vifo kutokana na ajali barabarani.
II. Umaskini- kutoa pesa nyingi kisha kukosa kazi.
III. Kufukuzwa shuleni au chuoni.
IV. Kufungwa jela.
V. Kudidimiza haki – kesi kuamuliwa visivyo
VI. Viongozi kupoteza nyadhifa.
VII. Familia kuteseka.
VIII. Kupoteza ajira.
IX. Nchi kubaki nyuma kiuchumi na kimaendeleo.
X. Kushuka kwa viwango vya elimu.
XI. Afisi za kiserikali kuchomwa – wafisadi wakijaribu kusitiri ushahidi wa wafisadi.
XII. Kushuka kwa viwango vya huduma kwa umma – kuajiri watu wasiohitimu.

**SULUHU/ JINSI YA KUKABILI UFISADI**

I. Hatua kali ya kisheria kujukuliwa kwa wafisadi.
II. Kulipa wafanyakazi mishahara mizuri na kwa wakati ufaao.
III. Kuelimisha kuhusu madhara ya ufisadi.
IV. Kufuta kazi wafisadi.
V. Watu kutangaza mali zao.
VI. Majina ya wafisadi kutangazwa hadharani.

VII. Kufumania wafisadi.
VIII. Kupiga picha kamera na video wafisadi k.v polisi wakichukua hongo.
IX. Kujifunza kutosheka kwa kile ulichonacho na kuishi maisha ya kiwango chako.

X. Shirika husika la kuchunguza ufisadi lichunguze wafisadi na kuwashtaki kwa mujibu wa sheria.
XI. Kunyaganywa pesa au mali waliyopata wafisadi kiharamu.

**d. Hitimisho**
Sahihi
Jina/ cheo

**Nakala kwa**
1. Mwenyekiti wa Tume
2. Katibu wa tume
3. Idara zinazohusika

Zote ziwe na anwani

**KUTUZA**
Muundo - alama 4
Msamiati – alama 2
Mtindo - alama 4
Maudhui – 10/20
Hoja ziwe tano 5x2= 10

**MAKOSA**
Makosa sita ya sarufi – alama 3S
Makosa sita ya hijai – alama 3h
Urefu – alama 2
Kutozingatia muundo – alama 4

2 Mikakati iliyowekwa na serikali kukabiliana na Magaidi nchini:
i) Kuwapa mafunzo na kuwaajiri walinda usalama.
ii) Kuhamasisha na kuwataka raia wawe macho.
iii) Kuanzisha mpango wa nyumba kumi-kila mtu amfahamu jirani yake.
iv) Kuweka kamera za siri /CCTV katika maeneo muhimu.
v) Kuimarisha ukaguzi na ulinzi mipakani.
vi) Kukabiliana na makundi haramu kama vile al-Shabaab – huko Somalia.
vii) Kuongeza zana za kutumiwa kulinda usalama.
viii) Kushauri vijana kutojiingiza katika makundi haramu.
ix) Kuhimiza uhusiano mwema na majirani.
x) Kutwaa silaha haramu baina ya wananchi. n.k

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SWALI LA TATU**

3. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Maana: Anayekusaidia wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli mifano ya visa:
- Mtu aliyekuwa na mahitaji ya fedha mwenzake akampa
- Anayeugua halafu ana yule anayemuuguza/anayemlipia gharama ya hospitali.
- Anayetuhumiwa kwa kosa ambalo hakulifanya halafu akasaidiwa na mwenzake kumwondoa lawamani.
- Aliyekuwa kavamiwa na majambazi kisha mwenzake akamsaidia
- Mwanafunzi anaweza kuonyesha alimthamini mtu fulani na kumdharau mwengine: aliyedhadharauliwa ndiye anayemsaidia anapopatwa na shida.

**ZINGATIA**
Usaidizi ujitokeze wakati wa shida lau sivyo mwanafunzi asipite kiwango cha c+ (09 – 10).

**SWALI LA NNE**

4 Mwanafunzi aonyeshe juhudi za kuokoa ambazo:
Zinaambulia patupu. Hata hivyo, mwathiriwa anashukuru kwa kusaidiwa na kuhuzunika kwa hasara aliyopata.
**ZINGATIA**: Shughuli za kuokoa hazikufua dafu.

- Anayeonyesha juhudi zimefaulu baada ya usaidizi na aonyeshe huzuni na hasara amepungukiwa kimtindo.
- Anayeonyesha juhudi zimefaulu baada ya usaidizi na asionyeshe huzuni lakini aonyeshe hasara amepungukiwa kimaudhui (asipite c+ 09 – 10)

- Anayeonyesha juhudi zimefaulu bila usaidizi kisha huzuni na hasara hazipo amepotoka kimaudhui (atuzwe D 03)

**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KCNM**

**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA PILI 102/2**
**JARIBIO LA PILI, 2020**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**

**1. UFAHAMU**

a) Ndoa/kunyanyaswa kwa wanaume ( 1 x1=alama 1)

b) i) Kutowajibika kwao
ii) Wengine hawajulikani nyumbani kwao.
iii) Wamezama katika ulevi
iv) Wanawake kuwa na kipato kikubwa kuliko waume zao ( 4 x 1=alama 4)

c) Hawafiki nyumbani kwa jamaa zao ( 1 x 2=alama 2)

d) Kuwaombea kuhusu matatizo ya kinyumbani ( 1x2=alama 2)

e) i) Wanaume kutowajibika
ii) Wanawake kupewa uwezo
iii) Wanawake kuwadharau na kuwapiga waume zao ( 3x1=alama3)

f) i) Anayepigania haki za wengine
ii) Kulewa
iii) Walisherehekea ( 3x1=alama3)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**2. UFUPISHO: (ALAMA 15)**

(a) Mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 – 70)

- ✓ Kushirikiana na walimu wakuu.
- ✓ Gharama ya vitabu, karatasi za uchapishaji wa mitihani.
- ✓ Ununuzi wa kemikali katika maabara.
- ✓ Gharama za kuendesha michezo na tamasha za muziki.
- ✓ Gharama ya shule za malazi.
- ✓ Kupanda kwa gharama ya maisha.
- ✓ Maeneo yapatikanapo shule.
- ✓ Kiwango cha shule.
- ✓ Programu za kitathmini shuleni / mfumo wa masomo katika shule husika
- ✓ gharama ya kununua vyombo vinavyohitajika katika masomo haya
- ✓ . - Motisha ya walimu na wafanyikazi wengine.
- ✓ - Kuwaajiri walimu wa ziada. - Gharama ya lishe bora.

(hoja zozote 8, alama 8, 1 ya mtiririko)

(b) Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 – 45)

- ✓ Serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule.
- ✓ Hili huenda likazua mgogoro wa kiutawala.
- ✓ Shinikizo la kupunguzwa karo katika shule ya upili zinafaa kutetewa kimantiki na wala si kihisia.
- ✓ Serikali ingewajibika kwa kuwaajiri walimu wa kutosha.
- ✓ Walimu wangeongezewa mshahara, kuwazidi na kuwapandisha vyeo.
- ✓ Hatua zichukuliwe dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu.
- ✓ Hatua ya waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu ni ya busara.
- ✓ Hii inafaa kutoa mwelekeo mzuri kuhusu maswala tata yaliyopo kwa sasa. (hoja zozote 5x1 = alama 5)

MATUMIZI YA LUGHA

(a) Toa maelezo ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. (al 2)
(i) /p/ **Hewa huzuiliwa / hubanwa kabisa kisha kuachiliwa ghafla / kwa nguvu**
(ii) /ch/ **Hewa huzuiwa, kisha nafasi ndogo huachwa ili ipite ikiwa na mkwaruzo**.
(iii) /m/ **Hewa hupita kinywani na puani**.
(iv) /r/ **Ulimi hugotagota ufizini**. **(2× $^{1}/_{4}$)**

(b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. (alama 1)
**a-li-m-hu-ku-mu** **(1/0)**

(c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi shirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. (al 3)
**Ameshinda shuleni ambako amecheza akisoma.**
**t vitenzi sambamba**

**Tulikuwa ibadani na tumeimba tukamsifu Mungu**
**t vitenzi sambamba**

**(3/0)**

(d) Tumia neno tausi kama kielezi cha mfanano. (alama 1)
**Bibi arusi alitembea kitausi** **(1/0)**

(e) Onyesha namna tatu za kutumia kiambishi "ji" katika sentensi moja, kisha ueleze matumizi husika. (alama 3)
**Jicho la jipaka limejifumba.**
**Jicho - Baadhi ya nomino katika ngeli LI-YA**
**Jipaka - nomino za ukubwa**
**Limejifumba – kujitendea/ kiima ni mtenda/ kirejeshi cha mtenda**
**Matumizi mengine: Mwimbaji – kuunda nomino kutoka kwa vitenzi.** **(3×1)**

(f) Ziweke nomino hizi katika ngeli zake. (alama 2)
(i) waya U-ZI
(ii) Kilembiwe A-WA (2×1)

(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya aina gani na uonyeshe miundo yake. (alama 4)

(i) Kikapu kilichofumwa juzi kitauzwa marikiti.
Kirai nomino – Nomino + kishazi tegemezi/kivumishi kirejeshi

(ii) Wenzetu walikuwa wakijinaki kabla ya dimba.
Kirai kitenzi – kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, kihusishi na nomino (2×2)

(h) Eleza maana mbili za sentensi: Zainabu alisema atakusaidia. (alama 2)
Zainabu alisema yeye mwenyewe atakufaa.
Zainabu alisema mtu mwingine atakufaa. (2×1)

(i) Onyesha majuku ya mofimu katika neno: awaliaye (alama 3)
a – nafsi
wa – watendwa
l – mzizi
i – kauli
a – kiishio
ye – kirejeshi
(6×$^{1}/2$)

(j) Andika kinyume: Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. (alama 2)
Aliiangua picha ukutani kabla ya sherehe. (2×1)

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kutumia kiambishi ku.
(alama 2)

Tuma - mtume / utume / mtumwa
Pinda - upinde (2×1)

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. (alama 2)
Kukanusha ni kukataa jambo ilhali kinyume ni upande wa pili wa jambo. (2/0)

(m) "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alalamika. (alama 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Mpishi alilalamika kuwa viungo hivyo havingetosha kuunga mchuzi wao. $(4\times{}^{1}/_{2})$

(n) Tumia visanduku kuchangana sentensi ifuatayo. (alama 4)

Alipotuona alitupuuza lakini sisi tulimsalimia.

(o)

| S | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | U | S2 | |
| | | | | | |
| KN | | KT | | KN | KT |
| N/W | Ṡ(Kishazi) | T | U | W | T |
| Ø | Alipotuona | alitupuuza | lakini | sisi | tulimsalimia |

Tumia vitate vya jua, toa na baka katika sentensi mbili tofauti. (alama 3)

Nilimchua kwa maji moto mguuni alipoumia.
Hili embe sitalila kwa kuwa lina doa.
Atalipaka jengo lote rangi nyeupe. (3×1)

(p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka. (alama 2)
(i) Ameanguka tapwi matopeni.
(ii) Mlango ulipishwa ngongongo. (2×1)

(q) Tofautisha sentensi. (alama 2)
(i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.
Hakuna uwezekano wa kupita wala nafasi ya kusoma kwa bidii.
(iii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.
Kuna uwezekanano wa kupita mtihani akisoma kwa bidii.
(2×1)

**3. ISIMU JAMII (Alama 10)**

Maswali

a) “........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa .........”

i) Bainisha sajili ya mazungumzo haya. (al.1)
Sajili ya mahakamani / kortini / sheria (1×1)

ii) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (al.4)

i) Kunukuu na kurejelea vifungu vya sheria za nchi ili kudhibitisha hoja.
ii) Kudadisi / kuuliza maswali na kujibu maswali ili kuthibitisha ukweli wa mambo.
iii) Lugha ya unyenyekevu, heshima na dabu hasa upande wa mshtakiwa kwa hakimu ili kudumisha uhusiano mwema mahakamani k.m Bwana Jaji, hakimu n.k
iv) Matumizi ya msamiati wa kukopwa kutoka kwa lugha nyingine ili kuhifadhi maana asilia ya neno k.m msamiati wa kilatini k.v harbeas corpus
v) Msamiati wa kawaida huwa na maana maalum unapotumiwa katika muktadha wa kisheria k.m ‘My learned friend’ kumaanisha, mwanasheria mwenzangu.
vi) Matumizi ya sentensi ndefu ili kutoa hoja zilizokamilika kama ushahidi.
vii) Sarufi huzingatiwa kwa uangalifu sana na ukiukaji wake hauruhusiwi kwa kuwa ukiukaji unaweza ukabadilisha mkondo wa uamuzi utakaofanywa na kumfanya mtu apoteze kesi.
viii) Matumizi ya msamiati wa kipekee/maalum unaoenda sambamba na shughuli inayofanyika kortini k.m wakili, jaji, korti, kata rufani n.k

Maelezo au mifano itolewe. (4×1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

b) Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa.(al.5)

a. Matumizi kiholela ya lugha bila kuzingatia kanuni za kisarufi miongoni mwa wananchi.
b. Athari za lugha nyingine za kiafrika.
c. Athari za sheng' mingoni mwa vijana.
d. Uhaba wa machapisho kwa lugha ya Kiswahili.
e. Somo la Kiswahili kutengewa vipindi vichache shuleni ikilinganishwa na somo la kiingereza.
f. Masomo mengi shuleni hufunzwa kwa lugha ya kiingereza kuanzia shule za malezi isipokuwa somo la Kiswahili.
g. Matumizi mabaya ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari ambavyo vinahitajika kukuza kiswahili.
h. Kasumba ya kikoloni miongoni mwa wananchi kuwa Kiswahili ni lugha ya hadhi ya chini inayotumika na wasiosoma.
i. Kutokuwa na sera madhubuti inayoelekeza kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili.

*(5×1)*

**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KCNM**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA TATU 102/3**
**JARIBIO LA PILI , 2020**

**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA</u>**

**SEHEMU YA A:**
**FASIHI SIMULIZI**

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1**.

a) i) Hekaya

ii) Ujanja na uongo hujitokeza.
Ushindi hujitokeza
Huwa na ubunifu mkubwa
Hustaajabisha na kuchekesha

iii) – Hutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja.
- Hufunza watu juu ya kutenda wema.
- Huonya juu ya upumbavu.
- Huwaokoa wanaodhulumiwa kwa kutumia uwezo mkubwa wa kiakili wa mhusika.
- Hufunza kuwa katika ulimwengu ulojaa hila na shaka, silaha ya maisha ni maarifa, wema na uadilifu.

Zozote 3 x 1

b) Kuanza hadithi
- Paukwa, pakawa, sahani ya mchele, giza la mwizi...........
- Hapo zamani za kale paliondokea.
- Hadithi ! hadithi! Hadithi njoo........
- Kaondokea, chengangaa, kajenga nyumba kaka, mwanangu mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita......

Zozote 2 x 1

Kumalizia hadithi
- Hadithi inaishia hapo
- Tangu siku hiyo
- Wakaishi raha mustarehe
- Maadili

Zozote 2 x 1

c) **-** Uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.

- Mbunifu – anaweza kubadilisha papo hapo katika usimulizi wake.
- Mcheshi.
- Huigiza/kutumia vitendo/ufaraguzi.
- Hutumia ishara kueleza ujumbe.
- Hushirikisha hadhira.
- Huelewa utamaduni na lugha ya hadhira yake.
- Matumizi mazuri ya jukwaa.
- Uwezo kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v huzuni.
- Uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

Zozote 4 x 1

d) i) Mighani – hadithi za fasihi simulizi zinazosimulia mashujaa au majagina.
Hadithi za kihistoria.
Wahusika hupigania haki ya wanyonge.

1 x 1

Maghani – Aina ya ushairi wa kujigamba ambao hutolewa kwa kalima au maneno badala ya kuimbwa.

1 x 1

ii) Lakabu
Ni majina ya kupanga, kubandikwa au ya utani ambayo watu hujipa au kupewa kutokanan na sifa au hulka na maumbile. 1 x 1

Misimu
- Maneno yanayozuka na kutumiwa katika mazungumzo na makundi maalum ya watu katika jamii
- Mengine huzuka na kutoweka baada ya muda. 1 x 1

2. TAMTHILIA - KIGOGO

2 Maswali
"Siwezi mimi, siwezi mimi. Sitaki kuwa gurudumu la akiba … hujayaacha hayo?"

a) Eleza muktadha wa dondoo (Alama 4)

Msemaji ni Majoka
Msemewa ni Ashua
Wako ofisini mwa Majoka
Majoka alikuwa akimshawishi Ashua kimapenzi
(Hoja 4)

b) Eleza sifa nne za msemaji wa kauli hii. (Alama 4)
Sifa zake
- Mpenda anasa – anamtaka Ashua ambaye ni mke wa Sudi kimapenzi.
- Mwenye majigambo – anasema , wewe wafikiri waliniita ngao kwa nini? Kifua kipana. (uk. 24)
- Ni mpyaro- anamtusi Sudi: "uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi! Aliyekudanganya yanapikiwa watoto ubwabwa ni nani? (uk. 24)
- Fisadi- kupitia kwake Asiya na Ngurumo wanapata kandarasi ya kuoka keki za kutumiwa katika sherehe za uhuru. Pia, amemmegea Mzee Kenga sehemu ya ardhi sokoni Chapakazi kutokana na kuungwa mkono naye katika Nyanja za kisiasa.
- Ni mzinzi – anamtaka Ashua kimapenzi.
- Katili- anafunga soko na kukosesha akina ashua kipato. Anaamuru waandamanaji washambuliwa na askari.
- Mwenye dharau- analidharau soko la chapakazi kiasi cha kusema hayuko tayari kutoa fedha za kulisafisha, kwani ni la wachochole.
- Mwenye tama – anafunga soko la chapakazi kwa tama ya kutaka kujenga hoteli ya kifahari katika soko hili.
- Ni dikteta – anataka kuwashurutisha wafadhili wa akina tunu waondoke sagamoyo ndipo wasiendele kuwafadhili msichana huyu na watu wake wanaoendelea kupigania haki kwa wote.
- Mwenye mapuuza – badala ya kulishughulikia maandamano yanayoendelea na ambayo yanaupaka matope uongozi wake, anayapuuza. Ni kutokana na kupuuza kiini cha maandamano haya ambapo mwishowe anaondolewa uongozini.
- Mwenye vitisho – Tunu anapomfahamisha kuwa yeye na watu wake ni wauaji, anamtisha kwa kumwambia achunge maneno yake asije akamtia ndani.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

- Ni muuaji – Alisababisha kuuawa kwa Jabali. (Hoja 4)

c) Tambua matumizi kumi na mawili ya jazanda katika tamthilia. (Alama 12)
JAZANDA – ni mbinu ya kutumia kitu Fulani ili kutoa maana fiche ya jambo fulani.

Mifano

- Bahari mchafukoge- ni jazanda ya mambo kumwendea mrama sudi. Kenga anamaanisha sudi atakumbwa na matatizo au changamoto kali za kimaisha iwapo hataacha kuingilia maswala ya uongozi mbaya wa mzee majoka.
- Keki ya taifa – ni raslimali za nchi ambazo zinanuiwa kuwanufaisha watu wote katika jamii ya sagamoyo. Rslimali hizi zinawafaidi watu wachache kama vile majoka na vibaraka wake.
- Makombo ya keki ya uhuru – (uk. 17) ni jazanda ya raslimali chache wanazopata watu kutoka kwa viongozi.
- Asali – ni jazanda ya mapenzimjo wa ashua unamfanya majoka kumwona mwanakme huyu kama mtu anayetaka maswala ya mapenzi kutoka ka majoka.
- Kutafuta nyuki – ni jazanda ya kutafuta mapenzi/mwanamume ili amkidhie mahitaji yake ya kimwili.
- Ala moja haikai panga mbili – ala inaashiria ashua nazo panga mbili ni sudi na majoka. Majoka anamfahamisha ashua kuwa wanaume wawili hawawezi kuwa na mwanamke mmoja. Kwa hivo ashua achague kuishi na mmoja wao.
- Milango i wazi – (uk 23) majoka anatumia kwa ashua kama mbinu ya kumwonyesha kwamba, ingawa ameolea yuko tayari kumchukua na kukaa naye.
- Kutoa tonge kinywani (uk. 27) – husda anatumia jazanda hii kumaanisha mumewe ambaye anashuku kuwa tayari amenyakuliwa na ashua. Ni kutokana na hili ambap yuko tayari kumshambulia mwanamke huyu.
- Kuku na kanga (uk. 28) – husda anatumia kama njia ya kuonyesha kuwa , kama ashua ameshindwa kumtunza mumewe kama ataweza kumtunza majoka ambaye ni wa kiwango cha juu akilinganishwa na mumewe ashua, bwana sudi.
- Vidhibitimwendo (uk. 33) – hii ni ishara ya kuwazua tunu na wengine wanaoongoza maandamano kukomesha tabia hii yao, na hatimaye kumaliza kabisa.
- Kuwaweka mahali pao (uk. 34) – hapa kenga anamaanisha yuko tayari kuwaua wote wanaoongoza maandamano na wanaopinga utawala wa majoka mmoja baada ya mwingine hadi waishe.
- Kuota mizizi na kukita na kumea pembe (uk. 35) – kenga anatumia kumwonyesha majoka kwamba tunu na wapinzani wengine wa mzee majika walianza mambo polepole kasha baadaye wakapata nguvu zaidi hadi sasa wanateleza vitrndo vinavyoenda kinyume na matakwa ya majoka bila woga wowote kama vile kuandaa maandamano.
- Kutotumia bomu kuulia mbu (uk. 35) – majoka anamfahamisha kenga kwamba hakuna haja ya kutumia nguvu nyingi kupambana na wapinzani wake kama vile akina tunu. Kwake anawaona wakiwa watu wadogo sana ambao wanahitaji nguvu kidogo kuwaangamiza.
- Kucheza na simba anayenyonyesha (uk. 37) simba ni ishara ya majoka ambaye ni hatari kama simba , huku kutia mikono katika mdomo wa simba ni ile hali ya tunu kuingilia uongozi wa majoka kwa namna ya kutaka kuuporomosha. Hapa majoka anamwonya tun kwmba ni hatari sana kuingilia utawala wake kwa njia hii.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SWALI LA TATU**

3. Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. Ukirejelea tamthilia ya kigogo, ipatie nguvu kauli hii.

(i) **Kuuawa**
Wapinzani wa uongozi Sagamoyo wanauawa katika jitihada za kuisaidia Sagamoyo. Jabali aliuawa kwa kuwa mpizani wa majoka.

(ii) **Kushambuliwa na vijana.**
Vijana walitumwa kumvamia Tunu, nia ikiwa kumuua. Aliishia kuumizwa vibaya kiasi cha kufanya atumie kiti cha magurudumu.

(iii) **Kudhihakiwa**
Tunu anadhihakiwa na waliouunga mkono uongozi wa Majoka. Alipokwenda Mangweni, anadhihakiwa kwa kuambiwa kwanza aolewe.

(iv) **Vifungo**
Ashua anafungwa kwa kukataa matakwa ya majoka. Kufungwa kwake kulikuwa na nia ya kumshinikiza Sudi amchonge Majoka kinyago.

(v) **Kugonganishwa**
Tunu na Sudi wanachochewa kukosana ili waachane na harakati za ukombozi. Tunu anachochewa dhidi ya Sudi kwa kuambiwa kuwa yeye na Ashua ndio walikuwa wakiwinda roho yake.

(vi) **Kukatiziwa vyanzo vya riziki.**
Sudi na Ashua wanaachwa bila namna ya kupata riziki baada ya soko la chapakazi kufungwa na majoka.

(vii) **Vitisho**
Sudi anatishwa na Kenga kuwa ulimi wake ungemtoma kwenye bahari mchafukoge.

(viii) **Umaskini**
Ashua anavaliwa na uhitiaji kiwango cha kumwendea Majoka kutafuta usaidizi. Watoto wao na Sudi (Pili na Pendo) wanalala njaa.

(ix) **Watu kufurushwa makwao**
Jamii ya kina Siti inaandikiwa vibarua vya kusema wahame Sagamoyo. Hii inatokana na wao kutouunga mkono uongozi wa Majoka.

(xi) **Matusi**
Sudi anarejelewa na Majoka kama Zebe. Majoka ana-nuia kumdunisha machoni pa mkewe Ashua.

(xii) **Ndoa zao kuingiliwa**
Majoka anapania kuisambaratisha ndoa ya Sudi na Ashua. Anamshawishi Ashua aachane na Sudi na akubali kuolewa naye.

(xiii) **Vyombo vya habari kufungwa**
Baadhi ya vyombo vya habari kama vile runinga ya Mzalendo inafungwa kwa kupeperusha habari kuhusu watetezi wa haki.

(xiv) **Kupigwa marufuku kwa maandamano**
Kenga anamshauri Majoka kutangaza kuwa maandamano yote ni haramu.

(xv) **Kukabiliwa kwa nguvu wanapoandamana.**
Polisi wanatumia nguvu kupita kiasi kuwakabili waandamanaji. Matumizi haya ya nguvu yalipelekea kuumizwa kwa watu na kuuawa kwa vijana kiwandani.

(xvi) **Usaliti kutoka kwa wenzao.**
Juhudi za kuleta ukombozi zinapingwa na baadhi ya Wanasagamoyo kama vile Ngurumo, Asiye na Boza.

(xvii) **Kutimuliwa kwa wafadhili wa watetezi wa haki**
Majoka anatoa pendekezo la wafadhili wa harakati za ukombozi kuvunja kambi.

(xviii) **Kukabiliwa na taasubi ya kiume**
Tunu anapuuzwa na baadhi ya watu kwa kuwa ni mwanamke. Ngurumo anasema, "Heri nimpe paka (kura)…lakini si mwanamke."

(xix) **Kupumbazwa kwa baadhi ya wananchi**
Baadhi ya wananchi wanapinga harakati ya ukombozi kwa kuwa walipumbazwa na Majoka na watu wake kwa kuachiwa kitu pale mangweni.

xx) **Kutenganishwa wakati mikutano muhimu**
Wakati Tunu na Sudi wanaenda kwa Majoka kusema naye, majoka anawatenga ili aweze kukabiliana na kila mmoja.

xxi) **Kuishi kwa hofu na wasiwasi**
Bi. Hashima anaeleza jinsi ambavyo wanaishi kwa wasiwasi kutokana na dhiki wanazokutishwa na uonghozi wa Majoka.

xxii) **Kukosa muda wa kuwa na familia**
Sudi alikuwa na shughuli nyingi za kiukombozi, zilizomfanya kukosa muda wa kuwa familia yake.

**SEHEMU YA D**

**<u>SEHEMU TUMBO LISILOSHIBA</u>**

**4.** a)

- Tukio la kubakwa linampotesea fahamu na anaaibika sana anapozinduka na kujipata akiwa uchi uk 47
- Mwanamke kujeruhiwa – Baada ya Sara kubakwa na janadume lile, anaharibiwa na kuvuja damu.
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake.
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa.
- Masomo yake yanakatizwa – mwalimu mkuu alimkabidhii Sara barua ya kumfukuza shuleni (uk 49)
- Mwalimu mkuu hamsikilizi wala kumhurumia – badala yake aliongoza kumkejeli na kumweleza ile haikuwa shuke ya wazazi bali wa wasichana. Anasema hawafundishi wanawake hapo.
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara anaingiwa na mawazo mengi jinsi atakvyoukabili ule ujauzito. Anafikiria hata kuitoa ile mimba, kuhama kwao na hata kujiua.

for more free exampapers visit www.freekcsepastpapers.com

- Mwanamke katika umri mdogo anabebeshwa mimba jinsi Sara alivyofanysihwa. Mzigo huo ungekuwa na changamoto nyingi kutokana na umri wake mdogo.
- Kuhofia adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.
- Kuogopa kutoa taarifa ya kubakwa kwa wazazi kwa sababu wazazi hawangemwamini.
- Kuishi maisha ya kimaskini – msimulizi anaeleza kuwa Sara angekuniwakunjiwa matambatra yake na kuruishiwa nje.
- Kila mara mwanamke anapobakwa, anayelaumiwa ni mwanamke na hata huonwa kama shetani. Uk 48

**(hoja 10 x 1 = 10)**

b)

(Mtahiniwa azingatie masharti ambayo mwanamume anafaa ayazingatie pamoja na athari zake katika maisha ya ndoa.)

- Dadi ndiye mchuma riziki-yeye ni muuza samaki na apatacho kinatumiwa kuilisha jamaa yake.  Pesa za mkewe ni za kununua fasheni mpya mpya na mapambo.
- Dadi anasaidia kazi za nyumbani lakini mkewe Kidawa hatosheki na hayo.
- Kidawa hakubali kuwa mwanamume kazi ni za nje si za ndani na kuwa Dadi kufanya kazi za ndani ni hisani tu. Uk 60.
- Dadi analazimika kushika shughuli za upishi kama vile kukuna nazi na kutia mboga tui.
- Dadi anaosha nyumba, kufagia, kufua na hata kupiga nguo pasi.
- Wanandoa kujiwekea masharti ya uzazi.  Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu kutokana na athari za usasa.
- Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa za kuwauzia wateja.  Kila mara mkewe anapofanya hivyo, anaumia sana. Anaiona hiyo kama fursa ya mkewe kuhusiana na wanaume wengine . Uk 61.
- Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashinda kumweleza.
- Licha ya kuwa Dadi aliona ugumu wa kuzingatia masharti aliyowekewa na mkewe, hangeyavunja. Angefanya hivyo ndoa yao ingevunjika na huko kungekuwa ni kumvunja yeye pia.
- Dadi kushuku mkewe ana uhusiano wa kimapenzi na mwalimu mkuu.  Hali hiyo inampa wasiwasi sana hata anashindwa kula.
- Kila mara Dadi alitarajiwa kuwa baada ya kula angeviondoa vyombo mezani na hata kuvisafisha.
- Dadi anapoamua kuzua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu akiwa amepanda paipu na anaanguka na kuumia vibaya sana jambo linalomshtua sana mkewe pamoja na mwalimu mkuu.

5 a) Muktadha wa dondoo hili

Msemaji wa maneno haya ni Mashaka. Anajisemea, akirejelea hali yake ya maisha ya kimaskini katika mtaa wa Tandale. Maisha yake ni yenye shida kuanzia kuzaliwa, kuelewa, ndoa .Ameachwa na mkewe na amefika mwisho wa subira na kilichobaki ni kufa –hajui mwisho wa mateso yake.

(4x1=4)

b) Mbinu mbili za lugha zilizotumika.

i) Swali la balagha – Hadi lini haya mashaka ya kutengenezwa?

ii) Nidaa- hisia za ndani za mashaka zinadhihirika anaposema “Mashaka ya Mashaka!”

(2x2=4)

c) Mambo yanayomfanya mrejelewa ajaribu kufa.

i) Maisha ya Mashaka yametawaliwa na mateso na maonevu.

ii) Mashaka anatorokewa na mkewe waridi kwa sababu ya umaskini.

iii) Anaishi katika kibanda duni – Mtaa wa Tandale.

iv) Ameajiriwa na Kampuni ya ulinzi ya ZWS kwa mshahara duni.

v) Mashaka amefikia kiwango cha kujichukia kwa sababu ya nafasi yake katika jamii.

vi) Mamake aliaga dunia kabla ya kumtia machoni

vii) Anampoteza babake kutokana na ukiwa.

viii) Anasoma kwa dhiki.

ix) Analazimishwa kufunga ndoa na mzee Rubeya bila mpango wowote.

x) Anaishi maisha ya dhiki mikononi Bi. Kedebe ambapo analazimika kufanya vibarua.

(za kwanza 6x2=12) **SEHEMU YA D:RIWAYA**

for more free exam papers visit www.freecsepastpapers.com

6 a) i) Ni maneno yake mwangeka
ii) Anamwambia Ridhaa
iii) Wamo katika uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Rubia.
iv) Ni baada ya kuyakumbuka maneno ya Tila kuwa haifai kucheza na uwezo wa vijana katika jamii (4x1=4)

b) i) Tashibihi – wao ni kama nanga.
ii) Jazanda –merikebu inasimamia taifa la wahafidhina.
iii) Taswira – Picha ya merikebu inayozamishwa. (2x2=4)

c) Jinsi vijana walizamisha merikebu ya wahafidhina

- Genge la wavulana watano linawabaka lime na mwanaheri kwa kukisia kwamba wazazi wao hawakumpagia kwa mwanzi.
- Wanazorotesha usalama kwa kumvamia Subira na kumkata kwa sime kwa kumdhania kuwa hakumpigia kura Mwanzi.
- Vijana wanawavamia abiria barabarani wakiongozwa na kijana aliyekuwa amevaa shati lenye maandishi “Hitman” na kuwachomea ndani ya magari.
- Wanayachoma magari barabarani.
- Sauna awaiba watoto wake Lunga-Dick na Mwaliko na kuwatenga na dada yao Umu.
- Pete anameza vidonge ili kuavya kitoto chake cha pili ila hakufanikiwa.
- Zohali anajiingiza katika mapenzi na kupata mimba akiwa kidato cha pili.
- Wanawe Kiriri wanakataa kurundi nyumbani. Kutoka ughaibuni walikoenda kusoma
- Vijana wanamdhalilisha Mwekevu baada ya kuibuka mshindi katika uchaguzi.
- Kipanga anaachia masomo kidato cha pili na kuanza kunywa kangara –ananusurika kifo.
- Wanafunzi shukeni –anakomesea Ridhaa, wanaendeleza ukabila dhidi ya wanafunzi walowezi.
- Vijana wanapokea hongo kutoka kwa wanasiasa kama papa iti wawachague, hivyo kuimarisha uongozi mbaya.
- Vijana wasichana wanajifungua watoto na kuwatupa kwenye majaa ya taka kama Yule aliyeokolewa na Neema.
- Wanavunja sheria kwa kuandamana huku wamebeba picha za Mwanzi na kumhimiza atawale ingawa alikuwa ameshindwa n.k (6x2=12)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

7. Baada ya dhiki faraja. Onyesha vile ukweli wa methali hii unavyodhihirika kwenye riwaya

- Ridhaa anapata uchungu baada ya mali yake kuteketezwa, na kuwa mkimbizi. Anarejea hali ya kawaida baadaye anapojenga kituo cha afya cha mwanzo mpya.
- Ndugu Kaizari anapitia adha mbalimbali na kuishia katika kambi ya wakimbizi. Baadaye anaajiriwa na Ridhaa katika kituo cha afya kama Afiza wa matibabu.
- Salome anafurushwa kwa mumewe kwa sababu ya ukabila na kuwa mkimbizi. Mwishowe anajiunga na kitui cha afya cha mwanzo mpya kama muuguzi.
- Zohali anaringwa akiwa kidato cha pili na kusimangwa na wazazi wake. Baadaye anajifungua salama na kurejea shuleni.
- Mwangeka anasononeka kwa kumpoteza mkewe Lily na mwanaye Becky. Baadaye anamwoa Apondi na kuishi kwa raha.
- Apondi anaishi kwa woga wa kuhusiana na mwanamume wingine kwa miaka sita lakini baadaye anakutana na mwangeka na kufunga nikaha.
- Pete anakataliwa na babake, kuozwa kwa lazima, kujaribu kuavya na kujitia kitanzi. Baadaye anawaza jinsi ya kuboresha maisha yake bila kujjidhalilisha.
- Maisha ya Umu yamejaa mateso-kuachwa na mama, kufa kwa babake na kutoroshwa kwa ndugu zake, Dick na Mwaliko. Baadaye anaishi kwa raha nyumbani mwa Mwangeka, kusoma na muhitimu kama mtaalamu wa Zaraa.
- Dick anaingizwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya. Hatimaye anaanza biashara yake mwenyewe –kuuza vifaa vya umeme.
- Mwaliko anaibwa na sauna na kuishia mikononi kwa Bi. Kangara. Baadaye anaokolewa na polisi na kupelekwa kwa kituo cha watoto ambako anapangwa na Mwangemi.
- Mwangemi na Neema wanaishi bila mtoto baada ya kifo cha Bahati. Hata hivyo wanafaulu kumpanga mtoto mvulana,Mwaliko.
- Chandachema anaishia kuchuna majani katika shirika la chai la Tengenea baada ya kumpoteza nyanyake. Baadaye anaokolewa na kupelekwa katika makao ya watoto mayatima anakoendeleza masomo. n.k (10x2=20)

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

**8** (a) Tathlitha – Mishororo mitatu kila ubeti
Kikwamba – neno tunda kurudiwa rudiwa
Msuko – Kibwagizo mizani chache.
Ukara – Vina vya nje vyatiririka – vya ndani vyabadilikabadilika. ( alama 4 )

(b) Vina :

| Ubeti 6 | Ubeti 7. |
| --- | --- |
| mi, a | ma – sha |
| mi, a | ma, sha |
| po | po |

Mizani :

| ubeti 6 | Ubeti 7 |
| --- | --- |
| 8, 8 | 8, 8 |
| 8, 8 | 8, 8 |
| 6 | 6 |

(alama 4)

(c ) Tunda ni kivuno kinachotoka shambani baada ya kulima na kupalilia. Mazao mazuri hupatikana baada ya kushughulika kwa jasho. Je, kuna lingine? (alama 4 )

(d) Balagha (alama 2 )

(e)
- Zao la mti
- Tokeo la kazi
- Kizazi / watoto
- Uhuru
- Uchumi
- Vitu vyema
- Kutoa matini

(f) (i) Kutunda
(ii) Kulimia
(iii) Kujitafutia riziki ( alama 3 )

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA PILI - NAIROBI**
**102/1 – KISWAHILI – KARATASI YA 1**
INSHA
**JARIBIO LA MTIHANI KIDATO CHA NNE**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)***

1. Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, uliweza kujiunga na kundi la vijana wa kaunti yenu wanaojaribu kuboresha maisha yao. Mwandikie gavana wa kaunti hiyo barua pepe ukimweleza changamoto mnazopitia na jinsi anavyoweza kusuluhisha.

2. Teknolojia ya kisasa ni kama sarafu yenye sura mbili. Jadili.

3. Umdhaniye ndiye siye. Onyesha ukweli wa methali hii.

4. Andika insha itakayomalizika kwa

   ………… tulijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi. Lakini jitihada zetu ziliambulia patupu.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA PILI - NAIROBI**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**(LUGHA)**

1. **UFAHAMU: (alama 15)**
   **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi

sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika.Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

(a) Yape makala haya kichwa. (alama 2)

(b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. (alama 3)

(c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. (alama 4)

(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. (alama 2)

(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. (alama 3)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. (alama 1)

(i) Gandwa ______________________________________________

(ii) Tunguka ______________________________________________

2. **UFUPISHO**: **(alama 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi. Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wan chi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa zinazoingia nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya wananchi wasio na hatia.

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

(a) Kwa maneno yasiyozidi **themanin**i, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa. (alama 7)
(1 mtiririko)

(b) Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. (alama 6)
(1 mtiririko)

3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40):**

(a) (i) Taja sifa **mbili** bainifu za konsonanti /ny/. (alama 1)
(ii) Taja sauti **mbili** ambazo ni vikwamizo vya meno. (alama 1)

(b) Andika maneno matatu yenye miundo tofauti ya silabi. (alama 3)

(c) Kuwa kutoa mifano mwafaka tofautisha kati ya viwakilishi nafsi huru na nafsi viambata. (alama 2)

(d) Tumia neno lililopigwa mstari kama nomino kuandika sentensi upya.
Jengo hili lilifadhiliwa na umoja wa mataifa. (alama 1)

(e) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya: Songa
Zonga (alama 2)

(f) Unda sentensi **moja** yenye sehemu zifuatazo. (alama 3)
(i) Kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja. ___________________________________
(ii) Wakati uliopita ________________________________________________________
(iii) Yambwa tendwa _ _____________________________________________________
(iv) Mzizi _________________________________________________________________
(v) Kauli ya kutendesha ____________________________________________________
(vi) Kitamatishi ____________________________________________________________

(g) Tunga sentensi moja yenye kirai vumishi chenye muundo wa V + E. (alama 2)

(h) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi vya silabi moja vya: (alama 3)
(i) wakati _________________________________________________________
(ii) mahali ________________________________________________________
(iii) namna ________________________________________________________

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(i) Pambanua sentensi hii kwa kutuma visanduku/jedwali.
Jengo lililoporomoka limejengwa tena. (alama 3)

(j) Bainisha kiima na kiarifa katika sentensi ifuatayo:
Mhadhiri huyo alifutwa jana jioni. (alama 2)

(k) Tumia kiwakifishi kifuatacho kubainisha matumizi yake katika sentensi ili kutoa maana **mbili** tofauti. (alama 4)
Ritifaa

(l) Tambua kishazi na kipozi katika sentensi hii. (alama 3)
Ijapokuwa ameolewa tutamwandalia karamu leo.

(m) Amrisha vitenzi vifuatavyo katika **umoja** na **wingi**. (alama 2)
(i) Fa ______________________________________________________________
(ii) Imba ____________________________________________________________

(n) Andika katika kauli ya kutendeshewa: Amebatili muradi wa maji. (alama 2)

(o) Eleza maana **tatu** za sentensi ifuatayo. (alama 3)
Mwaliko huo ulitushitua.
Yakinisha.
Hatacheza wala kutuzwa. (alama 1)

(q) Andika katika **udogo** na **wingi**. (alama 2)
Mjusi aliyekuwa na jicho moja alianguka mtoni.

4. **ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**
(i) Watu wanapozungumza huenda wakafanya makosa ya sarufi kimatamshi na hata kutumia msamiati vibaya.
(a) Eleza sababu za kufanya makosa haya. (alama 8)
(b) Makosa haya huathiri vipi mawasiliano. (alama 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA PILI - NAIROBI**
**102/3**
**KIDATO CHA NNE**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**SEHEMU A:**
**"Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine"**
**Swali la lazima**

1. "Akanyangapo chini ardhi inatetemeka…………………..
Amejitia hamnazo. Kabwela kama mimi nina faida gani?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
(b) Fafanua mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (ala. 6)
(c) Eleza madhila kumi yaliyompata Kabwela (ala. 10)

**SEHEMU B:**
**Chozi la heri**
**Chagua swali la 2 au 3**

2. "…………. wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinavyowalisha…………..
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
(b) Taja maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili na ueleze (ala. 2)
(c) Kwa kutoa hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (2b) yanavyojitokeza katika riwaya (ala. 10)
(d) Eleza sifa nne za msemaji (ala. 4)

3. (a) Migogoro ni maudhui muhimu katika riwaya hii. Fafanua (ala. 10)

(b) Uozo umetamalaki katika jamii ya Chozi la Heri. Tetea kauli hii kwa kutolea hija kumi zilizoelezwa (ala. 10)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**
**Kogogo**
**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Na mwamba ngoma huvuta wapi?"
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
(b) Tambua tamathali mbili za sauti zilizotumika katika muktadha huo (ala. 2)
(c) Fafanua sifa za msemewa wa maneno (ala. 6)
(d) Thibitisha ukweli kuwa kila mwamba ngoma huvuta kwake ukirejelea Tamthilia nzima ya Kigogo (ala. 8)

5. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyokas"
Jadili usemi huo kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo (ala. 20)

**SEHEMU D: USHAIRI**
**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. Shairi**

La adhabu hili wingu, lataka kutunyeea
Himahima kwalo vungu, pasi nako kuchelea,
Kujikinga hili wingu, sije katunyeshea.

Wengineo hawajali, wasinayo wasiwasi,
Tahadhari hawabali, wajiunge nasi
Aidha watafakali, mengine yalo hasi.

Vua hili halibagui, jinsia wala umri,
Na kama hawajui, tuwajuze vizuri,
Kwani siso adui, kuwao msumari.

Tangazo haliwapiku, wahimizwa kujikinge,
Wingu hili la usiku, ukicheza likuringe,
Latutia usumaku, daima likunyonge.

Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba,
Yavuma kwa machungu, bila lolote huba,
Tunza chako kijungu, fungia kwalo juba.

Japo nafika tamati, nawaacha tafakari,
Madhara linalo wananti, wingu hili sukari,
Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

1. Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne (ala. 2)
2. Onyesha ufundi wa kimuundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili (ala. 4)
3. Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu. (ala. 2)
4. Kwa kuzingatia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu (ala. 1)
5. Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi yaidhini ya kishairi (ala. 3)
6. Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti (ala. 3)
7. Andika ubeti wanne kwa lugha ya tutumbi (ala. 4)
8. Eleza sifa moja ya nafsi neni katika shairi hili (ala. 1)

**7. Ushairi**

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata**

1. Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Ni kama jinga la moto
Bei juu

2. Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

3. Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa matajiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni ustiimari
Lo! Warudia

4. Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki

5. Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa

6. Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la

7. Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

(a) Toa anwani mwafaka ya shairi hili (ala. 1)
(b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako (ala. 2)
(c) Eleza dhamira ya mwandishi kuandika shairi hili (ala. 3)
(d) Toa mifano miwili ya urudiaji katika shairi hili, Je urudiaji huu una kazi/majukumu gani? (ala. 4)
(e) Onyesha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili (ala. 4)
(f) Eleza toni ya mshairi. Toa sababu (ala. 2)
(g) Nafsi neni ni nani? (ala. 1)
(h) Toa mfano mmoja wa twasira katika hili. Je, twasira hiyo inajengwa na nani? (ala. 3)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Fafanua sifa za matambiko katika jamii (ala. 4)
   (b) Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa (ala. 10)
   (c) Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya Ulumbi katika jamii ya kisasa (ala. 2)
   (d) Tofautisha dhana zifuatazo
      (i) Miviga na maapizo (ala. 2)
      (ii) Ngoma na ngomezi (ala. 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA PILI - NAIROBI**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI 1**
**INSHA**
**JARIBIO LA PILI**

**MWONGOZO**

1. **Mwanafunzi azingatie muundo wa barua pepe mfano;** Anwani kama vile:
   **i)** kwa: jketch@yahoo.com
   ii) kutoka kwa :juma@yahoo.com
   iii) Mada kuu: changamoto zinazowakumba vijana katika kaunti yetu
   iv) Tarehe: (mfano) Julai 5, 2015

   NB: Mwanafunzi azingatie urasmi kwa sababu ya cheo cha gavana katika maandishi yake.

**Mifano ya Maudhui**

- ✓ Ukosefu wa miundo – msingi mwafaka kama vile barabara bora
- ✓ Vijana kukosa uadilifu kazini.
- ✓ Matumizi ya vileo na mihadarati
- ✓ Uvivu/kulaza damu
- ✓ Mapato duni
- ✓ kukosa motisha
- ✓ ukosefu wa fedha za kujiendeleza
- ✓ kukosa kazi kwa waliohitimu kwa shahada mbalimbali.

***Tanbihi:*** Sahihisha hoja zozote tano zinazo oana na mada. Hoja zielezwe zikilenga mada.

Mifano ya Suluhisho

Serikali ihakikishe kuna miundo msingi kama barabara, vileo mitaani vipigwe marufuku, vijana wapewe mikopo ya fedha ili wajiendeleze, wapate masomo zaidi kuhusu jinsi ya kujitegemea kibiashara.

***Tanbihi:*** Hoja za suluhisho zilenge maudhui husika.

2. **Teknolojia ya kisasa ni kama sarafu yenye sura mbili. Jadili.**
   Ni swala la mjadala. Kuna hoja za kuunga na hoja za kupinga. Mwanafuzi atoe uamuzi mwishoni kulingana na uzito wa hoja zake.

Tazama upande ambao ameegemea. Huo ndio msimamo wake. Hoja zozote tano zinafaa.

3. **Umdhaniye ndiye siye**. Hii ni insha ya methali. Mwanafunzi ashugulikie sehemu zote mbili za methali katika kisa atakachobuni. Kisa kibainishe kinyume cha matarajio kuhusu matendo ya wanaohusika.

4. Mtahiniwa asimulie kisa kuhusu jumba au jengo lililoporomoka na kuwafunika watu. Lazima aonyeshe jinsi yeye na wengine walivyojitolea kuwaokoa watu waliokuwa wamekwama kwenye vifusi. Aonyeshe namna walivyokumbana na tatizo la kuwa okoa manusura mpaka wakashindwa. Asiongezee neno lolote kwenye haya maneno. Asipomalizia kwa haya maneno atakuwa amejitungia swali hivyo basi atuzwe D- $^{02}/_{20}$

**JARIBIO LA PILI - NAIROBI**
**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA SEKONDARI**
**102/2 – KISWAHILI LUGHA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **UFAHAMU**

(a) Uvutaji sigara/tumbaku.
Madhara ya uvutaji sigara/tumbaku 3 x 1

(b) (i) Husababisha saratani
(ii) Husababisha shida za macho na masikio.
(iii) Huathiri mifupa na meno.
(iv) Husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. 3 x 1

(c)
- Madhara kwa njia ya uzazi huifanya iwe vigumu kuhimili.
- Ni rahisi kwao kuzaa njiti.
- Huzaa watoto wepesi
- Huweza kusababisha kifo cha mtoto aliye tumboni.
- Mtoto huweza kuzaliwa akiwa na kasoro.
- Mimba huweza kutunguka. 4 x 1

(d) Ndio: Kwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kwa sababu ya kutumia tumbaku/kwa siku watu 10,800 hufa. 1 x 2

(d)
- Ngozi ya mvutaji hukauka/fanya mtu kuonekana mzee.
- Vidole hugandwa na kutu ya sigara.
- Kucha za vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano/hudhurungi.
- Nywele hukosa nguvu
- Nywele hung'oka mapema. Zozote 3 x 1

(f) (i) Kwamiliwa/kataliwa.
(ii) Toka mapema/haribiwa 1 x 1

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

2. **UFUPISHO**

(a) **Umuhimu**
- Ukuaji wa uchumi.
- Kupata bidhaa kutoka nchi nyingine.
- Masoko kwa bidhaa yake.
- Huduma za kitaalamu.
- Hukuza ushurikiano wa kimataifa.
- Hukuza ushindani.
- Ushirikiano wa kisiasa. 7 x 1 = 7 + 1 mtiririko = 8

(b)
- Masoko huru yanayoleta ushindani wa wafanyibiashara wadogo.
- Biashara kufungwa.

- Ucheleweshaji, wa bidhaa zilizoagizwa.
- Bidhaa kuchukua mda.
- Bidhaa duni huweza kupenyezwa.
- Ulanguzi wa madawa. 6 x 1 = 6 + 1 = 7

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) (i) Ni sauti nazali.
(ii) Hutamkwa kwenye kaa kaa gumu.
(iii) Ni sauti sighuna. 2 x ½ = 1
- th, dh 2 x ½ = 1

(b) (i) Irabu pekee – au, ua
(ii) KIKI – baba
(iii) KKI - ndoa, kwao
(iv) KKKI - mbwa, nywea 3 x 1 = 3

(c) Viwakilishi nafsi huru ni maneno kamili ilhali viwakilishi nafsi viambata ni viambishi vinavyosimama badala ya nomino – Mimi, sisi
Nitaenda 2 x 1 = 2

(d) Jengo hili limetokana na <u>ufadhili</u> wa umoja wa mataifa. 1 x 1 = 1

(e) Songa
Zonga 2 x 1 = 2
(Mwanafunzi atunge sentensi moja)

(f) (i) Kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja si
(ii) Wakati uliopita ku
(iii) yambwa tendwa m
(iii) Mzizi - som
(iv) Kauli ya kuetendesha esh
(vi) Kitamatishi a
(Mwalimu akadirie) 6 x ½ = 3

(g) Kivumishi kifuatwe na kielezi,
Mfano, mtoto mzuri sana analia. 2 x 1 = 2

(h) (i) Ali<u>po</u>fika tulitulia (wakati)
(ii) Pana<u>po</u>jengwa nyumbani pana hatari. (wakati)
(iii) Hakufurahishwa na aliv<u>yo</u>cheza (jinsi) 3 x 1 = 3

(i)

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | | KT | |
| N ✓ | 3 ✓ | T ✓ | E ✓ |
| Jengo ✓ | lililoporomoka ✓ | limejengwa ✓ | tena ✓ |

(3)

(j) Mhadhiri huyu/alifutwa jana jioni
kiima kiarifa 2 x 1 = 2

(k) (i) Kuonyesha kuwa herufi fulani imeondolewa.
(ii) Kuonyesha sauti ng'ongo.
(iii) Kuonyesha tarakimu fulani imeachwa. 2 x 2 = 4

(l) Ijapokuwa ameolewa – Tegemezi
Tutamwandalia karamu leo – huru
Karamu – kipozi 3 x 1 = 3

(m) Fa – Kufa!
- Kufeni! Feni!
Imba - Imba!
- Imbeni! 4 x ½ = 2

(n) Muradi wa maji umebatilishwa (2)

(o) (i) Tendo la kumweka mgonjwa ndani kufanywa dawa.
(ii) Sauti kali.
(iii) Mwito wa kuhudhuria 3 x 1 = 3

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(p) Atacheza na kutuzwa. (1)

(q) Vijijusi au vijusi vilivyokuwa na vijicho vilianguka vijitoni.(2)

4. **ISIMU JAMII**

1.
- Athari za lugha awali.
- Ujuzi wa lugha nyingi wa mzungumzaji.
- Mwingiliano wa sauti katika lugha ya kigeni ya asili na Kiswahili.
- Kutofahamu kanuni za sarufi ya Kiswahili.
- Kutafsiri lugha ya mama katika Kiswahili.
- Upungufu wa viungo vya kutamka kama meno/ndimi.
- Ukosefu wa baadhi ya sauti za Kiswahili katika lugha ya asili.
- Kuzunguma kwa haraka.
- Ugonjwa.
- Makusudi – ukiwa miongoni mwa wanajamii wasiojua lugha ya Kiswahili.
- Kurithishwa lugha isiyo sanifu – pewa matamshi mabaya aidha na walimu au wazazi
- Kutoijua lugha vizuri.
- Athari za Kiingereza.
- Taaluma za wazungumzaji.
- Kitembe cha elimu.
- Wanasarakasi wanapoigiza. (8 x 1)

2. (a) (i) Huzua tatizo la kimantiki msemaji asijulikane kuwa analenga nini.
(ii) Mawasiliano hukwamizwa kabisa.
(iii) Yumbe uliokusuduwa halipitishwi. (2 x 1)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JARIBIO LA PILI- NAIROBI**
**102/3**
**KIDATO CHA NNE**
**FASIHI - MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)
Msemaji - mawazo yake Dennis
Alikuwa anarejerea Shakira

Mahali - Katika afisi ya Shirika la kuchapisha magazeti
Tukio - Ni baada ya kumwona mamake Shakira (pandikizi la mama) akipita huku akisubiri kufanya mahojiano.

(b) Fafanua mbinu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (alama 6)
Chuku - Akanyagapo chini, ardhi inatetemeka.
Taswira - picha ya ardhi ikitetemeka
Msemo/ Nahau - kujitia hamnazo

Za kwanza 3 x 2 = 6
Kutaja - 1
Maelezo - 1

(c) Eleza madhila <u>kumi</u> yaliyompata Kabwela (alama 10)
- Anakosa kazi katika shirika la magazeti
- Kuachwa na Penina
- Kukejeliwa na Daktari Mabonga
- Hapewi pesa za masurufu na wazazi
- Kushindwa kujibu maswali wakati wa mahojiano – anaaibika
- Njaa – Anaamua kupika uji
- Hana nguo za kisasa/ simu/tarakilishi n.k.
- Anasumbuka kiakili kwa sababu ya hali /asili/umaskini
- Kufukuzwa na Penina

– Shuka zake zimechanika

**SEHEMU B: CHOZI LA HERI**

2. "……………. Wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinanyowalisha ……………."

(a) Eleza Muktadha wa dondoo hili (alama 4)

Msemaji: Mwaliko

Msemwa: Mwangemi

Mahali: katika hoteli ya Majaliwa ambapo wote wawili walikuwa wameenda

Tukio: Wanaongea kuhusu ndugu zake Mwaliko, Umulkheri na Dickson, waliokuwa wametoroshwa na Auntie Sauna. Mwangemi anampa Mwaliko matumaini kuwa wako hai na bila shaka wangekutana. Mwaliko anashuku kukutana kwake na ndugu zake kwa kuwa polisi hawakuwajibika ipasavyo kuwafuata kutokana na kuhongwa na walaguzi wa watoto.

(b) Taja maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili.

Maudhui ya ufisadi

(c) Kwa kutumia hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (1b) yanajitokeza riwayani (alama 10)

- Viongozi wanawanunua raia ili wawapigie kura
- Hazima ya jitegemee inayotarajiwa kuwapa vijana mtaji wa kuanzisha biashara inaandamwa na ukabila na unasaba.
- Viongozi wananyakua maelfu ya maelfu ya ekari na kujenga viwanda na maduka ya bishara.
- Katika ukurasa wa 57 watu walilaghaiwa na kuuziwa shamba la wenyewe kwa njia za kifisadi
- Majumba ya Ridhaa yalibomolewa kwa kisingizio kuwa yalinjengwa katika eneo lililotengewa ujenzi wa barabara mbadala. Barabara haikujengwa na shamba la Ridhaa kunyakuliwa.
- Katika uk 41 tunapata kuwa kuna tume za kupigana na ufisadi ambazo zinaundwaa, na jambo hili ni ishara kuwa kuna ufisadi unaoendelezwa.
- Pia katika uk 13, "Uchukuzi wa milungula pia ni aina ya ufisadi katika serikali" "Wengine walionekana wakitoa milungula hadharani, wengine wakatishia kuishtaki, uizara husika kwa kile walichokiita ukiukaji wa haki za umiliki mali"
- Wasimamizi wa hospitali wananyakua dawa na kuziuza kwenye maduka yao
- Uongozi haumpi Shamsi kazi baada ya kuhitimu. Unamtaka atoe hongo.
- Bwana mabavu ananyakua shamba la kina Shamsi kiasili na kuwageuza vibarua kwenye shamba lao.
- Familia ya bwana Kute inafisidi chakula cha msaada kwa kujigawa mara tatu kupata mara tatu zaidi ya posho waliyopata wengine.
- Baada ya kutangazia raia kuwa msitu wa mamba ni marufuku, viongozi wanaendeleza ukataji wa miti na uchomaji wa makaa usiku.
- Baadhi ya viongozi wananyakua hata madhabahu kwenye mlima wa nasibu ili kujenga hoteli kubwa za kitalii
- Halmashauri ya elimu inawasaliti wanafunzi wanaotoka katika familia maskini kwa kuwapa mikopo wanafunzi kutoka familia zinazojiweza na kuwacha wanafunzi maskini wajifanyie vibarua ili kujilipia karo.

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

(d) Eleza sifa nne za mzungumzi (alama 4)

- Msomi - anasoma hadi chuo kikuu na kuhitimu kwa shahada ya isimu na lugha
- Mdadisi - Anamuuliza Mwangemi kama anadhani kuwa ndugu zake Dick (Dickson) na Umulkheri (Umu) wako hai
- Mwenye haya - Anacheka kwa haya Neema anapomuuliza kama alikuwa anataka kuwaletea mkaza mwana.
- Mwenye Kumbukumbu - Anakumbuka kuwa dada yake Umulkheri (Umu) alimwambia kuwa mamke alimwacha akiwa na umri wa miaka mitano
- Mwenye shukrani - Anawashukuru wazazi wake Mwangemi na Neema ambao walijisabilia kumwelimisha licha ya kuwa hakuwa mwanao halisi.
- Mwenye bidii - Anafanya kazi yake kwa bidii ya mchwa katika kampuni ya magazeti ya Tabora kama mhariri katika kitengo cha biashara. Tunaelezwa kuwa Mwaliko anaifanya kazi yake kwa bidii ya Mchwa.
- Mwenye mapenzi ya dhati - Anawapenda wazazi wake, Mwangemi na Neema kwa dhati. Anamwambia Neema "Nitakwenda nawe mama"

**3. (a) Migogoro katika Chozi la Heri**

Migogoro ni hali ya kuwepo kwa mivutano/mikinzano/mfarakano baina ya wahusika katika kazi ya fasihi. K.m.

1. Mgogoro kati ya Mzee Kedi na familia ya Ridhaa wakati mzee Kedi anashiriki katika mauaji ya familia ya Ridhaa.
2. Mgogoro shuleni kati ya Ridhaa na wanafunzi wenzake wanapomwita "mfuata mvua"
3. Mgogoro wa kijnsia kati ya Mwekevu na Mgombea wa kiume. Mwekevu anarushiwa cheche za matumizi.
4. Mgogoro wa kijamii unajitokeza baada ya mkoloni kupuuza sera za mwafrika za umiliki wa ardhi.
5. Mgogoro katika familia yam zee Mwimo Msubili kwa sababu familia yake ilikuwa kubwa na hangeitosheleza kwa chakula.
6. Mgonjwa mmoja kwenye hospitali ya mwanzo mpya anapata majeraha mabaya baada ya kuvamiwa kwenye mzozo wa ardhi kule Tamuchungu.
7. Panatokea mgogoro kati ya baba na mama Pete. (uk 147)
8. Ridhaa anajipata katika hali ya mgogoro wa nafsi. (uk. 12) ……… baada ya muda wa mvutano wa hisis na mawazo.
9. Mgogoro wa kisiasa kuhusu ni nani atakayekuwa kiongozi wa jamii kati ya mwanamme na mwanamke (uk. 19)
10. Mgogoro kati ya raia na polisi wakiwa katika harakati za kudumisha amani (uk. 19)
11. Nyamvula anajikuta katika mgogoro wa nafsi yake wakati ambapo imani yake inakinzana na kazi ya mmewe ya kuwa mwanajeshi (uk.62) (10 x 1= 10)

**(b) Uozo katika Chozi la Heri**

1. Kuvunjika kwa ndoa/ kuwacha waume k.m. Naomi, Subira.
2. Mapenzi kati ya baba mlezi na bintiye Sauna alipopachikwa mimba na babake.
3. Wanawake kuavya mimba. Mamake Sauna anamsaidia mwanawe kuavya mimba.
4. Wizi/uporaji wa mali. Nyumba na maduka yaliporwa wakati wa vita vya baada ya kutawazewa kwa kiongozi mpya.
5. Ukatili. Mabarobaro wanawavamia watu na kuwafanya unyama …. Uk 25 alikula mikato miwili ya sime akazirai kwa uchungu.
6. Uendelezaji wa biashara haramu km. ulanguzi wa watoto
7. Ubakaji. Lime na Mwanaheri walibakwa babayao akitazama
8. Ulanguzi wa dawa za kulevya. Dick anafanya kazi ya kusafirisha dawa za kulevya
9. Kutupwa kwa watoto wachanga, km. kitoto Nasibu
10. Matumizi ya pombe haramu - vijana wa vyuo vikuu wanabugia pombe na kufanya wengine kuaga dunia
11. Ukeketaji wa watoto wa kike
12. Mauaji. Watu kupigwa risasi na kuuawa kam kuku
13. Ndoa za mapema – Pete aliolewa akiwa mdogo.
14. Ukosefu wa malezi bora- Naomi na Subira kuwaacha watoto wao.
15. Ufisadi – watu kunyakua sehemu zilizotengewa ujenzi wa barabara.
16. Ubaguzi wa kikabila (10 x 1 = 10)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**<u>SEHEMU C: KIGOGO</u>**

4. "Na mwamba ngoma huvuta wapi?

**(a) Eleza muktadha wa dondoo hili** **(alama 4)**

(i) Msemajio ni Kenga
(ii) Msemewa ni Majoka
(iii) Wako katika ofisi ya Majoka
(iv) Ni baada ya Majoka kumwelezea kuhusu habari gazetini kuhus umaarufu wa Tunu

(1 x 4 = 4)

**(b) Tambua tamathali mbili za semi zilizotumika katika muktadha huu** **(alama 2)**

(i) Methali – mwamba ngoma huvuta……
(ii) Swala la balagha - huvuta wapi?

(1 x 2 = 2)

**(c) Fafanua sifa sita za msemewa wa maneno haya**

Msemewa ni Majoka

(i) Ni katili – alishiriki katika mauaji ya Jabali
(ii) Ni mkware - Alikuwa amemuoa Husda lakini alitaka kujihusisha kimapenzi na Ashua
(iii) Ni mpyaro – aliwatukana wanasagamoyo wajinga

(iv) Ni fisadi – alinyakua mali ya uma kam vile soko la chapakazi
(v) Ni msaliti – Aliwasliti wanasagamoyo kwa kuwa walimchagua ilhali anajinufaisha yeye, pia anamsaliti Husda kimapenzi.
(vi) Ni mwenye dharau
(vii) Ni laghai
(viii) Ni dikteta
(ix) Ni mwoga

(1 x 6 = 6)

**(d) Thibitisha ukweli kuwa kila mwamba ngoma huvuta kwake ukirejelea Tamthilia nzima ya Kigogo (alama 8)**

- Kenga anamfuata Majoka na uongozi dhalimu kwani ananufaika nao. Mfano ardhi
- Ngurumo anaunga mkono uongozi thalimu wa Majoka ili aendelee kunufaika. Mfano pombe.
- Mama pima anautetea uongozi wa Majoka kwa kuwa ananufaika nao, mfano. Kandarasi ya kuoka keki, kibali cha kuuza pombe haramu
- Majoka ana ari ya kuwafurusha wafanyabiashara kutoka sokoni ili alinyakue kwa matumizi yake kibinafsi ya kujenga hoteli ya kifahari.
- Wafadhili wa kina Tunu wanatia habari chumvi kuhusu umaarufu wa Tunu.
- Wanapolisi wanayafuata maagizo ya Majoka ya kuwashambulia wanasagamoyo ili walinde kazi yao.
- Chopi anatekeleza uhuni wa Majoka ndiposa asije akamwaga unga wake. (Kufutwa kazi)
- Husda anaolewa na Majoka kwa sababu ya utajiri wa Majoka.
- Boza anajipendekeza kwa kenga ili apewe mradi wa kuchonga kinyago. Pia anasema mke wake ndiye aliyeioka keki (8 x 1 = 8)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**5. KIGOGO**

Sumu ya nyoka husababisha madhara mengi kwa mhusika/ kiwemo kuua. Kuna mambo mengi yanayodhuru au kuwaua wananchi katika utawala wa Majoka.

- ✓ Unyakuzi wa ardhi - majoka na mshairi wajifurahia eneo la soko la chapakazi ili ajenge hoteli iya kifahari
- ✓ Kuamrisha askari kutawanya waandamanaji na kuasababisha kifo cha vijana watatu
- ✓ Vitisho – wanaharakati wanaopinga utawala wa Majoka wanatishwa. Kuna vikaratasi vinavyorushwa katika makazi yao ili wahame (siti anamweleza mamake Tunu)
- ✓ Kuangamiza wapinzani wake – Jabali aliuawa kwa njama za Majoka na chama chake bila kikasambarakati
- ✓ Ukosefu wa utu. Majoka hathamani utu/uhai wa mtu. Majoka anaamrisha watu wapigwe risasi bila kujali.
- ✓ Tengatawala – uhasama unapandwa na viongozi ili kuwagaza wananchi mf. Sudi ana uhasama na Boza sababu wako katika mirengo tofauti ya kisiasa.
- ✓ Kuzorota kwa maendeleo. Jimbo la Sagamoyo limetimiza miaka sitini ya uhuru lakini bado liko nyuma kimaendeleo.
- ✓ Rushwa - Mamapima anatoa hongo ya uroda kwa Ngurumo ilia pate mradi wa kuoka keki ya uhuru.
- ✓ Elimu mbovu – elimu inayotolewa katika shule za kifahari inawalemeza vijana badala ya kuwandaa wawe wazalendo Majoka and majoka academy.
- ✓ Utawala wa kiimla – majoka anataka aendelee kutawala ingawa urubani umemshinda na amekwisha zorotesha nchi.
- ✓ Matabaka – Sumu ya nyoka iliyozagaa katika jimbo la Sagamoyo imesababisha kuwapo kwa matabaka. Mambwenyenye – majoka, Kenga - maskini - wananchi
- ✓ Uvivu na ubwete – Majoka ni kiongozi ambaye hajali umuhimu wa kazi. Anatenga mwezi mmoja ya kupumzika katika kuadhimisha miaka 60 ya uhuru.
- ✓ Ukimtamba – Majoka ana rasilimali nyingi na miradi mingi mikubwa. Anamiliki Majoka and Majoka Company, Majoka and Majoka modern resort
- ✓ Ukoloni mamboleo. Jimbo la sagamoyo linaongozwa kwa mikono amabayo halipwa kwa muda mrefu. Halipwa kwa vizazi vya sasa na hata vyavyo
- ✓ Ufujaji wa fedha za umma. "mikopo iliyochukuliwa haikutumika vizuri. Kenga anamweleza Sudi kuwa akikubali kuchonga kinyago cha marara bin Ngao angepata fedha za kubadilisha maisha yake.
- ✓ Kuwafunga raia bila sababu – mf. Ashua kutiwa mbarani ili iwe funzo kwa Sudi
- ✓ Kupanga njama ya kumwua Tunu.
- ✓ Kufunga soko la chapakazi ambayo ni tegemeo kwa raia wa sokomoko
- ✓ Majoka anamwambia Kenga lazima chatu mmoja atolewe kafara (auawe)

- ✓ Anapanga kutumia mamlaka kuzima uchunguzi wa Tunu kuhusu kifo cha jabali
- ✓ Anafuja pesa za kusafisha soko la chapakazi
- ✓ Anatumia mamlaka yake kudhibiti vyombo vya habari

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**SHAIRI LA A**

**1. Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne (alama 2)**

Hatari ya wingu na umuhimu wa kujikinga

Anasema tangazo haliwapiti, wahimizwa kujikinga na hatari (2 x 1 = 2)

**2. Onyesha ufundi wa kimuundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili (alama 4)**

- Ametumia beti sita
- Kila ubeti una mishororo mitatu
- Vina vimepangwa kwa mtindo wa ukaraguni
- Idadi ya vipande katika kila mshororo ni viwili
- Idadi ya mizani inatofautiana katika mishororo (4 x 1 = 4)

**3. Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu (alama 2)**

- Wingu - ni hatari iliyopo
- Vungu - ni mikakati ya kujikinga kutokana na hatari yenyewe (2 x 1 = 2)

**4. Kwa kuzingztia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu (alama 1)**

Tamthlitha – kila ubeti una mishororo mitatu (1 x 1 = 1)

**5. Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi ya idhini ya kishairi (alama 3)**

- Inkisari – yalo – yaliyo
- Lahaja – wananti – wananchi
- Tabdila – tafakali – tafakari (3 x 1 = 3)

**6. Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti (alama 3)**

- Mathnawi – jina vipande viwili katika kila mshororo
- Ukaraguni – vina vyake vinafanana kulingana na beti. Vinabadilika kutegemea ubeti
- Tathlitha – lina mishororo mitatu kila ubeti (3 x 1= 4)

**7. Andika ubeti wane kwa lugha ya kwaida / tutumbi (alama 4)**

Hampitwi na tangazo linalowahimiza mjikinge na hatari hii kwani ukiichezea kwa vile ina nguvu za kukuvuta na kukuua.

**8. Eleza sifa mmoja ya nafsi neni katika shairi hili (alama 1)**

Mshawishi/ mwelekezi mwema

Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari

Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SHAIRI LA B**

a) Maendeleo ya umma (1 x 1 = 1)

b) Ni shairi huru - halina mpangilio wa vina
 Mahususi
 Idadi ya mizani inabadilika
 Mishororo haitoshani (aina alama 1)
 (sabau alama1)

c) Kuonyesha ni mambo gani muhimu katika maendeleo ya umma kama vile kuheshimiana usawa na kumiliki vitu (alama 3)

d) Urudiaji wa maneno
 Urudiaji muundo – mstari wa kwanza } Kusisitiza
 Urudiaji wa silabi - Urari wa vina (3 x 2 = 6)

e) Jazanda tama ya fisi
 Istiari - dola – shilingi (2 x 2 = 4)

f) Masikitiko – baada ya kuondoka mkoloni walidhani hali ingeimarika kutaja al. 1
 Sababu al. 1

g) Ni msimulizi (1 x 1 = 1)

h) Vitu kubaki gulioni – kuviona madukani wanaoweza kununua ni matajiri pekee (ala. 1)

Msimulizi anarejelea maskini asiyejiweza kiuchumi na hawezi kumudu bei ya bidhaa madukani

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**8. a) Sifa**

- ✓ Hutolewa na wazee maarufu walioteuliwa.
- ✓ Hufanywa mahali maalum k.v. pangoni, mwituni n.k.
- ✓ Huandamana na sala
- ✓ Huandamana na utoaji kafara k.v. kuchinja mbuzi, n.k
- ✓ Huandamana na maombi (Hoja 5 x 1 = 5)

**b) Tofauti**

| Maigizo yakawaida | Sanaa yamaonyesho |
|---|---|
| ✓ Mazingira ya kuzua/maalum | ✓ Hutumia mazingira halisi |
| ✓ Matukio ya kuiga | ✓ Matumio halisi/ ya kila siku |
| ✓ Huwa na wahusika na hadhira maalum | ✓ Washiriki na waigizaji walio pia hadhira |
| ✓ Matumizi ya ukumbi na jukwaa maalum | ✓ Hakuna haja ya ukumbi wala jukwaa |
| ✓ Hutumia maleba na vifaa vya kuzua mazingira maalum | ✓ Hakuna vifaa maalum bali huwa mazingira yenyewe |
| ✓ Hugawika katika maonyesho kutumia lugha kwa njia maalum | ✓ Muundo wake hufululuza au hayajagawika katika maonyesho |
| ✓ Wahusika hufanya mazoezi kabla ya igizo halisi | ✓ Hawahitaji kufanya mazoezi kwa nini matukio ya kila siku |
| ✓ Huwa na malipo | ✓ Hamna malipo |

(Hoja 5 x 2 = 10)

c) Miktadha ambamo ulumbi hutumika katika jamii

- ✓ Katika mijidala bungeni
- ✓ Katika hotuba za kisiasa
- ✓ Katika mahubiri maabadini
- ✓ Katika mijadala shuleni
- ✓ Kortini
- ✓ Katika shughuli za kijamii k.v. posa
- ✓ Katika sala / dua
- ✓ Katika maapizo
- ✓ Katika malumbano ya utani
- ✓ Katika majigambo/ vivungo

d) (i) Miviga ni ibada au sherehe za kitamanduni ambazo kwa kawaida ufanywa kipindi Fulani cha mwaka. Sherehe hizi utaratibu wa sanaa za kimaonyesho.

Maapizo ni kauli za kuomba Mungu, miungu au mizimu kumwadhibu mtu Fulani au watu katika jamii kutokana na matendo yao maovu. (2 x 1 = 2)

(ii) Ngoma ni unenguaji wa viungo vya mwili kuambatana na midundo maalum ya ala za muziki au mahadha ya muziki wenyewe.

Ngomezi ni maigizo ya sanaa ya kuwasilisha ujumbe kwa kutumia ngoma

(2 x 1 = 2)

for more free exam papers visit www.freekcsepastpapers.com